RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI
HESABU ZA SERIKALI NA MASHIRIKA (PAC) YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR, 2021/2022

SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Katika mwaka wa fedha 2019/2020) Kamati hii ilifuatilia pia Ripoti mbili za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali licha ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Haroun Ali Suleiman kuwasilisha Ripoti tTano mbele ya Baraza la Wawakilishi katika Baraza la kumi katika kikao cha tarehe 10 Febuari 2021

Kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Kamati ya PAC ilifuatilia ripoti zifuatazo:-

i. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia 30Juni,2020.
ii. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2017/2018
iii. Ripoti ya Ukanguzi wa Mifumo ya Tehama kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2020
iv. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) kwa kipindi chakuanzia mwaka 2016 hadi 2018
v. Ripoti ya Ukaguzi Maalum Unaohusu Utekelezaji wa Maagizo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt Hussein Ali Hassan Mwinyi wakati wa kuwaapisha Viongozi Wakuuu unaohusu Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Pemba.

## 1.1 WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati hii inaundwa na Wajumbe 7 na Sekretarieti kama ifuatavyo:

1) MHE. JUMA ALI KHATIB MWENYEKITI.
2) MHE. SALHA MOH'D MWINJUMA MAKAMO MWENYEKITI.

3) MHE. ASHA ABDALLA MUSSA — MJUMBE
4) MHE. MIHAYO JUMA N'HUNGA — MJUMBE
5) MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN — MJUMBE
6) MHE. MARYAM THANI JUMA — MJUMBE
7) MHE. SULUBU KIDONGO AMOUR — MJUMBE

Sekretarieti ya Kamati hii ilikuwa na Maafisa watatu ambao ni Makatibu wa Kamati na Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama wafuatao:-

Sekretarieti

1) NDG. HAJI KHATIB HAJI — KATIBU
2) NDG. MARYAM HAJI ALI — KATIBU
3) NDG.NASSOR MDACHI MWINYI — MKAGUZI- OFISI YA MDHIBITI- (UNGUJA)
4) NDG .SALUM SULEIMAN ALI — MKAGUZI- OFISI YA MDHIBITI - (UNGUJA)
5) NDG .JUMA MOHAMMED JUMA — MKAGUZI- OFISI YA MDHIBITI -(UNGUJA)
6) NDG.MOHAMAD SALEH JUMA — MKAGUZI - OFISI YA MDHIBIT - (PEMBA)
7) NDG. SAAD OTHMAN SAAD — MHANDISI WA BARAZA LA WAWAKILISHI

## 1.2 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI

Vile vile, Kamati imezingatia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo hutumika kuwa ni Hadudi Rejea, sambamba na kutekeleza kazi zake chini ya matakwa ya Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020.

Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilikutana na Wizara na Taasisi za Serikali zilizohusika na kazi, na hatimae Kamati ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kushuhudia uhalisia wa maelezo ya Wizara, Taasisi husika, Kamati za Mfuko wa Jimbo kama zinavohusika na hoja ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Aidha, Kamati kwa kuzingatia haja iliyokuwepo, ilifanya ziara katika maeneo husika na baadae ilifanya mijadala ya hoja mbali mbali.

Shughuli hizi zilifanyika ndani ya mizunguko mitano kama ifuatavyo:

Mzunguko wa Kwanza: i. Tarehe 11/1/2021 hadi tarehe 16/2/2021

Mzunguko wa Pili: i. Tarehe 20/3/2021 hadi tarehe24/4/2021

Mzunguko wa Tatu: i. Tarehe 9/8/2021 hadi tarehe26/8/2021

Mzunguko wa Nne: i. Tarehe 8/11/2021 hadi tarehe 26/8/2021

Mzunguko wa Tano : Tarehe 17/1/2022 hadi 4/2/2022

## SEHEMU YA PILI

## UCHUNGUZI WA RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI JUU YA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2020

### 1.3 FUNGU D 01 WIZARA YA NCHI (OR0 TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IARA MAALUM

### Taarifa ya Mapato

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 (AR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ilijipangia kukusanya Tsh 603,119,000 za ada ya ulinzi hadi kumalizika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ilifanikiwa kukusanya Tsh 450,000,000 sawanaasilimia 75 yamakadirio.

| KASMA | MAELEZO | MAKADIRIO KWA MWAKA 2019/2020 | HALISI 2019/2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1422086 | Ada yaUlinzi | 603,119,000 | 550,000,000 | 91 |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa ingawa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 (AR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ (FUNGU DO1) iliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi 604,119,000 katika Bajeti yake na kufanikiwa kukusanya jumla ya 550,000,000 lakini taarifa hizo za mapato hazikuingizwa katika taarifa za kifedha za mwaka za Wizara hiyo (Financial Statement) zilizowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kufanya hivyo, ni kwenda kinyume na kifungu cha 121 (10(a) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.Namba 12 ya 2016. Kamati ilihoji juu ya sababu zilizoplekea Wizara hiyo kufanya kosa hilo, ililelezwa kuwa lilikuwa ni kosa la kibninaadamu tu.

Aidha, Kamati imeabini kuwa Mapato ya Wizara ni ya ulinzi tu unaofanywa na Wakala wa

Ulinzi wa JKU ambapo Kamati ya PAC ilihoji juu ya sababu zilizopelekea Wizara hiyo kutofikia malengo ya makusanyo na kuelezwa kuwa sababu hasa ilikuwa ni maradhi ya Corona (Uviko 19) yaliyopelekea wawekezaji kufunga hoteli zao na hivyo kupelekea kutotolewa kwa huduma ya ulinzi katika mahoteli na mapato hayo kushuka.

Kwa upande wa madeni yatokanayo na huduma za ulinzi Kmati ya PAC imebaini kuwa hadi Kmati ilipokuwtana na Wizara tarehe 17/8/2021, Wakala wa Ulinzi wa JKU inawadai Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) deni la jumla ya shilingi 400,000,000 mablo limekuwa likiendelea kufuatiliwa. Hata hivyo, Wakala wa Ulinzi wa JKU inaenedelea kuipatia NIDA huduma hiyo ya ulinzi.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC.

1. Wizara iwe makini unapoaandaa hesabu zake pamoja na kuzifanyia uhakiki wa kutosha taarifa zake za fedha inazoziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kutekeleza kikamilifu masharti ya Sheria ya Usimamizi Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016.

2. Kwa kuwa Wakala wa Ulinzi wa JKU ni chanzo kizuri cha mapato, Kamati ya PAC iliishauri Wizara iangalie utaratibu utakaoiwezsha Wakala wa Ulinzi wa JKU kutoa huduma za ulinzi hata katika Sekta Binafsi ikiwemo katika mabenki na kampuni mbalimbali ili kuongeza mapato ya Serikali badala ya kazi hizo kufamywa na kampuni nyengine.

Taarifa ya Matumizi

Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa ,Serikali za Mitaa na Idara Maalum ilikadiriwa kutumia jumla ya shilling 24,530,400,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2020.Kati ya fedha hizo shilling 11,169,300,000 zilikadiriwa kutumika kwa matumizi ya kazi za kawaida ,shilling 12,610,000,000 zilikadiriwa kutumika kwa matumizi ya kazi za maendeleo na shilingi 751,100,000 ikiwa ni ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara.

Hadi kufikia Juni ,2020 jumla ya shilingi 21,360,375,947 zimeingizwa na kutumika sawa na asilimia 87 ya makadirio. Kati ya hizo shilingi 9,218,486,295 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 82.5 ya makadirio,shilingi 11,390,786,652 zimetumika kwa matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 90.3 ya makadirio na shillingi 751,100,000 zimetumika kwa ruzuku sawa na asilimia 100 ya makadirio

Majibu ya Wizara

Taarifa za Matumizi za (AR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni kama ifuatavyo:-

MATUMIZI YA KAWAIDA

| SN | MAELEZO | MAKADIRIO | UHALISIA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mishahara | 1,492,500,000/= | 1,696,746,865/= | 114% |
| 2. | MatumiziMengineoOC | 9,676,800,000/= | 7,521,739,430/= | 78% |
| 3. | Ruzukuya OC | 751,100,000/= | 751,100,000/= | 100% |
| | JUMLA | 11,920,400,000/= | 9,969,586,295/= | 84% |

MATUMIZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO

| SN | MAELEZO | MAKADIRIO | HALISI | ASILI MIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MradiwaUgatuziwaMadarakaSeri kalizaMitaa | 1,110,000,000/= | 300,000,000/= | 27 |
| 2. | MradiwaKiwanda cha nguo cha IdaraMaalum(ZQTL) | 4,500,000,000/= | 3,941,531,562/= | 89 |
| 3. | MradiwaMjiSalama (CCTV) | 7,000,000,000/= | 7,149,258,090/= | 102 |
| | JUMLA | 12,610,000,000/ = | 11,390,789,652/= | 90 |

MAELEZO YA MIRADI NA FEDHA ZA MAENDELEO

Mradi wa Mji Salama

Mradi huu ni wa mji salama ,ambapo fedha zake hutumika kuweka miundo mbinu ya CCTV. Kwa upande wa malipo hulipwa moja kwa moja na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mujibu wa mkataba ambapo hadi mwaka ulipomalizika mradi ulitumia Tsh. 7,149,258,090 swa na aslimia 102, omhezeko linatokana na ununuzi wa fedha za kigeni (dollar)

Mradi wa Ugatuzi wa Madaraka ya Serikali za Mitaa

Mradi wa Ugatuzi wa Madaraka ya Serikali za Mitaa umal;izaji wa skuli tatu na m madarasa sitini. Lengo halikufikiwa kutokana na kutoingiziwa fedha za kutosha kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na janga la maradhi lililoikumba dunia kupelekea kusita shughuli za mikusanyika kupunguza maambukizi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji juu ya sababu zililizopelekea ongezeko la mishahara ambapo matumizi ya mishahara yalikuwa kwa asilimia 114 na kuelezwa kuwa ongezeko hilo lilitokana na mishahara kwa ajili ya ajira mpya ambapo wafanyakazi 92 waliajiriwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, ilielezwa kuwa mishahara ya wafanyakzi wapya hupitishwa katika Fungu la Marekebisho ya Mishahara (Salary Adjustment) lililopo katika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

Kamati ya PAC ilikagua baadhi ya vielelezo vinavyohusiana na ajira mpya vkiwemo vibali vya ajira hizo pamoja na barua aliyoandikiwa Katib mKuu Wizara ya Fedha na Mipango ya kuwaombea kuingizwa katika “Pay Roll”wafanyakazi hao wapya (barua ya tarehe 11 Febuari, 2020 yenye nambari ya kumbukumbu AB. 196/240.01/9). Kamati iliridhika na vielelezo hivyo.

Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na taarifa ya matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ iliyowasilishwa mbele ya Kamati, pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Wizara juu ya taarifa hiyo.

Hoja Namba 5.2.1.1 Kushindwa kuthibitisha uwepo wa manunuzi ya shilingi 755,297,780

Ukaguzi umebaini Wizara ya Nchi Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum imefanya malipo ya shilinhi 755,297,780 kwa ajili ya manunuzi ya chakula cha askari wa Idara Maalum, ukaguzi umwbaini dosari zifuatazo katika manunuzi hayo

- Taratibu za kutafuta wasambazaji wa manunuzi hayo hazikupitia kigezo cha manunuzi nauondoshaji wa mali cha Wizara,kufanya hivyo ni kwenda kunyume na kufungu nambari 29(a) cha sharia ya Manunuzi na Ondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

- Ukaguzi haukupatiwa muhtasari wa kikao cha bodi ya zabuni ya Wizara iliyoizinisha taratibu iliyotumika katika manunuzi hayo,kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 28(1) (j) cha sharia ya manunuzi na uondoshaji wa mali za umma sheria nambari 11 ya mwaka 2016.

- Ukaguzi umebaini kuwa taratibu za manunuzi hayo hazikuwa na ushindani angalau wasambazaji watatu wenye uwezo wa ktoa huduma hiyo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 68(3)(b)cha sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma.

Aidha , kutokana na dosari zote zilizobainika ukaguzi umeshindwa kudhibitisha uwepo wa manunuzi yaliyofanyika na uhalali wa upokezi wa chakula kilichonunuliwa katika madaftari ya kutunza kumbukumbu za ghalani . maelezo ya malipo hayo yanaonekana katika jeduweli lifuatalo:-

Jadweli la malipo kwa ajili ya manunuzi ya chakula cha askari wa idara maalum

| Namba | Nambari ya hati ya malipo | Aliyelipwa | Jumla ya fedha (SHS) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 30/11, 7/11/2019 | SABAH STORE | 157,500,690 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya gharamaza chakula kwa ajili ya Askariwapya waliopo mafunzoni. |
| 2 | 39/12, 18/12/2019 | SABAH STORE | 170,763,700 | Ikiwa ni maipo kwa ajili ya ununuzi wa chakula cha wanafunzi walioko mafunzoni katika kambi tofauti |
| 3 | 19/10, 3/10/2019 | SABAH STORE | 157,500,690 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya gharama za chakula kwa ajili ya Askari wapya walioko mafunzoni. |
| 4 | 41,1 15/1/2020 | SABAH SROTE | 170,763,700 | Ikiwa ni amlipo kwa ajili ya ununuzi wa chakula kwa ajili ya askari walioko mafunzoni. |
| 5 | 14,1 9/1/2020 | Mwinyi General Traders | 98,769,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya gharama za chakula kwa ajili ya Askari wapya waliopo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | mafunzoni. |
| | Jumla | 755,297,780 | | |

Majibu ya Wizara

Taratibu za kutafuta wasambazaji wa manunuzi hayo yamepita katika kitengo cha manunuzi na uondoshaji mali cha Wizara kwa mujibu wa sheria nambari 11 ya mwaka 2016 kifungu 29 (a) na kupelekwa katika bodi ya Zabuni ya Wizara.
Aidha, manunuzi hayo yalipita katika kikao cha bodi yazabuniyaWizara, mukhtasari wa vikao vya bodi ya zabuni vipo kwa mujibu wa sheria ya manunuzi na uondoshaji mali za Umma nambari 11 yamwaka 2016.
Ni kweli kuwa taratibu za manunuzi hayo haikuwa na ushindani, Ofisi imenunua chakula kwa kutumia njia ya "single source" kwa mujibu wa sheria ya manunuzi namba 11 ya mwaka 2016 kifungu namba 73(c) inayoruhusu single source kwa ajili ya ulinzi (Protection of National security).
Kumbukumbu za mapokezi ya chakula hicho zimerikodiwa katika madaftari ya kutunzia kumbukumbu za ghalani ambayo yalikaguliwa na wakaguzi wa ndani na wa nje na kuthibitihswa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatatyo:-

i. Kokusekana kwa mashirikiano ndani ya Wizara na baina ya Wizara na Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kumepekea kukosekana kwa maelezo stahiki na vielelezo husika wakati wa ukaguzi. Kamati imethibitishsa kasoro hii baada ya kupitia vielelezo mbalimbali vinavyohusiana na hoja hii ambavyo Wizara ilishindwa kuwapatia wakaguzi kwa wakati. Miongoni mwa vielelezo muhimu ambavyo vilikosekana wakati wa ukaguzi lakini Kamati ilipatiwa na kuridhika navyo ni kumbukumbu za kikao cha Bodi ya Zabuni cha tarehe 24 Septemba 2018 (KCTB/ 2018/2019/03) ambacho kiiipitia kitabu cha Zabuni cha Ununuzi wa Chakula (mchele, unga,wasembe, sukari,,maharagwe na mafuta ya kupikia). kwa ajili ya Idara Maalum.

   Katika kikao hicho ambacho kiliwashirikisha Ma afisa Ununuzi wa Wizara (kama sekretarieti ya Bodi), Bodi ya Zabuni ilikubaliana itumike njia ya kumtumia msambazaji mmoja (single source) na kuamuliwa kupelekewa kitabu hicho Sabah Store, ingawa haikuelezwa katika kumbukumbu hizo sababu za kutumia njia hiyo na sababu ya kumtumia Sabah Store. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilihoji juu ya

vigezo vya kumtumia Sabah Store na kuelezwa kuwa ni Mzalendo, Muadilifu, Amesajiliwa na Mamalaka ya Ununuzi, Mlipa Kodi,na ni makini kwa kuwa Wizara iliwahi kufanya kazi nae bila ya tatizo.

Sambamba na hayo, Kamati ya PAC ilielezwa kuwa wakaguzi kwa upande wao hawakutumia lugha nzuri wakati walipokuwa wakitaka taarifa na vielelezo kutoka kwa watendaji wa Wizara wakati walipokuwa wakifanya ukaguzi

ii. Kutotimizwa kikamilifu kwa Sheria ya Ununuzi na Uondosji wa Mali za Umma. Kifungu cha 36 (2),(3) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Namba 11 ya mwaka 2016 kinavitaka Vyombo vya Idara Maalum kukubaliana na Mamlaka ya Ununuzi kwa kila mwaka juu ya bidhaa ambazo zitanunuliwa bila ya ushindani kuingizwa katika orodha ya za zabuni zilizokuwa sio za ushindani ambapo vyombo hivyo vinapaswa kufanya ununuzi kwa kuzingatia orodha mbili (ununuzi wa vitu vitakavyokuwa na ushindani wa wazi na ununuzi utakaofanywa bila ya ushindani).

Vielelezo vilivyowasilishwa kwenye Kamati ya PAC vinaonesha kuwa Kikao cha Bodi ya Zabuni kichoidhinisha njia ya ununuzi ya "Single Source' kilifanyika tarehe 24 Septemba, 2018 wakati kikao cha makubaliano juu ya orodha za ununuzi baina ya Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma na Idara Maalum za SMZ.kilifanyika tarehe 17/7/2019. Hata hivyo, kwa mujibu wa Ripoti ya makubaliano hayo ununuzi wa chakula ulipaswa ufanyike kwa njia isiyo ya wazi (Restricted) sambamba na kukubaliana kulifanyia utafiti suala hilo, ingawa njia hiyo ya Restricted bidding ni tofauti na njia iliyotumiwa na Wizara ya kumtumia msmbazaji mmoja tu (Single Source).Ingawa njia ya kumtumia msambazaji mmoja (Single Source) inaweza kutumika kwa kuzingatia.sababu zilizowekwa kisheria zikiwemo za kiusalama, kulipaswa kuwe na makubaliano baina ya Idara Maalum za SMZ na Mamlaka ya Ununuzi juu ya matumizi ya njia hiyo ya Single Source kabla ya kufanya ununuzi kama kifungu cha 36 (2) na (3). cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, kinavyoelekeza.

iii. Pamoja na kuainishwa sababu ya kiusalama iliypolekea kutumiaka niia ya kumtafuta msambazaji mmoja wa chakula, Kamati ilelezwa kuwa sababu nyengine ya kutumia njia hiyo ni kuwa kulikuwa hakuna muda wa kutosha wa kuitisha zabuni ya wazi

iv. Kwa upande wa kumbukumbu za mapokezi ya chakula hicho, Kamati ya PAC baada ya kukagua madaftari ya kumbukumbu za ghalani ya Wizara na yale yaliyoko katika kambi za Dunga na Pnagatupu,yanayotunza kumbukumbu za unga wa

sembe, mchele na uskari, Kamati imejiridhisha kuwa chakula hicho kilipokelewa katika kambi za Idara Maalum za SMZ kama kilivyokusudiwa.

Aidha , Kamati ya PAC iliapata nafasi ya kuukagua mkataba baina ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum na Sabah Store (Mkataba Namba; SMZ/D01/GSS/2018/2019/340 wa tarehe 18 Juni, 2019 wenye thamani ya shilingi 1,149,677,760 pamoja na VAT na kuridhika nao.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati ya PAC iliwashauri viongozi na Watendaji wa Wizara washirikiane kwa pamoja katika kutoa maelezo na vielelezo vinavyohusika wakati wa ukaguzi paomja na kutoa ushirikiano kwa wakaguzi kwa kufuatailia kwa karibu zaidi majibu ya hoja za ukaguzi na kuhakisha kuwa hoja hizo za ukaguzi zinapata ufafanuzi wa kutosha kwa wakati unaostahiki.

2. Wizara pamoja na Idara Maalum za SMZ ziandae vizuri mipango ya kazi zao ili wakati wa utekelezaji wa mipango hiyo kusiwe na sababu za ukiukwaji wa Sheria zilizopo ambazo zimetungwa kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli za Serikali.

3. Watendaji wa Wizara wawe na utaratibu mzuri wa utunzaji wa kumbiumbu za nyaraka mbalimblai zikwemo nyaraka za ununuzi na za kifedha ili zinapohitajika kwa ajili ya kazi za Serikali zikiwemo kazi ukaguzi ziweze kupatikana kwa urahisi.

4. Katika kulinda ubora na uhalisia wa ,matokeo ya ukaguzi, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iandae utaratibu wa kuwafuatilia na kuwafanyia tathmini wakaguzi wake ili kubaini iwapo kama kuna dosari zozote zinzoweza kuharibu kazi za ukaguzi na kuzichukulia hatua zinzofaa.

Hoja Namba 5.2.1.2 Dosari zilizobainika katika uhaulishwaji wa shilingi 1,000,000,000

Ukaguzi umebaini Wizara ya Nchi Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum, imefanya uhaulishaji wa shilingi 1,000,000,000 kwa hati nambari 1/5 ya tarehe 04/05/2020 na kuingizwa katika Hesabu ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa ,Serikali za Mitaa na Idara Maalum ,imefanya uhaulishaji wa shilingi 1,000,000,000 kwa hati nambari 1/5 ya tarehe 04/05/2020 na kuingizwa katika hesabu ya Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum kwa ajili ya matumizi ya Wizara , dosari iliyobainika ni kwamba hadi ukaguzi unabainika tumeshindwa kupatiwa kipaumbele kilichopelekea Wizara kufanya uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na matumizi na vieelezo

vya fedha hizo.

Kuwepo kwa bakaa ya fedha ambayo haikutumika kunaweza kupelekea mipango iliyopangwa kushindwa kutekelezwa kwa muda uliopangwa na hatimae kunaweza kujitokeza matumizi ambayo hayakupangwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria nambari 3 ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

### Majibu ya Wizara

Fedha hizi zipo kwenye hesabu ya benki ya Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ajili ya matumizi ya ununuzi wa Zana. Afisi ya Raisi Fedha na Mipango imekubaliana na Afisi ya Raisi, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi huo wa Zana, bajeti yake iko Idara yab Uratib yan Uratib wa Idara Maalum za SMZ, ila kutokana na maradhi yalioikumba dunia imesababisha kutozitumia Fedha hizo kwa wakati. Matumizi yake yalilipwa Regalia shilingi 283,200,000 na pia kulipwa Mzinga Cooperation SHILINGI 284,900,000 na bakaa ya shilingi 431,900,000.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilielezwa kuwa malipo hayo yalikuwa ni kwa ajli ya ununuzi wa zana maalum za Idara Maalum za SMZ na ilikuwa ni kpaumbele cha Wizara  pamoja na Idara hizo Maalum ambapo kwa mujibu wa makubaliano, shilingi 284,900,000 ni malipo ya awali ambayo ni asilimia 22 ya fedha zote.

Kwa ujumla Kamati ya PAC baada ya kupata ufafanuzi na kukagua baadhi ya vieielezo husika, iliridhika na maelezo na vielelezo hivyo.

### Hoja Namba 5.2.1.3 Dosari katika utayarishaji wa malipo ya usambazaji wa madaftari USD 271,448.82

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum ilikuwa inadaiwa jumla ya dola za Marekani USD 157,546 na kampuni ya Young Honey ikiwa ni malipo ya mwisho kwa ajili ya usambazaji wa madaftari. Ukaguzi umebaini katika matayarisho ya malipo hayo Wizara ilifanya uhaulishaji wa jumla ya shilingi 1,000,000,000 kupitia hati nambari 6/12 ya tarehe 2/12/2019 ikiwa sawa na dola za Marekani 428,994.82 kwenda hesabu ya fedha za kigeni ya Wizara yenye nambari

0400018000.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni uwepo wa ziada ya dola za Marekani USD 271,448.82 ambazo ni sawa na shilingi 629,409,464.73 ukilinganisha na fedha halisi zinazodaiwa na msambazaji wa madaftari hayo ambapo vielelezo vilivyopelekea kufanyika kwa ziada hiyo ya malipo havikupatikana kwa ukaguzi, kufanya uhaulishaji wa ziada ya malipo ambayo hayalingani na kiwango halisi kinachodaiwa kunaweza kupelekea uwepo wa matumizi ambayo hayakupangwa. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Wizara

Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ilikiri kuwa kulikuwa na ziada ya fedha kama ilivyoainishwa na mkaguzi, ziada hiyo ilikuwa na lengo la ununuzi wa mabuku kama ilivyoainishwa katika shughuli za Idara ya Uratib wa Serikiali za Mitaa. Ikumbukwe kwamba. Ni maelekezo yalioitaka Wizara kuhakikisha kuna fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya skuli za Maandalizi na Msingi, hata hivyo, ziliendelea kutumika kwa lengo husika. Kwa kutekeleza hilo, Wizara iliingia mkataba na Mchapaji Mkuu wa Serikali kwa lengo la kutengeneza mabuku hayo na tayari ameshalipwa asilimia 40 ya mkataba.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa awali mnamo tarehe 6 Julai 2019, Wizara iliingia mkataba na kiwanda cha kutengeneza madaftari cha  China kiitwacho Anhui Heneyoung Paper Printing Factory kwa ajili ya kupata madaftari ya elimu ya Maandalizi na Msingi , Hata hivyo, Wizara iliachana na huduma za kupatiwa madaftari kutoka Kampuni hiyo ya China na kwa kuwa mahitaji ya vifaa vya huduma ya elimu ya msingi na kati yalikuwa yanaendelea, tarehe 16, April, 2021 Wizara iliingia mkataba na Wakala wa Serikali wa Uchapaji, Zanzibar.kwa ajili uchapiashaji wa madaftari hayo ya elimu ya Maandalizi na Msingi kwa gharama ya shilingi 1,697,,609,040..

Aidha, Kamati ilielezwa kuwa ziada ya fedha hizo ililipwa kwa kuwa lengo la kuipatia huduma elimu ya msngi na kati lilikuwa linaendelea..

.
Kamati ilikagua hati za malipo pamoja vielelezo mbalimbali vinavyohusika ukiwemo Mkataba baina ya Wizara na Wakala wa Serikali wa Uchapaji (Mkataba Namba: SMZ/D01/G/D2020-2021/04) na stakabadhi kutoka Wakala wa Serikali wa Uchapaji yenye namba 01043 yatarehe 6/5/2021 yenye jumla ya shilingi 679,043,616

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Wizara iandae vizuri mipango ya kibajeti ya kazi zake ili uhaulishaji na uingizwaji wa fedha uweze kuakisi mipango na bajeti ya kazi hizo kwa ajili ya kuepusha kuwepo kwa ziada za fedha zinazoonekana kukosa mipango mizuri ya utekelezaji.

ii. Watendaji wawe na utaratibu wa kutoa ufafanuzi wa taarifa za matumizi katika nyaraka muhimu zinazohusiana na masuala ya fedha ili matumizi yanayokusudiwa kufanyika yaweze kufahamika kwa uwazi kulingana na malengo na vipaumbele vya Wizara.

Hoja Namba 5.2.1.4 Kutokuripotiwa kwa bakaa ya dola za Kimarekani USD 856,305.32

Ukaguzi umebaini dosari katika utayarishaji wa taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka za Wizara ya Nchi Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum , dosari hiyo ni kutooneshwa (Disclosure)katika taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka salio la jumla USD 856,305.32 ambazo sawa na shilingi 1,985,518,570.71 katika hesabu za fedha za kigeni ya wizara yenye namabari 0400018000,ukaguzi haukupatiwa vielelezo vya kuwepo kwa bakaa hiyo katika hesabu ya kigeni.

Ukaguzi umebaini kamba fedha hizo zimebakishwa katika hesabu ya Amana bila ya kuwepo kwa ahadi ya matumizi ya shughuli za Wizara na ruhusa ya matumizi kutoka kwa mlipaji mkuu wa Serikali kwa ajili ya kubakisha fedha hizo ili kukidhi mahitaji ya matumizi yaliyokusudiwa baadaye .Kufanya hivyo ni kwendakinyume na kifungu nambari 52(2)cha sheria ya usimamizi wa fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Wizara

Kwa mujibu wa miongozo ya ufungaji wa hesabu za kimataifa zilielekeza kuwepo na maelezo (disclose) kiwango hicho cha fedha kwa bahati mbaya hakikuwepo. Tayari yamefanyika marekebisho katika hesabu za mwaka wa fedha 2019/2020 na USD 856,305.32 zimeonyweshwa kama zinavyoelekezwa na miongozo ya ufungaji wa hesabu. Kufuatia mabadiliko ya uongozi ilichelewa kuwekwa saini na afisa masuli (accounting officer).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilipata nafasi ya kuikagua taarifa ya fedha ya mwaka zinazohusika (Financial Statement) yenye kasoro ambayo iliwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati na ile iliyofanyiwa marekebisho baadae.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wahasibu wa Wizara na Taasisi za Serikali wahakikishe kuwa Ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka unafanyika kwa kuzingatia misingi ya Sheria, Kanuni, Miongozo na viwango viivyopo ikiwa ni pamoja na kuzijumuisha hesabu zote katika taarifa za fedha za mwaka (Financial Statements) kwani kushindwa kuzionesha na kuzitolea taarifa kwa wakati baadhi ya hesabu zikiwemo za bakaa ni dalili za kutaka kutokea upotevu wa fedha za Serikali.

2. Kwa kuwa baadhi ya Wahasibu wanaonekana kufanya kazi zao kwa mazoea, Kamati ya PAC inaishauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuandaa utaratibu wa kufanya vikao vya mara kwa mara na wahasibu wa Wizara na Taasisi za Serikali ili pamoja na mambo mengine kujadiliana juu ya changamoto zinazawakabili pamoja kukiumbushana na kuelekezana juu ya masuala mbalimbali ya kitaaluma katika utekelezaji bora wa kazi zao..

Hoja Namba 5.2.1.5 Malipo yaliyozidi bajeti iliyoidhinishwa katika Mradi wa Mji Salama shilingi 742,769,500

Mradi Mji Salama ulidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 7,000,000,000kwa mwaka wa fedha 2019/2020 , ukaguzi umebaini kufanyika malipo ya shilingi 7,742,769,500 ambayo yamezidi kiwango kilichoidhiniswa kutumika kwa matumizi ya mradi wa mjim salama ,aidha ukaguzi haukupatiwa udhibitisho wa kufanyika kwa uhaulishaji wa fedha kutoka katika mradi mwengine kufidia ziada iliyolipwa katika matumizi ya mradi Mji Salama.
kufanya matumizi ya ziada ambayo ukaguzi umeshindwa kupatiwa uthipitisho na vieelezo vya matumizi hayo yanapelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa matumizi hayo ambayo yanapelekea kuadhiri utekelezaji wa mipango iliyopangwa.
Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1)cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nambari 12 ya mwaka 2016 pamoja na sheria ya nambari 3 ya Makisio na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2019/2010 . Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo

Jadweli la Malipo yaliyozidi bajeti iliyoidhinishwa katika Mradi wa Mji Salama

| namba | Tarehe ya malipo | Jumla ya fedha | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 10/07/2019 | 599,460,000 | ROM Solution | Ikiwa ni malipo ya urejeshaji wa dola za Marekani 257,000 kwa rate |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | ya shilingi 2,328 kwa kampuni ya Rom Solution. |
| 2 | 1/08/2019 | 594,825,000 | ROM Solution | Ikiwa ni malipoyaurejeshaji wa dola za Marekani 257,000 kwa reti ya shilingi 2,310 kwa kampuni ya RomSolution |
| 3 | 2/09/2019 | 594,567,500 | ROM Solution | Ikiwa ni malipoyaurejeshaji wa dola za Marekani 257,000 kwa reti ya shilingi 2,309 kwa kampuni ya RomSolution |
| 4 | 1/10/2019 | 593,537,500 | ROM Solution | Ikiwa ni malipoyaurejeshaji wa dola za Marekani 257,000 kwa reti ya shilingi 2,305 kwa kampuni ya RomSolution |
| 5 | 31/10/2019 | 593,537,500 | ROM Solution | Ikiwa ni malipoyaurejeshaji wa dola za Marekani 257,000 kwa reti ya shilingi 2,305 kwa kampuni ya RomSolution |
| 6 | 2/12/2019 | 1,187,077,000 | ROM Solution | Ikiwa ni malipoyaurejeshaji wa dola za Marekani 514,333.5 kwa reti ya shilingi 2,308 kwa kampuni ya Rom Solution |
| 7 | 2/01/2020 | 595,340,000 | ROM Solution | Ikiwa ni malipoyaurejeshaji |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | wa dola za Marekani 257,000 kwa reti ya shilingi 2,312 kwa kampuni ya RomSolution |
| 8 | 3/02/2020 | 596,112,500 | ROM Solution | Ikiwa ni malipoyaurejeshaji wa dola za Marekani 257,000 kwa reti ya shilingi 2,315 kwa kampuni ya RomSolution |
| 9 | 2/03/2020 | 596,112,500 | ROM Solution | Ikiwa ni malipoyaurejeshaji wa dola za Marekani 257,000 kwa reti ya shilingi 2,315 kwa kampuni ya Rom Solution |
| 10 | 2/04/2020 | 596,112,500 | ROM Solution | Ikiwa ni malipoyaurejeshaji wa dola za Marekani 257,000 kwa reti ya shilingi 2,315 kwa kampuni ya Rom Solution |
| 11 | 4/05/2020 | 597,400,000 | ROM Solution | Ikiwa ni malipoyaurejeshaji wa dola za Marekani 257,000 kwa reti ya shilingi 2,320 kwa kampuni ya RomSolution |
| 12 | 1/06/2020 | 598,687,500 | ROM Solution | Ikiwa ni malipoyaurejeshaji wa dola za Marekani 257,000 kwa reti ya shilingi 2,320 kwa kampuni ya Rom |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Solution |
| Jumla | | 7,742,769,500 | | |

Majibu ya Wizara

Ziada hio sio sahihi kiwango sahihi ni Tsh149,258,090 ambazo zilizozidi kutokana na tafauti ya badiliko la uvunjaji fedha za kigeni (dolar).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na majibu Wizara na haikuwa na maelezo zaidi juu ya hoja hii.

Hoja Namba 5.2.1.6 Dosari katika taratibu za ununuzi wa gari Dola za Kimarekani 316,620

Ukaguzi umebaini Wizara ya Nchi Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum imelipiwa jumla ya dola za marekani 316,620 kupitia Hesabu ya Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali kwenda kwa kampuni ya Kemisy Investment Co. Ltd kwa ajili ya ununuzi wa gari tano (5) kwa matumizi ya Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
Ukaguzi umebaini ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa kutofuatwa taratibu za manunuzi zilizoekwa na Sheria hiyo, dosari hizo ni kama zinavyoonekana:-

- Kutoitishwa kwa zabuni za wazi ya kimataifa ya kuwaalika wasambazaji wenye uwezo wa usambazaji wa gari hizo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 69 (1) cha sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali Umma sheria namba 11 ya mwaka 2016.
- Ukaguzi umebaini Wizara imetumia utaratibu wa manunuzi wa zabuni isiyokuwa ya wazi, hata hivyo ukaguzi haukupatiwa ushahidi kualikwa wazabuni. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 71(3) (a).
- Ukaguzi haukusibitisha idhini ya kikao cha bodi ya zabuni ya Wizara iliyoidhinisha taratibu za manunuzi zilizotumika katika manunuzi ya gari, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 28 (1) (j) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Sheria nambari 11 ya mwaka 2016.

Aidha, msambazaji wa gari hizo hakukatwa kodi ya ongezeko la thamani inayotokana na mauzo ya gari, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) nambari 4 ya mwaka 1998. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli la Malipo yaliyofanyika kwa ajili ya ununuzi wa Gari 5 za Idara Maalum.

| Nambari ya hati ya malipo | Jina la Hesabu | Jumla ya fedha USD | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 49/04/2019 | Hesabu ya huduma za mfuko mkuu wa Serikali | USD 189,972 | Kemisy Investment Co. Ltd | Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa gari 5 za Idara maalum malipo haya ni asilimia 60. |
| 19/10/2019 | Hesabu ya huduma za mfuko mkuu wa Serikali | USD 126,648 | Kemisy Investment Co. Ltd | Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa gari 5 za Idara maalum malipo haya ni asilimia 40 |
| Jumla | | 316,620 | | |

Majibu ya Wizara

Ni kweli kuwa taratibu za manunuzi hayo haikuwa na ushindani, Ofisi imenunua gari kwa kutumia njia ya "single source" kwa mujibu wa sheria ya manunuzi namba 11 ya mwaka 2016 kifungu namba 73(c) inayoruhusu single source kwa ajili ya ulinzi (Protection of National security) na usalama wa Askari. Mukhtasari wa kikao cha bodi ya zabuni ya Wizara kupitia taratibu ya ununuzi iliyotumika katika manunuzi ya gari hizo upo kwa ajili ya ukaguzi, Malipo hayo yamefanywa Wizara ya Fedha na Mipango.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatatyo:

1. Ingawa malipoo ya gari hizo yalifanywa na iliyokuwa Wizara ya Fedha na Mipango lakini mchakato wote wa ununuzi ulifanywa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ambapo Kikao cha Bodi ya Zabuni cha tarehe 24 Septemba, 2018 ndicho kilichoidhinisha kutumika kwa njia ya msambazaji mmoja (Single Source) ambapo gari zote kwa ujumla zilkuwa ni kumi na zilihitajika kwa

ajili ya ulinzi wa Idara Maalum na gari moja ilikuwa aina ya Prado. Bodi hiyo ya Zabuni iliagiza gari tano zinunuliwe kutoka kampuni ya Kemisy Investment Co. Ltd na gari tano zinunuliwe kutoka Kampuni ya Rom Solution.

2. Hakukuwa na uthibitisho iwapo kulikuwa na makubaliano baina ya Idara Maalum za SMZ na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma juu ya njia hiyo iliyotumika ya ununuzi wa gari hizo kama masharti ya .Kifungu cha 36 (2),(3) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Namba 11 ya mwaka 2016 yanavyoelekeza.

3. Kwa upande wa kutolipiwa kodi ya VAT malipo hayo, katika kikao cha pamoja baina ya Kamati ya PAC, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais Twala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kilichofanyika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, tarehe 20/8/2021 kwa ajili ya kujadili hoja hii, Kamati ilielezwa kuwa malipo hayo yalilipwa kwa mujibu wa Mkataba ambapo hakukuwa na kipengele cha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT Exclusive), Hivyo, malipo yamefanyika bila ya kodi hiyo kwa mujibu wa mkataba. Aidha, katika uchunguzi wake Kamati ya PACimebaini kuwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ililipa malipo hayo ya USD 316,620 bila ya VATkwa kufuata kipengele Namba 1 kwenye masharti mahsusi ya mkataba kilichoweka sharti la kulipwa malipo hayo bila ya VAT. (Mkataba Namba SMZ/D01/G/Q/2018/2019/30 uliotiwa saini tarehe 4 Machi, 2019)

Kamati ilikagua nyaraka mbalimbali ukiwemo Mkataba, hati za malipo pamoja na vielelezo vyengine vya ununuzi wa gari hizo zikiwemo ankara (invoices) za Kemisy Investment Co. Ltd (Invoice yenye namba 0122 ya tarehe 25/9/2019 yenye USD 126,648 na Invoice yenye namba 0120 ya tarehe usd 189,972) ambapo Kamati ya PAC iliridhika na nyaraka hizo.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Taasisi zinazohusika na masuala ya kodi (Bodi ya Mapato Zanzibar - ZRB na Mamlaka ya Mapato Tanzania- TRA) ziandae mafunzo maalum na ya mara kwa mara kwa Wziara na Taasisi za Serikali pamoja na Vyombo vya Ukaguzi juu ya masuala ya Kodi na Misamaha ya Kodi ili kupata uchanganuzi mpana na ufahamu wa pamoja juu ya masuala ya kodi hasa misamaha ya kodi inayoainishwa katika mikataba mbalimbali inayoingiwa na Wizara na Taasisi za Serikali.

### Hoja Namba 5.2.1.7 Dosari za taarifa za Mfumo wa Usimamizi wa fedha (IFMIS) na tarifa za hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 593,538,500.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari za taarifa za Mfuko wa Usimamizi wa Fedha na taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka zilizowasilishwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya ukaguzi. Dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kwa mujibu wa taarifa za hesabu wa mwisho wa mwaka zilizowasilishwa kwa ukaguzi, ukaguzi umebaini Wizara ya Nchi Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum imetumia jumla ya shilingi 11,390,328,152 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo,

- Kwa mujibu wa taarifa za mfumo wa Usimamizi wa matumizi (IFMIS) ukaguzi umebaini Wizara ya Nchi Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum imetumia jumla ya shilingi 11,984,328,152 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo na kujitokeza tofauti ya shilling 593,538,500.

Kujitokeza kwa tofauti iliyobainika kumepelekea kutokuwepo kwa uwiyano kati Mfumo wa Usimamizi wa matumizi (IFMIS) na taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka na kupelekea kutokuonesha sura sahihi na halisi.

Majibu ya Wizara

Haya ni Malipo yaliyofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango, malipo haya hayakua na kiasi hicho, kiasi halisi kilicholipwa ni 593,538,500 kwa Rom solution. Tatizo limetokea katika mfumo wa Malipo (System error) kiasi hicho kimejitokeza mara mbili. Kwa mujibu wa mtiririko (exchequer release) wa fedha kutoka Hazina Wizara haikupokea ziada hiyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuifuatilia hoaja hii Kamati ya PAC ilifanya kikao cha pamoja baina yake na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais Twala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kilichofanyika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, tarehe 20/8/2021, ambapo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ilitoa majibu yafutayo:-

Hakuna dosari za kimfumo (IFMS) isipokuwa kulifanyika makosa ya kihasibu wakati wa kuingiza taarifa katika mfumo. Fedha hizo zilikuwa na lengo la kuathiri Bajeti ya Vifungu (Dummy) ambapo muingizaji taarifa aliingiza taarifa mara mbili yaani (shilingi 1,187,077,000), hivyo kihasibu ililazimika irejeshwe kiasi cha shilingi 593,593,538,500 ili kusahihisha makosa ya kihasibu yaliyofanyika.

Tatizo hili ililazimika kuwasilishwa kwa wataalamu na kufanyiwa marekebisho ambayo yanaoneka tarehe 2 Disembs 2019 kwa kumbukumbu namba 147730.

Aidha, Kamati ya PAC imebaini kuwa muingizaji wa taarifa hizo alikuwa ni mtendaji wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na nIdara Maalum ambapo chanzo cha

kuingiza taarifa mara mbili kilikuwa ni kukatika kwa umeme na umeme ulipowashwa, muingizji taarifa aliingiza taarifa mara ya pili alisahau kama taarifa hizo alikwshaziingiza hapo awali.

Pia, Kmati ilibaini kuwa katika mfumo wa fedha, (IFMIS), yanapofonyika marekebisho ya taarifa (data), taarifa iliyokosewa pia inaonekana (haifutiki) na jumla iliyokosewa pia haifutiki. Hivyo kwa taarifa iliyoingizwa mara ya pili unatoa (debit) ili kupata taarifa iliyo sawa na inayokubalika.. Uningizaji wa taarifa (data) zote hizo (za manzo, za mara ya pili/ zilizokosewa, pamoja na za marekebisho huwa zinaonekana katika mfumo).

Kamati ilikagua taarifa zote hizo zilzotoka katika mfumo wa wa IFMIS ambazo zinaonesha mtiririko wa uingizjaji wa taarifa zote hizo ulivyotokezea. Na kuridhika nazo. Hata hivyo ilitoa mapendekezo yake akam ifuatavyo:-

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango itumie utaratibu mzuri zaidi wa kuweka muhusika anaestahili kupewa taarifa pindi watendaji wakifanya makosa katika mfumo wa taarifa za kifedha ili taarifa za makosa hayo ziweze kufahamika kwa uwazi na hatua zilizochukuliwa.
2. Watendaji wanaoingiza taarifa za kifedha katika mfumo wa IFMIS wawe makizi zadi wakati wa uingizaji wa taarifa hizo ili kuepusha makosa ambayo yanaweza kuwaingiza katika matatizo.

## 1.4 FUNGU D 02 JESHI LA KUJWNGA UCHUMI ( JKU)

### Taarifa ya Mapato

Jeshi la kujenga Uchumi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 57,089,000 kupitia vyanzo vyake vya mapato.Hadi kufikia 30 Juni,2020 jumal ya shilingi 46,744,209 zilikusanywa ikiwa sawa na asilimia 82 ya makadirio.

### Majibu ya Jeshi la Kujenga Uchumi

Jeshi la Kujenga Uchumi lina vyanzo vyake vya ndani vinavyotumika kuwasilisha au kuchangia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwaka wa fedha kama ifuatavyo:-

a. Mapato ya kodi za maduka
b. Mapato ya Karafuu
c. Mapato ya Mpunga
d. Mapato ya mazao ya Bustani

e. Mazao ya Baharani
f. Mapato ya kazi ya Useremala
g. Ada ya Mafunzo/Wanafunzi
h. Mapato ya mifugo
i. Mapato ya kazi ya Ujenzi

Kwa mwaka 2019/2020 JKU haikuvuka lengo la makusanyo kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo hali ya hewa namlipuko wa ugonjwa wa Corona. Ni jambo linalofahamika kuwa sehemu kubwa ya vyanzo vya mapato ya JKU yanategemea mvua za msimu ambazo mara nyingi hupekelea kukosekana kwa mavuno ya uhakika hasa mpunga. Lifuatalo ni jeduweli linaloonyesha makadirio na makusanyo pamoja na asilimia ya makusanyo kwa kila fungu.

MPANGO WA UKUSANYAJI MAPATO YA JKU KWA MWAKA 2019/20

| GFS CODE | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO YA MAPATO KWA 2019/20 | MAKUSANYO HALISI 2019/20 | ASILIMIA YA MAKUSANYO KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|
| 1415004 | Kodi ya Maduka | 2,000,000 | 1,600,000 | 80 |
| 1415010 | Karafuu | 5,000,000 | 5,000,000 | 100 |
| 1421004 | Mapato ya Mpunga | 10,000,000 | 7,000,000 | 70 |
| 1421006 | Mapato ya mazao ya Bustani | 8,689,000 | 8,391,808 | 97 |
| 1422027 | Mazao ya Baharani | 2,000,000 | 500,000 | 25 |
| 1422052 | Mapato ya kazi ya Useremala | 2,400,000 | 1,410,201 | 59 |
| 1422088 | Ada ya Mafunzo/Wanafunzi | 18,000,000 | 16,000,000 | 89 |
| 1421011 | Mapato ya mifugo | 4,000,000 | 3,242,200 | 81 |
| 1422085 | Mapato ya kazi ya Ujenzi | 5,000,000 | 3,600,000 | 72 |
| | Jumla | 57,089,000 | 46,744,209 | 82 |

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilihoji juu ya mapato yatokanayo na karafuu na kuelezwa kuwa mapato hayo yanatokana na shamba la mikarafuu ambalo ni moja tu lililoko Machui. Aidha , Kamati ilielezwa kuwa kwa upande wa mapato yatokanayo na bustani hayakuwa ya kuridhish kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Vile vile, Kamati ya PAC ilitaka kujua juu ya

sehemu yanapowasilishwa mapato yatokanayo na hospitali ya JKU na kuelezwa kuwa mapato hayo hutuika katika kusaidia kuchangia huduma mbali mbali za hospitali hiyo zikiwemo huduma za maabara iwapo vifaa kutoka Bohari Kuu ya vinapokuwa havipatikani. Mapato hayo pia huchangia katika upatikanaji wa vifaa vya upasuaji vikiwemo vifaa vya ganzi na vyenginevyo.

Vile vile, Kmati imebaini kuwepo na vyanzo vyengine vya mapato vya JKU vikiwemo duka la dawa na mapato ya mauzo ya misitu na vitalu vya miche. Hata hivyo, vyanzo hivyo vya mapato havijaingizwa katika hatua ya kuanza kuchangia katika mapato ya Serikali.

Kwa kuwa vyanzo vingi vya mapato viliathiriwa na kuzuka kwa maradhi ya Corona, Kmati ilihaji juu ya namna maradhi hayo yalivyoathiri vyanzo mbalimbali vya mapato, na kuelezwa kuwa mapato ya ada za wanafunzi yaliathirika kwa kuwa katika miezi ya Machi, Aprili, Mei na Juni Skuli zilifungwa kutokana na maradhi ya Corona na hivyo ada hizo hazikulipwa. Kazi za Ujenzi pia ziliathirika kutokana na maradhi hayo.

Sambamba na hilo, Kamati ya PAC ilielezwa kuwa JKU inahitaji kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya kuwa na kilimo cha uhakika na kukuza mapato ya mazao ya kilimo (mpunga nakadhalika) lakini hawakupata fedha za kutosha kufanikisha malengo hayo

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kamati ya PAC iliishauri JKU kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kujiepusha kutegemea sana vyanzo vingi vya kutegemea mvua ambavyo havina uhakika.

ii. Katika kuimarisha mapato ya Serikali, JKU kupitia Wakala wa Ulinzi wa JKU lijipange vizuri zaidi ili liweze kutoa huduma za ulinzi katika hoteli mbalimbali na majengo mengine badala ya huduma hiyo kutolewa na kampuni nyengine. za kibinafsi

## Taarifa ya Matumizi

Jeshi la kujenga Uchumi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 3,500,000,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 25,003,206,044 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 97 ya makadirio na jumla ya shilingi 3,485,000,000 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 99 ya makadirio.

## Majibu ya Jeshi la Kujenga Uchumi

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 JKU iliidhinishiwa kutumia jumla ya TZS25,702,522,000/=kwa ajili ya kazi za kawaida na TZS 3,500,000,000/= kwa kazi

za maendeleo. Hadi kufikia Juni 2020, JKU iliingiziwa na kutumia jumla ya TZS25,003,206,044/= ambazo ni sawa na asilimia 97 ya makadirio kwa kazi za kawaida na TZS 3,485,000,000/= kwa kazi za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 99 ya makadirio.Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar lilitekeleza shughuli zake ipasavyo kwa uweledi na ufanisi mzuri kutokana upatikanaji wa fedha kuwa mzuri katika shughuli zote zilizopangwa. Lifuatalo ni jeduweli linaloonyesha makadirio na matumizi halisi ya mshahara, matumizi mengineyo(OC)na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

MATUMIZI YA JKU KWA MWAKA 2019/2020

| S/NO | MAELEZO | MAKADIRIO | MATUMIZI HALISI |
|---|---|---|---|
| 1 | Mishahara | 18,783,500,000 | 22,526,516,910 |
| 2 | Matumizi mengineyo | 2,602,600,000 | 2,476,689,134 |
| 3 | Maendeleo | 3,500,000,000 | 3,485,000,000 |
| | | 24,886,100,000 | 28,488,206,044 |

Kwa upande wa miradi ya maendeleo, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, JKU ilikuwa na muemdelezo wa utekelezaji wa miradi miwili ya maendeleo iliyotengewa jumla ya shilingi 3,500,000,000. Hadi kufikia mwezi Juni 2020, miradi hii iliingiziwa jumla ya shilingi 3,485,000,000. Utekelezaji wa miradi hii ni kama ifuatatavyo:-

a) Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Ufundi ya JKU
Mradi huu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ulitenegewa jumla y shilingi 1,500,000,000 kwa kutekeleza lengo la kuweka jamvi la ghorofa ya pili na kuanza ujenzi wa tofali kwa sehemeu ya chini ya jingo pamoja ya ghorofa ya kwanza. Hadi kufikia Juni, 2020 mradi huu uliingiziwa jumla ya shilingi 1,494,270,000 sawa na aslimia 95. Kwa mwaka huu mradi ulivuka lengo la utekelezaji kwa kuweka jamvi la ghorofa ya pili, kujenga tofali katika sehemu ya chini na ghorofa ya kwanza pamoja na kunyanyua nguzo juu ya ghorofa ya pili.

b) Mradi Wa Ujenzi Wa Mahanga Na Nyumba Za Askari
Mradi huu kwa mwaka fedha 2019/2020 ulitengewa jumla TZS 2,000,000,000 kwa kutekeleza lengo la kuanza ujenzi wa tofali hadi hatua ya linta kwa majengo matatu na kuyaezeka . Hadi kufikia juni 2020 mradi huu asilimia 95. Hadi kufikia mwezi Juni mradi huu , tauari majengo mawili yamahanga na bwalo moja la kulia

kikosi cha JKU Msaani tayari yameshaelekwa na ujeni uliendelea kwa hatua ya kumaliza.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilibaini juu ya ongezeko la matumzi katika mishahara na kuhoji juu y sababu za ongezeko hilo na kuelezwa kuwa ongezeko hilo lilitokana na hii ilitokana na ajira mpya ya Maaskari , upandaji wa vyeo na mapungufu ya bajeti yenyewe tangu mwanzoJKU ilimuandikia barua Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango yenye kumbukumbu namba MMJKU/U.10/2/B/JD.14/75 ya tarehe 20 Machi 2020. Kamati iliagiza kuwasilishwa kwa barua hiyo na barua hiyo iliwasihshwa katika Kamati hapo baadae na kuridhika nayo

Aidha Kamati ilihoji iwapo JKU kama inayo Kamati ya Ukaguzi kama mashrti ya kifungu cha 118(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma inavyoelekeza na kubaini kuwa watendaji wa Jeshi hilo hawana taarifa ya kuwepo kwa Kamati hiyo ya Ukaguzi.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati imeitaka JKU kuhakikisha kuwa Kamati ya Ukaguzi inakuwepo na kufanya kazi kwa mujibu wa Sheria iliyopo.

Hoja Namba 5.2.2.1 Malipo ambayo hayakuzingatia thamani halisi ya fedha, shilingi 1,881,508,822.

Ukaguzi umebaini kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya malipo ya shilingi 1,881,508,822 kwa ajili ya ununuzi na ujenzi wa Skuli ya Ufundi ya JKU kupitia msambazaji wa vifaa Kampuni ya Sabah Store, ukaguzi umebaini kazi iliyofanyika hailingani na kiwango kikubwa cha cha fedha klichotumika katika ujenzi huo, ufanisi na tija ya malipo yaliolipwa haukuweza kufikiwa. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo unaonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jaduweli nambari 8: malipo ambayo hayakuzingatia thamani halisi ya fedha

| Namba | Tarehe | Nambari ya Hati ya Malipo | Jumla ya Fedha Zilizilipwa |
|---|---|---|---|
| 1 | 26/09/2019 | 2/9 | 627,085,750 |
| 2 | 30/09/2019 | ¾ | 84,420,000 |
| 3 | 24/12/2019 | 4/12 | 188,897,500 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4 | 27/12/2019 | 8/12 | 171,105,900 |
| 5 | 27/02/2020 | 3/2 | 350,000,000 |
| 6 | 4/3/2020 | 1/3 | 50,000,000 |
| 7 | 1/6/2020 | 1/6 | 166,138,672 |
| 8 | 1/6/2020 | 2/6 | 132,655,000 |
| 9 | 1/6/2020 | 4/6 | 26,206,000 |
| 10 | 23/06/2020 | 6/6 | 85,000,000 |
| Jumla | | | 1,881,508,822 |

## Majibu ya Jeshi la Kujenga Uchumi

Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Ufundi ya JKU Mtoni umepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka minne ambapo miaka mitatu ilipangwa kwa ujenzi na mwaka wa mwisho kwa ajili ya kupatiwa mashine za karakana za ufundi pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Kwa miaka mitatu yote ya ujenzi (ingawa inaonekana baadae ilitaka kuongezwa kuwa minne), Mradi ulifikia malengo yake kama yalivyopangwa katika Mipango ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2018/2019, 2019/2020 na 2020/2021 kama inavyoonekana hapa chini:

a. Usafishaji wa eneo la ujenzi, kuchimba msingi, kufukia pamoja na kujenga ghorofa ya chini kazi ambayo ilikamilika Juni, 2019.
b. Kuendelea na ujenzi wa ghorofa ya kwanza, ukataji wa madarasa na kufanya kazi za plaster kwa ghorofa ya chini. Kazi hizi zilikamilika Juni 2020.
c. Kunyanyua nguzo na kuweka jamvi la ghorofa ya pili na kuanza ujenzi wa tofali kwa sehemu ya ghorofa ya pili. Kazi hiyo imekamilika Juni 2021.

Hadi kufikia sasa kazi zote zilizopangwa kwa miaka mitatu ya Mradi zimetekelezwa kwa asilimia 100. Hata hivyo kutokana na kuwa malengo yalionekana ni madogo na kupunguzwa katika ngazi za juu, ujenzi uliendelea kwa kazi za ziada na hivyo shughuli zifuatazo zimefanyika katika mwaka ambao ungekuwa wa mwisho:

a. Kujenga nguzo za zege za juu (beams) kwa ajili ya ujenzi wa paa pamoja na kuezeka jengo lote.
b. Kufanya kazi za ukataji wa madarasa katika ghorofa ya pili pamoja na ujenzi wa ukumbi na vyoo.
c. Kukamilisha kazi za plaster kwa baadhi ya sehemu za ghorofa ya chini na ghorofa ya kwanza na sehemu za ghorofa ya pili.
d. Kuanza kazi za rangi pamoja na kufunga vyuma vya varanda na reli na ngazi.
e. Kufunga mfumo wa umeme, maji safi na maji machafu.
f. Kuanza kazi ya kutia tarazzo kwa ghorofa zote za jengo hilo.

Kwa upande wa fedha kwa kipindi hicho Mradi ulitengewa fedha kama inavyoonekana katika jadueli hapa chini:

| MWAKA | FEDHA ILIYOPANGWA | FEDHA ILIYOPATIKANA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| 2018/19 | 1,028,000,000 | 220,058,956 | 21.41 |
| 2019/20 | 1,500,000,000 | 1,494,270,000 | 99.62 |
| 2020/21 | 2,500,000,000 | 1,662,185,725 | 66.00 |
| JUMLA | 5,028,000,000 | 3,376,514,681 | 67.15 |

Kutokana na tathmini hii, inawezekana kuwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati anakagua Mradi huo kwa kipindi hicho, vifaa vingi vilikuwa vimeshaletwa katika eneo la ujenzi lakini kazi iliyokuwa imefanyika ilikuwa bado ni ndogo. Hata hivyo kwa kuwa Mradi ulikuwa umekamatana kutoka awamu moja hadi nyengine, kazi hizo ziliweza kufungamanishwa vyema na hatua iliyofuata katika utekelezaji wa awamu ya tatu ya Mradi. Kwa sababu hiyo, hivi sasa kama utaangaliwa Mradi huo utajieleza wenyewe kuwa kazi imefanyika kwa umakini na kulingana na kiwango cha fedha iliyotolewa. Kwa lengo la kujiridhisha, naomba Mwenyekiti na Kamati yako hii ifike kwenye eneo la ujenzi ili kuona kwa karibu haya tunayoyaeleza.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji juu ya viwango tofauti vya fedha vilivyoonekana kutumika katika miradi ya maendeleo kwa mwaka 2019/2020 ambapo katika hoja ya Mdhibiti ilibainisha jumla ya shilingi 1,881,508,822 wakati katika majibu ya ufafanuzi ya JKU ziliainishwa shilingi 1,494,270,000 ambazo zilitumika katika miradi ya maendeleo kwa mwaka 2019/2020. Kutokana na tofauti hiyo Kamati ya PAC ililiagiza Jeshi la Kujenga Uchumi kutafuata usahihi wa matumizi hayo na kuwasilisha kwa Kamati ya PAC hapo baadae (tarehe 16/8/2021) pamoja na kutoa ufafanuzi wake.

Aidha, Kamati ya PAC ilipohitaji nyaraka za Zabuni zilizohusika ilielezwa kuwa mnamo mwezi Novemba 2020, JKU ilitakiwa kuwasilisha nyaraka halisi za mikataba na BOQ katika Mamlaka ya Kuzuwia na kupambana na RushwaZanzibar (ZAECA). Hadi wakati huo (tarehe 9/8/2021)nyaraka hizo zilikuwa zipo ZAECA kwa hatua za uchunguzi.

Katika Uchunguzi wake kupitia kikao hicho cha awali baina yake na JKU kilichofanyika tarehe 9/8/2021 Kamatu pia ilibaini mambo mengine yafuatayo:

i. Kuwepo kwa mazingira yaliyotiliwa shaka ambapo ankara (invoice) za malipo zilikuwa zikiwasilishwa JKU kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango badala ya kuwasilishwa na msambazaji mwenyewe moja kwa moja katika Ofisi za JKU, Aidha, wakati uongozi wa JKU unapokuwa ukipitia nyaraka stahiki kwa ajili ya kutaka kufanya malipo hubaini kuwa msambazi huwa ameshalipwa moja kwa

moja kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

ii. Kukosekana kwa uhalisia wa bei za vifaa vya ujenzi zilizoainishwa katika ankara (invoices) zilifanyiwa malipo. Kamati imebaini kuwa baadhi ya bei za vifaa vya ujenzi zilizoainishwa katika Ankara zilikuwa ni kubwa zaidi kuliko bei halisi ya bidhaa hizo iliyokuwa katika soko kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Miongoni mwa bidhaa hizo ni saruji ambapo katika ankara (invoice) yenye namba 0381 ya tarehe 13/11/2019 iliainishwa kuuzwa shilingi 22,000 kwa mfuko mmoja. Katika miradi mengine kama hiyo ya ujenzi kwenye Taasisi za Serikali kwa kipindi hicho hicho cha mwaka 2019/2020, mfuko mmoja wa saruji uliainishwa kuuzwa shilingi 14,000 ambayo ndiyo iliyokuwa bei ya sokoni kwa wakati huo. Hali hiyo, imepelekea kukosekana kwa thamani halisi ya fedha katika matumizi ya fedha za mradi huo (Value for Money)

iii. Kusitishwa kuingiziwa fedha za maendeleo kutoka Serikalini kwa ajili ya ujenzi wa Skuli ya JKU Mtoni ambapo JKU kuanzia mwaka 2020/2021 imekuwa ikitumia fedha zake za ndani kwa ajili uendelezaji wa ujenzi huo.

iv. Kuwepo kwa miradi mikubwa ya ujenzi zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja ambapo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 JKU ilikuwa ina miradi miwili kwa wakati mmoja ambayo ni ujenzi wa Skuli ya Ufundi Mtoni na Ujenzi wa Kambi ya JKU Msaani (Pemba). Kwa mujibu makubaliano baina ya JKU na Sabah Store yaliyoingiwa tarehe 1 Julai 2018, gharama za usambazaji wa vifaa vya ujenzi kwa Unguja ni shilingi 2,988,759,460 na kwa Pemba ni shilingi 1,791,844,476 kwa Pemba na kufanya jumla ya fedha zote kwa ajili ya vifaa vya ujenzi kwa Unguja na Pemba) ni shilingi 4,786,,603,927 pamoja na VAT.

Katika taarifa ya ufafanuzi wa ziada juu ya utofauti baina ya shilingi 1,494,270,000 zilizoainishwa katika Ripoti ya Majibu ya JKU na shilingi 1,881,508,822 zilizoaininshwa katika Hoja hii kwenye Ripoti ya Mdhibiti, JKU iliwasiliosha taarifa ya ufafanuzi ifuatayo:-

Ufafanuzi wa fedha TZS 1,494,270,000/ na sio TZS 1,881,508,822 zilizoelezwa na CAG

Mapitio tuliofanya katikaNambari8 la Mkaguzi na Mdhibiti Mkuuwa Serikali yamebaini kuwepo mambo matatu ndio sababu ya kutofautiana hesabu yake na zile tulizonazo ndani ya JKU . kwa kipindi hiki , JKU ilikuwa inatekeleza miradi miwili ambayo ni ule wa skuli ya Ufundi Mtoni na ujenzi wa mahanga na Nyumba za Watumishi huko Msaani na wakati huo huo palikuwepo na shughuli za kumalizaia malipo ya Mradi ya Jengo la Skuli ya Sekondari . kwa sababu hiyo, malipo yaliofanyika kwa kipindi hicho kama yanavyooneshwa hatika hati ya malipo yanaweza kugawanyika katika sehemu mbili kubwa kama ifuatavyo

a) Kulipia malipo ya Skuli ya Sekondari au Skuli ya Ufundi ambayo yanaonekana katika hati ya malipo ambayo barua yake ina maelezo yenye tafsiri hizo

| S/NO | TAREHE | NAMBA YA VOCHA NA MAELEZO | FEDHA ILIYOTUMIKA |
|---|---|---|---|
| 1. | 26SEP 2019 | DO2PV1900000127 Skuli ya Sekondari | 627,085,750 |
| | | JUMLA | 627,085,750 |

b) . Kulipia vifaa vya Sekondari na Ufundi kwa wakati Mmoja kama inavyoonekana katika hati za malipo zifuatavyo

| S/NO | TAREHE | NAMBA YA VOCHA NA MAELEZO | FEDHA ILIYOTUMIKA |
|---|---|---|---|
| 1 | 24DEC 2019 | D02VI900000293 Sekondari na Ufundi | 188,897,500 |
| 2 | 27 FEB 2020 | D02VI900000378 Sekondari na Ufundi | 359,000,000 |
| 3 | 4 MAR 2020 | D02VI900000379 Sekondari na Ufundi | 50,000,000 |
| 4 | 01 JUN 2020 | D02VI900000490 Sekondari na Ufundi | 132,655,000 |
| | | JUMLA | 722,552,500 |

c) Kulipia vifaa vilivyotumika kwa ujezi wa Kikosi cha JKU Msaani kama inavyoonekana katika hati ya malipo ifuatavyo

| S/NO | TAREHE | NAMBA YA VOCHA NA MAELEZO | FEDHA ILIYOTUMIKA |
|---|---|---|---|
| 1 | 23 juni 2020 | D02VI900000526 Kikosi cha JKU Msaani | 85,000,000 |
| | | JUMLA | 85,000,000 |

Kwa muhtasari , hali hii inaashiria kuwa hesabu za hakika ambazo zimetumika kwa Skuli ya Ufundi peke yake ni TZS 1,074,956,322 na fedha iliyobaki iimekuwa na mashirikiano kati ya Skuli hiyo ya Ufundi, malipo ya baadhi ya madeni ya vifaa vya ujenzi vya Skuli ya Sekondari na vile vya Ujenzi wa JKU Msaani.

Kwa sabubu hiyo hitimisho la maelezo haya linapatikana kwa Mradi katika Taatifa ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa JKU kwa mwaka wa huo ambao unaonesha kuwa fedha iliyopatikana kwa Mradi ya Ujenzi wa Skuli ya Ufundi Mtoni ni TZS 1,493,270,000/=.

Kwa kmuzingatia ufafanuzi huo na kutokana na Kikao chengine kilichofanyika tarehe 16/8/2021 baina ya PAC na JKU kilichojadili uchanganuzi wa fedha hizo za miradi Kamati ya PAC iliendelea kubaini yafuatayo:-

1. Uwekaji mbaya wa kumbukumbu za matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo ambapo matumizi na nyaraka za matumizi ya fedha za miradi tofauti kuchanganywa pamoja na hivyo kuwepo kwa ugumu wa kuchanganua matumizi halisi yaliyofanyika kwa kila mradi.

2. Fedha za ujenzi wa Skuli ya Ufundi Mtoni kuhaulishwa na kutumika katika ujenzi wa kambi ya JKU Msaani bila ya kuwepo kwa umaKini katika uwekaji wa takwmu za matumizi ya miradi hiyo.

3. Kukosekana kwa utaalaum wa kutosha na uzoefu katika masuala ya fedha, ununuzi na usimamizi wa miradi mikubwa ya ujenzi.

Katika kikao cha Kamati ya PAC na Mamlaka Kuzuia Rushwa na Uhujumu Ucbumi (ZAECA) kilichofanyika katika Ofisi za Mamlaka hiyo tarehe 12/11/2021 kwa ajili ya kufuatilia nyaraka zinazohusiana na Hoja hii, ilibainika kuwa nyaraka nyingi zilizoko ZAECA ni kopi ambapo ni baadhi tu ya nyarakhizo ndio halisi (original) ikiwemo michoro, tofauti na ilivyolezwa na watendaji wa JKU kuwa nyaraka zote halisi za mchakato wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi (nyaraka za Zabuni, BOQ na mkataba) zipo ZAECA. Hata hivyo, Kamati ilizikagua nyaraka hizo pamoja na nyenginezo zinazohusiana na Hoja hii.

Katika Uchunguzi wake wa nyaraka za ununuzi zikiwemo kumbukumbu za Vikao vya Bodi ya Zabuni vilivyohusika na Zabuni hii (kikao cha tarehe 3/9/2018, Kikao cha tarehe 17/9/2018 na Kikao cha tarehe 21/ 9/2018) pamoja na Ripoti ya Kamati ya Tathmini iliyotoa tathmini ya Zabuni hiyo (mwezi wa Septemba 2018). Kamati ya PAC imebaini yafuatayo

i. Wajumbe wa Bodi ya Zabuni ndio hao hao walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati ya Tathmini ya Zabuni hiyo.Kifungu cha 33 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016 kinaelekeza kuwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, Afisa Mhasibu, Bodi ya Zabuni, Kitengo cha Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Idara husika na Kamati ya Tathmini zitafanya kazi zake bila ya kuingiliwa kulingana na kazi na uwezo wao. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(4)(iv), Mjumbe wa Bodi ya Zabuni hafai kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Tathmini ya Zabuni katika Taasisi husika, Hivyo, kuteuliwa kwa Wajumbe wa Bodi ya Zabuni kuwa Wajumbe wa Kamati ya Tathimin ya Zabuni hiyo ni ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma na pia ni kwenda kinyume na misingi ya Utawala Bora kukaribisha mgongano wa maslahi katika mchakato wa Ununuzi wa mali za Umma.

ii. Kamati ya PAC baada ya kupitia michoro iliyoonekana kwa ujenzi wa Chuo cha

ufundi imebaini kuwa michoro haiendani na uhalisia wa ujenzi uliotakiwa katika mpango kazi wa awali kwani kulikusudiwa madarasa 40 badala yake mchoro unaofanyiwa kazi umeonyesha madarasa 16, hakukuwa na taarifa za maandishi inayoonesha sababu ya mabadiliko hayo ya kupungua kwa idadi ya madarasa.

iii. Kujitokeza kwa mkanganyiko kwenye Ripoti ya Tathimini ya Zabuni hiyo ya Ununuzi wa vifaa vya ujenzi ambapo ukurasa wan nje wa Ripoti hiyo (Cover Page) inaonesha hiyo ni Zabuni ya Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi wakati ambapo maelezo ya utangulizi yaliyomo ndani ya Ripoti hiyo yanaonesha ununuzi wa kompyuta kwa ajili ya Skuli ya Ufundi ya JKU.

iv. Kutokana na ripoti ya tathmini Kampuni zilizoshindana na M/S SABAH STORE hazikuwa na uwezo kwani kampuni ya M/S BABA THREE ilikuwa haina kigezo chochote kati ya vigezo vilivyohitajika katika Zabuni hiyo na kampuni ya IRRA AUTO PARTS haikuwa na taarifa za kibenki. Hivyo, kampuni hizi mbili zilikuwa kama zinaishindikiza tu kampuni M/S SABAH STORE kuwa mshindi.

v. Kamati ya PAC imebaini makubaliano ya kusambaza vifaa vya ujenzi kwa Kampuni ya M/S SABAH STORE na JKU ya tarehe 01/07/2020 kwa thamani ya Tsh. 1,950,000,000/= bila kodi ambapo hakuna nyaraka yeyote inayoonesha mchakato wa kuipata kampuni hiyo.

Kwa ujumla, Kamati ya PAC haikuridhika na matumzi ya fedha yaliyofanyika katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Skuli ya Ufundi ya JKU Mtoni.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Serikali ichukue hatua za makusudi za kuhakikisha kuwa JKU linakuwa na watendaji walio weledi na wanaoweza kufanya kazi hasa katika michakato ya ununuzi wa mali za umma kwa kufuata misingi Sheria, Kanuni na taratibu za ununuzi na Uondoshaji wa mali za umma ili kuliepusha Jeshi hilo kujiingiza katika ukiukaji wa Sheria unaoweza kusababisha upotevu wa fedha za Serikali.

## 1.5 FUNGU D 03 CHUO CHA MAFUNZO

### Taarifa ya Mapato

Chuo cha Mafunzo kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 54,541,000 ni makusanyo kutoka vyanzo vya mapato ya Chuo cha Mafunzo. Hadi kufikia 30 Juni,2020 jumal ya shilingi 45,215,000 zilikusanywa ikiwa sawa na asilimia 82 ya makadirio.

### Majibu ya Chuo cha Mafunzo

Chuo cha Mafunzo kilikadiriwa kukusanya jumla ya Sh 54,541,000 katika kipindi cha mwaka 2019/2020. Hadi kufikia tarehe 30,Juni 2020 jumla ya Sh 45,215,000 zilikusanywa sawa na asilimia 82% ya makadirio. Jaduali lifuatalo linaonesha makadirio na makusanyo

yaliokusanywa pamoja na asilimia ya mapato kwa kila chanzo.

TAARIFA YA UKUSANYAJI MAPATO YA CHUO CHA MAFUNZO KWA MWAKA 2019/2020

| Kasma | Chanzo cha makusanyo | Makisio 2019/2020 | Makusanyo halisi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1421002 | Kazi za Mikono | 5,375,000 | 4,220,450 | 61% |
| 1421003 | Mapato ya Viwanda vidogo vidogo | 10,000,000 | 6,277,550 | 63% |
| 1422068 | Mapato ya mashamba na mifugo | 14,000,000 | 11,922,840 | 85% |
| 1422085 | Malipo kwa kazi za ujenzi | 25,166,000 | 22,794,160 | 91% |
| | Jumla | 54,541,000 | 45,215,000 | 82% |

Chuo Cha Mafunzo haikufikia lengo la makusanyo kutokana na sababu mbali mbali zifuatazo:

a. Mabadiliko ya tabia ya nchi yaliyosababisha kupungua kwa kiwango cha uzalishaji wa mazao ya kilimo.
b. Kupungua kwa upatikanaji wa mapato katika vyanzo vyetu vikuu kama vile kazi za mikono,mifugo na ujenzi.
c. Kazi za ujenzi wa Nyumba za Askari,Mahanga na majengo ya urekebishaji kumepelekea kupunguza kazi za ujenzi kwa taasisi za nje ambazo zinachangia kwa kiasi kikubwa mapato ya Chuo cha Mafunzo.
d. Kutokulipwa kwa mapato kwa baaadhi ya taasisi za serikali tunazozifanyia kazi kama vile Chuo Cha Utawala wa Umma (IPA), ofisi ya makamo wa pili wa Rais,Manispaa Magharibi "B",Chuo cha Uandishi wa Habari n.k

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilibaini kuwa Chuo cha Mafunzo kinadai madeni mengi wanadai kutoka baadhi ya taasisi za serikalini ambazo zimefanyiwa kazi za ujenzi na Chuo cha Mafunzo ingawa kwa hivi sasa kaza huduma za ujenzi hawattoi tena.. Aidha, Kamati ilihoji juu ya sababu za kushuka kwa mapato ya kazi za mikono na mifugo na kuelezwa kuwepo kwa mabadiliko ya hali ya hewa pamoja na kutokuwa na soko la uhakika kwa bidhaa wanazozalisha ni miongoni mwa sababu za kushuka kwa mapato yatokanayo na shughuli hizo. Kwa upande wa kazi ujenzi mapato yamepungua, hii inatokana na kampuni za ujenzi zimekuwa nyingi na pia sabaubunya UVIKO 19 umesababisha vipato vya watu wengi vimeshuka .

Vilevile Kamati ya PACilihoji iwapo kuna vyanzo vyenine vya mapato vya Chuo cha Mafunzo na kuelezwa vyanzo vyengine vilivyopo kama vile biashara , mashamba na mifungo ambavyo havikuorodhesha kwenye majibu ya kikosi.

Taarifa ya Matumizi

Chuo cha Mafunzo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kilikadirwa kutumia jumla ya shilingi 16,133,500,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na jumla ya shilingi 1,000,000,000 zilikadiriwa kutumika kwa matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia tareje 30 Juni 2020 jumla ya shilingi 17,725,,206,371 zilitumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 109 ya makadirio na shilingi 1,000,000,000 zilitumika kwa matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 100 ya makadirio.

Majibu ya Chuo cha Mafunzo

Chuo Cha Mafunzo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kilikadiriwa kutumia jumla ya Sh.16,133,500,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na sh 1,000,000,000 kwa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia June 2020, jumla ya shilingi 17,725,206,371 zimeingizwa sawa na asilimia 109 kwa kazi za kawaida na shilingi 1,000,000,000 sawa na asilimia 100 kwa kazi za maendeleo.

Jaduali Lifuatalo linaonesha makadirio na matumizi halisi ya mshahara na kazi za kawaida ( OC) kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

TAARIFA YA MATUMIZI YA CHUO CHA MAFUNZO KWA MWAKA 2019/2020

| S/N | Kifungu | Makisio ya mwaka 2019/2020 | Matumizi halisi mwaka 2019/2020 | Asilimia | Ongezeko |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mishahara | 13,610,500,000 | 15,014,916,250 | 110% | 1,404,416,250 |
| 2 | Matumizi Mengineyo | 2,523,000,000 | 2,710,290,121 | 107% | 187,290,121 |
| JUMLA KUU | | 16,133,500,000 | 17,625,225,588 | 109% | 1,591,706,371 |

Fedha za mishahara zimeongezeka kutokana na kupandishwa vyeo kwa maafsa na wapiganaji wapatao 315(ASP-10,INSP-25,A/INSP-22,RSM-1,S.MAJOR-4,S/GNT-39,SGNT-66,CPL-148) pamoja na kuajiriwa wapiganaji wapya 445(mkupuo wa tatu-03).

Fedha za matumizi ya kawaida zimeongezeka kutokana na uhitaji wa ziada wa chakula cha

kuwalishia wanafunzi na mahabusu ambapo idadi halisi ya Wanafunzi na mahabusu kwa kipindi cha 2/8/ 2019 ilikuwa ni 660 (mahabusu 293 na wanafunzi 367) hadi kufikia 5/03/2020 idadi halisi ya wanafunzi na mahabusu iliongezeka hadi kufikia 896 (mahabusu 432 na wanafunzi 464) .

Ongezeko la mahitaji ya chakula cha Askari wapya baada ya kutoka kozi (mkupuo wa tatu 03) nalo pia limesababisha kuongezeka kwa matumizi ya fedha za- OC.

Kwa upande wa Mradi wa Maendeleo. Idara ya chuo cha mafunzo iliweza kufanya ujenzi na Ukarabati kwa Mradi wa Mahanga na Nyumba za Askari katika kambi ya Kangagani kwa thamani ya TZS 1,000,000,000

Jaduweli lifuatalo; linaonesha makadirio na matumizi halisi ya kazi za maendeleo zilizofanywa na Chuo Cha Mafunzo kwa mwaka 2019/2020.

| JINA LA MRADI | MAKADIRIO | MATUMIZI HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Ujenzi na ukarabatiti wa Nyumba za Askari na Mahanga | 1,000,000,000 | 1,000,000,000 | 100% |
| Jumla kuu | 1,000,000,000 | 1,000,000,000 | 100% |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji kuhusu ungezeko la mishahara kutoka 13,610,500,000 mapaka 15,014,916,250 kuelezwa kuwa lilitokana na kupandishwa vyeo wafanyakazi 315 na waajiriwa wapya na kamati ikekagua vielelezo

Kamati ya PAC imekagua barua inayohusu waajiriwa wapya yenye nambari ya kumbu OR/I.M/ Y.1.O / VOL .XVJ/21 ya tarehe 16/03/2020, Aidha Kamati ya PAC ilikagua barua inayohusu maombi ya kupandishwa vyeo maafisa 25 iliyokwenda kwa Katibu wa Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ( barua ya tarehe 5/11/2019 yenye nambari ya kumbu MF/K25/VOL.II/47/2019).Aidha, Kmati ya PAC ilikagua vielelezo mbalimbali vinavyohusu mradi wa maendeleo wa ujenzi na ukarabati wa nyumba za Askari. Kwa ujumla Kamati imeridhika na ufafanuzi ulioteolewa pamoja vielelezo vilivywasilishwa kwake kwa ukaguziz

Hoja Namba 5.2.3.1 Kukosekana kwa ripoti ya ukaguzi wa ndani

Kwa mujibu kifungu namba 117 cha sheria ya usimamizi wa fedha namba za umma 12 ya mwaka 2016 inamtaka Afisa Mas uul (accounting Officer)kuanzisha kitengo cha ugaguzi

wa ndani ambacho ni imara na madhubuti kwa lengo la kuimarisha udhibiti wa ndani hadi ukaguzi unakamilika Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani wa Idara ya Vyuo vyA Mafunzo haikupatiwa kwa ukaguzi ,kutoa ndaa taarifa ya mwaka ya ukaguzi wa ndani ni kwenda kinyume na kifungu namba 117(6)cha sheria ya usimamizi wa fedha za Umma na Sheria namba 12 ya mwaka2016

Majibu ya Chuo cha Mafunzo

Chuo cha Mafunzo kilikiri kuwa wakaguzi hawakuweza kupata ripoti ya ukaguzi wa ndani ya Idara ya Chuo Cha Mafunzo ingawa wakaguzi wa ndani walifanya ukaguzi na kuwasilisha ripoti ijapokuwa si katika wakati husika ambapo wakaguzi waliweza kuhitaji.Rejea barua ya tarehe 10/05/2021,kumbu; OR/I.M/V.10/C.2/VOL.VI/10. kuhusu kuwasilisha ripoti ya Mkaguzi wa ndani.

Uchunguzi wa Kamatiya PAC

Kamati imebaini kuwa wakati Mkaguzi Kutoka Ofisi ya Mdhibti alipofika katika Chuo cha Mafunzo kwa Ukaguzi ailipokwenda kwa ajili ya ukaguzi wakaguzi wa ndani wa Chuo cha ,Mafunzo walikwenda kwenye mafunzo, hivyo kupelekea kukosekana kwa Ripoti ya Ukaguzi wa ndani

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Chuo cha Mafunzo pamoja na Idara nyengine za SMZ ziandae utaratibu mzuri utakaowezesha kazi za ukaguzi wa ndani ziweze kuendelea pindi inapotokezea watendaji wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (katika Idara Maalum) wanapokwenda kozi ili Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani iweze kupatikana kwa wakati hasa kwa kuzingatia kuwa Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti anategemea sana Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani ili aweze kufanya Ukaguzi wake.

Hoja Namba 5.2.3.2. Kutokufanya kazi kwa Kamati ya ukaguzi

Kwa mujibu kifungu namba 118 cha sheria ya usimamizi wa fedha namba za umma 12 ya mwaka 2016 inamtaka Afisa Masuuli (accounting Officer) kuanzisha kamati ya ukaguzi kwa ajili ya kutathamini mfumo wa udhibiti wa ndani. Ukaguzi umeshindwa kudhibitisha ufanyaji kazi wa kamati ya ukaguzi,kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 118 cha sheria cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Chuo cha Mafunzo

Ni kweli ukaguzi umeshindwa kutathmini ufanyaji kazi wa kamati ya ukaguzi wa ndani ya Idara ya Chuo Cha Mafunzo kwa sababu hadi kufikia muda wa ukaguzi kamati hiyo ilikuwa bado haijakamilisha muundo wake ambapo katika kuiunda kamati hiyo Idara Maalum za

SMZ zilitakiwa kuteuwa wajumbe ambao wataweza kushiriki,rejea barua ya tarehe 21/4/2020 yenye Kumbukumbu OR/I.M/V.10/C.2/VOL.VI/30 kutoka wizarani iliagiza kuundwa kwa kamati ya ukaguzi na barua ya tarehe 13/5/2020 ya kumteuwa mjumbe huyo kutoka Chuo cha mafunzo ili kuweza kushiriki katika kamati hiyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilithibitisha kutokea kwa dosari hiyo ya kuche;elewa kuundwa kwa Kamati ya Tathmin ili kuweza kutathamini mfumo wa udhibiti wa ndani. Kamati ilijiridhisha na hatua zilizochukuliwa kupitia vielelezo husika kama ivilivyoainishwakatika majibu ya Chuo cha Mafunzo

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaitaka Ofisis ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali Za Mitaa na Idara Maalum kuhakikisha Kamati ya ukaguzi wa ndani inakuwepo na inafanyakazi zake kwa mujibu wa kifungu cha 118 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma 12 ya mwaka 2016 kinachomtaka Afisa Masuuli (accounting Officer) kuanzisha Kamati ya Ukaguzi wa Ndani kwa ajili ya kutathamini mfumo wa udhibiti wa ndani.

Hoja Namba 5.2.3.3 Dosari katika malipo ya fedha za maendeleo shilingi 536,427,750

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Chuo Cha Mafunzo kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya kuendesha miradi miwili ya ujenzi wa gereza la watoto na ujenzi wa nyumba za askari katika kambi ya Tungamaa Pemba hadi kufikia 30 juni ,2020 jumla ya shilingi 1,000,000,000ziliingizwa na kutumika .

Ukaguzi umebaini kati ya shilingi 1,000,000,000 ziliingizwa na kutumika jumla ya shilingi 536,427,750 zililipwa katika hesabu ya Chuo cha Mafunzo na Duka la Chuo cha Mafunzo badala ya kulipwa kwa Msambazaji kampuni ya Sabah Store ambaye ndie ameingia Mkataba na Chuo cha Mafuzo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa miradi hiyo ukaguzi haukupatiwa vielelezo vya kudhibitisha matumizi ya fedha hizo kutumika katika miradi iliyokusudiwa , kufanya hivyo ni kwenda kinyume kifungu nambari 34(1)cha sheria ya usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Maelezo ya malipo hayo yanaonekana katika jaduweli lifuatalo

| Namba | Tarehe ya malipo | Nambari ya hundi | Jumla ya fedha(SHS) | Alielipwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 25 julai 2019 | 50001064 | 87,930,000 | Duka la Chuo Cha Mafunzo |
| 2 | 5 Agosti 2019 | 50001105 | 80,000,000 | Duka la Chuo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Cha Mafunzo |
| 3 | 3 Disemba | 50001350 | 20,000,000 | Duka la Chuo Cha Mafunzo |
| 4 | 27Disemba 2019 | 50001445 | 97,000,000 | Duka la Chuo Cha Mafunzo |
| 5 | 30 Disemba 2019 | 50001678 | 96,000,000 | Duka la Chuo Cha Mafunzo |
| 6 | 9 April 2020 | 50001775 | 24,045,000 | Duka la Chuo Cha Mafunzo |
| 7 | 1 juni 2020 | 50001874 | 92,021,000 | Duka la Chuo Cha Mafunzo |
| Jumla | | | 536,427,750 | |

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kufanya matumizi kwa kufuata bajeti iliyoidhinishwa fedha iliyopangwa katika miradi inatumika kama ilivyokusudiwa

Majibu ya Chuo cha Mafunzo

Ni kweli wakaguzi walipokuja waligundua jumla ya shilingi 536,427,750 zililipwa katika hesabu ya Chuo Cha Mafunzo na Duka la Chuo Cha Mafunzo badala ya kulipwa kwa msambazaji kampuni ya SABAH STORE ambae ndie ameingia mkataba na Chuo Cha Mafunzo kwa ajili ya ununuzi wa vifa vya ujenzi wa miradi hiyo, Chuo Cha Mafunzo kiliamua kufanya hivyo kwa sababu zifuatazo:

1) Ucheleweshaji wa vifaa, Msambaziji ambae tuliingia nae mkataba wa usambazaji wa vifaa alikua anacheleweshа sana kuleta baadhi ya vifaa pale idara inapohitaji vifaa hivyo.
2) Mzabuni kukiuka masharti ya mkataba kwa kusubiria malipo kabla ya kusambaza bidhaa hii hupelekea baadhi ya vifaa kuchelewa kuwasilishwa kwenye eneo husika na ndio maana Idara iliamua kununua yenyewe kupitia duka
3) Baadhi ya vifaa alivyokua akitusambazia tulibaini havikukidhi viwango( low quality) na baadhi ya wakati tulivirejesha.
   Hata hivyo; kabla ya kulipwa hesabu ya Chuo Cha Mafunzo na Duka la Chuo Cha Mafunzo kulifanyika vikao mabali mbali baina ya Chuo Cha Mafunzo na supplier kwa lengo la kumlalamikia kuhusu changamoto hizo sambamba na kumuandikia barua ya wito ili kuweza kuzirekebisha changamoto hizo (barua ya tarehe 23/12/2019 yenye kumbu:MF/W.IB/14/2019

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilihoji kuhusu taratibu walizozitumia katika kuipata kampuni ya SABAH STORE na kielezwa utaratibu uliotumika kuwa ni RETRICTRED TENDER

Aidha, Kamati ya PAC ilikagua vielelezo mababmbali vinavyohusianana Hoja hii vikiwemo mkataba baina ya Chuo cha Mafunzo na Sabah Store wenye thamani ya shilingi 925,074,098 pamoja naVAT( makataba namba SMZ/DO3/G/SCM/2019-2020/03) uliotiwa saini tarehe 2/0/2019, Kumbukumbu za Kikao cha Bodi ya Zabuni zabuni namba 03/019/2020 cha tarehe 7/8/2019 na za kikao cha Bodi ya zabuni namba 04/2019/2020 ambacho kiliihinisha mapendekezo ya Kmati ya Tathimini ya kumteua mshindi wa zabuni hiyo ya ununuzi wa vifaa vy ujenzi, barua ya kumjulisha kushinda zabuni (notification letter) ya tarehe 26/8/2019 yenye namba SMZ.D03.GSCM.2019-20120/03, barua ya kumwita Mkurugenzi wa Sabah Store yenye kumbkumbu namba 1B/VOL.1/14/2019,Vilevile Kmati ya PAC ilikagua nyarka mmbalimbali za malipo zinzohusika. Kwa ujumla, Kamati ya PAC imerdihika na majibu pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Chuo cha Mafunzo ingawa ilikuwa na mapendekezo yayonaohusu Hoja hii.

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imekishauri Chuo cha Mafunzo kutoa ushirikaono wa kutosha wakati wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti wanapokwenda kwa ajili ya Ukaguzi kwa maelezo na vielelezo vyote vinavyohitajika badala ya kuisubiri Kamati ya PACkuipatia vielelezo hivyo.

## Hoja Namba 5.2.3.4 Malipo yaliyokosa vielelezo hesabu ya Kamishna vyuo vya mafunzo shilingi 395,242,4000

Ukaguzi umebaini kuwa Idara ya vyuo vya mafunzo imehaulisha jumala 395,242,400 kutoka hesabu ya matumizi ya maendeleo na kuingia kwenye hesabu ya Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo hesabu namba 0404296000 matumizi ambayo hayakutumika katika miradi iliyopangwa katuka mwaka wa fedha 2019/2020, aidha maelezo na vieelezo vya matumizi hayo havikupatikana kwa ukaguzi , kufanya hivyo ni kwenda kinyume na bajeti iliyopangwa . maelezo ya matumizi hayo yanaonekana katika jaduweli lifuatalo:-

### Malipo yaliyokosa vielelezo katika hesabu ya Kamishna wa mafunzo

| Namba | Tarehe ya malipo | Nambari ya hundi | Jumla ya fedha (shs) | aliyelipwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 3/9/2019 | 66 | 12,300,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| 2 | 12/11/2019 | 71 | 65,840,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3 | 28/12/2019 | 79 | 20,000,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| 4 | 31`/12/2019 | 80 | 42,100,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| 5 | 2/1/2020 | 81 | 35,075,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| 6 | 31/1/2020 | 94 | 5,090,400 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| 7 | 3/3/2020 | 98 | 96,000,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| 8 | 9/4/2020 | 103 | 15,000,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| 9 | 21/4/2020 | 104 | 2,000,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| 10 | 2/6/2020 | 121 | 42,347,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| 11 | 2/6/2020 | 120 | 18,000,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| 12 | 4/6/2020 | 122 | 10,000,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| 13 | 5/6/2020 | 123 | 5,000,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| 14 | 9/6/2020 | 126 | 26,490,000 | Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo |
| Jumla | | | 395,242,400 | |

Majibu ya Chuo cha Mafunzo

Chuo cha Mafunzo kilikiri kuwa wakanguzi walipokuja waligundua malipo hayo yalifanyika bila ya kua na vielelezo lakini kwa sasa marekebisho yameshafanyika na kuonekana katika vocha husika kama ifuatavyo .

Malipo yaliokosa vielelezo hesabu ya Kamishna Vyuo vya Mafunzo

| NAMBA | TAREHE YA MALIPO YA HUNDI | NAMBARI YA HUNDI | TAREHE YA MALIPO YA VOCHA HUSIKA | NAMBA VOCHA HUSIKA | JUMLA YA FEDHA ALIELIPWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 3/9/2019 | 66 | 02/09/2019 | D03PV11900000057 | 12,489,720 |
| 2 | 12/11/2019 | 71 | 09/11/2019 | D03PV11900000141 | 65,840,000 |
| 3 | 28/12/2019 | 79 | 26/12/2019 | D03PV11900000206 | 20,000,000 |
| 4 | 31/12/2019 | 80 | 28/12/2019 | D03PV11900000207 | 42,100,000 |
| 5 | 2/1/2020 | 81 | 20/12/2019 | D03PV11900000207 | 35,075,000 |
| 6 | 31/1/2020` | 94 | 29/12/2019 | D03PV11900000246 | 5,090,400 |
| 7 | 3/3/2020 | 98 | 29/12/2019 | D03PV11900000283 | 96,000,000 |
| 8 | 9/4/2020 | 103 | 08/04/2020 | D03PV11900000341 | 15,000,000 |
| 9 | 21/4/2020 | 104 | 08/04/2020 | D03PV11900000341 | 2,000,000 |
| 10 | 2/6/2020 | 120 | 29/05/2020 | D03PV11900000402 | 18,000,000 |
| 11 | 4/6/2020 | 122 | 29/05/2020 | D03PV11900000402 | 10,000,000 |
| 12 | 5/6/2020 | 123 | 29/05/2020 | D03PV11900000402 | 5,000,000 |
| 13 | 9/6/2020 | 126 | 29/05/2020 | D03PV11900000402 | 26,490,000 |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeelezwa kuwa fedha hizo zilizoingizwa katika akaanti ya Kamiishna zimetumika katika masuala ya ufuatailiaji na uendeshaji wa miradi, Haukafanyika uhaulishaji kutoka Fungu la Maendeleo kwenda Fungu la matumizi ya kawaida. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa kilichotokea ilikuwa ni kutofautiana kwa ufahamu tu baina yao na wakaguzi ju ya suala hilo.

Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa watendaji wa Chuo cha Mafunzo huwa wanakosa kushirikiana katika kutoa maelezo ya kutosha na vielelezo vinavyostahiki wakati wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti wanapofika hapo kwa ukaguzi. Kamati ya PAC imekagua vielezo mbalimbaii vinavyohusiana na Hoja hii na kuridhika navyo.

Mapendekezo ya Kamati

Viongozi na watendaji wa Chuo cha Mafunzo wajipange vizuri zaidi wanapokuja wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibti kwa kuwapa uzito unaostahili na kuwapa taarifa na vielelezo vinavyohusika kwa wakati hasa kwa kuzingatia kuwa wakaguzi hao wanatekeleza

majukumu ya Kikatiba

**Hoja Namba 5.2.3.5 Matumizi ya fedha bila ya kuwa na mkataba shilingi 173,681,325**

Ukaguzi umebaini kuwa Chuo cha mafunzo kimefanya malipo ya shilingi 173,681,325 kupitia hesabu ya duka la mafunzo kwa kwa ajili ununuzi wa vifaa mbali mbali vya ujenzi wa Jengo la Mamlaka ya Vitenga Uchumi Zanzibar (ZIPA), ukaguzi haukupatiwa mkataba wa kazi hiyo kati ya Chuo cha Mafunzo na Mamlaka ya Vitenga Uchumi ili kujiridhisha kiwango halisi cha kazi hiyo. Kutopatikana kwa Mkataba wa makubaliano kunapelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha gharama halisi inayotakiwa kutumika katika ujenzi huo.

Maelezo ya malipo hayo yanaonekana katika jadweli lifuatalo :-

| namba | Tarehe ya malipo | Namabari ya hati ya malipo | Nambari ya hundi | Jumla ya fedha (SHS) | aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 28/11/2019 | 10/11 | 917 | 32,000,000 | Duka la Chuo Cha Mafunzo | Ikiwa ni mali[po kwa ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ujezi ZIPA |
| 2 | 12/3/2019 | 12/11 | 919 | 50,000,000 | Duka la Chuo Cha Mafunzo | Ikiwa ni mali[po kwa ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ujezi ZIPA |
| 3 | 12/10/2019 | 3/12 | 922 | 11,000,000 | Duka la Chuo Cha Mafunzo | Ikiwa ni mali[po kwa ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ujezi ZIPA |
| 4 | 25/2/2020 | 2/2 | 950 | 44,502,325 | Duka la Chuo Cha Mafunzo | Ikiwa ni mali[po kwa ununuzi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | wa vifaa mbalimbali vya ujezi ZIPA |
| 5 | 25/2/2020 | 3/2 | 953 | 17,910,000 | Duka la Chuo Cha Mafunzo | Ikiwa ni mali[po kwa ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ujezi ZIPA |
| 6 | 3/2/2020 | 4/2 | 953 | 18,269,000 | Duka la Chuo Cha Mafunzo | Ikiwa ni mali[po kwa ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ujezi ZIPA |

Majibu ya Chuo cha Mafunzo

Chuo cha Mafunzo kilikiri kuwa wakaguzi walipokuja walishindwa kuona mkataba wa ujenzi wa Mamlaka ya vitega uchumi Zanzibar (ZIPA),ambapo kwa awamu ya pili (verification period) ya ukaguzi mkataba huu uliweza kuwasilishwa na kuweza kujiridhisha.

Matumizi ya fedha bila ya kua na mkataba

| Tarehe ya malipo | Nambari ya hati malipo | Nam. Ya hundi | Risiti/ invoice | Jumla ya fedha iliyolipwa | Alielipwa | Maelezo ya hati ya malipo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 28/11/2019 | 10/11 | 917 | 1050 | 32,000,000 | DUKA DUKA LA CHUO CHA MAFUNZO | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi ZIPA |
| 12/03/2019 | 12/11 | 919 | 1119/1 | 50,000,000 | DUKA | Ikiwa ni malipo ya |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 054 | | DUKA LA CHUO CHA MAFUNZO | vifaa vya ujenzi vitakavyo tumika ZIPA |
| 12/10/2019 | 03/12 | 922 | 1165/1055 | 11,000,000 | DUKA DUKA LA CHUO CHA MAFUNZO | Ikiwa ni malipo ya vifaa vya ujenzi vitakavyotumika ZIPA |
| 25/2/2020 | 2/2 | 950 | 1055/1113 | 44,502,325 | DUKA DUKA LA CHUO CHA MAFUNZO | Ikiwa nimalipo kwa ununuzi wa vifaa mbali mbali ZIPA |
| 25/2/2020 | 3/2 | 953 | 1056/1112 | 17,910,000 | DUKA DUKA LA CHUO CHA MAFUNZO | Ikiwa ni malipo kwa ununuzi wa vifaa vya ujenzi ZIPA |
| 03/02/2020 | 4/2 | 953 | 1057/1111 | 18,269,000 | DUKA DUKA LA CHUO CHA MAFUNZO | Ikiwa ni malipo kwa ununuzi wa vifaa vya ujenzi ZIPA |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilihoji juu ya sababu za kutopatikana kwa mkataba wakati wa ukaguzi wa Mdhibiti na kubaini udhaifu katika mawasiliano miongoni mwa Watendaji wa Chuo cha Mafunzo pamoja na uwekaji usioridhisha wa nyaraka muhimu za taasisi hiyo. Hata viongozi wa waandamizi wa waChuo vha Mafunzo walishangzwa na kukosekana kwa mkataba huo wakati wa ukaguzi wakiamini kuwa mkataba huo ulikuwepo na wao ndio waliokuwa wakiusimamia. Hata hivyo Kamati iliridhia kuukagua mkataba huo wenya namba SMZ /F/O109/W/NCB/18-19/24 wenye jumla ya shilingi 187,610,058. Aidha,

Kamati ya PAC ilikagua barua kutoka ZIPA iliyokwenda Chuo cha Mafunzo kukijuilisha Chuo hicho kushinda zabuni (Notification letter) ya ukarabati wa jengo la ZIPA lilipo Maruhubi ( barua yenye kumbukumbu nambaZIPA/B7/VOL.II/45

1.6 CHUO CHAMAFUNZO PEMBA

Hoja Namba 5.2.3.6 Malipo kwa wafanya biashara ambao hawkusajiliwa na mamlaka ya ununuzi na Ondoshaji wa Mali za Umma shilingi 4,705,071

Jumla ya shilingi 4,705,071 zimetumika kuwalipa wafanyabiashara kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na huduma kwa matumizi ya Chuo cha Mafunzo. Ukaguzi umebaini kwamba wafanyabiashara hao hawakusajlikwa kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar ili kuweza kufanya biashara na taasisi za Serikali. Kufanya hivyo ni kwemda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha sheria ya ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar nambari ya mwaka 2016. Malipo yenyewe ni kama ifuatavyo:-

Jadweli la Malipo kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ua Manunuzi na Uondoshaji wa mali za Umma

| Hati namba | Hundi namba | Fedha zilizolipwa | Aliyelipa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 01/9 | 34,342251 | 845,778 | SULEIMAN MOH'D OMAR | Ikiwa ni malipo ya vifaa vya ujenzi wa nyumba<br>Taiz 13box 30x30 18000<br>6kg grouty 3500,<br>1pc choo complity |
| 2/9 | 342251 | 230,300 | SULEIMAN MOH'D OMAR | Malipoya fedha kwa ajili ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya ujenzi |
| 4/9 | 342252 | 326,555 | ALI MOHAMMED JUMA | Malipo ya fedhakwa ajili ya ununzi wa vifaa vya kilimo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6/10 | 342261 | 592,619 | ALI MOHAMMED JUMA | Malipo ya fedhakwa ajili ya ununzi wa vifaa vya kilimo |
| 1/12 | 342266 | 1,890,000 | ALI MOHAMMED JUMA | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 11/12 | 342270 | 82,131 | LIMBANI FARM INPUT | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mbengu za kuoteshea bidhaa za kilimo |
| 01/5 | 342280 | 175,573 | LIMBANI FARM INPUT | Malipoya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mbengu |
| 2/5 | 342282 | 561,636 | LIMBANI FARM INPUT | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali |
| Jumla | | 4,705,071 | | |

Majibu ya Chuo cha Mafunzo

Ni kweli Jumla ya shilingi 4,705,071 zimetumika kuwalipa wafanyabiashara kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na huduma kwa matumizi ya Chuo Cha Mafunzo pasina kusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar ili kuweza kufanya biashara na taasisi za serikali. Hata hivyo wafanya biashara hao wameshasajiliwa katika mamlaka husika kama inavyoonekana katika jadweli

| Hati namba | Hundi nama | TAREHE | Fedha zilizolipwa (Shs.) | Alielipwa | Reg: namba | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 01/9 | 342251 | 25/09/2019 | 845,778 | SULEIMAN MOH'D OMAR | ZPPDA/NC/0105/2021 | Ikiwa ni ununuzi wa vifaa vya Ujenzi |
| 2/9 | 342251 | 25/09/2019 | 230,300 | SULEIMAN MOH'D OMAR | ZPPDA/NC/0105/2021 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi. |
| 4/9 | 342252 | 25/09/2019 | 326,555 | ALI MOH'D JUMA | ZPPDA/G/0187/2021 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 6/10 | 342261 | 11/10/2019 | 593,619 | ALI MOH'D JUMA | ZPPDA/G/0187/2021 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifa vya ujenzi |
| 1/12 | 342266 | 23/12/2019 | 1,890,479 | ALI MOH'D JUMA | ZPPDA/G/0187/2021 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 01/03 | 342270 | 10/03/2020 | 82,131 | LIMBANI FARM INPUTS | ZPPDA/G/0197/2021 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kilimo |
| 01/5 | 342280 | 18/05/2020 | 175,573 | LIMBANI FARM INPUTS | ZPPDA/G/0197/2021 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kilimo |
| 2/5 | 342282 | 19/05/2020 | 561,636 | ALI MOH'D JUMA | ZPPDA/G/0187/2021 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilibaini kuwa Chuo cha Mafunzo Pemba kikitumia mazoea tu kwa kufanyiwa huduma kutoka kwa watoa huduma mbalimbali bila ya kuangalia misingi ya Sheria iliyopo ya Ununuzi wa Umma ambapo watoa huduma walioukuwa wakiwatumia ni ni wauza maduka ya vifaa vya ujenzi na kilimo.

Kwa kuwa Chuo vcha Mafunzo Pemba kilieleza kuwa watoa hudua hao hivisasa wameshasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi, Kamati ilijiridhisha kwa kuangalia vyeti vyausajili wa watoa huduma hao na kuridhika navyo. Miongoni mwa vyeti vya usajili watoa huduma hao vilivyokaguliwa ni cha Ali Moh'd Juma chenye nambari ya usajili ZPPPDA/G//0187/2021kilichotolewa tarehe 26 Januari, 2021 na cheti cha Juma Amour Moh'd chenye nambari ya usajili ZPPDA/G/0197/2021. Baada ya kuridhika na vyeti hivyo vya usajili, Kamati haikuwa na maelezo zaidi juu ya Hoja hii.

## 1.7 FUNGU D O5 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

### Taarifa ya Mapato

Kikosi cha Zimamoto na Ukozi kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 92,536,000 kutoka katika vyanzo vya ndani. Hadi kufikia 30 Juni ,2020 jumla ya shilingi 27,827,000 ziliusanywa sawa na asilimia n30 ya makadirio.

### Majibu ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

Kwa mwaka wa fedha 2019/20 Kikosi kilikadiriwa kuchangia Tzs 92,536,000.00 katika mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Kikosi kimefanikiwa kuchangia Tzs 27,827,000.00 sawa na asilimia 30 ya makadirio.

Vyanzo vya mapato vya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ni:

1. Ukodishaji wa vifaa.
2. Uuzaji wa mitungi ya kuzimia moto.
3. Matengenezo ya mitungi ya kuzimia moto.
4. Utoaji wa vyeti vya usalama wa moto.
5. Malipo ya kazi za ujenzi
6. Ada ya ulinzi

Kikosi kilishindwa kufikia malengo ya uchangiaji wa mapato yasiyokuwa ya kodi katika mfuko mkuu wa Serikali kwa sababu zifuatazo:

1. Kuingia kwa wimbi la kwanza la maradhi ya UVIKO (COVID 19) ambapo ilipelekea kwa mahoteli mengi kufungwa ambao ndo wateja wakuu wa Kikosi.
2. Makisio kuwa makubwa sana kulingana na uhalisia wa vyanzo vya ukusanyaji.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilitaka kujua vyanzo vyengine vya mapato na ilielezwa kuwa mapato mengine yanapatikana kwenye ukodishwaji wa vifaa -gari la ngazi kwa ajili ya huduma mbali mbali Aidha Kamati ilihoji juiu ya  makisio makubwa bila ya uhalisia wa vyanzo na kuelezwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ndio wanaopanga makisio jambo ambalo linawapa tabu sana katika uhalisia. Pia Kamati ilielezwa kuhusu vyeti vya usalama wa moto (Fire Safety Cetaficate) ambavyo hutolewa baada ya kufanywa ukaguzi kuhusu usalama wa moto ambapo bei ya cheti inategemea na ukubwa wa jingo. Cheti kimoja kinafikia

1,000,000 hadi 1,000,000, Kamati ya PAC ilipata kukagua baadhi ya mifano ya vyeti kikiwemo NO.C/04/21/22 ACCUPIER PREMISE AFCONS VIJETA JV ZANZIBAR, CERTIFICATE NO . 11/40/21/22 RECENT SIN0.B 112363. Kamati pia ilikagua mkatba wa ulinzi baini ya Kikosi cha Zimamoto na Wizara ya Elimu kwa ajili ya ulinzi wa Skuli Mombasa. Kamati ya PAC imeridhoika na majibu na ufafanuzi ulotolewa.

Mapendekezo ya Kamati

- Kutokana na suala la wimbi kubwa la maduka ya gesi Kamati inashauri kikosi kiwe kinapitia maduka yote ya gesi kwa ajiliya usalama wa raia na kuhakikisha kuwa kila duuka la gesi linakuwa na mitungi ya kuzimia moto.

- Aidha Kamati inashauri kikosi kutumia vyombo vya habari kutoa elimu kuhusu matumizi ya gesi pamoja na kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuweka vifaa vya kuzimia moto hasa katika majumba makubwa.

- Pia Kamati inashauri kuweka maeneo mazuri ya gesi hasa ambapo yapo baadhi ya maeneo kama Welezo ni hatari kuwepo kwa gesi

  Kwa sababu ni maeneo ya kucheza watoto

Taarifa ya Matumizi

Kikosi cha Zimatoto na Uokozi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 10,398,500,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na jumla shilingi 500,000,000 kwa matumizi ya maendeleo .Hadi kufikia 30 Juni,2020 jumla ya shilingi 11,404,637,686 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ikiwa sawa na asilimia ya makadirio 109 na jumla ya shilingi 500,000,000 zilitumiaka ikiwa sawa na asilimia 100 ya makadiriao .

Majibu ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

Kikosi kwa mwaka wa fedha 2019/20 kilipanga kutumia jumla ya Tzs 8,536,800,000.00 kwa ajili ya kulipa mishahara maafisa na wapiganaji wa KZU. Hadi kufikia 30 Juni 2020 Kikosi kimeingiziwaTzs 9,624,287,686.00 sawa na asilimia 112 ya makiso. Ongezeko la asilimia 12 limetokana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuajiri wapiganaji wapya.

Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida (OC) Kikosi kiliidhinishiwa kutumia Tzs

1,861,700,000.00. Hadi kufikia 30 Juni 2020 Kikosi kimeingiziwa Tzs 1,780,350,000.00 sawa na asilimia 95.6 ya makisio.

Kikosi kilikuwa na mradi mmoja wa ujenzi wa vituo vya uokozi na uzimaji moto, mahanga na nyumba za kulala maafisa ambapo kilipanga kuanza na ujenzi wa kituo cha uokozi na uzimaji moto Kijichame – Pemba ambapo kilikadiriwa kutumia Tzs 1,380,000,000.00 hadi kukamilika kwake. Kwa mwaka wa fedha 2019/20 Kikosi kiliidhinishiwa kutumia Tzs 500,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi huo na kilipanga kufanya yafuatayo:

1. Kukamilika kwa structure ya jengo la Kijichame
2. Kukamilika kwa gound floor na kuweza kutumika
3. Kituo cha Kijichame kuanza kutoa huduma kwa wananchi

Kikosi kilifanikiwa kutimiza malengo yake niliyoyanukuu hapo juu kutokana na kuingiziwa kwa asilimia 100 ya makadirio ya mwaka wa fedha 2019/20 kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo Tzs 382,000,000.00 kwa ujenzi, Tzs 30,000,000.00 kwa gharama za upatikanaji wa gari ya kutolea huduma na 88,000,000.00 ni gharama za usafirishaji wa mafundi na gharama za ufatiliaji na tathmini. Aidha ujenzi huo umekamilika katika mwaka wa fedha 2020/21.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati Ilihoji ongezeko la mshahara 8,536,800,000 hadi 9,624,287,686 na kuelezwa kuwa ongezeko hili limetokana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuajiri wafanyakazi wapya. Juimla ya waajiriwa wapya hao walikuwa 449. Kamati ilikagua baadhi ya vielelezo niavyohusiana waajriwa hao ikiwemo barua yenye nambari ya kumbukmbu OR/1.M/Y.01C/VOL:XY1/22,

Kwa upande miradi ya maendeleo, Kamati ya PAC ilielezwa kuwa Kikosi cha Zimamoto kilikuwa na ujenzi Kijichame ambapo ujenzi huo ulifanywa na Kikosi wenyewe ambapo Kmapuni ya Ms Juma F Mcha ilipewa kazi ya kupeleka vifaa vya ujenzi kwa gharama ya shilingi 519,601,200. Kmati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali zinazohusiana na matumzi ya mradi huo zikiwemo hati za malipo na mkataba huo wa upelekaji vya vya ujenzi vifaa (SMZ/D05/G/SBM/2019/2020/07) na kuridhika nazo. Kamati ya PAC haikuwa na maelezo zaidi juu ya hoja hii.

### Hoja Namba 5.2.5.1 Malipo yasiokuwa na vielelezo shilingi 71,000,000

Ukaguzi umebaini kufanyaika kwa malipo ya shilingi 71,000,000 kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya kikosi cha Zimamoto na Uokuzi. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosaekana kwa vielelezo vya matumizi hayo. Kufanya matumizi bila ya kuwa na

vielelelzo nim kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1)cha sheria ya usimamizi wa fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2016 . Mchanganuo wa malipo hayo yanoaonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadwel Nambari 14:Malipo yasikuwa na vielelezo

| Namba | tarehe | Nambari ya hundi | aliyelipwa | Fedha iliyolipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2/1/2020 | Tiss/048/674 | Juma fumu mcha | 7,600,000 | ikiwa ni malipo ya vifaa vya ujenzi |
| 2 | 2/1/2020 | Tiss/1603/0559 | Msa auto part | 6,650,000 | ikiwa ni malipo ya ununuzi wa spare part |
| 3 | 1/2/2020 | Tiss/0171/0112 | S H trader and fermigation | 14,250,000 | Ikiwa ni malipo yaununuzi kitambaa cha sare kwa ajili ya maafisa mita 100 green |
| 4 | 1/2/2020 | Tiss/254/686 | Juma foum mcha | 4,700,000 | Ikiwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kutolea huduma zima moto |
| 5 | 1/2/2020 | Tiss/1602/0560 | MSA AUTO PART | 4,750,000 | Ikiwa nimalipo kwa ajili ya ununuzi wa spare part |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 6 | 2/3/2020 | Tiss/ | Kamishna wa zima motona uokozi | 15,000,000 | Ikiwa ni malipokwa ajiliya matumizi mbali mbali |
| 7 | 2/3/2020 | Tiss/730/030 | Omar Muhammed Omar | 3,800,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mipira ya gari |
| 8 | 3/3/2020 | Tiss1609/0564 | Msa auto part | 5,700,000 | Ikiwa malipo kwa ajili ya ununuzi wa spare part |
| 9 | 10/3/2020 | Tiss269/695 | Juma foum mcha | 5,550,000 | ikiwa nimalipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |

Majibu ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

1. Hati zisizokuwa na vielelezo zenye jumla ya Tzs 71,000,000.00.
2. Hati zilizokosamaelezo wakati wa ukaguzi zenye jumla ya Tzs 174,567,466.00.
3. Kikosi hakikuandaa mpango wa manunuzi wa mwaka 2019/2020

Ni kweli Kikosi kilipokea hoja hizo kutoka Afisi ya Mdhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kutoa majibu ya hoja hizo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti anaefuatana Kamati ya aliiyhibitishia Kamati ya PAC kuwa ni kweli Kikosi cha Zimamoto kiliwasilisha majibu ya Hoja hizo kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hata hivyo, wakati majibu hayo yalipokuwa yanawasilishwa Ofisi ya Mdhibiti, harakati za kutaka kuanza kuchapisha kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi zilikuwa zimeanza na haikuwezekana kuziondoa hoja za Kikosi cha Zimamoto katika Kitabu cha Ripoti.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Ni vyema Kikosi cha Zimamoto kikajipanga vizuri zaidi ili kuaanda majibu (ya management letter) na vielelezo mapema kwa Mdhibiti bila ya kusubiri siku zamwisho kuwasilisha majibu hayo.

5.2.5.2 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 174,567,466

Ukaguzi imebaini kufanyika kwa malipo ya shilingi 174,567,466 kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya kikosi cha zimamoto na uokozi .Dosari iliyobaika na ukaguzini kukosekana kwa hatiza malipo ya matumizi hayo. Kufanya matumizi bila ya kuwa na hati za malipo ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma sheria namba 12 ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa hati hizo za maliponi kama inavyoonekana katika jadwel lifuatalo

Jadweli Nambari 15 ; Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi .

| Namba | Nambari ya hati ya malipo | Aliyelipwa | Jumla ya fedha iliyolipwa | Maelezom ya malipo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 3/7 | KAMISHNA ZIMAMOTO NA UOKOZI | 6,700,000 | Maelezo ya malipo husika hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 2 | 5/7 | KAMISHNA ZIMAMOTO NA UOKOZI | 49,741,963 | Maelezo ya malipo husika hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 3 | 17/7 | OMAR MUHAMMEDOMAR | 15,150,000 | Maelezo ya malipo husika hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 4 | 12/8 | KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA | 27,755,655 | Maelezo ya malipo husika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | UOKOZI | | hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 5 | 16/8 | KAMISHNA ZIMAMOTO NA UOKOZI | 8,300,000 | Maelezo ya malipo husika hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 6 | 19/8 | KAMISHNA ZIMAMOTO NA UOKOZI | 47,656,163 | Maelezo ya malipo husika hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 7 | 3/9 | KAMISHNA ZIMAMOTO NA UOKOZI | 3,000,000 | Maelezo ya malipo husika hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 8 | 9/9 | KAMISHNA ZIMAMOTO NA UOKOZI | 11,263,685 | Maelezo ya malipo husika hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 9 | | KAMISHNA ZIMAMOTO NA UOKOZI | 4,000,000 | Maelezo ya malipo husika hayakupatikana kwa ukaguzi |
| Jumla | | | 174,667,466 | |

Majibu ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

4. Hati zisizokuwa na vielelezo zenye jumla ya Tzs 71,000,000.00.
5. Hati zilizokosamaelezo wakati wa ukaguzi zenye jumla ya Tzs 174,567,466.00.
6. Kikosi hakikuandaa mpango wa manunuzi wa mwaka 2019/2020

Ni kweli Kikosi kilipokea hoja hizo kutoka Afisi ya Mdhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kutoa majibu ya hoja hizo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti anaefuatana Kamati ya aliiyhibitishia Kamati ya PAC kuwa ni kweli Kikosi cha Zimamoto kiliwasilisha majibu ya Hoja hizo kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hata hivyo, wakati majibu hayo yalipokuwa

yanawasilishwa Ofisi ya Mdhibiti, harakati za kutaka kuanza kuchapisha kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi zilikuwa zimenza na haikuwezekana kuziondoa hoja za Kikosi cha Zimamoto katika Kitabu cha Ripoti.

## 1.8 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI PEMBA.

### Hoja Namba 5.2.5.3 MALIPO YALIYOKOSA VIELELEZO SHILINGI 50,440,500

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 50,440,500 zimetumika kwa matumizi mbalimbali lakini vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kudhibitisha uhalali wa malipo hayo ambapo kunapelekea kukosekana uthibitisha kufanyika kwa malipo , wafanya biashara kutokulipa kodi stahiki kwa serikali na kutokujua aina ya malipo yaliyofanyika .

aidha kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1)cha sheria ya usimamizi wa fedha za ummma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.baadhi ya malipo hayo kama ifuatavyo:-

: Malipo yaliyokosa vielelezo

| Hati Namba | Hundi Namba | Fedha zilizolipwa (shs) | aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 12/8 | 000617 | 940,000 | Mkuu wa KZU | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto pamoja na mafunzo kwa jengo la Elimu mbadala Wingwi Pemba |
| 5/11 | 000643 | 1,000,000 | Mkuu wa KZU | Malipo kwa ajili yaununuzi wa madawa ya kuzimi moto pamoja na ufanyaji wa service na mafunzo kwa ofisi ya wizara ya fedha pemba |
| 9/11 | 000647 | 1,000,000 | Mkuu wa KZU | Malipo kwa ajili ya matumizi ya uitaji zenge jengo la kijichame, chakula na mafuta pamoja na mahitaji ya wanafunzi wa chuo cha Mafunzo. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11/3 | 000691 | 15,288,500 | Mkuu wa KZU | Malipokwa ajili ya matumizi ya mikato ya Askari wa zima moto na uokozi Pemba kwa mwezi wa maech 2020 pamoja na service ya DCPna training . |
| 9/4 | 000700 | 18,037,500(15,037,500mka to<br>3,000,000 Matofali) | Mkuu wa KZU | Malipokwa ajili ya mikato mbali mbali waliokatwa asakari wa KZU Pemba pamoja na ununuzi wa matofali kwa ajili ya ujenzi wa jengo la zimamoto |
| 4/5 | 004348 | 5,960,000 | KZU | Ni malipoya kununua vifaa na kufanya service vifaa mbali mbali na kufanya training kwa walimu na wanafunzi wa chuocha mwalimu Nyerere tawi la Pemba |
| 2/8 | 000609 | 2,014,5000 | KZU | Ni ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto vya mamlaka ya viwanja vya ndege Pemba. |
| 6/10 | 000635 | 3,000,000 | Mkuu wa KZU | Ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto kwa ajili ya matumizi ya skuli ya Moh’d Juma Pindua |
| 8/1 | 000668 | 3,200,000 | Mkuu wa KZU | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya zima moto. |
| Jumla | | | 50,400,5000 | |

Majibu ya Kikosi cha Zimamoto

| S.NO | HUNDI NO. | KIASI (TZS) | ALIYELIPWA | MAELEZO | MAJIBU |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 000617 | 940,000 | MKUU WA KZU | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto pamoja na mafunzo kwa jengo la Elimu mbadala Wingwi | Vielelezo husika vimeambatanishwa katika Hati husika |
| 2 | 000643 | 1,000,000. | MKUU WA KZU | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa madawa ya kuzimia moto pamoja na ufanyaji "service" na mafunzo kwa Ofisi ya Wizara ya Fedha Pemba | Vielelezo husika vimeambatanishwa katika Hati husika |
| 3 | 000647 | 1,000,000 | MKUU WA KZU | Malipo kwa ajili ya matumizi ya utiaji zege jengo la Kijichame, chakula na mafuta pamoja na mahitaji ya wananfunzi wa Chuo cha Mafunzo | Vielelezo husika vimeambatanishwa katika Hati husika |
| 4 | 000691 | 15,288,000 | MKUU WA KZU | Malipo kwa ajili ya matumizi ya mikato waliokatwa askari wa Zimamoto na Uokozi Pemba kwa mwezi Mar, 2020 pamoja na service ya DCP na training. | Vielelezo husika vimeambatanishwa katika Hati husika |
| 5 | 000700 | 18,037,500 (15,037,5000 mkato na 3,000,000) | MKUU WA KZU | Malipo kwa ajili ya matumizi ya mikato waliokatwa askari wa KZU Pemba pamoja na ununuzi wa matofali kwa ajili ya ujenzi wa jengo la zimamoto | Vielelezo husika vimeambatanishwa katika Hati husika |
| 6 | 004348 | 5,960,000 | MKUU WA KZU | Ni malipo ya kununua vifaa na kufanya service vifaa mbalimbali na kufanya training kwa walimu na wanafunzi wa Chuo cha Mwalimu Nyerere Tawi la Pemba. | Vielelezo husika vimeambatanishwa katika Hati husika |
| 7 | 000609 | 2,014,500 | MKUU WA KZU | Ni ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto vya mamlaka ya viwanja vya ndege Pemba | Vielelezo husika vimeambatanishwa katika Hati husika |
| 8 | 000635 | 3,000,000 | MKUU WA KZU | Ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto kwa ajili ya matumizi ya Skuli ya Moh'd Juma Pindua | Vielelezo husika vimeambatanishwa katika Hati husika |
| 9 | 000668 | 3,200,000 | MKUU WA KZU | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya zimamoto na uokozi | Vielelezo husika vimeambatanishwa katika Hati husika |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa ingawa hati za malipo zilipatikana wakati wa ukaguzi lakini baadhi ya hati za malipo zilikosa vielelezo zikiwemo stakabadhi za matumizi hata wakati wa ukaguzi wa mara ya pili (verification) ambapo katika ukaguzi wa awali hati za malipo

zilizokosa vielelezo zilikuwa na jumla ya shilingi 66,000,000 na wakati ukaguzi wa mara ya pili (verification) baadhi ya matumizi yaliendelea kukosa vielelezo yenye jumla ya shilingi 50,440,000 na kuingizwa katika kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi kama inavyoonekana katika Hoja hii. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilivikagua vielelezo hivyo na kuridhika navyo. Baadhi ya vielelezo vilivyokaguliwa na Kamati ni stakabadhi za matumizi mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

i. Stakabadhi yenye nambari 0135 ya tarehe 12/8/2019 kutoka Moh'd Surprise Spplies yenye jumla ya shilingi 2.014,500 kwa ajili ya malipo ya ujazaji wa gesi ya kuzimia moto katika "cylinder" yenye ujazo wa kilogram 50..

ii. Stakabadhi yenye nambari 0067 ya tarehe 27/1/ 2020 kutoka Coast Belt Agro Glass Investment Ltd yenye jumla ya shilingi 3,200,000 kwa ajili ya malipo ya ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto.

iii. Stakabadhi yenye nambari 191 ya tarehe 13/4/2020 kutoka Zanzibar Fire Prevention yenye jumla ya shilingi 700,000 ikiwa ni malipo ya kufanya service vifaa mbalimbali.

iv. Stakabadhi yenye nambari 193 ya tarehe 20/10/2019 kutoka Zanzibar Fire Prevention yenye jumla ya shilingi 2,700,000 kwa ajili ya malipo ya ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati imewashauri watendaji wa masuala ya fedha katika Kikosi cha Zimamaoto Pemba kubadilika katika utendaji wao kwa kuhakikisha kuwa wanafanya kazi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni na taratibu za fedha zilizopo ikiwa ni pamoja na kuambatanisha vielelezo vyote vya matumizi na hati za malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi yanayofanywa na Kikosi hicho.

### Hoja Namba 5.2.5.4 Malipo kwa watoa huduma wasiosajiliwa na mamlaka ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma shilingi 17,450,000

Jumla ya shilingi 17,450,000 zimelipwa kwa ajili huduma mbalimbali za kikosi cha zimamoto.ukaguzi umebaini kwamba watoa huduma hao hawakusajiliwa katika Mamlaka ya Ununuzi na uondoshaji wa mali za umma ambopo kunaweza kuikosesha serikali mapato.
Aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za Umma ya Umma ya Zanzibar nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na sheria ua usimamizi wa fedha za umma ya Zanzibar namba ya 12 ya mwaka 2016.

Baadhi ya manunuzi hayo ni kama yafuatayo :-

Jadweli Nambari 17 : malipo kwa watoa huduma waliosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji yaliyofanyika kwa kampuni ya ROM ambayo hayakukatwa kodi

| tarehe | Hati namba | Hundi namba | Fedha zilizolipwa (shs) | aliyelipwa | maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 6/3/2020 | 5/3 | - | 3,200,000 | Omar Mohmmed Omar | Malipo kwa ununuzi wa vifaa vya ujezi wa majengo ya zimamoto pemba |
| 4/2/2020 | 2/2 | 0673 | 14,250,000 | Trater and fermigation | Malipo kwa ununuzi wa vifaa vya ujezi wa majengo ya zimamoto pemba |
| JUMLA | | | 17,450,000 | | |

Majibu ya Kikaosi cha Zimamoto

| S. N | HUNDI NO. | KIASI (TZS) | ALIYELIPWA | MAELEZO | MAJIBU |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 000617 | 3,200,000 | M/S OMAR MOHAMMED OMAR | Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya matumizi ya | Msambazaji wa huduma ya vifaa vya ujenzi amesajiliwa kwa namba ya usajili ZPPDA/G/0261/2020 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Zimamoto Pemba | |
| 2 | 000643 | 14,250,000 | M/S SH TRADERS AND FUMMIGATION | Malipo ya vifaa vya ujenzi kwa ajili ya matumizi ya Zimamoto Pemba | Msambazaji wa huduma ya vifaa vya ujenzi amesajiliwa kwa namba ya usajili ZPPDA.78/NC/2019 |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kukosekana kwa uelewa wa kina juu ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016 ambapo watendaji wa masuala ya fedha wa Kikosi cha Zimamoto Pemba walieleza kuwa walikuwa hawajui kama walikuwa wanatakiwa kuhakikisha kuwa watoa huduma wanaaowatumia wawe wamesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi. Walichokuwa wakifahamu ni kuwa mpaka kuwe na zabuni ndio wanapaswa kuwachunguza watoa huduma wanaowatumia. Hata hivyo, watoa huduma hao hivi sasa wameshasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi ambapo Kamati imevikagua vyeti hivyo vya usajili na kuridhika navyo. Miongoni mwa vyeti vilivyakaguliwa ni cha Omar Mohammed Omar amabe ni msambazaji wa vifaa vya ujenzi mwenye nambari usajili ZPPDA/G/0261/2020,

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma izidi kutoa taaluma juu ya Sheria za Ununuzi wa Mali za Umma na Usimamizi wa Ferdha Umma kwa wahasibu na watendaji wengine wa masuala ya fedha walio katika Idara Maalum za SMZ ili watendaji hao waweze kuwa na ufahamu mpana zaidi wa Sheria hizo na kujiepusha na makosa mbalimbali ya uvinjaji wa Sheria na taraiibu zinazoongoza masuala ya fedha na ununuzi wa mali za umma.

Hoja Namba 5.2.5.5 Malipo yaliyofanyika kwa matumizi ya fedha taslim kwa mtoa huduma shilingi 6,500,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 6,500,000 zimetumika kwa malipo ya kumlipa mtoa huduma malipom ya fedha taslima.

Kueendelea kumlipa mtoa huduma malipo ya fedha taslima kunaweza kupelekea kuikosesha mapato serikali yatokanayo na kodi aidha ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2016 ya Zanzibarpamoja na sheria za kodi za mwaka 2004. B aadhi ya malipo hayo ni kama ifuatavyo

Malipo yaliyofanyika kwa matumizi ya fedha taslim kwa mtoa huduma

| Hati namba | Hundi namba | Fedha zilizolipwa (SHS) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 7/5 | 000703 | 3,000,000 | Ni malipo ya safari unguja –pemba na pemba –unguja (1000,000).<br><br>Malipo ya vitakasa mikono .(2,000,000)(SH TRADER AND FUMIGATION) |
| 3/6 | 000711 | 3,500,000 | Ikiwa ni matengenezo ya gari ya KZU yenye namba 218 kuitia mbao na kuichomea weldingi |
| Jumla | | 6,500,000 | |

Majibu ya Kikosi cha Zimamoto

| SN | HUNDI NO. | KIASI (TZS) | ALIYELIPWA | MAELEZO | MAJIBU |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 000617 | 3,200,000 | MKUU WA KZU | Ni malipo ya safari Ungj-Pba (1,000,000) na malipo ya vitakasa mkono (2,000,000.00) | 1.Ni posho la kujikimu.<br>2.Ni kweli Kikosi kimelipo malipo ya fedha taslimu kutokana na aina ya huduma inayohitajika na upatikanaji wake kwa kuzuka kwa janga la UVIKO kwa wimbi la kwanza. |
| 2 | 000643 | 3,500,000 | MKUU WA KZU | Ikiwa ni matengenezo ya | Ni kweli Kikosi kimelipo malipo ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | gari ya KZU yenye namba 218 kuitia mbao na kuichomea welding | fedha taslimu kutokana na uharaka wa matumizi ya gari hiyo na aina ya watowaji wa huduma wanaopatikana Pemba. |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa ingawa Kikosi cha Zimamoto kilifanya matumizi ya fedha taslim kwa mtoa huduma kutokana na sababu za uharaka, hata hivyo matumizi hayo yangeweza kufanyika kwa hundi kwa mtoa huduma husika kama taratibu na miongozo ya matumizi ya fedha za umma inavyoelekeza.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Watendaji wa Kikosi cha Zimamoto Pemba wafanye jitihada ya kuzifahamu na kuzitumia vizuri Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ili kazi za ununuzi na za kifedha za Kikosi hicho ziwe zinatekelezwa kwa kufuata kikamilifu misingi ya Sheria hizo.

ii. Kikosi cha Zimamoto Pemba kitoe ushirikiano mzuri kwa Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kazi za ukaguzi katika Kikosi hicho ziweze kutekelezwa kama zilivyokusudiwa.

iii. Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti Pemba watumie taaluma na weledi wao vizuri kwa kufanya ukaguzi na kujenga maelewano baina yao na Taasisi wanazazikagua.

## 1.9 FUNGU D 06 KIKOSI CHA VALANTIA

Taarifa ya Matumizi

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Kikosi cha Valantia kilikadiwa kutumia jumla ya shilingi 11,853,660,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 500,000,000 kwa kazi za maendeleo .Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jmla ya shilingi 14,470,125,533 zimetumika kwa kazi zam kawaida sawa na silimia 122 ya makadirio na jumla ya shilingi 500,000,000 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 100 ya makadirio.

Majibu ya Kikosi cha Valantia

Kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kikosi cha Valantia Zanzibar, kiliidhinishiwa kutumia jumla ya Tsh Bilioni Kumi na mbili, milioni mia tatu na hamsini na tatu laki sita na elfu sitini (12,353,660,000/-) hadi kufikia June 30, 2020 Kikosi kiliingiziwa jumla ya Tsh. Bilioni Kumi na nne, milioni mia tisa na sabini, laki moja ishirini na tano elfu mia tano thelathini na tatu (14,970,125,533/-), sawa na asilimia 121 kama inavyoonesha katika jeduali lifuatalo hapo chini.

Hii inamaana kuwa, kuna ongezeko la kiasi cha Tsh Bilioni mbili Milioni nane na thelathini na nne laki tisa hamsini na moja elfu mia nne na themanini (2,834,951,480/-). Ongezeko hilo la fedha limetokana na kuajiriwa kwa Askari wapya 701 pamoja na kupandishwa vyeo kwa baadhi ya Maafisa na Askari wa KVZ.

Upatikanaji wa fedha za Matumizi mengineyo haukuwa wa kuridhisha na hivyo kusababisha baadhi ya kazi zifuatazo kushindwa kutekelezeka kwa asilimia mia moja:-

1. Kuandaa Mpango mkakati wa Kikosi.
2. Ununuzi wa Vifaa vya Ofisi, Vifaa Tiba, Usafi, Mawasiliano na Kompyuta.
3. Kushindwa kufanya ukarabati Mkubwa na mdogo wa majengo ya Kikosi, mfano Ujenzi wa ukuta wa kambi ya Mtoni.
4. Kushindwa kutanua kituo cha Afya cha KVZ - Mtoni

Kwa upande wa Matumizi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kikosi kilikua na mradi mmoja tu wa maendeleo ambao ulihusisha ujenzi wa hanga la kulala Askari katika kambi ya Ndugu Kitu Pemba na ujenzi wa Nyumba ya Mkuu wa Kanda iliyopo Mgogoni Pemba.Mradi huu ulikadiriwa kutumia kiasi cha Tsh 500,000,000 na matumizi halisi ni Tsh 500,000,000 sawa na asilimia (100%).

Kazi za maendeleo zilitekelezwa kwenye mradi huu ni :-

Ujenzi wa Hanga la kulala Askari katika kambi ya Ndugu Kitu Pemba, ambao umegharimu kiasi cha Tsh Milioni mia mbili (200,000,000/-).

Ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Kanda ya Pemba, ambao umegharimu kiasi cha Tsh milioni mia moja na themanini (180,000,000/-).

Fedha zilizobaki zimetumika kwa kumlipa mzabuni wa Ujenzi wa Ofisi na Hanga katika Kambi ya Ndugukitu Pemba pamoja na matumizi mengine ya Utawala.

Ujenzi huo wa Hanga na Nyumba umekamilika kwa asilimia (100%), na tayari majengo hayo yameshaanza kutumika kwa shunghuli iliopangwa.

JADWELI LA MCHANUO WA MATUMIZI AYA KIKOSI CHA VALANTIA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

| S/No | MAELEZO | KILICHOPANGWA | KILICHOPATIKANA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| | Mapato ya Kikosi cha Valantia | Kikosi cha Valantia Zanzibar hakina chanzo chochote cha Mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020 | | |
| 1. | Mishahara na Maposho | 10,123,890,000/- | 12,958,841,480/- | 128% |
| 2. | Matumizi Mengineyo | 1,729,770,000/- | 1,511,284,053/- | 87% |
| 3. | Kazi za Maendeleo | 500,000,000/- | 500,000,000/- | 100% |
| | Jumla | 12,353,660,000/- | 14,970,125,533/- | 121% |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kmati ya PAC ilihoji juu ya ongezeko la mishahara na kuelezwa kuwa lilitokana na ajira mpya mbazo zilikuwa zinashughulikiwa na Serikali Kuu kupitia Ofisis ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa ambapo Kikosi cha Valantia kililetewa na kupokea askari tu. Aidha, ongezeko hilo pia lilisababishwa na kupandishwa vyeo kwa baadhi ya askari wa Kikosi, Kamati ya PAC barua ya maombi ya kupatiwa fedha za ziada za mishahara (KV/M/339/VOL.1V/22 ya tarehe11 Septemba, 2019) ilikaguliwa na Kamati ya PAC. Kamati ya PAC imeridhika na Matumizi Ya Kikosi cha Valantia kwa mwaka 2019/2020.

Hoja Namba 5.2.6.1  Kukosekana kwa ripoti ya ukaguzi wa ndani

Kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016 kifungu namba 117 inaika kila taasi ya umma kuanzisha kitengo cha ukaguzi wa ndani ambacho ni imara na madhubuti kwa lengo la kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani.

Kikosi cha Valantia kinatumia kitengo cha ukaguzi wa ndani ya Wira ya nchi  Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa,Serikali za Nitaa na Idara Maalum ambacho kinaongozwa na mkaguzi mkuu wa ndani  dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana ripoti ya ukaguzi ya mwaka na kuwasilishwa na mkaguzi Mkuu wa Hesabu , kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 117(6)cha sheria ya usimamami za fedha za Umma sheria namba 12 mwaka 2016.

Majibu ya KIkosi cha Valantia

Ni kweli Kikosi cha Valantia Zanzibar kinatumia Kitengo cha Ukaguzi wa ndani Cha Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na hivyo Ripoti ya Mkaguzi wa ndani hutolewa na Ofisi hiyo. Hadi kufikia mwisho wa  mwaka wa fedha 2019/2020 Mkaguzi wa ndani wa Wizara hajatoa Ripoti yake ya Ukaguzi wa Ndani

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa Ukaguzi wa ndani haukuweza kufanyika hata robo maoja ya mwaka kwa kipindi hicho kwa sababu wakaguzi wa ndani walikuwa kwenye mafunzo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum kwa kushirikina na Kikosi cha Valantia zijipange vizuri zaidi ili kuhakikisha kuwa Ukaguzi wa ndani unafanyika kwa wakati bila vikwazo vyovyote.

Hoja Namba 5.2.6.2 Matumizi ambayo hayanavielelezo shilingi 52,500,000

Ukaguzi umebaini kuwa Kikosi Cha Valantia Zanzibar kimefanya malipo ya jumla ya shilingi 52,500,000 kwa ajili ya kuharamia matumizi mbali mbali ya Kikosi hicho, dosari iliyobaikia na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo, kufanya malipo bila kuwa na vielelezo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 43(1)cha sheria ya usimamaizi wa fesda za umma nambari 12 ya mwaka 2016. Maelezo ya malipo hayo yanaokana katika jadwel lifuatalo:-

Jadwel Nambari 19: Matumizi ambayo hayana vielelezo

| Namba | Namabari ya hati ya malipo | Nambari ya hundi | Fedha iliyolopwa | aliyelipwa | maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 25/7 | TISS | 2,00,000 | Kamanda Mkuu KVA | Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa umeme |
| 2 | 26/7 | TISS | 7,000,000, | Kamanda Mkuu KVA | Ikiwa ni ya safari ya safari yaliyofanyw a na kvz |
| 3 | 4/8 | TISS | 2,550,000 | Kamanda Mkuu KVA | Ikiwa nimalipo ya maposho |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | na nauli kwa wachezaji |
| 4 | 3/9 | TISS | 5,650,000 | Kamanda Mkuu KVA | Ikiwa ni malipo ya safari za nje na ndani safari ya wakuu pemba , uhamisho wa askari pemba |
| 5 | 4/9 | TISS | 2,500,000 | Kamanda Mkuu KVA | Ikiwa ni malipo ya mafunzo ya ndani yaliyofanyika kvz |
| 6 | 5/9 | TISS | 2,000,000 | Kamanda Mkuu KVA | Ikiwa ni malipo ya umeme na maji |
| 7 | 12/9 | TISS | 1,500,000 | Kamanda Mkuu KVA | Ikiwa ni malipo ya vyakula na vinywaji katika ofisi |
| 8 | 3/10 | TISS | 14,300,000 | Kamanda Mkuu KVA | Ikiwa ni malipoya matumizi mbalimbali yaliyofanywa na kvz |
| 9 | 14/10 | TISS | 15,000,000 | Kamanda Mkuu KVA | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | matumizi mbalimbali |
| | | | 52,500,000 | | |

Aidha, ukaguzi umebaini kufanyika uhaulishaji wa jumla ya shilingi 56,000,000 kwenda katika hesabu ya Mkuu wa Kikosi cha Valantia pemba , dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo, kufanya malipo bila ya kuwa na vielelezo vya matumizi ni kwenda kinyume na sheria ua usimamaizi wa fedha za umma sheria nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadwellifuatalo:-

Jadwel Nambari 20 : malipo yaliyofanyika kwa uhaulishaji wa fedha.

| namba | Nambari ya hati ya malipo | Nambari ya hundi ya malipo | Fedha iliyolipwa | aliyelipwa | maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 3/5 | TISS | 8,000,000 | Mkuu wa Kikosi cha Valantia Pemba | Malipo kwa ajili ya chakula kwa wapiganaji walikuwa kwenye ulinzi |
| 2 | 18/7 | TISS | 5,000,000 | Mkuu wa Kikosi cha Valantia Pemba | Ikiwa ni malipom kwa ajili ya mafuta |
| 3 | 21/8 | TISS | 4,000,000 | Mkuu wa Kikosi cha Valantia Pemba | Ikiwa ni malipo ya chakula cha askari |
| 4 | 7/8 | TISS | 8,000,000 | Mkuu wa Kikosi cha Valantia Pemba | Ikiwa ni malipo ya chakula |
| 5 | 6/9 | TISS | 5,000,000 | Mkuu wa Kikosi cha | Ukiwa ni malipo kwa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Valantia Pemba | matumizi tofauti |
| 6 | 9/9 | TISS | 8,000,000 | Mkuu wa Kikosi cha Valantia Pemba | Ikiwa ni malipo ya chakula |
| 7 | 2/10 | TISS | 10,000,000 | Mkuu wa Kikosi cha Valantia Pemba | Ikiwa ni malipo ya matumizi tofauti |
| 8 | 6/10 | TISS | 8,000,000 | Mkuu wa Kikosi cha Valantia Pemba | Ikiwa ni malipo ya chakula |
| | | | 56,000,000 | | |

Majibu ya Kikosi cha Valantia

Kikosi cha Valantia mara baada ya kupokea barua yenye Kumbukumbu No AUD/WN/AR/TMIMS/KV/4/5/1 ya tarehe 15 Feb, 2021 kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya kutupa siku 30 za kujibu hoja, Kikosi kilichukua juhudi ya kujibu hoja hizo na kumuomba kuja kufanya uhakiki (Verification) wa vocha hizo kwa kumuandikia barua yenye Kumbukumbu No KV/M/118/VOL.II/36 ya tarehe 01 March, 2021. Hata hivyo Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali (CAG) alishindwa kuja kufanya uhakiki (Verification) huo na hivyo kupelekea Ripoti ya Mwisho kuonesha kuwa kuna matumizi yasiyokuwa na Vielelezo jambo ambalo sio sahihi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibti anaefatana na Kamati ya PAC alieleza kuwa Wakaguzi walifanya mawasiliano na watendaji wa Kikaosi cha Valantia wakati walipokuwa katika ziara za Ukaguzi, Hata hivyo wakaguzi hao walipokuja tena vielelezo hawakuvikuta. Hata hivyo, Kmati ya PAC iliridhia kuvipitia vielelezo hivyo na kuridhika navyo.

1,10 KIKOSI CHA VALANTIA PEMBA

Hoja Namba 5.2.6.3. Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzishilingi 24,250,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 24,250,000 zimetumika kwa matumizi mbali

mbali katika Kikosi cha Valantia Pemba .hadi ukaguzi unakamilika hati za malipo hayo hazikupatikana kwa ukaguzi.
Kukosekana kwa hati ya malipo kwa ajili ya ukaguzi ni kwenda kinyume na sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Baadhi ya hati zenyewe ni kama zifuatazo .

Jadweli Nambari: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi

| Hati namba | Hundi namba | Fedha zilizolipwa | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|
| 1/1 | 000375 | 500,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 4/1 | 000378 | 2,000,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 3/3 | 000391 | 1,000,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 6/3 | 000395 | 1,500,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 7/3 | 000394 | 1,000,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 1/5 | 000402 | 2,000,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 5/5 | 000406 | 1,500,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 1/6 | 000407 | 2,000,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 2/6 | 000409 | 900,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 4/6 | 000410 | 1,850,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| ½ | 000383 | 2,000,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 5/2 | 000388 | 500,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 8/10 | 000354 | 1,500,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 9/10 | 000356 | 2,000,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 5/11 | 000363 | 2,000,000 | Kikosi Cha Valantia |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Zanzibar |
| 8/11 | 000366 | 1,000,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 10/11 | 000368 | 500,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| 11/11 | 000369 | 500,000 | Kikosi Cha Valantia Zanzibar |
| Jumla | | 24,250,000 | |

Majibu ya Kikosi cha Valantia

| S/No | HOJA | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1. | Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi pamoja na malipo yasio na vielelezo. | Kikosi cha Valantia Pemba mara tu baada ya kupokea nakala ya barua yenye kumbukumbu No. AUD/WN/AR/TMIMS/KV/4/5/1 tarehe 15 Feb,2021, kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Barua ambayo imetupa siku 30 za kujibu hoja hizo , kwa upande wa Kikosi cha Valantia Pemba mara tu baada ya kupokea nakala hiyo tulichukua juhudi ya kujibu hoja hizo na kuiomba Makao Makuu ya KVZ kuwasilisha kwa pamoja maombi ya kuwataka kuja kufanya Verification kwa barua yenye kumbukumbu No. KV/M/118/VOL.II/36 yatarehe 01 March,2021. Hata hivyo, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alishindwa kuja kufanya uhakiki huo na hivyo kupelekea ripoti ya mwisho kuonesha kuwa kuna matumizi mbalimbali ya mekosa hati na vielelezo jambo ambalo sio sahihi. |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilielezwa na Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anaefatana na Kamati hiyo kuwa Hoja hizo zinatokana na Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka 2018/2019 ambapo baada ya kuona kuwa Hoja hizo hazijapata majibu zikaingizwa tena katika Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka 2019/2020 kama tataratibu za ukaguzi zinavyolekeza.

Aidha, kwa kuzingatia maelekezo ya Kamati ya Uongozi ya Baraza la Wawakilishi kwa Kamati zinzosimamia mausala ya kifedha za Baraza hilo uliozitaka Kamati hizo kutozifanyia kazi Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka

2018/2019 kutokana na sababu mbalimbali, hivyo Kamati ya PAC haikuweza kuifanyia kazi Hoja hiyo.

Hoja Namba 5.2.6.4 Malipo yasiokuwa na vielelezo shilingi 12,170,000

Ukaguzi umebaini kwa malipo ya jumla ya shilingi 12,170,000 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbali mbali za uendeshaji , dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya malipo hayo. Kufanya malipo bila ua kuwa na vielelezo ni kwenda kinyume na sheria ya usimamaizi wa fedha wa umma nambari 12 mwaka 2016, maelezo ya malipo yanaonekana jadweli.

Jadweli Nambari22: malipo yasiyokuwa na vielelezo.

| T\areh e | Nambari ya hati ya malipo | Fedha zilizolipwa | Alielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 13/8/ 18 | 4/2 | 1,500,000 | Ali Khamis | Malipo ya ununuzi wa kuni |
| 13/8/ 18 | | 2,000,000 | Ali Khamis | Malipo ya ununuzi wa kuni |
| 11/3/ 19 | 2/3 | 1,240,000 | Salim Hamdan | Malipo ya vifaa vya ujenzi na kuni |
| 14/3/ 19 | 000390 | 1,960,000 | Sharif Petrol Station | Ununuzi wa mafuta na disel |
| 15/9/ 18 | 7/9 000344 | 3,800,000 | Hamoud Seif Said | Malipo ya ununuzi wa chakula |
| 10/9/ 18 | 3/9 | 1,670,000 | Assa Hamad Mbwana | Ununuzi wa mlango, madirisha, na viti |
| Jumla | | 12,170,000 | | |

Majibu ya Kikosi cha Valantia

| S/ No | HOJA | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1. | Hati za malipo | Kikosi cha Valantia Pemba mara tu baada ya kupokea |

| | | |
|---|---|---|
| | zilizokosekana kwa ukaguzi pamoja na malipo yasio na vielelezo. | nakala ya barua yenye kumbukumbu No. AUD/WN/AR/TMIMS/KV/4/5/1 tarehe 15 Feb,2021, kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Barua ambayo imetupa siku 30 za kujibu hoja hizo , kwa upande wa Kikosi cha Valantia Pemba mara tu baada ya kupokea nakala hiyo tulichukua juhudi ya kujibu hoja hizo na kuiomba Makao Makuu ya KVZ kuwasilisha kwa pamoja maombi ya kuwataka kuja kufanya Verification kwa barua yenye kumbukumbu No. KV/M/118/VOL.II/36 yatarehe 01 March,2021. Hata hivyo, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alishindwa kuja kufanya uhakiki huo na hivyo kupelekea ripoti ya mwisho kuonesha kuwa kuna matumizi mbalimbali ya mekosa hati na vielelezo jambo ambalo sio sahihi. |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilielezwa na Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anaefatana na Kamati hiyo kuwa Hoja hizo zinatokana na Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka 2018/2019 ambapo baada ya kuona kuwa Hoja hizo hazijapata majibu zikaingizwa tena katika Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka 2019/2020 kama tataratibu za ukaguzi zinavyolekeza.

Aidha, kwa kuzingatia maelekezo ya Kamati ya Uongozi ya Baraza la Wawakilishi kwa Kamati zinzosimamia mausala ya kifedha za Baraza hilo uliozitaka Kamati hizo kutozifanyia kazi Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2018/2019 kutokana na sababu mbalimbali, hivyo Kamati ya PAC haikuweza kuifanyia kazi Hoja hiyo.

2,0 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII PEMBA

Hoja Namba 5.2.7.2 Hati za malipo ambazo hazikurikodiwa kwenye daftari la fedha taslim shilling 7,916,500

Jumla ya shilingi 7,916,500 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Wakala wa Matukio ya Kijamii. Ukaguzi umebaini kwamba hati za malipo hayo hazikurikodiwa katika daftari la fedha taslim ili kuweza kujua uhalali wa matumizi hayo .

Kutokurikodiwa kwa hati za malipo katika daftari la fedha taslim ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha sheria ya usimamizi wa fedha za umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Majibu ya Wakala wa Matukio ya Usajili wa Matukio ya Kijamii Pemba

Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Pemba inafuata Sheria na taratibu za kihasibu kwa kuhakikisha kwamba malipo yote yaliyomo katika hati za malipo yamerikodiwa katika Cash Boo

Baada ya kufuatiiia kwa kina Hoja hii tumebaini kuwa kwamba malipo hayo yamerikodiwa kimakosa kupitia hati moja ya mtandao ambayo inaonesha mkusanyiko wa hati mbali mbali za Wakla badala ya kurikodi malipo kwa hati moja moja za ndani za Wakala kama ilivyo kawaida . Kwa hivyo, tunaaahidi kuwa makini zaidi katika kurikodi hati moja moja katika cash book badala ya kurikodi mkusanyiko wa hati.

Jadweli Nambari 24: Hati a malipo ambazo hazijarikodiwa katika daftari la fedha.

| Nambari ya hati ya malipo | Nambari ya hundi | Fedha zilizolipwa | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 9/1A 2/1/2020 | 012094 | 1,836,500 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (ZCSRA) Pemba | Malipo kwa wafanyakazi walioshiriki Mkutano wa siku mbili pamoja na chakula na ukumbi |
| 9/1B/ 2/1/2020 | 012094 | 190,000 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (ZCSRA) Pemba | Malipo ya posho nyeti na posho la kujikimu anayolipwa Nd. Zahour Salim Ali na Moh'd Zubeir Ame kwa mwezi wa November 2019 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9/1C 21/11/2019 | 012094 | 368,000 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (ZCSRA) Pemba | Malipo ya Nd. Ali Hamad Khamis kwa safari ya unguja kikazi. |
| 9/1E 5/11/2019 | 012094 | 725,000 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (ZCSRA) Pemba | Malipo kwa Nd. Hamad Shamata Hamad kaimu mkuu wa ZCSRA |
| 14/7A 26/7/2019 | 012094 | 1,055,000 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (ZCSRA) Pemba | Marejesho ya malipo kwa Nd. Hamad Shamata Hamad |
| 14/7B 27/7/2019 | 007837 | 285,000 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (ZCSRA) Pemba | Malipo ya Nd . Zahor Salim Ali na Nd . Moh'd Zuber Ame |
| 14/7C 26/7/2019 | 007839 | 725,000 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (ZCSRA) Pemba | Malipo ya Nd. Hamad Shamata Hamad kwa ajili ya safari ya unguja kikazi |
| 14/7D 27/7/2019 | 007839 | 452,000 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (ZCSRA) Pemba | Malipo ya limbikizo kwa ajili ya Nd Zuhura Ali Hassan |
| 14E/7 27/7/2019 | 007839 | 1,555,000 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya | Malipo wanayolipwa wafanyakazi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Kijamii (ZCSRA) Pemba | walioshiriki kwenye mafunzo ys mfumo wa payment. |
| 14F/7 26/7/2019 | 007839 | 725,000 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (ZCSRA) Pemba | Malipo ya Nd. Omar Abdalla Ishaka kwa ajili ya safari Unguja kikazi. |
| Jumla | | 7,916,500 | | |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilizikikagua hati za malipo zilizohusika katika kurekodi na kujumuisha malipo mbali mbali ambazo ni hati namba 14/7 pamoja na Cash book la mtandao kuanzia tarehe 1 Julai 2019 hadi 30 Julai 2019 na hati namba 9/1 pamoja na Cash book la mtandao kuanzia tarhe 1 Januari hadi tarehe 31 Januari 2020. Kamati ya PAC imeridhika na ufafanuzi pamoja na vielelezo hivyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imewashauri watendaji wa kitengo cha fedha katika Ofisi ya Wakala wa Matukio ya Kijamii Pemba kuyafanyia kazi ipasavyo maelekezo yanayotolewa na wakaguzi wanapofaya ukaguzi kwa kurekodi hati moja moja za malipo katika daftari la kumbukumbu za matumizi (cash book) ili kuleta mtiririko mzuri wa uwekaji wa kumbukumbu za matumizi mbalimbali ya Ofisi hiyo.

## 2.1 FUNGU D 11 MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Taarifa ya Mapato

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 9,725,000 kutoka kwenye vianzio vyake mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Hadi kufikia 30 Juni, 2020, jumla ya shilingi 7,447,7000 zilikusanywa na Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini ikiwa sawa na asilimia 47.2 ya makadirio.

Majibu ya Mkoa wa Kaskazini Pemba

Kwa mwaka 2019/2020 Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba ilipanga kukusanya Shilingi 36,380,000 ambapo hadi kufikia mwezi Juni 2020 ilikusanya na kuingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali Shilingi 9,725,000 sawa na asilimia 26.7 ya makadirio. Upungufu katika makusanyo hayo unatokana na kuwa vyanzo vya Afisi ya Mkuu wa Mkoa ni vitatu ambavyo ni Ada za Usajili wa Vizazi na vifo (Late registration), Ada itokanayo na Uhaulishaji wa Ardhi, Ukodishaji wa Kituo cha Mafuta (Wete Petrol Station) ambapo vyanzo viwili kati ya hivyo ni tegemezi.

MAPATO FUNGU D11-MKOA WA KASKAZINI PEMBA
KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

| CHANZO | MAKADIRO | HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| UHAULISHAJI WA ARDHI | 16,084,000 | 1,080,000 | 6.7 |
| KODI YA MAJENGO | 3,000,000 | 3,000,000 | 100.00 |
| FOMU ZA VYETI VYA KUZALIWA | 17,296,000 | 5,645,000 | 32.64 |
| JUMLA YA MAPATO | 36,380,000 | 9,725,000 | 26.73 |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa taarifa za makadirio ya mapato na makusanyo halisi zilizoainishwa katika Ripoti ya Ukaguzi ya Mdhibiti ziko tofauti na taarifa za Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba zilizowasilishwa mbele ya Kamati ya PAC ambapo kwa mujibu wa Ripoti ya Ukaguzi makadirio ya mapato ya Ofisi hii kwa mwaka 2019/2020 ni shilingi 9,725,000 na makusanyo halisi yalikuwa shilingi 7,449,700. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa taarifa za majibu ya Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba ndio sahhi kama zilivyoonekana katika taarifa ya Hesabu ya Mwaka ya Ofisi hiyo (Financial Statement).

Aidha,Kamati imebaini kuwa Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba haikuipitia kwa makini taarifa ya awali ya matokeo ya ukaguzi wa Ofisi hiyo iliyowaslishwa Ofisini hapo katoka Ofisi ya Mdhibti (Managemenet Letter) ambapo Ofisi hiyo ya Mkoa ingeweza kusahihisha mapema taarifa hizo na kuziwasilisha katika Ofisi ya Mdhibiti,

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Katibu Tawala wa Mkoa pamoja na Mhasibu wa Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba wazipitie taarifa zote zinazoainishwa katika Ripoti ya awali ya matokeo ya Ukaguzi inayowasilishwa katika Ofisi hiyo kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Management Letter) na kuwasilisha majibu ya

ufafanuzi kwa Ofisi ya Mdhibiti katika wakati uliowekwa kwa mujibu wa taratibu za Ukaguzi.

ii. Wakaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wawe makini zaidi katika katika kuchukua taarifa kutoka katika ripoti za Hesabu za Mwaka za Taasisi mbalimbali (Financial Statements) ili kupata usahihi wa taarifa za ukaguzi na kuepusha migongano ya taarifa kati yake na Taasisi za Serikali.

Taarifa ya Matumizi.

Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 15,077,629,000 kwa kazi za kawaida

Hadi kufikia 30,juni,2020 , kiasi cha shilingi 12,497,849,975 zimetumika kwa kazi za kawaida ikiwa sawa na asilimia 82.89 ya makadirio.

Majibu ya Mkoa wa Kaskazini Pemba

Kwa upande wa Matumizi, Mkoa ulipanga kutumia Shilingi 15,041,249,000 ambapo kati ya fedha hizo Shilingi 2,086,644,000 ni matumizi kwa kazi za kawaida, Shilingi 1,356,154,000 ni Mishahara na Shilingi 730,490,000 ni Matumizi Kuendeshea Afisi (OC). Aidha Shilingi 12,954,605,000 ni Ruzuku kwa ajili ya Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.Kwa Mwaka 2019/2020 Upatikanaji wa fedha ulikuwa wa kuridhisha ambapo Shilingi 12,488,124,975 sawa na asilimia 83 ya Makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,844,901,995 sawa na asilimia 88 ni kwa kazi za kawaida, Shilingi 1,190,429,795 sawa na asilimia 88 ni Mishahara na Shilingi 654,472,200 sawa na asilimia 90 ni Fedha za kuendeshea Afisi (OC). Aidha Shilingi 10,643,222,980 sawa na asilimia 82 ni Ruzuku kwa ajili ya Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

MATUMIZI FUNGU D11- MKOA WA KASKAZINI PEMBA
KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

| FUNGU | MAKADIRIO | HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 1,356,154,000 | 1,190,429,795 | 87.78 |
| MATUMIZI MENGINEO | 730,490,000 | 654,472,200 | 89.59 |
| RUZUKU | 12,954,605,000 | 10,643,222,980 | 82.16 |
| JUMLA YA MATUMIZI | 15,041,249,000 | 12,488,124,975 | 83.03 |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa taarifa za makadirio ya matumizi na matumizi halisi zilizoainishwa katika Ripoti ya Ukaguzi ya Mdhibiti ziko tofauti kidogo na taarifa za Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba zilizowasilishwa mbele ya Kamati ya PAC ambapo kwa mujibu wa Ripoti ya Ukaguzi makadirio ya matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka 2019/2020 ni shilingi 15,077,629,000 na matumizi halisi yalikuwa shilingi 12,497,,899,975. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa taarifa za matumizi ya Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba ndio sahhi kama zilivyoonekana katika taarifa ya Hesabu ya Mwaka ya Ofisi hiyo (Financial Statement).

Kamati haikuwa na maelezo zaidi juu ya Hoja hii ambapo mapendekezo yake ya jumla kwa Hoja zote hizi za mapato na matumizi ni kama yanavyoonekakana katika Hoja ya Mapato ya Afisi hii.

Hoja 5.2.8.1 Mafuta na vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari la ghalani shilingi 6,711,269

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 6,711,269 zimetumika kwa ununuzi wa mafuta na vifaa mbali mbali lakini mafuta na vifaa hivyo havikuingizwa kwenye daftari la ghalani ilikuweza kudhibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake.
Kutokuingizwa mafuta na vifaa katika daftari la kutunziz vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na sharia ya usimamizi wa fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. M changanuo wa manunuzi hayo ni kama ifuatavyo

Jadweli nambari 25 : Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye dafatri la ghalani

| namba | Nambari ya hati ya malipo | Nambari ya hundi | Aliyelipwa | Jumla ya fedha (SHS) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 13/02 | 13035 | Adult Traingi Centre | 219,588 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa stationaries |
| 2 | 2-Feb | 12835 | Wete Petrol Station | 1,116,200 | Ikiwa ni malipom kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |
| 3 | 6-Nov | 15569 | Suleiman Said Omar | 237,500 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | matengezo ya gari |
| 4 | 53/6 | 15911 | Suleiman Said Omar | 190,120 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |
| 5 | 49/11 | 11082 | Wete Petrol Station | 400,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 6 | 11-Mar | 10481 | Mlinge Enterprise | 47,530 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya magari |
| 7 | 23/6 | 15726 | Rashid M'ohd Soud | 4,002,026 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mipira ya magarimaha |
| 8 | 22/6 | 15577 | Khatib Hholding | 498,305 | |
| jumla | | | | 6,711,269 | |

Majibu ya Mkoa wa Kaskazini Pemba

Afisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba inapenda kukiri kuwa ni kweli Ukaguzi wa matumizi ya fedha ulipofanyika baadhi ya vifaa vya mafuta vielelezo vyake havikuonekana katika Daftari la kutunzia kumbukumbu katika ghala. Hii inatokana na Afisi ya Mkuu wa Mkoa kutumia mfumo wa kukopa vifaa, mafuta na huduma nyengine za kiofisi pale inapotokea fedha za uendeshaji wa Afis (OC) zinapochelewa kuingizwa, Hata hivyo, vielelezo huambatanishwa na matumizi husika baada ya wahusika (supplier) kukubaliana na Afisi kutoa vielelezo na huduma.

Katika Hoja hii vielelezo vifuatavyo ambavyo havikuonekana hapo awali vimeorodheshwa kama ifuatavyo:-

| Namb a | Namba ya hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Aliyelipwa | Jumla ya Fedha | LPO na Tarehe ilipoingizwa kwenye Daftari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 13/02 | 13035 | Adult Training Centre | 219,588 | LPO 13614 5/10/ 2019 |
| 2. | 2 Febr. | 12835 | Wete Petrol Station | 1,116,200 | LPO 13563 4/2/ 2020 |
| 3. | 6 Nov | 15569 | Suleiman Said Omar | 237,500 | LPO 50680 4/6/2020 |
| 4. | 53/6 | 15911 | Suleiman Said Omar | 190,120 | LPO 50692 10/6/ 2020 |
| 5. | 49/11 | 11082 | Wete Petrol Station | 400,000 | LPO 13611 3/10/2019 |
| 6. | 11 March | 10481 | Malinge Enterprise | 47,530 | LPO 13622 22/10/2019. |
| 7. | 23/6 | 15726 | Rashid Moh'd Soud | 4,002,026 | LPO 50690 9 Juni 2020 |
| 8. | 22/6 | 15577 | Khatib Holdings | 498,305 | LPO 50689 8/06/2020. |

Pamoja na ufafanuzi huo, Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba inapenda kuihakikishia Kamati yako kuwa kasoro zilizojitokeza katika matumizi mbali mbali ya fedha za Umma mwaka 2019/2020 hazitajitokeza tena katika matumizi mengine ikiwa ni pamoja na kuboresha mifumo ya uwekaji wa kumbukumbu za fedha na nyenginezo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika Hoja hii imebaini yafuatayo:-

1. Wakati mafuta na vifaa hivyo vilipoingizwa katika Afisi ya Mkoa, Mtunza Ghala alikuwa yupo likizo na hakukuwa na msaidizi.

2. Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti walipokuwa wakifanya ukaguzi katika Ofisi hii waliona taarifa za vifaa vyengine vimeingizwa katika daftari la ghalani isipokuwa taarifa za mafuta na vifaa vyenye thamani ya shilingi 6,711,269 vilivyoainishwa katika Hoja hii.

3. Mtunza ghala husika ana elimu ya Kidato cha Nne, amesomea kompyuta pamoja na kupata mafunzo madogo madogo ya Utunzaji Ghala.

Aidha, Kamati ililikagua daftari la kutunza vifaa ghalani pamoja na vielelezo husika kwa kujiridhisha. Miongoni mwa vielelezo vilivyokaguliwa na Kamati ni pamoja na :-

i. Hati ya malipo yenye namba 2/2 ya tarehe 4/2/2020, na Local Purchase Order (LPO) yenye nambari 23563 ya terehe 4/2/2020 kwa ajili ya ununuzi wa petrol lita 300 na diesel lita 200 iliyokwenda Wete Petrol Station pamoja na stakabadhi yenye nambari 0006 ya terehe 5/2/2020 kutoka Wete Petrol Station yenye jumla ya shilingi 1,116,200 kwa ajili ya malipo ya mafuta.

ii. Hati ya malipo yenye namba 23/6 ya tarehe 16/6/2020, na LPO yenye nambari 50690 ya tarehe 9/6/2020 aliyopelekewa Rashid Mohammed Soud kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya gari ya Mkuu wa Mkoa. Pia, Ankara (invoice) yenye nambari 0336 ya tarehe 9/6/202 ya Rashid Moammed Soud pamoja na stakabadhi yenye nambari 229 ya tarehe 19/6/2020 kutoka kwa Rashid Mohammed Soud yenye jumls ya shilingi 4,002,026 kwa ajili ya malipo ya vifaa vya gari hiyo.

iii. Hati ya Malipo yenye nambari 11/6 ya tarehe 9/6/2020 na LPO yenye nambari 50680 ya terehe 4/6/2020 aliyopelekewa Suleiman Said Pmar pamoja na Ankara (invoice) yenye nambari 0062 ya tarehe 4/6/2020 ya Suleiman Said Omar kwa ajili ya vifaa vya kufanyia “service” ya gari. Pia stakabadhi yenye nambari 0271 ya terehe 11/6/2020 kutoka kwa Sulaiman Said Omar yenye jumla ya shilingi 237,500 kwa ajili ya malipo ya “service” ya gari.

Mapendekezo ya Kamati

1. Kwa kuwa Mtunza ghala katika Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba ni mmoja tu na asiye na taaluma ya kutosha, Kamati imeishauri Ofisi hiyo kufanya utaratibu wa kumuongezea taaluma mtunza ghala huyo pamoja na kufanya utaratibu kuongeza mtunza ghala mwengine mwenye sifa na uwezo wa kutosha ili kazi za uwekaji wa kumbkumbu ghalani ziweze kufanyika kwa uhakika na ufanisi unaostahiki.

2. Kamati imemtaka Katibu Tawala wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kuhakikisha kuwa anasimamia vizuri zaidi utekelezaji wa kazi za vitengo vyote vilivyomo katika Ofisi hiyo ilik majukumu ya kazi katika sehemu na vittengo hivyo yawe yanatekelezwa wakati wote kama Sheria, Kanuni na taratibu za Utumishi Serikalini zinavyoelekeza.

2.2 FUNGU G 02 MAHKAMA KUU

Taarifa ya Mapato

Mahkama kuu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 710,310,000 . Hadi kufikia 30 Juni 2020 Mahkma Kuu imekusanya Jumla ya shilingi

534,457,408 sawa na asilimia 75.24 ya makadirio.

### Majibu ya Mahkama Kuu

Mapato ya Mahkama Zanzibar kwa kiasi kikubwa yanategemea maeneo mawili (2) makubwa ambayo ni Faini ya Mahakama na Ada ya Mahakama (Court Fine na Court fees) na ni maeneo ambayo huwezi ukayatabiria. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 mapato kwa upande wa fine ambapo ndio mapato makubwa yanapatikana yalipungua kutokana na kutokuwepo kwa kesi nyingi na hizo zilizokuwepo washtakiwa walifungwa na hawakupigwa fines. Kwa upande wa kupungua kwa kesi hii imeonyesha kwamba wananchi wanatii sana sheria ambapo ni kitu cha kujivunia kwa sababu Mahkama haipo kukusanya mapato bali ni kuirekebisha jamii ifuate sheria za nchi. Lakini kwa upande wa "Court fees" hizi zinakuwa ni mapato madogo madogo sana ambapo pia yanategemea ni kwa kiasi gani wananchi walihitaji huduma hizo.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilibaini kuwa mapato ya Mahkama yanajumuisha mapato ya Mahkama zote zikiwemo Mahkama za Mwanzo, Mahkama za Wilaya, Mahkama za Mikoa na Mahkma Kuu. ambapo maapto hayo yote huingia katika Mfuko wa Hazina. Aidha, mapato hayo hayajumuishi tozo zinazotozwa na na Manispaa na Mabaraza ya Miji.

kwa upande wa tozo za Manispaa na Mabaraza ya Miji, Kamati ya PAC ilielezwa kuwa asilimia 20 ya fedha hizo wanachukua Baraza la Mji na Manisapaa na asilima 80 zinakwenda katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Kamati ya PAC iliridhika na ufafanuzi wa majibu yaliyotolewa na Mahkama Kuu.

### Taarifa ya Matumizi

Katika Kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, Mahkama Kuu ya Zanzibar ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 7,849,900,000 kwa matumizi ya kawaida na mishahara. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020, jumla ya shilingi 7,576,299,493 zilingizwa na kutumika kwa matumizi ya kawaida na mishahara sawa na asilimia 97 ya makadirio.

### Majibu ya Mahkama Kuu

Kwa upande wa matumizi, Mahkama katika mwaka huo wa fedha 2019/2020 ilidhinishiwa jumla ya shilingi **7,849,900,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida na mishahara. Hadi kufikia 30 Juni 2020 Mahakama imepokea jumla ya shilingi Tzs.7,576,299.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida na mishahara ambazo ni sawa na asilimia 97% za fedha zilizoidhinishwa kama zilivyofafanuliwa kwenye Jadueli hapo chini:-

| Maelezo | Makadirio | Fedha halisi zilizo patikana | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 4,411,100,000 | 4,537,262,695 | 103% |
| Ruzuku | 1,635,500,000 | 1,343,169,009 | 82% |
| Matumizi ya kawaida | 1,803,300,000 | 1,695,867,789 | 94% |
| Jumla | 7,849,900,000 | 7,576,299,493 | 97% |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilihoji juu ya sababu za ongezeko la Mishahara (asilimia 103), , Mahakama Kuu imeelezwa kuwa ongezeko la Mishahara ni jambo la kawaida kwa sababu kuna kuwa na ajira mpya hata hivyo Wizara ya Fedha na Mipango kunakuwa na kifungu cha marekebisho ya mishahara (salary Adjustment) . hata hivyo Kamati ilihitaji baadhi ya vielelezo vinavyohusiana na ongezeko la mishahara kama vile barua ya ongozeko la mishahara

Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Kwa kawaida bajeti ya mishahara haiwezi kutumika kama ilivyopangwa kutokana na sababu nyingi zinazojitokeza ndani ya mwaka wa fedha husika. Miongoni mwa sababu hizo n imalimbikizo ya mishahara kwa wafanyakazi, upandaji wa madaraja kwa wafanyakazi na kuongezeka elimu kwa wafanyakazi. Kwa sababu hizi Taasisi hulazimika kuomba kuongezewa bajeti katika fungu la mshahara. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Mahakama ililazimika kufanya hivyo.

Kamati ya PAC ilikagua barua inayohusiana na maombi ya kuhaulishwa Vifungu vya Bajeti ya Mahkama Kuu Tsh 917,500,000 kwa ajili ya malipo ya mishahara ya Mahkama Kuu.(barua ya terehe 11/3/2020 yenye nambari ya kumbkumbu MMK/AC/20/VOLXI/1 iliyotoka Mahkama Kuu kwenda kwa Kati bu Mkuu Wizara ya Fedha). Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na ufafanyzi wa taarifa za matumzi za Mahkama Kuu.

Hoja Namba I: 5.3.2.1 Malipo ya safari za nje yaliyokosa vielelezo shilingi 92,979,400

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 92,979,400 zimetumika ikiwa ni posho na nauli kwa ajili ya safari za nje ya nchi kushiriki katika mikutano ya kimataifa kwa Majaji na Watendaji Wakuu wa Mahkama. Ukaguzi umeshindwa kupatiwa kielelezo chochote kinacho husiana na safari hizo ikiwemo barua ya mualiko wa safari, kibali cha ruhusa za safari zote zilizofanyika nje ya nchi, tiketi za safari hizo zilizoambatanishwa na boading pass ya kusafiria, ripoti maalum mara kwa mara baada ya kurudi safari hiyo ambayo itaeleza faida/tija itakayopatikana kwa nchi au kwa taasisi juu ya uwepo wa safari hiyo na hasara itakayopatikana pindipo ikiwa safari hiyo haikufanyika.

Kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha juu ya uhalali wa safari hizo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha sheria ya usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Orodha ya safari hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

| Namba ya hati | Namba ya hundi/tarehe | Fedha zilizolipwa | Waliolipiwa | Nchi aliyokwenda |
|---|---|---|---|---|
| 39/7 | 50025798 ya 31/7/2019 | 12,960,000 | Jaji Mkuu, Jaji Mkusa, Nd Haji Pandu | Afrika Kusini |
| 2/9 | 50028016 ya 5/9/2019 | 21,178,400 | Mtendaji Mkuu wa Mahkama | China |
| 4/9 | 50028271 ya 10/9/2019 | 9,000,000 | Khamis Ramadhan, Rabia Mohammed | Afrika Kusini |
| 94/10 | 50032527 ya 30/10/2019 | 46,391,000 | Jaji Mkuu, Ms Jaji Mkuu, Mrajis wa Mahkama na Mtendaji Mkuu. | India |
| 15/1 | 50037999 ya 13/1/2020 | 3,450,000 | Aziza Iddi Suleiman | Zimbabwe |

Majibu ya Mahkama Kuu

Vielelezo husika vipo tayari kwa Ukaguzi, safari hizi zina tija kubwa sana katika kuwajengea uwezo watendaji wa Mahkama na Serikali kwa ujumla. Aidha, kwa kawaida kabla ya watendaji hao hawajaondoka nchini maombi ya kupata ridhaa ya Serikali huwasilishwa katika ngazi husika na ndipo ruhusa inapotolewa. Kabla ya ruhusa kutolewa Serikali pamoja na mambo mengine inajiridhisha juu ya tija zitazopatikana na gharama husika. Mbali na safari za kimafunzo, safari nyengine ni mikutano/mafunzo ya Jumuiya za Kikanda ambazo Serikali Kuu inalipia gharama za Ada ya uanachama wake.

Uchunguzi wa Kamat y PAC

Kamati ya PAC imehoji  kuhusu kutopatikana kwa vielelezo vya safari za nje  kwa wakaguzi walipokwenda, kama vile kibali cha ruhusa ya kusafiria, tiketi, boardingi pass ya kusafirishia na ripoti maalum baada ya kurudi safari,

Hata hivyo Kamati imebaini hapo mwanzo kulikuwa hakuna utaratibu wa Jaji Mkuu kuandika Ripoti baada ya kurudi safari  kinachofanyika  baada ya kurudi anakwenda moja kwa moja kwa Mheshimiwa RIais  kumpa maelezo  Mhe Raisi wa Zanzibar na Baraza la Mapinduzi kutoa maelezo kuhusiana na safari hii kuhusu mafanikio na tija iliyopatikana . Kamati haikuridhika na majibu ya Mahkama Kuu juu ya Hoja hii ingawa ilivikagua vielelezo mbalimbali vinavyohusiana na safari hizo..

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeitaka Mahakama kuaacha utamaduni au mazoea yanayakiuka Sheria na miongozo ya Serikali kwa viongozi na watendaji kuwasilisha kikamilifu vilelezo vya safari mara tu baada ya kurudi safari zao za kikazi na vielelezo hivyo viwasilishwe kwa wakati kwa wakaguzi pindi vinapohitajika.

Hoja Namba 5.3.2.2 Malipo ya fidia yaliyokosa vielelezo shilingi 6,405,00

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 6,405,000 zimetumika katika kulipa sehemu ya malipo ya fidia kwa waathirika wa mazao katika eneo la Ujenzi wa Jengo la Mahkama Kuu ya Tunguu ambao ni kama wafuatavyo:_

- Maryam Khamis Omar
- Maryam Ramadhan Seif.
- Halida Ali Iddi.

Aidha, ukaguzi umeshindwa kupatiwa vielelezo vyenye kujitosheleza juu ya uthibitisho wa uhalali wa malipo hayo, vielelezo vyenyewe ni kama vile:-

- Barua iliyotoka Idara ya kilimo sehemu ya ukaguzi wa mazao iliyothibitisha bei halisi za mimea na miti mengine iliyoorodheshwa katika madai.
- Barua ya Sheha wa shehia ya Tunguu iliyothibitisha uhalali wa wakaazi hao na vipando vyao waliolipwa fidia hizo.
- Ulipaji wa fidia bila ya kuwepo kwa vielelezo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Mahkama Kuu

Mahkama Ililipa fidia hii baada ya kupata maombi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja iliyothibitisha madai hayo. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ndio iliyochukuwa dhima ya kujiridhisha juu ya uhalali wa madai haya na kutafuta mtathmini wa kufanya kazi hiyo. Vielelezo husika vipo tayari kwa ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji kuhusu kutpotikana kwa barua ya Sheha ili kuthibitisha uhalali wa wananchi hao kudai na kulipwa fidia hizo na kuwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ndio iliyohusika na

uchukuaji wa barua ya Sheha wa Shehia ya Tunguu. Aidha, Mahkama ilielezwa kuwa Mahkama iliona iridhike na kazi iliyofanywa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na ilifanya malipo kutokana na barua kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na haikuwa na vielelezo vyengine hata barua ya Sheha yenyeorordh ya majina ya anaostahiki kulipwa fidia hiyo.

Sababu za kutokupatikana kwa vielelezo wakati wa ukaguzi hazikuweza kubainishwa na Mahkama ingawa  Kamati ya PAC ilielezwa kuwa Meajis wa Mahkama Kuu alikaa na Sheha wa Tunguu katika kushughulikia madai ya fidia. Hata hivyo Kamati ya PAC ilikagua nyaraka za malipo za Ndg. Maryam Khamis Omar aliyelipwa shilingi 6,000,000.

Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kati ya watu watatu waliostahiki kulipwa fidia walioainishwa katika Hoja hii, ni mtu mmoja tu ndie aliyelipwa ambae pia hajamaliziwa malipo yake.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Ni vyema kwa Mahkama kuthibitisha kwa masuala yanayohitaji kufanyiwa malipo kwa kupata vielelezo vyake vinavyohusika ili iweze kujirihdisha kwanza juu ya uhalali wa malipo hayo hata kama masuala hayo katika hatua za awali yanashughulikiwa na Taasisi nyengine ya Serikali

### Hoja Namba 5.3.2.3 Kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa jengo la Mahkama Kuu Tunguu

Ukaguzi umebaini kwamba Mahkama Kuu ya Zanzibar imefunga mkataba na kampuni ya Advent Construction Limited ya Dar es salam tarehe 21/10/2019 kwa ajili ya Ujenzi wa Jengo la Mahkama Kuu Tunguu katika Mkoa wa Kusini Unguja kwa gharama ya shilingi 16,862,373,757.95. Kwa mujibu wa mkatabata huo mkandarasi alitakiwa kukamilisha na kukabidhi kazi hiyo mnamo tarehe 21/10/2020.

Ukaguzi umebaini hatua za ujenzi huo zimefikia katika hali ya kuridhisha na jumla ya fedha ya shilingi 11,039,570,376.64 ikiwa sawa na asilimia 65 ya fedha zote, kwa mujibu wa hati za madai (certificate) zilizowasilishwa na mkandarasi hadi kukamilika ukaguzi huu imebainika mkandarasi anadai 1,347,600,921.40 ambazo ni madai yaliyowasilishwa hadi sasa.

Aidha ,kutokana na kuchelewa kukamilika kwa ujenzi huo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wa awali ilitarajiwa ujenzi huo utakamilika na kukabidhiwa mnamo mwezi wa januari 2021.

Hadi tunakamilisha ukaguzi huu, ujenzi wa jengo la Mahkama Kuu Umefikia asilimia 80 ya

utekelezaji ingawa bado ni wenye kusuasua jambo ambalo linapelekea miradi ya maendeleo kutokukamilika kwa wakati uliopangwa.

Ukaguzi unashauri jitihada za makusudi zichukuliwe na serikali ikiwemo kusimamia miradi mikubwa iliyoibuliwa kwa manufaa ya jamii ili iweze kuleta tija na mafanikio kwa wajamii husika.

Majibu ya Mahkama Kuu

Ushauri umepokelewa na kufanyiwa kazi, aidha hadi taarifa hii inatayarishwa Mradi huu umekamilika kwa asilimia 99 na wakati wowote Mkandarasi ataukabidhi. Kazi nyengine zinazoendelea kufanyika ambazo hazikuwemo katika mkataba wa awali ni ufungaji wa samani za ofisi na zile za kumbi za kuendeshea kesi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini sababu kadhaa zilizopeleka kuchelewa kumaliza ujenzi kama ifuatavyo:-

- Serikali kuchelewa kuchelewa kulipa “certificate za malipo” ambapo baadhi ya wakati “certificate”tatu zenye thamani ya shilingi bilioni 3zilikuwa hazijalipwa
- Mkandarasi hata alipolipwa alikuwa akifanya kazi polepole (slow)
- Tatizo la uhaba wa mchanga kama tunavojua kipindi kile kulikuwa na uhaba wa rasilimali ya mchanga .
- Maradhi ya COVID 19 pia imepelekea pia kuchelewa kwa jengo kwa sababu kulikuwa kuna baadhi ya vifaa vilikuwa vinatoka nje ya nchi , pia baadhi ya makampuni yalisitisha uzalishaji  na usafirishaji wa vifaa ulisita .
-

Kutokana sababu hizi  Serikali imechukua juhudi mbali mbali ili kuhakisha ujenzi unaendelea kama vile Serikali imetoa fedha ili ujenzi uendelee

Aidha, Kamati ilipata fursa ya kulitembelea jengo jipya la Makhaka Kuu ililopo Tunguu na kuona ujenzi  umefikia asilimia 99. Hata hivyo kulikuwa kuna baadhi ya matengenezo yalikuwa hayajakamilika kama vile fremu za Mahkama na zilikuwa hazimo kwemye mkataba , Hata hivyo Kamati imeridhika sana na hatua ya ujenzi  iliyofikia.. Sambamba na hilo Kamati ya PAC ilielezwa kuwa Mahkama Kuu imetoa wafanyakazi 20 kuwapeleka Tanzania Bara kwa ajili ya kujifunza zaidi mafunzo ya elektroniki jambo ambalo kamati imeridhika na hatua hiyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaishauri  Mahkama Kuu itoe ushirikiano wa kutosha wanapokuja wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti kwa kuwapa vielelezo vyote pale vinapoitajika

## 2.3 MAHKAMA KUU - PEMBA

### Hoja Namba 5.3.2.4. Hati za malipo zilizokosekana vielelezo shilingi 4,328,220

Jumla ya shilingi 4,328,220 zimelipwa kwa matumizi mbali mbaliya Mrajis wa jimbo Mahkama Kuu Pemba. Ukagazi umebaini kwamba kutoambatanishwa kwa vielelezo vya matumizi husika katika hati za malipo ili kuweza kudhibitisha uhalali wa malipo hayo.
Kutokuambatanisha vielelezo vya matumizi katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 3491)cha sheria ya Ununuzi wa fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 28: hati za malipo zilizokosa vielelezo

| Namba | Nambari ya hati za malipo | Aliyelipwa | Fedha zilizolipwa (SHS) | MAELELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2/11,6/11/2019 | Mahkama Kuu-Pemba | 1,640,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya shughuli za Mahkama |
| 2 | 22/11,29/11/2019 | Mahkama Kuu-Pemba | 1,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya shughuli za Mahkama |
| 3 | 1/16/1/2020 | Mahkama Kuu-Pemba | 1,688,220 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya shughuli za Mahkama |
| | | | 4,328,220 | |

Majibu ya Mahkama Kuu Pemba

Hoja imeziita vielelezo hivyo kuwa ni stakabadhi ya malipo, barua ya idhini ya malipo , na malipo kwa ajili ya tofauti ya mshahara .Vielelezo hivyo vilikosekana wakati wa ukaguzi kwa sababu baadhi ya vielelezo vilikuwa havijapatikana kutoka kwa wahusika na vyengine viliambatanishwa na hati nyengine kimakosa.Hivyobasi, naomba kukutaarifu kwamba vielelezo hivyo

vimeambatanishwa na hati husika na vipo tayari kwa ajili ya ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa kukosekana kwa vielelezo katika Hoja hii kulitokana na kukosekana kwa umakini katika uwekaji wa kumbukumbu kwa kuwa ukaguzi wa awali uliofanywa na Wakuguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti ulibaini kuwepo kwa Hoja nyingi za kukosekana kwa vielelezo vyenye thamnai ya shilingi 35,000,000. Hata hivyo, baada ya wakaguzi kufanya uhakiki na ukaguzi wa mara ya pili (verification), Hoja nyingi za vielelezo zilibainika kusawazishwa na kuondolewa isipokuwa Hoja hii moja ya vielelezo vyenye thamnai ya shilingi 4,324,220. ambapo hadi unafanyika ukaguzi wa mara ya pili (verification) vielelezo vyake viliendelea kukosekana.

Hata hivyo, Kamati ilipata nafasi ya kuvikagua na kuridhika navyo vielelezo mbalimbali vinavyohusiana na Hoja hii kama ifuatavyo :-

i. Hati ya Malipo Nambari 2/112019 pamoja na dokezo la tarehe 23/10/2019 linaloomba idhini ya malipo kwa ajili ya posho za wafanyakazi shilingi 1,640,000 ambao walitumia muda wao wa ziada na siku za mapumziko kwenda kufanya kazi.

ii. Orodha ya wafanyakazi 23 waliolipwa posho hizo pamoja na viwango vyao vya malipo hayo.

iii. Hati ya Malipo Nambari 22/11/2019 na dokezo la tarehe 5/1/2020 la kukabidhi marejesho ya stakabadhi yenye thamani ya shilingi 1,000,000 iliyolipiwa ukumbi wa Samail, Gombani uliotumika kuendeshea mafunzo ya wafanyakazi wote wa Mahkama Pemba pamoja na wadau wengine wa wa Mahkama.

iv. Stakabadhi yenye nambari A 008 ya tarehe 29/2/2019 yenye thamani ya shilingi 1,000,000 waliopewa Mahkama Kuu kutoka Samail College of Science and Technology Company Ltd ambayo ni malipo ya kodi ya Ukumbi kwa muda wa siku mbili.

v. Hati ya Malipo Nambari 2/12020 yenye jumla ya shilingi 1,688,220 ikiwa ni malipo kwa ajili ya tofauti ya mshahara.

vi. Dokezo la tarehe 8/4/2020 linalohusu malipo ya malimbikizo ya Mshahara wa Ndg. Maryam Salum Fereshi.

vii. Barua tarehe 6 Mei, 2019 yenye nambari ya kumbukumbu CB.174/196//06/3 kutoka kwa Katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango inayohusu kulipwa mshahara kamili Ndg Maryam Salum Fereshi.

viii. Karatasi ya Malipo yenye nambari 202 ya tarehe 22/4/2020 iliyotumika kum;lipa Ndg. Maryam Salum Fereshi malipo ya malimbikizo ya mshahara.

Mapendekezo ya Kamati

Watendaji wanaohusika na masuala ya fedha wa Mahkama Kuu Pemba wawe makini katika

utunzaji wa vielelezo na kuviwsilisha kwa wakaguzi kwa wakati ili wakati wa Ukaguzi kupatikane uthibitisho na uhalalli wa matumizi yaliyofanyika.

Hoja Namba 5.3.2.5 Hati za Malipn ambazo zimelipwa kwa fedha.Shillingi 4,800,000/=

Jumla ya shilingi 4,800,000 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya mahakama kuu Pemba , ukaguzi umebaini kuwa malipo hayo yamefanywa kwa njia ya fedha taslim ambapo ni kinyume na taratibu za malipo.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba malipo hayo hayakukatwa kodi ya zuio na kupelekea kuikosesha serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Hati za malipo zilizolipwa kwa fedha taslim

| Namba | Nambari ya Hati ya malipo | Fedha zilizolipwa (SHS) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 7/4, 16/4/2020 | 500,000 | Mahkama kuu – Pemba | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Ndugu Faki Hamad Faki |
| 2 | 6/4, 16/4/2020 | 4,300,000 | Mahkama Kuu Pemba | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Mrajis wa Mahkama Kuu Pemba |
| Jumla | | 4,800,000 | | |

Majibu ya Mahkama Kuu

Ni kweli fedha hizo zililipwa kwa fedha taslimu, kwa kuziingatia madai mbalimbali yaliyokuwa yakidaiwa na watendaji wa Mahkama Kanda ya Pemba, kama vile malipo ya walinzi huduma ya mtandao, malipo ya ubani wa ufiwa kwa wafanyakazi, Sare za madereva pamoja na marejeesho ya fedha zilizoazimwa kwa ajili ya kuendeshea shughuli za Mahkama katika kipindi ambacho Mahakama haikuwa na fedha na hivyo kulazimika kuazima fedha ili kukudhi matakwa ya kuendeshea kazi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC baada ya kuzichunguza Hati husika za malipo ( hati namba 7/4 ya tarehe 16/4/2020 na hati namba 6/4, ya 16/4/2020) pamoja na vielelezo mbalimbali, imebaini yafuatayo:-

i. Kuwepo kwa malipo ya watoa huduma na wasambazaji bidhaa (Suppliers) waliolipwa kwa fedha taslim (cash) kinyume na miongozo na taratibu za kifedha ambayo inaelekeza kuwa malipo yote ya watoa huduma na wasambazaji bidhaa (suppliers) yanapaswa kufanyika kwa hundi (cheque) na sio kwa fedha taslim (cash) Mfano wa malipo yaliyofanyika kwa fedha taslim (cash) kinyume na utaratibu ni malipo ya Mums Food and Refreshment kupitia stakabadhi yenye nambari 0549 ya tarehe 11/2/2020 ikiwa ni malipo ya chakula na viburudishaji katika Siku ya Sheria Zanzibar (Law Day) iliyoadhimishwa tarehe 11/2/2020.

ii. Kuchanganywa katika Hati moja ya malipo baina ya matumizi ya ndani na matumizi ya nje kwa ajili ya watoa huuma na wasambazaji bidhaa. Kwa mfano, hati ya malipo namba 6/4 yenye jumla ya shilingi 4,300,000 imechanganya malipo kwa ajili ya matumizi ya ndani (zikiwemo posho za wafanyakazi) pamoja na malipo ya nje kwa ajili ya wasambazaji bidhaa na watoa hudua (suppliers).

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Mahkama Kuu, Pemba ihakikishe kuwa inafuata kikamilifu miongozo na taratibu za kiferdha kwa kufanya malipo kwa watoa huduma  na wasmabazaji bidhaa kupitia hundi (cheque) badala ya kuwalipa watoa huduma na wasambazaji bidhaa hao kwa fedha taslim.
2. Ili kuweka utaratibu mzuri wa kumbukumbu za kifedha, watendaji wa sehemu ya fedha wa Mahkama Kuu Pemba, wametakiwa kutoshanganya matumizi ya ndani na matumizi ya nje (ya suppliers) katika hati moja ya malipo na vadala yake kila aina ya matumzi kati ya aina hizi mbili za matumizi yaandaliwe hati zake za malipo.

## 2.4 FUNGU G 04 OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA (DPP)

### Tarifa ya Mapato

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka  inakusanya mapato yake kupitia Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar. Kwa mwaka wafedha 2019/2020 Kituo kilikadiria kukusanya jumla ya Tshs.100,000,000/=.kwa bahati nzuri kituo kimefanikiwa kukusanya jumla ya Tshs 123,065,000/=.
Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti kimevuka malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa

mwaka wa fedha 2019/2020, hali hii imetokana na kuwa Kituo kimepata kusajili wanafunzi wengi kwa kipindi hicho kwa kupitia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.

MAPATO NA MAINGIZO YA RUZUKU KWA 2019/2020

| MWEZI | MAKUSANYO YA ADA | RUZUKU/OC KUTOKA DPP | JUMLA |
|---|---|---|---|
| | | | |
| JULY-SEPT | 31,596,925.00 | 3,466,666.00 | 35,063,591.00 |
| OCT-DEC | 22,785,925.00 | 5,199,999.00 | 27,985,924.00 |
| JAN-MAR | 54,706,225.00 | 3,466,666.00 | 58,172,891.00 |
| APR-JUNE | 13,975,925.00 | 4,733,000.00 | 18,708,925.00 |
| JUMLA | 123,065,000.00 | 16,866,331.00 | 139,931,331.00 |

Taarifa ya Matumzi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,890,300,000 kwa matumizi ya kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 2,527,893,079 kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 87 ya makadi

Majibu ya Ofisi ya DPP

Matumizi ya Kazi za Kawaida

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 2019/2020 ilidhinishiwa jumla ya Tshs 1,199,600,000/= kwa kazi za kawaida na fedha halisi zilizopatikana kwa kipindi hicho ni jumla ya Tshs 772,003,625/=.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilifanikiwa kuendesha kazi zake kwa kiwango kikubwa .Hata hivyo , Ofisi haikufanikiwa kukamilisha malengo yake kwa kiwango cha asilimia

mia moja kutokana na kukabiliwa na uhaba wa fedha. Kwa mfano kwa mwaka huo wa fedha, 2019/2020 Ofisi ilipanga kununuwa gari mbili aina ya Alphard lakini kutokana na uhaba wa fedha Ofisi haikuweza kununua gari hizo na badala yake Ofisi ilinunuwa gari moja ili kuiewezasha Ofisi kufanya kazi zake ili kutimiza malengo iliyojiwekea

KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

| MAELEZO | MAKADIRIO | MATUMIZI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 1,669,900,000 /= | 1,739,022,790/= | 104% |
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 1,199,600,000 /= | 772,003,625/= | 64% |
| RUZUKU | 20,800,000/= | 16,866,664/= | 81% |
| JUMLA | 2,890,300,000 /= | 2,527,893,079/= | 87% |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji kuhusiana asilimia ya mishahara imevuka asilimia 104 kwa asilimia 4. Kamati ilielezwa kuwa hali hiyo hiiimetokana na kuajiriwa kwa wafanyakazi wapya wanane

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeelezwa kuwa mapato yao sana yanategemea na idadi ya wanafunzi wanapoingia kwa hiyo mapato yanaweza kuoanda au kushuka kutokana na idadi ya wanafunzi

Hoja Namba 5.3.4.1 Kutokufungwa Hesabu za Mwisho wa Mwaka

Katika ukaguzi uliofanyika, imebainika kwamba Kituo cha Sheria (ZLRC) hakijafunga hesabu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa mujibu wa kifungu cha 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Kutokufunga na kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kwenda kinyume na kifungu nambari 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka inakiri kutokea kwa mapungufu hayo kwa kipindi hicho cha ufungaji wa hesabu. Hili lilitokana na Mhasibu wa Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti kupata uhamisho wa kikazi kwenda Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar na kupelekea kutokuwepo kwa Mhasibu wa kusimamia jambo hilo.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka tayari imeshasawazisha kosa hilo ambapo kwa sasa Ofisi imeshaweka Mhasibu mwengine wa Kituo kwa ajili ya kusimamia masuala yote ya hesabu za Kituo hicho ili kuepuka kutokea mapungufu kama hayo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashataka imekiri kufanya kosa hilo la kutokuwa na Mhasibu na kutofungwa hesabu kwa Kituo cha Sheria. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilielezwa kuwa Ofisis ya Rais Fedha na Mipango haikuweza kumpeleka mhasibu mwengine katika Kituo hicho kutokana nay a upungufu wa Watendaji na kulikuwa hakuna ajira mpya .. Aidha, ilibainika pia kuwa Aliyekuwa mhasibu wa Kituo hicho amehamishwa mwezi wa April 2020 na kuhamishiwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango). Aidha, Kamati ya PAC ilibaini kuwa Ofisis ya Mkurugenzi wa Mashtaka imechelewa kuomba Mhasibu mwengine ambapo barua ya kumuomba mhasibu mwengine kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ni yat tarehe 18/11/2021.

Sambamba na hilo, Kamati imebaini kuwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imemtoa Msaidzi Mhasibu wa Ofisi hiyo Makao Makuu kufunga hesabu za Kituo ingwa Msaidzi Mhasibu huyo hajapata uzoefu mkubwa.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ihakaikishe kuwa inafunga hesabu za Taasisi zake kwa wakati ambapo ikitokea uhamisho unahitaji watendaji kujaza nafasi ifuatilie kwa maandishi na kwa wakati

Hoja Namba 5.3.3.2 Madeni ya Wanafunzi Shilingi 32,962,000

Katika ukaguzi uliofanyika, kumebainika uwepo wa madeni ya wanafunzi ya muda mrefu ambayo hakuna jitihada zozote zilizofanywa katika ufuatiliaji wa kuhakikisha madeni hayo yanalipwa jambo ambalo linapelekea kuathiri shughuli za Kituo cha Sheria.

Aidha, kutokuwepo kwa ufuatiliaji mzuri wa madeni kunapelekea uwepo wa madeni sugu ambayo hayataweza kulipika na kupelekea kuibabasha mzigo mkubwa Serikali. Kuongezeka kwa madeni kunachangiwa na kutokuwepo kwa jitihada za kulipa madeni hayo kwa wakati.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kushirikiana na Kituo cha Sheria kufuatilia madeni na kuhakikisha kwamba madeni hayo yanalipwa kwa wakati. Mchanganua wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 31: Madeni ya Wanafunzi wa Ngazi ya Astashahada

| Namba | Jina Kamili | Bakaa (SHS) |
|---|---|---|
| 1 | Hamad M. Hamad | 485,000.00 |
| 2 | Imani Yahya Iddi | 485,000.00 |
| 3 | Shaaban Khamis Yussuf | 485,000.00 |
| 4 | Mohd Juma Mohd | 485,000.00 |
| 5 | Fatma Kassim Suleiman | 285,000.00 |
| 6 | Fatma Nyanga Rashid | 485,000.00 |
| 7 | Khairat Haji Kombo | 485,000.00 |
| 8 | Magret Edward Kaleza | 485,000.00 |
| 9 | Tauhyda Haji Nyonje | 485,000.00 |
| 10 | Taubat Ali Hamdu | 125,000.00 |
| 11 | Nassra Suleiman Ali | 485,000.00 |
| JUMLA | | 4,775,000.00 |

: Madeni ya Wanafunzi wa Ngazi ya Stashahada

| Namba | Jina Kamili | Bakaa (SHS) |
|---|---|---|
| 1 | Abdulsalami Muhamed Ameir | 500,000.00 |
| 2 | Abdulhamid Masiku Juma | 535,000.00 |
| 3 | Abdulkadir Hassan Hassan | 535,000.00 |
| 4 | Amir Omar Fakih | 535,000.00 |
| 5 | Khamis Omar Said | 532,000.00 |
| 6 | Mahfoudh Shaame Mahfoudh | 535,000.00 |
| 7 | Mohd U. Mjenge | 535,000.00 |
| 8 | Ramadhan Omar Ali | 535,000.00 |
| 9 | Saleh M. Saleh | 535,000.00 |
| 10 | Shehe O. Hamad | 535,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 11 | Waziri Kh. Abdulla | 535,000.00 |
| 12 | Haitham Suleiman Soud | 535,000.00 |
| 13 | Hajira Abeid Omar | 535,000.00 |
| 14 | Moza Said Ali | 535,000.00 |
| 15 | Naifat Kombo Hafidh | 535,000.00 |
| 16 | Nasira Mikidadi Nuru | 535,000.00 |
| 17 | Perus Erenes Joseph | 535,000.00 |
| 18 | Raudha Ali Mohamed | 535,000.00 |
| 19 | Salma K. Salim | 535,000.00 |
| 20 | Faidha Hemed Hai | 535,000.00 |
| | Jumla Ndogo | 10,662,000.00 |
| 1 | Suleiman Haji Iddi | 535,000.00 |
| 2 | Yussuf Suleiman Mohd | 535,000.00 |
| 3 | Alistidius John Kaloli | 835,000.00 |
| 4 | Huzaima Saleh Mohamed | 140,000.00 |
| 5 | Maryam Nurdin Hashim | 535,000.00 |
| 6 | Mwatima Maulid Khamis | 535,000.00 |
| 7 | Raiye Mohamed Juma | 535,000.00 |
| 8 | Samira Hassan Maulid | 335,000.00 |
| 9 | Farhiya M. Farhan | 535,000.00 |
| Jumla Ndogo | | 4,420,000.00 |
| | Jumla Kuu | 15,082,000.00 |

MADENI YA MUDA MREFU

Jadweli Nambari 33: Madeni ya Wanafunzi wa Legal Drafting Course 2018/2019

| Namba | Jina Kamili la Mdaiwa | Taasisi Anayotokea | Bakaa la Deni Analodaiwa | Tarehe na Mwaka wa Masomo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mwanaasha Khamis | Baraza la Wawakilishi | 1,000,000.00 | 4/4/2018 |
| 2 | Said Khamis Ramadhan | | 1,000,000.00 | 19/12/2017 |
| 3 | Said Nassor Said | Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala Bora | 1,000,000.00 | 1/5/2014 |
| 4 | Rahma S. Fundi | Tume ya Kurekebisha Sheria | 200,000.00 | 20/1/2015 |
| 5 | Amina M. Jabir | Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais | 900,000.00 | 1/4/2015 |
| 6 | Ramadhan Seif Salum | Ofisi ya Rais | 400,000.00 | 1/7/2014 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7 | Nassor Said Massoud | Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto | 300,000.00 | 26/3/2018 |
| 8 | Juma Ngwali Ahmed | KMKM (PEMBA) | 1,000,000.00 | 28/8/2018 |
| Jumla Ndogo | | | 6,800,000.00 | |

| Mafunzo ya Muda Mfupi Wiki 2 (Tarehe 16 – 31/12/2019) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Amina Ali Haji | KMKM | 300,000.00 | |
| 2 | Hamza Hassan Juma | Baraza la Wawakilishi | 800,000.00 | |
| 3 | Fatma Omar Ali | | 800,000.00 | |
| 4 | Mohammed Said Mohammed | | 800,000.00 | |
| 5 | Abdulla Ali Shauri | | 800,000.00 | |
| 6 | Ame Burhan Shadhil | Tawala za Mikoa | 800,000.00 | |
| | Jumla Ndogo | | 4,300,000.00 | |
| JUMLA KUU | | | 11,100,000.00 | |

Majibu ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka inakiri kuwa wakati mkaguzi alipofanya kazi zake alibaini kuwa kuna deni la shilingi 32,962,000/= kwa wanafunzi ambao wanajifunza katika ngazi mbali mbali zinazotolewa na kituo hicho cha sheria zikiwemo ngazi ya cheti na diploma.

Ofisi kwa kushirikiana na Kituo imechukua hatua thabiti ya kufuatilia madeni yote ya Kituo nahadi sasa deni lililobakia ni Shilingi 7,300,000/= Deni ambalo Ofisi inaendelea na juhudi za kulifuatilia.

MADENI YA WANAFUNZI WA CHETI

| NAMBA | JINA KAMILI | KIWANGO ANACHODAIWA |
|---|---|---|
| 1 | HAMAD M HAMAD | NIL |
| 2 | IMANI YAHYA IDDI | NIL |
| 3 | SHABAAN KHAMIS YUSSUF | NIL |
| 4 | MOHD JUMA MOHD | NIL |
| 5 | FATMA KASSIM SULEIMAN | NIL |
| 6 | FATMA NYANGA RASHID | NIL |
| 7 | KHAIRAT HAJI KOMBO | NIL |
| 8 | MAGRET EDWAED KALEZA | NIL |

| | | |
|---|---|---|
| 9 | TAUHYDA HAJI NYONJE | NIL |
| 10 | TAUBAT ALI HAMDU | NIL |
| 11 | NASRA SULEIMAN ALI | NIL |
| | Jumla ndogo | 00.00 |

:MADENI YA WANAFUNZI WA DIPLOMA

| NAMBA | JINA KAMILI | KIWANGO ANACHODAIWA |
|---|---|---|
| 1 | ABDULSALAMI MUHAMED AMEIR | 500,000/= |
| 2 | ABDULHAMID MASIKU JUMA | NIL |
| 3 | ABDULKADIR HASSAN HASSAN | NIL |
| 4 | AMIR OMAR FAKIH | NIL |
| 5 | MAHFOUDH SHAAME MAHFOUDH | NIL |
| 6 | MOHD U MJENGE | NIL |
| 7 | RAMADHANI OMAR ALI | NIL |
| 8 | SALEH M SALEH | NIL |
| 9 | SHEHE O HAMAD | NIL |
| 10 | WAZIR KH ABDULLA | NIL |
| 11 | HAITHAM SULEIMAN SOUD | NIL |
| 12 | KHAMIS OMAR SAID | NIL |
| 13 | HAJRA ABEID OMAR | NIL |
| 14 | MOZA SAID ALI | NIL |
| 15 | NAIFAT KOMBO HAFIDH | NIL |
| 16 | NASIRA MIKIDADI NURU | NIL |
| 17 | PERUS ERENES JOSEPH | NIL |
| 18 | RAWDHA ALI MOHAMED | NIL |
| 19 | SALMA K SALIM | NIL |
| 20 | FAIDHA HEMED HAI | NIL |
| | Jumla ndogo | 500,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 1 | SULEIMAN HAJI IDDI | NIL |
| 2 | YUSSUF SULEIMAN MOHD | NIL |
| 3 | ALISTIDIUS JOHN KALOLI | NIL |
| 4 | HUZAIMA SALEH MOHAMED | NIL |
| 5 | MARYAM NURDIN HASHIM | NIL |
| 6 | MWATIMA MAULID KHAMIS | NIL |
| 7 | RAIYE MOHAMED JUMA | NIL |
| 8 | SAMIRA HASSAN MAULID | NIL |
| 9 | FARHIYA M FARHAN | NIL |
| | Jumla ndogo | 00.00 |

J:Madeni ya wanafunzi wa Legal Drafting Course 2018/2019

| Nambari | Jina kamili la mdaiwa | Taasisi anayotokea | Bakaa la deni | Tarehe na mwaka wa masomo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mwanaasha Khamis | Baraza la Wawakilishi | 1,000,000/= | 4/4/2018 |
| 2 | Said Khamis Ramadhan | Baraza la Wawakilishi | NIL | 19/12/2017 |
| 3 | Said Nassor Said | Wizara ya Katiba na Sheria na Utawala Bora | 1,000,000 | 1/5/2014 |
| 4 | Rahma S. Fundi | Tume ya Kurekebisha Sheria | 200,000/= | 20/01/2015 |
| 5 | Rahma S.Fundi | Tume ya Kurekebisha Sheria | 900,000/= | 01/04/2015 |
| 6 | Amina M. Jabir | Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais | 400,000 | 01/07/2014 |
| 7 | Ramadhani Seif Salum | Afisi wa Rais | 300,000/= | 26/03/2018 |
| 8 | Nassor Said Masoud | Wizara ya kazi uwezeshaji wazee wanawake na watoto | 1,000,000/= | 26/03/2018 |
| 9 | Juma Ngwali Ahmed | KMKM (PEMBA) | 1,000,000/= | 28/08/2018 |
| | Jumla ndogo | | 5,800,000/= | |

Mafunzo ya muda mfupi wiki 2 (Tarehe 16-31/12/2019

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Amina Ali Haji | KMKM | 200,000/= |
| 2 | Hamza Hassan Juma | BLW | NIL |
| 3 | Fatma Omar Ali | BLW | NIL |
| 4 | Mohammed Said Mohammed | BLW | NIL |
| 5 | Abdulla Ali Shauri | BLW | NIL |
| 6 | Ame Burhan Shadhil | TAWALA ZA MIKOA | 800,000/= |
| | Jumla ndogo | | 1,000,000/= |
| | JUMLA KUU | | 7,300,000/= |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imetaka kujua ni hatua gani zilizochukuliwa katika kudai deni kwa mwanafunzi ambao alokuwa hajalipa na kuelezwa kuwa huwa hafanyi mtihani , na kamati imebaini wadaiwa wakubwa ni wa mafunzo ya uda mfupi (short course) ambao wengine wanatoka Taasisi za Serikali. Kamati ilikagua baadhi ya vilelezo vya madeni yaliolipwa kama vile stakabadhi (risiti) mbalimbali.

Vile vile Kamati ilielezwa kuwa Mkurungezi wa Mashataka wamechukua jitihada mbali mbali za kuandika barua kwa ajili ya kulipa madeni kwa baadhi ya taasisi ambapo Kamati ilielezwa kuwa deni limelipwa limelipwa kwa asilimia 78. Aidha, Kamati ilikagakua barua za ukiumbusho wa kulipa madeni Kamati imeridhika na maelezo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Ofisis ya Mkurugenzi wa Mashtaka izidishe juhudi za kiuyafuatilia madeni ya wanafunzi wa Kituo cha Sheria ili kiweze kuimarisha vyema shughuli zake.

## 2.5 OFISI YA KURUGENZI WA MASHTAKA PEMBA

### Hoja Namba 5.3.4.3 Mmanunuzi yaliyofanyika kinyume na utaratibu shilling 5,569,500

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha sheria ya Manunuzi na uondoshaji wa Mali za Umma Kinaeleza “kulinga na masharti ya sharia hii mtu,kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya umma isipokuwa mtu huyo , kampuni au chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka chini ya sheria hii”
Kwa mujibu wa kifungucha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.
Ukaguzi umebaini Ofisi ya Mkurungenzi wa Mashtaka imefanyika manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambapo watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi kwa mujibu wa sheria ambapo kumepelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa malipo hayo.
Kuwatumia watoa huduma ambao hawakusajiliwa kwa mujibuwa sheria kunapelekea kuikosesha mapato yanayotokana na kodi ya thamani na nikwenda kinyume na sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za umma nambari 11 ya mwaka 2016.
mchanganuo wa manunuzi hayo ni kama inavyoonekana katika jadwel lifuatalo.

Jadwel Nanbari 32: Manunuzi yaliyofanyika kinyume na utaratibu

| Namba | Nambari ya hati ya malipo | Nambari ya hundi ya malipo | Jumla ya fedha | aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1/11, 10/11/2019 | 10570 | 500,000 | Afsi ya Mkurugenzi Mashataka (Nabhsny auto mobile) | Ikiwa ni malipo ya awali |
| 2 | 27/12, 30/12/20219 | 11957 | | Afisi ya Mkurugenzi Mashataka | Ikiwa ni malipo ya awali kwa ajili ya vitasa vya ujenzi wa sehaemu ya kuegesha magari |
| 3 | 1/1, 3/1/2020 | 12100 | | Afisi ya Mkurugenzi Mashataka | Ikiwa ni malipo ya awali kwa ajili ya vitasa vya ujenzi wa sehaemu ya kuegesha magari |

**Majibu ya Ofisi ya DPP Pemba kuhusu taa za gari SMZ 233A kutoka kwa Mtoa Huduma ambae hahasajiliwa.**

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imepokea pendekezo na ushauri uliotolewa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikalipamoja na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa kuchukuwa jitihada za kuhakikisha kwamba mtu, kampuni, taasisi au chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) kama sheria inavyotaka.

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka inakiri kuwa manunuzi yamefanyika kwa mtowa huduma (Nabhany Auto Mobile) ambae hakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi kwa mujibu wa kifungu cha 23(2).

Manunuzi haya yalifanyika kwa mtoa huduma huyo kutokana na kuwa gari SMZ 233A aina ya Suzuki Saloon kupata ajali na kusababisha taa za mbele (Head lamp) kuvunjika.Afisiilifanya juhudi ya kutafuta taa hizo kwa watoa huduma wa Pemba nakwa wakati huo ilishindikana kuzipata taa hizo kwa watoa huduma hao. Afisi ililazimika kuendelea na juhudi ya kuzitafuta taa hizo Unguja ambapo pia ilikosa kupata taa hizo na kuanza hatua za kuangalia uwezekano wa kuagizia nje ya nchi lakini kwa bahati mbaya kuagiza nje ya nchi ingelichukuwa muda mrefu wa kuzipata taa hizo.Hata hivyo juhudi za kutafuta taa hizo ziliendelea na Afisi ilifanikiwa kuziona taa hizo kwa mtoa huduma mmoja tu kwa wakati huo ambaye ni Nabhany Auto Mobile.

Kwa kuwa aina ya gari hii ni kongwe na hapa Zanzibar ni chache na vipuri vyake vimekuwa adimu kwa watoa huduma wengi wa vifaa vya magari, na kwakuwa Afisi inaitegemea gari hii kwa utekelezaji wa shughuli zakeza kila siku, Afisi iliona busara kufanya ununuzi wa taa hizo kwa madhumuni ya kuiwezesha gari hiyo kutumika ili kunusuru kukwama kwa shughuli za Afisi.

Hata hivyo Afisi inakiri kwamba imepata funzo kutokana na ununuzi huu na inaahidi kuwa ununuzi kwa mtoa huduma ambae hajasajiliwa hautofanyika tena.

Majibu ya Hoja za vifaa vya ujenzi wa eneo la megesho ya gari awamu ya kwanza nay a pili

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka inakubali kuwa wakati Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alipokuwa akifanya kazi zake, alibaini kuwa Afisi imefanya malipo kwa ajili ya ununuzi wa mchanga, kokoto na kifusi kwa mtowa huduma (Ndg. Azizi Mahmoud Nassor) ambae hakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi kwa mujibu wa kifungu cha 23(2).

Kabla ya malipo haya kufanyika Afisi ilifanya juhudi za kuwasiliana na Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi kwa ajili ya kupatiwa tathmini za ujenzi wa maegesho ya magari. Wizara hio iliipatia tathmini ya T.shs 11,957,000/ kwa sehemu moja ya nje tu ya maegesho. Kutokana na uhaba wa fedha Afisi ilishindwa kumudu gharama hizo za ujenzi na kuanza kutumia njia nyengine mbadala, na ndipo ilipoamua kuwasiliana na kampuni binafsi ya ujenzi inayoitwa ALBATNA. Kampuni hio iliipatia Afisi tathmini ya T.shs 8,500,000/ kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya nje tu ya maegesho. Hivyo kutokana na uhaba wa fedha Afisi ilishindwa kumudu gharama hizo, na kwa kuzingatia umuhimu mkubwa na unyeti wa ujenzi huo, Afisihaikuvunjika moyo na badala yake ilibuni wazo la kuomba kifusi katika Wizara ya Mawasiliano ambapo ombi hilo lilikubaliwa na kupewa tani 45 bila ya malipo. Kutokana na hali hiyo Afisi ilishawishika na kutoa maamuzi ya

kujenga ujenzi huokwa kutumia mafundi na watoa huduma wa vifaa vya ujenzi binafsi.

Pamoja na maelezo hayo, Afisi inakiri kwamba imepata funzo kutokana na ununuzi huu na inaahidi kuwa ununuzi kwa mtoa huduma ambae hajasajiliwa hautofanyika tena.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kujirdhisha na maelezo hayo na kuhakikisha kuwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba imejirekebisha kutokana na makosa iliyokiri kuyafanya hapo awali, Kamati kupitia stakabadhi za baadhi ya watao huduma waliokuwa wanaoendelea kutoa huduma za bidhaa mbali mbali kwa Ofisi hiyo hivi sasa wakiwemo Yussuff Grafix, Capital Technology Centre, na Ngoto Auto Accessories imeridhika kuwa watoaji huduma hao (hadi wakati Kamati ilipofanya kikao na watendaji wa DPP Pemba tarehe 25/8/2021) wamesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Zanzibar kama inavyyonekana katika jadweli lifuatalo:-

| S/N | JINA LA MTOA HUDUMA | AINA YA HUDUMA | NAMBARI YA USAJILI | TAREHE YA KUMALIZA MUDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | CAPITAL TECHNOLOGY | “STATIONERIES” | ZPPDA/G065/2021 | 13/1/2022 |
| 2 | NGOTO AUTO ACCESSORIES | “SPARE AND DECORATION” | Zppda/g/088/2021 | 16/1/2021 |
| 3 | YUSSUF GRAFIX | “STATIONERIES” | ZPPDA/G0335/2021 | 5/3/2022 |

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba inapaswa kutekeleza kikamilifu Sheria zilizopo ikiwemo Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma pale inapohitaji kununua bidhaa na huduma mbalimbali hasa ikizingatiwa kuwa Ofisi hii ni miongoni mwa Taasisi muhimu zinasomima utekelezaji wa Sheria hapa nchini

## 2.6 FUNGU F 02 HESABU ZA HUDUMA ZA MFIKO MKUU WA SERIKALI

Taarifa ya Matumizi

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Hesabu za Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali ilikadiriwa kutumia jumla ya shiingi 159,417,700,000 kwa ajili ya utoaji wa huduma mbali za Mfuko Mkuu zikiwemo ulipaji wa Kiinua Mgongo, Pencheni, Madeni ya Serikali na Mishahara ya Viongozi wanaostahiki kwa mujibu wa Sheria kulipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia tareh 30 Juni 2020, jumla ya shilingi 155,388,853,705 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ikiwa sawa na asilimia 97.5 ya makadirio.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Miapngo

Mfuko Mkuu wa Serikali unahusisha usimamizi wa matumizi ya huduma zinazotolewa na Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwemo ulipaji wa Kiinua Mgongo na Pencheni kwa Wastaafu wa SMZ, kulipa madai ya Wazabuni wa Serikali, kulipia hati fungani zilizofikia muda na malipo mengineyo.

FEDHA ZILIZOINGIZWA MFUKO MKUU WA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 NA UCHAMBUZI WAKE.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya TZS. 155.38 bilioni zimeingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Makadirio ilikuwa ni kupokea jumla ya TZS. 159.42 bilioni sawa na asilimia 97 ya makadirio.

Jadweli lifuatalo hapo chini linaonesha mchanganuo wa fedha zilizokadiriwa kutumika, fedha zilizotumika na kiwango cha matumizi kwa asilimia ukilinganisha na makadirio.

| VIFUNGU | MAKADIRIO YA MATUMIZI 2019/2020 TZS. BILIONI | MATUMIZI HALISI 2019/2020 TZS. BILIONI | UTEKELEZAJI % |
|---|---|---|---|
| Malipo ya mafao ya Kiinua Mgongo kwa wastaafu wa SMZ | 27.50 | 26.11 | 95 |
| Malipo ya Pencheni kwa wastaafu wa SMZ | 27.93 | 27.77 | 99 |
| Malipo ya Mikopo ya ndani | 14.51 | 13.83 | 95 |
| Matumizi mbali mbali ya Serikali | 89.47 | 87.67 | 98 |
| **Jumla ya Matumizi** | **159.41** | **155.38** | **97** |

*Chanzo: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS)*

MCHANGANUO WA VIFUNGU

MALIPO YA MIKOPO YA NDANI

Malipo ya Mikopo ya Ndani imejumuisha malipo ya riba ya hati fungane, riba ya Mkopo wa ZSSF, marejesho ya mkopo wa Benki ya Watu wa Zanzibar na dhamana za Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Mfuko Mkuu umetumia jumla ya TZS.13.83 bilioni kwa ajili ya malipo ya Riba na Mikopo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mchanganuo unaonekana katika jadweli la hapo chini:

| MADHUMUNI YA MALIPO | IDADI TZS. BILIONI |
|---|---|
| Riba ya Hati Fungane "Interest on Treasury Bond" | 7.80 |
| Riba ya Mkopo ya ZSSF | 1.25 |
| Marejesho ya Mkopo ya Benki ya Watu ya Zanzibar (PBZ) | 1.96 |
| Dhamana za Serikali | 2.82 |
| JUMLA | 13.83 |

*Chanzo: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS)*

MALIPO YA KIINUA MGONGO NA PENCHENI

Mfuko Mkuu ulikadiria kutumia jumla ya TZS. 27.5 bilioni kwa ajili ya kulipa Kiinua Mgongo kwa wastaafu 991 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hadi kufikia tarehe 30/06/2020, Mfuko umefanikiwa kulipa TZS. 26.11 bilioni sawa na asilimia 95 ya makadirio. Aidha, kwa upande wa Pencheni Mfuko ulikadiria kutumika TZS. 27.9 bilioni na kutumia TZS. 27.7 sawa naasilimia 99 ya makadirio kwa wastani wa wastaafu 13,000 kwa mwezi.

MATUMIZI MENGINEYO

Hadi kufikia tarehe 30/06/2020 Mfuko Mkuu umetumia jumla ya TZS. 87.68 bilionikwa ajili ya malipo mbali mbali ya huduma za Serikali. Malipo yenyewe ni kama ifuatavyo Safari za Ndani na Nje za Viongozi Wakuu, Mishahara ya Viongozi Wakuu, Ruzuku kwa Vyama vya Siasa vyenye Uwakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi, Madeni ya Wazabunina Matumizi maalum ya Serikali. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

| VIFUNGU | IDADI YA FEDHA ILIYOTUMIKA TZS. BILIONI |
|---|---|
| Safari za Ndani na Nje za Viongozi wakuu | 6.14 |
| Mishahara ya Viongozi wakuu | 1.23 |
| Ruzuku kwa Vyama vya Siasa vyenye Uwakilishi BLW | 1.29 |
| Matumizi mbali mbali ya Serikali | 79.02 |
| JUMLA | 87.68 |

*Chanzo: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS)*

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilhoji malipo ya Pencheni hawakufikia lengo na wangapi wamelipwa na wangapi hawajalipwa. Kamati imepata majibu kuwa kwa mwaka 2021 wamelipwa pencheni wastaafu 26 kutoka na uwezo wa Serikali wa kifedha. Kamati ya PAC imekagua baadhi ya nyaraka za amlipo ya pencheni. Kwa ujum ujmla Kamati ya PAC imeridhika na

majibu pamoja naufafanuzi uliotolewa

2,7 MFUKO MKUU WA SERIKALI

MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUKO MKUU WA SERIKALI

Hoja namba 3.2.1 – Mapungufu katika uandaaji wa Hesabu Jumuishi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ukaguzi wa Hesabu jumuishi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinazoishia 30 Juni, 2020 ulibaini kutojumuishwa hesabu za Taasisi mbalimbali ikiwemo hesabu za Serikali za Mitaa , hesabu za Mashirika ya Umma pamoja na baadhi ya hesabu za Mamlaka za Serikali. Kutojumuishwa kwa baadhi ya hesabu za Taasisi zilizobainishwa katika ripoti hii kunaondoa sura sahihi na halisi ya hesabu jumuishi na kupelekea kutoonesha uhalisia wa hali ya kifedha za Serikali.

Majibu kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Jumuisho la Hesabu za Serikali huandaliwa Hesabu zake kwa kutumia Vote husika , hivyo basi Hesabu za Serikali za Mitaa zinakuwemo kwenye Vote ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.
Kwa upande wa Mashirika nikweli hazijumuishwi kwenye Jumuisho za Hesabu za Serikali kutokana na sababu zifuatazo:

a) Kukosa uwiano wa pamoja wa ufungaji wa Hesabu za Serikali  na Hesabu za Mashirika ikiwemo muda wa ufungaji wa Hesabu na mifumo yao ya uandaaji wa Taarifa za za Hesabu.

b) Kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya ufungaji wa hesabu, Mashirika ya Umma hutumia viwango (Standards) tofauti na Taasisi za Kibajeti kwa maana ya Wizara na Taasisi zinazopata bajeti ya Serikali. Kutokana na hali hiyo Taasisi zinazosimamia utoaji wa Viwango vya Ufungaji wa hesabu vya Kimataifa imetoa muongozowa  uandaaji wa Hesabu za Serikali "IPSAS"35kwa Hesabu za Serikali zenye mfumo sawa wa uwandaaji.

Hata hivyo Idara ya Muhasibu Mkuu waSerikali imeanza taratibu na kuanza kujumuisha hesabu za Mashirika ya Umma ambao mifumo yao ya ufungaji wa Hesabu zao zinafanana.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kwa ujumla Kamati Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Wizara

**Hoja Namba 3.2.2 Kuwepo kwa utofauti wa Uaandaaji na Uwasilishwaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka kwa Wizara na Mashirika ya Umma**

Kwa mujibu wa kifungu 119 (1) cha Sheria ya Usimamaizi wa Fedha za Umma Nanba 12 ya mwaka 1016, Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatakwa zitayarishe na ziwasilishwe kw aMdhibiti na Mkanguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu badala ya kumalizika mwaka wa fedha ambapo hesabu hizo zitajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya taasisi hizo

Ukaguzi wa Hesabu jumuishi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinazoishia 30juni, 2020 ulibaini kuwepo kwa tofauti wa tarehe za ufungaji wa uwasilishwaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa Wizara na Mashirika ambapo Mashirika ya Umma yanafunga hesabu kwa mujibu wa mwaka wa fedha unayoishia 31 Disemba

**Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango**

Kwa upande wa Mashirika nikweli hazijumuishwi kwenye Jumuisho za Hesabu za Serikali kutokana na sababu zifuatazo:

a) Kukosa uwiano wa pamoja wa ufungaji wa Hesabu za Serikali na Hesabu za Mashirika ikiwemo muda wa ufungaji wa Hesabu na mifumo yao ya uandaaji wa Taarifa za za Hesabu.

b) Kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya ufungaji wa hesabu, Mashirika ya Umma hutumia viwango (Standards) tofauti na Taasisi za Kibajeti kwa maana ya Wizara na Taasisi zinazopata bajeti ya Serikali. Kutokana na hali hiyo Taasisi zinazosimamia utoaji wa Viwango vya Ufungaji wa hesabu vya Kimataifa imetoa muongozowa uandaaji wa Hesabu za Serikali "IPSAS"35kwa Hesabu za Serikali zenye mfumo sawa wa uwandaaji.

Hata hivyo Idara ya Muhasibu Mkuu waSerikali imeanza taratibu na kuanza kujumuisha hesabu za Mashirika ya Umma ambao mifumo yao ya ufungaji wa Hesabu zao zinafanana.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imeelezwa kuwa kuna baadhi ya Mashirika kama vile PBZ kwa ajili ya biashara wao wanao mfumo wao wa ufungaji wa hesabau wanafunga Januari mpaka Disemba .lakini kama Mashirika mengine kama vile kamapuni ya mafuta na Gesi asilia yanaweza kufata mfumo wa Taasisi Julai mpaka Juni. Vile vile Mashirika kama PBZ yana msimamzi wake Benki kUuu na Shirika Bima msomamzi wake ni TIRA. Kamati ilielezwa kuwa tayari Wizara ya Fedha na Mipango wapo kwenye kutayarisha kitabu kimoja cha ufungaji wa Hesabu.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipnago kuyaangalia Mashirika ya Serikali ilikuwe na mfumo mmoja tu wa ufungaji wa hesabu baina ya Taasisi na Mashirika

Hoja namba: 3.2.3 Kukosekana kwa mchanganuo wa mapato.

Hesabu jumuishi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinaonyesha kuwa Serikali imekusanya mapato yenye jumla ya TZS 675,461,000,000 yanayotokana na kodi na TZS 100,740,000,000 zinazotokana na makusanyo yasiyo na kodi.

Ukaguzi umebaini kuwa hesabu jumuishi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka wa fedha 2019/2020 haikuambatanishwa na mchanganuo wa kiasi kilichokusanywa na kila Taasisi ya Serikali inayotoza kodi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kiasi cha mapato yaliyokusanywa na kila Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Kutokuweka mchanganuo wa mapato ya hesabu jumuishi kunapelekea kukosekana kwa uhalisia na ukamilifu wa mapato yaliyoripotiwa katika hesabu jumuishi za Serikali.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Katika uwaandaaji wa Hesabu za Serikali uwasilishaji wake unakua kwa mfumo wa " by nature" na sio " by function" hivyo basi Mapato hayo yamewekwa na yamewasilisha kwa "nature" yake kwenye ripoti za Fedha na uchanganuzi wake upo kwenye "note statements" kama zilivyowasiliswa kwenye "Financial Statements." Kwa uchanganuzi wa vyanzo vya Mapato zinaonekana kwenye ripoti za Fedha ya kitabu cha Wizara Fedha na Mipango Ripoti za kiutendaji za Divisheni ya usimamizi wa fedha., Idara ya Mhasibu Mkuu imechukua ushauri wa Mkaguzi na kuongeza uwasilishaji ulopendekezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilielezwa kuwa mapato ya by nature ni mapato ya kodi na mapato ya by function ni mapato yasiyo ya kodi. Kamati ya PAC ilitaka kuona financial statement ili kujua kama kunamchanganuo wa kina wa mapato kama hoja ya Mdhibiti ilivyo na kubainika kuwa hakuna mchnganuo wa mapato yanayotoka katika Taasisi moja moja na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imekiri dosari hiyo na kahidi kuirekebisha

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inapendekeza kuwa Afisi ya Raisi Fedha na Mipango waoneshe mchanganuo wa mapato ya kila Taasisi au Wizara na vyanzo vya Mapato katika hesabu jumuishi

### Hoja namba 5.6.2: Malipo ambayo hayakufata utaratibu wa manunuzi USD 1,937,900. [TZS 4,450,306,238]

Ukaguzi umebaini Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imefanya malipo ya TZS 4,450,306,238 kupitia Hesabu ya Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Kampuni ya Al- Noor Motors ya Dubai, kupitia hati za malipo nambari 30/07 ya tarehe 12/07/2019, 36/09 ya tarehe 16/09/2019 na hati ya madai nambari 100170 ya tarehe 11/06/2019 kwa ajili ya ununuzi wa gari 43 kwa matumizi ya Taasisi mbalimbali za Serikali.

Ukaguzi umebaini kukiukwa kwa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa kutofuatwa taratibu za ununuzi zilizoelekezwa na Sheria hiyo, dosari hizo ni kama zifuatazo:

i. Kutoitishwa kwa zabuni za wazi ya kimataifa ya kuwaalika Wasambazaji wenye uwezo wa usambazaji wa gari hizo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 69 (1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.
ii. Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Fedha na Mipango inatumika kama Wakala wa kununua magari kwa niaba ya Taasisi nyengine za Serikali, utaratibu ambao unazibana Taasisi za Serikali zisizo na uwezo wa kumudu gharama za ununuzi wa magari ya gharama kubwa kwa mujibu wa bajeti zao ambapo, Taasisi hizo hazina uwezo wa kumudu gharama za matengenezo pamoja na mafuta kwa ajili ya uendeshaji .Kufanya hivyo kunapelekea kuibana Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Utaratibu wa manunuzi ulifuatwa kwa kuwa njia iliyotumika ya zabuni (Ristricted bidding method) imepitishwa na Bodi ya zabuni ya Wizara na imeruhusiwa na sheria ya Manunuzi namba 11 ya 2016 kifungu nambari 71, na kuhakikisha ushindani unapatikana kampuni sita (6) za usambaji wa magari zimeshirikishwa na mzabuni aliyeshinda zabuni ni Al-Noor Motors ambae alikuwa na gharama nafuu kutokana na ripoti ya tathmini.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati yaPAC ilitaka kujua sababu za kutumia Risstrected Bidding method, na kuelezwa kuwa Wizara imezingatia muda pia wamepata ruhusa kutoka mamlaka ya wanunuzi na uthibitisho wa barua (ya tarehe 2/1/2019 yenye nambari ya kumbukumbu AB/173/01/67) hata hivyo, barua hiyo ilikisha mtaja msambazaji awe Al Nour Motors.

Hata hivyo, Kamati imeelezwa kuwa wametumia pre-qualification ndani na nje ya Zanzibar katika kutafuta mshindani wa tender hii.kamavile Dar es salam hata Dubai, viel viel Wizara ilifanya pia Pre –colification pia walikwenda hadi kwenye kampuni kabla hawajaingia kwenye mkataba ili kujua ubora wa kampuni hizo.

Kamati ilielezwa kuwa kampuni ya AL –NOOR MOTOR alipewa kwa sabaubu alikuwa na sifa mbalimbali ,muda mdogo wa kusubiri magari yafike na ni gharama nafuu

Kamati imebata uthibitisho wa barua mamlaka ya manunuzi na uondoshwaji wa mali za Umma KUMB:AB.7/173/01/67 Tarehe 2/01/2019 inayosema kufanya kwa manunuzi ya pamoja magari kwa matumizi ya taasisi mbali mbali. Kamati iloipata nafasi ya kukagua nyaraka mbalimbali zinazhusiana na na ununuzi wa gari hizo.

Kwa upande wa suala la Ofisis ya Rais Fedha na Mipango kuwa Wakala wa kunua magari, ililezwa kuwa ilitumika busara tu ya kunua kwa pamoja kwwa kuwa Wizara tofauti zilikuwa zinahitaji kununua gari kwa wakti mmoja. Hivyo, ilifanyika hivyo ili kupata unafuu wa bei

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kamati ya PAC inashauri kuwa kuwe na sheria maalum ya manunuzi iyotoa ruhusa ya kununua kama "bulk procument" badala ya kuwa Wizara ya Fedha wanatumia kama mazoea tu

ii. Serikali iweke viwango vyake (standardization) ili kuepusha kupata gari zisizodumu kwa muda mrefu.

Hoja nambari 5.6.2.1 Malipo ambayo hayajakatwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) USD 928,107

Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) nambari 4 ya mwaka 1998 inatoa ufafanuzi juu ya Taasisi ya Serikali iliyopewa mamlaka na Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) kuzuia kodi ya asilimia 18 kwa Mfanyabiashara aliyetoa huduma kwa Taasisi hio.

Ukaguzi umebaini kwamba Huduma ya Mfuko Mkuu wa Serikali imefanya malipo kwa Kampuni mbalimbali ambazo zilitoa huduma kwa Taasisi za Serikali bila ya kukatwa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani namba 4 ya mwaka 1998.

Majibu kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

Huduma za Mfuko mkuu wa Serikali imefanya malipo kwa kampuni mbali mbali bila ya kukatwa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa sababu Taasisi husika zilipata ruhusa ya msamaha wa kodi pamoja na kufunga mikataba ambayo imeonyesha kusikatwe kodi katika kampuni husika. Kiambatanisho cha vivuli vya barua inazoelezea msamaha wa kodi kwa Ms Al Zarouni na Z-IT Solution na mikataba kwa Hewlett na Indigo B.V.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Vielelezo vya msamaha wa kodi ukiwemo mkatab wenyewe vimewasilishwa mbele ya Kmati na kuridhiwa na Kamati

2.8 FUNGU L 01WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI (WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO)

Taarifa ya Mapato

Wiraza ya Kilimo , Maliasili, Mifungo na Uvuvi ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 10,468,264,000 katika kipindi cha mwaka 2019/2020 kutokana na vyanzo vyake vya mapato hadi kufikia 30,juni 2020 Wizara ilikusanya jumla ya shilingi 8,611,334,350 sawa na asilimia 82.3 ya makadirio

Majibu ya Wizara

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara haikuweza kufikia lengo kamili la ukusanyaji wa mapato kutokana na changamoto mbali mbali zilizojitokeza zikiwemo:-

i. Kutopatikana kwa Mapato yanayotokana na Uvuvi wa Bahari Kuu kutokana na ongezeko la tozo za 0.4 USD /kilo ya samaki.

ii. Mzao mdogo wa karafuu
iii. Kuzuka kwa janga la Maradhi ya Korona kulipelekea kukosa mapato yatokanayo na utalii katika Msitu wa Jozani, Ngezi na Kiwengwa.
iv. Ukongwe wa mtambo wa liquid nitrogen umepelekea kutofanya kazi kwa ufanisi.

Wizara ilichukuwa juhudi kadhaa za kutatua changamoto hizo ikiwemo:-

I. Sheri ya Bahari Kuu sura 388 ya 2020 imefanyiwa mapitio na kupitisha katika Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania
II. Wizara ya Kilimo Umwagiliaji, Maliasi na Mifugo imepeleka ombi IAEA kwa ajili ya kupatiwa mtambo mpya wa kuzalishia Liquid Nitogen

Uchunguzi wa kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa sababu ya kushuka kwa mapato ,mtambo wa liquid nitron umeharibika hata hivyo kamati ilihoji kama kuna jitihada zozote zimefanyika kutoka serikali, Wizara imesema kuwa serikali wamechukua juhudi mbali mbali ili mtambo huo ufanye kazi..

Vile vile Kamati imebaini kuna hoja ya kisiwa cha Mnemba kuwa kuna mapato makubwa ,fedha zinazopatikana pale wanachukua Wizara na zilizobaki wanapewa wanavijiji na hazipelekwi Mfuko Mkuu wa Sikali jambo ambalo imeifanya Serikali kukosa mapato

Mapendekezo ya kamati ya PAC

Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo Maliasili na Mifugo kuchukua agizo hili ili mapato yanayopatikana kwenye kiaiwa cha Mnemba yanapelekwa Serikali kuu ili kuengeza uchumi wa Taiafa,

Taarifa ya matumizi

Wizara ya Kilimo ,Maliasili ,Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 23,233,100,000 kwa kazi za kawaida na jumla ya shilingi 60,264,700,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia 30,juni 2020, jumla ya shilingi 21,257,831,157 zimeingizwa na kutumia kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 92, na jumla ya shilingi 4,696,400,000 kwa kazi za maendeleo sawa naasilimia 95 ya makadirio.

Majibu ya Wizara

*Taarifa ya Matumizi ya Kazi za Kawaida*

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 22,978,600,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi

11,416,800,000 kwa ajili ya mishahara, shilingi 5,696,900,000 kwa matumizi mengineyo na ruzukushilingi 5,864,900,000(3,534,700,000 kwaruzuku ya mishahara na ruzuku ya matumizi mengineyo ni shilingi 2,330,200,000)
Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 21,257,831,157 zilingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 92, kati ya hizo shilingi 11,360,226,283 kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 99, shilingi 4,721,916,886 kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 82.9, shilingi( shilingi3,470,246,821 kwa ruzuku ya mshahara sawa na asilimia 98.2 na shilingi 1,705,441,167 kwa ruzuku ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 73.2.
kutokana na hali ya asilimia ya upatikanaji wa fedha za kazi za kawaida Wizara imeweza kutekeleza malengoyake yaliojipangia kwa kiasi kikubwa kama yalivyopangwa.

*Taarifa ya Matumizi ya Kazi za Maendeleo*

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi4,930,000,000 kwa kazi za maendeleo kutoka SMZ. Kati ya fedha hizo shilingi 1,000,000,000kwa Mradi wa Umwagiliaji Maji, Shilingi 1,000,000,000 kwa Mradi wa Miundombinu ya Sekta ya Kilimo,shilingi 1,200,000,000 kwa Mradi wa Kuuendeleza Utafiti wa Sekta ya Mifugo, shilingi 200,000,000 kwa Mradi wa Uimarishaji wa Mazao ya Baharini,shilingi 1,400,000,000 kwa Mradi wa Ujenzi wa Soko la Malindi, shilingi 50,000,000 kwa ajili ya Mradi wa Uvuvi wa Bahari Kuu na shilingi 80,000,000 kwa Mradi wa ERPP.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 4,696,400,000 zilingizwa na kutumika kwa kazi za Maendeleo sawa na asilimia 95, kati ya hizo shilingi 2,004,000,000 kwa Mradi wa Umwagiliaji Maji, sawa na asilimia 200, Shilingi 677,000,000kwa Mradi wa Miundombinu ya Sekta ya Kilimosawa na asilimia 67.7,shilingi 1,400,000,000 kwa Mradi wa Ujenzi wa Soko la Malindisawa na asilimia 100 na shilingi 36,000,000 kwa Mradi wa ERPPsawa na asilimia 45. Aidha wizara kupitia Idara ya misitu iliingiziwa jumla ya shilingi 579,400,000 kwa ajili ya fidia ya vipando na mashamba.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2019/2020Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 60,264,700,000kwa kazi za maendeleo kutoka kwa Washirika wa maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 32,867,000,000kwa Mradi wa Umwagiliaji Maji, Shilingi 988,440,000 kwa Mradi wa TANIPAC, shilingi 692,423,000 kwa Mradi wa Uimarishaji wa Mazao ya Baharini,shilingi 13,200,000,000 kwa Mradi wa Ujenzi wa Soko la Malindi, shilingi 2,894,693,000 kwa ajili ya Mradi wa Uvuvi wa Bahari Kuu, shilingi 6,950,283,000 kwa Mradi wa ERPP, shilingi 399,261,000 kwa mradi wa MIVARF, shilingi 1,420,600,000 kwa mradi wa Agri-Connect Supporting Value Chains for Shared Prosperity, shilingi 228,200,000 kwa mradi waSafeguarding Zanibar Forest and Coastal Habitants for Multiple Benefits na shilingi 44,400,000 kwa mradi wa Food Resilient Project.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 28,935,548,980 zilipatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 48, kati ya hizo shilingi 9,873,484,232 kwa Mradi wa Umwagiliaji Maji sawa na asilimia 30, shilingi 2,273,667,678kwa Mradi wa Uimarishaji wa Mazao ya Baharini sawa na asilimia 328, shilingi 6,929,030,000 kwa Mradi wa Ujenzi wa Soko la Malindi sawa na asilimia 52 , shilingi 4,338,696,179 kwa Mradi ya Mradi wa Uvuvi wa Bahari Kuu sawa na asilimia 150, shilingi 5,245,398,841 kwa Mradi wa ERPP sawa na asilimia 75 na shilingi 275,272,050 kwa mradi wa MIVARF sawa na asilimia 69. (Angalia Kiambatanisho Namba 5)

Ingawa Wizara haikufikia lengo la upatikanaji wa fedha zote za maendeleo. Wizara iliendelea kutekeleza shughuli za Miradi kama ilivyopangwa.

Uchunguzi wa kamati ya PAC

Kamati ilitaka kujua kuhusu pesa za maendeleo shilling 1,000,000,000 kwa Mradi wa Umwangiliaji maji , kati ya hizo shillingi 2,004,000,000 zilitumika kwa mradi wa Umwangiliji maji

Hoja Namba 5.7.1.1 Mapato ambayo hayakupelekwa Benki

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna ucheleshaji mkubwa wa uwasilishaji wa mapato yanayokusanywa na idara kupitia Mfumo wa Hifadhi ya Jozani. Mapato hayo yanajumuisha fedha za KItanzania ,Dola za Kimarekani, na Fedha za Ulaya (Euro).

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 30(1)(2)(3) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Uchunguzi wa kamati ya PAC

Kamati yaPAC imehoji juu ya sababu ya kuchelewa pesa kwenda bank , kamati imebaini kuwa Wizara haikuwa na majibusahihi kwa kuchelewa kupelekwa pesa bank,hata hivyo kamati imebaini kuwa kuna rati tofauti ambazo watuwanalipa jambo ambalo linalipa ugumu Wizara ,

Kamati imeitaka Wizara iwe na mfumo maalum wa kulipa rate moja hususan watumie Tsh au Dola , pia Wizara imeiambia kamati kuwa tayari wameshafungua acaunti maalum pesa zinaingia moja kwa moja, kwa upande wa kamati haikuridhishwa na majibu ya wizara

Mapendekezo ya kamati ya PAC

Kamati imeitaka wizara kuwa pesa zote zitakazo kusanywa zipelekwe mfuko mkuu wa Serikali.

Kamati imeitaka Wizara ya Kilimo kuwaharakisha Wizara ya Fedha kuanzisha mfumo

**Hoja Namba 5.7.1.2 Tofauti ya fedha zilizoripotia katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 579,400,000**

Kwa mujibu wa taarifa za ufugaji wa hesabu za mwisho wa mwaka zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, Wizara ya kilimo iliwaslishwa fedha halisi iliyotumika katika Miradi ya Maendeleo ni shilingi 4,696,400,000 . Aidha , kwa mujibu wa taarifa za fedha zilizoripotiwa kuptia mfumo wa usimamizi wa Fedha (IFMIS) kwa kumbukumbu nambari EXRR11 –C payment EXP TISS ya tarehe 01 julai 2019 hadi 30 juni 2020 iliripotiwa matumizi halisi ya Miradi ya maendeleo ni jumla shilingi 4,117,000,000 ambapo matumizi hayo yanaenda sambasamba na taarifa za daftari la kumbukumbu za fedha taslim la Wizara

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika tofauti ya shilingi 579,400,000 zilizoripotiwa katika taarifa ya hesabu za maendeleo zilizowasilishwa ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi.

Kujitokeza kwa tofauti iliyobainika kumpelekea hesabu hizo kutokukosekana sura sahihi na halisi.Kufanya hivyo nmi kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 . Mchanganuo wa tofauti hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo.

**Jadweli Nambari 55: Tofauti za fedha zilizoripotiwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka**

| Meelezo | Jumla ya Fedha |
|---|---|
| Fedha iliyoripotiwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka 2019/2020 | 4,696,400,000 |
| Fedha halisi iliyoripotiwa kupitia taarifa za mfumo wa IFMS pamoja na Cashbook la Wizara | 4,117,000,000 |
| | 579,400,000 |

Majibu ya Wizara

Ni kweli Wizara iliziripoti fedha hizo shilingi 579,400,000 katika taarifa ya fedha za hesabu za mwisho wa mwaka 2019/2020. Fedha hizizilitokana na michango wa SMZ kwa fidia ya vipando na mashamba kwa ajili ya kupishaujenzi wa barabar za mashimo ya mchanga.Fedha hizi zilikuwa nje ya mfumo wa kibajeti wa Wizara na zikalipwa kuoka mfuko mkuu wa Serikali. Kwa kuwa fedha hizi zilipokelewa na Idara ya Misitu na kuwekwa katika vitabu vya kumbukumbu. Hivyo,Wizara iliona ipo haja ya kuripotiwa katika hesabu za mwisho.

Uchunguzi wa kamati ya PAC

Hoja Namba 5.7.1.3 Kukosekana kwa mgao wa fedha kutoka katika mfuko wa maendeleo ya misitu katika maeneo ya hifadhi jozani shilingi 640,341,58

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia Ripoti ya Utekelezaji , imebaini kwamba Wizara ya Kilimo ,Maliasili,Mifugo na Uvuvi imetoa mgao wa shilingi 226,399,589 kwa kipindi cha januari hadi juni 2019 na shilingi 413,941,996 kwa kipindi cha julai hadi Disemba 2019 kwa jumui ya UWEMAJO,JECA na kamati 9 za vijiji vinavyoizunguka hifadhi ya taifa ya Jozani kwa lengo la uhifadhi na kuendeleza miradi ya maendeleo kwa jamii.

Baada ya kufanya ziara ya matembezi katika maeneo vijiji hiyo na kuhujiana na wadau husika wa hilo ukaguzi umebaini kwamba jumuiya hizo zimekiri kwamba hazikupokea mgao huo fedha hadi tunakamilisha ukaguzi huu.

Kutowapatia fedha hizo jumuiya hizo ni kwenda kinyume na makubaliano ya wazara na wadau husika.

. Kukosekana kwa mgao wa fedha

| namba | Jumla ya fedha (SHS) | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | 226,399,589 | Ikiwa ni malipo kwa jumuiya ya UWEMAJO,JECA na kamati 9 za vijiji vinavyoizunguka hifadhi ya Taifa ya Jozani kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| | | wa Januari hadi juni 2019 |
| 2 | 413,941,996 | Ikiwa ni malipo kwa jumuiya ya UWEMAJO , JECA na kamati 9 za vijiji vinavyoizunguka hifadhi ya taifa ya jozani kwa mwezi wa Julai hadi Disemba 2019. |
| 3 | 640,314,585 | |

Majibu ya Wizara

Hata hivyo, baada ya wakaguzi kufanya ziara katika maeneo ya vijiji na kuhojiana na wadau husika na kudai ya  kwamba jumuiya hizo hazikupokea mgao huo wa fedha, jambo ambalo sio la kweli.

Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi kupitia Idara ya Maendeleo ya Misitu ilifanya mgao huo wa fedha kwa mujibu wa taratibu na kanuni kwa Jumuiya na kamati za vijiji vinavyoizunguka hifadhi ya Taifa ya Jozani. Hati za malipo pamoja na vielelezo vya upokeaji wa fedha hizo vipo kwa uthibitisho zaidi

Uchunguzi waKamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti alipokuja hakukuta vielelezo vyovyote hata hivyo alirudi kwa mara ya pili hakukuta vielelezo

Vile vile kamati imebaini kuwa Mkurungenzi alitengeneza document akasaini bila kamati mkuu saini kwa sababu pesa hazikulipwa. Kamatiya PAC haikuridhishwa na majibu ya hoja hii

Hoja Namba 5.7.1.4 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 29,272,230

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 kuna hati za malipo zenye thamani ya shilingi 29,272,230 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali lakini hati za malipo hayo hazikupatikana kwa kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo .

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya Zanzibar ya mwaka 2016 pamoja na kifungu 95(4) cha Kanunui ya Fedha ya mwaka

2005. Mchanganuo wa malipo ni kama inavyoonekana katika jadwel lifuatalo.:-

| Namba | Nambari ya Hundi | Tarehe ya hundi | Jumla ya fedha | aliyelipwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 4316 | 8/4/2020 | 641,000 | Fatma Mussa Abdulkadir |
| 2 | 4312 | 31/03/2020 | 570,000 | Khamis Shekha Haji |
| 3 | 4302 | 4/3/2020 | 1,576,500 | Khamis Shekha Haji |
| 4 | 4299 | 13/02/2020 | 1,000,000 | Khamis Shekha Haji |
| 5 | 4290 | | 1,576,000 | Khamis Shekha Haji |
| 6 | 4290 | | 500,000 | Khamis Shekha Haji |
| 7 | 4280 | 9/1/2020 | 3,470,000 | Kampuni ya Sheby Inteprise |
| 8 | 4266 | 20/12/2020 | 7,080,000 | Khamis Shekha Haji Khamis Shekha Haji |
| 9 | 4267 | 24/12/2020 | 2,761,300 | Khamis Shekha Haji |
| 10 | 4262 | | | hakijarikodiwa |
| 11 | 4253 | 11/12/2020 | 1,960,000 | Khamis Shekha Haji |
| 12 | 4235 | 13/11/2020 | 1,473,430 | |
| 13 | 4233 | 8/11/2019 | 895,000 | Khamis Shekha Haji |
| 14 | 4224 | 24/10/2019 | 1,000,000 | Khamis Shekha Haji |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 15 | 4216 | 16/10/2019 | 500,000 | Khamis Shekha Haji |
| 16 | 4189 | 21/08/2019 | 4,240,000 | Bakari Ali Abdalla |
| Jumla | | | 29,272,230 | |

Majibu ya Wizara

Wizara inakiri kukosekana kwa hati za malipo wakati wa ukaguzi.Hata hivyo, hati hizo zipo tayari kwa ajili ya uhakiki na uthibitisho kwa kamati yako

Uchunguzi wa kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa Wizara ya Kilimo imekiri kuwa kweli ilifanya uhaulishajiwa fedha hizo ,hata hivyo kamati iliitaka Wizara kuleta vielelezo vya matumizi hayo na walipatiwa lakini Kamati haikuridhika na vielelezo hivyo .

Hoja Namba 5.7.1.5 kukosekana kwa utaratibu wa uhaulishaji wan fedha shilling 111,573,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Kilimo imefanya uhaulishaji wa fedha shilingi 111,573,000 kutoka hesabu nambari 05110300000515 ya maendeleona Huduma za Kilimo Unguja na kuingizwa katika hesabu nambari 043945000 ya Maendeleo na Huduma Pemba katika kipindi cha mwakawa fedha 2019/2020.

Ukaguzi haukuweza kupatiwa vielelezo vilivyopelekea Wizara kufanya uhaulisho wa fedha hizo jambo ambalo limetia dosari za uwepo wa uhaulishaji huo.

Kufanya uhaulishaji bila kufuata utaratibu ni kwenda kinyume na kifungu nambari 50(1)(2) cha sheria ya usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 mwaka 2016.

Mchanganuo wa fedha zilizohaulishwa ni kama unavyoonekanakatika jadwel

Jadwel Nambari 58 : kukosekana kwa utaratibu wa uhaulishaji wa fedha

| namba | Namba ya hati ya malipo | tarehe | Jumla ya fedha | aliyelipwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 6/11 | 18/11/2019 | 45,573,000 | Maendeleo ya Huduma za Kilimo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2 | 7/11 | 5/5/2019 | 51,000,000 | Maendeleo ya Huduma za Kilimo |
| 3 | 15/6 | 17/6/2020 | 15,000,000 | Maendeleo ya Huduma za Kilimo |
| jumla | | 111,573,000 | | |

Majibu ya Wizara

Ni kweli Wizara ilifanya uhaulishaji wa fedha hizo kutoka hesabu nambari 051103000015 ya Maendeleo na Huduma za kilimo Unguja na kwenda hesabu nambari 0403945000 ya Maendeleo ya huduma za kilimo Pembakwa ajili ya kufanikisha maonesho ya 8/8.

Wizara imefanya uhaulishaji (Transfers) wa fedha hizo ikiwa ni sehemu ya malipo (tansactions) kutoka hesabuya Wizaraya Maendeleo na Huduma za kilimo *(Mlipaji)* kwenda hesabu ya Maendeleo na huduma Pemba *(Mlipwaji)*na sio uhaulishaji wa fungu la bajeti kutoka kasma moja kwenda nyengine kama ilivonukuliwa katika kifungu cha 50(1)(2) cha sheria ya Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.Vielelezo vya malipo hayo pamoja na hati za malipo husika vipo tayari kuhakikiwa na kamati kwa ajili ya uthibitisho.

Uchunguzi wa kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa wakaguzi wa kutoka Ofisi ya Mdhibiti hawakupatiwa vielelezo vilivyopelekea Wizara kufanya uhaulishaji wa fedha hizo.

Pia, kamati imebaini kuwa kutokufahamia kwa lugha baina ya CAG na watu wa Wiazara , Wizara ilifanya transfer ya pesa na si malipo.nakwa upande wa kamati iliridhaka na majibu yao.

Mapendekezo ya kamati ya PAC

Kamati inapendekeza kuwa kuwe na mashirikiano baina ya Ofisi ya Mdhibiti na Wizara wanapokwenda kwenye ukaguzi.

5.7.1.6 Kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya fedha shilingi 1,300,000,000

Ukaguzi umebaini kupitia mfumo wa Usimamizi wa matumizi ya fedha (IFMIS) kwa

mujibu mujibu kwa kumbukumbu nambari 20CR3058 NA MOFPB10200615 ya tarehe 23, juni 2020 Wizara imefanya matumizi ya shiliingi 1,300,000,000 kwa ajili ya huduma mbali mbali . dosari iliyobainika na ukaguzi ni kama ifuatavyo

- Kukosekana kwa taarifa ya matumizi ya fedha
- Kukosekana kwa hati ya malipo
- Kukosekana kwa uthibitisho wa malipo

Kukosekana kwa vielelezo vya malipo ya fedha hizo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha sheria ya usimamamizi wa Fedha za Umma nambari12 ya mwaka 2016.

**Majibu ya Wizara**

Ni kweli Wizara iliingiziwa fedha hizo kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwa kumbukumbu namba 20CR30580 na MOFPB10200615 ya tarehe 23 Juni,2020 kwa ajili ya malipo ya fidia ya miti na mazao kwa wakulima wa Unguja walioathirika na ujenzi Mradi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji kupitia mkopo wa Exim Bank – Korea.
Malipo hayo ya fidia yalifanyika kwa hati namba M8/6 YA TAREHE 26/6/2020 na kuingizwa katika hesabu ya Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo 0406433000 ambapo shilingi 1,288,124,500 walilipwa wahusika katika hesabu zao za benki, shilingi 10,634,000 walilipwa wahusika kwa fedha taslimu, shilingi 317,500 yalikuwa ni malipo ya masheha na maafisawaliosimamia zoezi hilo. Na jumla ya shilingi 924,000 zilibakia na kurejeshwa katika hesabu ya Mfuko Mkuu wa Hazina. Vielelezo vya malipo hayo vipo tayari kwa uthibitisho kwa kamati.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa kulikuwa na kutofahamiana baina ya Wizara ya Fedha na Mipango katika ule mfumowa (IFMIS) jambo ambalo lilifanya sitofahamu kwenye kamati , hata hivyo , kamati ilienda mapaka Wizara ya Fedha ili kupata uhakika mfumo mzima wa (IFIMIS) ili kupata maelezo kuhusiana na matumizi ya fedha hizi

**Hona Namba 5.7.1.7 Mapato yanayotumika bila kuwasilishwa mfuko mkuu wa Hazina shilinhi 192,169,600**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika mwamba katika kipindi mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Kilimo inamiliki hesabu ya Maendeleo na Huduma za Kilimo katika wizara ya kilimo maliasili ,mifungo na uvuvi.

Ukaguzi umebaini kwamba mapato yatokanayo na uuzaji wa mbolea htumika kwa shughuli mbali mbali za Wizara kabla ya kuwasilishwa katika Mfuko wa Hazina kwa mujibu wa taratibu , Aidha ukaguzi umekosa kupatiwa ruhusa ya matumizi ya fedha hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 30(3)cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadwel lifuatalo.

| Namba | Aina ya mbolea | Kiwango kilichouzwa (kg) | Jumla ya fedha |
|---|---|---|---|
| 1 | UREA | 159,209 | 31,841,800.00 |
| 2 | TSP | 118,826 | 35,647,800.00 |
| 4 | MBRNGU | 107,990 | 21,598,000.00 |
| 5 | ZANSUNIL | 10,308 | 103,080,000.00 |
| jumla | | 396,333 | 192,169,600 |

Majibu ya Wizara

Ni kweli Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo inamiliki hesabu ya Maendeleo na Huduma za Kilimo ambayo hutumika kwa ajili ya uwezeshaji wa Miradi midogo midogo ambayo wafadhili wametaka fedha hizo zipite nje ya mfuko wa serekali pamoja na ukusanyaji wa mauzo yanayotokana na ruzuku ya pembejeo (Dawa, Mbole na Mbegu). Kutokana na changamoto ya fedha iliyokuwepo kwa wakati huo na, Wizara ilifanya mashauriano na Wizara ya Fedha na Mipango juu ya kutumia fedha hizo kwa ajili ya ununuzi wa mbolea ya Ureaili kukabili changamoto hizo kwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hata hivyo, Wizara ilipokea ushauri kutoka kwa wakaguzi na kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imeanza na utaratibu wa kuzipeleka katika Mfuko Mkuu wa Hazina fedha hizo ikiwa ni mapato yatakanayo na Kilimo.

## 2.9 WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI – PEMBA

**Hoja Namba 75,7.1.8 Bidhaa ambazo hazikuingizwa katika madaftari ya ghalani shilingi**

21,920,517

Majibu ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugoi

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (C.A.G) baada ya ukaguzi wake wa awali wa Mwaka 2019/2020 iliileta hoja ili kupatiwa Majibu kwa Barua Ref No.AUD/PK.I/VOL/10 ya tarehe 18/11/2020. inahusika na hoja.

Kwa upande wa iliyokuwa Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na uvuvi iliijibu hoja hiyo kwa barua yenye Ref. No.WKMMU/P/29/12/16/2020 ya tarehe 4.Dec.2020 inahusika na majibu hayo.

Kwa wakati huo mwenendo yote(Transaction) zote ni kumi natisa(19), kumi na sita(16) ilikuwa tayari zimesharikodiwa katika vitabu vya ghalani(Store ledger) isipokuwa tatu nazo ni Hati (Voucher No.)92-93/11/2019. na VR No.96/11/2019 na sababu kwamba hazikurekodiwa ni kwamba Mtunza ghala wetu kwa wakati huo alikuwa yuko katika likizo jambo amabalo aliye muachia hakufanya Recording kwa kutegemea kumuachia Muhusika halisi. Mdhibiti na Mkaguzu Mkuu wa Hesabu baada ya kumpelekewa Majibu hatukupata mrejesho .

Wizatra inapopokea vifaa ghalani tunarekodi pamoja na kumuelekeza mkaguzi kwamba vifaa hivi ataviona katika ukurasa No.(L/F.No.)

Majibu ya Wizara

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (C.A.G) baada ya ukaguzi wake wa awali wa Mwaka 2019/2020 iliileta hoja ili kupatiwa Majibu kwa Barua Ref No.AUD/PK.I/VOL/10 ya tarehe 18/11/2020. inahusika na hoja.

Kwa upande wa iliyokuwa Wizara ya Kilimo Mali Asili Mifugo na uvuvi iliijibu hoja hiyo kwa barua yenye Ref. No.WKMMU/P/29/12/16/2020 ya tarehe 4.Dec.2020 inahusika na majibu hayo.

Kwa wakati huo mwenendo yote(Transaction) zote ni kumi natisa(19), kumi na sita(16) ilikuwa tayari zimesharikodiwa katika vitabu vya ghalani(Store ledger) isipokuwa tatu nazo ni Hati (Voucher No.)92-93/11/2019. na VR No.96/11/2019 na sababu kwamba hazikurekodiwa ni kwamba Mtunza ghala wetu kwa wakati huo alikuwa yuko katika likizo jambo ambalo aliye muachia hakufanya Recording kwa kutegemea kumuachia Muhusika halisi. Mdhibiti na Mkaguzu Mkuu wa Hesabu baada ya kumpelekewa Majibu hatukupata mrejesho .Wizara inapo pokeavifaa ghalani tunarekodi pamoja na kumuelekeza mkaguzi kwamba vifaa hivi ataviona katika ukurasa No.(L/F.No.)

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa msingi wa Hoja hii ni kwamba iliyokuwa Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi Pemba imekuwa ikiingiza katika daftari la ghalani kumbukumbu za bidhaa mbalimbali ikiwemo mafuta pale bidhaa hizo zinapopokelewa na kuningizwa ghalani pamoja na kutumika zinapkuwa Wizarani tu. Bidhaa hizo zinapotolewa na kupelekwa katika Idara mbalimbali za Wizara hiyo huwa hazirekodiwi katika daftari la ghalani la Idara husika wala uchukuaji wa bidhaa hizo kwa matumizi ya mfanyakazi mmoja mmoja (au kwa vitengo) katika Idara huwa hauwekewi kumbukumbu yoyote katika daftari la ghalani la Idara hizo. Miongoni mwa Idara zilizokumbwa na dosari hiyo ni Idara ya Kilimo, Idara Mifugo na Idara ya Umwagiliaji Maji.

Tatizo la kutorekodiwa kwa bidhaa katika Idara. mbalimbali za Wizara hii linatokana na sababu zifuatazo:-

i. Ufahamu mdogo wa watendaji juu ya taratibu za Serikali za uwekaji wa kumbukumbu ghalani (Store Keeping) na taratibu za uchukuaji na matumizi ya vifaa vya Serikali ambapo Wizara ilidhani hatua ya uwekaji wa kumbukumbu za bidhaa katika ghala la Wizara pekee ilikuwa inatosha kwa utunzaji wa kumbukumbu.

ii. Upungufu wa watunza ghala katika Wizara hiyo ambao pia umechangia kwa kutowekwa kwa kumbkumbu hizo katika Idara

Barua ya Majibu ya Ufafanuzi wa Hoja zilizobainika katika Ukaguzi ya tarehe 4/12/2020 yenye nambari ya kumbukumbu WKMMU/P/29/12/16/2020 iliyotoka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwenda kwa Mdhamin Afisi ya Mdhibti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Pemba inathibitisha hali hiyo.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wizara ya Kilimo,Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba ifanye utaratibu wa kupata watunza ghala wenye sifa ambao watatumika katika Idara mbalimbali ili kuweka utunzaji sahihi wa kumbukumbu za bidhaa zinazoingizwa katika Idara pamoja na matumzi ya bidhaa hizo.

2. Ili kuepusha upotevu na ubadhirifu wa bidhaa za Serikali unaoweza kutokea yakiwemo mafuta, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba iandae utaratibu maalum utakaoziwezesha bidhaa zinazotolewa kutoka ghala kuu la Wizara na kuingizwa katika Idara mbali mbali zinarekodiwa pamoja na kuwekewa kumbukumbu kwa matumizi ya mfanyakazi mmoja mmoja anaepatiwa bidhaa hizo katika Idara.

3. Katika kufuata utaratibu maalumu wa utoaji wa bidhaa ghalani kwa ajili ya matumizi, Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo Pemba inapaswa kuwafahimsha

wafanyakazi wake wote juu ya utaratibu sahihi utakaotumika pindi wafanyakazi waliyopo Idarani watapohitaji bidhaa kutoka ghalani.

### Hoja Namba 5.7.1,9 Malipo ya Mishahara kwa watumishi waliosimamishwa kazi kwa muda mrefu shilingi

Ukaguzi umebaini uwepo wa matumizi ya shillingi 55,641,000 zilizolipwa kwa watumishi wawili (2) ambao hawapo kazini kwa muda mrefu na watumishi watatu (3) walio simamishwa kazi .

Ukaguzi umebaini kwamba pamoja na kuwepo barua za kusimamishwa kazi na kutohudhuria kazini kwa muda mrefu , bado eafanyakazi hao wanaendelea kulipwa mishahara kikamilifu kupitia hisabu ya akiba nambari 046693000 ya Wizara ya Nchi (OR) Fedha na Mipango

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 84(3) cha Sheria ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya mwaka 2011.

Mchanganuo wa malipo ya mishahara hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

Jadweli Nambari 61: Malipo ya mshahara kwa watumishi waliosimamishwa kazi muda mrefu.

55,641,000

kazi muda mrefu.

| Namba | Majina ya watumishi | Nambari ya ajira | Barua za kusimamishwa kazi | Kiwango cha mshahara kwa mwezi (SHS) | Kiwango cha mshahara kwa mwaka (SHS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Masoud Mo'hd Aboud | 533056 | MAA/MCA/M.2005 ya tarehe 17/02/2017 | 327,000 | 14,388,000 |
| 2 | Abdalla Ali Khamis | 853900 | WKMMU-P/29/4/13/52/017 ya tarehe 13/04/2017 | 381,500 | 16,023,000 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Juma Amini Juma | 146378 | MAA/MEA/J.O ya tarehe 13/04/2017 | 313,000 | 13,146,000 |

Watumishi waliopewa barua za likizo na hawajaripoti kazini

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | Alin Faki Makame | 807203 | MAA/MBA/A.02956 ya tarehe 3/12/2019 | 325,000 | 7,800,000 |
| 5 | Masuod Suleiman Masuod | 547134 | WKMMU/OPF.197 ya tarehe 17/07/2019 | 306,000 | 4,284,000 |
| Jumla 55,641,000 | | | | | |

Majibu ya Wizara ya Kilimo

Wizara inakubaliana na Hoja ya Mkaguzi ya kwamba Wafanyakazi hawa walisimamishwa kazi kwa utoro kazini lakini sio sahihi kabisa alichosema Mkaguzi kwamba wafanykazi hawa waliendelea kulipwa kupitia Hesabu **No.040669300 ya Deposite** ya Ofisi ya Rais Fedha

Badala yake fedha hizi ilikuwa zinaletwa katika Hesabu **No.0406692000 Reccurent** ya Ofis ya Rais fedha katika Mishahara ya wafanyakazi wote na kwa wao waliohusika na hoja hii fedha hii ilikuwa inazuiwa na badala yake kufanyiwa malipo na kuingizwa Hesabu **No.0406693000 Deposite** ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.( kurejeshwa Hazina)

Uhalali wa hilo la kurejesha fedha hizo unaonekama kila Mwezi na kila hati(Vouchar) ya Malipo imeaambatanishwa na hati ya kurejesha fedha Bank **(Pay in slipi).** katika hesabu hiyo.

Wizara ya kilimo Umwagiliaji Mali Asili na Mifugo imefanikiwa kuokoa fedha hizo kwa kutoziingiza katika Hesabu(Account) za wahusika.

Hata hivyo taratibu za kiutumishi zinaendelea kuhakikisha wahusika hawa wanatolewa kwenye Pay roll ya Wizara (utaratibu za kuwafukuza Kazi zinaendelea)

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

1. Kuwepo kwa tatizo la muda mrefu la utoro kazini linalowahusu watumishi waliolezwa katika Hoja hii kama inavyofafanuliwa katika jadweli lifuatalo:-

| S/N | JINA KAMILI | NAMBARI YA AJIRA | IDARA ANAYOTOKA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Abdalla Ali Khamis | 643900 | Idara ya Umwagiliaji Maji | Ni Bwana Shamba ambae ameajiriwa mwaka 2013 ambapo hajaripoti kazi tangu tarehe 15/4/2015 alipohamishiwa Idara ya Umwagiliaji Maji kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Pemba |
| 2 | Masoud Moh'd Aboud | 533056 | Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka | Ni mfanyakazi aliyeajiriwa mwaka 2005 ambae aliomba ruhusa ya kwenda masomoni nchini Uganda, ingawa hakuweza kufika Uganda.Hatimae alirudi kazini tarehe 5/1/2015 na tangu tarehe 7/1/2015 hajafika tena kazini |
| 3 | Juma Amini Juma | 146378 | Idara ya Misitu na Malisili Zisizorejesheka | Ni mhudumu wa shamba (Tumbe) aliyeajiriwa mwaka 2009 ambapo hali ya kutokuwepo kazini imejitokeza kuanzia mwezi Novemba 2015. |
| 4 | Ali Faki Makame | 205368 | Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe | Ni mlinzi wa Ofisi aliyeajiriwa mwaka 1992 ambapo hajaripoti kazi tangu alipopewa likizo ya kawaida iliyoanzia tarehe 20/9/2018 hadi 5/11//2018 na |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | alitakiwa kuripoti kazi tarehe 6/11/2018 |
| 5 | Masoud Suleiman Masoud | 547134 | Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka | Ni mlinzi wa Ofisi aliyeajiriwa mwaka 2009 ambae hajaripoti kazini tangu alipopewa likizo ya kawaida iliyoanzia tarehe 22/7/2019 hadi 30/8/2019 na kutakiwa kuripoti kazi tarehe 2/9/2019 ingawa amekuwa na tabia ya utoro kazini tangu miaka ya 2017 na 2018. |

2. Kuchukuliwa kwa hatua mbalimbali na Wizara zikiwa ni pamoja na :-

   i. Kuwasimamisha kazi wafanyakazi hao baada ya kuchukuwa hatua za kiwatafuta zikiwemo za kutoa barua za wito na matangazo ya wito kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) bila ya mafanikio,

   ii. Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Pemba ilimuomba Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kuwaombea wafanyakazi watoro kuzuiwa mishahara yao (salary block) kupitia barua mbalimbali zikiwemo barua ya tarehe 20 Disemba, 2017 yenye nambari ya kumbukumbu WKMMU/P/29/4 na barua ya tarehe 5/7/2021 yenye nambari ya kumbukumbu WKUMM.P/BLOCK.4/10.VOL.1/2021. Hata hivyo, hakuna uthibitisho uliooneshа kuwa Wizara ya Kilimo Makao Makuu iliomba kuwekewa kizuizi cha mishahara wafanyakazi hao.

   iii. Kutokana na Ripoti za Uchunguzi wa wafanyakazi hao zilizopendekeza kuachishwa kazi kwa wafanyakazi hao, Wizara ya Kilimo (Makao Makuu) iliomba kibali kutoka Tume ya Utumishi Serikalini cha kuwaachisha kazi wafanyakazi hao kupitia barua ya tarehe 11/1/2021 yenye nambari ya kumbukumbu WKUMM/29/2/5/VOL.1 na barua ya tarehe 18/1/2021 yenye nambari ya kumbukumbu WKUMM/29/2/5/VOL.1I.

   iv. Kutokana na barua hizo za maombi, Tume ya Utumishi (kupitia barua yake ya tarehe 25 Febuari, 2021 yenye nambari ya kumbukumbu

TUS/0R/C/KK/31.VOL.6/33) iliitaka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Malisili na Mifugo kutoa ufafanuzi juu ya maeneo matano (5) ikiwa ni pamoja na kueleza kwa kiana hatua zilizochukuliwa na Wizara kwa wafanyakazi hao, kutoa maelezo ya kina juu ya hatua zitakazochukuliwa katika kurejesha fedha kwa watumishi ambao bado wana mikopo PBZ, kuzingatiwa kwa haki ya kusikilizwa kabla ya mtumishi kufukuzwa kazi na pia kuambatanisha barua za kuwawekea kizuizi cha mishahara.

v. Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Malisili na Mifugo ilitoa ufafanuzi huo kwa Tume ya Utumishi Serikalini kupitia barua yake ya tarehe 5/7/2021 yenye nambari ya kumbukumbu WKUMM/29/2/5/VOL.III.

3. Kuendelea kuingizwa fedha hizo za mishahara ya wafanyakzai hao kwa Wizara ya Kilimo na baadae Wizara ya Kilimo kuzirejesha fedha hizo kupitia akaunti ya Diposit ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, ingawa wafanyakazi wenyewe walikwishaandikiwa barua za kuziuliwa mishahara yao.

4. Viwango vya mishahara vilivyoaininshwa katika Ripoti ya Mdhibiti vilianzia mwaka 2017 hadi 2020

5. Hali ya kutokuwepo kazini kwa baadhi ya wafanyakazi hao (wafanyakazi watatu) imejitokeza tangu mwaka 2015 ambapo barua za kuwasimamisha kazi zimetolewa mwaka 2017 na mishahara yao kamili imekuwa ikiendelea kuingizwa Wizara ya Kilimo kwa kipindi chote hicho.

Hata hivyo, uchunguzi zaidi wa Kamati ya PAC umebaini kuwa wafanyakzi hao wameshafukuzwa kazi kwa mujibu wa Sheria isipokuwa Ndg. Amini Juma Amini ambae shauri lake bado linafanyiwa kazi na Tume ya Utumishi Serikallini

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kwa kuwa suala la kuendelea kutolewa malipo ya mishahara kwa watumishi walisiomamishwa kazi kwa muda mrefu lilichukua muda mrefu kushughulikiwa na kukamilishwa na kupelekea usumbufu na kutiliwa shaka malipo hayo ya mishahara yaliyokuwa yakiingizwa na kurejeshwa, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kutochelewa kuyafanyia kazi masuala ya kiutumishi na ya kifedha ili kuepusha athari mbali mbali za kuchelewa kuyafanyia kazi masuala hayo..

Hoja Namba 5.7.1.10Malipo yaliyolipwa kwa fedha taslim shilini 9,709,90

Jumla ya shilingi 9,709,090 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya mfuko ya maendeleo ya huduma za kilimo, ukaguzi umebaini kuwa malipo hayo ya mefanywa kwa njia ya fedha taslim ambapo ni kinyume na taratibu za malipo.

Aidha, Ukaguzi umebaini kwamba malipo hayo hayakukatwa kodi ya zuio na kupelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo.

Kufanya malipo kwa fedha taslim ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016, pamoja na kifungu nambari 83 cha Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ya mwaka 2008. Mchanganuo wa malipo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 62: Malipo yaliyolipwa kwa fedha taslim.

| Namba | Nambari ya hati ya malipo | Nambari ya Hundi ya malipo | Jumla ya fedha (SHS) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 10/11<br>12/11/2019 | 711 | 4,257,000 | Maendeleo ya Huduma za kilimo | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme |
| 2 | 15/11<br>13/11/2019 | 713 | 2,272,090 | Maendeleo ya Huduma za Kilimo | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa umeme na vifaa vya ujenzi |
| 3 | 10/4,<br>6/4/2020 | 750 | 3,180,000 | Maendeleo ya Huduma za Kilimo | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kusafirisha mbolea ya urea |
| Jumla | | | 9,709,090 | | |

Majibu ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.

Wizara inakubaliana na hoja ya Mkaguzi lakini haya hayakuwa Malipo ya Taslim cash bases badala yake Maofisa wetu ambao walihusika na zoezi la Matayarisho ya Maonyesho ya Kilimo Chamanangwe walilazimika kutoa huduma za kiutendaji na baadae kuomba marejesho ya fedha walizotoa, Ki Msingi Malipo hayakukatwa  ile kodi ya zuio (With Holding Tax)lakini manunuzi hayo  yalifanyika kwa wafanya Biashara ambao wamesajiliwa na Taasisi za kodi (ZRB,TRA,ZPPDA) ukweli wa hilo katika stakabadhi zao Zimo ZRB No. na TRA No.

kwa mnasaba huo basi Mamlaka za kodi zitakapokwenda kukagua Mauzo yao ni mategemeo yetu kwamba watakatwa kodi za Stakabadhi hizo kwani sisi kama Wizara hatujawapatia hati ya Zuio la kodi(With Holding Certificate) kwenye Manunuzi hayo yanayohusisha Stakabadhi hizo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imethibitisha kuwa kuwa malipo hayo yamelipwa kwa fedha taslim kama ilivyoainishwa katika Hoja ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kamati imebaini kuwa malipo hayo yalikuwa ni marejesho kwa watendaji waliotumia fedha zao kwa ajili ya kufanikisha maonesho ya siku ya Kilimo  yaliyofanyika kuanzia 10/10/10/219 hadi 18/10/2019 ambapo Mratib wa maeonesho hayo alitakiwa kutumia gharama zake katika maaandalizi ya maonesho hayo zikiwemo gharama za miundombinu ya ememe na baadae kurejeshewa fedha hizo..

Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa hakukuwa na idhini ya maandashi iliyomtaka msimamizi wa maeonesho au watendaji wengine kufanya.

Kamati pia imebaini kuwepo kwa fedha za marejesho alizolipwa mfanya biashara ((Mbarouk Ali Salum) Shilingi 2,272,.090 kupitia hati ya malipo nambari 15/11 ya tarehe 13/11/2019 kwa ajili ya vifaa vya umeme na ujenzi wa choo cha viongozi katika eneo la Maonesho ambapo licha ya kutolipwa kwa hundi malipo hayo ya mtoa huduma kama ulivyo utaratibu wa kifedha lakini pia malipo hayo hayakukatwa kodi ya zuio ingawa ilieleawa kuwa mafunzo ya utaratabu wa kupata kodi ya zuio yalikuwa yamehsfanyaka kwa watendaji wa masuala ya fedha.

Aidha, kwa marejesho ya shilingi 4,257,000 alizolipwa  Afisa Mkuu wa idara Umwagiliaji – Pemba ( Ndg. Ndg. Mbarouk ali Mgau) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme katika eneneo hilo la Maonesho (Chamanangwe) kupitia hati ya malipo namba 10/11 ya tarehe 12/11/2019, Kamati imebaini kuwa Wizara ya Kilimo haikukopa moja kwa moja kwa watoa huduma ili kuweza kupata bidhaa na huduma zilizohitajika katika maandalizi ya maonesho hayo ambapo kufanya hivyo kungewezesha malipo kwa watoa huduma hao kulipwa kwa hundi kama ulivyo utaratibu wa kifedha. Aidha kufnya malipo kwa njia ya

hundi kunawezesha mapato mbalimbali stahiki kuweza kupatikana na kushindwa kufanya hivyo ni kukiuka taratibu za malipo na kunaikosehsa mapato Serikali.

Kamati ya PAC ilikagua Hati za malipo hayo pamoja na vielelezo husika. Hata hivyo, haikuridhika na utaratibu wa uliotumika wa kutowatumia moja kwa moja watoa huduma kupata hidhaa na huduma zilizohitajika katika maandalizi ya maonesho hayo na hata pale ilipowatumia watoa huduma hao, Wizara iliwalipa kwa fedha taslim badala ya kupitia hundi na pia Wizara haikukata kodi ya zuio.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati ya PAC inaiomba Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo (Pemba) itumie njia zilizopo kisheria katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kuwatumia watoa huduma wenyewe moja kwa moja kupata bidhaa na huduma inazozihitaji katika kufanikisha shughuli mbalimbali za Serikali..

2. Kamati inaitaka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo (Pemba) kufanya malipo kwa watoa huduma kwa kuzingatia misingi ya Sheria na taratibu za kifedha na ununuzi wa mali za umma ikiwa ni pamoja na kuwalipa watoa huduma kwa njia ya hundi na kuwakata kodi ya zuio.

## 3,0 FUNGU R O1 WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO (WIZARA YA BIASHARA NA MAENELEO YA VIWANDA)

### Taarifa ya Mapato

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,895,963,000 kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Hadi kufikia 30 Juni, 2020 wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 744,585,183 sawa na asilimia 39 ya makadirio.

### Majibu ya Wizara ya Niashara na Maendeleo ya Viwanda

,Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilipangiwa kukusanya mapato ya Shilingi bilioni 1.895 kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa ajili ya huduma inazotoa. Aidha hadi kufikia mwishoni mwa Juni, 2020 jumla ya Shilingimilioni 744.5 zilikusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 39 ya makadirio kwa kipindi cha mwaka 2019/2020.

Hivyo kupelekea Wizara kutokufikia malengo kama nilivyoeleza hapo awali, sababu kuu ni pamoja na zifuatazo;Kutokamilika kwa Kanuni za Sheria ya Ushindani.Kupunguzwa kwa Ada ya uandikishaji majina ya Biashara kutokashilingi 30,000 mpaka shilingi 15,000 kwa mtu na Kuzuka kwa ugonjwa wa Corona (UVIKO 19) ambapolimeathiri ukusanyaji wa mapato kwa asilimia kubwa katika maeneo ya biashara.Wizara inategemea wawekezaji

kusajili makampuni jambo ambalo limekuwa gumu kutokana na kadhia hiyo.Ukaguzi wa Vipimo na Mizani ulisitishwa kabisa kwa kipindi hiki.Taasisi ya Viwango imeshindwa kufikia malengo kutokana na kushindwa kuingia kwa bidhaakutoka nje ya Nchi.

UKUSANYAJIWAMAPATOKUANZIAJULAI2019-JUNI2020

| KIFUNGU | MAELEZOYAMAPATO | MAKADIRIOYAMWAKA2019-2020 | MAKUSANYOYAMWAKA2019-2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **R0104** | **IdarayaBiasharanaUkuzajiMasoko** | **649,978,000** | **80,711,041** | **12.4%** |
| 1422014 | UkaguziwaMezaninaVipimo | 91,655,000 | 67,351,041 | 73% |
| 1422077 | MalipoyakazizaBiashara | 558,323,000 | 13,360,000 | 2.4% |
| | | | | |
| **R0106** | **WakalawaUsajiliBiasharanaMali** | **495,000,000** | **286,727,154** | **58%** |
| 1146002 | Adayautunzajiurithi | 1,000,000 | 3,098,391 | 310% |
| 1422030 | AlamazaBiashara | 240,000,000 | 84,912,050 | 35% |
| 1422031 | UandikishajiwaMakampuni | 171,000,000 | 153,520,625 | 90% |
| 1422032 | UandikishajimajinayaBiashara | 50,000,000 | 18,848,000 | 38% |
| 1422034 | Ujirawakutengenezanyaraka | 33,000,000 | 26,348,088 | 80% |
| | | | | |
| **R0107** | **TaasisiyaViwangoZanzibar** | **700,000,000** | **345,861,037** | **49%** |
| 1112008 | Malipoyausimamiziviwango | 700,000,000 | 345,861,037 | 49% |
| | | | | |
| **R0101** | **AfisiKuuPemba** | **50,985,000** | **31,285,950** | **61%** |
| 1422014 | UkaguziwaMezaninaViimo | 26,345,000 | 10,429,650 | 40% |
| 1422077 | MalipoyakazizaBiashara | 11,640,000 | 7,530,000 | 65% |
| 1422030 | AlamazaBiashara | 2,000,000 | 0 | **0** |
| 1422032 | UandikishajimajinayaBiashara | 1,000,000 | 0 | **0** |
| 1422034 | Ujirawakutengenezanyaraka | 10,000,000 | 13,326,300 | 133% |
| | **JumlaKuu** | **1,895,963,000** | **744,585,182** | **39%** |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilitaka kujua kwanini Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko imefikia asilimia 12.4 imeshuka sana na kuelezwa hii imetokana na sababu mbali mbali ikiwemo maradhi ya covid ya mwaka 2019 .

Kamati ya PAC pia ilitakaufafanuzi juu ya sababu za malipo ya kazi za biashara kushuka sana sawa na asilimia 2.4 ,Kamati ilielezwa kuwa kuna changamoto kubwa ya kodi za maghala , hii imetokana na maghala mengi yamekodishwa tangu zamani, mkodishwa alishalipa fedha za miaka yote mpaka anamaliza mkataba wake, kwa maana hiyo ukusanya wa mapato unapugua kila mwaka ,hata hivyo Wizara tayari imeshaanza marekebisho ya mikataba hiyo .

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri kuwaWizara ya Biashara wakae pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuakisi muendelezo wa mapato na pia thamani ya fedha ipatikane na kupitiwa tena baadhi ya mikataba ya maghala kwa ajili ya marekebisho **.**

Taarifa ya Matumizi

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 1920 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 12,926,756,133 kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 3,483,400,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 wizara ilifanikiwa kupokea jumla ya shilingi 6,730,917,081 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 52 ya makadirio na shilingi 2,650,773,529 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 76 ya makadirio

Majibu ya Wizara

kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Biashara na Maendeleo yaViwanda iliidhinishiwa matumizi ya **shilingibilioni 15.597** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake. Kati ya fedha hizo,shilingi bilioni7.547zilipangwa kutumika kwa kazi za kawaida ikiwe m omishahara na ruzuku na shilingi bilioni 8.050 zilipangwa kutumika kwa kazi za maendeleo (bil.4.6serikalina3.45washirika).Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020, jumla ya **Shilingi bilioni 9.381** zilipatikana ambapo ni sawa naasilimia **60** ya fedha zilizopangwa katika kipindi hicho kwa ajili ya matumizi.Katiya fedha hizo ,jumlaya**Shilingibilioni3.544**ziliingizwa kwa ajili ya mishahara najumla ya **Shilingi bilioni 5.836** zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, ruzuku na maendeleo.

| S/N | PROGRAMUKUU | FEDHAZILIZOTENGWAKWAMWAKA 2019/20 | FEDHAZILIZOPATIKANAKWAKIPINDICHAMWAKA2019-2020 | ASILIMIAYAFEDHAILIYOPATIKANA |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Prog.Kuu1:Uendeshajina UratibuwaWizara yaBiashara | Prog.Ndogo1:UendeshajiwaWizarayaBiashara,ViwandanaMasoko. | 2,139,511,316 | 2,287,668,679 | 106% |
| | Prog.Ndogo2:Uratibu waMipango,SeranaUtafiti | 367,121,800 | 336,830,311 | 91% |
| | Prog.Ndogo3: Uratibu naUtekelezaji wa shughuli zaWizaraPemba | 485,988,684 | 523,784,740 | 108% |
| | JUMLAKUUYAPROGRAMU | 2,992,621,800 | 3,148,283,730 | 105% |
| Prog.Kuu2: MaendeleoyaViwandana Ujasiriamali | Prog.Ndogo1: UkuzajiwaViwanda | 3,286,514,000 | 1,573,127,944 | 48% |
| | Prog.Ndogo2:MaendeleoyaUjasiriamali | 3,567,397,000 | 23,041,752 | 0.6% |
| | JUMLAKUUYAPROGRAMU | 6,853,911,000 | 1,596,169,696 | 23% |
| Prog.Kuu3:Ukuzaji naUendelezaji waBiashara | Prog.Ndogo1:UkuzajiwaMasoko naUsafirishaji | 754,857,200 | 490,878,225 | 65% |
| | Prog.Ndogo 2:UshindaniHalaliwakibiashara naKumlindaMtumiaji | 344,810,000 | 272,232,350 | 79% |
| | Prog.Ndogo3:UrahisishajibiasharanaUkuzajiBiasharaza Ndani | 1,105,500,000 | 685,906,000 | 62% |
| | Prog.Ndogo4:Usajili waBiasharanaMali | 820,900,000 | 763,896,348 | 93% |
| | JUMLAKUUYAPROGRAMU | 3,026,067,200 | 2,212,912,923 | 73% |
| Prog.Kuu4: Viwangona Tathminiya Ubora. | Prog.Ndogo1:Viwango naUthibitiUbora | 2,724,800,000 | 2,424,324,261 | 89% |
| | JUMLAKUUYAPROGRAMU | 2,724,800,000 | 2,424,324,261 | 89% |
| JUMLAKUU | | 15,597,400,000 | 9,381,690,610 | 60% |

Wizara ilipangiwa **shilingi bilioni 8.050** kwa kazi za maendeleo ambapo shilingi bilioni 4.6 kutoka serikalinina 3.45 kutoka kwa washirika (Khalifa Fund).Miradi ifuatayo ilipangwa kutekelezwa

| | Program/Mradi | Fedhailiyopangwa | iliyopatikana | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Programu ya kuendeleza | 1,000,000,000 | 644,581,318 | 64.5 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | viwanda<br>- Ofisi ya SMIDA | 1,000,000,000 | 42,000,000 | 4.2 |
| 2. | Kuimarisha Taasisi ya Viwango | 2,000,000,000 | 1,666,227,636 | 83 |
| 3. | Kuanzisha Mfumo wa utoajiLeseni | 400,000,000 | 41,000,000 | 3.5 |
| 4. | Program ya Mazingira BorayaBiashara | 200,000,000 | - | 0 |
| | JUMLA | 4,600,000,000 | 2,393,808,954 | 52 |

Fedha kwa ajili ya kuwaendeleza wajasiriamali kupitia Khalifa Fund hazikupatikana, hivyo mradi huo haukutekelezwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji kuhusiana na program ya Uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Biashara kwa nini imezidi asilimia 5 na ilielzwa ilielezwa kuwa imetokana na kuongezeka kwa mishahara kutokana wafanyakazi kutoka ZRB waliohamishiwa katika Wizara hiyo pia kupandisha daraja baaadhi ya watendaji nafasi za wakurugenzi wa ndani. Kamati pia ilipata fursusa ya kuona vielelezo vinayotokana na ongezeko la mishahara na kuridhika navyo. Vile vile Kamati ya PAC imebaini kuwa program ya maendeleo ya viwanda na ujasiri amali kila mwaka inashuka asilimia japokuwa Serikali inaingiliaa kati suala la wajasiriamali ,kama vile fedha za KHALIFA FUND kama awamu tatu hazijatoka lakini saivi Wizara imeshughulikia wapo tayari kutoa fedha hizo. kwa upande wa Viwanda Serikali imefanya juhudi mbali mbali ili kuwapata wawekezaji hata hivyo Wizara Wizara ya Biashara tayari wanauza Miradi kwa ajili ya Wawekezaji.

Hoja Nambari 5.8.1.1: Fedha za Fidia ambazo Hazijapokelewa na Wananchi Shs.5,099,550.

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 5,099,550 ikiwa ni fidia kwa baadhi ya wananchi katika eneo la uwekezaji kijiji cha Chamanangwe, Wilaya ya Wete Pemba kwa ajili ya kupisha ujenzi wa viwanda. Hadi ukaguzi unakamilika fedha hizo bado hazijakabidhiwa kwa wananchi hao. Orodha ya majina ya wananchi waliostahiki malipo ya fidia ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

: Fedha za Fidia Ambazo Hazijapokelewa

| Namba | Jina Kamili | Jumla ya Fedha | Shehia |
|---|---|---|---|
| 1 | Mohamed Ali Juma | 400,000 | Mchanga Mdogo |
| 2 | Amina Mohamed Ali | 200,000 | Mchanga Mdogo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | Hamad Bakar Njabu | 400,000 | Mchanga Mdogo |
| 4 | Time Hamad Haji | 1,102,300 | Mchanga Mdogo |
| 5 | Ali Mohamed Ali | 600,000 | Mchanga Mdogo |
| 6 | Biabu Thani Khamis | 400,000 | Mchanga Mdogo |
| 7 | Ali Mohamed Ali | 400,000 | Mchanga Mdogo |
| 8 | Mhusika hajafika | 174,400 | Mchanga Mdogo |
| 9 | Mhusika hajafika | 468,450 | Mchanga Mdogo |
| 10 | Asha Juma Faki | 626,400 | Kiuyu Minungwini |
| 11 | Said Hamad Said | 200,000 | Kiuyu Minungwini |
| 12 | Muhamed Bakari Faki | 128,000 | Kiuyu Minungwini |
| | Jumla | 5,099,550 | |

Majibu ya Wizara ya Biashara na Maeneleo ya Viwanada

Wizara inakubaliana na hoja kuwa hadi tarehe ya ukaguzi Fedha hizi zilikuwa hazijalipwa kwa wahusika. Hali hii imesababishwa na kukosekana vielelezo sahihivya wahusika ambao ni wananchi 12 fedha zao ni TZS5,099,550/=. Aidha wapo wananchi wengine ambao walikataa kutambuliwa na hivyo kukataa kupokea malipo ya fidia jumla ya TZS 192,951,180/= kwa mujibu wa tathmini ya Mthamini  Mkuu wa Serikali. Baada ya vikao na mazungumzo ya kina kati ya Wizara na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba, ilikubalika fedha hizi ziingizwe katika Akaunti ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba ili kuwawezesha wananchi hao kupata malipo yao kupitia Ofisi ya Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini - Pemba. Vocha ya tarehe 04/01/2021 inahusika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa kwa ujumla Wizara ilifuatilia na kuyatambua maeneo matatu kwa ajili ya kuyaendeleza kwa utaratibu wa maeneo ya kiviwanda (Industrial Parks) ambayo ni eneo la Chamanangwe liliopo katika Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, eneo la Nungwi liliopo Wilaya ya Kaskazini A Unguja na eneo la Dunga liliopo katika Wilaya ya Kati Unguja. Maeneo hayo yapo katika hatua tofauti  ya kuyaendeleza.

Vile vile imebainika kuwa eneo la Viwanda la Chamanangwe lililopo Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba, lina ukubwa wa hekta 55.37 ambalo linapatikana (located) katika shehia ya mchanga mdogo na shehia ya Kiuyu Minungwini. Eneo hili tayari limepimwa na Wizara ilipatiwa hati ya umiliki yenye namba DP 1610/2019 iliyotolewa tarehe 02/04/2019. Imabainika pia kuwa eneo la Viwanda la chamanangwe ndio eneo pekee ambalo hatua za kuliendeleza zimeanza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja kulipa fidia TZS TZS 332,346,630/= kwa wananchi wenye mashamba/Vipando na majengo (maboma) katika eneo hilo.
Katika mchakato mzima wa malipo ya fidia, Kamati ya PAC ilielezwa zaidi kuwa Ripoti ya Mdhamini Mkuu wa Serikali ambayo iliwasilishwa Wizarani ilibainisha kuwa jumla ya TZS

332,346,630 zinahitajika kulipwa kama fidia kwa wenye mashamba pamoja na maboma ambayo yalikuwa katika hatua tofauti za ujenzi wakati tathmini hii inafanyika mwaka 2019/2020. Aidha; TZS 139,395,450/= ni malipo ya fidia kwa wananachi 122 waliokubali kujitokeza na kuorodheshwa mashamba yao katika Shehia ya Kiuyu Minungwini na Shehia ya Mchanga mdogo.

Aidha; TZS 112,168,180/= ilikuwa ni fidia kwa maeneo mawili "Block A na B" ambayo tathmini ilifanyika bila ya wenye mashamba hayo kujitokeza kutokana na mgomo uliokuwa ukiendelea wa wananchi wa shehia ya Kiuyu Minungwini. Vile vile TZS 80,783,000/= ilikuwa tathmini ya maboma matano (5) ambapo wamiliki 4 walijitokeza na 1 hakujitokeza wakati wa tathmini hyo inafanyika. Hivyo jumla ya TZS 192,951,180/= zilizobakibaki zimehifadhiwa kwenye hesabu ya Ofisi ya Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba wakati juhudi za kuwasihi wananchi hao kujitokeza kwenda kuchukua fedha zao zinaendelea. Orodha ya waliolipwa na ambao walijitokeza lakini bado hawajalipwa kutokana na kasoro mbali mbali ikiwemo :-

a. Kujirejea kwa Majina, kwa hivyo ilihitaji muda wa kujiridhisha ili kuepuka kufanya malipo mara mbili kwa mtu mmoja.
b. Kujitokeza kwa watu ambao ni miongoni mwa warithi kutaka kuchukua malipo hayo pasina uthibitisho wa kupata ridhaa kutoka kwa warithi wenzake.
c. Kukosekana kwa Majina ya mwenye mashamba katika ripoti ya uthamini kutokana na kutokujitokeza wakati tathmini inafanyika.
d. Kukosekana kwa vielelezo vya utambulisho vya wenye mashamba

JADUELI LA MCHANAGANUO WA MALIPO YA FIDIA KWA WAMILIKI WA MASHAMBA KATIKA SHEHIA YA KIUYU MINUNGWINI
NA MCHANGAMDOGO

| SHEHIA | IDADI YA WADAU | KIASI KINACHODAIWA (TZS) | WALIOLIPWA | KIASI KILICHOLIPWA (TZS) | KIASI KILICHOBAKI (TZS) | WALIOBAKI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| KiuyuMinungwini | 20 | 48,055,900 | 17 | 47,101,500 | 954,400 | 3 |
| MchangaMdogo | 102 | 91,339,550 | 93 | 87,194,400 | 4,145,150 | 9 |
| JUMLA | 122 | 139,395,450 | 110 | 134,295,900 | 5,099,550 | 12 |

.

Hoja Namba 5.8.1.2 Kukosekana Vielelezo vya Malipo ya Dummy Shilingi 1,254,947,109

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 1,254,947,109 zimelipwa kwa kazi mbali mbali za Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Hadi ukaguzi unakamilika tumeshindwa kupata vielelezo vya uthibitisho wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 65: Kukosekana kwa Vielelezo vya Malipo ya Dummy

| Namba | Nambari ya Hati ya Malipo | Aliyelipwa | Jumla ya Fedha (SHS) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 135/12 | ZRB | 30,000,000 | Malipo ya Dummy |
| 2 | 1/1 | K/MKUU | 240,010,000 | Malipo ya Dummy |
| 3 | 121/5 | ZBS | 689,369,289 | Malipo ya Dummy |
| 4 | 125/6 | K/MKUU | 81,346,630 | Malipo ya Dummy |
| 5 | 120/6 | K/MKUU (ESTEC) | 214,221,190 | Malipo ya Dummy |
| | | JUMLA | 1,254,947,109 | |

Majibu ya Wizara

Wizara inakubaliana kuwa wakati wa ukaguzi vielelezo havikuweza kupatikana.Hata hivyo, kwa sasa vielelezo vyote tayari vimepatikana.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa kuna baadhi ya vielelezo alipokwenda mkaguzi hakuvikuta hii imetoka na muhasibu hakwenda kuchukua Wizara ya Fedha , na inavotakiwa Wizara ya fedha wao wanafanya malipo ila kopi wakachukua wenyewe Wizara husika jambo ambalo halikufanyika. Hata hivyo, vielelezo hivyo vilikaguliwa na kuridihiwa na Kmati ya PAC

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaishauri Wizara ya Biashara isifanye dharau ya kutokuchukua kopi za velelelzo vya matumizi ya fedha kutoka Wizara ya Fedha ili kutimiza tataritibu za matumizi ya fedha za Serikali.

Hoja Nambari 5.8.1.3: Mapungufu Katika Mkataba wa Ujenzi wa Maegesho ya Gari Shs.37,181,800.

Ukaguzi umebaini kwamba katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 wizara iliingia mkataba na Kampuni ya Al- Qassmy Trading Limited kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya magari katika eneo la Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko uliogharimu jumla ya shilingi 37,181,800, ambapo kwa mujibu wa mkataba huo ndani ya siku 30 kuanzia tarehe 30/11/2018 ya makubaliano ujenzi huo uwe umeshakamilika.

Ukaguzi umebaini kwamba ujenzi wa maegesho hayo bado haujakamilika licha ya mkandarasi kukamilishiwa malipo yote ya ujenzi huo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba huo pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

### Majibu ya Wizara

Wizara iliingia Makubaliano na Mkandarasi ya Ujenzi wa maegesho ya magari katika ofisi ya Migombani kwa jumla ya **Shilingi 37,181,800**. Hadi sasa Mkandarasi ameshalipwa**Shilingi 24,500,000** sawa na asilimia 66 na kufanya bakaa ya **Shilingi 12,681,800**. fedha ambazo hazijalipwa hadi sasa. Mkandarasi bado hajalipwa fedha zilizobaki kwa sababu kazi ya ujenzi haijakamilika.

Kamati imebaini kuwa kuna utofauti wa malipo ambapo majibu baina ya Ripoti ya Mdhibiti malipoyalikuwa shilingi milioni31 lakini Kamati ilielezwa kuwa malipo yalikuwa shilingi milioni 24 kamati ilitaka ufafanuziwa kina kutoka Wizaran. Hata hivyo Wizara imekiri kweli kumetokea utofauti wa fedha hizo , hata hivyo eneo husika tayari limeshatengezwa

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya imebaini kuwa kuwepo kwa tofauti ya kiwango cha fedha kilicholipwa ambapo katika majibu manangement letter kwa Mdhibiti Wizara imesema imeshalipa 31,000,000 wakati majibu ya Wizara kwa Kamati ya PAC imesema imelipa 24,000,000

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC Wizara iwe na uhakika inapotoa taarifa zake katika vyombo mbalimbali vya Serikali

### Hoja Namba 5.8.1.4 Uwepo wa madeni ya muda mrefu shilingi 153,112,673

Katika ukaguzi uliofanyika, kumebainika jumla ya shilingi 153,112,673 ikiwa ni madeni yanayodaiwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2018 hadi 2020. Kuendelea kuwepo kwa madeni hayo kunaathiri bajeti pamoja na shughuli za wizara kutokutekelezeka kwa wakati

Ukaguzi unashauri uongozi wa wizara kulipa madeni kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano na watoaji huduma. Mchanganuo wa orodha ya wadai hao ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Madeni ya Muda Mrefu

| Namba | Jina la Mdai | Jumla ya Fedha(Shs.) |
|---|---|---|
| 1 | Nyerere International Airport | 1,150,000 |
| 2 | Zenj Holding Ltd | 5,500,000 |
| 3 | Steam Com Technologies | 14,827,408 |
| 4 | Tanzania Standard Newspaper | 3,303,000 |
| 5 | Kondo Building & Furniture | 5,455,500 |
| 6 | Aakia | 5,712,000 |
| 7 | Wakala wa Uchapaji | 2,250,000 |
| 8 | Multirefrigaration | 5,870,000 |
| 9 | Mekon Arch Consult Ltd | 31,591,545 |
| 10 | Zanzibar Cleaning Services | 16,343,220 |
| 11 | Simba Spare Parts | 8,460,000 |
| 12 | Multirefrigaration | 52,650,000 |
| | Jumla | 153,112,673 |

Majibu ya Wizara

Wizara ya Biashara na Viwanda imepokea ushauri wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kututaka kulipa madeni kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano na watoaji huduma. Katika kuufanyia kazi ushauri huu, Wizara imefanya jitihada za makusudi kulipa deni hilo kwa kiwango cha Shs. 114,794,765.00 sawa na asilimia 74.97 na kubakia deni la Shs.38,317,908.00 ambapo Serikali inalipa taratibu kwa mujibu wa upatikanaji wa Fedha za Matumizi mengineyo (O.C.).Mchanganuo wa madeni na namna yalivyolipwa yanaoneshwa katika Jadweli lifuatalo.:-

Mchanganuo wa madeni na namna yalivyolipwa

| . | MDAI | JUMLA YA DENI | ALICHOLIPWA | BAKAA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Nyerere International Air port | 1,150,000 | 0.00 | 1,150,000 |
| 2 | Zenj Holding Ltd | 5,500,000.00 | 5,500,000. | 0.00 |
| 3 | Steam Com Technologies | 14,827,408.00 | 0.00 | 14,827,408 |
| 4 | Tanzania Standard News Papers | 3,303,000.00 | 0.00 | 3,303,000 |
| 5 | Kondo Building & Furniture | 5,455,500.00 | 0.00 | 5,455,500.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6 | AAKIA | 5,712,000.00 | 0.00 | 5,712,000.00 |
| 7 | Wakala wa Uchapaji | 2,250,000.00 | 2,250,000.00 | 0.00 |
| 8 | Multirefrigaration | 5,870,000.00 | 0.00 | 5,870,000.00 |
| 9 | Mekon Arch Consult Ltd | 31,591,545.00 | 31,591,545.00 | 0.00 |
| 10 | Zanzibar Cleaning Services | 16,343,220.00 | 16,343,220. | 0.00 |
| 11 | Simba Spare Parts | 8,460,000.00 | 6,460,000. | 2,000,000.00 |
| 12 | Multirefrigiration | 52,650,000.00 | 52,650,000.00 | 0.00 |
| | JUMLA | 153,112,673.00 | 114,794,765 | 38,317,908 |

Katika uchunguzi wa kamati imebaini kuwa Wizra imechukua jitihada la kupunguza deni la shilingi 114,794,765 sawa na asilimia 74.97 kamati ilipata furusa ya kuviona baadhi ya villelezo vya malipo haya. Kamati imeridhika na uamuzi huu , Wizra ina changamoto ya fedha katika ulipaji madeni maana wanategemea fedha zao kutoka kwenye Matumizi mengineyo (OC )

Vile vile kamati ya PAC  imebaini kuwa Wizara ,kutokana na kukaa namadeni ya muda mrefu kuna changamoto nyingi zinajitokeza ,kamati imebaini kuwa kuna mdai anaitwa KONDO BULDINGIAND RURNITURE alikuwa anadai shilingi 5,455,500 hadi anafariki deni lilikuwa halijalipwa, ingawa saivi tayari deni limeshalipwa kwa wahusika.

Uchunguzi ya Kamati

Kamati ya PAC imehoji namna ya Wizara inavyowalipa waridhi madeni na kuelezwa anapofariki mdai kama mtu binafsi ataandikishwa kupitia waqfu iwapo waqfu itamtambua na kumuombea deni au kumpa nyaraka za kuweza kudai mwenyewe.kwa kampuni huwa haifu kwa sababu mwenyehisa ndio watashughulikia.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

- Kamati ya PAC Serikali ifanye uhakikiwa madeni yote ili iweze kujipanga vizuri na kulipa

- Ni vizuri kwa wadai ambao wamefariki waridhi wao wasiwalipe kidogo kidogo wawalipe fedha zote ili kupunguza mtafaruku katika jamii.

## 3.1 WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO – PEMBA

### Hoja Namba 5.8.1.5 Manunuzi yaliofanyika kinyume na utaratibu shilling 4,213,000

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza 'Kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au venginevyo kushiriki katika manunuzi ya umma ispokuwa mtub huyo kampuni au chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi chini ya sheria hii'.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu au kampuni ambayo hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambapo watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi, kwa mujibu wa sheria ambapo kumepelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa malipo hayo.

Kuwatumia watoa huduma ambao hawakusajiliwa kwa mujibu wa sharia kunapelekea kuikosesha serikali mapato yanayotokana na kodi ya thamani nan i kwenda kinyume na Sheria yan Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa manunuzi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 67: Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu

| Nambari ya Hati ya Malipo | Nambari ya Hundi | Jumla ya fedha (SHS) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 10/10<br>15/10/2019 | 009709 | 168,000 | Wizara ya Biashara na Viwanda. | Ikiwa ni malipo ya fedha za marejesho kwa ajilin ya ununuzi wa rangi. |
| 8/12<br>11/12/2019 | | 680,000 | Wizara ya Biashara na Viwanda. | Ikiwa ni malipo ya fedha ya ununuzi wa vyakula na viburudishaji. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3/2<br>04/2/2020 | 000020 | 2,000,000 | Mau Food and Snacks. | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula . |
| 14/9<br>5/11/2019 | 008752 | 750,000 | Wizara ya Biashara na Viwanda Pemba. | Ikiwa ni malipo ya fedha za marejesho kwa ajili ya unuuzi wa chakula na viburudishaji. |
| 3/09<br>4/9/2019 | | 615,000 | Wizara ya Biashara na Viwanda Pemba. | Ikiwa ni malipo ya fedha za marejesho kwa ajili ya ushonaji wa mapazia, ununuzi wa henga na upakaji wa rangi wa Ofisi. |
| Jumla | | 4,213,000 | | |

Majibu ya Wizara

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ni kweli inakabiliwa na deni la muda mrefu kama lilivyotajwa kwenye Hoja hiyo hapo juu, hii imetokana na upatikanaji mdogo wa Fedha za matumizi mengineo hivyo kushindwa kukamilisha malipo ya madeni tunayodaiwa kutokana na mahitaji tuliyoyapata kwa watoa huduma wetu Kama Kiambatanisho namba tatu (3) linavyoonesha.

Hata hivyo Wizara tayari imeshapeleka madeni yote tunayodaiwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar ili kupatiwa uwezekeno kwa kulipa madeni hayo

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilielezwa kuwa katika siku zilizopita watendaji wa Kitengo cha Ununuzi cha Wizara walikuwa hawako vizuri kiutendaji lakini kwa hivi sasa wamekuwa wanaenda vizuri na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara iwe makini katika kutekeleza kazi zake kwa kufuata Sheria zilizopo kwa kuhakikisha kuwa inapotaka kufanya ununuzi inawatumia watoa huduma waliosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ili kasoro kama hizo zisitokee tena.

Hoja Namba 5.8.1.6 Wizara kushindwa kulipa deni la muda mrefu shilingi 5,397,225.

Wizara ya Biashara na Maendeleaya Viwanda – pemba huingia katika makubaliano ya ununuzi wa bidhaa na huduma mbali mbali kutoka kwa wafanya biashara tofauti kwa ajili ya matumizi ya Wizara.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara inadaiwa na Tahfif Auto Parts jumla ya shilingi 5,397,225 ambazo ni fedha zinazodaiwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia 2016 hadi 2020 kwa ajili ya utengenezaji wa magari.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(3) (b) cha sheria ya usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ni kweli inakabiliwa na deni la muda mrefu kama lilivyotajwa kwenye Hoja hiyo hapo juu, hii imetokana na upatikanaji mdogo wa Fedha za matumizi mengineo hivyo kushindwa kukamilisha malipo ya madeni tunayodaiwa kutokana na mahitaji tuliyoyapata kwa watoa huduma wetu Kama Hata hivyo Wizara tayari imeshapeleka madeni yote tunayodaiwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar ili kupatiwa uwezekeno kwa kulipa madeni hayo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa awali deni hilo lilikuwa kubwa zaidi (lililofikia zaidi ya shilingi milioni 7) na liliwahi kulipwa kidogo ambapo kwa hivi sasa Wizara ya Biashara Pemba inaendelea kujiridhisha juu ya deni hilo kutokana na tatizo lilibainika la mtoa huduma huyo kutolipa kodi vizuri na pia Wizara kuwa na shaka ya kupandshiwa madeni. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa Wizara Makao Makuu inakusudia kukaa pamoja na watendaji wa Wizara hiyo Pemba kwa ajili ya kulipitia kwa kina deni hilo na kuona uhalali wake ili

kuweza kulilipa. Aidha, imebainika kuwa kwa hivi sasa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Pemba haiitumii mtoa huduma huyo (Tahfif Auto Parts) kwa ajili ya kutengeneza gari zake na badala yake inatumia Karakana Kuu Pemba. Hali halisi ya deni hilo na malipo yake inaonekana katika Jadweli lifuatalo.

Jadweli la Uchambuzi wa Deni na Malipo

| TAREHE | INVOICE NO; | KIMA CHA DENI | RECEIPT NO; | KILICHOLIPWA |
|---|---|---|---|---|
| 16/02/2018 | 2237 | 2,930,000 | | _ |
| 29/07/2019 | 2863 | 1,000,000 | 1645 | 830,509 |
| 09/08/2019 | 2879 | 856,680 | 1685 | 830,509 |
| 16/08/2019 | 2308 | 2,930,000 | 1773 | 830,509 |
| JUMLA | | 7,716,680 | | 2,491,527 |
| BAKAA LA DENI | | 5,225,153 | | |

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kwa kuwa deni inalodaiwa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda (Pemba) na Tahfif Auto Parts ni deni la muda mrefu, Kamati ya PAC imeitaka Wizara hiyo kufanya haraka kulihakiki deni hilo ili liweze kulipwa kama linavyostahiki.

3.2 FUNGU K 02 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Taarifa ya Mapato

Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali ulikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 195,655,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 .hadi kufikia 30 juni , 2020 Wizara ilikusanya jumla ya shilingi 108,651,790 sawa na asilimia 55.53 ya makusanyo.

Majibui ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi 195,655,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019-2020. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 Wizara ilikusanya jumla ya shillingi 108,651,790 sawa na asilimia 55.53 ya makadirio kama inavyyonekana katika jadweli

FEDHA ZILIZOKUSANYWA

| CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO TZS | MAKUSANYO TZS | ASILIMIA |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| LESENI ZA USAJILI WA SKULI BINAFSI | 98,827,000 | 57,689,500 | 58.37 |
| LESENI ZA WALIMU | 96,828,000 | 50,962,290 | 52.63 |
| JUMLA | 195,655,000 | 108,651,790 | 55.53 |

Wizara ya Elimu imekukusanya kiwango hicho cha fedha kama ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Makusanyo hayo yamepungua kutokana na sababu zifuatazo;

Kuwepo kwa ugonjwa wa UVIKO-19 imepelekea kupungua kwa ukusanyaji wa mapato kwa wakati huo kwa vile skuli zililazimi

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imehoji kupungua kwa makusanyo na kuelezwa kuwa wakati wa corona skuli nyingi zilifungwa na kupelekea malipo kupitia lesseni za walimu kushuka ,pia hivi sasaWizara ya Elimu tayari wameshaanza kutumia system ya kielectonic katika ukusanyaji wa mapato.
Hata hivyo Kamati imebaini kuwa Tawala za Mikoa wanatumia kutoa kodi skuli za private kama sehemu ya biashara jambo ambalo wanakinzana na Waraya ya elimu

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamaiti imeshauri Wizara ya Ealimu kukaa pamoja naOfisi ya Rais Tawala za Mikoam Serikali za Mitaa na Idara Maalum katika kubadilisha vifungu vya sheria katika utoajiwa kodi za skuli ya private ili kuondo usumbufu

## Taarifa ya Matumizi

Wizara ya Elimu na Mifungo ya Amali katika mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 70,057,655,116 kwa matumizi ya kawaida ,shilingi45,619,400,721 ikiwa ni ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu na mafunzo ya Amali na shilingi 5,800,000 ,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia 30,juni , 2020 jumla ya shilingi 61,654,026,656 zilitumika kwa kawaida sawa na asilimia 88 ya makadirio ,shilingi 36,324,323,640 zilitumika kwa ruzuku za taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu sawa na asilimia 79.62 ya makadirio, na shilingi 2,406,000,000 zilitumika kwa kazi za maendeleo ikiwa sawa na asilimia 41.48 ya makadirio.

## Majibu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla TZ 189,021,464,137 kati ya hizo TZS 70,057,655,116/= kwa kazi za kawaida, TZ 45,619,400,721 ikiwa ni ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, TZ 5,800,000,000 kwa kazi za maendeleo kupitia mchango wa Serikali na TZ 67,544,408,300 kutoka kwa wahisani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 Wizara ilitumia jumla ya TZ 120,876,921,148 sawa na asilimia 63.95 kati ya hizo TZ 61,654,026,656 zimetumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 88, TZS 36,324,323,640 kwa ruzuku za Taasisi sawa na asilimia 79.62 ya makadirio na TZS 2,406,000,000 zimetumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 41.48 ya makadirio kwa mchango wa Serikali zimetumika na kwa upande wa wahisani TZ 20,492,570,852 sawa na asilimia 30.34 ya makadirio.

MAKADIRIO NA MATUMIZI HALISI KWA KAZI ZA KAWAIDA

| MAELEZO | MAKADIRIO | HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 53,603,655,116 | 51,145,087,202 | 95.41 |
| MATUMIZI MENGINEYO | 16,454,000,000 | 10,508,939,454 | 63.87 |
| RUZUKU | 45,619,400,721 | 36,324,323,640 | 79.62 |
| JUMLA | 115,677,055,837 | 97,978,350,296 | 84.70 |
| MAENDELEO | | | |
| SERIKALI | 5,800,000,000 | 2,406,000,000 | 41.48 |
| WAHISANI | 67,544,408,300 | 20,492,570,852 | 30.34 |
| JUMLA KUU | 189,021,464,137 | 120,876,921,148 | 63.95 |

Ni kweli kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imepatiwa kiwango hicho cha fedha kwa matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo. Kiwango hicho cha fedha ni kizuri ukilinganisha na miaka mingi ya nyuma iliyopita. Wizara inaipongeza Serikali kwa uingizaji mzuri fedha ambao umepelekea kuweza kutekeleza majukumu tuliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo bado ipo haja ya kuhakikisha fedha zote zilizopangwa zinaingizwa ili kuhakikisha yote tuliyopanga tunatekeleza kwani ongezeko la fedha za makadirio ya bajeti kwa kila mwaka wa fedha hayaendani na ukuwaji wa mahitaji halisi ya shughuli za kielimu kwa nchi yetu.

Kiwango cha fedha ambacho hakikupatikana kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na udogo wa makadirio ya fedha za bajeti imepelekea baadhi ya shughuli za Wizara

kutokukamilika utekelezaji wake.

Zifuatazo ni Shughuli ambazo hazikukamilika utekelezaji wake:

i. Upungufu wa upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika skuli zetu Unguja na Pemba kama vifaa vya Maabara, Madaftari, Chaki, Vifaa vya ufundi n.k.

ii. Malipo ya mitihani ya Kidato cha Nne na Sita kwa Baraza la Mitihani la Taifa, kwani hadi sasa Wizara ina deni la mwaka 2019/2020 TZS1,334,200,000 na deni hilo hatujalipa.

iii. Malimbikizo ya mishahara kwa Wafanyakazi 559 hayakukamilika (Kwa sasa fedha za malimbikizo zimepatikana kwa awamu ya kwanza kwa wafanyakazi 314 kwa bajeti 2021/2022. Hadi sasa wafanyakazi 245 wa mwaka 2019/2020 hawajalipwa.

iv. Kutokukamilika kwa ujenzi wa Madarasa 15 ya Skuli za Sekondari yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi kwa Unguja na Pemba.

v. Kutokamilika kwa ukarabati wa Skuli 7 za Unguja na Pemba.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inatekeleza miradi ifuatayo;

1. Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi.
2. Uimarishaji wa Elimu ya Lazima.
3. Uimarishaji wa Elimu ya Mbadala na Amali.
4. Kupanga na kusimamia kazi za Wizara.
5.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji deni la la malipoya mitihani ya kidatu cha nne na sitakwa Baraza lamtihani la Taifa na kamati iliambiwa kila kwa wanalipa hayo madeni lakini bado halijamaliza kwa sababu deni ni kubwa sana ,kamati ilitaka kuwapatiwa vielelezo vya amlio ya deni hilo na ilipata kukagua stakabadhi (risiti) za malipo ya madeni

Mapendekezo ya kamatiya PAC

Kamati ya PAC inashauri Wizara ya elimu ilipe deni la Mitihani ya Taifa kwa wakati unaotakiwa

Hoja Namba 5.9.1.1 Fedha ambazo zimebakia katika hesabu ya Amana bila yakuwa na ahadi ya matumizi shilingi 90.404.613.17

Jumla ya shilingi 90,404,613.17 zimebainika kubakia katika hesabu ya amana ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya amali yenye jina la Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na nambari 0433888000 iliyopo Benk ya Watu wa Zanzibzr (BPZ) ikiwa ni fedha zinazotokana na matumizi ya kawaida ya Wizara katika gharama za uendeshaji.

Kifungu nambari 52(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 (2016) kinaeleza kuwa bakaa ya matumizi ambayo hayakutumika hadi mwisho wa mwaka wa fedha ambao matumizi hayo yameidhinishwa , kuingizwa katika hesabu ya Mfuko Mkuu wa Serikali .

Ukaguzi umebaini kwamba fedha hizo zimebakishwa katika hesabu ya Amnana pasi ns kuwepo na ahadi ya matumizi (commitment) ya shughuli za Wizara na ruhusa ya matumizikutoka kwa mlipaji Mkuu wa Serikali (paymaster General) kwa ajili ya kubakisha fedha hizo ili kukidhi mahitaji ya matumizi yaliyokusudiwa ya daadaye.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 52(2) chs Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Hoja Namba 5.9.1.2 Malipo yasiyokuwa na vielelezoshilingi 1,304,827,147

Ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo kupitia hesabu ya Maendeleo yamefanyika la kini vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kudhibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanisha vielelezo vya malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha sheria Usimamizi wa Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Malipo yenyewe ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chin

Malipo yasikuwa na vielelezo

| Nambari ya hati ya malipo | Jumla ya fedha (SHS) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 7/6,19/6/2020 | 833,417,680.00 | BNKTRF | Ikiwa ni malipo ya dummy |
| ½, 10/2/2020 | 160,000,000.00 | MOE BADEA project | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya maandalizi ya mradi mpya pamoja na ununuzi wa vifaa vya kupitia skuli ya secondary kibuteni |
| 30/6,26/6/2020 | 152,422,890.00 | Katibu Mkuu Wizara | Ikiwa ni malipo ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | ya Elimu | shughuli mbali mbali za Wizara |
| 3/2,10/2/2020 | 100,000,000.00 | Third Education Project | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ujenzi wa skuli tisa za mradi wa ZATEP |
| 4/7,26/7/2019 | 36,000,000.00 | MOE BADEA P roject | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ujenzi wa skuli ya Sekendari kibuteni |
| 23/6,26/6/2020 | 22,986,576.00 | Salem Consraction Limeted | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ujenzi wa skuli ya Micheweni |
| Jumla | 1,304,827,147 | | |

Majibu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Fedha ambazo zilizokuwemo katika hesabu nambari **0403888000** yenye jina la Katibu Mkuu Wizara ya Elimu zote zilikuwa ni fedha za mishahara ya wafanyakazi wapya ambao hulipwa taslim na mkopo wa dharura (Revolving Fund).

Kamati imehoji kuhusu kutokuwepewa kwan CAG vielelezo vya malipo na wizara walikiri kuwa vilelezo vilikuwa havijaakamili kwa baadhi ya kampuni wakati CAG alipokwenda lakini kamti ilipokwenda ilipatiwa hizo hati za malipo ,kwa hiyo wizara ilichelewa kuji hoja ya vielelezo kumpa CAG

Mapendekezo ya kamati ya PAC

Wizara inatakiwa kuwasilisha kumbukumbu vizuri ili CAG anapokwenda acute kumbukumbu zote.

Majibu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Wizara iliweza kufanya malipo hayo na Vielelezo vyote vya matumzi hayo vipo. Wakati ukaguzi unaendelea, baadhi ya risiti za makampuni ilikuwa hawajatuwasilishia baada ya ufuatiliaji makampuni hayo yaliweza kuwasilisha vielelezo hivyo na kwa sasa tayari

vimesha ambatanishwa na vocha husika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeihoji wizara ya Elimu na wamekiri kweli hawakupata ruhusa ya ma tumizi kwa hiyo wamefanya kosa, kwa hali hii Kamati haikuridhika , hata hivyo kamati ilitaka kuona vielelezo vya amtumizi ya fedha hizo hizo ,kamati ilipata kukagua vitelezo husika.

Vocha NO OC/E/46/06 malipo kwa ajili ya mishahara ya waafanyakzi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amalikwa mwezi wa juni 2020.

Mapendekezo ya  Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na vielelezo vya matumizi ya fedha hizo

Hoja Namba 5.9.1.3 Kutokuwasilishwa kwa taarifa za fedha za miradi ya maendeleo kwa ajili ya ukaguzi  shilingi 9,351,278,254

Katika ukaguzi uliafanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 9,351,278,254 zimetumika kwa ajili ya matumizi ya baadhi  ya miradi ya maendelao ya Wizara ya Elimu kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Ukaguzi umebaini kuwa taarifa za Fedha za mwaka za miradi hiyo hazikuwasilishwa kwa mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serekali kwa ajili ya ukaguzi .

Kufanya hivyo ni kwenda kinyme na kifungu nambari 119(1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12(2016) .Mchanganuo wa taarifa za miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika jadwel lifuatalo.

Miradi ya maendeleo

| Namba | Jina la Mradi | Aina ya maradi | mfadhili | Fedha zilizopatikana kwa 2019/2020 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uimarishaji wa elimu ya Maandalizi na msingi (HGSFP) | Msaada | TFT(Japan) | 691,213,145 |
| 2 | Uimarishaji wa elimu ya lazima | Mkopo | BADEA | 2,739,048,448 |
| 3 | uimarishaji elimu ya lazima (ZATEP) | mkopo | OFID | 5,921,061,664 |
| JUMLA | | | | 9,351,278,278,254.00 |

Majibu ya Wizara

Miradi ya maendeleo hupata fedha zake kutoka SMZ ikiwa kama mchango wa Serikali. Fedha hizo hutoka Ofisi ya Raisi Fedha na Mipango baada ya kupeleka maombi ambayo yamethibitishwa kutoka kwa wahusika katika miradi, wahusika wa Wizara na kuhakiki maombi kwa kujiridhisha kwa ajili ya kuomba kwa mkandarasi kufanyiwa malipo yake alioomba. Malipo hayo yanaweza kufanywa kupitia hesabu ya Wizara au mradi kwa sababu ili yakamilike ni lazima kuwe na ushahidi wake ambao unaambatanishwa kwa Wizara zote husika. Miradi hiyo ya mkopo ni ya malipo ya moja kwa moja kutoka kwa wafadhili (Direct Payment). Kwa hiyo malipo hufanywa moja kwa moja na mfadhili baada ya Wizara kupitia maombi ya malipo na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, kwa upande wa fedha za mchango wa Serikali zinakuwa zimo katika hesabu ya Wizara na zinakaguliwa na Mkaguzi wa nje.

Uchunguzi wa kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeihoji Wizara ya Elimu kutowasilishwa kwa taarifa ya fedha za miradi , kamati imebaini kuwa taarifa ya fedha za miradi hazipo hii imetokana na miradi yote malipo yanakuwa yanalipwwa moja kwa moja kwa hiyo inakuwa ngumu kuwasilisha kwa mkaguzi na wizara imekiri kutokuwepo kwa hati za malipo.

### Hoja Namba 5.9.1.4 Kuchelewa kuleta madfatari ya Wanafunzi wa Sekondari 886,000 ya kurasa 2000

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilisaini mkataba wenye kumbukumbu nambari SMZ/KO1/G/ICT/2018-2019-2019/13 wa tarehe 12 Juni, 2019 na kampuni ya IRG ELECTRIC COMPANY LTD kwa ajili ya ununuzi wa madafatari ya skuli ya sekondari Zanzibar .

Mkataba huo ulikuwa na kiasi cha shilingi 2,774,823,100 (pamoja na kodi ya ongozeka la thamani ). Kwa mujibu wa mkataba huo muuzaji alitakiwa alete madaftari1,074,250 yenye kurasa 200 na madftari 1,075,823,820 yenye kurasa 400 . Madaftarihayo yalipaswa kuletwa si zaidi ya siku 120 baada ya kusainiwa mkataba.

Ukaguzi umebaini kuwa muuzaji alilipwa shilingi 460,902,820 kupitia hati ya malipo nambari 5/10 ya tarehe 7 oktoba ,2019n ikiwa ni malipo ya awali ya ununuzi wa madaftari hayo.

Aidha ukaguzi umebaini kuwa muda wa mkataba umeshamaliza na hadi ukaguzi unakamilika ,Madaftari yaliyopelekwa ni 886,000 ambayo yalichelewa kuletwa zaidi ya mwaka mmoja kutoka tarehe iliyopangiwa ,na jumla ya madaftari 1,264,500(1,075,250 ya kurasa 400 na 189,250 ya kurasa 200) bado hayajapelekwa ambayo ni zaidi ya nusu ya idadi ya madaftari yote yaliyokubaliwa katika mkataba na Wizara haijachukua hatua zozote kupata fidia (recover for damages) baada ya mzabuni kuvunja masharti ya

mkataba ikiwemo kudai fedha za dhamana ya malipo ya awali (advance payment guarantee) ya asilimia 20 na dhamana ya kazi (performance security) ya asilimia 10. Tarifa za madaftari yaliyoletwa ni kama inavyoonekana katika jadwel lifuatalo.

Madfatari yaliyopokelewa

| Namba | Tarehe | Hati ya upokeaji bidhaa (delivery note) | Idadi ya madaftari (ya kurasa 200) |
|---|---|---|---|
| 1 | 26 0ctoba | 119 | 271,760 |
| 2 | 10 Disemba | 124 | 325,040 |
| 3 | 11 Disemba | | 289,200 |
| Idadi ya madaftari | | | 886,000 |

Majibu ya Wizara

Wizara iliingia mkataba na kampuni ya IRG kwa ajili ya usambazaji wa madaftari ya kuandikia pamoja na ya majina kwa skuli zetu za sekondari. Kutokana na janga la UVIKO-19, mzabuni alishindwa kutusambazia madaftari hayo kwa wakati. Wizara haikuweza kumshinikiza kutokana na vipengele vya mkataba GCCF.27.1. Kwa sasa tayari Wizara imeshapokea makontena yote ya madaftari kutoka kwa msambazaji huyo na tayari madaftari hayo yashasambazwa katika skuli.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini Wizara iliamua kutafuta msambazaji mwengine bila ya kumuarifu msambazaji wa mwanzo ambaye alipata maradhi ya KORONA hata hivyo Wizara imeeleza kuwa msambazaji anao uwezo kusitisha mkataba iwapo kutatokezea maradhi kwa mujibu wa Mkataba.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara iwe makini katika kuchagua msambazaji wanaoingia nao Mikataba

Hoja Namba 5.9.1.5 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 92,454, 978

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwambakwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 kuna hati za malipo zenye thamani ya shilingi 92,454,978 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Wizara ya Elimu ambapo hati za malipo hayo hazikupatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo

Kufanya hivyo hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya Zanzibar ya mwaka 2016 pamoja na kifungu nambari 95(4) cha kanuni ya fedha ya mwaka 2005. Mchanganuowa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadwel lifuatalo.

Jadwel Nambari 80:Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi

| Namba | Nambari ya | Aliyelipwa | Jumla ya fedha (SHs) |
|---|---|---|---|
| 1 | 41/9 ya 10/9/2019 | Zanzibar Shipping Cooperation | 33,600,000.00 |
| 2 | 46/10 ya 10/10/2019 | SM Store | 58,854,978.00 |
| Jumla | | | 92,454,978.00 |

Majibu ya Wizara

Wizara ilifanya malipo hayo kugharamia sherehe za Elimu Bila Malipo kwa bajeti ya 2019/2020. Hati za malipo ziliombwa na Afisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) kwa uchunguzi. Stakabadhi ya makabidhiano ya hati hizo zipo.

Uchunguzi wa kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeihoji Wizara yaElimu katika hoja hii na ikakiri kuwa walipokuja wakaguzi wa Mdhibiti vielelezo vya amlipo havikupatikana ila vilikuwepo ZAEKA kwa hiyo CAG hakuweza kuviona , hata hivo kamati ilipa tafurusa ya kukaguaa hati hizo za malipo

3.3 FUNGUU H 01 WIZARA YA AFYA (WIZARA YA AFYA, USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO.

Taarifa ya Mapato.

Wizara ya afya ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilinhi 387,235,000 katika kipindi cha waka

wa fedha 2019/20201. Hadi kufikia tarehe 30juni, 2020 Wizara ya Afya imekusanya jumla ya shilingi 204,453,069 sawa na asilimia 52.8 ya makadirio

Majibu ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto

Wizara ya Afya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 387,235,000.00 kutoka katika vyanzo vyake vya makusanyo ya mapato. Vyanzo vyenyewe ni kama vifuatavyo:

IDARA YA KINGA

1. Shahada ya maradhi ya kuambukiza
2. Huduma za daktari na orodha ya wafanyakazi
3. Huduma za uchunguzi wa Afya.

IDARA YA TIBA.

1. Ada za usajili wa tiba asili.

IDARA YA UENDESHAJI NA RASILIMALI WATU.

1. Nyaraka za zabuni.

OFISI KUU PEMBA.

1. Huduma za uchunguzi wa Afya.

Kwa upande wa Wizara ya Afya hadi kufikia 30 June 2020 imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 233,741,984.00 ikiwa ni sawa na asilimia 60 ya makadirio. Wizara ya Afya haikufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kama ilivokadiriwa kutokana na sababu ya kuwepo kwa maradhi ya UVIKO-19 (COVID 19) hali ambayo imeathiri mwenendo wa uchumi na kuathiri ukusunyaji wa mapato hususan katika Idara ya Kinga. Kupungua sana kwa shughuli za usafiri za kuingia kwa wageni kutoka nje ya nchi na wenyeji wa Zanzibar kwenda nje ya nchi.
Jaduweli lifuatalo linaonesha makadirio na makusanyo halisi vya mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kuanzia Julai 2019 hadi Juni 2020.

Vyanzo vya Mapato

| GSFC H01 | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO | MAKUSANYO HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1422035 | Shahada ya maradhi ya kuambukiza | Tsh. 105,893,000/- | Tsh. 99,299,000/- | 91% |
| 1422050 | Huduma za Daktari na Orodha ya wafanyakazi | Tsh. Tsh. 80,254,000/- | Tsh. 22,919,000/- USD 9030 | 55% |
| 1422051 | Huduma za uchunguzi wa Afya. | Tsh. 976,000/- | Tsh. 45,200,248/- | 72% |
| 142209 | Ada za usajili wa tiba asili | Tsh.36,705,000/- | 21,771,296/- | 59% |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | | | | |
| 142208 4 | Nyaraka za zabuni. | Tsh. 10,073,000/- | 7,200,000/- | 71% |
| 142205 1 | OFISI KUU PEMBA<br>Huduma za uchunguzi wa Afya | Tsh. 15,362,000/- | Tsh. 16,150,000/- | 105% |
| | Vyanzo vyenginevyo (matibabu bure) | 75,969,000/- | 0 | 0% |
| | **JUMLA** | **387,232,000/-** | **233,741,984/-** | **60%** |

Kwa upande wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi **560,471,000** kwa kipindi cha mwaka 2019/2020. Hadi kufikia Juni, 2020 Hospitali ilikusanya jumla ya shilingi **629,140,366** ambazo ni sawa na asilimia 112 ya makadirio.

UFAFANUZI WA MAKADIRIO.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Hospitali ya Mnazi Mmoja ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi **560,471,000.** Hadi kufikia Juni, 2020 jumla ya shilingi **629,140,366** sawa na asilimia 112 zilikusanywa. Sababu ya ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa wanafunzi wa kigeni (Elective students)waliokuja kufanya mafunzo kwa vitendo kutoka sehemu mbali mbali

Vyanzo vikuu vya mapato vya Hospitali ya Mnazi Mmoja v ni Huduma za Haraka, Bima na malipo ya huduma za Afya ikiwemo wanafunzi wa kigeni.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa kuna tofauti ya tarifa ya makusanyo baina ya Wizara ya Afya na Mdhibiti ,kwa uapande wa Wizara ya Afya imekusanya jumla ya shilingi 233,741,984 na kwa uapande wa Mdhibit imekuanya jumala ya shilingi 387,235,000 ,kamati imebaini kuwa financial statement haikutoa taarifa sahihi hii Kamati imebainikuwa vyanzo vya mapoto vinapanda na kushuka ,hata hivyo kamati haikuridhishwa na majibu ya financial statementya Wizara . Kamati ya PAC haikuridhika na taarifa ya mapato ya Wizaraya afya.

Taarifa ya Matumizi

Wizara ya Afya ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 52,004,500,000 kwa matumizi ya kawaida za wizara , na jumla ya shilingi 17,869,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo , na jumla ya shilin gi 2,470,602,000 ni ruzuku kwa ajili ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya .

Aisha , Wizara ya Afya ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 16,242,798,000 kwa kazi za maendeleo michango ya wafadhili.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 48,776,873,948 ziliingizwa na kutumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 93.8 ya makadirio, na shilingi 2,163,805,351 ikiwa ni ruzuku kwa ajili ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ua Afya sawa na asilimia 97 ya makadirio. Aidha , jumla ya shilingi3,863,250,500.14 ziliingiozwa na kutumika ikiwa ikiwa ni fedha za wahisani kwa miradi ya maendeleo sawana asilimia 24 ya makdirio.

Majibu ya Wizara

Katika kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Afya ilikadiriwa kutumia jumla ya shillingi 88,613,900,000.00 na hadi kufikia 30 June wizara ya Afya ilitumia jumla ya shilingi 70,105,538,694.14 sawa na asilimia 79%. hivyo kupelekea Wizara kutokufikia makadirio ya matumizi yaliyopangwa.

Jaduweli la hapo chini linaonesha makadirio ya mishahara na matumizi halisi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama ifuatavyo.

| MAELEZO | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA | Tsh. 17,018,733,540.00 | Tsh. 18,749,932,439.00 | 110% |
| MATUMIZI YA KAWAIDA | Tsh. 34,985,766,460.00 | Tsh. 30,027,141,509.00 | 86% |
| MATUMIZI YA RUZUKU | Tsh 2,470,602,000.00 | Tsh. 2,163,805,351.00 | 97% |
| MIRADI YA MAENDELEO SMZ | Tsh. 17,896,000,000.00 | Tsh. 15,301,608,895.00 | 88% |
| MCHANGO KUTOKA KWA WAHISANI | Tsh. 16,242,798,000.00 | Tsh. 3,863,250,500.14 | 24% |
| JUMLA KUU | 88,613,900,000.00 | 70,105,538,694.14 | 79% |

Matumizi ya mishahara yamevuka makadirio halisi ya mshahara hali hii ilisababishwa na ongezeko la uajiri kwa wafanyakazi katika mwaka wa fedha 2019/2020. Barua ya tarehe 01/06/2020 na barua ya 26/05/2020 zinaonesha maombi ya WAUJWJW kwenda Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kuombea fedha hizo kwa ajili ya nyongeza ya mshahara.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji kuhusu ongezeko la mishara ilitika Wizara ya Afya kutoa vielelezo vya ajira mpya kama barua ya utumishi ,vibali vya uajiri vilipatiwa na kukaguliwa na Kamati kuridhika navyo.

Hoja Namba 5.10.1.1 Uhaulushaji wa fedha jumla ya shilingi 139,488,789 kutoka hesabu ya Amana nambari 040644600

Ukaguzi umebaini kuhaulishwa jumla ya shilingi 139,488,789 kutoka hesabu nambari 0406446000 ya Amana (Deposite Account) Wizara ya Afya kwa kufanyika matumizi ambayo hati za malipo, maelezo na vielelelzo vyake kavikupatikana kwa mkaguzi.

Kutokupatikana kwa hati za malipo na vielelezo vya matumizi kunapelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa matumizi hayo. Kufanya hivyo nikwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Maelezo ya uhaulushaji huo yanaonekana katika jadwel lifuatalo:-

Uhaulishaji wa fedha

| Namba | Tarehe | Aliyelipwa | Jumla ya shilingi (SHS) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 6/8/2019 | PG Transfer B2B | 8,999,991 | Matumizi ya fedha hizo hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 2 | 12/2/2020 | PG Transfer B2B by +255777423165 | 8,552,332 | Matumizi ya fedha hizo hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 3 | 20/2/2020 | PG Transfer B2B by +255777423165 | 42,108,000 | Matumizi ya fedha hizo hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 4 | 27/2/2020 | PG Transfer B2B | 48,400,000 | Matumizi ya fedha hizo hayakupatikana |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | kwa ukaguzi |
| 5 | 1/4/2020 | PG Transfer B2B | 2,950,000 | Matumizi ya fedha hizo hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 6 | 6/4/2020 | PG Transfer B2B | 5,200,000 | Matumizi ya fedha hizo hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 7 | 9/4/2020 | PG Transfer B2B | 2,410,483 | Matumizi ya fedha hizo hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 8 | 20/4/2020 | PG Transfer B2B | 2,410,483 | Matumizi ya fedha hizo hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 9 | 12/6/2020 | PG Transfer B2B | 6,527,500 | Matumizi ya fedha hizo hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 10 | 12/6/2020 | PG Transfer B2B | 11,930,000 | Matumizi ya fedha hizo hayakupatikana kwa ukaguzi |
| Jumla | | | 139,488,789 | |

Majibu ya Wizara

Matumizi ya **TZS 139,488,789.00** kutoka hesabu ya amana yalifanyika kwa vielelezo na vimepatikana tayari kwa ukaguzi. Naomba kuwasilisha kama jaduweli nambari 82 la hoja linavyojionesha

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa hoja hii vielelezo vyake havikupatikana wakati wa ukaguzi wa CAG , hali hii imetokana na kukosekana kwa mashirikiana baina ya Wizara ya Afya na ofisi ya CAG , kwa upande wa CAG wamesema kuwa wametoa barua ya manangement letter lakini Wizara ya afya hawakukamilisha baadhi ya vielelezo hata hivyo kulikuwa na muda wa kutosha wa kupeleka wa ajili ya kupeleka hivo vielelezo hata hivyo Wizara imekiri watajirekebisha.

Hata hivyo, kamati ya PAC walipokwenda walikuta vielelezo vyote jamabo ambalo kamati ilipata mashaka na vielelezo hivyo na kushindwa kuvikaguo , na Wizara ya Afya imekiriki kutokea kwa kadhia hiyo.

HOJA NAMBA 5.10.1.2: Uhaulishaji wa fedha jumla ya **TZS 118,568,569.00** kutoka hesabu ya Bohari kuu ya Madawa nambari 0404182000.

Ukaguzi umebaini kuhaulishwa jumla ya shilingi 118,568,569 kutoka hesabu nambari 0404182000 ya Bohari ya Madawa ya Wizara ya Afya kwa kufanya matumizi ambayo hati za malipo pamoja na maelezo na vielelezo vyake havikupatikana kwa ukaguzi, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya usimamamizi wa fedha , maelezo ya uhaulushaji huo yanaonekana katika jadwel lifyatalo:-

| Namba | Tarehe | Aliyelipwa | Jumla ya fedha | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2/7/2019 | PG-Transer B2B 0207 16:03:21 REF : 002RTG19072016;Ref:002rtg1907170 | 61,105,798 | Matumizi hayo hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 2 | 18/7/2019 | PG-Transer B2B 0207 16:05:45 REF : 002sw190717005;ref:002sw1907170 | 20,584,545 | Matumizi hayo hayakupatikana kwa ukaguzi |
| 3 | 12/12/201 | PG-Transer B2B CBS :Fund Trans | 16,694,370 | Matumizi hayo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 9 | by 0777424084 Ref 005rtg19121203 | | hayakupatikan a kwa ukaguzi |
| 4 | 27/12/2019 | Transfer from an Account to an account charge AB.36/393/07 | 12,024,988 | Matumizi hayo hayakupatikan a kwa ukaguzi |
| 5 | 2/5/2020 | Director transfer TRF firm Afya Med store to Mult Customer DOC :20000031 | 4,312,213 | Matumizi hayo hayakupatikan a kwa ukaguzi |
| 6 | 2/3/2020 | Direct transfer W.Afya central Medical store Doc :20000005 | 3,846,655 | Matumizi hayo hayakupatikan a kwa ukaguzi |

Majibu ya Wizara
Uhaulishaji wa fedha TZS 118,568,569 kutoka hesabu ya Bohari kuu ya dawa. Malipo haya yalifanyika kwa kufuata taratibu za malipo na vielelezo vipo kwa ukaguzi. Naomba kuwasilisha kama jaduweli nambari 83 linavyoonesha.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC
Kamati haikuridhika na hali ya kukosekana kwa vielelezo wakati wa Ukaguzi na hivyo haikuridhia kuvikagua.

HOJA NAMBA 5.10.1.3: Matumizi yaliyofanyika bila ya hati za malipo shilingi 80,933,805.00. Ukaguzi umebaini kufanyika kwa matumizi ya shilingi 80,933,805.00 kutoka Hisabu ya amana Wizara ya Afya nambari 0406446000. Malipo ya fedha hizo ni tofauti kati ya matumizi ambayo vielelezo vyake vilipatikana kwa ukaguzi na malipo ambayo maelezo na vielelezo vyake havikupatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya Wizara
Kufuatia kuingiliana kwa ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kulipelekea nyaraka kuhitajika kwa mkaguzi mkuu wa ndani na kwa wakati huo huo kwa mkaguzi mkuu wa nje. Hali ilipelekea kushindwa kukamilika taarifa sahihi kwa mkaguzi wa nje. Kutokana na hali hiyo tumeweka taarifa sahihi za nyaraka ambazo hazikupatikana kwa mkaguzi wa nje. Nyaraka zote zipo tayari na naomba kuwasilisha kwa ukaguzi kama inavyoonekana kwenye jaduweli namba 84 la hoja.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati haikuridhika na hali ya kukosekana kwa vielelezo wakati wa Ukaguzi na hivyo haikuridhia kuvikagua.

HOJA NAMBA 5.10.1.4: Tofauti ya malipo ambayo hayakupatikana kwa ukaguzi shilingi 8,811,416.00.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa tofauti ya shilingi 8,811,416 kutoka hesabu ya Bohari Kuu ya madawa nambari 0404182000 ambazo matumizi yake hayakupatikana kwaukaguzi, tofauti hiyo ni kati ya jumla ya fedha iliyolipwa kwa mujibu wa hundi za malipo ambazo matumizi yake yalipatikana ka ukaguzi ,Kukosekana kwa maelezo pamoja na vielelezo vya fedha hizo ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za Umma pamoja na taratibu za malipo za Serikali. Maelezo ya malipo hayo yanaonekana katika jadwel.

Jadwel Nambari 85: Malipo ya matumizi ambayo hayakupatika na ukaguzi

| Nambari ya Hundi | Jumla ya Fedha iliyolipwa (Shs) | Jumla ya Fedha iliyokaguliwa (Shs) | Malipo yaliyokosekana vielelezo | aliyelipwa | maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 261 | 11,521,416 | 2,710,000 | 8,811,416 | Katibu Mkuu Wizara ya Afya | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya mafunzo mafupi ya dereva |

Majibu ya Wizara

Kiwango cha fedha kilichotajwa katika hoja hii,vielelezo vyake vipo na vipo tayari kwa kukaguliwa. Jaduweli nambari 85 linaonesha maelezo ya hoja husika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Wakati Mkaguzi alipokwenda hakupatiwa vielelezo Kamati ilishindwa kuhalalisha vielelezo hivo

HOJA NAMBA 5.10.1.5: Malipo yasiokuwa na mkataba ya shilingi 500,000,000.00. Katika mradi wa ujenzi wa Maabara kuu Binguni. Ukaguzi umebaini kufanyika kwa malipo ya shilingi 500,000,000.00 kwenda kwenye hesabu ya kampuni ya Serekali. Dosari

iliyobainika na ukaguzi ni kuwa malipo hayo yamefanyika bila ya kuwepo kwa mkataba baina ya Wizara ya Afya na kampuni ya ujenzi wa Serikali. Ukaguzi umeshindwa kujuwa hatua ya kazi ya ujenzi iliyokusudiwa kufanywa kwa mujibu wa fedha zilizolipwa.

Majibu ya Wizara

Kiasi cha fedha kilicholipwa katika hoja hii ni sahihi. Malipo yalifanyika bila ya mkataba kufuatia agizo la Mheshimiwa Rais wa Zanzibar wa awamu ya saba baada ya kuunda kamati kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Binguni. Malipo ya fedha hizi yaliombwa na iliokua Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara za SMZ kwa ajili ya kuwalipa wakala wa ujenzi huo. Malipo hayo yalifanyika kwa kufuata taratibu zote za kisheria za malipo na nyaraka halisi za malipo zinathibitisha uhalisia wa malipo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kutokana na Mkaguzi kukosa vielelezo wakati wa ukaguzi bila ya sababu za msingiKamati haikukubali kupokea vilelezo hivo.

Hoja Nmaba 5.10.1.6: Dosari katika taratibu za manunuzi shilingi 533,220,462.00.

Ukaguzi umebaini Wizara ya Afya imefanya malipo ya jumla ya shilingi 533,220,462.00 kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi na watoa huduma mbali mbali. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutopatiwa taratibu za manunuzi zilizo tumika katika kuwateuwa wazabuni waliopewa kazi na huduma hizo pamoja na kukosekana muhutasari wa vikao vya Bodi ya Zabuni ya Wizara ili kujirizisha iwapo manunuzi yaliyofanyika yamefuata taratibu na sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma namabri 11 mwaka 2016.

Majibu ya Wizara

Taratibu za manunuzi pamoja na vikao vya bodi vya wazabuni wa wizara walikaa kwa mujibu wa sheria na taratibu na vielelezo halisia vipo kwa ajili ya kukaguliwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kutokana na Mkaguzi kukosa vielelezo wakati wa ukaguzi bila ya sababu za msingiKamati haikukubali kupokea vilelezo hivo.

Hoja Namba 5.10.1.7: Kukosekana kwa uthibitisho wa matumizi ya shilingi 160,044,550.00

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wizara ya Afya imefanya matumizi ya jumla ya shilingi 160,044,550.00 kwa ajili ya huduma mbali mbali ya Wizara, ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa matumizi hayo kwa kukosekana hati ya malipo na vielelezo

vinavyothibitisha uhalali wa matumizi hayo.

**Majibu ya Wizara**

Malipo ya hoja hii yalifanyika kwa kufuata taratibu zote za malipo, naomba kuwasilisha nyaraka halali za malipo halisia yanayohusiana na hoja hii..

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kutokana na Mkaguzi kukosa vielelezo wakati wa ukaguzi bila ya sababu za msingiKamati haikukubali kupokea vilelezo hivo.

## 3.4 WIZARA YA AFYA PEMBA

**Hoja Nam. 5.10.1.8 Kutokulipwa kwa posho la mazingira hatarishi shilingi 5,175,000**

Katika ukaguzi ulipfanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 5,175,000 ni fedha za posho la mazingira magumu ambazo zimepaswa kulipwa kwa baadhi ya wafanyakazi waWizara ya Afya Pemba lakini posho hilo halijalipwa kwa wafanyakazi hao . Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni ya utumishi wa Umma ya Zanzibar ya mwaka 2014 kifungu nambari 87(1)

**Majibu ya Wizara ya Afya,Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto**

Ni utaratibu wa Wizara ya Afya kuwapatia posho la mazingira hatarishi wafanyakazi wake, hata hivyo kumekuwa na baadhi ya wafayakazi wa Wizara wakiwemo wale walioainishwa kwenye kiambatanishonamba 3 katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hawapati posho hili.

Hali hii ilijitokeza kutokana na maelekezo yaliyotolewa na Ofisi Kuu Unguja juu ya uingizwaji wa maposho hayo kwa awamu, kwa kada na kwa maeneo maalumu ya kazi ambapo waliohitajika kupatiwa posho hili ni wale tu ambao katika kazi zao za kawaida wanamfikia mgonjwa moja kwa moja. Hata hivyo wafanyakazi wote ambao hawajapatiwa posho hii wameshaorodheshwa wakiwemo walioko hospitali, vituo vya afya, ustawi na wale wanaofanyia kazi zao Wizarani

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

i. Kwa mujibu wa kanuni ya 87(1) ya Kanuzi za Utumishi wa Umm za mwaka 2014 mtumishi wa umma anaefanya kazi katika mazingira hatarishi atalazimika kulipwa posho la mazingira hatarishi kama muongozo utakavyotolewa kutoka Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma. Aidha, kanuni ya 87 (2) inafanunua kuwa kwa madhumuni ya ya kanuni ndogo (1) ya kanuni hii, watumishi watakaostahiki kulipwa posho la mazingira hatarishi miongoni mwao ni watumishi wa kada za afya, madaktari wa wanyama, wanaohusika na madawa ya mionzi, wanaowahudumia wazee, wachimbaji mafuta na gesi asilia ma watumishi wengine kama watakavyoainishwa katika matoleo ya Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma.

ii. Muongozo uliotolewa na Wizara ya Afya kuhusu posho ya mazingira hatarishi (ingawa ilielezwa kuwa haukupatikana wa maandishi) ni kwamba posho hiyo inastahiki kulipwa kwa wale watumishi wanaomuhudumia mgonjwa moja kwa moja tu. Hivyo, mtumishi hata kama ni wa kada wa afya iwapo hamfikii mgonjwa moja kwa moja hastahiki kulipwa posho hiyo ya mazingira hatarishi.

iii. Kwa mujibu wa viongozi wa Wizara ya Afya (Pemba), na kwa kuzingatia muongozo uliotolewa na Wizara, watumishi walioorodheshwa katika Kiamabatanisho Nambari 3 kinachohusiana na Hoja hii, hawakustahiki kulipwa posho ya mazingira hatarishi.

iv. Wakati wa ukaguzi Wizara ya Afya (Pemba) haikutoa uchambuzi sahihi kwa Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali juu ya watumishi waliostahiki kulipwa posho ya mazingira hatarishi na wale wasiostahiki kupata posho hiyo.

v. Pamoja na yote hayo, yapo manung'uniko ya wafanyakazi yanayodai kuwa wafanyakazi wengine zaidi waingizwe katika kulipwa posho hiyo..

Kamati ya PAC imeridhika na ufafanuzi uliotolewa na viongozi na watendaji wa Wizara ingawa ilitoa mapendekezo mbalimbali kwa viongozi na watendaji hao juu ya Hoja hii.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wakati wa Ukaguzi watendaji wa Wizara ya Afya (Pemba) watoe mashirikiano ya kutosha kwa Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti kwa kutoa ufafanuzi ulio sahihi unaohusu miongozo na maelekezo yanayotolewa katika Wizara hiyo.
2. Watendaji wa Wizara ya Afya (Pemba) watumie utaratobu mzuri wa kutoa na kufuatilia malalamiko yao katika sehemu inayostahili.

3. Kamati ya PAC ilimuomaba Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Junsia na Watoto kufuatilia katika Mamlaka zinzostahiki hali ya malalamiko ya wafanyakazi juu ya posho ya mazingira hatarishi ili kuepusha manung'uniko ya wafanyakazi hao juu ya posho hiyo.

Hoja namba. 5.10.1.9 Malipo yenye shaka kwa madaktari shilingi 117,245,000

Ukaguzi umebaini kuwa kuna malipo 117,245,000 ambayo yamelipwa kwa ajili ya ya wito wa madaktari lakini baadhi ya madaktari hao hawakuwepo kazini katika kipindi hicho cha malipo bali walikuwa wapo masomoni na baadhi ya wengine walipohojiwa walikataa kukiri kupokea fedha hizo hivyo kupelekea malipo hayo kuwa na shaka ya ulipwaji wake.

Kufanya malipo kwa wafanyakazi wasiostahiki ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2016

Mchanganuo wa madaktari hao ni kama inavyoonekana katika majadweli lifuatalo.

Jadweli nambri 89: madaktari waliopo masomoni

| NAMBA | JINA LA MFANYAKAZI | CHUO ANACHO SOMA | MUDAWA MASOMO | JULY, 2019 | OCT ,2019 | NOV ,2019 | DEC ,2019 | JAN,20<br>0 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ALI MOH'D ALI | UDOM | MAY 2018 -2020 | 200,000 | 200,000<br>200,000 | 200,000 | 230,000<br>230,000 | 230,00<br>230,00 |
| 2 | MARYAM ABDALLAH SALUM | CUBA | OCT 2018-2022 | 200,000 | 200,000<br>200,000 | 200,000 | 200,000<br>200,000 | 200,00<br>200,00 |
| 3 | SALMA ALLI HAMAD | EGYPT | AUG 2018 -2020 | 240,000 | 240,000<br>240,000 | 240,000 | 130,000<br>190,000 | 190,00<br>190,00 |
| 4 | ALI OTHMAN SALIM | UHAMISHO KIKAZI | 21/9/2018 | 180,000 | 180,000<br>180,000 | 180,000 | 180,000<br>180,000 | 180,00<br>180,00 |
| 5 | OTHMAN KHAMIS OTHMAN | FUNDI BIOMEDICAL | - | 270,000 | 270,000<br>270,000 | 270,000 | 180,000<br>180,000 | 180,00<br>180,00 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | HAROUB ABDALLAH ALI | ECUREI | APRIL 2019-2023 | 190,000 | 190,000<br>190,000 | 190,000 | 190,000<br>190,000 | 190,00<br>190,00 |
| 7 | FATMA SAID MOHAMMED | CATHOLIC UNIVERSITY | NOV 2020 -2023 | 270,000 | 170,000<br>170,000 | 225,000 | 135,000<br>135,000 | 135,00<br>135,00 |
| 8 | HIDAYA ABDALLAH SAID | CHINA | NOV 2019 -2022 | 285,000 | 285,000<br>285,000 | 285,000 | 285,000<br>285,000 | 285,00<br>285,00 |
| 9 | HAJRA ALI HAMAD | CHINA | NOV 2019 -2023 | 190,000 | 190,000<br>190,000 | 190,000 | 190,000<br>190,000 | 190,00<br>190,00 |
| 10 | MOH'D MUSSA AHMAD | CUBA | SEPT 2018-2022 | 190,000 | 190,000<br>190,000 | 190,000 | 190,000<br>190,000 | 190,00<br>190,00 |
| 11 | KHALFAN ALI MOH'D | MZUMBE | NOV 2019 -2021 | 220,000 | 220,000<br>220,000 | 220,000 | 120,000<br>160,000 | 160,00<br>210,00 |
| | JUMLA | | 18,525,000 | 2,435,000 | 4,870,000 | 2,390,000 | 4,160,000 | 4,670,0<br>0 |

Majibu ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamiii,Wazee, Jinsia na Watoto

Kwa kawaida hakuna zuio la kufanya malipo yoyote baada ya kukamilika taratibu za kisheria (supporting documents) juu ya malipo hayo. Katika utekelezaji wa hili haizingatii kuwa mfanyakazi huyo yupo kazini, masomoni, nyumbani, au hata kama amefariki kinachozingatiwa ni kupatikana kwa vielelezo vinavyoruhusu kufanyika kwa malipo hayo.

Kuhusu hoja ya kuwa, kuna watu ambao wamehojiwa na kukataa kukiri kupokea fedha hizo ni jambo linalowezekana kutokea kwani tatizo kubwa lililokuwa linaikabili Wizara hii ni ufinyu wa fedha za malipo ya miito ya madaktari (call allowance). Jambo hili lilipelekea madai ya posho za miito kuwa mengi na ya muda mrefu. Katika hali hii ni wazi kuwa mfanyakazi anaweza kusema hajapokea malipo yoyote kutokana na kuwa bado anadai

madai hayo kwa muda mrefu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati baada ya kupata maelezo kutoka kwa watendaji wa Wizara ya Afya (Pemba) na kupitia vielelezo mbali mbali vinavyohusiana na Hoja hii zikiwemo hati za malipo, barua kadhaa zikiwemo za ruhusa za kwenda masomoni kwa baadhi ya madaktari, imebaini yafuatayo:-

i. Kuwepo dalili za kufanyika kwa udanganyifu katika orodha ya majina ya madaktari waliorodhshwa kuwa wameingia kazini katika miezi mbali mbali ya mwaka 2019 na kufanyika malipo kwa ajili ya wito wa madaktari (call allowance) kupitia majina ya madaktari hao katika mwaka huo wa 2019 ambapo baadhi ya madaktari hao walikwishapewa ruhusa ya kwenda masomoni tangu mwaka 2018. Ni dhahiri kuwa kwa mujibu wa barua zao za ruhusa ya kwenda masomoni madakatari hao hawakustahiki kuwemo katika orodha ya madaktari walioingia kazini katika mwaka wa 2019 na hivyo hawakustahiki kuwemo katika orodha ya malioo hayo ya " calls".. Majina ya Madaktari hao kama yanavyoonekana katika Hoja ya Mdhibti, wote ni madkatari wa Hospitali ya Mkoani (Pemba) (Hati Namba H01PV1900000891ya tarehe 8 Januari 2020 na barua ya tarehe 6/5/2019, pamoja na Hari ya malipo yenye nambari H01 PV1900000b59 ya tarehe 31 Disemba, 2019 na barua tare 8/12/2019 zinahusika

ii. Kutofautiana kwa saini zinazomhusu mtu huyo huyo mmoja katika orodha za malipo. (jina la mtu huyo huyo mmoja kuonekana kupokea fedha na kutia saini tofauti katika orodha mbalimbali za malipo). Hali hii imebainika katika majina ya madakatari walioko masomoni pamoja na madaktari wengine.wa Hospiatali ya Mkoani na Chake Chake.

iii. Kuwepo kwa jina la daktari mmoja (Ali Othman Salum) ambae amepewa uhamisho kutoka Hospitali ya Mkoani (Pemba) kwenda kuendelea na kazi katika Hospitali ya Kivunge (Unguja) tangu tarehe 21.9/2018 lakini bado jina lake lilionekana katika orodha ya majina ya madaktari waliuongia kazini na kulipwa malipo ya calls katika miezi mbalimbali ya mwaka 2019. (Barua ya Uhamisho yenye nambari ya kumbukumbu AA/ACA/A.10289/C ya tarehe 21/9/2018 inahusika) Kwa mujibu wa barua hiyo uhamisho huo aliuomba mwenyewe na kwa hali hiyo hakuwepo katika Hospitali ya Mkoani katika mwaka 2019.

iv. Ingawa malipo hayo yanaonekana kuchelewa kulipwa kutegemea na hali ya uingizwaji wa matumizi mengineyo (OC), mazingira ya udanganyifu yaliyobainika,

yanaashiria kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha hizo kwa kuwa malipo hayo yanannekana kuchukuliwa na watu wasio halali na wasiostahiki kulipwa malipo hayo.

Hovyo, Kamati ya PAC imethibitisha Hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kuwepo kwa malipo yenye shaka kwa madaktari wa Hospitali za Pemba shilingi 117,245,000 kulikotokana na udanganyifu uliobainika ambao unaashiria matumizi mabaya ya fedha hizo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee Jinsia na Watoto na Serikali kwa Ujumla kupitia vyombo vyake vinavyohusika iwachukulie hatua zinastahiki wale wote waliohusika kwa niia moja au nyengine na udanganyifu uliofanyika ambao umepelekea matumizi mabaya ya Shilingi 117,245,000 zilizotolewa kwa ajili ya malipo ya wito wa madaktari (Calls) kwa hospitali za Pemba kwa mwaka wa fedha 2019/2020

Hoja namba. 5.10.1.10Kukosekana kwa uthibitisho wa mapokezi ya dawa – Hospitali ya Chake Chake

Ukaguzi umebaini kuwa kuna dawa za aina mbalimbali ambazo zimetoka bohari kuu na kupelekwa katika ghalala kuhifadhia dawa katika hospitali ya chake chake lakini ukaguzi haukuweza kuthibitisha mapokezi na matumizi ya dawa hizo.

Kutokupokelewa ka dawa hizo ni kwenda kinyume na sharia namba 11 ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma za Zanzibar ya mwaka 2016. Orodha ya dawa ni kama inavyoonekana katika

Majibu ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, jinsia na Watoto.

Bohari Kuu ya dawa ina jukumu la msingi la kupokea, kuhifadhi na kusambaza dawa katika hospitali na vituo vya Afya vya Serikali. Aidha, dawa zilizotajwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikaliya 2019/2020 kupitia kiambatisho namba 7 ( cha Ripoti ya Mdhibiti) kuwa hazikuthibitishwa mapokezi na matumzi yake katika hospitali ya Chake Chake, dawa hizi zilitoka bohari kuu ya dawa Unguja kupitia bohari kuu ya dawa Pemba na hatimae kupelekwa na kupokelewa katika Ghala (Store) ya kuhifadhia dawa ya hospitali ya Chake Chake kama ilivyo kawaida.

Aidha, upokelewaji wa dawa hizi unathibitishwa na nyaraka za usambazaji (invoice) na nyaraka za upokeaji wa dawa (*bim cards)*

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imezikagua “invoces” na “bim cards”zinazohusika na mapokezi ya dawa hizo (za mwezi wa Septemba na Novemba 2019) ambapo pamoja na kurdhika nazo na kuthibitisha kupokelewa na kurekodiwa kwa dawa hizo katika ghala ya dawa ya Hospitali ya Chake Chake, lakini imebaini yafuatayo:-

1. Kutofautiana kwa majibu ya Wizara baina ya majibu ya Hoja hii aliyojibiwa Mdhibiti na yale iliyojibiwa Kamati ya PAC ambapo kwa mujibu wa majibu aliyojibiwa Mdhibiti (kupitia barua ya tarehe 30/4/2021 yenye nambari ya kumbukumbu AD.31/32/01/69) Wizara ilisema kuwa changamoto ya kutorikodiwa kwa dawa katika daftari (kadi) la ghala ya dawa ya Hospitali ya Chake Chake ilichangiwa na tatizo la uhaba wa wafanyakazi wenye weledi kwa muda mrefu, ingawa hatua ilichukuliwa baadae ya kuweka Mfamasia mwenye uwezo.

2. Kufutwa futwa kwa baadhi ya bim cards ambazo miongoni mwao zilionekana kufutwa futwa katika maeneo zaidi ya matatu kwa kadi moja jambo ambalo linaweza kuleta shaka juu ya uwezo na umakini wa watunza ghala ya dawa ya Hospitali hiyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Wizara iwe makini inapotoa taarifa zake kwa kuwa na msimamo mmoja ulio sahihi pale inapowasilisha taarifa zake katika vyombo vya uchunguzi ikiwemo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ili kujiepusha kujiingiza katika makosa ya kutoa taarifa zisizo sahihi kwa vyombo hivyo.

ii. Watunza ghala ya dawa katika Hospitali ya Chake Chake wajiepushe na kufuta mara kwa mara katika taarifa za utunzaji wa kumbukumbu za dawa kwa kuongeza umakin wakati uingizaji wa taarifa hizo ili kuepuka kutiliwa shaka uwekaji wa kumbukumbu za dawa katika ghala ya Hospitali hiyo.

iii. Wizara ya Afya iandae utaratibu wa kuongeza wataalamu hasa katika ghala za dawa ili uwekaji wa kumbkumbu za upokeaji na utoaji wa dawa katika ghala hizo uwe wa uhakika zaidi..

iv. Wizara iandae utaratibu wa kuongeza wataalamu hasa katika ghala za dawa ili kuongeza ufanisi katika uwekaji wa kumbukumbu za taarifa za dawa katika ghala husika

Hoja nam. 5.10.1.11 Bakaa ya fedha ambazo hazikutumika Shilingi 36,549,253

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 36,549,253 ni ni bakaa ya fedha

zilizobaki mwisho wamwaka 2019/2020 lakini fedha hizo hazikutumika na hazikurejeshwa katika mfuko mkuu wa serikali

Aidha,ukaguzi uliofanyika umebaini jumla ya shilingi 9,647,361,664 kutoka mfuko mkuu wa serikali hadi kufikia 30 juni,2020 fedha iliyotumika ni jumla ya shilingi 9,610,812,411 na kupelekea kuwepo kwa bakaa ya shilingi 36,549,253 ambazo hazikurejeshwa kwenye mfuko mkuu wa serikali kwa mujibu wa sheria.

Kufanyahivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 52(2) cha sheria ya usimamizi wa fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2016

Majibu ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto

Kwa kawaida kila ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha kunakuwa na ufungaji wa hesabu za Serikali ambapo kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu hufungwa kila ifikapo mwishoni mwa mwezi wa Juni katika mwaka husika.

Kwa mujibu wa utaratibu, hesabu za fedha za matumizi ya kawaida (Recurrent) zinatakiwa kutokuwa na bakaa yoyote kila ifikapo mwishoni mwa mwaka wa fedha.

Wizara inakiri kuwa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2019/2020 kulikuwa na bakaa ya shilingi milioni ishirini laki nane sitini na tatu elfu mia moja sitini na tisa (20,863,169/=) na sio shilingi milioni thalathini na sita laki tano arubaini na tisa elfu mia mbili hamsini na tatu (36,549,253/=) kama zilivyoelezwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu zaSerikali.

Wizara ya Afya kupitia muhasibu wake ilifuatilia na kugundua kuwepo kwa fedha ambazo kwa Wizara haikuwa na uwezo tena wa kuzifanyia matumizi kwani vitabu vilishafungwa kabla ya tarehe 30/6/2020. Aidha, kwa wakati huo hesabu hiyo ilikuwa chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ambao waliamua kuzihaulisha na kuzirejesha katika Mfuko Mkuu waSerikali.

Kurejeshwa kwa fedha hizo katika Mfuko Mkuu wa Serikali, kulipelekea kuondoa dhima kwa upande wa Wizara hii na kuwepo kwa uwiano baina ya kitabu cha mtandao (system) cha Wizara ya Fedha na Mipango na kitabu cha hesabuhiyo cha Wizara ya Afya ambavyo vyote vilikuwa na bakaa ya sufuri (Nill balance).

Pamoja na maelezo hayo, naambatanisha kitabu (Cash book) cha mtandao cha Wizara ya Fedha na Mipango ambacho kinaonesha fedha zilizohaulishwa na kupelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali tarehe 30/6/2020 kuwa ni shilingi 20,863,169 na si vyenginevyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilielezwa kuwa Wizara ya Afya ilikuwa haijui kama kulikuwa kuna bakaa ya shilingi milioni 20,863,169 na pia ilikuwa haijui kama kulikuwa na bakaa yoyote kwa sababu iliyoelezwa ya kuwepo kwa hitilafu ya kimfumo kwa upande wa Wizara ya Afya kwa wakati huo ingawa kwa upande wa Wizara ya Fedha iliiona bakaa hiyo na ilikuwa inatafuta Wizara gani iliyokuwa na bakaa hiyo.

Hata hivyo, kutokana na maelezo ya Wizara, Kamati ya PAC imegundua kuwepo kwa uwekaji na ufuatailiaji usioridhisha wa kumbukumbu za kifedha za Wizara, jambo ambalo lilichangia Watendaji wa masuala ya fedha wa Wiazra hiyo kutokuwa na taarifa juu ya kuwepo na kubakia kwa fedha katika Hesabu na Taarifa za fedha za Wizara hiyo..Kutokufahamu kumbukumbu za kifedha ni kwenda kinyume na kifungu cha 34 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha Namba 12 ya mwaka 2016 kinachomtaka Afisa Mhasibu kuweka kumbukumbu zote na sahihi zinzohusiana na masuala ya fedha za Idara, taasisi za biashara au taasisi za kikatiba kulingana na masharti na viwango.

Kwa kupitia “Cash book” ya mfumo wa mtandao iliyowasilishwa, Kamati ilithibitisha kuwa kwa kipindi hicho Wizara ya Afya ilikuwa na bakaa ya shilingi 20,863,169 ambazo zilikuwa ni fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC)

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wakati wa Ukaguzi, Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto (Pemba) itoe ushirikiano wa kutosha kwa Wakaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.ikiwa ni pamoja na kutoa ufafanuzi wa kutosha kwa wakaguzi katika wakati unaostahiki.
2. Mhasibu wa Wizara ya Afya (Pemba) pamoja na wahasibu wa Wizara na Taasisi nyengine za Serikali kuweka kumbukiumbu vizuri na wafuatatilie kwa karibu zaidi taarifa za kifedha za Wizara na Taasisi zao ikiwa ni pamoja ni kufanya usuluhishi wa kibenki (bank reconciliation) mara kwa mara ili kuwa na taarifa sahihi za kifedha za Wizara na Taasisi zao kila wakati.

## KAMISHENI YA ARDHI PEMBA

### Majibu ya Kamisheni ya Ardahi Pemba

Kama ilivyoelezwa madeni hayo yanatokana na taasisiza Serikali, kazi hizo zilifanyika kwa kuzingatia uharaka uliohitajika kwenye utekelezaji wa miradi kwa manufaa ya wananchi na kutoa ushirikiano wa taasisi za Kiserikali katika kuwahudumia wananchi. Aidha, waliahidi wangefanya malipo ya gharama hizo haraka. Kazi hizo zilifanyika kati ya kipindi cha 2015 hadi 2019. Kwa bahati mbaya ulipita muda mrefu bila ya taasisi hizo kufanya

malipo ya aina yeyote pamoja na kazi hiyo kufanyika. Kutokana na kumbukumbu zetu deni halisi lilikuwa Shilingi Milioninane, laki saba na elfu themanini na nane (8,788,000/=) badala ya Milioni tisa, laki moja na elfu thelathini na nane (9,138,000/=) kama lilivyobainishwa katika hoja.

Kamisheni ya Ardhi ofisi ya Pemba iliripoti madeni hayo kwa Bodi ya Kamisheni ya Ardhi pamoja na Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/2020. Ili kulipwa madeni hayo tulishauriwa kuziandikia barua za ukumbusho taasisi hizo ambapo hatua hiyo ilifanyika. Kwa bahati mbaya sana hadi sasa ni Shirika la Umeme (ZECO) pekee waliolipa deni lao. Aidha, zipo baadhi ya taasisi zilijibu kwa kuahidi kulipa madeni yao lakini bado nyengine hazijalipa. Hadi sasa deni halisi lililobaki ni shilingi Milioni saba, laki tisa na elfu themanini na nane (7,988,000/=)

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji juu ya deni lililopaswa kuandikwa katika Ripoti ya ukaguzi baina ya shilingi 8,788,000 na shilingi 9138,000 zilizoaininshwa katika Hoja na kubainika kuwa deni lililopaswa kuainishwa ni shilingi 8,788,000 ambapo orodha ya madeni iliyoainishwa katika Ripoti ya Ukaguzi ilirekodiwa kimakosa kwa kuyawaka madeni mawili tofauti ya Baraza la Mji Chake Chake kwenye deni nambari 1 na deni nambari 3 wakati ambapo deni namba 3 (shilingi 350,000) tayari limejumuishwa katka deni namba 1 la Baraza hilo la Mji Chake Chake ambalo ni shilingi shilingi 2,100,000. Kwa ujumla Baraza la Mji Chake Chake pekee linadaiwa jumla ya shilingi 3,100,000 kama inavyoonekana katika deni nambari 1 na nambari 2 kwenye Hoja hii.

Kamati ilikagua barua mbali mbali za ukumbusho wa madeni hayo kwa taasisi tofauti kama hatua zilizochukuliwa na Kamisheni ya Ardhi Pemba kuyafuatalia madeni hayo. Miongoni mwa barua zilizokaguliwa na Kamati ya PAC ni barua aliyopelekewa Mkurugenzi wa Baraza la Mji Chake Chake ya tarehe 2/12/2019 yenye nambari ya kumbukumbu WANMN/P/KA/UR/CH.10/VOL.111/88 inayokumbushia deni la gharama za upimaji wa maeneo ya Baraza la Mji Chake shilingi 3,100,000.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kwa kuwa taasisi moja tu (ZECO) ndiyo iliyolipa deni kati ya taasisi 11 zinazodaiwa gharama za upimaji, Kamati ya PAC imeishauri Kamisheni ya Ardhi Pemba kuongeza nguvu za kuyafuatilia madeni yaliyobakia ili kasi ya kulipwa kwa madeni hayo iwe kubwa zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

2. Ni vyema katika barua zenyewe za ukumbusho wa madeni zikaainishwa kiwango

cha deni ambacho Kamisheni inadai kwa kila taasisi pamoja na kujiwekekea utaratibu wa kuyafuatilia madeni hayo kila baada ya kipindi fulani

### 3.5 FUNGU P 01 WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI (WIZARA YA UJENZI MAWASILIANO NA UCHUKUZI)

Taarifa ya mapato

Wizara yaujenzi mawasiliano na usafirishaji ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,387,008,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020

Hadi kufikia 30 juni, 2020 wizara ilikusanya jumlaya shilingi 2,509,124,000 sawa na asilimia 74 ya makadirio.

Majibu ya Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi

a. Vyanzo vya Mapato.

Wizara kupitia Idara ya Usafiri na Leseni ambayo sasa hivi inaitwa Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani inakusanya mapato yake kupitia vyanzo mbalimbali ambavyo ni: Mapato yatokanayo na ukaguzi wa vyombo vya moto, magari ya biashara, mitihani ya madereva, beji za utingo na dereva, lena, vibali, ruhusa za njia na usafirishaji na mapato yanayotokana na usajili na leseni za vyuo vya udereva.

b. Makusanyo ya Mapato Kupitia Vyanzo Mbalimbali. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Idara ya Usafiri na Leseni kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 3,387,008,000 na hadi kufikia Juni, 2020 jumla ya TZS 2,509,124,000 zilikusanywa sawa na asilimia 74 ya makadirio ya mwaka kwa Unguja na Pemba. Ufafanuzi wa mapato hayo unaonekana katika jadweli lifuatalo:-

: Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa Kila Chanzo cha Mapato (000,000).

| S/NO. | Chanzo cha Mapato | Makadirio ya Mwaka 2019/2020 | Makusanyo Halisi kwa mwaka 2019/2020 | Asilimia | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ukaguzi ya Vyombo vya Moto | 1,147.0 | 1,051.2 | 91.6 | Kushuka kwa mapato kumesababishwa kupunguwa kwa vyombo |

| S/NO. | Chanzo cha Mapato | Makadirio ya Mwaka 2019/2020 | Makusanyo Halisi kwa mwaka 2019/2020 | Asilimia | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | vilivyoletwa kufanyiwa ukaguzi kutokana na maradhi ya CORONA. |
| 2 | Leseni kwa Magari ya Biashara | 865.9 | 464.0 | 53.5 | Vyombo vilivyoomba kufanya biashara vilipunguwa kutokana na Janga la COVID 19 na kusababisha wamiliki wa vyombo kushindwa kuingiza vyombo vyao kwenye biashara (Private hire na Staff Buss). Vyombo vinavyotoa huduma yenye mnasaba na utalii vilishindwa kutoa huduma. |
| 3 | Mapato ya Lena | 449.2 | 232.1 | 51.6 | Kupunguwa kwa Mapato kumesababishwa kupunguwa kwa idadi ya wanafunzi waliosajiliwa katika vyuo vya udereva. |
| 4 | Mapato ya Beji (Dereva na Konda) | 156.2 | 111.6 | 71.4 | Upungufu wa mapato umesababishwa na kupunguwa kwa beji zilizoombwa kutokana na huduma hii kutolewa na taasisi mbili tofauti. |
| 5 | Vibali | 67.1 | 27.0 | 40.0 | Vibali zilivyombwa vilipunguwa kutokana na kuibuka kwa Janga la Corona na wageni kushindwa kuja nchini. |
| 6 | Kipande cha Njia | 54.6 | 149.8 | 274.0 | Mapato yameongezeka kutokana na wamiliki wa magari kubadilisha ruti mara kwa mara na hatimae |

| S/NO. | Chanzo cha Mapato | Makadirio ya Mwaka 2019/2020 | Makusanyo Halisi kwa mwaka 2019/2020 | Asilimia | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kuongezeka kwa idadi ya ruti zinazotolewa. |
| 7 | Usajili na Leseni za Vyuo vya Udereva | 18.3 | 4.0 | 21.7 | Makisio yalikuwa makubwa kuliko uhalisia wa Idadi ya vyuo vilivyopo. |
| 8 | Mitihani ya Madereva (Nadharia na Vitendo) | 628.7 | 469.4 | 74.6 | Idadi ya wanafunzi waliofanyiwa mitihani ilipunguwa kutokana na kupunguwa kwa wanafunzi waliosajiliwa katika vyuo vya udereva |
| | JUMLA | 3,387 | 2,509 | 74 | |

1. TAARIFA YA MATUMIZI

Taarifa ya matumizi

Wizara ya ujenzi, mawasiliano na usafirishaji ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 10,137,450,000 kwa kazi za matumizi ya kawaida, shilingi 8,149,227,011 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 80 ya makadirio, shilingi 73,706,531,624 zimetumika kwa kazi za maendeleo sawa naasilimia 84 makadirio na shilingi 192,125,000 ikiwa ni ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya wizara ikiwa sawa na asilimi 59 ya mkadirio

MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mawaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia Jumla ya TZS 10,464,450,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo TZS 6,158,850,000 ni Mshahara, TZS 3,978,600,000 ni matumizi mengineyo (OC) ya Wizara na TZS 327,000,000 ni ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara (Bodi ya Usafiri Barabarani).
Hadi kufikia mwezi wa Juni 2020, kiasi cha TZS 8,341,352,011 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida (Matumizi mengineyo na Ruzuku) sawa na asilimia 79.7 ya makadirio. Ufafanuzi wa fedha hizo zinaonekana katika Jadweli lifuatalo: -

| S/No. | Maelezo | Makadirio ya Matumizi ya Kawaida 2019/2020 (000,000) | Matumizi Halisi kwa Mwaka 2019 /2020 (000,000) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mishahara | 6,159 | 6,124 | 100 |
| 2 | Matumizi Mengineyo (OC) | 3,979 | 2,026 | 51 |
| 3 | Ruzuku | 327 | 192 | 59 |
| | Jumla Kuu | 10,464 | 8,341 | 79.7 |

Kwa kipindi hicho, Wizara ilipata asilimia 51 ya bajeti yake ya matumizi mengineyo (OC) hali hii ilipelekea kukosekana kwa mambo muhimu ya msingi ikiwemo vifaa mbali mbali vya ofisi ambavyo ni muhimu katika kurahisisha utoaji wa huduma mbali mbali za ofisi. Wizara ilitumia fedha zilizopatikana kwa ajili ya kukidhi mahitaji muhimu ya ofisi kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake licha ya changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika kipindi hicho kutokana na uhaba wa fedha zilizopatikana. Aidha, kutokana na hali ilivyokuwa katika kipindi hicho, Wizara ililazimika kukopa baadhi ya vifaa kwa taasisi (Suppliers) ikiwemo Wakala wa Uchapaji Zanzibar ili iweze kutoa huduma kwa jamii.

MATUMIZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mawaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia Jumla ya TZS 115,594,600,000 kwa kazi za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo TZS 88,130,000,000 ni fedha kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na TZS 27,464,600,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Juni 2020, kiasi cha TZS 91,012,836,552/= zimeingizwa na kutumika kwa ajili miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 78.7 . Kati ya fedha hizo, TZS 73,706,531,624 ni zimetolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na TZS 17,306,304,928 zimetolewa na Washirika wa maendeleo.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ilikuwa na miradi 10 ambayo imeelezwa katika Jadweli linalotoa ufafanuzi wa bajeti na matumizi halisi ya fedha zilizotumika katika kipindi hicho.

Jadweli 3A: Mgawanyo wa Fedha kwa kila Mradi kwa Mwaka wa fedha 2019/2020

(Mchango wa Serikali).

| S/NO. | Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2019/2020 | Makadirio ya Bajeti 2019/2020 (000,000) | Matumizi Halisi 2019 /2020 (000,000) | Asilimia ya Fedha. |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Barabara ya Ole – Kengeja km 35 kwa kiwango cha lami | 9,000.0 | 2,550.0 | 28.3 |
| 2 | Ujenzi wa Barabara ya Koani – Jumbi km 6.3 kwa kiwango cha lami | 2,000.0 | 615.0 | 30.7 |
| 3 | Ujenzi wa Barabara Wete – Chake km 22.1 kwa kiwango cha lami | 1,000.0 | | 0.0 |
| 4 | Ujenzi wa Barabara ya Bububu – Mahonda – Mkokotoni km 31, Pale – Kiongele km 4.6, Matemwe – Muyuni km 7.5 na Barabara ya Fuoni – Kombeni km 8.5 kwa kiwango cha lami. | 4,000.0 | 2,882.5 | 72.1 |
| 5 | Upembuzi Yakinifu wa Barabara ya Tunguu – Makunduchi km 48, Chake Chake – Mkoani km 43.5 na Barabara ya Fumba – Kisauni km 12. | 2,800.0 | 2,673.4 | 95.5 |
| 6 | Ujenzi wa Barabara ya Jozani – Charawe – Ukongoroni km 23km | 3,000.0 | 1,445.2 | 48.2 |
| 7 | Upembuzi Yakinifu wa Barabara ya Kitogani – Paje, Mahonda – Donge, Kinyasini – Kiwengwa, Dunga –Chwaka, Muyuni – Nungwi na Makunduchi - Kizimkazi. | 400.0 | 10.5 | 2.6 |
| 8 | Ujenzi wa Jengo jipya la abiria (Terminal III AAKIA) | 61,030.0 | 61,470.0 | 100.7 |
| 9 | Upembuzi Yakinifu wa Bandari ya Mpiga Duri | 3,000.0 | | 0.0 |
| 10 | Ununuzi wa boti ndogo tano za abiria kwa maeneo ya Visiwa (land Craft) | 2,100.0 | 2,059.9 | 98.1 |

| S/NO. | Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2019/2020 | Makadirio ya Bajeti 2019/2020 (000,000) | Matumizi Halisi 2019 /2020 (000,000) | Asilimia ya Fedha. |
|---|---|---|---|---|
| | JUMLA KUU | 88,330.0 | 73,706.5 | 83.4 |

Mgawanyo wa Fedha kwa kila Mradi kwa Mwaka wa fedha 2019/2020 (Mchango wa Washirika wa Maendeleo).

| S/NO. | Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2019/2020 | Makadirio ya Bajeti 2019/2020 (000,000) | Matumizi Halisi 2019/2020 (000,000) | Asimia ya Fedha. |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Barabara ya Ole – Kengeja km 35 kwa kiwango cha lami | 9,000.0 | 6,842.8 | 76.0 |
| 2 | Ujenzi wa Barabara ya Koani – Jumbi km 6.3 kwa kiwango cha lami | 6,571.0 | | |
| 3 | Ujenzi wa Barabara ya Bububu – Mahonda – Mkokotoni km 31, Pale – Kiongele km 4.6, Matemwe – Muyuni km 7.5 na Barabara ya Fuoni – Kombeni km 8.5. kwa kiwango cha lami. | 11,893.6 | 10,463.5 | 87.9 |
| | JUMLA KUU | 27,464.6 | 17,306.3 | 63.0 |

Hoja Namba 1.12.1.1Kutokuonyeshwa kwa Mapato ya Karakana Kuu katika taarifa za hesabu Shilingi 13,795,555

Jumla ya shilingi 13,795,555 ikiwa ni fedha za mapato zilizokusanywa katika karakana kuu ya serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 ukaguzi umebaini kwamba fedha za makusanyo hayo hazikuripotiwa na kuonyeshwa katika taarifa za hesabu mwisho wa mwaka husika.

Kutokuingizwa na kuonyeshwa mapato hayo katika taarifa za hesabu za mwisho wa

mwaka kunapelekea taarifa ya mapato kutokuonesha sura halisi na sahihi,kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo

Jadweli nambari 97: Mapato yaliyokuwa hayakuingiwa kwenye taarifa ya hesabu

| Namba | Mwezi | jumla ya fedha zilizokusanywa (shs) |
|---|---|---|
| 1 | julai | 470,000 |
| 2 | Agosti | 770,000 |
| 3 | Septemb a | 1,040,000 |
| 4 | Oktoba | 1,680,000 |
| 5 | Novemb a | 435,000 |
| 6 | Disemba | 1,575,000 |
| 7 | Januari | 5,075,555 |
| 8 | Febuari | 635,000 |
| 9 | Machi | 1,075,000 |
| 10 | April | 700,000 |
| 11 | mei | 100,000 |
| 12 | juni | 240,000 |
| Jumla | | 13,795,555 |

Majibu ya Wizara

Wakala wa karakana kuu inakadiriwa kukusanya mapato yatokanayo na utengenezaji wa gari na utoaji wa huduma nyengine bila ya kuyaingiza kama ni mapato kutokana taratibu za uendeshaji wa karakana hiyo.  Karakana kuu hutoa huduma na kununua vifaa hivyo vya utengenezaji magari kwa kutumia fedha ambazo hulipwa na wateja wake. kutokana na

upatikanaji mdogo wa fedha za kuendesha ofisi,  Karakana hutumia hizo fedha kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi lakini hivi sasa tupo katika majadiliano na  Ofisi ya Rais Fedha  na Mipango ili sehemu ya makusanyo hayo iachiwe kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufanyia kazi.
Aidha, Wizara haikuweka fedha za karakana kuu kama ni mapato kwenye hesabu ya mwisho wa mwaka kwa sababu fedha hizo hazikuwemo katika bajeti ya makusanyo ya mapato kwa Wizara, hata kwenye makadirio ya mapato kutoka Wizara ya Fedha haikuwemo. Hivyo ingekuwa siyo sahihi kuyakusanya na kuyaingiza Mfuko Mkuu wa Serikali kwa sababu hakuna kifungu (kasma) ya kurikodi mapato hayo kwenye kitabu cha bajeti kilichoainishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa mapato ya karakana kuu hayakuingizwa katika taarifa ya fedha ya mwisho wa mwaka Idara ya karakana kuu imeeundwa mwaka 2020 kabla ya hapo ilikuwa ni kitengo ndani ya Idara ya Usafiri na Leseni fedha za karakana Kuu bado zipo katika Account ya Idara hiyo, Aidha kwa mujibu wa legal notice ya Wakala wa Karakana kuu ya Serikali inaitaka imuandikie Waziriwa Fedha ili aweze kuruhusu kiasicha mapato Karakana Kuu (Retention).Mapato hayo yanakuwa ya services charge na fedha za vifaa vya magari.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Serikali ikae pamoja ili kutatua suala la mapato ya wakala karakana kuu na pia Wizara juhudi za kuanzisha sheria ya karakana kuu ili iwe na uwezo mkubwa zaidi ya kufanya kazi na kuengeza mapato ya Serikali.

Hoja Namba 5.12.1.2. Tasisi za Serikali ambazo zinadaiwa na Karakana Kuu ya Zanzibar Shilingi 69,777,500.

Katika ukaguzi ulofanyika ,kumebainika kuwepokwa madeni ya muda mrefu ya shilingi 69,777,500 ambayo yanatokanana huduma mbali mbali zinazotolewa na karakana kuu kwa Taasisi za serikali,pamoja na jitihada zinazochukuliwa ili kuhakikisha madeni hayo yanalipwa kwa wakati ukaguzi umebaini jitihada hizo haziendani na kasiya ulipaji wa madeni hayo,jambo ambalo linapelekea uwepo wa madeni sugu amabayo hayataweza kulipika na kupelekea kukibebesha mzigo mkubwa serikali,

Ukaguzi unashauri uongozi wa wizara kupitia karakana kuu ya Zanzibar kuchukua jitihada za makusudi na kuhakikisha madeni hayo yanalipwa kwa wakati ikiwemo kuweka tozo maalumu kwa wale watakaoshindwa kulipwa madeni yao kwa mujibu wa kipindi kinachopaswa kulipwa madeni hayo.

Majibu ya Wizara

Baadhi ya Taasisi za Serikali zimepunguza Madeni jumla ya Tzs. 33,221,540 lakini kuna taasisi ambazo bado hazijalipa kabisa ambazo hadi sasa jumla TSH. 36,555,960zinadaiwa. Hata hivyo, Karakana Kuu bado inaendelea kufatilia madeni hayo kwa taasisi hizo ili waweze kulipa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imeelezwa katika kufuatilia madeni hayo Uongozi wa Karakana kuu walitakiwa na Wizara ya Fedha wadaiwa onyo la mwisho kasha wapeleke orodha ya wadiwa wa mwishona wadaiwa hao watakatwa na Taasisi zao (oc).

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Serikali iandae utaratibu mzuri zaidi wa malipo ya madeni ya Karakana kuu.

Hoja Namba 5.12.1.3 Kuchelewa Kufika kwa Boti tano za kusafiria katika Visiwa vidogo vidogo vya Zanzibar.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 2,059,879,300 zimelipwa kupitia hati nambari 6/10 ikiwa ni sehemu ya malipo ya fedha zilizotumika kwaajili ya utengenezaji wa boti tano (5) ndogo ilikuweza kusaidia wananchi kwa ajili ya usafiri (vivuko ) katika visiwa vidogo vidogo vya unguja na pemba katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019-2020 .

Mkataba wa utengenezaji boti hizo ulitiwa sahihi tarehe 5/6/2019 baina ya wizara na kampuni damen shipyard gorinchem ya netherlands kwa thamani ya dola za kimarekani (USD) 1,772,160 bila ya VAT ikiwa sawa na shilingi 4,076,535,091 za kitanzania.

Ukaguzi umebaini kwamba kwa mujibu wa mkataba boti hizo ziloitakiwa kukamilika ndani ya miezi kumi na mbili (12 ) ambapo hadi sasa kumebakiwa na miezi miwili kumalizika kwa mkataba huo na hakuna jitihada zozote zilizobainika kuwa boti hizo zitakamilika na kukabidhiwa kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba

Majibu ya Wizara

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika bajeti ya mwaka 2018/2019 ilitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa boti ndogo ndogo (landcrafts) tano kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wanaoishi katika visiwa vya Kojani, Makoongwe, Kisiwa Panza, Fundo na Tumbatu. Mkataba wa ujenzi wa boti hizo baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Kampuni ya Damen Shipyards ya Uholanzi ulitiwa saini tarehe 20 Juni, 2019 kwa gharama ya USD 1, 772,160 bila ya VAT sawa na Tzs. 4,076,535,091/- na ujenzi huo ulitarajiwa

kukamilika ndani ya miezi tisa.

Hata hivyo kutokana na janga la maradhi ya COVID-19 ujenzi huo haukuweza kukamilika kwa wakati na badala yake ulikamilika rasmi mwezi Februari, 2021 na boti hizo zikawasili hapa Zanzibar tarehe 4 Aprili, 2021. Boti nne kati ya hizo zimeshapelekwa Pemba na moja ipo Mkokotoni Unguja zikiwa zinasubiri taratibu za makabidhiano ambayo yamepangwa kufanyika hivi karibuni.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali zinahusika na utaratibu wa Ununuzi wa boti hizo Aidh Katika kujiridhisha kamati ya PAC imefanya ziara mbalimbali ili kujionea boti tano za kusafiria katika visiwa vidogo vidogo vya Zanzibar zenye thamani ya shilingi 2,059,897,300 maeneo yenyewe ni kama ifuatavyo :-Kwa upande wa Unguja Mkokotoni –Tumbatu Kwa upande wa Pemba Kojani,Kisiwa Panza na Fundo ziara hiyo kamati imebaini mambo yafuatayo :-

- Kuchelewa kufika kwa boti na hata zilipofika zimechelewa kufanya kazi halii imetoke eneo la kojani pale kamati ilipokwenda kwa ajili ya ziara boti ndo imeeanza kufanya kazi.

Hoja Namba 5.12.1.4 Kuchelewa Kufika kwa Vipuri vya Mashine ya Kusagia Kokoto (Crusher) Pemba Shilingi 156,615,172.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla yashilingi 156;615;172 zimetuka kupitia hati nambari6/12 ikiwa ni malipo ya awali kwa ajili ya ununuzi wa vipuri vya mashine ya kusagia kokoto kwa matumizi ya wizara pemba katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

Wizara ya ujenzi mawasiliano na usafirishaji iliiingia katika makubaliano na kampuni ya M/S ASTRA PARTS LIMITED tarehe 3/72019 kwa ajili ya ununuzi wa vipuri vya mashine ya kusagia kokoto iliyoko pemba kwa thamani ya shilingi 538,792,720.

Ukaguzi umebaini kwamba,kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba huo vifaa hivyo vilitegemewa kupokewa ndani ya siku sitini (60) mara baada ya mkataba kusainiwa.

Aidha ,imebainika hadi sasa ni muda wa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja vifaa hivyo havijapokelewa na hakuna taarifa yoyote iliyopatikana na ukaguzi juu ya hatua zinazochukuliwa kuhakikisha vifaa hivyo vinapatikana na kupokelewa kwa mujibu wa

makubaliano.

Majibu ya Wizara

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilitiliana saini na Kampuni ya M/s Astra Parts Limited ya Dar Es Salaam kwa ajili ya ununuzi wa vipuri vya mashine ya kusagia kokoto kwa matumizi ya Wizara Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Pemba katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Hata hivyo, vifaa hivyo vilichelewa kufika Pemba kwa wakati kutokana na janga la maradhi ya COVID – 19 ambayo yalisababisha athari za usafirishaji wa bidhaa mbalimbali duniani. Hivi sasa, tayari vifaa hivyo vimeshawasili kisiwani Pemba na kazi ya kutengeneza mtambo huo wa Crusher itaanza hivi karibuni.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilitaka kujua juu ya bei ya matambo mpya wa kusagia kokoto na kuelezwa kuwa ni USD 360,000 sawa na shilingi 800,280,000 wakati gharama za vifaa vilivyonunuliwa ni shilingi 538,792,720. Katika kujirdhisha na majibu ya Wizara, Kamati ya PAC ilifanya ukaguzi katika mashine ya kusagia kokoto iliyoko Pemba ili kujionea vipuri vilivyonunuliwa pamoja na kukagua nyaraka mbalimbali zinzohusiana na ununuzi na mapokezi ya vifaa hivyo.ingawa mafundi waliokuwa wakifunga mtambo huo walikuwa hawapo kutokana na dharura za kibinafsi.

Hoja Namba 5.12.1.5 Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria (Terminal III)

Katika ujenzi wa jengo la abiria terminal 3 uwanja wa ndege wa abeid amani karume ukaguzi umebaini kuwepo kwa mkataba wa nyongeza (Addendum) uliotiwa sahihi tarehe 28 julai 2017 baina ya wizara ya ujenzi,mawasiliano na usafirishaji na kampuni ya Beijing construction engineering group co Ltd mkataba huu wa nyongeza umetokana na mabadiliko ya mchoro yaliyofanywa kulingana na mkataba huo ambao umegharimu jumla ya dola za kimarekani 70,400,000 na mkataba wake ulisainiwa mwaka 2009.

Kutokana na ongezeko ( Addendum) la malipoya mkataba huo serikali ya mapinduzi ya zanzibar itailipa kampuni ya Beijing construction engineering group co Ltd ziara ya jumla ya dola za kimarekani 58,347,089.51 ambazo zinalipwa kwa awamu 25 kuanzia 0ktoba 2017 hadi juni 2022. Mchanganuo wa malipo hayo ya ziada ni kama inavyoonekana katika

jadweli lifuatalo :

Jadweli nambari 98:Malipo ya ziada yaliyotokana na ongezeko la mkataba

| NAMBA | MAELEZO | FEDHA INAYOTAKIWA KULIPWA KILA MWEZI( USD) |
|---|---|---|
| 1 | AGOSTI 2019 | 11,669,417.90 |
| 2 | OKTOBA 2019 | 5,534,708.02 |
| 3 | NOVEMBA 2019 | 1,055,097.02 |
| 4 | DISEMBA 2019 | 1,055,097.02 |
| 5 | JANUARI 2020 | 1,055,097.02 |
| 6 | FEBRUARI 2020 | 1,055,097.02 |
| 7 | MACHI 2020 | 1,055,097.02 |
| 8 | APRILI 2020 | 1,055,097.02 |
| 9 | MEI 2020 | 1,055,097.02 |
| 10 | JUNI 2020 | 1,055,097.02 |
| 11 | JULAI 2020 | 1,055,097.02 |
| 12 | AGOSTI 2020 | 2,075,811,.25 |
| 13 | SEPTEMBA 2020 | 2,075,811.25 |
| 14 | OKTOBA 2020 | 2,075,811.25 |
| 15 | NOVEMBA 2020 | 2,075,811.25 |
| 16 | DISEMBA 2020 | 2,075,811.25 |
| 17 | JANUARI 2021 | 2,075,811.25 |
| 18 | FEBRUARI 2021 | 2,075,811.25 |
| 19 | MACHI 2021 | 2,075,811.25 |
| 20 | APRILI 2021 | 2,075,811.25 |

| | | |
|---|---|---|
| 21 | MEI 2021 | 2,075,811.25 |
| 22 | JUNI 2021 | 2,075,811.25 |
| 23 | JULAI 2021 | 2,075,811.25 |
| 24 | DISEMBA 2021 | 3,218,677.24 |
| 25 | JUNI 2022 | 3,218,677.24 |
| JUMLA | | 58,347,089.50 |

Aidha ukaguzi umebaini katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya shilingi 21,081,295,836 zimelipwa kwa kampuni ya Beijing construction group co Ltd kwa kaziya ujenzi wa terminal 3 kama zinavyoonekana katika jadweli lifuatalo:

Jadweli Nambari 99: orodha ya malipo yaliyofanyika kwa kampuni ya Beijing construction group c.Ltd

| HATI NAMBA | HUNDI NAMBA | THAMANI SHILINGI | ALIYELIPWA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 42/11 | TISS | 13,411,370,234 | BEIJING CONSTRUCTION GROUP CO. LTD | ikiwa ni ya fedha kwa ajiliya jengola abiria terminal 3 la uwanja wa ndege kwa mwezi wa novemba 2019 |
| 26/2 | DUMMY | 2,503,179,934 | BEIJING CONSTRUCTION GROUP CO. LTD | ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya jengo la abiria terminal 111 la uwanja wa ndege kwa mwezi februari 2020 |
| 21/1 | TISS | 2,736,276,928 | BEIJING CONSTRUCTION | ikiwa ni malipo ya fedha kwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | GROUP CO LTD | ajili ya jengo la abiria terminal 111 la uwanja wa ndege kwa mwezi januari 2020 |
| 16/5 | TISS | 2,430,468,740 | BEIJING CONSTRUCTION GROUP CO. LTD | ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya jengo la abiria terminal 111 la uwanja wa ndege kwa mwezi mei 2020 |
| JUMLA | | | | |

Ukaguzi umebaini kasoro zifuatazo katika ujenzi huo:

- Mkandarasi kulipwa malipo ya ujenzi kwa kila mwezi pasi na kuzingatia thamani ya kazi aliyofanya kwa mujibu wa cheti cha malipocha mshauri elekezi wa ujenzi huo
- Kuwepo kwa mkataba wa ziada ( Addendu) wenye jumla ya USD. 58,347,089.51 ambazo ni sawa na asilimia 83 bei ya mkataba wa awali pasi na kupata idhini ya mlipaji mkuu wa serikali au baraza la wawakilishi kinyumena kanuni namba 49 (4) ya sheria ya ununuzi na uondoshaji wamali za umma nambari 11 ya 2016.
- Kukosekana kwa idhini kutoka kwa mwanasheria mkuu wa serikali juu ya mkataba wa ziada ( Addendum ) wenye jumla ya USD 58,347,089.51

Kuwepo kasoro zilizobainishwa hapo juu kunaweza kupelekea kazi ya ujenzi kuchelewa kumalizika kwa wakati na kutokuwa na ubora uliokusudiwa na ni kwenda kinyume na sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma nambari 11 ya 2016.
Ukaguzi unashauri uongozi wawizars kusimamia kwa karibu ujenzi huo ikiwemo kuzifanyia kazi kasoro zilizobainishwa ili kuhakikisha kwamba ujenzi huo unamalizika kwa wakati na kwa kiwango kinachotarajiwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa .

Majibu ya Wizara

Mkataba wa Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria la Terminal III kati ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Kampuni ya Beijing Construction Engineering Group (BCEG) ulitiwa saini tarehe 22 Oktoba, 2009 kwa gharama za USD 70,400,000/-.

Mradi ulikuwa na lengo la kujenga jengo lenye uwezo wa kuhudumia abiria 1.1 milioni kwa mwaka likiwa na mita za mraba 15,600. Hata hivyo ilionekana kwamba kuna haja ya kuongeza ukubwa wa jengo hilo kutoka mita za mraba 1,600 hadi kufikia mita za mraba 2,209 pamoja na kuongezwa kwa mambo mengine mbali mbali kama vile mitambo ya ziada ya ukaguzi wa abiria na mikanda ya kubebea mizigo. Baada ya majadiliano baina ya Serikali na Kampuni ya BCEG, Kampuni hiyo ilikubalika kuwepo kwa mkataba wa nyongeza wa USD 58,347,089.51/-.

HOJA

**Mkandarasi kulipwa malipo ya ujenzi kwa kila mwezi pasi na kuzingatia thamani ya kazi aliyofanya kwa mujibu wa cheti cha malipo cha Mshauri Elekezi wa ujenzi huo.**

Majibu ya Wizara

‚Mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya la abiria unajengwa kwa kupitia njia ya “Design and Build” ambapo Mkandarasi hulipwa kutokana na kazi aliyoifanya. Kwa mujibu wa Mkataba ulioingiwa baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Kampuni ya BCEG, mkandarasi huyo atalipwa kulingana na Milestones alizofikia.

HOJA

Kuwepo kwa mkataba wa ziada (Addendum) wenye jumla ya USD 58,347,089.51/- ambazo ni sawa na asilimia 83 ya bei ya makataba wa awali pasi na kupata idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikai au Baraza la Wawakilishi kinyume na kanuni nambari 49 (4) ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya 2016.

Majibu ya Wizara

Kutokana na kuchelewa kupata mkopo kutoka Exim Bank ya China Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya maamuzi ya kutoa fedha zake za ndani ili kukamilisha ujenzi wa Jengo hilo. Katika bajeti ya mwaka 2019/2020 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilitengewa jumla ya Tzs. Bilioni 16.0 kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi wa

Jengo hilo.

HOJA
Kukosekana kwa idhini kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya mkataba wa ziada (Addendum) wenye jumla ya USD 58,347,089.51/-.

Majibu ya Wizara
Maamuzi ya kufanya malipo hayo ya ziada yalifanywa na Serikali kwa hiyo haikuonekana haja ya kulipitisha suala hilo kwa Mwanasheria Mkuu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji sababu zilizopelekea zilizopelekea kumlipa mjenzi kila mwezi na kuelezwa kuwa Wizara ya Ujenzi haikuhusika na uwamuzi huo bali ilikuwa uwamuzi wa Serikali Kuu.na kamati ilikuwa haina maelezo zaidi.

## 3.6 FUNGU Q 01 WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, WANAWAKE NA WATOTO (WIZARA YA NCHI (OR) KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI)

### Taarifa ya Mapato

Katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,039,464,000 kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 732,853,807 sawa na asilimia 71 ya makadirio

### Majibu ya Wizara ya Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji

Iliyokuwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto ilikadiriwa kukusanya Jumla ya Shilingi Bilioni Moja Milioni Thalathini na Tisa Laki Nne Sitini na Nne Elfu tu. (Tshs.1,039,464,000/=) ambapo ukusanyaji halisi ulikuwa shilingi Milioni Mia Saba Thalathini na Mbili Laki Nane Hamsini na Tatu Elfu Mia Nane na Saba (Tshs.732,853,807/=) sawa na asilimia Sabini Na Moja (71%) ya makadirio ya mwaka.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilielezwa kuwa Ada ya ukodishwaji wa ukumbi imeshuka asilimia imekuwa ndogo kutokana na janga Uviko 19 kutokana na agizo la Serikali kuzuia mikusanyiko katika kipindi cha mripuko wa maradhi ya Korona (COVID 19) .

Aidha, Kamati ilielezwa kuwa ada ya usajili wa vyama vya Ushirika ilipanda sana imetokana na vyama vingi vya Ushirika vimesajiliwa kwa hivyo imepitiza makadirio hali hii inaonesha vya vingi vya ushirika vimepata muwamko

Taarifa ya Matumizi

Katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 17,988,806,259 kati ya hizo shilingi 15,329,900,000 zilipangwa kwa kazi za kawaida na shilingi 2,658,906,259 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto imeingiziwa na kutumia shilingi 13,900,231,311 kwa kazi za kawaida ikiwa ni sawa na asilimia 90.7 ya makadirio na shilingi 1,208,067,625 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 45.4 ya makadiri

Majibu ya Wizara

Kwa upande wa matumizi Wizara ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Nne Arobaini na Tano na Laki Sita (Tshs. 17,445,600,000) kati ya hizo Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Tatu Ishirini na Tisa na Laki Tisa (Tshs. 15,329,900,000) zilipangwa kwa kazi za kawaida na jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja na Kumi na Tano na Laki Saba (Tshs. 2,115,700,000) kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia mwezi wa Juni 2020, jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Tisa, Laki Mbili Thalathini na Moja Elfu, Mia Tatu Kumi na Moja (Tshs. 13,900,231,311/=) zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia (91%) ya makadirio. (Kiambatanisho namba 2). Kwa upande wa fedha za Maendeleo, Wizara iliingiziwa jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili na Nane, Sitini na Saba Elfu, Mia Sita na Ishirini na Tano tu (Tshs. 1,208,067,625) sawa na asilimia (57%) ya makadirio ya fedha za maendeleo.

UTEKELEZAJI WA MIRADI WA FEDHA ZA MAENDELEO

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ilitekeleza Miradi ifuatayo:

1) Mradi wa Hifadhi ya Wazee (SERIKALI)

2) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kulelea na Kukuza Wajasiriamali Pemba (SERIKALI)

3) Mradi wa Jinsia (UNFPA)

4) Mradi wa kijinsia na Uwezeshaji wa wanawake (UNWOMEN).

5) Mradi wa Hifadhi ya Mtoto (UNICEF).

6) Mradi wa Hifadhi ya Jamii (UNICEF)

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuna utofauti wa fedha katika taarifa ya kazi za Maendeleo katika ripoti ya Mdhibiti shilingi 2,658,906,259 na majibu ya Wizara ilikuwa shilingi 2,115,700,000 kamati imeelezwa kuwa mkaguzi alitoa taarifa hii kwenye financial statement ya Wizara hivyo taarifa sahihi ya kazi za Maendeleo ni kutoka katika majibu ya Wizara. Halkadhalika, kamati imeelezea kuwa kutokana na utofauti huu Wakaguzi wapo sawa na financial statement hivyo wizara imekiri kutokea mapungu hayo

Hoja Namba 5.13.1.1 KUTOTHIBITISHWA KWA WATENDAJI WALIO AJIRIWA

Kanuni namba 9(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014, kinamtaka mtumishi wa umma aliyekuwepo katika muda wa majaribio kupatiwa nafasi ya kuthibitishwa katika nafasi yake aliokuwa nayo ya ajira baada ya kumaliza muda wa majaribio ambao ni miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuajiriwa.

Ukaguzi umebaini kwamba wizara ina watendaji ambao wameajiriwa zaidi ya miezi kumi na mbili na wameshamaliza muda wa majaribio, lakini bado hawajapatiwa barua zao za kuthibitishwa kuwa watendaji wa kudumu wa wizara hiyo.

Jadweli lifuatalo linaonyesha majina ya watendaji hao pamoja na tarehe za kuanza kazi.

Jadweli Namba 100: Wafanyakazi Ambao Hawajathibitishwa Kazini

| Namba | Jina Kamili | Idara Aliyoajiriwa | Tarehe ya Kuajiriwa | Muda wa Kutothibitishwa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Zainab Ayoub Naim | Ustawi wa Jamii | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 2. | Amina Khamis Hafidh | Ustawi wa Jamii | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 3. | Sihawa Ali Zahor | Ustawi wa Jamii | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | aajiriwe |
| 4. | Wahida Khamis Ali | Ustawi wa Jamii | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 5. | Abdulnassir Yussuf Salum | Ustawi wa Jamii | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 6. | Subira Mohamed Amour | Ustawi wa Jamii | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 7. | Kombo Hamdu Kombo | Ustawi wa Jamii | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 8. | Hassan Juma Haji | Ustawi wa Jamii | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 9. | Rukaiyya Abdi Mohd | Ustawi wa Jamii | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 10. | Khairat Shaib Faki | W/Watoto | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 11. | Zainab Haji Msuri | Ustawi wa Jamii | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 12. | Chiku Hassan Vuai | Ustawi wa Jamii | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 13. | Fatma Ali Hassan | Ustawi wa Jamii | 3/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 14. | Jamila Ali Khamis | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 15. | Khamis Mohd Abeid | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 16. | Farida Abdalla Ali | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | aajiriwe |
| 17. | Fatma Ramadhan Mweleza | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 18. | Halima Salum Shaaban | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 19. | Suhaila Amour Makame | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 20. | Mwanakhamis Suleiman Adam | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 21. | Lawahidha Yussuf Mohd | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 22. | Maryam Mohd Nassor | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 23. | Nassra Makame Ibrahim | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 24. | Zainab Juma Khamis | Mipango, Sera na Utafiti | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 25. | Latifa Mustafa Suleiman | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 26. | Awadh Ramadhan Hussein | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 27. | Munira Hassan Ali | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 28. | Asha Haji Pandu | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 29. | Khamis Fumu Fadhil | Ustawi wa Jamii | 17/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | aajiriwe |
| 30. | Fatma khatb Tulas | Ustawi wa Jamii | 28/1/2019 | Mwaka mmoja na miezi kumi na moja toka aajiriwe |
| 31. | Mohamed Amour Kisisa | Utumishi na Uendeshaji | 7/3/2019 | Mwaka mmoja na miezi tisa toka aajiriwe |
| 32. | Mosi Rashid Ubwa | Ustawi wa Jamii | 9/5/2019 | Mwaka mmoja na miezi saba toka aajiriwe |
| 33. | Nuru Issa Mohamed | Ustawi wa Jamii | 9/5/2019 | Mwaka mmoja na miezi saba toka aajiriwe |

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa Wafanyakazi waliokuwa hawajadhibitishwa kulikuwa na hakuna fedha ya kuwalipia katika mafunzo , na mfanyakazi mmoja gharama yake shilingi 150,000 hata hivyo kamati imeelezwa kuwa tayari Wizara imefanya utaratibu kwa ajili ya kuwapatia mafunzo na kamati imeridhika na majibu yao

MAPENDEKEZO YA KAMATI YA PAC
Kamati inashauri kuwa Wizara wawe na utaratibu mzuri katika ulipaji wa wanafunzi

Majibu ya Wizara

Katika watumishi 33 waliokuwa hawajathibitishwa, ni watumishi wawili (2) tu (Nd. Zainab H. Msuri na Nd. Zainab J. Khamis) ambao kwa sasa wako chini ya Wizara ya Kazi, Uchumi na Uwekezaji na tayari wameshathibitishwa, kwa barua namba NAA/NBA/Z.1029 na namba NAA/NBA/Z.1030/C ya Tarehe 5/10/2021 zinahusika. Mtumishi mmoja (1) (Mohamed A. Kisisa) alirudishwa Utumishi wa Umma kwa barua namba WKUWWW/0006/3/VOL.5/49 ya tarehe 3/4/2019 inahusika na Watumishi Thalathini (30) waliobakia wako Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto wanategemea watathibitishwa ndani ya mwaka huu wa fedha 2021/2022 fedha itakaporuhusu.

HOJA 5.13.1.2 BAKAA YA FEDHA AMBAZO HATUJAPATA UHALALI WA MATUMIZI YAKE TSHS 412,672,327

Ukaguzi umebaini kuwa kwa kupitia Ripoti yake ya utekelezaji ya mpango kazi wa Wizara

imeeleza kuwa baadhi ya shughuli hizozilipangiwa kutumia shilingi Tshs. 939,779,487 lakini kilichopatikana Tshs. 584,661,633 kwa kipindi cha mwaka 2019/2020. Hata hivyo, fedha ziliotumiwa kwa shughuli hizo kwa kupitia hati za malipo mbalimbali ni Shilingi Tshs. 171,988,806 tu kati ya Tshs. 584,661,633 zilizopatikana kwa mwaka wa fedha husika na kubakia Tshs. 412,672,327 ambazo hati zake za malipo pamoja na vielezo vya matumizi havikupatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya Wizara

Majibu ya hoja hii ya bakaa ya fedha ambazo hazijapatiwa uhalali wake yanajionesha katika majadweli yafuatayo;-

KAMISHENI YA KAZI

| SHUGHULI ZILIZOPANGWA | MAKADIRIO KWA MWAKA (TSHS) | FEDHA ZILIZOPATIKANA (TSHS) | FEDHA ZILIZOTUMIKA (TSHS) | BAKAA YA FEDHA (TSHS) | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya ukaguzi kazi ili kuhakikisha utekelezaji wa Sheria za Kazi | 146,170,000 | 35,087,500 | 12,910,000<br>. | 22,177,500 | Hakuna bakaa iliyojitokeza katika shughuli<br>hii na fedha zote zilitumika kama zilivyopatikana.<br>Hati za malipo nambari 8/11, 1/04, 2/6,<br>5/8, 7/11,4/5, 5/12, 5/3, 5/9, 12/10, 15/11, 3/9, 4/6 zipo tayari kwa ukaguzi |
| Kutoa elimukazi juu ya Sheria za kazi, ushirikishwaji katika sehemu za kazi | 5,200,000 | 3,550,000 | 2,300,000<br>. | 1,250,000 | Katika shughuli hii kuna bakaa iliyojitokeza ya Tshs.<br>300,000 ambayo imeingia katika matumizi<br>mengine ya uendeshaji kutokana na kwamba<br>Mwaka huu baadhi ya vipindi vilidhaminiwa<br>na vyombo vya habari bila ya malipo yoyote |
| Kuimarisha huduma | 7,100,000 | 5,325,000 | | 5325,000 | Hakuna fedha zilizobakia katika utekelezaji<br>wa shughuli hii, fedha zote |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| za utoaji wa vibali kwa wafanya kazi wa kigeni | | | | | zimetumika kama zilivyopatikana. Vocha ya matumizi nambari 26/6 na vielelezo vipo tayari kwa ukaguzi.- |
| Kufanya kikao cha bodi ya mambo ya mishahara. | 3,120,000 | 3,120,000 | .- | 3,120,000 | Hakuna fedha zilizobakia katika utekelezaji wa shughuli hii, fedha zote zimetumika kama zilivyopatikana. Vocha ya matumizinambari 26/6 na vielelezo vipo tayari kwa ukaguzi |
| Kushiriki mikutano ya Kimataifa na ya Kikanda kuhusu masuala ya kazi na ajira | 7,600,000 | 6,600,000 | 4,387,890 | 2,212,110 | Bakaa ya fedha Tshs 7,890 imejitokeza katika shughuli hii ambayo imetokana na tofauti ya ubadilishaji wa fedha za kigeni (exchange rate). Vocha nambari 3/8, 3/10, 1/11na 4/8 zipo tayarikwa ukaguzi. |
| Kuratibu vikao vya Wajumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi. | 5,000,000 | 3,500,000 | 2,500,000 | 1,000,000 | Kamisheni ya Kazi kwa kipindi hicho, iliingiziwa Tshs 3,200,000 na siyo Tshs 3,500,000 kwa ajili ya kuratibu vikao hivyo. Kamishenikutokana na Fedha hizo, ilitumia Tshs. 1,500,000 kwa ajili ya kudhamini kikao kimoja cha Wajumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi. Fedha zilizobakia (Tshs. 1,700,000) zilitumiwa kwa matumizi mengineyo ya kupambana na maradhi ya Uviko 19. Vocha nambari 4/9 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | na 1/3<br>zipo tayari kwa ukaguzi. |
| Kuanzisha mfumo wa kuhifadhia taarifa (database). | 150,000,000 | 13,967,505 | | 13,967,505 | Mpaka kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2019/2020, Fedha hizi hazikutumika kutokana na kutokamilika kwa tathmini ya awali juu ya maeneo ambayo Mfumo huo uweze kujumuisha. Fedha hizi zilifanyiwa matumizi mengine kwa mwaka wa fedha 2020/2021.<br>Vielelezo vipo kwa ukaguzi- |

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

| SHUGHULI ZILIZOPANGWA | MAKADIRIO KWA MWAKA (TSHS) | FEDHA ZILIZOPATIKANA (TSHS) | FEDHA ZILIZOTUMIKA (TSHS) | BAKAA YA FEDHA (TSHS) | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| Kununua vifaa ya kujikinga na maradhi ya Covid 19 | 22,140,000 | 18,819,000 | - | 18,819,000 | Shughuli hii imeripotiwa katika Taarifa ya Utekelezaji lakini haijakuwepo katika Mpango kazi. Kutokana na kuwepo kwa maradhi ya Uviko 19 na Wizara ilikuwa inasimamia makundi mbali mbali ikiwemo Wazee, Watoto hivyo ililazimika kutumia fedha mbali mbali za uendeshaji kutumika katika kupambana na maradhi hayo kwa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kununua vifaa kinga na kuvisambaza sehemu mbali mbali zikiwemo Idara na Taasisi mbali mbali zilizomo katika Wizara. Hati za malipo mbali mbali ziko kwa ukaguzi |
| Kuandaa safari za kikazi ndani na nje ya nchi | 188,000,000 | 158,520,000 | 61,321,520 | 97,198,480 | Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha, zilitumika Tshs 201,830,695. Hakuna bakaa ya fedha. Hati za malipo mbali mbali ziko kwa ukaguzi |
| Kufanya vikao vya kamati ya Uongozi, Tendaji na Baraza la Wawakilishi | 20,400,000 | 18,768,000 | | 18,768,000 | Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2019/2020, zilitumika Tshs 20,540,000 Kwa kufanya vikao mbalimbali na hati za malipo ziko kwa ukaguzi - |
| Kununua vifaa vya michezo | 14,045,000 | 13,764,000 | - | 13,764,000 | Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha, zilitumika Tshs 3,900,000. Fedha zilizozidi katika eneo hili ni fedha zilizotumika katika Safari. Vielelezo vya safari vipo kwa ukaguzi |

IDARA YA WAZEE NA USTAWI WA JAMII

| SHUGHULI ZILIZOPANGWA | MAKADIRIO KWA MWAKA (TSHS) | FEDHA ZILIZOPATIKANA (TSHS) | FEDHA ZILIZOTUMIKA (TSHS) | BAKAA YA FEDHA (TSHS) | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuzika maiti zisizokuwa na wenyewe | 4,600,000 | 5,756,000 | 5,756,000 | .- | Makisio ya kuzika maiti 16 zilipangwa kwa mwaka husika lakini Idara ilizika maiti 18 kwa hivyo fedha hiyo imeengezeka kwenye kuzika. Gharama za kuzika hutegemea na hali ya maiti. Kwa kawaida isiyoharikibika huzikwa kwa Tshs.350,000/- na iliyoharibika inafika Tshs.400,000/-Hati za malipo zipotayari kwa ukaguzi |
| Kufanya | 2,655,000 | 1,000,000 | | 1,000,00 | Hakuna bakaa lililobakia fedha zote zimetumika |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ufuatiliaji wa kesi katika mahakama za watoto | | | | 0 | katika tarehe 27/01/2020 Tshs.500,000 zilitumika kwa ajili ya maposho ya chakula na mafuta ya ufuatiliaji, Na tarehe 04/2020 Tshs.500,000/ zilitumika kwa ajili ya maposho ya chakula na mafuta ya ufuatiliaji.Hati za malipo zipo tayari kwa ukaguzi.- |
| Kusimamia uendeshaji wa Nyumba ya kuhifadhia wahanga wa udhalilishaji | 6,000,000 | 2,000,000 | | 2,000,000 | Hakuna bakaa lililobakia fedha zote zimetumika katika tarehe 29/11/2019 Tshs.1,500,000/- ilitumika kwa ajili ya uendeshaji, na tarehe 9/04/2020 Tshs.500,000 zilitumika kwa ajili ya uendeshaji. Hati za malipo zipo tayari kwaukaguzi.- |
| Kuwapatia huduma Watoto wa Nyumba ya kulelea watoto Mazizini | 115,230,000 | 110,073,500 | 82,813,396 | 27,260,104 | 20/05/2020 Tshs.11,400,000/- zilitumika kwa ajili ya kuwanunulia nguo za sikukuu watoto wa mazizini, 14/05/2020 Tshs. 8,000,000/- kwa ununuzi wa chakula mazizini, 16/06/2020 Tshs. 7,860,104/- kwa ununuzi wa chakula mazizini. |
| Kufany | 10,350,00 | 10,315,43 | | 10,315,4 | • Tshs.211,900/- bima ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| a ufuatiliaji wa shughuli za kiustawi | 0 | 5 | | 35 | gari<br>• 08/2019 Tshs.840,000/- safari za ndani<br>• 11/2019 Tshs.1,105,000/-safari za ndani<br>• 01/2020 Tshs. 2,938,535/-Safari nje ya nchi<br>• 04/2020 Tshs. 1,805,000/- safari za ndani<br>• 04/2020 Tshs. 1,000,000/- matengenezo ya gari<br>• 06/2020 Tshs.800,000/- safari za ndani<br>• 06/2020 Tshs.472,000/- matenegenezo ya gari<br>• 06/2020 Tshs.390,000/- matenegenezo ya gari<br>• Tshs.660,000/- Ufuatiliaji wa watu wa mazingira magumu.<br>• 09/2019 Tshs.93,000/- msaada kwa mama alietelekezwa<br>Hati za malipo zipo tayari kwa ukaguzi.- |

IDARA YA WANAWAKE NA WATOTO

| SHUGHULI ZILIZOPANGWA | MAKADIRIO KWA MWAKA (TSHS) | FEDHA ZILIZOPATIKANA (TSHS) | FEDHA ZILIZOTUMIKA (TSHS) | BAKAA YA FEDHA (TSHS) | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya matengene | 45,147,487 | 45,147,487 | | 45,147,487 | Fedha hii iliombwa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| zo ya nyumba salama | | | | | Wizara ya Fedha na Mipango lakini haikuingizwa. Matengezo ya nyumba salama yalifanywa kupitia Fedha za Mradi wa Jinsia. Hati za malipo zipo kwa ukaguzi.- |

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

| SHUGHULI ZILIZOPANGWA | MAKADIRIO KWA MWAKA (TSHS) | FEDHA ZILIZOPATIKANA (TSHS) | FEDHA ZILIZOTUMIKA (TSHS) | BAKAA YA FEDHA (TSHS) | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuchapisha Sera ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi 2019, Sera ya Watoto pamoja na kuchapisha toleo Pendwa la Uwezeshaji Wananchi kiuchumi 2019 | 8,020,000 | 9,510,000 | - | 9,510,000 | Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2019/2020, Hakuna bakaa ya fedha. Hati za malipo mbali mbali ziko kwa ukaguzi |
| Kufanya | 41,100,00 | 10,610,000 | - | 10,610,00 | Utafiti huu maandalizi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| utafiti wa maradhi yanayotoka na na sehemu ya Kazi | 0 | | | 0 | yake yalikuwa yameshaanza kwa kipindi hicho hadi hatua ya kumtafuta Mtaalamu Elekezi. Kwa bahati mbaya kutokana na kuzuka kwa maradhi ya Uviko 19, Fedha hizi zilitumika kwa kununua vifaa vya kujikinga na maradhi ya UVIKO 19 na shughuli za uendeshaji wa Afisi kutokana na uhaba wa fedha uliokuwepo Serikalini kwa kipindi hicho. Hati za malipo mbali mbali ziko kwa ukaguzi |
| Kuimarisha Uwezo wa Idara kufanya shughuli zake kwa ufanisi (gari 1 imenunuliwa kwa shughuli za Ufuatiliaji) | 85,000,000 | 73,545,000 | - | 73,545,000 | Kwa mpango kazi 2019/20 hakuna fedha hiyo na badala yake Fedha zake zilikuwepo katika mwaka wa fedha 2018/2019, Gari (SMZ 531 B) ilipatikana mwaka 2019/2020 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Hati zipo kwa ukaguzi |

IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI

| SHUGHULI ZILIZOPANGWA | MAKADIRIO KWA MWAKA (TSHS) | FEDHA ZILIZOPATIKANA (TSHS) | FEDHA ZILIZOTUMIKA (TSHS) | BAKAA YA FEDHA (TSHS) | MAELEO |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya utafiti wa maradhi yatokanayo na kazi | 14,569,500 | 14,569,500 | | 14,569,500 | Baadhi ya fedha hizi zilianza kutumika kwa utafiti ambapo Watendaji wawili walilipwa kwa safari ya Pemba, ununuzi wa mafuta kwa Idara na Fedha nyengine zilitumika kwa shughuli za uendeshaji wa Afisi kutokana na uhaba wa fedha uliokuwepo Serikalini kwa kipindi hicho.- |
| Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Idara ya Usalama na Afya Kazini kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu | 12,000,000 | 9,350,706 | | 9,350,706 | Fedha hizi zilitumika kwa shughuli za uendeshaji wa Afisi kutokana na uhaba wa fedha uliokuwepo Serikalinikwa kipindi hicho.- |

IDARA YA AJIRA

| SHUGHULI ZILIZOPANGWA | MAKADIRIO KWA MWAKA (TSHS) | FEDHA ZILIZOPATIKANA (TSHS) | FEDHA ZILIZOTUMIKA (TSHS) | BAKAA YA FEDHA (TSHS) | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuelimisha | 4,200,000 | 4,200,000 | | 4,200,000 | Vocha |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| jamii kuhusu soko la ajira | | | | | inaonesha kuwa fedha zilitumika kwa kutoa mafunzo kuhusiana na maradhi ya Korona pamoja na kuwanunulia vifaa vya kujikinga (sabuni, vitakasa mikono na Barakoa )- |
| Kutoa mafunzo kwa vijana juu ya umuhimu wa ajira na kujiajiri | 7,563,000 | 7,563,000 | - | 7,563,000 | Vocha zipo kwa ukaguzi |
| JUMLA KUU | 939,779,487 | 584,661,633 | 171,988,806 | 412,672,827 | |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa alipokuja Mkaguzi Wizara haikuwapa ushirikiano wa kutosha katika kuona hati za malipo na vielelezo vya bakaa fedha shilingi 413,672,327 , kamati ya PAC ilipewa walipewa vielelezo hata hivyo kamati haikuridhika na vielelezo hivi.

Mapendekezo ya Kamati PAC

Kamati inashauri Wizara watoe ushirikiano wa kutosha pale anapokuja mkaguzi ili kuondokana na matatizo ya kutofahamiana .

Hoja Namba 5.13.1.3 Matumizi Yasiyokuwa na Tija Shilingi 186,069,600

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 186,069,600 zimetumika kwa ajili ya uimarishaji wa vitengo mbali mbali vya wizara, ukaguzi umebaini kupitia ripoti ya utekelezaji ya wizara kwamba baadhi ya vitengo ambavyo vya Idara ya Utumishi na

Uendeshaji vimeimarishwa ili kuweza kuleta ufanisi mzuri katika kazi zake.

Katika uimarishwaji wa vitengo hivyo ukaguzi haukuweza kujirishisha juu ya hatua ya uimarishaji huo ulioelezwa pamoja na matumizi ya fedha yalivyotumika kutokupatikana kwa hati za malipo pamoja na vielelezo vya matumizi hayo, jambo ambalo limeleta shaka juu ya uhalali wa matumizi hayo. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 102: Matumizi Yasiyokuwa na Tija

| Namba | Jina la Kitengo | Fedha Zilizokadiriwa (SHS) | Fedha Zilizotumika (SHS) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ukaguzi wa ndani | 37,000,000 | 35,890,000 | Hakukupatikana kwa taarifa ya shughuli iliyotekelezwa |
| 2 | Kitengo cha manunuzi | 27,575,000 | 26,472,000 | Hakukupatikana kwa taarifa ya shughuli iliyotekelezwa |
| 3 | Kitengo cha hesabu | 31,240,000 | 27,803,600 | Hakukupatikana kwa taarifa ya shughuli iliyotekelezwa |
| 4 | Kuimarisha mfumo wa TEHAMA wa wizara | 103,300,000 | 95,904,000 | Hakukupatikana kwa taarifa ya shughuli iliyotekelezwa |
| | | | 186,069,600 | |

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC

Kamati ilihitaji kupata ufafanuzi juu ya majibu ya Wizara na kuelezwa kuwa kasoro ilijitokeza katika uandaaaji wa ripoti ya utekelezaji hata hivyo baadhi ya vitengo ikiwemo kitengo cha Manunuzi matumizi yalifanyika yakiwemo safari za kikazi na mafunzo na vielelezo hivo vipo  na kitengo cha ukaguzi wa ndani fedha hazikutumika na badala yake zimetumika kwa shughuli nyengine za kikazi

Kamati imepata mashaka kuhusiana na hoja hii.

MAPENDEKEZO YA KAMATI YA PAC

Kamati inashauri kwamba ripoti ya utekelezaji ifanye uhalisia wa matokeo halisi

HOJA5.13.1.4 Madeni ya Muda Mrefu Yanayotokana na Ulipwaji wa Fidia Shilingi 58,789,503.50

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika wizara kupitia Idara yake ya Ustawi wa Jamii chini ya Kitengo chake cha Fidia kimekuwa na deni la shilingi 58,789,503.50 zinazotokana na watumishi wanaopata ajali wakiwa kazini, wanaopatwa na maradhi pamoja na fedha zinazotumika kwa ajili ya kujitibu kwa wale wanaoumia.

Aidha, pamoja na jitihada zinazochukuliwa na wizara za kuwalipa fidia wanaofikwa na matatizo hayo, ukaguzi umebaini uwepo wa madeni ya muda mrefu ambayo bado hayajalipwa jambo ambalo kupelekea wahusika kukata tama juu ya kupatiwa haki zao hizo.

Orodha ya wadai wa fidia wanaostahiki kulipwa kwa 2019/2020 ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Namba 103: Wadai wa Fidia Wanaostahiki Kulipwa

| Nam. | Nambari ya Kesi | Jina Kamili | Taasisi Aliyoajiriwa | Fedha Anazostahiki Kulipwa Fidia (SHS) | Fedha Alizolipwa (SHS) | Fedha Inayodaiwa (SHS) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Z/27/2017/2018 | ZUBEIDA ABDI SAID | WEMA | 6,140,345 | 3,698,506 | 2,441,839 |
| 2. | Z/04/2018/2019 | KAIJE JUMA MGENI | OMKR | 6,120,000 | 2,000,000 | 4,120,000 |
| 3. | Z/24/2018/2019 | ALI RAMADHAN MUSSA | W/AFYA | 3,058,366 | 1,000,000 | 2,058,366 |
| 4. | Z/25/2018/2019 | OMAR NGWALI ZUBEIR | WEMA | 1,322,707 | 322,707 | 1,000,000 |
| 5. | Z/26/2018/2019 | ABDALLA MWARAB KHALFAN | SUZA | 10,997,064 | - | 10,997,064 |
| 6. | Z/31/2018/2019 | ALI MWENI ZUBEIR | Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa | 1,115,500 | - | 1,115,500 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Hesabu za Serikali | | | |
| 7. | Z/34/2018/2019 | HALIMA ALI KHAMIS | MAHAKAMA | 940,867 | - | 940,867 |
| 8 | Z/37/2018/2019 | KHAMIS ALI HASSAN | WEMA | 1,069,300 | - | 1,069,300 |
| 9. | Z/86/2018/2019 | MUSSA HAMDU KHEIR | W/ARDHI | 1,271,416 | - | 1,271,416 |
| 10. | Z/87/2018/2019 | TAMIM HAMAD SAID | W/AFYA | 496,467 | - | 496,467 |
| 11. | Z/88/2018/2019 | HAMIDA MWINYI MAKAME | W/AFYA | 253,067 | - | 253,067 |
| 12. | Z/107/2018/2019 | ASSA JUMA RASHID | WEMA | 247,083 | - | 247,083 |
| 13. | Z/110/2018/2019 | SHAHIDA ALI ZUBEIR | W/AFYA | 2,258,299 | - | 2,258,299 |
| 14. | Z/111/2018/2019 | BIMKUBWA MBWANA KOMBO | WEMA | 509,433 | - | 509,433 |
| 15. | Z/112/2018/2019 | ABDALLA KHEIR HASSAN | WEMA | 2,547,600 | - | 2,547,600 |
| 16. | Z/02/2019/2020 | HIDAYA MAKAME HAJI | WEMA | 718,491 | - | 718,491 |
| 17. | Z/05/2019/2020 | ZUHURA ABDI SAID | WEMA | 199,433 | - | 199,433 |
| 18. | Z/07/2019/2020 | RAIFA SIMAI ALI | W/AFYA | 442,561 | - | 442,561 |
| 19. | Z/08/2019/2020 | SALAMA HASSAN SULEIMAN | WEMA | 403,333 | - | 403,333 |
| 20. | Z/10/2019/2020 | BAHATI OMAR JUMA | W/HABARI | 593,716 | - | 593,716 |
| 21. | Z/11/2019/2020 | OMAR JUMA MOHD | KILIMO | 6,446,650 | - | 6,446,650 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 22. | Z/15/2019/2020 | SHUWAYFA OMAR ALI | W/AFYA | 245,158 | - | 245,158 |
| 23. | Z/21/2019/2020 | KASSIM MOHD MUOMBWA | WEMA | 539,000 | - | 539,000 |
| 24. | Z/22/2019/2020 | HAJI MURID HASSAN | WILAYA YA MJINI | 1,259,549 | - | 1,259,549 |
| 25. | Z/23/2019/2020 | MTUMWA YUSSUF AMEIR | WILAYA YA KASK. B | 451,066 | - | 451,066 |
| 26. | Z/26/2019/2020 | ALI OMAR HAMDU | W/AFYA | 7,392,361.5 | - | 7,392,361.5 |
| 27. | Z/30/2019/2020 | YUSSUF SADIK ISSA | WKUWWW | 2,295,666 | - | 2,295,666 |
| 28. | Z/32/2019/2020 | MMANGA AME MACHANO | WKUWWW | 95,800 | - | 95,800 |
| 29. | Z/33/2019/2020 | MASOUD MRISHO SHEHA | WKUWWW | 197,667 | - | 197,667 |
| 30. | Z/34/2019/2020 | SARA HASSAN FEREJI | WKUWWW | 1,064,000 | - | 1,064,000 |
| 31. | Z/35/2019/2020 | MOHAMED JUMA MOHAMED | W/AFYA | 118,800 | - | 118,800 |
| 32. | Z/37/2019/2020 | KAZIJA ALI MSAADA | W/AFYA | 1,638,556 | - | 1,638,556 |
| 33. | Z/29/2019/2020 | MAKAME SHARIF MAKAME | WKUWWW | 2,470,399 | - | 2,470,399 |
| 34. | Z/36/2019/2020 | OMAR JUMA MWALIM | UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA | 620,800 | - | 620,800 |
| 35. | Z/42/2018/2019 | MAHMOUD FADHIL ABDALLA | W/UJENZI MAWASILIANO NA | 270,200 | - | 270,200 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | USAFIRISH AJI | | | |
| | JUMLA | | | | | |

Majibu ya Wizara
Idara ya Wazee na Ustawi wa jamii imejipangia kupunguza deni hili la fidia kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha ila changamoto kubwa ni uhaba waupatikanaji wa fedha na ongezeko la wadai linaendelea kujitokeza. Hata hivyo madeni hayo yamepunguzwa kwa watiu nane kwa wa mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya Tshs 1,200,000.

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC
Kamati ya PAC ilihoji kuhusiana na uchelewaji wa ulipaji wa fedha za fidia ,kamati ilielezwa kuwa changamoto kubwa katika uingiaji wa fedha za OC na kutokana na asili ya Wizara hawana mapangilio wa matokeo. Hata hivyo kamati iliridhika na majibu yao

MAPENDEKEZO YA KAMATI YA PAC

- Kamati inashauri wadai walipwe fedha zao zisikae mud mrefu .

- Kamati inashauri Wizara ya Fedha wasiwacheleweshe fedha za malipo ya fidia ili walengwa wapate fedha zao kwa wakati.

HOJA NAMBA 5.13.1.5 FEDHA ZILIZOTUMIKA KINYUME NA MALENGO YALIOKUSUDIWA KWA KIPINDI CHA 2019/2020 Tshs. 450,000,000
Wizara ya kazi kupitia Idara ya uwezeshaji wanachi kiuchumi ilipanga kutumia Tshs 600,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wakujenga kituo cha kulea wajasiri mali Pemba, Fedha zilizopatikana kwa ujenzi huo ni 450,000,000/= ya fedha iliopangwa.

Hata hivyo Ukaguzi umebaini kwa fedha hio haikutumika kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi ulio kusudiwa kutekelezwa na baadala yake kutumika kama:

- Tshs. 300,000,000 ilihaulishwa na kutumika kwa ajili ya ukarabati wa nyumba ya watoto yatima ya Mazizini.

- Tshs. 120,000,000 zilitumika kwa malipo ya awamu ya mwisho kwa ujenzi wa jingo na eneo la kuoshea maiti Sebuleni.

- Tshs. 30,000,000 Zilitumika kwa kumlipa Consultant kwa kuandaa mchoroBOQ

(BILL OF QUANTITY) kwa eneo la ujenzi wa kituo cha incubation Pemba.

MAJIBU YA WIZARA

Jumla ya Tshs. 300,000,000/= Zilitumika kwa dharura Kutokana uvujaji wa maji wakati wa mvua pamoja na kuharibika miundombinu ya mfumo wa maji safi na taka katika Nyumba ya Watoto Mazizini kulipelekea kuhatarisha usalama wa maisha kwa watoto na wafanyakazi waliopo katika nyumba hiyo.

Wizara ilifanya tathmini na kupeleka taarifa Serikalini na Kuamuliwa kufanyika ukarabati mara moja na watoto kuhamishiwa Makazi ya Wazee Sebleni.

Fedha Tshs. 120,000,000/= Malipo ya ujenzi wa jengo na eneo la kuoshea maiti SEBLENI KWA WAZEE

Fedha Tshs 30,000,000/= Malipo kwa ajili ya mshauri elekezi kwa kuandaa mchoro na BILL OF QUANTITY (BOQ) kwa eneo la ujenzi INCUBATION PEMBA.

Barua za uhalali wa uhaulisho huu zipo tayari kwa ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Wizara na haikuwa maelezo zaidi

WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, WANAWAKE NA WATOTO – PEMBA.

Haja Namba 5.13.1.6 MAdeni ya Muda Mrefu

Kuhusu majibu ya hoja no. 5.13.1.6 .Madeni ya muda mrefu yatokanayona ulipwaji wa fidia shilling 27,250,096. Katika ukaguzi iliuofanyika imebainika Wizara kupitia Idara ya Ustawi wa jamii chini ya kitengo cha fidia kumekuwa na deni 27,250,096 zinazotokana na watumishi wanaopata ajali wakiwa kazini , wanaopatwa na maradhi pamoja na fedha zinazotumika kwa ajuli ya kujitibu kwa wale wanaoumia. Aidha pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Wizara za kuwalipa fidia wanaofikwa na matatizo hayo, ukaguzi umebaini uwepo wa madeni ya muda mrefu ambayo bado hayajalipwa jambo ambalo linawapelekea wahusika kukata tama ya kupata haki zao. Ugaguzi huo ni wa mwaka wafedha unaoishia 30 juni,2020.

Majibu ya Wizara ya Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Uwekezaji

Ni kweli lipo deni la fidia la sh.milioni 27,250 096 kwa wakati huo ambao walioumia wanadai fidia zao ambazo zilishakubalika na kuidhinishwa kulipwa kisheria.Wafaidika ni wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambao huwa wanaumia wakati wa kazi..

Kiutaratibu fidia huwa inalipwa na idara ya wazee na ustawi wa jamii kupitia wizara husika kutokana na maingizo ya fedha za OC.Idara hii kwa sasa ipo wizara ya Afya Ustawi wa Jamii wazee Jinsia na Watoto.Wizara hili imehamisha rasmi deni hilo kwa barua no OR.KUU/P/W.S.110/VOL 11V /1 ya tarehe 8/2/2021.

Maelezo rasmi ya wizara hiyo ni kwamba deni hili limelipwa kwa asilimia ndoga sana hadi sasa ni mtu mmoja tu amekamilishiwa malipo yake na mmoja amelipwa sehemu tu ya malipo..(anadai 2,503,732 na amelipwa milioni moja) .taarifa hiyo pia imeeleza kwamba Wizara ya Afya imehakiki deni hilo na lipo katika vipaumbele vyake vya malipo na kuna matarajio makubwa ya kulipwa katika madeni inayodaiwa serikali hivi karibuni katika fedha ambazo zinakuja kulipa madeni ya ndani ya serikali.Ni imani yetu hatua hiyo itakamilika muda mfupi ujao.nambatanisha na orodha wa deni lililobakia la sh.25,241,949 ukitowa mbili zilizolipwa.

## Uchunguzi na Maependekezo ya Kamati ya PAC

Kwa kuwa madeni hayo muda mrefu kwa watumishi a Serikali, ni vyema kwa Srikali kulingalia suala hilo kwa moyo wa huruma.

### 3.7 FUNGU S 05 WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO ( WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO)

#### Taarifa ya Mapato

Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 255,063,000 kutoka katika taasisi za wizara katika kipindi cha mwaka 2019/2020.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 wizara ilikusanya jumla ya shilingi 122,443,900 sawa na asilimia 48 ya makadirio.

#### Majibu ya Wizara ya Habari, Vijana , Utamaduni na Michezo

Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa, na Michezo ilikadiriwa kukusanya jumla ya **shilingi 255,063,000/-** kupitia vyanzo mbali mbali vya mapato kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya **shilingi 122,443,900/-** zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia **48** ya makadirio, kama inavyoonekan akatika jadweli lifuatalo:-

MAKADIRIO NA MAPATO HALISI KWA MWAKA 2019/2020

| KASMA | MAELEZO | MAKADIRIO KWA MWAKA 2019/2020 | MAPATO HALISI 2019/2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| | Kibali cha ngoma | 230,000,000 | 120,638,700 | 52 |
| | Mauzo ya Machapisho | 16,126,000 | 1,850,200 | 12 |
| | Afisi kuu Pemba | 8,937,000 | 7,230,500 | 80 |
| | Jumla | 255,063,000 | 122,443,900 | 48 |

#### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilitaka kujua kwanini asilimia ya kibali cha ngoma kimeshuka asilimia 52 na pia ukusanyaji wake ni Unguja na Pemba.hapo mwanzo fedha zote zilikuwa zina account mmoja ilikuwa Unguja tu,vile vile kamati ilihoji fedha ambazo zinzokusanywa na mashekha zinalipiwa banka moja kwa moja na zinaingia mfuko mkuu wa Serikali , lakini saiv tayari Wizara imeshaanza kutumia account mbili Unguja na Pemba . hata hivyo kuna changamoto kubwa Wizara ya Fedha wanakadiria makadirio makubwa bila kuzingatia uhalisia wa chanzo cha mapato.

Taarifa ya Matumizi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilikadiria kutumia jumla ya shilingi 5,691,200,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 4,000,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020, wizara imeingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 4,820,665,422 ni kwa ajili ya kazi za kawaida, ikiwa ni sawa na asilimia 84 ya makadirio na jumla ya shilingi 1,393,994,916 kwa ajili ya kazi za maendeleo, ikiwa ni sawa na asilimia 34.8 ya makadirio.

Majibu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamadunzi na Michezo

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Vijana ilipanga kutumia jumla ya **shilingi 9,691,200,000/-** kati ya hizo shilingi 1,800,400,000/- kwa ajili ya kazi za kawaida,**shilingi 2,874,100,000/-**kwa ajili ya mishahara,**shilingi 1,016,700,000/- kwa** ajili ya ruzuku na **shilingi 4,000,000,000/-** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Wizara ilipata jumla ya **shilingi 6,214,680,338/-** kati ya hizo **shilingi 1,320,921,892/-** ni kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia **73**,**shilingi 2,737,998,200/-**kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia **95** ,**shilingi 761,765,330/- kwa** ajili ya ruzuku sawa na asilimia **75** na **shilingi 1,393,994,916/-**kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia **35** ya makadirio.

*Fedha za kazi za matumizi ya kawaida*

| SN | MAELEZO | MAKADIRIO | UHALISIA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mishahara | 1,800,400,000 | 2,737,998,200 | 95 |
| 2. | Matumizi Mengineo OC | 2,874,100,000 | 1,320,921,892 | 73 |
| 3. | Ruzuku ya OC | 1,016,700,000 | 761,765,330 | 75 |
| | **JUMLA** | **5,691,200,000** | **4,820,685,422** | **85** |

*Matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo nambari*

| SN | MAELEZO | MAKADIRIO | HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 2. | Mradi wa Ajira kwa vijana | 2,000,000,000 | - | - |
| 3. | Mradi wa Uimarishaji viwanja vya Michezo | 2,000,000,000 | 1,393,994,916 | 70 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | JUMLA | 4,000,000,000 | 1,393,994,916 | 35 |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imehoji kuhusiana na fedha za miradi ya maendeleo, katika mradi wa Uimarishaji viwanja vya michezo kamati ilitaka kujua matumizi yake kwa upana yametumika vipi , kiwanja cha Amani kiliwekwa nyasi bandia Fedha zote zilitumika hapa, viwanja vidogo vidogo vya wilaya hawakupata fedha .hata hivyo kamati ilipata fursu ya kuona vilelezo vya malipo hayo

5.14.1.1 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 78,936,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 78,936,000 zimelipwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali, lakini baadhi ya vielelezo vya malipo hayo havikuweza kupatikana kwa ukaguzi ili kuthibitisha uhalali wa malipo husika.

Kukosekana kwa baadhi ya nyaraka kwenye malipo yaliyofanyika ni kwenda kinyume na Kifungu Nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016. Malipo yenyewe ni kama yafuatayo:-

Majibu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Wizara ilikiri kuwa wakati ukaguzi unafanyika vielelezo husika vilikosekana kwa mara ya kwanza baadae waliporudi kwa ajili ya uhakiki wa mara ya pili vielelezo vyote vilikuwa tayari vimeshapatikana.

Uchunguzi wa Kamti ya PAC

Kamati ya PAC imethipitisha kweli wakati ukaguzi unafanyika vielelezo husika vilikosekana kwa mara ya kwanza hii imetokana na Afisa Masuuli alikuwa kapatauhamisho ,kwa hiyo vielelezo havikuweza kupatika lakini baadaye waliporudi kwa ajili ya uhakiki wa mara ya pili vielelezo vyote vilipatikana , hata hivyo kamati ya PAC ilipata fursa ya kukagua baadhi ya vilelezo kama risiti ya wakala wa Majengo na baadhi ya risiti na hati za malipo

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri endapo afisa Masuuli atakapoondoka atafutwe Mtendaji mwengine wa kufanya kazi zilizobaki

5.14.12 Kasoro katika utekelezaji wa maradi wa kilimo kwa mwaka wa fedha 2019/2020

Ukaguzi ulibaini Mapungufu katika ufungaji wa mkataba ikiwemo haya yafyatayo:-

a) Kukosekana kwa tangazo la zabuni na maelezo kwa waomba zabuni.

Majibu ya Wizara Habari, Vijana , Utamaduni na Michezo

kutokana na upekee wa kazi husika na uharaka wake,na kuchelewa kuingizwa fedha kwa kipindi hicho Wizara iliamua kutumia kifungu cha 71(1)(a) na (c),(2) na (3) (a) na (b) cha restricted bidding, kama inavyoagiza Sheria namba 11 ya 2016, Ili kupata wazabuni wakufanya kazi inayokusudiwa. Kampuni tatu ziliombwa kufanya kazi hii, ambayo ni JKU, PLUMBING & WATER WORKS na THE COASTAL YOUTH CENTRE PROJECT STONE TOWN YOUTHCENTRE.

b) Mkandarasi aliyepewa kazi hiyo hana uzoefu na utaalamu katika uchimbaji wa visima.

Majibu ya Wizara

Wizara ilitoa kazi hiyo kwa kumpa Mkandarsi mmoja ambae ni JKU baada ya uzoefu kuonesha kwamba kazi hizo zimekuwa zikifanywa na JKU, na kazi hiyo ilijumuisha uchimbaji wa Visima pamoja ujenzi wa Mahema. Lakini pia kwa mujibu wa mkataba kutoa “sub-contract” sio kosa kisheria, lakini hilo ni jukumu la JKU iwapo ataamua kutoa “sub-contract”. Aidha. Wizara iliwasiliana na ZAWA ili kusimamia kazi ya uchimbaji wa Visima. Lakini hata hivyo, Wizara imekua ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara na kila pale inapobaini kuna mapungufu au changamoto, pande husika zinakaa pamoja kuzitatua changamoto hizo.

c) Mkataba ulikosa nyaraka muhimu kama vile masharti ya mkataba , maelezo yakina ya jinsi ya kutekeleza mkataba, dodoso la bei n.k.

Majibu ya Wizara

Masharti muhimu ya mkataba baina ya Wizara na JKU yanaorodheshwa katika tamko la mkataba “Preamble” ambalo hupatikana katika maelezo ya awali ya mkataba kabla ya wahusika wa pande mbili kuweka sahihi zao ambalo pia linataja na kiasi cha fedha kitakachotumika katika kazi iliyotolewa. Aidha, kifungu cha 16 cha “GCC” pamoja na kifungu cha 3 “SCC” vinatoa ufafanuzi huo juu ya jinsi gani mkataba utekelezwe.

d) Kutotumia kifungu cha fidia kwa kuchelewa na kutokukamilisha kwa matakwa ya mkataba.

Majibu ya Wizara

Kifungu cha 51.1 cha masharti maalumu ya mkataba na kifungu 21 cha masharti mahsusi pia mkataba kinamtaka mwajiri kutoza asilimia 0.1 ya malipo yote ya kazi, lakini kutokana na tatizo la ukosefu wa fedha kwa JKU, kwa kua kazi hiyo inafanywa na taasisi ya Serikali na kutokana na uingiaji wa fedha, Wizara haikuona haja ya kuwatoza fedha hizo na imekua mara kwa mara ikifanya vikao ili kutatua changamoto zinazojitokeza katika mkataba.

e) Kutokuwepo kwa vikao katika eneo la mradi kutathmini utekelezaji wa mradi.

Majibu ya Wizara

Vikao vya mara kwa mara vimekua vikifanyika kila pale panapoonekana iko haja ya kufanya hivyo. Baadhi ya Ripoti na Vikao vilivyokuwa vikifanyika vimehifadhiwa. Rejea Ripoti/ Barua kadhaa kwa uhakiki zaidi kama vile barua yenye kumbukumbu ZAWA/U.10/10/26 ya tarehe 21/07/2020, WVUSM/PV.25VOL.1/176 ya tarehe 14/07/2020, WVUSM/PV.25/I/VOL.I/215 ya tarehe 18/11/2020, WVUSM/PV.25/I/214 pamoja na kikao cha mwisho kilifanyika siku ya tarehe 16/10/2020 n.k.

f) Kutokuwepo kwa uhakikisho wa ubora katika utekelezaji wa mkataba.

Majibu ya Wizara

Katika kuhakikisha kuwa Mkandarasi anaepewa kazi anatimiza vigezo na ataifanya kwa umahiri, Bodi ya Zabuni ya Wizara iliunda Kamati ya Tathmini ili kupitia nyaraka za Kampuni 3 ambazo zimeomba kuifanya kazi iliyotarajiwa. Hivyo basi, baada ya Bodi ya Zabuni kuridhia Tathmini iliyofanywa na Kamnati ya Tathmini ilishauri kazi hiyo, ipewe Taasisi ya Serikali ambayo ni JKU, na miongoni mwa sababu kuu ni kwamba JKU katika kipindi hicho ilikua na uzoefu mkubwa wa kufanya kazi iliyotakiwa kufanywa

g) Kazi zilizokamilika kama uchimbaji visima,kusambaza maji,ujengaji wa green house ,hazikufanyiwa tathmini kuona kama zimekidhi matakwa ya utekelezaji aliyopewa mkandarasi

Majibu ya Wizara

Tathmini ya ubora wa kazi umekua ukifanyiaka kila baada ya muda na kabla ya Mkandarasi kukabidhi kazi, Wizara pamoja na Washauri wake ambao ni ZAWA, ZECO pamoja na Wizara ya Kilimo wamekua wakiambatana katika ukaguzi huo.

h) Taarifa za utekelezaji wa mradi hazikuandaliwa

Majibu ya Wizara

Taarifa za utekelezaji wa miradi zilikua zikitolewa kila baada ya kukamilika kwa ziara na taarifa hizo zinapatikana kwenye kitabu cha mradi.

i) Mkataba haukuainisha uwepo wa msimamizi (consultancy),hivyo taarifa za msimamizi wa mradi hazikutayarishwa.

Majibu ya Wizara

Rejea katika kifungu cha 1.1 paragrafu namba 35 kimewataja wasimamizi wa Mradi. Aidha, rejea barua yenye kumbukumbu nambari WVUSM/BZ/VOL.I/14 ya taerehe 11/10/2019 imewataja wasimamizi wa mradi ambao ni;-

1. Mwakilishi kutoka Wizara ya Kilimo;
2. Mamlaka ya Maji ZAWA;
3. Msimamizi wa Mradi; na
4. Mkuu wa Miradi wa JKU.

j) Mkataba uliofungwa baina ya wizara na JKU haujapelekwa kwa mwanasheria mkuu kinyume na sharia namabari 11 ya 2016 ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma Zanzibar

Majibu ya Wizara

Mkataba huo ulipelekwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na barua yenye kumbukumbu nambari WVUSM/MM/22/8/VOL.1/11 YA TAREHE 4/10/2019 ilipelekwa na kujibiwa na barua yenye kumbukumbu L.D /784/VOL,1/20 ya tarehe 7/10/2019imejibiwa ili Wizara iendelee na hatua.

k) Kwa mujibu wa mkataba kazi hiyo ilikua ifanywe kwa siku 90, hadi tunamaliza ukaguzi na kutembelea maeneo ya mradi huo bado kazi za visima hazipo katika hali ya kuridhisha na kupata thamani halisi ya fedha iliyotumika.

Majibu ya Wizara

Kuchelewa kukamilika kwa mradi huu kulichangiwa na sababu mbili kuu;-

a. Kubadilika kwa hali ya hewa katika kipindi ambacho mradi unaanza kutekelezwa. Kipindi hicho mvua zilikua ni nyingi majira yalibadilika na kupelekea wingi wa mvua. Kwa upande wa uchimbaji visima vya

maji kina cha maji (water table) kilikua juu (hali hii haikutoa uhakika wa maji kuwepo katika pahala husika kwa vile kiwango na kina cha maji kilikua juu kwa kipindi hiki cha mvua) hivyo kupelekea kuona yamefikiwa maji ya kutosheleza. Hata hivyo baada ya kumalizika kipindi cha mvua na kuanza kipindi cha jua kina cha maji kilishuka sana na baadhi ya visima hivyo kukauka maji na hii ilikua ni matokeo ya ukweli kwamba visima vilichimbwa wakati wa mvua.

b. Mripuko wa maradhi ya COVID 19 kulisababisha kuchelewa kukamilika kwa uchimbaji wa visima na ujenzi wa mahema. Wizara ilichukua hatua za kukaa na mkandarasi ili kurekebisha kasoro zilizojitokeza na idadi ya visima mpaka kipindi inaandaliwa ripoti hii tayari vinafanya kazi. Hata hoivyo kwa visima ambavyo bado havijakamilika ni jukumu la Mkandarasi kuhakikisha anakamilisha kazi hiyo kwa gharama yake.

l) Kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu (feasibility study) kabla ya uchimbaji wa visima katika maeneo yaliyochimbwa visima.

Majibu ya Wizara

Ikumbukwe kuwa katika Mradi wa Ajira kwa Vijana, Wizara ya Kilimo ndiyo iliyopendekeza na kuandaa Kitabu cha Mradi “Project Documents ya ZANZIBAR YOUTH EMPLOYMENT. Kabrasha hilo lilionesha na kupendekeza maeneo yatakayochimbwa visima pamaoja na kujengwa kwa mahema. Ripoti ya uchambuzi wa vikundi vya vijana katika sekta ya kilimo ilioandaliwa na Wizara ya Kilimo imependekeza na kutaja maeneo yatakayotumika kujenga mahema na kuchimbwa visima.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilipitia nyaraka mbalimbali za mradi huu na kufanya ziara mbali mbali katika maeneo ya Mradi huu ya Unguja na Pemba ili ujionea hali halisi ya utekelezaji wa Mradi. Katika uchunguzi wake Kamati imebaini dosari zifuatazo:-

i. Kutokamilika kwa Mradi
ii. Zaidi ya asilimia 90 Visima na Vitalu nyumba havifanyi kazi
iii. Ukiukwaju wa masharti ya mkataba ambapo fedha zote za Mradi zimeshalipwa wakati mradi hajakamilika na haujakabidhiwa pamoja na kukiukwa vipengele vya ujenzi vya Mkataba huo.
iv. Mradi wa uchimbaji Visima kupewa Taasisi isiyokuwa na utaalam wa kazi hiyo.(badala ya kupewa ZAWA wamepewa JKU).

v. Mradi kuonekana kutofanyiwa upembuzi yakinifu kwa umakini (Mradi umeainisha kuchimbwa visima vya makalbi wakati baadhi ya maeneo hayafai kuchimbwa visima vya aina hiyo hata ujenzi wa vitalu nyumba havikuzingatia vigezo vya kitaalamu).

Taarifa ya kina juu ya ziara ya Kamati ya PAC katika maeneo ya Mradi wa Kilimo wa Ajira kwa Vijana.

Kamati ya PAC imefanya ziara mbalimbali katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba ili kujiridhisha katika utekelezaji wa mradi huo kwa kupitia maeneo mbali mbali. Kwa upande wa Unguja kamati ya PAC imefanya ziara katika maeneo mbalimbali yakiwemo

- Pangatupu
- Pangeni
- Donge Mchangani
- Kitogani na Makundichi
- Dimani,Fuoni,Kipondeni na Koani

Kutokana na ziara zilizofanyika baina ya Kamati ya PAC na Wizara ya Habari,Vijana,Utamaduni na Michezo Kamati imebaini mambo mbali mbali ambayo yamepelekea kushindwa kwa mradi wa Kilimo kama yafuatayo:-

- Kamati imebaini takriban ya visima vyote vya Unguja vilivotembelewa havitoi maji kwa sababu wamepewa JKU ambao waliopewa dhamana ya kuchimba visima kamati imebani kuwa hawakuwashirikisha watu wa ZAWA kwa ajili ya kupata utaalum zaidi na hata hivyo Kamati imebaini JKU hawakufanya utafiti wa kina ikiwemo visima havitoko maji,umeme, haujakamilika,minara ya matangi ya maji matofali yake hayakulaza na kima chake kifupi sana na makalbi ambayo yamekusudiwa kuwekwa kwenye visima ni 17 lakini kamati imebaini visima vingi makalbi hayakukamilika.
- Kwa upande wa Vitalu nyumba ( Green House) kamati ya PAC imebaini kuwa vitalu nyumba asilimia 99 havifanyi kazi, hali hii imeipelekea Wizara pamoja na JKU kushindwa kufanya kazi katika katika maeneo ya kujenga Vitalu nyumba . Katika vitalu nyumba 9green house) mambo ambayo yamebainika ni kama ifuatavyo:-
    I. Mapaa mengi ya vitalu yameezuka
    II. Baadhi ya nguzo za vitalku nyumba zimeliwa na mchwa

Kwa upande wa ziara ya Pemba Kamati imepitia vitalu nyuma na visima tofauti ikiwemo vifuatavyo:-

- Tumbe na Shumba Viamboni-Micheweni
- Hatukati Tamaa-Ngwachani
- Mjini Ole na Kibokoni-Chake Chake

Kutoka na ziara iliofanya Kamati ya PAC imebaini mambo yafuatayo:-

- Vitalu nyumba asilimia 99 havifanyika kazi

Kutokana na yote yaote hayo yaliyobainika. Kamati ya PAC haikuridhika na matumizi ya fedha ya mradi huu wa Kilimo uliolenga ajira kwa vijana kwa kuwa hadi sasa bado mradi haujaleta tija iliyokusudiwa na maeneo mengi yaliyolengwa katika mradi huu kushindwa kufanya kazi ipasavyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kwa kuwa shilingi 528,612,000 zilizofujwa ni fedha nyingi za Serikali Kamati ya PAC inashauri Serikali kuwachukulia hatua kwa wale wote waliohusika kwa namna moja au nyengine na uharibufu na ufujaji huo mkubwa wa fedha za Serikali.

ii. Kamati ya PAC inashauri Wizara na Taasisi za Serikali kufanya utafiti wa kutosha (due diligence) kwa Kampuni au Taasisi kabla hazijawapa kazi ili kujua uwezo wa kampuni hizo kwa lengo la kuepusha kuitia hasara Serikali.

TUME YA UTANGAZAJI

Hoja Namba 5.15.1.1 HOJA: UWEPO WA MADENI YA MUDA MREFU SHS. 29,697,710/-

Majbu ya Tume ya Utangazaji

Tume ya Utangazaji Zanzibar inakiri uwepo wa madeni ya muda mrefu inayodaiwa nawatoa huduma mbali mbali, kutokana na ufanyaji kazi wa kila siku Tume hulazimika kutumia njia ya mkopo kulingana na aina ya huduma na uharaka wa utumiaji wa huduma kwa uendeshaji wa ofisi. Aidha, madeni hayo yamekuwa ya muda mrefu kutokana na upatikanaji wa mdogo wa fedha za Ruzuku ambapo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Tume ilipangiwa kutumia jumla ya shilingi 108,200,000/-wakati fedha halisi zilizopatikana hadi kufikia June, 2020 zilikuwa ni ya shilingi85,550,864/- sawa na 79% ya fedha zote, hali inayochangia kutokulipwa madeni kwa wakati.

Hata hivyo, baadhi madeni hayo kwa sasa tayari yameshalipwa kwa jumla ya shilingi 14,183,238/-na kufanya bakaa ya deni kuwashilingi 15,514,472/-

Madeni yaliyobaki na Watoa huduma ni kama yafuatayo:

| S/NO | Watoa Huduma | Jumla ya Fedha (shs) |
|---|---|---|
| 1 | Zolla Stationary Center | 4,000,000 |
| 2 | One 2 One Ltd | 2,277,400 |
| 3 | Sahara Shopping Centre | 60,530 |
| 4 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | 1,200,000 |
| 5 | New Home Furniture | 3,186,000 |
| 6 | Saleh decoration | 4,791,242 |
| | Jumla | 15,515,172 |

Madeni yaliyolipwa

| S/NO | Watoa Huduma | Jumla ya Fedha (shs) |
|---|---|---|
| 1 | Zolla Stationary Center | 2,000,000 |
| 3 | Sahara Shopping Centre | 194,350 |
| 5 | Budda Auto Parts | 183,000 |
| 6 | Naj Global Planet Ltd | 10,780,000 |
| | Awami general Store | 1,025,188 |
| | Jumla | 14,182,538 |

Uchunguzi Kamati ya PAC

Kutokana na mwenendo wa ulipaji wa madeni imeonekana kuwa na Taasisi zake hajajiwekea utaratibu mzuri wa ulipaji wa madeni.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara na Taasisi zake Iweke utaratibu wa kuweka asilimia fulani ya fedha ya kulipa madeni kutokana fedha za na O.C inavyoingizwa

5.15.1.2 HOJA: KUTOKUWEPO KWA UFANISI KATIKA UKUSANYAJI WA MAPATO SHILINGI 7,800,000 HESABU NAMBARI 0404100000 KM/WHUMK MAPATO NA HESABU NAMBARI 0521030000 MAKUMBUSHO USD 206,769/-

Majibu ya Tume ya Utangazaji

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, Tume ya Utangazaji Zanzibar ilitakiwa kukusanya fedha za mapato **shilingi 7,800,000/-** na imefanikiwa kukusanya **shilingi 5,300,000/-** sawa na asilimia **68**, zinazotokana na vituo vyake kumi na moja ilivyokuwa ikividai na vituo vitano bado havijakamilisha madeni yao. Vituo vyenyewe ni hivi vifuatavyo:-

Vituo vilivyokamilisha malipo

| S/NO | KITUO | MALIPO Tshs |
|---|---|---|
| 1 | Mtegani Fm | 500,000 |
| 2 | Redio Jamii Micheweni | 300,000 |
| 3 | Redio Jamii Mkoani | 500,000 |
| 4 | Idara ya Habari Maelezo | 500,000 |
| 5 | KTv Online | 500,000 |
| 6 | Mubashara Media Net work | 500,000 |
| 7 | Zanznews .com | 500,000 |
| 8 | Alfatah Online tv | 500,000 |
| 9 | Jumuiya ya maimau | 500,000 |
| 10 | Annour Afrika TV | 500,000 |
| 11 | Pemba to day online | 500,000 |
| | Jumla | 5,300,000 |

Vituo ambavyo havijalipa madeni

| S/NO | KITUO | DENI |
|---|---|---|
| 1 | Radio Jamii Tumbatu | 500,000 |
| 2 | State House | 500,000 |
| 3 | Zan online Technology | 500,000 |
| 4 | Pemba TV | 500,000 |
| 5 | Noor Mustafah Online Tv | 500,000 |
| | JUMLA | 2,500,000 |

Kwa upande wa madeni ya **USD 206,769**, vituo kumi na saba vilivyokuwa vikidaiwa tayari vimekamilisha madeni yao, vituo vitano vimepunguza madeni yao na vituo vitano havijalipa kabisa madeni yao. Orodha ya vituo hivyo ni kama ifuatayo;

Vituo vilivyokamilisha malipo

| S/NO | KITUO | MALIPO(USD) |
| --- | --- | --- |
| 1 | BOMBA FM RADIO | 4,000 |
| 2 | AM 24 | 4,000 |
| 3 | RADIO MARIA | 3,000 |
| 4 | ADHANA FM RADIO | 2,200 |
| 5 | VOICE OF ISTIQAMA | 3,000 |
| 6 | ASSALAM FM RADIO | 2,000 |
| 7 | AL NOOR FM | 1,000 |
| 8 | WASAFI FM | 2,000 |
| 9 | HITS FM RADIO | 2,000 |
| 10 | RADIO IMAAN | 1,000 |
| 11 | ZUKU | 8,000 |
| 12 | ZANZIBAR CABLE TV | 8,000 |
| 13 | STAR MEDIA | 4,000 |
| 14 | AZAM TV | 8,000 |
| 15 | ISLAND TV | 3,000 |
| 16 | TIFU TV | 1,400 |
| 17 | WASAFI TV | 1,500 |
| JUMLA | | 58,100 |

Vituo vilivyopunguza deni.

| S/NO | KITUO | KILICHOLIPWA(USD) | DENI LILOBAKI (USD) |
| --- | --- | --- | --- |
| 1 | COCONUT FM RADIO | 1,078 | 2,081 |
| 2 | COCONUT TV | 2,155 | 7,408 |
| 3 | Z-MUX | 6,000 | 13,000 |
| 4 | ZBC TV | 8,000 | 79,661 |
| 5 | SWAHIBA FM RADIO | 870 | 416 |
| JUMLA | | 18,103 | 102,566 |

Vituo ambavyo havijafanya malipo.

| S/NO | KITUO | DENI (USD) |
| --- | --- | --- |
| 1 | ZENJ FM RADIO | 3,000 |
| 2 | ZENJ DIGITAL TV | 12,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | CLOUDS PLUS TV | 1,500 |
| 4 | REDIO HABARI | 1,500 |
| 5 | BAHARI FM | 10,000 |
| JUMLA | | 28,000 |

Hivyo, ukubwa huo wa madeni ya Tume ya Utangazaji Zanzibar unasababishwa na madeni ya vituo vinavyomilikiwa na taasisi za Serikali ambavyo vinashindwa kulipa madeni kwa wakati na kusababisha ongezeko la madeni hayo kila mwaka.

BARAZA LA SANAA, SENSA YA FILAMU NA UTAMADUNI

Majibu ya Baraza la Sanaa

Hoja Namba 5.14.2.4 Sababu za kukosekana kwa vitabu vya kukusanyia mapato

Baraza la Sanaa limepokea hoja ya mkaguzi kuhusu kukosekana kwa baadhi ya vitabu vya kukusanyia mapato kipindi cha ukaguzi 2019/2020. Kukosekana kwa vitabu hivyo kunatokana na sababu ya kwanza ni pale Masheha wengi wanapoondoshwa madarakani au kustaafu kwao utunzaji wa vitabu huwa mdogo na sababu ya pili ni kufariki kwa baadhi ya Masheha ambako hupelekea upotevu wa baadhi ya vitabu vya makusanyo ya Mapato.

Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu linaendelea kuchukuwa jitihada za makusudi kwa kufuatilia vitabu kwa masheha ambao walihusika kwenye upotevu wa vitabu hivyo.

BARAZA LA KISWAHILI LA ZANZIBAR (BAKIZA)

Hoja namba 5.14.2.1 Makusanyo ya mapato ambayo stakbadhi zake hatukuziona shilingi 2,844,875/-.

Ukaguzi umebaini uwepo makusanyo ya mapato katika miezi tofauti kwenye daftari la fedha (cash book), ambayo stakabadhi zake hatukuziona wakati wa ukaguzi, kukosekana kwa stakabadhi hizo ukaguzi haukuweza kuthibitisha fedha halisi ilikusanywa kupitia makusanyo hayo. Hali hii ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nambari 12 ya mwaka 2016. Mapato ambayo stakabadhi zake hatujaziona ni kama ifuatavyo:-

: Makusanyo ya Mapato

| Namba | Tarehe ya Makusanyo | Kiasi Kilichorikodiwa(Shs) |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | 12/9/2019 | 65,000 |
| 2. | 26/9/2019 | 45,000 |
| 3. | 24/10/2019 | 45,000 |
| 4. | 25/10/2019 | 45,000 |
| 5. | 29/10/2019 | 79,874.63 |
| 6. | 4/11/2019 | 65,000 |
| 7. | 4/11/2019 | 45,000 |
| 8 | 7/11/2019 | 45,000 |
| 9. | 7/11/2019 | 45,000 |
| 10. | 13/11/2019 | 65,000 |
| 11. | 13/11/2019 | 65,000 |
| 12. | 22/11/2019 | 45,000 |
| 13. | 23/11/2019 | 65,000 |
| 14. | 26/11/2019 | 45,000 |
| 15. | 10/12/2019 | 45,000 |
| 16. | 10/12/2019 | 45,000 |
| 17. | 10/12/2019 | 45,000 |
| 18. | 10/12/2019 | 45,000 |
| 19. | 10/12/2019 | 1,500,000 |
| 20. | 12/12/2019 | 45,000 |
| 21. | 12/12/2019 | 45,000 |
| 22. | 14/12/2019 | 65,000 |
| 23. | 16/12/2019 | 45,000 |
| 24. | 17/12/2019 | 45,000 |
| 25. | 17/12/2019 | 45,000 |
| 26. | 17/12/2019 | 45,000 |
| 27. | 18/12/2019 | 65,000 |
| | Jumla | 2,844,875 |

Majibu ya BAKIZA

Fedha hizi zilizotajwa kwenye hoja hii zilikuwa ni fedha za ada ya kongamano ambazo hulipwa moja kwa moja kwenye akaunti ya BAKIZA na sio akaunti ya mapato. Kwa hivyo hapo mwanzo hatukuziainisha kama fedha za mapato na wala hatukupata maelekezo yoyote ya kuwa pesa hizo ziingie kwenye mfuko wa mapato kwakuwa lengo lake ilikuwa ni kufanyia kongamano. Baada ya kushauriwa na wakaguzi wa nje fedha hizo tumeanza kuziingiza kwenye mfuko wa mapato kuanzia mwaka 2020/2021. Aidha, maelezo ya hesabu ya benki (bank statement) inayoonesha mtiririko wa fedha hizo za ada ya kongamano zilizoingia kwenye namba ya hesabu ya BAKIZA ipo kwa ajili ya uthibitisho.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilipata ufafanuzi wa kina kuhusiana na hoja hii kuwa fedha hizo za makusanyo zilikuwa ni fedha za ada ya kongamano ambazo hulipwa moja kwa moja kwenye akaunti ya BAKIZA na sio akaunti ya mapato, kamati imebaini kuwa hapo mwanzo hawakuainishiwa kama fedha za mapato na wala hawakupata maelezo yoyote ya kuwa fedha hizo ziingizwe kwenye mfuko wa mapato kwa kuwa lengo lao lilikuwa ni kufanyia kongamano .

Hata hivyo Kamati imepata maelezo kuwa baada ya kushauriwa na wakaguzi wa nje tayari BAKIZA wameshaanza kuingiza kwenye mfuko wa mapato kuanzia mwaka 2020/2021 , Kamati imepata fursa ya kuona mtiririko wa fedha za ada ya kongamano zilizoingizwa kwenye akaunti ya BAKIZA. Vilevile Kamati ilitaka kujua kama kuna chanzo chengine cha mapato na kuelezwachanzo cha mapato wamesema kwa kupitia kuuza vitabu ila changamoto wanayoipata Watanzania hawana utamaduni wa kusoma vitabu hata hivyo bakiza wamejipanga kufungua maktaba ile wapate soko na pia wanajitaarisha kufungua skulina kamati ya PAC imeridhika na ufafanuzi uliotolewa kuhusu hoja hii.

### 5.15.4.2 Malipo yasiyo na vielelezo shilingi 56,920,000/-.

Ukaguzi umebaini kwamba 54,920,000 zimelipwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali, lakini vielelezo husika havikupatikana kwa ukaguzi, ili kuthibitisha uhalali wa malipo. Kukosekana kwa vielelezo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo yanaonekana katika jadweli lifuatalo:-

: Malipo Yasiyokuwa na Vielelezo

| Nambari ya Hati | Nambari ya Hundi | Kiasi (Shs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 26/9/2019 | 000467 | 595,000 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Marejesho ya matumizi ya vifaa vya magari SMZ 374A |
| 9/10/2019 | 000469 | 520,000 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Malipo kwa ajili ya kushiriki katika vipindi vya lugha yetu, vinavyorushwa katika Redio na TV. |
| 4/11/2019 | 000475 | 560,000 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Matumizi mbali mbali ya ofisi. |
| 22/11/2019 | 000478 | 800,000 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Malipo kwa ajili ya kukodi ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdulwakil. |
| 10/12/2019 | 000482 | 48,380,000 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Malipo kwa ajili ya Kongamano la tatu Kiswahili cha Kimataifa. |
| 10/1/2020 | 0000484 | 4,850,000 | BAKIZA | Malipo kwa ajili ya Kutayarisha Kikao cha Baraza la Kiswahili. |
| 29/1/2020 | 0000489 | 1,215,000 | Baraza la Kiswahili | Malipo kwa ajili ya Matengenezo ya gari SMZ 374A. |
| JUMLA | | 56,920,000 | | |

Majibu ya BAKIZA

Vielelezo vyote vilikuwepo lakini kwa bahati mbaya havikuweza kupatikana kwa wakati kutokana na mhasibu aliyekuwepo alikuwa ni mpya na miongoni mwa faili alizokabidhiwa haliwemo faili la Kongamano ambamo vilikuwemo vielelezo hivo. Baada ya jitihada kubwa na kumpata muhasibu aliyekuwepo alikuja kumuonyesha

mhasibu mpya faili ambalo lilikuwa limechanganyika na mafaili mengine.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC Iilibaini kuwa Mhasibu aliyeondoka aliondoka mwezi Juni 2020 na ilichukuwa wiki mbili hadi tatu kuletwa mhasibu mwengine, Hata hivyo, Kmati ay PAC ilipata nafasi ya kuvikagua vielelezo hivyo na kuridhika navyo.

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango isichelewe kupeleka mhasibu katika Taasisi za Serikali pale napohamishwa mhasibu.

## Hoja Na,ba 5.14.2.3 Uwepo wa vitabu vya muda mrefu ambavyo havijapatiwa soko vyenye thamani ya shilingi 210,620,000/-

Ukaguzi umebaini kwamba BAKIZA imechapisha vitabu vya aina mbali mbali, ambavyo vimehifadhiwa katika chumba kilichopo Uwanja wa Amani, sehemu inayotumiwa kama ofisi ya wasafishaji wa kiwanja hicho, sehemu ambayo si salama kwa uwekaji na utunzaji wa vitabu hivyo, ambavyo vinagharimu jumla ya shilingi 210,620,000.

Hata hivyo, ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uwepo wa idadi sahihi ya vitabu hivyo, kutokana na kukosa taarifa ya uingiaji na utokaji wa vitabu hivyo. Vitabu vilivyoonekana wakati wa ukaguzi ni kama ifuatavyo:-

: Vitabu Vilivyoonekana Wakati wa Ukaguzi

| Nambari | Wakati wa Ukaguzi | | Bei ya Kitabu | Kiasi cha Fedha (Shs) |
|---|---|---|---|---|
| | Vitabu Vilivyoonekana | Idadi ya Vitabu Viliyopo | | |
| 1. | Kamusi la Kiswahili Fasaha | Box55*180=9,900 | 17,000 | 168,300,000 |
| 2. | Kamusi la Lahaja za Kitumbatu | Box 3*110 = 330 | 10,000 | 3,300,000 |
| 3. | Kamusi la Lahaja za Kimakunduchi | Box4*110 = 440 | 10,000 | 4,400,000 |
| 4. | Kamusi la Lahaja za Kipemba | Box35*55 =1,925 | 12,000 | 23,100,000 |
| 5. | Mawasiliano ya Msingi Kiswahili kwa Wageni | Box12* 80 =960 | 12,000 | 11,520,000 |
| Jumla | | | | 210,620,000 |

## Majibu ya BAKIZA

Katika kikao maalum kilichofanyika Ikulu baina ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar wa awamu ya saba na Baraza la Kiswahili tarehe 07/08/2017, mheshimiwa Rais aliliagiza Baraza la Kiswahili kugawa makamusi yote kwa taasisi za Serikali, vyuo na skuli za Serikali ili yatumike na aliahidi kuwa atalipia gharama za makamusi

yote yaliyokuwepo kwa wakati huo. Agizo hilo lilikuja baada wa Mwenyekiti wa BAKIZA wa wakati huo kumueleza Mheshimiwa Rais kuwa kuna changamoyo ya wananchi kutokununua vitabu hususan makamusi. Kwa bahati makamusi yaligaiwa lakini hayakulipwa na kutokana na mchakato wa kulipa kuwa mgumu hatukuweza kutoa makamusi yote.

Vile vile, tunavyo vitabu vyengine lakini uuzaji wake unasuasua kutokana na watu hawana utamaduni wa kununua na kusoma vitabu. Watu wachache hutumia maktaba na wengine hutoa nakla kwa ajili ya kukidhi shida zao matokeo yake kupelekea soko la vitabu kuwa ni gumu kwa hapa kwetu.

Hata hivyo, Baraza la Kiswahili Zanzibar linaendelea kusambaza vitabu katika maduka ya vitabu yaliyopo Zanzibar, kwenye maonyesho, Matamasha na Makongamano yanayofanyika Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Vitabu vya Baraza la Kiswahili Zanzibar limehifadhi vitabu katika chumba maalum katika uwanja wa Amani tokea mwaka 2010 ambapo chumba hicho hakikutumika kwa ajili ya shughuli zozote za kiofisi zaidi ya kuhifadhi vitabu. Hivyo Baraza litaendelea kuhakikisha vitabu vinaendelea kuhifadhiwa maeneo salama katika chumba hicho.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini baada vitabu kukaa muda mrefu Mheshima Raisi wa Zanzibar wa awamu ya saba na Baraza la Kiswahili tarehe 07/08/2017, Mheshimiwa Rais aliagiza Baraza la Kiswahili kugawa makamusi yote kwa taasisi za Serikali,vyuo na skuli za Serikali ili yatumike na aliahidi atalipia gharama za makamusi yote yaliyokuwepo kwa wakati huo.kamati ilitaka kujua kama kuna barua yoyote inayothibitisha agizo hilo.na kuelezwa kuwa hakuna barua yoyote iliyothibitisha kikao hicho na agizo hilo lilikuja baada ya mwenyekiti wa BAKIZA wakati huo kumeelezea Mheshima Raisi kuna changamoto ya wananchi kutokununua vitabu hususan makamusi .kwa hiyo ilikuwa ni agizo maaluma .

Kamati ya PAC ilitaka kujua hoja ya kuhifadhiwa katika chumba kilicho po chumba cha Amani sehemu iliyotumiwa kama ofisi ya wasafishaji wa kiwanja hicho , BAKIZA inasema kuwa n waliambiwa na MHE Horoun kipindi hicho alikuwan Wazir wa Elimu waviweke ndani ya uwanja wa Amani na vipo sehemu salama na kama hicho chumba wanatumia wasafisha basi watakuwa wanaenda kinyume na utaratibu na kama BAKIZA hawana taarifa hiyo ili wameahidi mbele ya kamati kuifanyia kazi hoja hii .

Hata hivyo Kamati ya PAC pia ilitaka kujua hoja ya mkaguzi kushindwa kuthipitisha uwepo wa idadi sahihi ya vitabu hivyo kutokana na kukosekana taarifa ya uingiaji na utoaji wa vitabu hivyo hii imetokea, na ilielezwa kuwa kwa wakati ule kulikuwa hakuna mtu wa store, baada ya kupata mtu wa store tayari kumbukumbu zipo vizuri na kamati imepata kuona baadhi ya store leger na kuridhika

## wa Kamati ya PAC

Aidha, Kamati ya PAC ilifanya ziara ya kuona uhifadhi wa vitabu hivyo na kubaini yafuatayo:-

i. Vitabu vimehifadhiwa katika maboksi kwa mida mrefu na baadhi ya maboksi hayo yameshaanza kufanya unyevu ulioanaza kuharibu vitabu hivo
ii. Hali ya joto iliyopo inaweza kuharibu viatbu hivyo,.

iii. BAKIZA hawana duka husambaza madukani kwa kushirikiana na wauza maduka.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. BAKIZA ifanye utaratibu wa kupata sehemu kuuzia kamusi kwa mfano katika mahoteli ya kitalii na nyenginezo
ii. BAKIZA iweke shelves maalum za kuwekea vitabu kwa kuwa kuweka vitabu katika maboksi kwa muda m,refu ni hatari
iii. BAKIZA ifanye uataratibu wa kujitanga zaidi ikiwa ni pamoja na kujenga ushirikiano na Vyuo vya ndani na nje ya Zanzibar vinavyosomesha Kiswahili

IDARA YA MICHEZO

5.14.2.5 Madeni ya kodi ambayo hayajalipwa shilingi 9,900,000/-

Ukaguzi umebaini kwamba Uwanja wa Amani unakodisha vyumba kwa taasisi za Serikali na binafsi, jumla ya shilingi 9,900,000 hazikuweza kulipwa na taasisi hizo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Hali hii inapelekea kiasi kikubwa cha fedha kushindwa kupatikana kwa wakati, hivyo kukwamisha mipango ya shughuli za Uwanja wa Amani kutotekelezeka kama ilivyokusudiwa. Madeni hayo ni kama ifuatavyo:-

Madeni Ambayo Hayajalipwa

| Namba | Taasisi | Idadi ya Vyumba | Idadi ya Miezi/mwaka | Kiasi cha Deni (Shs) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | UWAIDAMAZA | 1 | Mwezi-9 | 1,050,000 |
| 2. | Riadha (ZAAA) | 1 | Mwezi-9 | 450,000 |
| 3. | Ikulu | 1 | Mwezi-9 | 450,000 |
| 4. | Zanzibar Football Federation (ZFF) | 12 | Miaka-5 | 7,950,000 |
| Jumla | | | | 9,900,000 |

Majibu ya Wizara

Idara ya Michezo kupitia kitengo cha Uwanja wa Amaan inakiri kupokea tarifa ya Mkaguzi wa Nje wa Hesabu za serikali dhida ya wapangaji waliotajwa katika taarifa yake hiyo. Katika kufuatilia na kuhakikisha deni hilo linalipwa Uongozi wa Idara ya Michezo umechukua hatua mbalimbali za kuwasiliana nao kwa lengo na dhamira ya kuwakumbusha na kuwataka waweze kulipia gharama za kodi ya vyumba hivyo ambavyo wanavitumia kwa ajili ya shughuli zao mbalimbali. Miongoni mwa hatua hizo ni kuwaita kwenye kikao na kuwaeleza umuhimu wa kufanya malipo kwani ni njia moja ya kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa mikataba waliyopatiwa pamoja na kuwaandikia barua yenye lengo la kuwataka walipie kodi na kumbukumbu zao zote zipo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilitaka ufafanunuzi wa kina kuhusiana na hoja hii Idara ya Michezo kupitia kitengo cha Uwanja wa Amani inakiri kweli kuwepo kwa madeni ambayo hayajalipwa. Jitihada walizozichukua madeni yanalipwa na ZFF kwa kupitia kitengo cha uwezeshaji wanalipa madeni hayo na jitihada nyengine ni kama zilivotajwa kwenye majibu ya Idara ya Michezo.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati inashauri Idara ya Michezo wajitahidi deni limalize

### Hoja Namba 5.14.2.6 Limbikizo la deni la uwanja wa amani shilingi 48,449,975.87/-

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa deni la muda mrefu la Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) kwa ajili ya matumizi ya umeme katika Uwanja wa Amani, jumla ya shilingi 48,449,975.87, kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba ZECO/28/2/VOL.2020/08/506 ya1/9/2020, hadi tunamaliza ukaguzi deni hilo halijalipwa.

### Majibu ya Wizara

Idara ya Michezo kupitia Ofisi zake za Uwanja wa Amaan inakiri kupokea deni kubwa kutoka ZECO (Electricity bill) ambalo lipo kwa muda mref kwa zaidi ya miaka kumi hivi sasa na kila siku zikosonga mbele deni hilo linaongezeka. Idara imechukua hatua kadhaa za kupunguza kuongezeka kwa deni hilo kila uchao ikiwemo kuweka Miter za Tukuza kwenye baadhi ya Ofisi pamoja na kuitaarifu Wizara kwa mazingatio na kufanya malipo juu ya ongezeko la deni hilo. Aidha mara zote deni hilo huzidi kuongezeka wakati wa shughuli muhimum za Kitaifa pamoja na uwashwaji wa ubao wa matangazo (Scoreboard) ambapo matumizi ya umeme huwa yanaongezeka zaidi.

### Uchunguzi Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imethibitisha kweli Idara ya Michezo kwa kupitia ofisi za Uwanja wa Amani inakiri kupokea deni kubwa kutoka ZECO,Kamati ya PAC imebaini mpaka saza hivi zimelipwa shiliingi milioni kumi katika deni hilo. Kamati ya PACilipitia vielelezo vya malipo ya deni hilo. Kamati pia ilielezwa kuwa watakuwa na utaratibu wa kulipa kila mwezi ili kupunguza deni. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na hatua walizozichukua

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inapendekaza deni lililobakia lilipwe kwa haraka

## WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO PEMBA. ( WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO - PEMBA)

### HOJA NAMBARI: 5.15.1.3: HATI ZA MALIPO ZILIZOKOSA VIELELEZO SHILINGI 6,680,00

### Majibu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo

Jumla ya shilingi 6,680,000/- ambazo zilionekana kukosa vielelezo vya malipo, zilitumika kwa matumizi mbali mbali ya Wizara Pemba kama inavyoonekana katika jaduweli la hapo chini;

| S/No | KIASI CHA FEDHA | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1 | 1,180,000/- | Fedha hizi zililipwa kwa ajili ya safari kikazi katika kipindi hicho kati ya Ofisa mdhamini wa awamu hio na Afisa Utumishi, katika utekelezaji wa majukumu yakiofisi. |
| 2 | 1,000,000/- | Fedha hizi zililipwa kwa ajili ya kuwapa zawadi ya mikoba wanafunzi wa skuli mbali mbali za msingi katika kuibua vipaji vya masualambali mbali ya utamaduni |
| 3 | 1,500,000/- | Fedha hizi zililipwa kwa ajili ya deni la Umeme katika Uwanja wa Gombani Stadium, ambalo lilikua la muda mrefu, hii ilisababishwa na miundombinu iliyowekwa kabla ya "KV Voltage" ambayo matumiziyake yalikua ni makubwa kulingana na uwezo halisi. |
| 4 | 2,000,000/- | Fedha hizi zililipwa kwa keshi kwa ajili ya malipo ya mafunzo ya makocha wa Mpira wa Miguu na Mikono |
| 5 | 1,000,000/- | Fedha hizi zililipwa kwa keshi kwa ajili ya chakulachaMakocha walioshiriki katika mafunzo , |

Vielelezo vyote vya malipo hayo vilikuepo ila havikupatikana kwa wakati muafaka sambamba na mahitaji ya mkaguzi kwa sababu zilizokuwa nje ya uwezo wetu. Miongoni mwa sababu hizo ni kama ifuatavyo:-

i. Ofisi yetu ilipata bahati ya kubadilishwa watendaji katika kitengo cha fedha kwa mwaka 2019/2020 hali ambayo ilichangia kwa kiasi kikubwa kutopatikana vielelezo hivyo kwa wakati. Mshika fedha ambae alihusika na matumizi hayo alishapangiwa kazi sehemu nyingine na kwa wakati huo alikuwa safarini Dar- ess Salaam kwa ajili ya kutatua matatizo binafsi ya kifamilia. Hata hivyo aliporejea alikamilisha utatuzi wa hoja hizo kwa upatikakanaji wa vielelezo husika.

ii. Mkaguzi baada ya kujiridhisha kwa mara ya kwanza katika hoja zake, aliahidi kurudi tena kwa mara ya mwisho kujiridhisha kasoro zilizobakia. Bila ya kutarajia wakaguzi hao hawakuja tena na sisi tukibaki na matumaini ya ujio wao kwa ajili ya kuwasilisha majibu ya kasoro zilizosalia.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC iliyachunguza majibu ya Wizara na hatimae haikuridhishwa na majibu hayo kutokana na sababu zifuatazo:-

1. Kuhamishwa kwa Mshika fedha sio sababu ya kutopatikana kwa vielelezo hivyo wakati wa ukaguzi, kwa kuwa vielelezo hivyo vilipaswa kuwepo katika Ofisi husika.

2. Kulingana na taratibu za Ukaguzi, kulikuwepo na muda wa kutosha usiopungua siku 30 za kuweza

kusawazisha dosari zilizobainika katika ukaguzi wa awali (management letter) ambapo Wizara ilishindwa kurekebisha dosari hii ya kukosekana kwa vielelezo husika.

3. Ingawa majibu ya Wizara yalieleza kuwa wakaguzi hawakufanya ukagazi wa mara ya pili (verification), Kutokana na ufafanuzi na nyaraka zilizotolewa na Mkaguzi kutoka Afisi ya Mdhibiti anaefuatana na Kamati ya PAC imebainika kuwa ukaguzi huo wa mara ya pili ulifanyika ambapo kwa mujibu wa matokeo ya ukaguzi wa awali (management letter) Wizara ilikuwa na maeneo 12 ya Hoja ya vielelezo, na baada ya Wakaguzi kupatiwa ufafanuzi na kuwasilishiwa vieielezo husika kwa ukaguzi wa mara ya pili (verification). Wakaguzi baada ya kuridhika na baadhi vielelezo , waliyaondoa maeneo 10 ya Hoja ya vielelezo na kubakia maeneo mawili ambayo yalikosa vieielezo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya mwisho ya ukaguzi. (Ripoti ya awali ya matokeo ya ukaguzi *managemnt letter* ya tarehe 12/11/2020 pamoja na barua ya majibu ya Wizara kwa Mdhibiti, ya tarehe 1/12/2020 yenye nambari ya kumbukumbu WHVUM/UU/P/U 30/019/VOL.1/18 zinathibitisha).

4. Kwa kuwa baadhi ya vielelezo vilipatikana wakati wa ukaguzi wa awali na vielelezo vyengine vilipatikana wakati wa ukaguzi wa mara ya pili ( verification) isipokuwa vielelezo vilivyoainishwa katika Hoja hii ambavyo viliendelea kukosekana hata wakati wa ukaguzi wa mara ya pili (verification), ni wazi kuwa uwekaji mbaya wa kumbukumbu za kifedha ndio tatizo lililosababisha kukosekana kwa vieielezo hivyo.

Aidha, kutokana na sababu hizo Kamati ya PAC haikuweza kuvipokea na kuvikagua vilelezo husika ambavyo viliwasilishwa mbele yake.

Mapendekezo ya Kamati yanPAC

i. Watendaji wa masuala ya fedha wakiwemo Washika Fedha wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Pemba wawe makini katika uwekaji wa kumbukumbu za Hesabu na kuhakikisha kuwa hati zote za malipo zinaambatanishwa na vielelezo husika wakati wote.

ii. Wizara iwape ushirikiano wa dhati Wakaguzi wa Hesabu kutoka Ofisi ya Mdhibiti ambapo pamoja na mabo mengine inapaswa kuwasilisha maelezo na vielelezo kwa Wakaguzi hao katika wakati unaofaa kama Sheria, Kanuni na taratibu za Ukaguzi zinavyolekeza.

iii. Watendaji wa Wizara wawe makini zaidi katika kutoa taarifa za majibu kwa Kamati kwa kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinakuwa sahihi kikamilifu ili kujiepusha kujiingiza katika makosa kama masharti ya Sheria ya Kinga, Haki na Fursa za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Namba 4 ya mwaka 2007 yanavyoelekeza.

### Hoja Namba 5.15.1.4 kukosekana kwa mapato yatokanayo na huduma za sanaa,shilingi 25,950,000

Kwa mujibu wa sheria ya baraza la sanaa, sensa, Filamu na utamaduni zanzibzr nambari 7 ya mwaka 2015 inawataka wamiliki wa hoteli kukusanya mapato yatokanayo na sanaa ,filamu filamu na utamaduni katika mahoteli yao na mapato hayo kuwasilisha Baraza la sanaa.

Ukaguzi umebaini uwepo wamadeni yanayotokana na mapato yatokanayo na sanaa ambapo mapato hayo hayakukusanywa kwa zaidi ya miaka mitatu na kupelekea uwepo wa deni la shilingi 25,950,000 ambazo zinadaiwa kutoka katika mahoteli mbali mbali.

Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadwel lifuatalo

Jadwel Nambari 117: Madeni yanayotokana na mapato ya sanaa

| namba | Jina la Hoteli | Mwaka | kiwango kilichotakiwa kukusanya muda wa miaka mitatu | Jumla ya fedha zilizolipwa | kiasi kinachodaiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Master Resourse Makangale | 2007-2020 | 3,900,000 | - | 3,900,000 |
| 2 | Pemba Paradaci Makangale | 2007-2020 | 3,900,000 | - | 3,900,000 |
| 3 | Ayyana Hotel Makangale | 2007-2020 | 3,900,000 | - | 3,900,000 |
| 4 | Pemba Lodg Shamiani Mwambe | 2007-2020 | 3,900,000 | - | 3,900,000 |
| 5 | Planet Sankara Shamiani Mwambe | 2007-2020 | 3,900,000 | - | 3,900,000 |
| 6 | Sunset Hotel – Wesha | 2007-2020 | 3,900,000 | 700,000 | 3,200,000 |
| 7 | Fund Lagoon-Wambaa | 2007-2020 | 3,900,000 | 650,000 | 3.250,000 |
| Jumla | | | 27,300,000 | 1,350,000 | 25,950,000 |

Majibu ya Wizara

Ni kweli Wizara ya inakabiliwa hadi sasa na changamoto ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na huduma za Utamaduni na Sanaa kupitia Mahoteli na Kumbi za Starehe. Miongoni mwa hatua tulizochukuwa ni kuandaa ziara rasmi kwa baadhi ya hoteli kama vile; Aiyana Hotel, Manta Resort na Pemba Paradise kwa lengo la kufanya mazungumzo nao ya ana kwa ana juu ya utekelezaji wa wajibu wao wa kukata vibali na leseni za kutumia kazi za Utamaduni na Sanaa, kwa kutumia kigezo cha sheria nambari 7 ya mwaka 2015 inayotupa mamlaka sisi (Wizara) na wao kuwajibika katika suala hilo. Pamoja na hivyo, walikataa kulipa makusanyo hayo kwa kisingizio cha kutokutumia kazi za Utamaduni na Sanaa katika maeneo yao na kuwa na utitiri wa kodi wanazolipa.

Hatua nyengine tuliochukuwa kama ofisi ni kuandika barua ya zuio la kufanya shughuli yoyote ya Sanaa katika kumbi au hoteli ambazo hazijakata vibali na leseni, nakla ya barua hizo imepelekwa Afisi za Wakuu wa Mikoa, Afisi za Wakuu wa Wilaya, Makamanda wa Polisi Mkoa, OCD na Masheha wa Shehiahusika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilielezwa kuwa deni la mapato yatokananyo na mapato ya sanaa katika hoteli (shilingi 25,950,000) bado halijalipwa licha ya juhudi mbalimbali za Wizara za kuyafuatilia mapato hayo. Hatahivyo, Kamati imebaini kuwa ugumu wa ukataji leseni za kazi za Sanaa katika hoteli umetokana na sababu mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

1. Kukosekana kwa ushirikiano na mkakati wa pamoja baina ya viongozi wa Wizara mbalimbali zinazostahiki kukusnya mapato katika hoteli kwa mujibu wa Sheria zinazohusika.
2. Uelewa mdogo wa Sheria ya Braza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni Namba 7 ya 2015 ambapo baadhi ya wamiliki wa hoteli wenye hoteli pia Unguja wamekuwa wagumu kulipa wakidai kuwa wameshakata kibali hicho kupitia hoteili za Unguja,
3. Wingi wa kodi zinaotozwa katika hoteli.

Aidha, Kamati ilipata nafasi ya kuikagua barua ya kuzuiwa kufanya shughuli yoyote ya ya sanaa na muziki katika kumbi na hoteli mbalimbali (Pemba) kuanzia tarehe 20/3/2021- barua ya 15/03/2021 yenye nambatri ya kumbukumbu WHVUM/IU/P/BS.30/018/VOL.1/39.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Afisa Mdhamin Wizara ya Habari, Vijana , Utamaduni na Michezo Pemba kwa kushirikiana na Maafisa wadhamin wa Wizara wengine waunde timu itakayoandaa mkakati wa pamoja kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa utaoweka namna bora zaidi ya kudai mapato ya vibali vya kazi za sanaa katika hoteli na kumbi mbalimbali pamoja na ada nyenginezo zinazostahiki kulipwa Kisheria.

Hoja Namba 5.15.1.5: MANUNUZI YALIYOFANYIKA KINYUME NA UTARATIBU SHILINGI 3,911,682/-

Kwa mujibu kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshajiwa Mali za Umma kinaeleza “Kulingana na masharti ya sheria hii mtu ,kampuni au taasis ihaitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya umma isipokuwa mtu huyo , kampuni au chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi chini

ya sheria hii ''

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini Wizara ya Vijana Utamaduni Sanaa na Michezo imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali kupitia hesabu ya amana nambari 0406693000 ambapo watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi , kwa mujibu wa sheria ambapo kumepelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa malipo haypo .

Kuwatumia watoa huduma ambao hawakusajiliwa kwa mujibu wa sheria kunapelekea kuikoseshs Serikali mapato yanayotokana na kodi ya thamani na ni kwenda na Sheia ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa manunuzi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 118 :Manunuzi yaliyofanyika kinyume na utaratibu

| Namba | Nambari ya Hati ya Malipo | Nambari ya Hundi | Jumla ya Fedha | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2/6, 1/6/2020 | 15563 | 1,200,000 | Moharash restaurent | ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununzi wa viburudisho |
| 2 | 5/2,21/2/2020 | 241 | 1,451,353 | Moharash restaurent | Ikiwa nii malipo kwa ajili ya ununuzi wa virubitisho |
| 3 | 10/8, 29/8/2019 | 166 | 356,475 | Moharash restaurent | Ikiwa nii malipo kwa ajili ya ununuzi wa virubitisho |
| 4 | 8/2, 25/2/2020 | 254 | 903,854 | Suleiman Seif Rashid | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya viyu mbali mbali |
| Jumla | | | 3,911,682 | | |

## Majibu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Taarifa ya mkaguzi na mdhibiti wa hesabu za serikali ilibaini manunuzi ya kiasi cha shilingi 3,911,682/- yalifanyika kinyume na utaratibu. Kuhusu hoja hii tulijiridhisha kwa kufuatilia kwa wafanyabiashara tuliofanya nao miamala na kupata vielelezo vyao zikiwemo hati za manunuzi kutoka mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPAA).

## Uchuuguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo haikuwasilisha vilelezo hivyo vya uthibitisho wa usajili wa watoa huduma walioaininshwa katika Hoja hii, jambo lililopelekea Hoja hii kubakia katika Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi. Hata hivyo, Kamati ilipata nafasi ya kukgua barua zinazotoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondohsaji wa Mali za Umma zinazothibitisha kuwa Moharash Restaurant ya Chake Chake ni mtoa huduma aliyesajiliwa na Mamlaka hiyo kwa nambari ya usajili ZPPDA/P/45/NC/2020 (barua ya tarehe 24 Machi, 2020 yenye nambari ya kumbukumbu MUUM,.PCA.84/403/01/110 inathibitisha) na Suleiman Seif Rashid mwenye nambari ya usajili ZPPDA/P/35/G/2020 (barua ya tarehe 10 Januari, 2020 yenye nambari ya kumbukumbu MUUMU.P.C.A. 84/403/01/35 inathibitisha)

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kwa kuwa Wakaguzi hawakupatiwa uthibitisho wa usajili wa watoa huduma walioainishwa katika Hoja hii wakati wa Ukaguzi wa mara ya pili (verification) Kamati ya PAC imewashauri Watendaji wa Wizara kuutumia vizuri muda wa siku 30 za kutoa ufafanuzi na kusawazisha dosari zilizobainika katika ukaguzi wa awali kwa kutoa kila aina ya uthibitisho unaofaa wakati ukaguzi wa mara ya pili (verification).

## FUNGU J 02 KAMISHENI YA UTALII

## TAARIFA YA MAPATO

Katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 Kamisheni ya Utalii ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 4,876,099,000/- kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni leseni za biashara ya utalii (leseni za hoteli na nyumba za kulala wageni, kamapuni za kuandaa misafara ya utalii, mikahawa, michezo ya baharini, maduka ya zawadi n.k.), Stika za magari ya Utalii na Vibali (vibali kwa gari za utalii na waongozaji watalii).

Kwa kipindi cha julai 2019 hadi Juni 2020 Kamisheni ya Utalii imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 3,624,336,663/- sawa na asilimia 74 ya makadirio katika vyanzo vyake vya mapato kama inavyoonekana katika jadweli 1 hapo chini.

Miongoni mwa sababu za kutofikia lengo la ukusanyaji wa mapato ni kuibuka kwa janga la maradhi ya COVID-19 ambapo kumepelekea kupungua kwa shughuli za utalii nchini pamoja na upungufu wa vitendea kazi

ambavyo hupunguza kasi ya ufuatiliaji wa shughuli za utalii nchini.

Jadweli 1: Mapato yaliyokusanywa kwa Mwaka 2019/2020

| NO. | VYANZO VYA MAPATO | MAKADIRIO | HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Leseni za Biashara ya Utalii | 4,460,979,000 | 3,339,287,633 | 75 |
| 2. | Stika za Magari ya Utalii | 111,560,000 | 45,240,000 | 41 |
| 3. | Vibali | 303,560,000 | 239,809,030 | 79 |

Taarifa ya Matumizi

Matumizi ya Kazi za Kawaida:

Katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 Kamisheni ya Utalii ilitekeleza programu kuu mbili ambazo ni (i) Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii inayosimamiwa na Idara ya Masoko, na (ii) Uratibu na Uendelezaji wa Utalii inayosimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Maendeleo ya Utalii. Lengo la kutekeleza programu hizi ni (i) Kuongeza uelewa kwa wakaazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa kuhusu bidhaa za utalii ziliopo Zanzibar, na (ii) Kuweka mazingira na rasilimali watu bora katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 programu ya utangazaji na uhamasishaji wa utalii ilipangiwa kutumia jumla ya shillingi 573,145,000/- kutekeleza shughuli zake na kufanikiwa kuingiziwa jumla ya shilingi 301,503,950/- sawa na asilimia 53 ya fedha zilizopangwa kutumika. Aidha, katika programu ya uratibu na uendelezaji utalii ilipangiwa kutumia jumla ya shillingi 1,548,855,000/- (mishahara na matumizi mengineo) kutekeleza shughuli zilizopangwa na kufanikiwa kupata jumla ya shilingi 1,367,141,375/-sawa na asilimia 88 ya fedha zilizopangwa kutumika kama inavyoonekana katika jadweli 2 hapo chini. Utekelezaji kamili wa shughuli zilizopangwa unaonekana katika Jadweli lifuatalo.

Jadweli 2: Makadirio na matumizi halisi ya fedha za kazi za kawaida kwa Mwaka 2019/2020

| MAELEZO | MAKADIRIO | HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| Programu: Utangazaji na Uhamasishaji wa watalii | | | |
| Matumizi mengineo (OC) | 573,145,000 | 301,503,950 | 53 |
| Programu: Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya utalii | | | |
| Mishahara | 821,400,000 | 763,214,860 | 93 |
| Matumizi mengineo (OC) | 727,455,000 | 603,926,515 | 83 |
| Jumla Ndogo | 1,548,855,000 | 1,367,141,375 | 88 |
| Jumla Ndogo (OC) | 1,300,600,000 | 905,430,465 | 70 |
| JUMLA KUU | 2,122,000,000 | 1,668,645,325 | 79 |

Miongoni mwa shughuli ambazo hazikufanyika kutokana na upungufu wa fedha ni kutangaza huduma na bidhaa za utalii kwa kutumia majarida na televisheni na mabango ya kielektronik ndani na nje ya nchi na kuandaa ziara za mafunzo kwa Makamishna wa Kamisheni ya Utalii.

B: Matumizi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo:

Katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 Kamisheni ya Utalii ilitekeleza mradi wa kuimarisha utalii kwa Wote uliopo Bungi kwa Bi. Khole, lengo la mradi huu ni kujenga kituo cha utalii ambacho kitaongeza ushindani wa bidhaa za utalii pamoja na kuhakikisha kila mwananchi ananufaika na matunda ya utalii na anashiriki kikamilifu katika kutunza na kuendeleza utalii sambamba na kuimarisha huduma na vivutio kwa watalii. Kwa mwaka 2019/2020, mradi ulipangiwa jumla ya shillingi 1,500,000,000 kutoka Serikalini.

Kampuni ya Quality Building Constractors ndio iliyoshinda Zabuni ya kujenga mradi huo kwa kazi za kusafisha eneo na kuliweka sawa (leveling), ujenzi wa eneo la maegesho ya magari (Parking Area), kujenga maduka ya vyakula na vinywaji, bustani, vyoo na kuvuta umeme. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya shilingi 1,121,553,418/- zilipatikana ambazo sawa na asilimia 75 ya fedha zilizopangwa. Utekelezaji wa Mradi huu kwa awamu ya kwanza umekamilika na kukabidhiwa rasmi na tayari umeshawekewa jiwe la msingi na Mheshmiwa Zuber Ali Maulid Spika wa Baraza la Wawakilishi katika sherehe za kuadhimisha miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jadweli 3 linaonesha upatikaji wa fedha za mradi.

Jadweli 3: Makadirio na matumizi halisi ya fedha za Mradi kwa Mwaka 2019/2020

| MAELEZO | MAKADIRIO | HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Fedha za Ndani(SMZ) | 1,500,000,000 | 1,121,553,418 | 75 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| JUMLA | 1,500,000,000 | 1,121,553,418 | 75 |

HOJA NAMBARI 5.15.2.1 KUKOSEKANA KWA VIELELEZO VYA MATUMIZI SHILINGI 91,855,665

Matumizi tajwa hapo juu yamefanyika kwa shughuli mbili tofauti. Kwanza malipo ya shilingi 51,660,000 ($ 22,500) yamelipwa kwa JHIL Enterprises ikiwa ni malipo ya kodi na usimamizi wa Ofisi ya Utangazaji utalii nchini India iliyopo Mumbai. Pili malipo ya shilingi 40,195,665 (€15,447) yamelipwa kwa waandaji wa maonesho ya ITB-Berlin nchini Ujerumani (MESSE BERLIN) kwa ajili ya banda la Zanzibar katika maonesho hayo ambalo linasimamiwa na Jumuiya ya Kuandaa Misafara ya Utalii Zanzibar (ZATO).

Malipo halisi ya shilingi 91,855,665 uthibitisho wake ni kama hivi ifuatavyo:-

1. Waandaji wa Maonesho ya ITB-Berlin (MESSE BERLIN)

PV.3401/2020 ya tarehe 16/01/2020 (€15,447) 40,195,665

2. JHIL Enterprises

PV.92/08/2019 ya tarehe 28/08/2019 ($ 7,500) 17,227,425

PV.06/01/2020 ya tarehe 03/01/2020 ($15,000) 34,432,575

JUMLA 91,855,665.00

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa matumiz hayo yalifanywa na Wizara ya Fedha kwa njia ya Dummy ambapo Mhasibu wa Kamisheni aaliyehusika kwa wakati huo alishindwa kuvifuata vielelezo husika Wizara Fedha ndio sababu ya kukosekana vielelezo hivyo wakati wa Ukaguzi, Hata hivyo vielelezo hivyo vimepokelewa na Kamati.

5.15.2.2 MATUMIZI AMBAYO HAYAKUFUATA UTARATIBU SHILINGI 56,943,316

Kamisheni ya Utalii imefanya malipo ya shilingi 20,449,782 kwa Kampuni ya Melisha Media Production kupitia huduma zifuatazo:

| S/N | Huduma | Tarehe | Fedha |
|---|---|---|---|
| 1 | Uchapishaji wa Banner na T-shirt za maonesho ya Sabasaba | 04/07/2019 | 1,007,500 |
| 2 | Wino wa printa Xerox 7800 (16 pcs) | 10/07/2019 | 18,000,000 |
| 3 | Uchapishaji na ununuzi wa vifaa vya Pemba Tourisport Bonaza | 13/08/2019 | 1,305,000 |
| 4 | Uchapishaji wa fulana kwa ajili ya ziara ya | 23/08/2019 | 1,200,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wageni wa SADC | | |
| | VAT | | 1,062,718 |
| | JUMLA KUU | | 20,449,782 |

Kutokana na huduma zilizoainishwa hapo juu Kamisheni ya Utalii iliamua kufanya matumizi hayo kulingana na mahitaji yalivyojitokeza kwa wakati husika ili kuweza kufanikisha majukumu ya wakati huo. Aidha, malipo ya shilingi 18,000,000 yalifanyika kwa ununuzi wa wino ambao hutumika kwenye printa kwa ajili ya matumizi ya kazi mbali mbali za ofisi kama vile uchapishaji wa leseni, kadi za uingiaji wa wageni (domestic arraival) n.k.

Malipo ya shilingi 36,493,534 yanatokana na huduma ambazo Kampuni ya Melisha Media Production imezitoa kwa Kamisheni ya Utalii. Uchambuzi wa huduma hizo ni kama ifuatavyo:

| S/N | Huduma | Tarehe | Fedha |
|---|---|---|---|
| 1 | Uchapishaji wa T-shirt na kofia za ujumbe kutoka SADC | 15/08/2019 | 5,000,000 |
| 2 | Uchapishaji wa vifaa vya Pemba Tourisport Bonaza (jezi, kofia, saa, fulana, banner) | 31/07/2019 | 4,730,000 |
| 3 | Kubuni (design) vipeperushi vya utalii | 18/09/2019 | 1,100,000 |
| 4 | Uchapishaji wa T-shirt na Banner za maonesho ya Ver de Hotel | 24/09/2019 | 5,060,000 |
| 5 | Uchapisaji wa brochures za Kiengereza | 30/09/2019 | 5,500,000 |
| 6 | Uchapishaji wa Banner za maonesho ya Sherehe za Mapinduzi | 07/01/2019 | 915,000 |
| 7 | Uchapishaji wa banner Pemba Tourisport Bonaza | 08/10/2019 | 1,008,000 |
| 8 | Ununuzi na uchapishaji wa jezi Pemba Tourisport Bonaza | 21/07/2019 | 1,475,000 |
| 9 | Ununuzi na uchapishaji wa T-shirt, na kofia za Pemba Tourisport Bonaza | 14/08/2019 | 5,000,000 |
| 10 | Uchapishaji wa T-shirt na banner za Pemba Tourisport Bonaza | 21/09/2019 | 5,060,000 |
| 11 | Uchapishaji wa banner, kofia na fulana za Pemba Tourisport Bonaza | 09/10/2019 | 1,588,000 |
| | JUMLA KUU | | 36,493,534 |

Matumizi yaliyoainishwa hapo juu yamefanyika kulingana na mahitaji yalivyojitokeza kwa wakati husika, ili kuweza kufanikisha shughuli hizo. Aidha, malipo ya shilingi 18,861,000 yalifanyika kwa ajili ya kufanikisha Tamasha la utalii la “Pemba Tourisport Bonanza” ambapo fedha zilizotumika katika Tamasha hili zimetokana na michango mbali mbali kutoka kwa wadau tofauti wa sekta ya utalii.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa Kamisheni ya Utalii hupeleka kazi zake mbalimbali za machapisho na nyenginezo kwa kampuni binafsi kutokana na uharaka wa mahitaji yake kulingana na matukio ya shughuli na mikutano ya masuala ya Kiatalii zilizvyo bila ya kuanza kufanya mawasiliano rasmi na Wakala wa Serikaliwa Uchapishaji wa Serikali kwanza

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamisheni ya Utalii inapotaka kupeleka kazi kwa Taasisi binafsi ni vizuri kuiomba Kibali kwa Wakala wa Uchapishaji wa Serikali au Mamlaka ya Ununuzi wna Uondoshaji wa Mali za Umma kulingana na mahitaji

5.15.2.2 MALIPO YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA KIVUTIO CHA UTALII BUNGI SHILINGI 1,141,137,215.36

Malipo ya mradi wa Uimarishaji wa utalii kwa wote yanafanywa moja kwa moja na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Kamisheni ya Utalii imefuatilia na kupata vielelezo vya malipo hayo kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Vr N0. 1/5 ya tarehe 17/05/2019 | 144,832,590 |
| PV. 02/07 ya tarehe 08/07/2020 | 362,070,570.9 |
| PV.05/08 ya tarehe 01/08/2019 | 535,706,645.59 |
| Risiti N0. 028 ya tarehe 20/11/2019 | 98,543,043.99 |
| JUMLA KUU | 1,141,152,850.48 |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa vielelezo vya mradi huo havikupaikana wakati wa Ukaguzi wa Mdhibuti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa sababu mhasibu aliyekuwepo hakwenda kufuatalia vielelezo hivyo Wizara Fedha ambako ndiko kulikofanywa malipo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kamisheni ya Utalii ishirikiane na Wizara ya Kilimo ili kuona namna ya kuongeza vivutio katikaHifadhi ya ya Msitu wa Jozani badala kutegemea kima punju peke yake.

ii. Mhasibu wa Kamisheni ya Utalii ahakikishe kuwa kila kielelezo cha matumizi kinapatika wakati wa ukaguzi

iii. Kamisheni ya Utalii iwe na mashirikiano mazuri na Wakagazi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

KAMISHENI YA UTALII PEMBA

HOJA NAMBARI 5.15.2.4MALIPO YA ZIADA YA UTENGENEZAJI WA BOQ YA JENGO LA KAMISHENI SHS. 26,540,000/=

Kamisheni ya Utalii imeingia mkataba na kampuni ya Ecosense Engeneering Co . LTD kwa ajili ya utengezaji wa B.O.Q ya ujenzi jengo la Kamisheni.Ukaguzi umebaini kupitia Tax Invoice NO .2020 /pbz/05 na Barua ya kuwasilisha B.O.Q KUM NO. 2020/PBZ/O8 ZA 06/04/2020 kutoka kwa Ecosense Engeneering Co. LTD kwamba malipo ya B.O.Q kwa awamu zote ni shilingi 23,000,000.Aidha ukaguzi umebaini kufanyika kwa malipo ya shilingi 49,540,000 kinyume na Tax Invoice zilizoambatanishwa Kufanya hivyo kunapelekea matumizi mabaya ya fedha za umma , aidha ni kwenda kinyume na shreia ua usimamizi wa fedha za umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

Malipo hayo yamefanyika kama ifuatavyo:-

Jadwel Nambari 122 : Malipo ya ziada ya utengenezaji wa B.O.Q

| Nambari ya Hati | Nambari ya Hundi | Aliyelipwa | Kiasi kilicholipwa |
|---|---|---|---|
| 17/1<br>10/1/2020 | T.T | Ecosense Engeneering Co . LTD | 8,820,000 |
| 11/3<br>24/3/2020 | T.T | Ecosense Engeneering Co . LTD | 14,250,000 |
| 13/4<br>21/4/2020 | T.T | Ecosense Engeneering Co . LTD | 11,875,000 |
| 13/5<br>26/3/2020 | T.T | Ecosense Engeneering Co . LTD | 14,595,000 |
| JUMLA | | | 49,540,000 |

Majibu ya Kamisheni ya Utalii

Kwanza naomba kuiarifu Kamati yako kwamba ujenzi wa ofisi ya Kamisheni ya Utalii kisiwani Pemba, unaozungumziwa katika ripoti hii unahusianana Jengo lenye ghorofa 4 na mbili ni basement kwa vile eneo linalojengwa ni la Msingini. Ujenzi unafanyika kwa kutumia fedha za matumizi mengineyo (OC) ya fungu J02 la Kamisheni ya Utalii na sio Mradi. Hali inayo sababisha ujenzi huo kwenda taratibu kutokana na kutopatikana fedha za bajeti, ikizingatiwa kuwa Kamisheni ya Utaliii inaendeshwa kwa kutumia OC.

Kamisheni ya Utalii imechukua hatua hii kwa kuamini kwamba iwapo itafanikiwa kukamilisha ujenzi kwa hatua ya basement za jengo hilo, itakuwa rahisi kuishawishi Wizara ya Fedha kuingiza ujenzi wa ofisi hiyo katika Mradi mkuu wa majengo ya Serikali ambayo hujengwa chini ya usimamizi waWizara ya Fedha.

Malipo halisi ya BOQ ni shilingi milioni ishirini na tatu (23,000,000). Uthibitisho wa malipo hayo ni kupitia Invoice No 2020/PBA/05 kama hivi ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| VrNo 11/03 ya tarehe 24/03/2020 | | 11,875,000.00 |
| Vr No 13/05 ya tarehe 26/03/2020 | | 9,975,000.00 |
| JUMLA | 21,850,000.00 | |

Kazi ambayo ilikamilika kwa wakati kama ilivyotakiwa na kuwasilishwa kwa Kamisheni ya Utalii. Hivyo basi, wakati wa kuwasilisha BOQ hiyo na kupitiwa kwa kina na ofisi, ilionekana kuna mahitaji zaidi katika BOQ iliyowasilishwa. Hali hiyo ilipelekea kuitishwa kikao chengine baina ya Ecosense ambayo ndio watengezaji wa BOQ hiyo na Kamisheni ya Utalii kuihakiki. Katika kikao hicho kulionekana kuhitajika mambo mengine ambayo yanahitaji BOQ ya ziada. Katika mjadala huo kulionekana hakuna mfumo wa Umeme, maji machafu na maji safi, kutokana na mapungufu hayo ndiko Kulikosababisha kupewa kazi nyengine na si ziada ya malipo ya BOQ.

Katika kazi nyengine walizopewa katika kikao hicho ni Kuandaa michoro ya Kihandisi (Structural Drawing) ambapo gharama zake ni Tzsh. Milioni tisa tu (9,000,000) kama inavyoonesha kwenye Invoice No. 2020/PBA/01 na Invoice 2020/PBA/02 na karatasi ya malipo.

| | | |
|---|---|---|
| Vr No 11/01 ya tarehe 10/01/2020 | | 8,820,000.00 |
| Malipo ya TRA | 180,000.00 | |
| JUMLA | 9,000,000.00 | |

Kazi nyengine waliyopewa ni matayarisho ya BOQ kwa ajili ya kuitisha zabuni ya ujenzi yenye gharama ya Tzsh. 15,000,000 (Milionikuminatanotu) na malipo yamefanyika kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Vr No 11/03 yatarehe 20/03/2020 | | 14,250,000.00 |
| NaShs. 750,000 ni malipo ya TRA | 750,000.00 | |
| JUMLA | 15,000,000.00 | |

Pia katika karatasi/ waraka wa malipo No. 13/05/2020 kuna malipo ya BOQ ya shs. 4,620,000 ambazo ni kazi ya Jengo ambalo Kamisheni ya Utalii Iliomba na kukabidhiwa na Serikali kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ili ihamie kwa muda huku ikisubiri kukamilika kwa jengo kusudiwa, kwa lengo la kuipatia Kamisheni ya Utalii ofisi, pamoja na kuondosha gharama za kukodi ya Ofisi inayotumia sasa ambayo imekodiwa kwa mtu binafsi.

| | | |
|---|---|---|
| Vr No 11/03 yatarehe 20/03/2020 | | 4,620,000.00 |
| NaShs 300,000 ni malipo ya TRA | 300,000.00 | |
| JUMLA | 4,920,000.00 | |

| | | |
|---|---|---|
| Malipo yote ni | 27,690,000.00 | |
| TRA ya VR No 11/3 na13/05 | | (1,150,000.00) |

JUMLA 26,540,000.00

Kwa maelezo haya naomba niitaarifu Kamati kwamba, hakuna malipo ya ziada ya BOQ ambayo yamefanyika kama ilivyoelezwa kwenye kitabu cha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika jadweli husika kwenye ukurasa wa186, inawezekana kilichokosekana ni ufafanuzi kuhusiana na matumizi hayo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imepata maelezo ya Kamisheni na kuchunguza nyaraka mbalimbali zinazohusika na Hoja hiii zikiwemo barua walizoandikiwa kampuni za ujenzi, na hati za malipo na kubaini yafutatyo:

i. Kamisheni iliwaandikia watoa huduma watatu kuomba “quotations” ambao ni Ecosence Engineering Company (Ltd), Land Mark Conslt Limited, na Innovative Studio Design Conslt Co zote za Zanzibar.

ii. Hakukuwa na uthibitisho uliioonesha kuwa utataratibu uliotumiwa na Kamisheni ya Utalii ya kumpata mtoa huduma (Quotations) kama iliridhiwa na Bodi ya Zabuni ya Kamisheni ya Utalii kama ambavyo kifungu cha 28 (1)(j) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016 kinavyoelekeza kwa kuipa uwezo Bodi ya Zabuni ya Taasisi husika kuidhisha taratibu za ununuzi na uondoshaji wa mali za umma.

iii. Kamisheni ilikuwa ikitegemea fedha za matumizi mengineyo (OC0 kwa ajili ya kugharamaia kazi hizo hali amabyo iliifanya Kamisheni kukabiliwa na uhaba wa fedha katika mradi mzima wa ujenzi.

iv. Ingawa kazi ya uandaaji wa BOQ husika iligharimu jumla ya shilingi 23,000,000 (bila ya VAT), kazi hiyo ilifanyika bila ya kuwepo kwa mkataba wowote baina ya Kamisheni ya Utalii na Kmapuni ya Ecosense Engineering Company Ltd.

v. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 katika Kamisheni ya Utalii hakukuwa na Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani iliyoandaliwa kutakana kufariki kwa aliyekuwa Mkaguzi wa Ndani wa Kamisheni hiyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamisheni ijipange vizuri katika kutafuta wafadhili watakaoweza kusaidia kazi ya ujenzi wa jingo lake bada;a ya kutegemea fedha za O.C ambazo ni chache na zina mahitaji mengi.

HOJA NAMBARI 5.15.2.5MAPUNGUFU KATIKA UONDOSHAJI WA VIFAA VILIVYOTOKANA NA KUBOMOLEWA KWA JENGO

Kamisheni ya Utalii iliitisha Zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa Ujenzi. Baada ya kupatikana Mkandarasi ambae ameshinda zabuni hiyo, kampuni ya KIN INVESTMENT. Kwenye Mkataba wa Ujenzi Mkandarasi huyo pamoja na kazi nyengine, alitakiwa kusafisha eneo na kuondoa mabaki yote ili eneo liwe safi na liweze kutumika kwa kuanza ujenzi. Utekelezaji wa kazi hiyo ni kwa mujibu wa maelekezo kwenye BOQ ya kazi hiyo ‘Element No.1: (Demolition) iliyomuelekeza kama ifuatavyo “carefully demolish existing structures on the site. The item to include removing all debris off site ready for excavation works”.

Majibu ya Kamisheni ya Utalii

Eneo linalozungumzwa katika ripoti hii linahusiana na eneo ambalo limenunuliwa na Kamisheni ya Utalii mwaka 1997 kutoka kwa Nd. Ali Abeid Nassir likiwa na gofu ambalo kwa miaka yote hiyo ni kama jaa la kutupia taka, hivyo hakukuwa na vifaa chakavu, wala mali za Serikali wakati wa kusafisha eneo hilo ambavyo vingesababisha kupatikana mapato kwa Serikali kama ilivyoripotiwa katika hoja ya msingi ya Mdhibiti.

Kwa maelezo hayo, naomba kuieleza kamati kuwa yote hayo yalifanyika kwa jitihada na kuzingatia Sheria na taratibu zote, ili kufanikisha lengo la kuiwezesha Kamisheni ya Utalii kuwa na ofisi yenye hadhi na kuondokana na kadhiaya kuendelea kukodi ofisi kwa mtu binafsi, jambo linaloipa mzigo mkubwaSerikali.

Uchuguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya Kupata ufafanuzi wa suala hiylo haikuwa na maelezzo zaidi

## SEHEMU YA TATU

### UCHUNGUZI RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MAWIZARA YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### FUNGU D 01 - WIZARA YA NCHI (OR) TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM

Taarifa ya Mapato

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 (AR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ilijipangia kukusanya Tsh 781,000 za uuzaji wa zabuni hadi kumalizika mwaka wa fedha hatukufanikiwa kukusanya fedha yoyote.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikuwa na maelezo zaidi juu ya hoja hii

Taarifa ya Matumizi

Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 5,620,800,000 kwa kazi za kawaida, shilingi 20,500,,000,000 kwa kazi za maendeleo na shilingi 1.605,000,000 kutoka katika Mfuko wa Barabara katika kipindi cha kinachoishia tarehe 30 Juni, 2018.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 jumla ya shilingi 4,331,952,521 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za

kawaida sawa na asilimia 77 ya makadirio na shilingi 20,500,000,000 kwa matumizi ya maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 100 ya makadirio na shilingi 1,605,000,000 kutoka katika Mfuko wa Barabara.

Majibu ya Wizara

TaarifazaMatumiziza(AR) TawalazaMikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama ifuatavyo:-

MATUMIZI YA KAWAIDA

| SN | MAELEZO | MAKADIRIO | UHALISIA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MISHAHARA | 2,865,600,000/= | 2,089,679,300/= | 73% |
| 2. | OC | 2,060,200,000/= | 1,663,106,551/= | 81% |
| 3. | RUZUKU ZA OC | 695,000,000/= | 579,166,670/= | 83% |
| | JUMLA | 5,620,800,000/= | 4,331,952,521/= | 77% |

1.1. MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO

| SN | MAELEZO | MAKADIRIO | UHALISIA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | CCTV | 20,000,000,000 /= | 20,000,000,000/ = | 100% |
| 2. | UGATUZI | 500,000,000/= | 500,000,000/= | 100% |
| | JUMLA | 20,500,000,000 /= | 20,500,000,000 /= | 100% |

MAELEZO MAFUPI YA MIRADI NA FEDHA ZA MAENDELEO

MRADI WA MJI SALAMA

Mradi huu ni wa mji salama ,ambapo fedha zake hutumika kuweka miundombinu ya CCTV.Kwa upande wa malipo hulipwa moja kwa moja na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mujibu wa mkataba ambapo hadi mwaka ulipomalizika mradi ulitumia Tsh 20,000,000,000 sawa na asilimia 100.

MRADI WA UGATUZI

Mradi wa kupeleka madaraka kwa wananchi kwa lengo la kuboresha na kusogeza huduma bora kwa wananchi. Mradi wa ugatuzi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ulitekeleza kama ifuatavyo:-

1. Kuoanisha sera na sheria kulingana na sera za sekta zilizogatuliwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa
2. Kutoa miongozo na miundo mbalimbali ya uendeshaji wa Mamlaka ya Serikaliza Mitaa kuhusiana na huduma zilizogatuliwa kama vile, miongozo ya mipango na bajeti, ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ugawanyaji wa Rasilimali Watu, Miundo ya kitaasisi ya sekta zilizogatuliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, mkakati wa mawasiliano katika Mamlakaza Serikali za Mitaa, kuchapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali.
3. KuwekwakwamfumowaukusanyajimapatokwanjiazakieletronikikwaMamlakayaSerikalizaMitaa.
4. Kuunda Kamati za Mashauriano za shehia na Mabaraza ya Wadi pamoja na kutoa elimu kwa mujibu wa

kazi zao.

Mradi hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2017/2018 ulipokea Tsh 500,000,000 sawa na asilimia 100.

MATUMIZI YA MRADI WA "FEEDER ROADS"

| SN | MAELEZO | MAKADIRIO | UHALISIA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa barabara za ndani | 1,304,619,500 | 1,141,376,342 | 87 |
| 2. | Ufuatiliajiwamradi | 300,380,500 | 166,837,360 | 57 |
| | JUMLA | 1,605,000,000/= | 1,308,213,702/= | 81 |

MAELEZO YA MRADI WA "FEEDER ROADS"

Mradi huu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ulitengeneza barabara ya Magogoni hadi Kinuni, kuwajengea uwezo watendaji wa Kitengo cha Uhandisi cha Wizara pamoja na ununuzi wa vitendeakazi vya ofisi.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 mradi wa barabara za ndani ulikua na bajeti ya *Tsh1,605,000,000.*Hadi kukamilika mwaka wa fedha 2017/2018 mradi uliingiziwa jumla Tsh 1,308,213,702 sawa na asilimia 81ya bajeti iliyopangwa.Kati ya fedha hizoTsh 1,141,376,342 zililipwa moja kwa moja kwa njia ya mkataba na Mfuko wa Barabara sawa na asilimia 71 naTsh 166,837,360 ziliingizwa katika akaunti ya "Feeder Road" inayosimamiwa na Wizara sawa na asilimia 10 ya bajeti.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kutokana na ufafanuzi uliotolewa unaohusu pamoja na mambo mengine kuoneknana kwa utofauti kwenye taarifa za fedha za maendeleo ambapo Ripoti ya Mdhibiti ilianisha asilimia 100 lakini majibu ya awali ya Wizara yalionesha aslimia 99. Hivyo, ufafanuzi wa ziada wa taarifa sahihi ambayo imewasilishwa katika Kamati kama inavyoonekana katika majibu,

5.2.1.1 Kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya fedha za Mfuko wa Barabara shilingi 1,421,579,101

Ukaguzi umebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ilipokea jumla ya shilingi 1,605,000,000 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya materngenezo ya Barabara za ndani (Feeder Road). Ukaguzi umebaini katika hesabu nambari 021103000697 (Feeder Road Account), matumizi halisi yaliyofanyika kwa ajili ya utengenezaji wa barabara za ndani ni jumla ya shilingi 183,420,899. Ukaguzi umeshindwa kukagua matumizi na vielelezo vya jumla ya shilingi 1,421,579,101, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016. Maelezo ya matumizi ya fedha hizo yanaonekana katika jadweli

| JUMLA YA FEDHA ZILIZORIPOTIWA KATIKA TAARIFA ZA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA | MATUMIZI HALISI YALIYOPATIKANA KWA UKAGUZI | TOFAUTI AMBAYO HAIKUPATIKANA KWA UKAGUZI |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1,605,000,000.00 | 183,420,899.00 | 1,421,579,101.00 |

Majibu ya Wizaya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum

Mradiwa"feeder roads" unapokea fedha kutoka Mfuko wa Barabara ambapo fedha za usimamizi, na ufuatiliaji wa mradi zinaingizwa katika hesabu ya kibenki iliyo chini ya Wizara na fedha za ujenzi wa barabara na mikataba mengine hulipwa moja kwa moja kwa wakandarasi kupitia Mfukowa Barabara.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ilikua na bajeti ya shilingi 1,605,000,000 katika Mfuko wa Barabara, hadi mwishoni mwa mwaka Wizara ilitumia jumla ya shilingi 1,308,213,702. Kati ya hizo shilingi 166,837,360 ziliingizwa katika hesabu ya benki ya "feeder roads" inayosimamiwa na Wizara na kiasi cha shilingi1,141,376,342 zimelipwa moja kwa moja kutoka Mfuko wa Barabara kwenda kwa watoa huduma waliokubalika kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Kwa upande wa uwasilishaji hesabu za mwaka wa fedha 2017/2018 inavyotakiwa kuzitambua (recognize) shilingi 166,837,360 kama fedha tulizopokea kutoka Mfuko wa Barabara na sio kama ilivyoripotiwa kima kosa katika hesabu za mwaka.Vile vile shilingi1,141,376,342 zilitakiwa kuoneshwa (disclosure) katika hesabu za mwaka za Wizara kama fedha zilizolipwa moja kwa moja kutoka Mfuko wa Barabara na kulipwa na Mfuko kwa Mkandarasi.

Hivyo, Wizara inakiri kosa la kutoonyesha mchanganuo huo katika ripoti yake ya fedha(*financial Statement*) badala yake ilitambua 1,605,000,000/= kama fedha zilizopokelewa kutoka Mfuko wa Barabara kwa makosa ambapo uhalisia hii bajeti yake ya mwaka iliopo Mfuko wa Barabara na sio fedha ilipatikana kwa mwaka 2017/2018.

Wizara inaomba radhi kutokana na kosa hilo na limeshachukuliwa hatua katika ripoti ya fedha ya mwaka 2019/2020 kwa kuhesabiwa kama inavyotakiwa katika miongozo ya kimataifa ya uhasibu.

Aidha, vielelezo vya matumizi hayo vipo Mfuko wa Barabara ambapo wao ndio wanaolipa na kutunza kumbukumbu ya matumizi yaliofanyika.Tofauti itakayojitokeza ni zuio la kodi (*withholding tax*)na bakaa la mkataba (*retention money*).

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilkagua vielelezo mbalimbali kutoka Mfuko wa barabara zikiwemo hati mbalimbali za malipo pamoja na vielezo vyengine. Kwa ujumla Kamati imeridhika na ufafanuzi uliotolewa katika majibu ya Wizara

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Ni vyema kwa Wahasibu kuwa makini zaidi wanapondaa taarifa za kifedha na kuzipiria kwa kina pamoja na kuwapatia Ma afisa Masul ufafanuzi wa kutosha juu ya taarifa hizo ili kuepusha makosa yenye kuleta mashaka katika taarifa hizo.

FUNGU D 02 JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU)

Taarifa ya Mapato

Jeshi la Kujenga Uchumi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 84,555000 kupitia vyanzo vyake vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018, jumla ya shilingi 55,764m100 zilikusanywa ikiwa sawa na asilimia 65 ya makadirio.

Majibu ya JKU

Jeshi la Kujenga Uchumi ina vyanzo vyake vya ndani vinavyotumika kuwasilisha/kuchangia fedha za mfuko mkuu wa Serikali kila mwaka wa fedha kamai fuatavyo:-

j. MapatoyaMauzoyaMpunga
k. MapatoyamauzoyaMtama
l. MapatoyamazaoyaBustani
m. Mapatoyamifugo
n. MapatoyaadayaUlinzi
o. MapatoyaSkuliza JKU
p. Mapatoyaukodishajiwamaduka
q. MapatoyaKarafuu

Kwamwaka 2017/2018 JKU haikuvuka lengo la makusanyo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo haliyahewa, ikumbukwe kuwa sehemu kubwa ya vyanzo vya mapato ya JKU yanategemea mvua za msimu ambayo ilipelekea kukosekana kwa mavuno ya uhakika hasa mpunga na mtama. Kuanzishwakwa Wakala wa Ulinzi ndani ya JKU na kupelekea vituo vyote vya ulinzi vikabidhiwe kwa Wakala.

UKUSANYAJI MAPATO YA JKU KWA MWAKA 2017/18

| GFS CODE | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA 2017/18 | MAKUSANYO HALI KWA MWAKA | ASILIMIA YA MAKUSANYO KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|
| 1422004 | MapatoyaMauzoyampunga | 10,000,000 | 5,300,000 | 53 |
| 1421005 | MapatoyaMauzoyamtama | 500,000 | 225,000 | 45 |
| 1421006 | MapatoyamauzoyaBustani | 13,000,000 | 12,395,000 | 95 |
| 1422068 | MapatoyaMifugo | 7,000,000 | 2,580,000 | 37 |
| 1422086 | Ada yaUlinzi | 24,000,000 | 11,764,100 | 49 |
| 1422045 | Mapatoyaskuliza JKU | 15,000,000 | 12,000,000 | 80 |
| 1415004 | MapatoyaukodishajiMaduka | 1,500,000 | 1,500,000 | 100 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1422045 | MapatoyaKarafuu | 13,555,000 | 10,000,000 | 74 |
| | JUMLA | 84,555,000 | 55,764,100 | 65 |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa mapato ya mifugo yametokana na Mifugo ya ng'ombe, mbuzi na kuku, maziwa ya ng'ombe na pia huuza mayai. Aidha, Kamati ya PAC ilihoji juu ya sababu ya kutofikia malengo katika mapato yatokananyo na ulinzi na kuelezwa kuwa Ulinzi – Mapato yameshuka kutokana na kwa wakati huo ndio malindo ya JKU yalihamishwa kutoka JKU kwenda Wakala wa Ulinzi wa JKU – Malipo ya 2017/2018 yaliyoainishwa ni ya huduma za Ulinzi.

Kwa upande wa mapato yan Karafuu Kamatiilielezwa kuwa JKU wanalo shamba la Mikarafuu lilipo Machui – na hukodisha au huchuma wenyewe Katika Umwagiliaji, Kamati ilielezwa kuwa Umwagiliaji bado hawajafikia katika hatua ya kilimo cha umwagiliaji. Mwaka huu wa 2021 wataanza kilimo cha umwagiliaji wa mboga mboga – wameomba fedha Serikalini wakipata watanzisha huo mradi wa umwagiliaji maji – Bambi mboga mboga na sehemu ya mradi wa pamoja baina ya Zanzibar (JKU) na Misri

Kamati ya PAC ilielezwa kwa kuna eka 170 za ushirikiano baina ya JKU na Misri ingawa eneo linalotumika halifiki hata eka 5o, Mapato ya Mtama – Bambi yanakwenda Katika "Zanzibar Egyptian Joint Fund."Sehemu kubwa ya mapato ya JKU ya mtama Bambi kama Shamba la pamoja yamekwenda katika Mradi wa Shamba la pamoja, ingawa JKU inafanya kazi kubwa katika Shamba hilo la pamoja na mapato yake yanaingia katika Mradi huo wa pamoja.

Mkataba wa mradi wa pamoja baina ya Zanzibar (JKU) na Misri ulitiwa saini mwaka 2003 na ulikuwa wa miaka 10. Mkataba mpya bado haujafungwa. Kamati ilielezwa kuwa kwa mujibu wa Mkataba huo, Zanzibar (JKU) ilitakiwa itoe ardhi, nguvu kazi na baadhi ya vifaa na Misri itoe utaalam. Shamba hilo linazalisha mboga mboga zaidi ingawa kwa kipindi chote hicho faida bado haijapatikana. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa maagizo ya Serikali ni kuwa JKU iendelee na Ubia na Misri. Hata hivyo,Kamati mbali mbali zimeundwa kuchunguza mradi huu wa pamoja.

Kwa upande wa mapato ya Skuli ya ufundi, Kmati ilielezwa kuwa hawalipishi ada bali ni kujitolea na kutengeneza vifaa kama vitanda, viti, lakini kwa kuwa vfaa hivyo vinatengenezwa nawanafunzi huwa haviziuziki vinapouzwa.

Vile vile Kamati ua PAC ilelezwa juu ya utaratibu wa kuchangia mapato Serikalini kwamba JKU wanapotakiwa kuchangia kiasi fulani katika Serikali, Wao wenyewe JKU hupangiana kila kikosi kuchangia kiasi fulani cha fedha kupeleka Makao Makuu ili ziwasilishwe Serikalini.
Wizara ya Fedha ndio wanaovipangia vyanzo vya mapato ya J.K.U vichangie kiasi gani , vipo vyanzo vya mapato ambavyo havijapangiwa kichangiaWizara ya Fedha huwambia tu huwambia JKU kuvhangia kiasi fulani cha fedha kutokana na vyanzo vyake vilivyoainishwa. Mapato mengine ya J.K.U yameruhusiwa watumie wenyewe /wafanye "retention".

Katika kulifuatilia suala la shamba la pamoja baina ya Zanzibar na Misri,Kamati ya PAC iliukagua mkataba husika na Ripoti ya Kamati ya Uchunguzi wa Mradi huo iliyotolewa mwaka 2017 pamoja na kufanya ziara katika shamba hilo na kupatiwa taarifa mbalimbali zikiwemo zifuatazo

Eneo la mradi lina jumla ya ekari 175 ambazo zinatumika kwa kilimo cha mbogamboga, matunda na uzalishaji mbegu

Majukumu ya Kikosi cha JKU

Majukumu ya Kikosi yamegawika katika sehemu mbili tofauti

a) Jukumu la kutoa nguvu kazi kwa mradi wa pamoja kati ya Serikali ya Misri na SMZ ambao unashughulikia Kilimo cha mboga mboga
b) Kusimamia miradi ya kikosi pamoja na kutoa mafunzo kwa vijana wa kujitolea ili kuwajenga uzalendo pamoja na uwezo wa kujiajiri baada ya kumaliza muda wao wa miaka miwili.

Mradi wa Pamoja

Mradi huu ni mradi wa Serikali ambao umeanzishwa tokea mwaka 2006 kisheria, ambapo Serikali mbili hizi zilikubaliuana kwa mkataba wa miaka kumi ambao kwa sasa umeshamalizika na hakujasainiwa mkataba mpya. Kuna majukumu ya upande wa Zanzibar na majukumu kwa upande wa Misri, kwa bahati mbaya baada ya Zanzibar kuona maendeleo ya mradi huo sio mazuri, Zanzibar ilizuia bajeti ya mradi huo.

Badala yake JKU kama chombo cha Serikali kilichokabidhiwa dhamana hii hufanya kasma kutika bajeti yake kusaidia huduma ndogo ndogo kama vile umeme katika matumizi ya nyumbani kwa wataalam hao, wakati mwengine kudanya matengenezo ya nyumba na vifaa vya ndani kwa wageni hao pamoja na harakati nyengine za uzalishaji.

Kwa upande wa Serikali ya Misri, bajeti yao ipo pale pale na pia wanaendelea kufanya maboresho ya kupunguza changamoto zinazojitokeza kama vile uwekaji wa umeme wa jua (solar) kwa kupunguza gharama za umeme wa ZECO.

Kwa sasa mradi una program ya kuzalisha mbegu za mbogamboga na matunda. Ekari 22 zinaendelea na maandalizi ya "drip irrigation" pamoja na ujenzi wa green house mpya 11 ambazo zitatumika kuzalisha mbegu bora na kuuzwa kwa wakulima wote wa Zanzibar

Chngamoto za Mradi

Changamoto za msingi ni:

1. Kutokuwa na mkataba mpya wa Mradi baada ya kumalizika mkataba wa awali, hivyo, tokea mwaka 2013 JKU inafanya kazi pasipokuwa na mkataba wa uendeshaji mradi.
2. Kukosekana kwa bajeti ya uendeshaji kutoka SMZ.
3. Kutokuwepo kwa Kamati ya Kusimamia Mradi wa pamoja kati ya Serikali ya Misri na Seriikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na badala yake kuachiwa M/s Meneja peke yake wa JKU.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kwa kuwa ni muda mrefu shamba la mradi wa pamoja bana ya Zaznzibar na Misri limekuwa halijatoa tija iliyokusdiwa ipo haja kubwa kwa Serikali kuifanyia mapitio Ripoti ya Kamati ya Uchunguzi wa shamba la mradi wa pamoja baina ya Zanzibar na Misri na kuyafanyia kazi pamoja na mambo mengine mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa katika Ripoti hiyo ya kitaalam iliyotolewa mwaka 2017 ili matumizi ya shamaba hilo yawe na tija kwa pande zote mbili.

ii. Serikali kupitia JKU iwekeze fedha zaidi katika miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji maji ili wapate uzalishaji wenye tija kubwa zaidi na kuiongezea mapato Serikali.

Taarifa ya Matumizi

Jeshi la Kujenga Uchumi kwa mwaka wa fedha lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi19,407,409,126 kwa matumizi ya kazi za kawaida na jumla ya shilingi 1,200,000,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 jumla ya shilingi 19,396,574,933 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 99 ya makadirio na jumla ya shilingi 1,200,000000 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 100 ya makadirioo.

Majibu ya JKU

Kwa mwaka wafedha 2017/2018 JKU iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi19,407,409,126 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Julai 2018 JKU imeshaingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 19,396,574,933 ambayo ni sawa na asilimia 99 yamakadirio.

MAKADIRIO NA MATUMIZI HALISI YA (OC) KWA MWAKA 2017/2018

| S/N | | MAKADIRIO | MATUMIZI HALISI |
|---|---|---|---|
| 1 | Mishahara | 18,207,409,126 | 18,203,773,983 |
| 2 | Matumizimengineyo | 1,200,000,000 | 1,192,000,950 |

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar ilitekeleza shughuli zake ipasavyo kwa uweledi na ufanisi mzuri kutokana upatikanaJI wa fedha kuwa mzuri katika shughuli zote zilizopangwa.

Kwa upande wa matumizi ya kazi za miradi ya maendeleo Jeshi la Kujenga Uchumi limetekeleza mradi moja ambao ni mradi wa Skuli ya Secondari JKU Mtoni yenye thamani ya shilingi 1,200,000,000.

MAKADIRIO NA MATUMIZI YA KAZI ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

| S/N | JINA LA MRADI | MAKADIRIO | MATUMIZI HALISI |
|---|---|---|---|
| | UjenziwaSkuliyaSekondari JKU Mtoni | 1,200,000,000 | 1,200,000,000 |

Katika mradi huu wa Ujenzi wa Skuli ya Sekondari JKU Mtoni kazi iliyofanyika kutokana upatikanaji wa fedha kwa mwaka huo ni kununua vifaa vya vjenzi vya kukamilisha Jengo la ghorofa tatu, kuweka lift na kufunga vifaa vya Zimamoto na Ukozi kwenye jengo la ghorofa tatu la skuli, kufunga kuta, milango na madirisha ya Aliminiam pamoja na kulipa gharama za kodi ya vifaa. Mradi tayari umeshakamililika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji juu ya sababu za kuongezeka kwa matumzi ua ya mishahara na kuelezwa kuwa ongezeko la mishahara lilitokana na kupandishwa vyeo, ajira mpya na uteuzi. Aidha, katikakujiridhisha na hali hiyomKmati ya PAC ilikagua ya barua ya maombi ya fedha bilioni 3.2 ikiwa ni upungufu wa mishahara kuanzia April hadi Juni 2018 yenye kumbukumbu No. MMJKU/4.20/11/A/Jd.A/192 ya tarehe 16 Machi 2018. Aidha, Kamati ya PAC ilielezwa kuwa fedha za matumizi mengineyo (O.C) kwa baadhi ya wakati huwa hazipatikani na inapotokea hivyo J.K.U hutumia mapato yao madogo madogo ya ndani katika kufanikisha matumizi ya O.C . Aidha , Kamati ya PAC ilkagua nyaraka mbalimbali zinazohusiana mipango na matumizi ya JKU ikiwemo Mpango Kazi na kuridhika na nyaraka hizo.

FUNGU D 04 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Taarifa ya Mapato

Ingawa kikosi cha KMKM hakikuainisha mapato katika Financial Statement yake iliyoiwasilisha kwa Ofisi ya Mdhibiti, Kamati ya PAC imebaini kuwa kikosi cha KMKM kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kilikadiriwa kuchangia mapato ya Serekali jumla ya Tshs 39,025,000/= na hadi kufikia 30/06/2018 kikosi hicho kilichangia wastani wa shilingi 25,000,000/= fedha hizo zilitokana na chanzo cha mapato ya shughuli za ujenzi.

Kamati ilihoji juu ya sababu za kutofikia malengo ya kuchangia Serikalini na kuelezwa kuwa ilitokana na kutolipwa vizuri na Taasisi za Serikali walizozijengea, Taasisi hizo za Serikali hulipa kwa mujibu wa uwezo wao. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilielezwa kuwa kwa vile hivi sasa Serikali inatumia Kampuni ya Ujenzi, hivyo chanzo hicho baadae kitakufa..Kamayi ya PAC PAC pia ilielezwa kwa karibu miezi sita (hadi Kamati ya PAC ilipofika KMKM tarehe 6/4/20121) walikuwa bado hawajapata kazi ya kujenga.

Kamati ya PAC pia ilihoji iwapo kikosi cha KMKM kina mipango ya vyanzo vipya vya mapato na kuelezwa kuwa KMKM ina mpango kuanzisha kituo cha huduma za ushauri wa mambo ya baharini na pia kuanzisha Kituoa cha Mafunzo ya ya kuogelea na mambo mengineyo

Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Kikosi cha KMKM kimepewa jukumu la kutoa ulinzi kwa kampuni za uchimbaji wa mafuta hasa baharini, hivyo KMKM inahitaji kuwa na vyombo vya kisasa, kuimarisha huduma za uzmiaji na huduma za doria ili iweze kutoa huduma hizo za ulinzi ipasavyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kwa kuzingatia azma ya Serikali ya kutilia mkazo Uchumi wa Buluu, Kamati ya PAC inaishuri Serikali kukiimarisha Kikasi cha KMKM ili kiweze kutoa huduma ya ulinzi ipasavyo kwa miundombinu pamoja na

rasilimali za Uchumi wa Buluuu

Taarifa ya Matumizi

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 22,149,042,650 kwa matumizi ya kazi za kawaida na jumla ya shilingi 4,120,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018, jumla ya shilingi 22,092,436,090 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 99 ya makadirio na jumla ya shilingi 4,085,680,849 sawa na asilimia 99 ya makadirio.

Majibu ya KMKM

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo KMKM Kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 kilikadiriwa kutumia jumla ya Tshs 22,149,042,650/= kwa matumizi ya kazi za kawaida, na jumla ya Tshs 4,120,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Tarehe 30 Juni 2018, jumla ya Tshs 22,092,436,090/= zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 99 ya makadirio na jumla ya Tshs 4,085,680,849/= sawa na asilimia 99 ya makadirio.

Uchambuzi wa miradi.

- Mradi wa ujenzi wa mahanga ulitengewa Tshs 620,000,000/- kwa maana kwamba Tshs 310,000,000/= zilitengwa na kupatiwa jumla ya Tshs 310,000,000/= kwa ujenzi wa kambi ya Kojani na Tshs 310,000,000/- zilitengwa na kupatiwa Tshs 235,000,000/= kwa ujenzi wa Kambi ya Makombeni, ambapo jumla ya Tshs, 545,000,000/- zilipatikana kwa ujenzi wa Kambi ya hizo, na Tshs 78,278,500/= zilibakia na kupelekwa kwenye ujenzi wa jengo la mama na mtoto.

- Ununuzi wa Boti za uokozi na Uzamiaji ambazo ilitengewa Tshs, 2,100,000,000 na kupatiwa jumla ya Tshs 2,100,000,000/=

- Ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto, ulitengewa jumla ya Tshs, 1,400,000,000/- na kuingiziwa jumla ya Tshs, 1,478,278,500/=.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa Mkaguzi wa Ndani wa KMKM anatoka Wizrani na huenda kukagua KMKM kila baada ya miezi mitatu. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kuwa kikosi hicho cha KMKM hakina Ripoti hiyo ya Ukaguzi wa Ndani.

Aidha, Kmati ya PAC ilibaini kuwa makadirio ya mishahara ya KMKM kwa mwaka 2017/2018 ni shilingi 17,565,400,000 ambapo matumizi hali halisi ya mishahara yalikuwa ni shilingi,19,180,436,440. Mishahara ilongezeka kutokana na kuongezeka kwa mishahara ya Serikali.
Kwa upande wa miradi ya maendeleo Kamati ya PAC ilielezwa kuwa fedha za ujenzi wa kambi ya Makombeni

zilipata upungufu kutokana na fedha zake kupelekwa kwa ajili ya ujanzi wa jingo la mama na motto.

## Hoja Namba 5.2.4.1 Dosari katika utayarishaji wa malipo shilingi 1,456,010,000

Ukaguzi umebaini katika hesabu ya matumizi ya maendeleo Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo ya shilingi 1,456,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa pamoja na gharama za ujenzi wa wa hospitalu ya mama na watoto. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kufanyika kwa kwa malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa njia ya fedha taslimmu (Cash Payment) badala ya kutumia hundi zenye jina la msambazaji wa vifaa husika, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nambari 12 ya mwaka 2016. Uchambuzi wa malipo hayo unaonekana katika jadweli lifuatalo:-

| Nambari ya Hati ya Malipo | Nambari ya Hundi | Jumla ya fedha iliyolipwa | Aliyelipwa | Maelezo ya Malipo |
|---|---|---|---|---|
| 1/8 | TT | 132,231,000 | KMKM CANTEEN | Ikiwa ni malipo ujenzi wa bweni (hanga) pamoja na kota guard kambi ya Kojani Pemba |
| 2/8 | TT | 262,560,000 | KMK CANTEEN | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Jengo la hospitali la mama na watoto |
| 3/11 | TT | 85,125,000 | KMKM CANTEEN | Ikiwa ni malipo ya gharama ya ujenzi wa jengo la hospitali la mama wajawazito |
| 1/1 | TT | 174,595,000 | KMKM CANTEEN | Ikiwa ni malipo ya gharama ya ujenzi wa jengo la hospitali la mama wajawazito |
| 2/1 | TT | 225,405,000 | KMKM CANTEEN | Ikiwa ni malipo ya gharama ya ujenzi wa jengo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | la hospitali la mama wajawazito |
| 1/5 | \TT | 342,000,000 | KMKM CANTEEN | Ikiwa ni malipo ya gharama za umalizaji wa jengo la mama na watoto KMKM |
| 2/5 | TT | 234,094,000 | KMKM CANTEEN | Malipo ya ujenzi wa hanga la kulala askari kambi ya Makombeni, Pemba |
| Jumla | | 1,456,010,000 | | |

Majibu ya KMKM

Ni kweli Dosari hiyo ilikuwepo katika utayarishaji wa Malipo hayo. Hii ilitokana na utaratibu ambao ulikua ukitumika na Kikosi katika matumizi yake mbali mbali ya kibajeti kwa matumizi ya kimaendeleo na yale ya kawaida. Hata hivyo kwa hivi sasa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) tayari kimeshafanya marekebisho kwa kuwacha kutumia Canteen ya KMKM kwa malipo ya fedha taslim (Cash) katika huduma za malipo ya Ujenzi na Miradi yetu mbali mbali, kwa sasa tunatumia supplier katika kupata huduma za manunuzi ya vifaa mbali mbali.
Kikosi maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimefanya maamuzi hayo baada ya kupokea Ushauri kutoka kwa wakaguzi wa ndani na nje kwa lengo la kufata taratibu za manunuzi kama sheria inavyoelekeza. Hivyo kwa mujibu wa ushauri uliotolewa na wakaguzi hao KMKM haikua na pingamizi juu ya kufata utaratibu wa kisheria wa kufanya manunuzi kwa fedha za Umma.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilibaini kuwa katika miaka ya nyuma walikuwa wakitumi kupitia Kanteen, hivyo vifaa vyote vya ujenzi vilikuwa vinatumia akaunti ya moja tu, na fedha zote zilizoainishwa zilikuwa katika akaunti moja
Kamati ya PAC iltaka kujua kuhusu Kaa duka hilo kufanyanteen na Ikuelezwa kuwa Kanteen ni duka la KMKM ambalo linaingizwa bidhaa zote. Hivyo, KMKM ilinunua vifaa hivyo vya ujenzi kutoka duka hilo.

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali za malipo na kubaini yafuatatyo:

i. Hati za malipo kuwa na saini moja tu ya muidhinishaji (Authorizing Officer) kipengele cha Head of Account hakina saini. Aidha, sehemu ya Mlipaji (Payong Officer) haina saini.

ii. Ankara zilizotumika kukosa saini mfano Ankara (invoice) ya KMKM Kanteen ya tarehe 1/9/2017 yenye namba 00108 yenye jumla ya shilingi 262,560,000
iii. Delivery Note na Issue Note za ghalani hazikupatikana kwa ukaguzi ili kuthibitisha kama vifaa vilivyonunuliwa vimeingizwa ghalani kurekodiwa na kutolewa kwa ajili ya matumizi kwa mujibu wa taratibu.
iv. Uwekaji mbaya wa kumbkumbu za kifedha uliopelekea ktopatikana kwa ukaguzi hati moja ya mwisho ya malipo namba 2/5 (T/T) yenye jumla ya shingi 234,094,000 kwa ajili ya malipo ya ujenzi wa hanga la kulala askari kambi ya Makombeni, Pemba.
v. Mpango Kazi na Mapngo wa Ununuzi haukupatikana kwa ukaguzi ili kuthibitisha kama matumizi (ununuzi) yalifanywa kwa kuzingatia mipango hiyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Watebdaji wa KMKM wjipange kutekeleza kazi zao kwa mujibu wa tarartibu zinazoongoza kazi zao wakiwemo watendaji wa masuala ya kifedha, Afisa Mipango, Afisa Ununuzi na Mtunza ghala ili waweze kutekeleza kazi zao bila ya kujiingiza kwenye matatizo yatakayoharibu kazi zao.

## FUNGU D 06 KIKOSI CHA VALANTIA

Taarifa ya Mapato

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Kikosi cha Valantia kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 651,061,248 kutoka vyanzo vyake mbali mbali. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018 jumla ya shilingi 651,061,248 zilikusanywa sawa na asilimia 100 ya makadirio.

Majibu ya Kikosi cha Valantia

Chanzo cha mapato kwa Kikosi cha Valantia ni kutoa huduma ya Ulinzi, na kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Kikosi kiliidhinishiwa kukusanya shilingi 45,530,000/= ili kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 Kikosi kiliweza kuchangia shilingi 33,400,000/= sawa na asilimia 73.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilibaini kuwa Kikosi cha Valantia kilifanya makosa katika “Financial Statement”yao kk=wa kuainisha makadirio ya makusanyo ya shilingi 651,061248. Kikosi cha Valantia kilieleza Kmati ya PAC kuwa haina taarifa za makadirio ya mapato hayo ingawa taarifa hizo zimo katika taarifa za za fedha za mwisho wa mwaka zilizowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Mhasibu wa Kikosi hicho wa wakati huo alyesaini Financial Statement hiyo (Ndg Juma Haji Haji) ilibainika kuwa alisaini bila ya kuangalia na alikuwa hajui vizuri. Vilevile Kamati ilibaini kuwa Taarifa hizo za kifedha hazikuandalaiwa na Mhasibu huyo bali iliandaliwa na Captain Mwevura ambae anaaminika kuwa ndo mtaalam wa kuaanda taarifa za fedha ingawa

hakuwa Mhasibu wa Kikosi hicho, hata hivyo nae hakuweza kutoa ufafanuzi juu ya kiwango hicho cha fedha za mapato katika "financial statement

Aidha, katika makusanyo halisi kuna makosa mengine yametendeka ambapo katika financial statement ya Kikosi cha Valantia inaonesha makusanyo ya shilingi 41,000,000 na sio shilingi 33,000,000 kama ilivyoelezwa katika majibu ya ya Kikosi cha Valantia. Kikosi cha Valantia kiilikiri kufanya makosa yote hayo na kuithibitishia Kamati ya PAC kuwa makusanyo halisi ya Kikosi hicho kwa mwaka 2017/2018 ni shilingi 33,400,000.

Kwa upande mwengine Kamati ya PAC ilihoji juu ya sababu za kutofikia malengo ya makusanyo na kuelezwa kuwa ilisababishwa na kupelekwa kwa huduma za ulinzi kwa Wakala wa JKU. Vilevile kutolipwa kwa madeni kutoka taasisi mbalimbali ilizokuwa inazidai kutokana na huduma ya ulinzi iliyozipatia katika kipindi cha nyuma. Kwa mujibu wa barua zilizowasilishwa katika Kamati zilikuwa zinaonesha kuwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)ilikuwa inadaiwa shilingi 69,000,000, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (ZAA) shilingi 35,000,000, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalim Nyerere shilingi 8,170,000. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kuwa Kikosi cha Valantia hakina vilelezo vya kutosha kuthibitisha madeni hayo yote kwa ujumla.

Kwa ujumla Kamati haikuridhika na majibu na ufafanuzi pamoja na yale yaliyojitokeza juu ya uandaaji wa taarifa ya fedha ya mwaka (Financial statement)

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kikosi cha Valantia kiwe na utaratibu mzuri wa kuweka kumbkumbu za taarifa muhimu ikiwemo mikataba wnayoingia na taasisi mbalimbali

Taarifa ya Matumizi

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Kikosi cha Valantia kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 9,788,400,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 400,000,000,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018 jumla ya shilingi 10,737,265,628 zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 109 ya makadirio na juml ya shilingi 248,875,000 kwa kazi za maendeleo sawa na asi;imia 62 ya makadirio.

Majibu ya Kikosi cha Valantia

Kikosi cha Valantia kwa mwaka 2017/2018 kiliidhinishiwa kutumia Shilingi 10,188,400,000/=hadi kufikia Juni 30, 2018 Kikosi kilifanikiwa kupata shilingi 11,013,140,628/= sawa na asilimia 108 kama mchanganuo unavoonekana hapo chini.

MCHANGANUO WA MATUMIZI YA KVZ KWA MWAKA 2017/2018

| MAELEZO | KILICHOPANGWA | KILICHOPATIKANA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mshahara na maposho | 9,093,800,000/= | 10,022,782,940/= | 110% |
| Matumizi mengineyo (OC) | 694,600,000/= | 714,482,688/= | 102% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kazi za Maendeleo | 400,000,000/= | 248,875,000/= | 62% |
| JUMLA KUU | 10,188,400,000/= | 11,013,140,628/= | 108% |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji juu ya sababu za kuongezeka kwa mishahara na kuelezwa kuwa ongezeko hilo lilitokana na kupandishwa vyeo kwa askari. Katika mishahara kulikuwa na upungufu kulingana na Cyling waliyopewa. Vielelezo husika vimekaguliwa na Kamati ya PAC(barua ya terehe 20/7/2017 yenye nambari ya kumbukumbu CUB.228/281/0429inayohusu kupatiwa shilingi 5,475,500 ili kuwalipa tofauti ya mishahara walipandishwa vyeo katika Kikosi cha Valantia.

Kuhusu kazi maendeleo, Kamati ya PAC ilibaini kuwa kazi ya maendeleo iliyofanyika ilikuwa ni jingo la ushoni ambapo vilinunuliwa vifaa kwa jili ya ujenzi hatua ya mwanzo za kuweka janvi ingawa hawakuweza kumaliza (hatua ya kuweka jamvi). Shilingi milioni 248 zilitumika katikakuweka jamvi sehemu ya chini ingawa hawakumaliza.

Aidha, kamati ya PAC imekagua Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani (Jan – Machi 2018) na kubaini kasoro kadhaa zilizobainishwa katika Ripoti hiyo zikiwemo ukosefu wa mikataba, kuchelewa kuingiza taarifa za matumzi katika Cash book pamoja na kasoro za hati za malipo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kikoai cha Valantia kizifanyie kazi kasoro zote zilizobainikakatika Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani (2017/2018) zikiwemo za ukosefu wa mikataba na kuchelewa kuingiza taaifa za kifedha katoka daftari lamkumbukumbu za kifedha (Cash book)

WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII

Uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya Ukaguzi

Kwa mujibu wa Ripoti ya Ukagu, Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii ilichelewa kuwasilisha Taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka wa 2017/2018 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo iliwasilisha taarifa hizo tarehe 21/11/2018 kinyeme na kifungu cha 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016 kinachozitaka Wizara na Taasisi za Serikali kutayarisha na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kumaliza mwaka wa fedha ambapo hesabu hizo zitajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi hizo.

Majibu ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii

Ripoti iliyotajwa hapo juu ilichelewa kwa sababu zifuatazo:-
(i) Kutokea kwa mabadiliko ya nafasi ya uhasibu kwa Muhasibu aliekuwepo kubadilishana na Muhasibu

mwengine (muhasibu alikua mpya).

(ii) Muhasibu alikutana na zoezi la Usajili wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na aliagizwa kusimamia shughuli za matumizi ya zoezi hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilibaini kuwa ingawa Mhasibu aliyehusika alikuwa mpya kwa wakati huo kazi ya kuandaa Taarifa za Kifedha mapema kwa mhasibu aliyeeondoshwa changamoto ya kuchelewa kuwasilisha taarifa za fedha za mwaka ingepungua.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Mhsaibu wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii pamoja na Wahasabu wengine wa Taasisi za Serikali wakusanye mapema taarifa mbalimbali zinazohitajika katika kuandaa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka ili taarifa hizo za fedha ziweze kukamilika na kuiwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati uliowekwa kisheria.

Taarifa ya Mapato

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wakala Usajili wa Matukio ya Kijamii walikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 275,230,000 kutoka vyanzo mbali mbali. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018 jumla ya shilingi 240,597,350 sawa na asilimia 87 ya makadirio.

Majibu ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii

Wakala imeshindwa kufikia kiwango cha makusanyo yaliyokadiriwa kwa kukosekana asilimia 13, kutokana na makadirio hayo kuwa makubwa kulingana na uhalisia wa vyanzo vilivyopo. Aidha Vitambulisho vya Wageni havikuweza kuingiza chochote kutokana na shughuli za Usajili kwa ajili ya utoaji wa Vitambulisho vya aina hiyo, kutoanza ndani ya mwaka huo wa fedha 2017/2018.

MCHANGNUO WA MAPATO KWA MWAKA 2017/2018

| S/N | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO | AKUSANYO | ASILIMIA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uandikishwaji wa Vizazi na Vifo | 191,603,000 | 173,732,350 | 91 |
| 2 | Uandikishwaji wa Ndoa na Talaka | 47,901,000 | 33,899,000 | 71 |
| 3 | Ada ya Vitambulisho | 17,963,000 | 32,966,000 | 184 |
| 4 | Mapato ya Vitambulisho vya Wageni | 17,963,000 | 0 | 0 |
|  | JUMLA | 275,430,000 | 240,597,350 | 87 |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilihoji juu ya sababu za kutoanza utoaji wa vitambulisho kwa wageni na kuelezwa kuwa sababu ni mfumo wa kusajili ambapo ilibainika kuwa lengo la kuanzishwa Mfumo huo ni Usajili na utoaji wa Vitambulisho maalum kwa wageni (Alien Identity Cards) kwa wakaazi wanaoishi Zanzibar kwa mujibu wa Sheria pamoja na baadhi ya Watanzania ambao ni wakaazi na hawajatimiza masharti ya kisheria ya kupewa Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Mfumo wa awali wa Usajili wa Wageni ulikamilika tangu mwaka 2016 na ulitarajiwa kuanza kazi katika mwaka wa Fedha wa 2016/2017. Hata hivyo kazi za Usajili hazikuweza kuanza kama ilivyokusudiwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo:-

1. Agizo rasmi la kuanza kwa Usajili wa aina hiyo halikutolewa na Serikali kutokana na mgongano wa majukumu kati ya Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho wakati huo na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa NIDA. NIDA walianza kusajili wageni waishio Zanzibar kisheria tangu mwaka 2015. Hivyo ilionekana kuwa kungekuwa na usumbufu kwa Wageni wanaoishi Zanzibar kusajiliwa mara mbili.

2. Ofisi hii nayo baada ya kuanzishwa kwake, ilijipanga tena kuanza kutumia Mfumo huo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, lakini ilishindwa kwa sababu mkwamo uliokuwepo awali bado ulikuwa haujapatiwa Ufumbuzi. Aidha mwezi Februari 2018, Serikali iliamua kuubadili Mfumo uliopo na kuanza kutengeneza Mfumo mpya wa Usajili wa Vitambulisho vya Mzanzibari. Hali hii ilipelekea Mfumo uliokuwepo wa Usajili wa Wageni nao utengenezwe upya kwa sababu mifumo yote hii inatumia teknologia ya aina moja katika Utoaji wa kadi husika. Kulikuwa na ulazima wa kutengenezwa Mfumo mpya wa Usajili wa Wageni.

3. Awali ilipangwa na Ofisi hii kuwa, mara baada ya Mfumo husika kukamilika, katika robo mbili za mwaka wa fedha 2020/21 zoezi la Usajili wa Wageni lianze endapo mazungumzo baina ya SMZ na SMT kuhusu jambo hilo yatakuwa yamekamilika. Hadi sasa mfumo huu bado haujaanza kutumika kwa ajili ya Usajili wa Wageni kwa sababu mbalimbali zikiwemo:-

-Unasubiriwa muongozo mpya wa Serikali ya awamu ya 8 wa namna ya kuendelea na jambo hilo. Ofisi hii tayari imeshaanda ‘draft’ ya Kanuni 3

kwa ajili ya Usajili wa aina hiyo na pia imesha 'design' aina ya Kadi ambazo zinapendekezwa zitolewe kwa ajili ya Wageni. Kadi hizo tayari ameshafikishiwa Waziri mwenye dhamana kwa ajili ya kupata muongozo wa Serikali.
-Awali ilipangwa kuwa endapo kadi hizo zitakubaliwa, zinunuliwe ndani ya mwaka wa Fedha 2020/21 ili mara tu baada ya Mfumo na taratibu husika kukamilika, zoezi husika lianze. Hatua hiyo ya kuzinunua kadi hizo haikuwezekana kwa sababu za uhaba wa fedha za bajeti.

Aidha, Kamati imebaini kuwa Sheria ya Wakala (Namba 3/2018) inawataka pia kuwasajili wakaazi wazawa ambao wanatoka Tanzania Bara ambao hawatimizi masharti ya kupewa ZANID. Pia kuna wgeni kutoka nje ambao wanaishi Zanzibar kisheria.. HivyoWakala wa usajilu wa Vitambulisho hutoa vitambulisho vifuatatvyo

1) Kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi
2) Kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibar Mkaazi (a.) Tanzania Bara na (b) Wageni kutoka nje.

Vile vile Kamati ya PAC ilihoji juu ya sababu za uandikishwaji wa ndoa na talaka kutofikia asilimia 100 na kuelezwa kuwa ababu ni mwamko mdogo wa usajili wa ndoa na talaka kutoka kwa jamii ni Wanaokwenda kusajili ndoa ni watu wanaotaka kusafiri au wengine wanaotaka kuolewa tena hivyo, wanakuja kuchukua vyeti vya ndoa. Changamoto ni kuwa wananchi hawana msukumo/pressure ya kuvifuata kama ilivyo kwa vyeti vya kuzaliwa. Ada ya cheti ch ndoa ni Tsh25,000/-Ada ya kitambulisho ni Tsh.10,000/= na kinachohitaji marekebisho kinatozwa shilingi.5,000/-

Zaidi ya hayo, kwa kutaka kufanya mlinganisho wa mapato, Kamati ya PAC ilihoji juu ya mapato yatokananyo na uandikihsaji wa vizazi na vifo kwa mwaka 2019/2020 na kuelezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi hiyo ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 135,000,000/= kwenye chanzo hicho na ilifanikiwa kukusanya shilingi 89,000,000/= sawa na asilimia 65 ya mapato katika chanzo hicho.

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii iwe na udhibiti mzuri wa vitambulisho vya mzanzibari kwa kuwapatia vitambulisho hivyo wale wanaohusika peke yake.
ii. Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii iandae utaratibu wa kutoa elimu katika vyombo vya habari pamoja na kufanya mipango ya kutoa elimu katika maeneo ya vijijini (outreach programme)
iii. Kwa kuwa watu wengi hawana vyeti vya ndoa, kuna haja kwa wadau mbali kutoa mwamko kwa wanaofungisha ndoa kuwambia wanandoa kukata vyeti vya ndoa.

## Taarifa ya Matumizi

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa mwaka wa fedha 2017/2018 walikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,660,800,000kwa kazi za kawaida na jumla ya shilingi 2,105,790,135 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa ni asiimia 96.4 ya makadirio na jumla ya shilingi 45,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 9 ya makadirio.

Majibu ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii

Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,660,800,000/= kwa kazi za kawaida na jumla ya shilingi 500,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018 jumla ya shilingi 2,105,790,135/= zilipokelewa na kutumika kwa kazi za kawaida na jumla ya shilingi 45,000,000/= zilipokelewa na kutumika kwa kazi za maendeleo.

Matumizi ya Kawaida

Makadirio ya Mishahara yanaonekana kuwa makubwa kwa asilimia 9 kwa sababu yaliingiza pia nyongeza za Posho kwa kila Mfanyakazi. Pamoja na fedha hizo kuwekwa kwenye Bajeti, zilihitaji kibali cha Utumishi ambacho hakikupatikana hali iliyopelekea Wafanyakazi hao kukosa Posho hizo. Kwa upande wa matumizi mengineyo (OC), kulikuwa na upungufu wa fedha kwa asilimia 29, hali ambayo ilipelekea baadhi ya shughuli zilizopangwa kutofanyika. Miongoni mwa shughuli hizo ni pamoja na kushindwa kulipwa ipasavyo kwa gharama za mabuku ya Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka pamoja na mahitaji mengine, kutoka Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZAGPA), hatua ambayo imepelekea Ofisi hii kuwa na madeni.

MCHANGANUO WA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2017/2018

| S/N | MATUMIZI | MAKADIRIO | MATUMIZI HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MISHAHARA | 1,107,800,000 | 1,003,032,315 | 91 |
| 2 | MATUMIZI MENGINEYO (OC) | 1,553,000,000 | 1,102,763,820 | 71 |
| JUMLA | | 2,660,800,000 | 2,105,796,135 | 79 |

Matumizi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, ilikuwa na mradi wa maendeleo wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Vizazi,Vifo, Ndoa na Talaka Civil Registration and Vital Statistics (CRVS). Fedha zilizopatikana zilikuwa ni 45,000,000 ambazo zilitumika kununulia Server kwa ajili ya Mfumo wa CRVS na samani (Furnitures).

MATUMIZI YA MRADI WA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/2018

| S/N | MRADI | MAKADIRIO | MATUMIZI HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | KUIMARISHA MFUMO WA VIZAZI NA VIFO | 500,000,000 | 45,000,000 | 9 |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebini kuwa baada ya kuunganishwa Idara ya Vizazi na vitambulisho – Vizazi walikuwa na maposho nyeti na posho ya mazingira magumu. Lakini kulikuwa na changamoto za baadhi ya wafanyakazi kuwa na posho tofauti.Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamiiwaliomba kuwa posho walizozipata katika Taasisi moja (Vizazi) ziwe kwa Taasisi yote.

Kwa upande wa madeni, Kamati ya PAC imebaini kuwa Wakala wana deni kubwa linalodaiwa na Taasisi na Kampuni mbalimbali ambapo linekuwa likiongezeka. Wakala wa Uchapishaji wa Serikali (ZAGPA) wanaidai Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii shilingi milioni 130. Aidha,Kmapuni za ZIT Soltuion,Stone town na House of Stationeries pia zinawadai Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii madeni tofauti.

Aidha,Kamati ya PAC imebaini kuwa Watu 30,000, walikuwa hawana vyeti hadi Machi 2018. Hadi mwezi April 20121 walikuwa wamebakia watu 1,000 ambao hawajapatiwa vyeti vya vya kuzaliwa.

Kamati ya PAC ilielezwa kuwa kiutaratibu ndani ya siku 42 mtoto aliyezaliwe anatakiwa asajiliwe, kuanzia siku ya 43 na kuendelea huwa anafanyiwa usajili uliochelewa (late registration) Vile vile, Kamati imebaini kuwa wageni wengi wanatumaia njia ya vizazi vilivyochelewa kupata vyeti vya kuzaliwa. Wageni wanaomba vyeti na baada ya uhakiki imegunduliwa kuwa wengi hawastahili kupewa vyetu vya kuzaliwa , Wananchi wengine wanatimia nafasi hiyo (ya lete registration) kubadilisha umri, majina nakadhalika. Hadi kufikia mwezi Aprili 2021kulikuwa kuna maombi ya 7000 ya aina hiyo.

Kamati ya PAC pia ilipata nafasi ya kuukagua Mpango wa Ununuzi wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii na kubaini kuwa Mpango huo haukuainisha ni Mpango wa ununuzi wa Taasisi gani.

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Watendaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio wa Matukio ya Kijamii wakae pamoja ili kufahamu kwa kina changamoto zinazoikabili Ofisi hiyo na kubuni njia za kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo.

2. Watendaji wa masuala ya fedha watilie mkazo uwekaji mzuri wa kumbukumbu za fedha hata wanapotengeneza magari na shughuli nyenginezo.

3. Afisa Ununuzi wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii anapaswa kuona mbali na kufahamu mipango yote ya ununuzi ya Taasisi na kuiingiza katika Mpngo wa Mwaka wa Ununuzi (Annual Procurement Plan)

## FUNGU F 01 WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

### Taarifa ya Mapato

Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilikaqdiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,044,413,527,000 kutoka katika vyanzo vyake vya kodi na visivyo vya kodi.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 jumla ya shilingi875,669,135,400 zimekusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya kodi na visivyo vya kodi sawa na asilimia 83.5 ya makadirio Mchanganuo wa wa makusanyo ni kama ifuatavyo:-

| Chanzo cha Mapato | Makadirio 2017/2018 Tsh Milioni | Makusanyo Halisi 2017/2018 | Asilimia ya Makusanyo |
|---|---|---|---|
| Bodi ya Mapato (ZRB) | 347,289,392,000 | 346,875,657,136 | 99.9 |
| Mmalaka ya Mapato (TRA) | 258,723,935,000 | 255,949,366,000 | 98.9 |
| Gawio la Mashirika | 3,000,000,000 | 1,775,957,892.30 | 59.2 |
| Gawio la BOT | 3,000,000,000 | 13,500,000,000 | 450 |
| Mapato yasiyo ya kodi | 22,400,000,000 | 36,948,983,285.86 | 164.9 |
| Mikopo ya Ndani | 30,000,000,000 | 20,000,000,000 | 66.7 |
| | 380,000,000 | 196,992,000,000 | 51.8 |
| Jumla | 1,044,413,527,000 | 872,041,964,314 | |

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,044,413,527,000 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka vyanzo vyake vya kodi na visivyokuwa vya kodi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018 jumla ya shilingi 875,669,135,400 zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia 83.5 ya makadirio.

Taarifa za mapato zinajumuishavianzio vya mapatoyatokanayona kodi, ruzuku na mikopo, misaada kutoka Nje,mapato yasiyo ya kodi na misamaha ya madeni. Aidha,mchanganuo wa makusanyo ni kama inavyoonekana hapo chini:-

Mchanganuo wa Makusanyo

| Chanzo cha Mapato | Makadirio 2017/2018 Tsh. Milioni | Makusanyo Halisi 2017/2018 Tsh. Milioni | Asilimia Ya Makusanyo |
|---|---|---|---|
| Bodi ya Mapato (ZRB) | 347,289,592,000 | 346,875,657,136 | 99.9 |
| Mamlaka ya Mapato | 258,723,935,000 | 255,949,366,000 | 98.9 |
| Gawio la Mashirika | 3,000,000,000 | 1,775,957,892.30 | 59.2 |
| Gawio la BOT | 3,000,000,000 | 13,500,000,000 | 450 |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 22,400,000,000 | 36,948,983,285.86 | 164.9 |
| Mikopo ya Ndani | 30,000,000,000 | 20,000,000,000 | 66.7 |
| Mapato kutoka kwa washirika wa Maendeleo | 380,000,000,000 | 196,992,000,000 | 51.8 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jumla | 1,044,413,527,000 | 872,041,964,314 | 83.5 |

Uchuinguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilihoji juu ya vigezo vinavyotumika kufanya makadirio katika vyanzo vya mapato katika Mawizara na kuelezwa kuwa miongoni mwa njia zinazotumika ni kuangalia mwenendo wa ukusanyaji wa vyanzo hivyo, pia wanashirikiana na sekta husika na wadau mbali na kufanya mashauriano.

Aidha,Kmati imebaini kuwa ni mashirika manne  yenye faida ndio yanayotoa gawio ambayo ni Shirika la Bandari, Shirika la Bima, Shirika la Umeme (ZECO) na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kuna haja ya kutafuta njia mbadala ya kujua vyanzo vya mapato nauwezo wa vyanzo hivyo kwa kuwa kunakuna Taasisi zinaoonekana kupewa makisio madogo ya kukusanya mapato ambapo baadhi ya Taasisi zilizopewa makidirio ya mwaka zina uwezo wa kukusanya mapato hayo kwa mwezi mmoja tu.

ii. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ifanya utafiti wa kina ili kubaini Taasisi zenye makusanyo makubwa lakini hazichangii katika Mfuko Mkuu wa Serikali ili Taasisi hizo ziweze kuongeza mapato ya Serikali..

Taarifa ya Matumizi

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizaraya Fedha na Mipango iliidhiishiwa kutumia shilingi 18,519,838,000 kwa matumizi ya kawaida, shilingi 10.210,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na shilingi 27,853,510,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Washirika wa Maendeleo na shilingi 29,263,900,000 ikiwa ni ruzuku kwa Taasisi mbali mbali zilizopo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018 jumla ya shilingi 16,208,568,130 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 87.5, shilingi 5,432,975,382 zimeingizwa na kutumika sawa na asilimia 53 ya makadirio.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Ofisi ya Rais,Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi18,519,838,000 kwa kazi za kawaida,Shilingi 10,210,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na shilingi 27,853,510,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa washirika wa maendeleo. Aidha,Shilingi 29,263,900,000 zilikadiriwa kutumikaikiwa ni ruzuku kwa taasisi mbali mbali zilizopo chini ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.
Hadi kufikia 30 Juni, 2018 jumla ya shilingi 16,208,578,130 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 87.5 , shilingi 5,453,975,382 zimeingizwa na kutumika sawa na asilimia 53 ya makadirio kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, jumla ya shilingi 19,578,598,508 sawa na asilimia 70 ya makadirio ziliingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo ikiwa

ni mchango wa washirika wa maendeleo na Shilingi 29,450,377,981 sawa na asilimia 101 ya makadirio

:Mchanganuo wa Matumizi.

| Maelezo | Makadirio ya Bajeti TZS | Matumizi Halisi TZS | Wastani |
|---|---|---|---|
| Mishahara na Maposho | 8,287,538,000.00 | 6,714,335,130.00 | 81% |
| Matumizi Mengineyo | 10,232,300,000.00 | 9,494,243,002.96 | 93% |
| Ruzuku | 29,263,900,000.00 | 29,450,377,981.00 | 101% |
| Mchango wa Serikali (SMZ) katika shughuli za maendeleo | 10,210,000,000.00 | 5,453,975,382.00 | 53% |
| Mchango wa Washirika wa maendeleo | 27,853,510,000 | 19,578,598,508.20 | 70% |
| JUMLA | 85,847,248,000.00 | 70,691,530,004.16 | 82% |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilikagua Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani na kubaini dosari mbalimbali ikiwemo kuwepo kwa vifaa vyenye thamani ya shilingi 57,000,000 ambavyo hakuingizwa katika daftari la ghalani
Kamati ililiwasiisha suala lakutokuwepo kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Idara Maalum za SMZ ambapo Kmati ya PAC ilielezwa kuwa alikuwa amehamishiwa katika Kampuni ya Ujenzi ya Serikali na kwa kipindi cha miezi 6 nafasi hiyo ilikuwa wazi.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali wakae pamoja na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ili kujadili masuala mabalimbai yanayohusu wakaguzi wa Ndani wa Idara Maalum za SMZ ikiwa ni pamoja na kulishughulikia suala la kutokuwepo kwa Mkagu wa Ndani Mkuu wa Idara Maalum za SMZ.

FUNGU F02 - HESABU ZA HUDUMA ZA MFUKO MKUU WA SERIKALI.

Kwa mwaka wa fedha 20172018 Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali ziliidhinishiwa kutumia shilingi 150,710,000,000 kwa ajili ya utoaji wa huduma mbali mbali za Mfuko Mku zikiwemo ilipaji wa Kiinua Mgongo, Pencheni na malipo ya huduma za hati fungani. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 jumla ya shilingi 140,163,426,544 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na aslimia 93 ya makadirio. Aidha, Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali ulikuwa na salio la shilingi 706,935,242 mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2017/2018 katika hesabu yake ya Amana (Public Dept Deposit Account) ambazo zilitumika kwa malipo ya Viinua Mgongo na matumizi menngine maalum ya Serikali. Hadi kufikia Juni, 2018 Hesabu hii ya Amana ilikuwa na bakaa ya shilimgi 1,591,510,592.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Mfuko Mkuu wa Serikali unahusisha usimamizi wa matumizi ya huduma zinazotolewa na Mfuko Mkuu wa

Serikali ikiwemo ulipaji wa Kiinua Mgongo na Pencheni kwa Wastaafu wa SMZ, kulipa madai ya Wazabuni wa Serikali, kulipia hati fungani zilizofikia muda na malipo mengineyo. Katika mwaka wa fedha 2017-2018, Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali ulikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi150.71 bilioni na hadi kufikia Juni 30, 2018 jumla ya Shilingi140.163 bilioniambazo ni sawa na asilimia 93 ya makadirio zimeingizwa na kutumika. Jadueli lifuatalo linaainisha utekelezaji wa matumizi kwa Mfuko Mkuu wa Serikali:

Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali

| Vianzio | Makadirio2017-2018TZS | Matumizi Halisi 2017-2018 TZS | Wastani |
|---|---|---|---|
| Hati Fungani | 11,726,000,000.0 | 10,428,771,152.00 | 89% |
| Mikopo ya Ndani | 5,160,000,000.00 | 5,160,000,000.00 | 100% |
| Kiinua Mgongo | 31,366,000,000 | 23,892,249,051 | 76% |
| Pencheni | 23,000,000,000.00 | 21,958,242,178.00 | 95% |
| Wazabuni wa Serikali | 9,500,000,000.00 | 9,500,000,000.00 | 100% |
| Malipo Mengineyo | 69,958,000,000 | 69,224,164,163 | 99% |
| Jumla | 150,710,000,000 | 140,163,426,544 | 93% |

Katika Bajeti yamwaka 2017/2018 Mfuko Mkuu wa Serikali ulikosa asilimia saba (7%) ya Bajeti yake uliyojipangia na kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi. Upungufu huo ulipelekea Mfuko kushindwa kukamilisha lengo lake hususan katika ulipaji wa viinua mgongo vya wastaafu wa Serikali na hivyo kulimbikiza deni hilo kwenda mwaka unaofuata wa fedha. Hali hii hupelekea malalamiko kutoka kwa wastaafu waliosogezwa mbele katika malipo hayo.

Changamoto za Kifedha ambazo Mfuko Mkuu wa Serikali unazipata ni pamoja na uhaba wa upatikanaji fedha za matumizi ukilinganisha na makisio. Hii husababishwa na ukusanyaji wa mapato kuwa wa chini na hivyo kupelekea matumizi kuchelewa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na haikuwa na Maelezo zaidi.

### 5.5.2.1 Malipo yaliyofanywa naHazina kutokana na adhabu ya kuchelewa kulipa madeni kwa muda mrefu USD 200,120.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, ukaguzi umebaini kuwa hesabu ya huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali imefanya malipo kupitia hati nambari PV16/02/2018 yenye thamani ya USD 200,120.00 aliyolipwa Hassan & Sons kutokana na kucheleweshewa malipo ya malimbikizo ya madeni anayoidai Serikali kwa muda mrefu. Aidha, ukaguzi haukuweza kupatiwa mkataba baina ya kampuni ya Hassan & Sons na Serikali ili kuweza kujiridhisha kuwepo kwa adhabu inayotokana na ucheleweshaji wa malipo hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Kutokana na ukubwa wa mahitaji ya Serikali yanayopindukia uwezo wa ukusanyaji wa mapato, baadhi ya

wakati hulazimika kuchelewa kulipa madeni kwa muda unaostahiki na hivyo kupelekea kupatiwa adhabu inayotokana na kuchelewa kulipwa kwa mzabuni kinyume na makubaliano.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilibaini kuwa deni hilo ni la muda mrefu ambapo katika kipindi cha miaka 1990 hadi 2000 Kampuni ya Hassans ilikuwa ikipeleka vifaa mbambalimbali katika Wizara na Taasisi mbalimbali hata hivyo kilipita kipindi kirefu cha zaidi ya miaka 10 kutolipwa kwa malipo ya vifaa hivyo. Aidha, Kamati ya PAC ilibaini kuwa ngawa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango haikuwa na mkataba unaohusu usambazji wa vifaa ili kujenga msingi wa malipo hayo, bali yalilipwa kutokana na barua za Wizara ambazo zilikiri kuwa zilipokea vifaa mbalimbali kutoka kampuni ya Hassan abd Sons. Hivyo, Kamati haikuweza kuapatiwa mkataba wa malipo hayo ya adhabu ya kuchelewa kulipa madeni kwa muda mrefu USD 200,120.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Idara ya Mhasibu Mkuu ifanye malipo kwa kuzingatia misingi ya Sheria na taratibu zinzoongoza masuala ya usimamizi wa fedha z umma ikiwa ni pamoja na kutilia mkazo juu ya vielelezo vuanvyohusika juu ya malipo yanayofanywa

5.5.2.2 Malipoya Kiinua Mgongo yaliyolipwa mara mbili Shilingi 264,814,265.

Ukaguzi umebaini kufanyika kwa malipo ya Kiinua Mgongo ambayo yamelipwa mara mbili kwa watumishi waliofariki ambapo malipo hayo yalifanyika mwaka wafedha 2017/2018 na yamerudiwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria na usimamizi wa fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016, uchambuzi wa malipo hayo kama unavyoonekana katika Jadweli lifuatalo:

| Nambari ya Hati ya Malipo | Tarehe ya Malipo | Aliyelipwa | Kiasi cha Fedha | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| F02PV170000033 1 | 25/08/2017 | Marehemu. Chum Hassan Chum | 87,243,666 | Ikiwa ni Malipo ya Kiinua Mgongo |
| F02PV180000027 8 | 23/08/2018 | Marehemu Chum Hassan Chum | 87,243,666 | Ikiwa ni Malipo ya Kiinua Mgongo |
| F02PV170000043 5 | 13/09/2017 | Marehemu Amour Moh'd Ali | 22,147,466 | Ikiwa ni Malipo ya Kiinua Mgongo |
| F02PV180000027 9 | 23/08/2018 | Marehemu Amour Moh'd Ali | 22,147,466 | Ikiwa ni Malipo ya Kiinua Mgongo |
| F02PV170000033 2 | 25/08/2017 | Marehemu Khamis Omar Ali | 23,016,000 | Ikiwa ni Malipo ya Kiinua Mgongo |
| F02PV180000027 9 | 23/08/2018 | Marehemu Khamis Omar Ali | 23,016,000 | Ikiwa ni Malipo ya Kiinua Mgongo |

| JUMLA | | | 264,814,265 | |
|---|---|---|---|---|

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Uongozi wa Ofisi unapenda kufafanua kwamba malipo hayo ya Kiinua Mgongo yaliyofanyika mara mbili yalionekana hata kabla ya zoezi la ukaguzi wa mwaka husika wa fedha. Uongozi ulichukuwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Fedha na Mhusika alisimamishwa kazi kwa mujibu wa taratibu na kuripotiwa kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) kwa uchunguzi na hatua zinazostahiki.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa kupitia makubaliano bana ya washtakiwa na Mahakama Kuu yaliyofanywa tarehe 28/2/2020. Wamekubaliana kuwa.Washtakiwa warejeshe fedha Serikalini jumla ya shilingi 87,243667 kwa utaratibu ufuatao>-

i. Ndg. Juma Abdalla Othman (Mtumishi wa Wakfu na Mali ya Amana) arejeshe shilingi 13,415,000
ii. Ndg. Said Ali Makame (Mtumishi wa wa Wizara ya Fedha) arejeshe shilingi38,415,000
iii. Ndg. Othman Hussein Othman ( Mtumishi wa Wakfu na Mali ya Aamana) arejeshe shilingi 35,415,000

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara ya Fedha iweke mfumo wa elektroniki wa malipo ya kiinua mgongo ili taarifa hizo pia ziweze kuonekana pia katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

FUNGU R 01 –WIZARA YA BIASHARA,VIWANDA NA MASOKO

Taarifa ya Mapato

Wiazara ya Biashara ,Viwanda na Mosoko ilikadiriwa kukusanya jumla yashilingi 455,000,000.00 kwa mwaka wa fwdha 2017/2018. Hadi kufikia june 30 2018 Wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,016,744,611.00 sawa na asilimia 223.00 ya makadirio.

Majibu ya Wizara ya Biashara na na Maendeleo ya Viwanda

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi milioni 455. Hadi kufikia mwezi wa Juni 2018, jumla ya Shilingi bilioni 1,016.7 zilipatikana na kuingizwa katika Mfuko mkuu wa Serikali. Kiasi hicho cha makusanyo ni sawa na asilimia 223 ya makisio ya makusanyo yote kwa mwaka wa fedha.

Makusanyo haya makubwa ya mapato yalitokana na idadi kubwa ya wananchi kusajili nyaraka za kubadilisha umiliki wa vyombo vya moto kufuatia zoezi lililofanya na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) la kuwataka wananchi wanaomiliki vyombo vya moto kuhakikisha kadi za vyombo hivyo zina majina halisi ya wamiliki. Vile vile kutumika kwa sheria mpya ya kampuni ambayo pamoja na kuboresha masharti pia imeweka utaratibu mzuri na mwepesi wa ada mbalimbali za usajili.

Mapato kwa mwaka 2017/2018

| KIFUNGU | MAELEZO | MAKADIRIO | MAPATO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|

| | | (mil) | HALISI (mil) | |
|---|---|---|---|---|
| R 0104 | Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko | 160.00 | 589.48 | |
| 1422014 | Ukaguzi wa mezani na vipimo | 95.00 | 39.06 | 41 |
| 1422077 | Malipo ya kazi za biashara | 65.00 | 550.42 | 846 |
| | | | | |
| R0106 | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali | 294.00 | | |
| 1146002 | Ada ya Mali Maiti | 1.00 | 1.06 | 106 |
| 1422030 | Alama za Biashara | 156.00 | 70.32 | 45 |
| 1422031 | Uandikishaji wa Makampuni | 81.00 | 135.63 | 167 |
| 1422032 | Uandikishaji wa majina ya biashara | 31.00 | 43.83 | 141 |
| 1422034 | Ujira wa kutengeneza nyaraka | 26.00 | 176.40 | 678 |
| Jumla Kuu | | 455.00 | 1,016.71 | 223 |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji juu ya ada mali maiti na kuelezwa kuwa mali maiti inatokana vifo/warithi wa maiti isipokuwa waislamu. Watu wasiokuwa waislamu hupeleka maombi yao ya BPRA ili mali za warithi wao kugaiwa ambapo BPRA hupata asilimia 2 ya mali hiyo.
Aidha, Kmati ya PAC ilibaini kuwa Usajili wa vyombo vya moto kwa 2017/2018 alikuwa ni chanzo kipya – ada ya 50,000, kwa usajili na asilimia 1 kwa kila chmbo cha moto, Huo ilikuwa ni Utaratibu wa Serikali uliotokana na uamuzi wa Serikali ambapo iliagiza kuanzisha utaratibu wa usajili wa vymbo kwa majina ya umiliki.Katika usajili wamesajili nyaraka za mikataba ya viwanja, nyaraka za nyumba, mauziano, nyaraka za umiliki wa vyombo vya moto.

kwa mwaka 2017/2018 jumla ya alama za biashara 308 na kampuni478 zilisajiliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA)

Kwa upande wa ukaguzi wa mezani na vipimo, Kamati PAC imeabini kuwa makadirio ya makusanyo yalikuwa ni makubwa kuliko hali halisi ya wakati huo ambapo watendaji na vifaa vilikuwa ni hivyo hivyo . Kamati pia ilielezwa kuwa ada ya mezani na vipimo ni Tsh. 6,500 laki 3.000,000. Pia wanahakiki bidhaa zinazozalishwa kiwandani, ujazo wa maji na vinywaji n.k. kama kuna ujazo unaotakiwa. Aidha, Kamati ya PAC ilibaini kuwa watendaji wa mizani na vipimo hawakuwa na vifaa vya kutosha ndio sababu iliyoelezwa na Wizara ya makusanyo kuwa madogo katika ineo hilo..

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kuna haja ya kutoa elimu kubwa katika masuala ya mizani na vipimo hasa kwa kuwa kuna baadhi ya watu si waadilifu katika mizani na vipimo,

Taarifa ya Matumizi

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka fedha 2017/2018 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 7,275,461,762 kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 1,184,575,664 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia 30 juni 2018 Wizara ilifanikiwa kupokea jumla ya shilingi 5743,222,852 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 79 ya makadirio na shilingi 1,125, 459,055 kazi za maendeleo sawa na asilimia 95 ya makadirio.

Majibu ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

Katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara ilipangiwa kutumia kiasi cha Shilingi Bilioni 7.210 kwa ajili ya matumizi ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika program kuu ambazo zinahusisha matumizi ya kazi za kawaida, kazi za maendeleo, pamoja na matumizi ya Ruzuku. Hadi kufikia Juni 2018, Wizara iliingiziwa jumla ya Shilingi Bilioni 6.098 sawa na asilimia 85 ya bajeti ya mwaka. Kiambatanisho namba 1 kinatoa ufafanuzi zaidi.

Matumizi ya Fedha kwa kipindi cha Julai 2017 – Juni 2018

| Geresho (Code) | Programu Kuu/Programu ndogo | Makadirio 2017/2018 (mil) | Matumizi | asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **PR0101** | **Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko** | **2,344.36** | 2,415.67 | **104** |
| SR010101 | Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. | 1,613.13 | | |
| SR010102 | Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | 340.92 | | |
| SR010103 | Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | 390.31 | | |
| | | | | |
| **PR0102** | **Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali** | **912.58** | **337.90** | **37** |
| SR010201 | Ukuzaji wa Viwanda | 644.99 | | |
| SR010202 | Maendeleo ya Ujasiriamali | 267.59 | | |
| | | | | |
| **PR0103** | **Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara** | **1,469.46** | 1,286.20 | **87** |
| SR010301 | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | 316.20 | | |
| SR010302 | Ushindani Halali wa kibiashara na Kumlinda Mtumiaji | 143.34 | | |
| SR010303 | Urahisishaji biashara na Ukuzaji Biashara za ndani | 502.20 | | |
| SR010304 | Usajili wa Biashara na Mali | 507.72 | | |
| | | | | |
| **PR0104** | **Viwango na Tathmini yaUbora wa bidhaa** | **2,483.80** | | |
| SR010401 | Viwango na Uthibiti Ubora | 2,483.80 | 2,058.30 | 83 |
| | | | | |
| JUMLA KUU | | 7,210.20 | 6,098 | 85 |

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2017/2018

| NAM. | JINA LA MRADI | SHUGHULI ZILIZOPANGWA 2017/2018 | FEDHA ZILIZOPANGWA | FEDHA ZILIZOTUMIKA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MradiwakukondoeshaMazingirayaBiashara | Kujengauwezowakukondoeshabiashara | 24,300,000 | 20,000,000 | Wadau 60 walipatiwamafunzoyaudhibitinausalamawatakwimuzabiashara |
| | | Uwekajiwauziowauwanjawamaonesho Nyamanzi | 25,700,000 | 0 | |
| | | JUMLA | 50,000,000 | 20,000,000 | |
| 2 | Programuya Mazingira Bora yaBiashara | Ununuziwavifungashio | 150,000,000 | 0 | |
| | | JUMLA | 150,000,000 | 0 | |
| 3 | Programuya KuendelezaViwanda | Kuandaasheriaya SMIDA | 45,500,000 | 42,350,000 | Sheriaya SMIDA imeandaliwapamojanakuanzishaMakonganoyamwaninambogamboga. |
| | | Ujenziwamakaomakuuya SMIDA | 59,500,000 | 0 | |
| | | Ununuziwavifungashio | 30,000,000 | 0 | |
| | | | | | |
| | | Kuandaa Sera yaViwandanakufanyamapitio sera yawajasiriamali | 40,000,000 | 16,550,000 | Rasimuya Sera yaViwandaimekamilikanaSera yawajasiramaliimefanyiwamapitio. |
| | | KuimarishauzalishajiwaDagaa | 50,000,000 | 20,000,000 | Kiwanda cha kukaushiadagaakimefanyiwaukarabatimkubwa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Usarifuwazao la Mwani | 50,000,000 | 18,217,000 | Wizarailitoavifaavyakusarifunakuvunamwanipamojanakuvipatiamafunzovikundivilivyopewavifaahivyo. |
| | Programuya KuendelezaViwanda | KukuzaMaendeleoyaKiwanda cha Chumvi | 225,000,000 | 150,000,000 | Kiwandakilifanyiwamatengenezomadogopamojanakukamilishamatayarishoyaujenziwabarabara |
| | | JUMLA | 500,000,000 | 247,117,000 | |
| 4 | KuimarishaTaaasisiyaViwango Zanzibar | UjenziwaOfisina Ununuziwavifaavyamaabara | 2,000,000,000 | 2,000,000,000 | Ujenziwajengomojaumekamilikanavifaavyamaabaravimenunuliwa |
| | | JUMLA | 2,000,000,000 | 2,000,000,000 | |
| 5 | MfumompyawautoajiLesenikwamaendeleoyaSekta Binafsi | Kufanyautafitiwamatokeoyamfumowamageuziyautoajileseni | 50,000,000 | 50,000,000 | Utafitiulifanyikakwakuzingatiauzoefuwa EAC na SADC kuhusuidadiyaleseninafedhazilizopatikana. |
| | | JUMLA | 50,000,000 | 50,000,000 | |
| | JUMLA KUU | | 2,750,000,000 | | |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilielezwa kuwa Wafanyakazi wawili hao walikuwa ni miongoni mwa wafanyakazi katika mfumo wa malipo kimakosa, walipokuwa wametaka kuajiriwa wenzao lakini ikagundulika na Mkaguzi wa Ndani kuwa wafanyakazi hao ni walistaafu /walikuwa waajiriwa hapo zamani.

Ripoti ya maalam ya taarifa ya wafanyakazi wa Mkataba kuingizwa katika mfumo wa malipo ya mishahara ya watumishi wa Umma.ambao ni Mussa Machano Juma- Nambari ya uajiri 21037 na Ndg Muhammed Iddi Ramadhan – Namba ya Uajiri 216002 – Ripoti ya uchunguzi ilitolewa tarehe 30/1/2019 –( Mwenyekiti - Ali Khamis Juma na Katibu Abrahman M. Mohammed.) ns kuwalishwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Viwanda – Kamati hiyo ilipendekeza kuwa Wizara iwaarifu kuwa mikataba yao imemaliza muda – tokea mwaka 2007 pamoja na kuwaandikia rasmi barua za kusitisha ajira zao kwa kufuata utaratibu. Aidha,ilipendekeza Wizara ifikirie kuwapa mkono wa kwa heri iwe kama kifuta jasho kwa wafanyakazi.

Aidha Kmati ya PAC ilkagua nyaraka ,abalimbali za utunzaji wa matumzi ikiwemo Cash book na kuridhika nalo. Aidha, Kamati ya PAC ilikagua Ripaoti ya Mkaguzi wa Ndani wa Wizara..

Vilevile, Kamati ya PAC ilihoji juu ya sababu za Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali kuchelewakuwasilisha taarifa zake kwa Mdhibiti nakuelezwa kuwa kwa mwaka huo Tasisi hiyo ilikuwa bado ni mpya kuweaa kufunga hesabu zake wenyewe.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara iitunze taarifa zake kwa njia ya elektroniki hasa taarifa za matumzi ya fedha.

FUNGU H 01- WIZARA YA AFYA

Taarifa ya Mapato

Wizara ya Afya ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 221,143,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 .Hadi kufikia 30 juni 2018 Wizara imekusanya jumla ya shilingi 179,635,700 sawa na asilimia 81 ya makadirio.

Majibu ya Wizara ya Afya

kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Afya ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi **221,143,000/=** na Hospitali ya Mnazi Mmoja imepangiwa kukusanya shilingi **258,799,395/=**. Fedha hizo zilipangwa kukusanywa kutoka katika vyanzo vya mapato vilivyoainishwa katika Fungu Wizara ya Afya (H01) na Fungu la Hospitali ya Mnazi Mmoja (H02). Makusanyo ya fedha kutoka katika vyanzo hivyo hufanyika kupitia programu husika kama inavyoainishwa katika *Jadweli*

Vyanzo vya Mapato kwa mujibu wa Programu

| Programu | Chanzo cha Makusanyo |
|---|---|
| Programu ya Kinga na Elimu ya Afya | • Ada ya chanjo ya wasafiri |
| | • Uchunguzi wa vyombo vya usafiri na abiria |
| | • Malipo ya medical checkup |
| Programu ya Usimamizi wa Sera na Utawala | • Malipo ya zabuni |
| Programu ya Huduma za Tiba | • Malipo ya medical checkup (Pemba) |
| | • Malipo mengine ya hospitali |
| Programu za Hospitali ya Mnazi Mmoja | • Huduma za haraka (fast track) na Bima |
| | • Malipo ya huduma za afya |

Hadi kufikia Juni 30, 2018; Wizara ya Afya ilikusanya jumla ya shilingi 179,635,700/= ambazo ni sawa na asilimia **81.2** ya fedha zilipangwa kukusanywa na Hospitali ya Mnazi mmoja iliweza kukusanya **shilingi**

200,958,145/= sawa na asilimia 77.7 ya makadirio.

MAKUSANYO KWA MWAKA 2017/2018

| Chanzo cha Mapato | Makadirio | Makusanyo Halisi | Asilimia ya makusanyo |
|---|---|---|---|
| Ada ya chanjo ya wasafiri | 52,933,000 | 73,880,000 | 139.5 |
| Uchunguzi wa vyombo vya usafiri na abiria | 47,040,000 | 43,182,700 | 91.8 |
| Malipo ya medical checkup (Unguja) | 29,442,000 | 45,259,250 | 153.7 |
| Malipo ya zabuni | | 5,319,000 | |
| Malipo ya medical checkup (Pemba) | 9,408,000 | 4,876,000 | 51.8 |
| Malipo mengineyo ya hospitali | 82,320,000 | 7,118,750 | 8.6 |
| Jumla Kuu (H01) | 221,143,000 | 179,635,700 | 81.2 |

Ongezeko la ada ya chanjo kwa wasafiri limetokana na kubadilishwa kwa vitabu vya chanjo, ambapo wasafiri wote wenye vitabu vya zamani walitakiwa kubadilisha vitabu vyao kwa kununua vitabu

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kmati ya PAC ilihoji juu ya malipo mengineyo na kuelezwa kuelezwa kuwa malipo hayo mengineyo ya hospitali yalikuwa yakijumuisha malipo ya ada za maabara ingawa malipo hayo ya cost sharing" yalifutwa katika kuondoa malipo ya huuma za Afya.

Kwa upande wa uchunguzi wa vyombo vya usafiri na abiria Kamati ya PAC ilielezwa kuwa kwa mwaka 2017/2018 jumla ya vyombo 3328 vilivyochunguzwa Bandarini na abiria 268,393

Katika ada ya usafiri ada ya chanjo za wasafiri, Kamati ya PAC ilielezwa kuwa mwishoni mwa mwaka 2017 mwishoni walikubaliana waanzishe vitabu vipya /na kutumia vitabu cha aina moja ambavyo ni vya kielektroniki, Hayo yalikuwa ni makubaliano ya Afrika Mashariki kutumia na wazamani waliotaka kubadilisha vitabu na wapya pia waliotaka vitabu vipya.Wizara ilikuwa haina mpngo wa kubadilisha vitabu vipya , suala hilo lilikuja katikati ya Bajeti kuwa Zanzibar iendane na makubaliano ya Sfrika ya Mashariki ya kuwa ni vitabu vya elektroniki vya chanjo.

Pia, Kamati ya PAC ilielezwa kuwa kuongezeka kwa mapato ya 'medical check up" ilisababishwa baada ya kutokea kipindupindu na kubadilisha muongozo wa kufanya "medical check up" na hivyo hata wafanyabiashara ndogo ndogo walifanya medical check up.  Ingawa mapato hayo yalipungua kwa Pemba kutokana na nguvu za udhibiti .  Udhibiti wa Kipindupindu ulikuwa mkubwa zaidi Unguja.

Kwa ujumla Kamati ya PAC imeriudhika na majibu pamoja na ufafanuzi uliotelewa kuhsiana na taarifa ya mapato.

Taarifa ya Matumizi

Wizara ya Afya ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 37, 511,462,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na jumla ya shilingi 35,428,900,000kwa kazi za maendeleo .

Hadi kufikia june 30 jumla ya shilingi 37,963,068 766 ziliingizwa na na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 101.20 ya makadirio na shilingi 12,212,480,202 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleosawa na asilimia 34.47 ya makadirio.

Majibu ya Wizara ya Afya

kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Afya (H01) ilitengewa jumla ya **shilingi 72,940,362,000/=;** kati ya fedha hizo **shilingi 37,511,462,000/=** zilipangwa kwa kazi za kawaida na **shilingi 35,428,900,000/=** zilipangwa kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Juni 30, 2018; jumla ya **shilingi 50,175,548,968/=** sawa na **asilimia 69** ya fedha zilizotengwa zilitumika; kati ya hizo ambapo **shilingi 37,963,068,766/=** sawa na **asilimia 101.2** ya fedha zilizotengwa kwa kazi za kawaida na **shilingi 12,212,480,202/= (asilimia 34.5)** kwa shughuli za maendeleo. Katika kipindi kinachoripotiwa, Hospitali ya Mnazi Mmoja (H02) iliidhinishiwa **shilingi 11,939,111,040/=,** ambapo jumla ya **shilingi 11,290,007,030/=** sawa na **asilimia 95** ziliingizwa na kutumika.

Mchanganuo wa matumizi, 2017/2018

| Kasma | Matumizi | Fedha zilizotengwa | Fedha zilizopatikana | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| H01 | Kazi za Kawaida (OC) | 14,304,500,000 | 13,636,802,016 | 95.3 |
| | Mishahara na maposho | 22,673,962,000 | 23,852,914,750 | 105.2 |
| | Subvention | 533,000,000 | 473,352,000 | 88.8 |
| | Kazi za Maendeleo | 35,428,900,000 | 12,212,480,202 | 34.5 |
| Jumla | | 72,940,362,000 | 50,175,548,968 | 68.8 |
| H02 | Hospitali ya Mnazi Mmoja (OC) | 11,939,111,040 | 11,290,015,980 | 94.6 |
| | Maendeleo | 3,000,000 | 2,900,000 | 96.6 |
| | Jumla | 11,942,111,040 | 11,292,915,980 | 94.6 |

Sababu kuu zilizopelekea kuongezeka kwa mishahara iliyopangwa ni pamoja na mabadiliko ya mishahara ya wafanyakazi ambao walikuwa masomo na baada kurejea Wizara iliomba kupatiwa mishahara mipya ya

watendaji hao pamoja na stahiki nyenginezo (maposho).

Kwa mujibu wa ripoti ya utekelezaji mpango kazi wa mwaka 2017/2018, jumla ya shughuli tisa (9); i) Kuandaa register maalum la usajili wa wagonjwa wa cancer; ii) Kutoa mafunzo kwa watendaji juu ya matibabu ya maradhi yasioambaukiza (NCD); iii) Kufanya uchunguzi wa saratani ya matiti na shingo ya kizazi, iv) Kutoa mafunzo ya matibabu ya maradhi yasiyopewa kipaumbele; v) Kufanya uchunguzi wa macho katika skuli; vi) Kutoa mafunzo kwa wafanya kazi wa afya juu ya vihatarishi vya afya makazini; vii) Kuandaa mpango wa utekelezaji wa mawasiliano (Communication strategy); viii) Kufanya utafiti wa kuangalia usalama wa maji kutoka vyanzo tofauti ; na ix) Kufanya tathmini ya utendaji vituo vya afya kwa ajili ya kuvipatia nyota (star rating).

Shughuli hizo hazikuweza kutekelezwa katika kipindi hicho kutokana na kukosekana kwa fedha zilizoahidiwa kutoka kwa wahisani pamoja na uhaba wa watendaji kwa baadhi ya maeneo ambayo shughuli zilizopangwa zilihitaji utaalamu. Hatua zilizochukuliwa ni kuziingiza katika mpango kazi wa Wizara wa mwaka 2018/2019. Kazi ambazo hazikuweza kutekelezwa ni:-

Miradi ya Maendeleo

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Afya ilipanga kutekeleza miradi sita (6) ya maendeleo; ambayo ni mradi wa kupandisha hadhi hospitali za vijiji na Wilaya; Kuimarisha Hospitali ya Mnazi Mmoja; Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Miradi hii ilihusisha ujenzi na ukarabati wa baadhi ya majengo ikiwemo uimarishaji wa miundombinu ya hospitali pamoja na ununuzi wa vifaa. Miradi mingine iliyotekelezwa ni miradi endelevu, ambayo ni huduma za afya za uzazi wa mama na mtoto; UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma; na Kudhibiti Malaria Zanzibar.

MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/2018

| Mradi | Fedha zilizotengwa | Matumizi Halisi | % |
|---|---|---|---|
| Kupandisha hadhi hospitali za vijiji na Wilaya | 2,550,000,000 | 2,655,137,433 | 104.1 |
| Kuimarisha Hospitali ya Mnazi Mmoja | 5,350,000,000 | 5,350,000,000 | 100.0 |
| Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali | 1,868,595,250 | 1,080,315,348 | 57.8 |
| Huduma za afya za uzazi wa mama na mtoto | 1,000,000,000 | 1,000,000,000 | 100 |
| UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma | 96,000,000 | 96,000,000 | 100.0 |
| Kudhibiti Malaria Zanzibar | 110,000,000 | 110,000,000 | 100.0 |
| Jumla | 10,906,000,000 | 11,011,137,433 | 101.0 |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji juu ya sababu za kuongezeka kwa mshahara na maposho na kuelezwa kuwa kulitokana na kuwepo kwa wafanyakazi waliorudi masomoni na waajiriwa wapya, Katika ya Bajeti ya Wizara ya Afya huwa hawaingizi bajeti ya mishahara mipya na nyongeza za waliorudi masomoni. Jumla ya wafanyakzi 491 wapya walioajiriwa mwaka 2017/2018. Nyaraka za maombi ya fedha za ziada kwa ajili ya mishahara ya ajira mpya na waliorui masomoni ziliwasilishwa na kukaguliwa. Na Kamati ya PAC pia ilielezwa kuwa Fungu la miradi ya maendeleo la Hospiali ya Mnazi Mmoja linaingizwa katika fungu la Wizara

Vile vile Kamati ilikagua Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani ya Wizara ambayo ilibainisha kua manunuzi mengi yalifanywa bila ya kuzingatia Mpango wa Ununuzi wa Mwaka.

Kwa upande wa Miradi ya maendeleo Kamati ya PAC ilihoji juu ya matumizi ya mradi malaria na ilielezwa kuwa 110,000,000/= - zilitumika hasa kwa ajili ya ununuzi wa vifa kwa ajili ya uchunguzi wa malaria.. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa uchunguzi wa wagonjwa 130,000 waliokwenda katika vituo vya afya ulifanyika kati ya hao wagonjwa 2859 walifuatailiwa majumbani. Kamati ilielezwa pia kuwa asilimia ya utekelezaji inategemea na lengo linalowekwa na katika utekelezaji huwa haiipatikani kwa baadhi ya wakati – mfano upigaji dawa unaweza kuingiziwa fedha zote lakini usiweze kupiga dawa nyumba zote kama lengo lilivyo.

Kwa mwaka 2017/2018 wagonjwa 1,300.,000- ndio walikwenda katika vituo vya afya na kufanyiwa uchunguzi wa Malaria kati ya hao wagonjwa 3397 ndio waliogundulika na malaria

Kamati ya PAC iliikagua Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani kwa kipindi cha Julai – Septemba, 2017 na kubaini kasoro mbalimbali zilizobainihshwa ikiwemo malipo ya shilingi 50,556,592 yaliyolipwa kwa Kmapuni ya Zanlink bila ya LPO wala stakabadhi (risiti). Aidha Kamati ilibaini kuwa malipo hayo yalilipwa yote ya miezi 6 kinyume na maelekezo ya Meneja wa Kitengo wa Malaria aliyeelekeza kuwa yalipwe malipo ya miezi mitatu tu kwanza

Kwa upande wa gharama za matibabu nje ya nchi, Kamati ya PAC imebaini kuwa jumla ya shilingi bilioni 10 zilitumika kusafirisha wagojnjwa nje na ndani ya nchi ambapo kwa mwaka 2017/2018 – Wagonjwa waliopelekwa nje ya Tanzania ni 271 na Wagonjwa 63 walipeleka Tanzania Bara.

Katika madeni ya wafanyakazi Kamati ya PAC imebaini kuwa Wizara ilikuwa na deni la 25,000,000 la posho ya likizo kwa wafanyakazi 250.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Wizara iweke kumbukumbu vizuri za (data base) ya wafanyakazi wapya na wanaorudi masomoni ili iwe na taarifa kamili za wafanyakazi wake.

ii. Wizara Afya iimarishe mashirikiano na iwe na uratib mzuri baina ya vitengo vyake ili taarifa ziwe zinalingana /taarifa iwe moja kwa kuwa taarifa hizo zinatoka Wizara moja
iii. Dosari mbalimbali zilizoainishwa katika Ripoti ya Ukaguzi wa ndani zifanyiwe kazi kazi ipasavyo.

WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA KUU WA SEREKALI

Taarifa ya Mapato

Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serekali ya Zanzibar , ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 82,423,600 kwa wa fedha 2017/2018. Hadi kufiki 30 JUNI 2018 Wakala wa Waabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Zanzibar ilikusanya jumla ya shilingi 99,285,709 sawa na asilimia 120 ya makadirio hayo.

Majibu ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 82,423,600 kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018 jumla ya shilingi 99,285,709 sawa na asilimia 120 ya makadirio hayo zilikusanywa.

Vyanzo vya Mapato
VyanzovyamapatoyaWakalawaMaabarayaMkemiaMkuuwaSerikalikwamwakawafedha 2017/2018nihivivifuatavyo:

- UdhibitiwaKemikalina
- UchunguziwaSampuli.

Hali halisi ya makadirio na makusanyo

| s/n | Chanzo cha Mapato | Makadirioyafedha | Makusanyo | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | UdhibitiwaKemikali | 50,000,000 | 65,200,709 | 130.40 |
| 2 | UchunguziwaSampuli | 32,423,600 | 34,085,000 | 105.12 |
| | **Jumlakuu** | **82,423,600** | **99,285,709** | **120.46** |

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilivuka lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kukusanya asilimia 120 ya makadirio kama inavyooneshwa katika Jaduweli  Sababu kuu zilizopelekea makusanyo kuongezeka ikilinganishwa na makadirio ni hizi zifuatazo:-.

1. Kuongezeka kwa maeneo ya ukusanyaji wa mapato ikiwemo bandari ya Malindi, Wete, Mkoani na Wesha.
2. Kuongezeka kwa aina na idadi za sampuli zinazofanyiwa uchunguzi wa maabara;mfano ZBS walianza kuleta sampuli ambazo kabla walipeleka Tanzania Bara.
3 Kuongezekakwamwamkowawadauwakemikalikwahatuayakujisajilinakukatavibalivyakuingizanakusfirishakemikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilihoji ya anaefanya makisio ya Wakala wa Maabara ya Mkemia na kuelezwa kuwa Maabara yenyewe ndio inayofanya makisio kupitia kazi zao wanazofanya. Aidha, Kamati ya PAC ilielezwa kuwa awali Maabara ya Mkemia ilikuwa inafanya uchunguzi tu, walikuwa hawajaanza kazi ya udhibiti, baada ya kesi za tindikali kujitokeza, hivyo, ikaonekana Mkemia afanye kazi ya udhibiti wa tindikali . Mnamo mwaka 2014 Maabara ya Mkemia Mkuu ilianza kutayarisha Kanuni za udhibiti, Kabla ya hapo walikuwa hawana mapato yanayotokana na udhibiti. Mnamo mwaka 2015 ndio wameanza kazi ya udhibiti wa kemikali ambapo Sheria Mkemia ni Sheria Namba 10 ya mwaka 2011..Hivyo, Kanuni ndio iliyoweka ada za udhibiti. Kimsingi, kazi ya udhibiti wa tindikali  ilikuwa  ya Mkemia lakini ilikuwa haifanyiki.

Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kuna tofauti kubwa ya viwango vya faini vilivyomo katika Sheria ya Mkemia na vile vilivyoainishwa katika Kanuni (Industrial and Consumer Chemical Regulations, 2014) ambapo katika Sheria kumewekwa faini hadi ya shilingi 40,000,000 wakati katika Kanuni kuna faini ya shilingi 5,000,000 tu. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa Maabara ya Mkemia bado haijaanza kutoza faini katika makosa yanayohusiana na kemikali.

Kwa upande mwengine Kamati ya PAC imebaini kuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inaidai Jeshi la Polisi deni kubwa amabapo hadi mwaka 2020 Jeshi la Polisi lilikuwa linadaiwa zaidi ya shilingi 100,000,000.,Jeshi la Polisi wanadaiwa deni kubwa kwa sabaubu wao ndio wadau wakubwa katika masuala ya kuhitaji uchunguzi wa sampili mbalimbali.

Kamati ililezwa kuwa sampuli nyingi hufanyiwa uchunguzi hapa hapa bila ya kupelekwa Tanzania Bara kutokana na kuwepo kwa mashine ya DNA ambayo kimuundo ina sehemu nyingi. Kamati ya PAC imeelezwa kuwa kwa wiki moja hupata sampuli 8 hadi 10 ambazo huchunguzwa kupitia mashine ya DNA.

Kwa upande wa kemikali zinazotumika katika mabwawa ya kuogelea yaliyomo katika hoteli mbalimbali za kitalii, Kamati ya PAC imebaini kuwa bado Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu haijanza kufuatilia vya kutosha juu ya suala hilo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ifanye jitihada za kufuatailia kwa kina udhibito wa kemikali zinazotumika katika mbwawa ya kuogelea katika hoteli na kutoza ada.

Taarifa ya Matumizi

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Zanzibar ilikadiria kutumia jumla ya shilingi 495,823,600 kwa kazi za kawaida na maendeleo. Hadi kufikia june 30 2018 Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Zanzibar iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 490,328,715 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 98.89 ya makadirio, na shilingi 1,080,315,348 kwa kazi za maendeleo sawa na aslimia 57.81 ya makadirio.

Majibu ya Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilikadiria kutumia jumla ya shilingi 495,823,600 kwa kazi za kawaida ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018 jumla ya shilingi 490,328,715 ziliingizwa sawa na asilimia 98.89 yamakadirio.

Hali halisi ya makadirio na matumizi ya fedha za ruzuku

| Makadiriokwamwaka 2017/2018 | Matumizihalisi | Asilimia |
|---|---|---|
| 495,823,600 | 490,328,715 | 98.89 |

Asilimia iliyopungua ya fedha ilipangwa kuwapeleka wataalamu (wafanyakazi) mafunzo ili kuwajengea uwezo wa kiutendaji. Kutokana na kukosekana fedha hiyo idadi ya wataalamu waliopangwa kusomeshwa imepungua na hivyo waliobaki kusomeshwa mwaka wa fedha unaofuata.

Matumizi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo.

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilikuwa na mradi mmoja wa maendeleo ambao ni kuimarisha maabara kuwa ya kisasa. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilikadiria kutumia jumla ya shilingi 1,868,595,250 kwa kazi za kuimarisha maabara ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, jumla ya shilingi 1,080,315,348 ziliingizwa sawa na asilimia 57.81 yamakadirio.

Makadirio na Matumizi ya Mradi wa Maendeleo.

| Makadirio | Kilichopatikana | Asilimia | Matumizihalisi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1,868,595,250 | 1,080,315,348 | 57.81 | 1,080,315,348 | 57.81 |

Fedha zilizoingizwa zilitumika katika ununuzi wa mashine za uchunguzi wa vinasaba (DNA), vitenganishi vyake (consumable) na mafunzo kwa wataalamu. Kazi iliyoshindwa kufanyika niununuzi wa mashine nyengine kwa ajili ya kufungwa katika maabara nyengine zilizobaki.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilihoji juu ya suala la wataalam katika Wakala wa Maabara ya Mkemia na kuelezwa kuwa mwaka 2017/2018 walipata wataalam 16 (fresh from school) na walihitaji kuwapeleka katika mafunzo maalum (Tanzania Bara), walipanga kwenda katika mafunzo watu wane na waliokwenda ni wafanyakazi wanne. Aidha, Kamati ilihoji juu ya ruzuku ya shilingi 490,328,715 na kuelezwa kuwa fedha hizo hutumika kwa ajili ya matumizi mengineyo (matumizi ya bidhaa,kazi na huduma

Vilevile,Kamati ya PAC ilihoji juu ya ununuzi wa Mashine ya DNA na kuelezwa kuwa mashine hiyo ni mgawanyiko wa sehemu nyingi, ambapo mchakato wa ununuzi wa mashine hiyo umefanywa na Wizara ya Afya na malipo yamefanywa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Fedha hivyo nyaraka za ununuzi wa mashine hiyo zipo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu inapofanya kazi zake za uchunguzi wa sampuli sampuli mbali ijipange vizuri pia katika kufuatilia madeni yake inayodai kwa Taasisi na watu mbalimbali.

WAKALA WA CHAKULA ,MADAWANA VIPODOZI

Uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya Ukaguzi

Kwa mujibu wa Ripoti ya Ukaguzi, Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi ilichelewa kuwasilisha Taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka wa 2017/2018 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo iliwasilisha taarifa hizo tarehe 21/11/2018 kinyeme na kifungu cha 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016 kinachozitaka Wizara na Taasisi za Serikali kutayarisha na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kumaliza mwaka wa fedha ambapo hesabu hizo zitajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi hizo.

Majibu ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi

Kuchelewa huku kumetokana na mabadiliko ya Mhasibu wa Wizara ambaye amebadilishwa mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kuletwa Mhasibu mwengine ambaye alipata muda mchache wa kukusanya na kuzichambua taarifa za fedha kwa ajili ya utayarishaji wa ripoti ya mwisho kwa kipindi hicho.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilielezwa kuwa awali walikuwa hawana akaunti na wakati huo walikuwa wakipeleka taarifa zao za kifedha Wizarani (Wizara ya Afya). Mwaka 2018/2019 ndio waliidhinihiwa akaunti zao za mwisho wa mwaka. Mwaka 2017 ndio waliokuwa wakibadilisha rasmi lakini kulikuwa ndio kipindi cha mpito kuelekea katika marekebisha/mabadiliko ya muundo. Awali walikuwa ni Bodi ya Chakula Dawa na Vipodozi ( kuanzia miaka ya 1996) walikuwa na Mshika Fedha tu ambapo mwaka 2018 ndio waliletewa Mhasibu na pia kukaanzishwa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa Mahsibu wa Wakala na alikuwa akiwasiliana na Mhasibu wa Wizara wakati wa kuandaa taarifa za kifedha ingawa mawasiliano yao hayakuwa rasmi.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Wahasibu wajipange vizuri ili waweze kutatyarisha na kuwaailoisha taarifa za fedha kwa wakati kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mujibu wa Sheria
ii. Mawasiliano ya baina ya Watendaji wa Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi na Wizara au taasisi nyengine yanapaswa yawe rasmi ili kupatikane uthibtisho wake wakati wa ukaguzi.

Taarifa ya Mapato

Wakala wa Chakula ,Madawa na Vipodozi wa Serikali ya Mapinduzi ilikadiria kusanya jumla ya shilingi 582,014,000 kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Hadi kufikia june 30 2018 Wakala alikusanya jumla ya shilingi 594,143,029 sawa na asilimia 102.08 ya makadirio.

Majibu ya Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ZFDA ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 876,970,000**fedha ambazozitatokana na vyanzo mbali mbali zikiwemo ruzuku kutoka Serikalini, makusanyo ya ada na tozo kwa huduma zinazotolewa na Wakala wa Chakula na Dawa (ZFDA na michango kutoka kwa wahisani. Kiasi cha TZS **120,000,000** sawa na asilimia (**14%**) ni mchango kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ruzuku ya matumizi ya kawaida, TZS **462,014,000** sawa na asilimia (**53%**) ni kutokana na makusanyo ya ada na tozo kwa huduma zinazotolewa na Wakala wa Chakula na Dawa (ZFDA) na TZS **294,956,000**sawa na asilimia (**34%**) mchango kutoka kwa Wahisani.

Hadi ufikia 30 Juni 2018, ZFDA ilikusanya **875,039,029**sawa na asilimia **99** ya makadirioambayo yanajumuisha **111,912,000(13%)** ni mchango kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ruzuku ya matumizi ya kawaida, TZS **482,231,029 (55%)** ni kutokana na makusanyo ya ada na tozo kwa huduma zinazotolewa na Wakala wa Chakula na Dawa (ZFDA) na TZS **280,896,000** (**32**%) mchango kutoka kwa Wahisani.

| CHANZO CHA FEDHA | MAKADIRIO | KILICHOPATIKANA | ASIMILIA |
|---|---|---|---|
| Ruzuku kutoka Serikalini | 120,000,000 | 111,912,000 | 93% |
| Makusanyo | 462,014,000 | 482,231,029 | 104% |
| Wahisani | 294,956,000 | 280,896,000 | 95% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jumla | 876,970,000 | 875,039,029 | 99% |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilibaini kuwa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi hupata fedha kupitia Serikali (Ruzuku), fedha kutokana na ada wanazokusanya kutokana kazi zao mbali mbali za uchunguzi pamoja namchango wa Wahisani. Aidha, Kamati ilihoji juu ya matumizi ya Ruzuku na kuelezwa kuwa hutumia kwa ajili ya mishahara na pia hupata ruzuku ya uendeshaji (OC).

Kamati pia ilibaini kuwa fedha kutoka Washirika wa Maendeleo hazikuingizwa katika Financial Statement ya Wakala na kuelezwa kuwa fedha hizo hazikupitia katika akaunti yao bali Wakala wa Chakula walifanya matumzi tu ya kazi mbali mbali. Kwa kawaida fedha za Global Fund zilikuwa zikipitia (recipient) katika Kitengo cha Malaraia, Hata hivyo,hivi sasa Wakala wa Chakula ana akaunti yake na fedha za Global Fund wanazitumia moja kwa moja.

Vilevile, Kamati ya PAC ilibaini kuwa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi inapewa ruzuku kutoka Serikalini na pia inakusanya mapato ambayo inatumia wenyewe. Hukusanya kupitia uchunguzi na kazi za kufanya ukaguzi katika wauzaji maziwa, maduka ya madawa nakadhlika
Pia ZFDA hufanya ukaguzi wa kawaida viwandani kunakozalishwa bidhaa nje ya nchi, na kufanya usajili wa bidhaa. walikusanya jumla ya shingi 850,000,000 na walizitumia wenyewe

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi iongeze mikakati ya kuongeza makusanyo ili iweze kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali

Taarifa ya Matumizi

Wakala wa Chakula ,Madawa na Vipodozi wa Serikali ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 116,833,050 kwa kazi za kawaida.. Hadi kufikia 30 juni Wakala alitumia jumla ya shilingi 749,694,381 sawa na asilimia 641.68 ya makadirio.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA) ilikadiriwa kutumia jumla ya shilling 869,842,580 ambayo yanajumuisha 120,000,000 ni mchango kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ruzuku ya matumizi ya kawaida, TZS 454,886,580 ni kutokana na makusanyo ya ada na tozo kwa huduma zinazotolewa na Wakala wa Chakula na Dawa (ZFDA) na TZS 294,956,000mchango kutoka kwa Wahisani.

Hadi kufikia 30 Juni 2018, ZFDA ilitumia jumla ya shillingi 749,694,381 sawa na asilimia 86 ya makadirioambayo yanajumuisha 101,912,000 ni mchango kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ruzuku ya matumizi ya kawaida, TZS 406,886,283 ni kutokana na makusanyo ya ada na tozo kwa huduma zinazotolewa na Wakala wa Chakula na Dawa (ZFDA) na TZS 240,896,098mchango kutoka kwa Wahisani.

| CHANZO CHA FEDHA | MAKADIRIO | KILICHOTUMIKA | ASIMILIA |
|---|---|---|---|
| Ruzuku kutoka Serikalini | 120,000,000 | 101,912,000 | 85% |
| Makusanyo | 454,886,580 | 406,886,283 | 89% |
| Wahisani | 294,956,000 | 240,896,098 | 82% |
| Jumla | 876,970,000 | 749,694,381 | 86% |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilibaini utofauti wa makadirio baina ya Ripoti Mdhibiti na na Majibu ya ZFDA na kuelezwa kuwa muda waliambiwa wawasilishe financial account ulikuwa mfupi na ilipkea kutokea kwa maaosa ya figure hata hivyo ZFDA wamekiri makossa yaliyotokea katika tofauti za figure. Aidha, Kamati ya PAC Ruzuku kutumia kwa ajili ya mishahara na pia hupata ruzuku ya uendeshaji (OC).
Kamati ya PAC ilikgua Utekelezaji wa bajeti, Mapango wa ununuzi wa mwaka hati za malipo ya ununuzi wa vifaa vya 145,000,000 Hati za malipo ya matengenezo ya jengo la ZFDA No. 0097 ya tarehe 24/7/2018 yenye Tshs1,540,000= na 01041 ya tarehe 13/8/2018 – Tsh.4,415,00/=.

Kamati ya PAC ilielezwa kuwa ZFDA ilifanyia matengenezo makubwa jengo lake ambalo lilikuwa na Al khairia Press. Pia ZFDA wanalipia kodi ya ofisi Bandarini . Na pia wana ofisi Uwanja wa Ndege - Unguja. Aidha. ZFDA wamekodi Ofisi – Pemba. Kamati pia imebaini kuwa ZFDA wana Mhasibu mmoja hawana Mshika Fedha

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi izidi kufuatilia Ofisi ya Rais Fedha Nna Mipango ili waweze kupata kupata watendaji wa kutosh wa kutosha wa masuala ya fedha wakiwemo washika fedha ili shughuli za kifdha ziweze kufanyika kwa ufanisi zaidi

## SEHEMU YA NNE

## RIPOTI YA UKAGUZI WA MFUMO WA USIMAMIZI WA FEDHA (*IFMS*) KATIKA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO – IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

Hoja Namba 1.6.1 Kutokutumia mfumo wa IFMIS katika hesabu za mapato ya hazina

Ukaguzi umebaini kwamba Mapato ya Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hayajaunganishwa moja kwa moja katika Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Serikali – *IFMS* ambapo mapato hayo yaliyokusanywa huingizwa katika mfumo wa *IFMS* kwa njia ya kawaida (*manually*). Hali hii inasababisha Serikali kukosa kupata taarifa sahihi za mapato halisi yaliyokusanywa. Hivyo, mfumo wa*IFMS* unarikodi moja kwa moja

upande wa matumizi tu kutoka Hazina, kwa maana ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

Aidha, baadhi ya hesabu za benki zinazofanya matumizi ya Hazina hazijaunganishwa na mfumo huo kama vile hesabu ya matumizi ya miundombinu na hesabu ya matumizi ya fedha za kigeni. Hali hii imepelekea kuwepo kwa matumizi yasiyo taslim (*Dummy*) katika mfumo wa *IFMS*.

Baadhi ya hesabu za Hazina ambazo hazijaunganishwa katika mfumo wa*IFMS*ni kama zifuatazo:-

- Hesabu ya mapato ya Kitengo cha Hazina (*Exchequer Revenue Account*).
- Hesabu ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Kigeni (*Forex Account*).
- Hesabu ya malipo ya mkopo (*Sinking Fund Account*).
- Hesabu ya makusanyo yanayotokana na malipo ya *VISA* (*CRDB Account VISA Collections*).

Ukaguzi unapendekeza kwa uongozi wa wizara kuhakikisha kuwa hesabu zote za mapato ya Hazina yanaunganishwa na Mfumo wa *IFMS* moja kwa moja badala ya kuingiza mapato hayo kwa njia ya kawaida (*manually*) ili kuweza kupunguza uwezekano wa kufanya makosa katika uingizaji wa mapato hayo na kuweza kudhibiti upotevu wa fedha za Umma.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Ni kweli kuwa Ofisi ilikuwa ikiingiza taarifa za mapato kwa njia ya kawaida (manually). Hata hivyo, taarifa hizo huingizwa kwa usahihi. Aidha, Ofisi imefanya maandalizi ya muunganiko wa Mifumo kwa kushauriana na wadau wote wa suala hili (SOFTECH, PBZ na ORFM). Kutokana na uwepo wa mpango wa kubadilisha mfumo wa matumizi Serikalini, Ofisi iliwaandikia barua Wakala wa Serikali Mtandao (EGAZ) ya kuomba muongozo wa muendelezo wa hatua za muunganiko wa Mifumo. Ofisi ilipokea maelekezo ya kuzuia mpango wa maboresho ya Mfumo na kusubiri mfumo Mpya wa BAMAS utakaoanza kutumika mwaka mpya wa fedha 2022/2023. Hivyo, changamoto hiyo itaondoka mara baada ya kumalizika Mfumo wa Zan Malipo kuunganishwa na Mfumo Mpya wa BAMAS

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa mfumo wa IFIMIS una doasari na changamoto nyingi kama zilizoainishwa katika ripoti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali Zanzibar.Hata hivyo, Kamati imeelezwa kuwa Idara ya Mhasibu Mkuu imefanya maandalizi ya muunganiko wa mifumo kwa kushauriana na wadau wote wa suala hili (SOFTECH, PBZ na ORFM) na Kamati imepata fursa ya kukagua barua inayoonesha usimamizi na uboreshaji wa Mfumo wa kihasibu wa Serikali IFIMIS,(barua yenye kumbukumbu namba EA.184/372/01/01/27 tarehe 28/10/2021).

Hivyo, Wizara imekiri kutokea kwa dosari hii katika Mfumo wa IFIMS na Kamati imeridhika majibu na ufafanuzi uliotolewa na Wizara.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kwa kuwa tayari Idara ya Mhasibu Mkuu imepokea muongozo wa muendelezo wa hatua za muunganiko wa

Mfumo, Kamati ya PAC inashauri kuwa hatua za haraka zifinyike ili mwaka mpya wa fedha 2022/2023 uwe tayari umekamilika.

Hoja Namba 1.6.2 Kutokurikodiwa Kwa Katika Mfumo Wa IFIMS Kwa Fedha Zinazotoka Hazina Kwenda Kwenye Hesabu Ya Maendeleo Kwa Ajili Ya Matumizi Ya Mfuko Wa Miundobinu (Manual Transfer)Shilling 67,965,543,856.71

Ukaguzi umebaini kwamba kuna baadhi ya fedha ambazo hupokewa katika Hesabu ya Matumizi ya Maendeleo kutoka Hazina na baadae huhaulishwa kwenda katika Hesabu ya Mfuko wa Miundombinu iliyopo Hazina kwa ajili ya kutekeleza matumizi ya maendeleo kwa miradi mbali mbali iliyoidhinishwa na Tume ya Mipango na kulipwa kupitia hesabu ya Mfuko wa Miundombinu.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa fedha hizi hazirikodiwi katika Mfumo wa *IFMS*, si wakati fedha zinapopokelewa katika hesabu ya matumizi ya maendeleo wala wakati zinapohaulishwa kwenda katika hesabu ya Mfuko wa Miundombinu.

Kiasi kilichopokelewa kutoka Hazina kinaonekana tu katika taarifa ya benki (*bank statement*), lakini hakionekani katika daftari la fedha taslim la *IFMS (IFMS Cash Book)*.

Aidha, fedha hizi hazioneshwi katika taarifa ya usuluhishi wa kibenki ya mwezi. Kinachofanyika ni kwamba wakati matumizi yanapofanywa katika hesabu ya Mfuko wa Miundombinu, fedha za mapato na matumizi yasiyo taslimu '*dummy*' huingizwa katika Mfumo wa *IFMS*, ili kuathiri bajeti ya Fungu Kuu la Bajeti husika.

Jadweli lifuatalo linaonesha fedha zilipokelewa katika Hesabu ya Matumizi ya Maendeleo kutoka Hazina katika kipindi cha miaka mitatu (2018/2019 – 2020/2021) ambazo hazijarekodiwa katika Mfumo wa *IFMS*:-

Jadweli Namba 1: Baadhi ya Fedha Ambazo Zimetoka Hazina Kwenda Hesabu ya Matumizi ya Maendeleo Ambazo Hazijarekodiwa Katika Mfumo.

| Mwaka wa Fedha | Mwezi | Kiasi Kilichoingizwa (Shs.) |
|---|---|---|
| 2018/2019 | July, 2018 | 2,047,434,150.00 |
| | Aug, 2018 | 2,641,291,401.98 |
| | Sep, 2018 | 0 |
| | Oct, 2018 | 3,038,624,751.00 |
| | Nov,2018 | 2,657,211,804.00 |
| | Dec,2018 | 0 |
| | Jan, 2019 | 6,184,603,612.63 |
| | Feb, 2019 | 4,383,519,466.00 |
| | Mar, 2019 | 5,736,578,228.10 |
| | Apr, 2019 | 2,594,700,790.00 |
| | May, 2019 | 2,840,842,252.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | June, 2019 | 192,003,200.00 |
| | Jumla Ndogo | 32,316,809,655.71 |
| 2019/2020 | July, 2019 | 1,787,418,524.00 |
| | Aug, 2019 | 4,836,538,083.00 |
| | Sep, 2019 | 2,695,520,201.00 |
| | Oct, 2019 | 3,167,794,128.00 |
| | Nov,2019 | 4,804,793,562.00 |
| | Dec,2019 | 0.00 |
| | Jan, 2020 | 0.00 |
| | Feb, 2020 | 3,040,402,741.00 |
| | Mar, 2020 | 0.00 |
| | Apr, 2020 | 2,761,960,638.00 |
| | May,2020 | 2,039,839,832.00 |
| | June,2020 | 1,332,154,552.00 |
| | Jumla Ndogo | 26,466,422,261.00 |
| 2020/2021 | July, 2019 | 1,818,768,613.00 |
| | Aug, 2019 | 0.00 |
| | Sep, 2019 | 2,324,184,896.00 |
| | Oct, 2019 | 2,591,796,956.00 |
| | Nov,2019 | 2,447,561,475.00 |
| | Dec,2019 | 0.00 |
| | Jumla Ndogo | 9,182,311,940.00 |
| JUMLA KUU | | 67,965,543,856.71 |

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Wizara ya Fedha kuhakikisha kuwa hesabu zote za matumizi za Hazina ziwe zinaunganishwa na Mfumo wa *IFMS*, ili kuongeza uwazi katika matumizi ya fedha za umma na kupunguza fedha za mapato na matumizi yasiyo taslimu (*dummy*).1

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Kutokana na kuwepo kwa changamoto ya kuendelea kufanya muunganiko “integration” kwa hesabu ya muundo mbinu iliopo PBZ, kwa agizo lililotoka kwa wakala wa Serikali mtandao, suala la dummy litaendelea kufanyika mpaka pale utakapokuja mfumo mpya wa BAMAS ambapo utaruhusu kufanyika kwa muunganiko kwa hesabu hio na suala la dummy litaondoka. Barua yenye kumbukumbu nambari CBC.182/193/01 inaeleza.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilielezwa kuwa kutokana na kuendelea na mfumo wa IFIMS suala la dummy litaendelea kufanyika mpaka pale utakapokuja mfumo mpya wa bajeti na matumizi (BAMAS) ambapo utaruhusu muunganiko wa hesabu , Kamati imeoneshwa vithibitisho vya barua ya Muongozo wa hesabu (ACCOUNT) za fedha za kigeni na mifumo inayosimamiwa na hazina barua yenye kumbukumbu namba CBC .182/193/01 tarehe 17/01/2022.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kwa kuwa muongozo huo umetoka hivi karibuni, Kamati ya PAC inashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuuzingatia vizuri muongozo huo utakapokuwa tayari kufanyiwa kazi kwa ajili ya utekeleaji bora wa mapato na matumizi ya Serikali.

Hoja Namba 1.6.3 Dosariza taarifa za usuluhishi wa kibenki kwa hesabu za Ofisi Kuu ya Malipo

Ukaguzi umebaini dasari mbalimbali katika uandaaji wa taarifa za usuluhishi wa kibenki (*bank reconciliation statements*) kwa hesabu za Ofisi Kuu ya Malipo (*Central Payment Office - CPO*) ambazo huandaliwa kila mwisho wa mwezi.
Mapato na matumizi yasiyo taslimu (*Dummy Transactions*) hayaonyeshwi katika taarifa za usuluhishi wa benki, ingawa yanaonekana katika daftari la mapato na matumizi la *IFMS*.
Aidha, ukaguzi umebaini kwamba taarifa za usuluhishi wa kibenki za hesabu ya maendeleo hazioneshi fedha zilizopokelewa benki kutoka Hazina, fedha ambazo mwishowe huhamishiwa katika hesabu ya miundombinu. Upokeaji wa fedha kutoka Hazina na uhaulishaji wa fedha kwenda hesabu ya miundombinu hauoneshwi kabisa katika daftari la fedha taslim (*cash book*) wala katika taarifa za kusuluhishiwa kibenki.

Ukaguzi umebaini kuwa kuna baadhi ya miezi haina taarifa za usuluhishi wa kibenki zilizokubaliana na bakaa za mwezi husika na kupelekea tofauti kati ya bakaa ya fedha kwa mujibu wa daftari la fedha taslim la *IFMS* na bakaa ya fedha baada ya kuandaa taarifa ya usuluhishi wa kibenki. Tofauti zilizobainika ni kama ilivyoonekana katika jadweli lifuataloː-

Jadweli Namba 2: Tofauti Zilizobainika Katika Taarifa za Usuluhishi wa Kibenki za Hesabu za Ofisi Kuu ya Malipo

| Hesabu | Tarehe | Bakaa ya Fedha Kwa Mujibu wa Daftari la Fedha Taslim la *IFMS* (Shs.) | Bakaa ya Fedha kwa Mujibu wa Taarifa ya Usuluhishi wa Kibenki (Shs.) | Tofauti (Shs.) |
|---|---|---|---|---|
| Hesabu ya Matumizi ya Kawaida - 9928182004 | 31 Julai, 2018 | 8,847,484,357DR | 8,814,533,625DR | 32,950,732DR |
| Hesabu ya Matumizi ya Kawaida - 9928182004 | 31 Disemba, 2018 | 21,016,848,452DR | 20,775,392,142DR | 241,456,309DR |
| Hesabu ya Public Debt-9928182004 | 31 Januari, 2019 | 12,062,978,741DR | 12,737,950,875DR | 674,972,134DR |
| Hesabu ya Matumizi ya | 28 Februari, 2019 | 28,724,925,190DR | 28,721,636,601DR | 3,288,589DR |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kawaida – 9928182004 | | | | |

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Wizara kuhakikisha wanaondosha mapato na matumizi yasiyo taslimu (*dummy*) ndani ya mfumo kwa kuiwezesha kila idara kukusanya na kutumia fedha za Serikali ndani ya mfumo. Aidha, fedha zote zinazoingia na kutoka katika hesabu za benki za Serikali lazima ziwe zinahusishwa katika taarifa ya usuluhishi wa kibenki za kila mwezi.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Ni kweli dosari za taarifa za usuluhishi wa kibenki kwa Hesabu ya matumizi ya kawaida na hesabu ya Public Debt ulikuwepo kama mkaguzi alivoanisha kwenye ripoti yake. Usuluhishi katika ofisi kuu ya malipo hufanywa kwa kutumia mfumo wa (TMS) kutokana na changamoto ya mfumo ilipeleka baadhi ya miezi bakaa ya fedha kutofautiana kwa sababu ya mfumo kushindwa kusoma kaaarifa sahihi zilizokuwepo kwenye daftari la fedha taslimu (cashbook), dosari hio ilisawazishwa mwishoni mwa mwaka wa fedha juni 2019 wakati wa kufunga hesabu na kwa sasa dosari hio haipo.

Aidha suala la dummy litaendelea kufanyika mpaka mfumo mpya wa BAMAS utaporuhusu kufanyika kwa muunganiko kwa hesabu hio na suala la Dummy litaondoka.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kwa suala la dummy Kamati imeelezwa kuwa litaendelea kuwepo mpaka mfumo mpya wa bajeti na matumizi (BAMAS) utakapoanza, Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Hoja hii pamoja na ufafanuzi uliotolewa na haikuwa na maelezo zaidi juu ya Hoja hii.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaishauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuendelea kufuatilia mfumo mpya wa BAMAS ambao utasaidia kuokoa upotevu mkubwa wa fedha za Serikali

**Hoja Namba 1.6.4 Tofauti kati ya fedha iliyoizinishwa kupelekwa katika mafungu makuu ya bajeti na fedha halisi zilizohaulishwa kwenda katika mfungu hayo shilingi 1,358,829,378**

Fedha kutoka Hazina hupelekwa katika Mafungu Makuu ya Bajeti kupitia Mfumo wa*IFMS* kila mwezi kulingana na mtiririko wa fedha ulioidhinishwa kwa Wizara husika kwa kila mwezi. Fedha hizo kutoka Hazina zinaingizwa katika Mfumo wa*IFMS* baada ya kuishinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa hali ya kifedha na kiuchumi.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa tofauti kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali na kiasi halisi cha fedha kilichoingizwa katika Mafungu Makuu ya Bajeti. Vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa tofauti hivyo havikupatikana kwa ukaguzi.

Uwepo wa tofauti kwa fedha zinazoingizwa katika Mafungu Makuu ya bajeti kama ilivyoainishwa hapo chini kunapelekea kukosekana kwa uhalali wa fedha za ziada zilizoingizwa katika Mafungu Makuu ya Bajeti. Tofauti ya fedha hizo ni kama ilivyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Namba 3: Tofauti kati ya Fedha Zilizoidhinishwa Kupelekwa Katika Mafungu Makuu ya Bajeti na Fedha Halisi Zilizohaulishwa

| Tarehe | Fedha Iliyoidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali Shs. | Fedha Halisi Iliyoingizwa Katika Mfumo wa IFMS Shs. | Tofauti Shs. |
|---|---|---|---|
| 21-Dec-2016 | 2,507,130,644.00 | 3,584,112,952.00 | 1,076,982,308.00 |
| 6-Aug-19 | 5,022,325,240.00 | 5,036,812,740.00 | 14,487,500.00 |
| 11-Nov-19 | 6,564,238,952.00 | 6,589,160,452.00 | 24,921,500.00 |
| 25-Mar-20 | 55,000,000.00 | 250,075,070.00 | 195,075,070.00 |
| 23-Jun-20 | 9,474,456,000.00 | 9,521,819,000.00 | 47,363,000.00 |
| Jumla | | | 1,358,829,378.00 |

Ukaguzi unapendekeza kuwepo kwa mfumo wa uwazi kwa fedha zinazoidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali kutoka Hazina kwenda katika Mafungu Makuu ya Bajeti, ili tofauti baina ya fedha hizo iweze kubainika na kupatiwa maelezo ya wazi.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Tofauti hiyo ilitokana na kuwepo kwa maagizo mengine yaliyoidhinishwa ya kuingiza fedha katika Taasisi husika. Hata hivyo, barua zilizoidhinisha uingiaji wa fedha hizo katika mafungu makuu ya bajeti zipo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilitaka kujua kwa nini alipokuja Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti hakupatiwa vielelezo , Kamati ilielezwa kuwa jalada la Vielelezo hivyo liliwasilishwa kwa wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibti wakati wa ukaguzi, ingawa Wakaguzi hao waliiambia Kamati kuwa vielelezo hivyo hawakuviona.Hata hivyo, vilelezo hivyo viliwasilishwa mbele ya  Kamati ya PAC kwa ukaguzi.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaiomba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu a Hesabu za Serikali wakati wanapofanya ukaguzi ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kikatiba kwa ufanisi unaotakiwa.

Hoja Namba 1.6.5 Fedha Zilizohaulishwa Mwishoni Mwa Mwaka wa Fedha Kwenda Katika Hesabu za Amana Shilingi 5,047,449,249.16

Kwa mujibu wa kifungu nambari 52(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016, bakaa ya fedha za matumizi ambayo hayakutumika hadi mwisho wa mwaka wa fedha ambao matumizi yao yameidhinishwa itaondoshwa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali au katika Hesabu ya Serikali ya Mtaa kwa kadri itakavyohitajika.

Ukaguzi umebaini kufanyika kwa uhaulishaji wa fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha kwenda katika Hesabu za Amana kwa ajili ya matumizi ya mwaka wa fedha uliokwisha malizika, ambapo ruhusa ya kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali haikupatikana kwa ukaguzi. Taarifa za uhaulishaji huo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 4: Fedha Zilizohaulishwa Mwishoni Mwa Mwaka wa Fedha Kwenda Katika Hesabu za Amana

| Tarehe | Fedha Kutoka Hesabu ya: | Fedha Kwenda Hesabu ya Amana: | Kiasi cha Fedha Shs. | Fungu Kuu la Bajeti | Kumbukumbu ya Benki |
|---|---|---|---|---|---|
| 29-Juni-2020 | CAPITAL ACCOUNT | 021103000778 KATIBU MKUU WIZARA YA KILIMO | 1,300,000,000.00 | WIZARA YA KILIMO | L01PV1900001873 |
| 29-Juni-2020 | CAPITAL ACCOUNT | ZANZIBAR CENTRAL MISCELLANEOUS DEPOSIT-9928161804 | 257,683,229.62 | WIZARA YA FEDHA | F01PV1900002259 |
| 30-Juni-2020 | CAPITAL ACCOUNT | ZANZIBAR CENTRAL MISCELLANEOUS DEPOSIT-9928161804 | 23,846,898.00 | TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA | C04PV1900000470 |
| 26-Juni-2019 | CAPITAL ACCOUNT | C Miscellaneous Deposit | 419,817,500.00 | WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI | S01PV1800001282 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Account | | | |
| 30-Juni-2020 | PUBLIC DEBT ACCOUNT | 021103000709 PUBLIC DEBT DEPOSIT ACCOUNT | 1,072,142,934.98 | HUDUMA ZA MFUKO MKUU | F02PV1900002453 |
| 29-Juni-2020 | RECURRENT ACCOUNT | ZANZIBAR CENTRAL MISCELLANEOUS DEPOSIT-9928161804 | 516,706,745.56 | WIZARA YA FEDHA | F01PV1900002260 |
| 27-Juni-19 | RECURRENT ACCOUNT | C Miscellaneous Deposit Account | 534,197,102.00 | WIZARA YA FEDHA | F01PV1800002188 |
| 26-Juni-19 | RECURRENT ACCOUNT | C Miscellaneous Deposit Account | 923,054,839.00 | WIZARA YA FEDHA | P01PV1800001483 |
| Jumla | | | 5,047,449,249.16 | | |

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Wizara ya Fedha kuhakikisha kuwa kifungu nambari 52(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016, kinawajibishwa kwa bakaa ya fedha za matumizi mwisho wa mwaka na kama kuna dhima ya matumizi, basi taasisi ya matumizi lazima ipate ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ya kubakisha fedha hizo katika Hesabu ya Amana.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Uhaulishwaji wa fedha uliofanywa mwishoni mwa mwaka kwenda katika hesabu ya Amana ya Hazina ni Shilingi 2,675,297,314.18, uhaulishaji huu ulipata ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kama zilivyoombwa na Wizara husika.Barua zipo.
Hata hivyo kiasi cha Shilingi 1,300,000,000.00 na Shilingi 1,072,142,934.98 malipo haya yalifanywa moja kwa moja kwa Taasisi husika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa uhaulishwaji wa fedha ulipata ruhusa kutoka kwa mlipaji mkuu wa Serikali kama

zilivyoombwa na Wizara husika kama ilivyoolezwa kwenye majibu ya Wizara ,na Kamati ilipata fursa ya kukagua vielelezo vya uthibitisho vya uhaulishwaji huu vikiwemo vifuatavyo:-

i. Dokezo la tarehe 25/06/2020 kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango linalohusu uhaulishwaji wa fedha jumla ya shilingi 257,683,225/=kutoka Hesabu ya Development no.992819070 kwenda Hesabu ya Deposit ya tarehe 25/06/2020.

ii. Barua ya ombi la kuhifadhi shilingi 23,846,896 ya tarehe 19/06/2020 yenye nambari ya kumbukumbuTKKUDK/WF.01/VL.1/30,

iii. Barua kutoka Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwenda Wizara ya Fedha na Mipango yenye nambari ya kumbukumbu WVUSM/WF.32/8/VOL.1/83 ya tarehe 18 Juni 2019 fedha za mradi wa ajirabkwa vijana shilling 419,817,500 na shilingi 68,830,373 za deposit ujenzi wa viwanja vya wilaya

Hata hivyo, Kamati ya PAC ilielezwa kuwa katika uhaulishwaji wa fedha hizi kuna "deposit account" ya Serikali na "deposite account" ya Wizara, iwapo Wizara au taasisi ikihaulisha fedha kwenye akaunti yake wenyewe haihitaji saini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali, Kamati ya PAC meridhika na majibu pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Hoja Namba 1.6.6 Matumizi ya Nambari Moja ya Kumbukumbu ya Hati ya Exchequer ya IFMS (SameReference Number) Kwa Fedha Zilizotolewa Kwa Mafungu Makuu Tofauti ya Bajeti.

Ukaguzi umebaini kuwa hati za utoaji fedha za *Exchequer* zilizomo ndani ya Mfumo wa*IFMS* zinatumia namba za kumbukumbu zinazofanana kwa fedha zilizotolewa kwenda Mafungu Makuu tofauti ya Bajeti kwa tarehe husika.

Hii inapelekea ugumu katika usawazishaji wa matumizi ya fedha za Mafungu Makuu ya Bajeti Katika taarifa za upatanishi wa bajeti hasa kwa fedha za mapato na matumizi yasiyo taslimu (*dummy*) kutokana na ukweli kwamba, ili matumizi ya '*dummy'* ya Fungu Kuu fulani la bajeti yaonekane katika Mfumo wa *IFMS* ni lazima fedha zote za '*dummy'* za Mafungu Makuu mengine yenye nambari ya kumbukumbu inayofanana nayo yawe yameshasawazisha matumizi ya fedha hizo katika mfumo.

Baadhi ya nambari za kumbukumbu zinazofanana za hati za utoaji wa fedha za *Exchequer* kwa vifungu tofauti vya bajeti zilizobainika ni kama inavyoonekana katika kiambatisho nambari 1.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wizara kuhakikisha kuwa nambari za kumbukumbu za hati za utoaji wa fedha za *Exchequer* kwa vifungu tofauti vya bajeti ziwe tofauti kwa kila Fungu Kuu la Bajeti, ili kuondosha utata wakati wa ukaguzi wa fedha hizo pamoja na kurahisisha utayarishaji wa taarifa za upatanishi wa kibenki.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Hii inatokana na Serikali inapotoa fedha kutoka kwenye Mfuko Mkuu hutoa fedha kwa ujumla kwa kutumia kumbukumbu namba moja (same reference number) kwenda kwenye mafungu makuu tofauti ya bajeti, hivyo kwenye mfumo inatumia kumbukumbu moja iliyotumika kuhamisha fedha iliyotoka kwenye hesabu ya mfuko mkuu iliyoko Benki Kuu, ili kutofautisha muamala mmoja na mwengine inabidi kulinganisha kumbukumbu namba na mafungu makuu (Vote)

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kutokana na dosari iliyojitokeza Kamati ya PAC imebaini kuwa Serikali inapotoa fedha kutoka kwenye Mfuko Mkuu wanatoa fedha kwa ujumla kama majibu ya Wizara yanavoeleza na baadae wanasambaza fedha hizo kwanye kila Taasisi au Wizara husika na kamati pia imeelezwa kuwa ikiwa Wizara watatumia kumbukumbu namba tofauti (diferent refence number) itakuwa changamoto kubwa kwa sababu barua zitakuwa nyingi sana na hatimaye itapelekea usumbufu.

Pamoja na majibu na maelezo ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Kamati iliridhika ma majibu hayo..

Hoja Namba 1.6.7 Dosari Zilizobainika Katika Uhakiki wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha – *IFMS*.

Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imeanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Fedha – *IFMS*, kwa ajili ya kuimarisha malengo yake ya utoaji wa huduma za taarifa za fedha katika Taasisi za Serikali.

Mfumo huo umetengenezwa ili kuweka usimamizi wa taarifa za fedha za taasisi za Serikali, ambapo umegawika katika moduli tofauti, ikiwemo moduli ya "*Account Payable", Account Receivable", "Purchasing Order", Fixed Assets", "General Ledger", "Cash Management" na "e-Procurement".*

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika Mfumo huo wa*IFMS/EPICOR Version 10.1.4,* ambapo dosari hizo zinaweza kusababisha hatari katika utendaji kazi wa mfumo huo. Baadhi ya dasari zilizomo ni kama zifuatazo: -

i. Kuwepo kwa watumiaji wa mfumo ambao waliojirudia na wenye shaka (*duplicated/ ambiguoususers*) pamoja na watumiaji wasiojulikana (*uknown users*) ambao wamepewa haki kubwa za matumizi ya mfumo huo (*Administrative Rights*) Kiambatisho Nambari 2(a) kinahusika.
ii. Baadhi ya watumiaji wa Mfumo wa *IFMS* nenosiri "*Domain Password*" zao zimeshaisha muda, hivyo watumiaji hao huingia kwenye mazingira ya mfumo huo kupitia akaunti za watumiaji wengine (*Sharing of login credentials*).
iii. Baadhi ya watumiaji wa mfumo wapo likizo kwa muda mrefu, lakini ndani ya mfumo wanaonekana wapo hai (*active status*) na akaunti zao hazijasimamishwa. Kiambatisho Nambari 2(a) kinahusika.
iv. Tathmini ya Upimaji wa kuwepo kwa vihatarishi haifanyiki ndani ya Mfumo wa *IFMS*, ili kuweza kubaini viashiria hatarishi vilivyomo katika mfumo huo na kudhibiti visije kutokea "*Vulnerability Assesment and Penetration Testing*".

v. Kutumika kwa Akaunti Asilia za wasimamizi wa mfumo na kanzidata "*Administrators Account*" ambazo *account* hizo zilipaswa kusitishwa "*disabled*" na badala yake kutumika kwa haki zao tu *Administrators Rights".* Kiambatisho Nambari 2(a) kinahusika.

Hali hii inaweza kusababisha kupotea au kubadilishwa kwa makusudi taarifa za fedha za taasisi katika mfumo huo na hatimae kusababisha upotevu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa idara kuweza kutatua dosari zote zilizopo katika mfumo huo, ili kuweza kuepukana na vihatarishi vya upotevu wa taarifa na fedha za Serikali.

Maiibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

*(i)* Mfumo unatumia "user ID" na sio "username" kama alivobainisha mkaguzi, ambayo ndio inayotumika kuingia katika Mfumo. Hivyo hakuna (dublcate users) kama ilivooneshwa katika kiambatanisho namba 2a cha ukaguzi.

Kwa upande wa watumiaji wasiojulikana (uknown users) ambao nambari zao za utambulisho hazina nambari za mshahara hawa ni wasimamizi wa mtandao ambao tulipokea ushauri wa awali kutoka kwa Washauri Elekezi wa Mfumo tangu 2007 kuwa wasimamizi hawana ulazima wa kuwekewa nambari za Mshahara katika nambari zao za utambulisho. Kwakuwa ukaguzi huu ubaini hii ni dosari ushauri tumeupokea na tayari umefanyiwa kazi Mfano Mfano katika kiambatanisho nambari 2 (a) Msimamizi mwenye utambulisho AYHYA nambari ya usajili imefanyiwa marekebisho AshaYH104865

(ii) Hii ni changamoto inayotokana na watumiaji wa mfumo, Ofisi imeanza kuchukua juhudi ya kuwaelimisha.

(iii) Hii inatokana kukosekana kwa uthibitisho wa nakala ya barua ya likizo ya mtumiaji. Hata hivyo, hatua zimechukuliwa kwa kuanzisha utaratibu wa kufanya uhakiki watumiaji waliokuwa hawaingii katika mfumo kuanzia siku 20 na kuzuiwa "inactive" na watakapohitaji kuingia katika mfumo wanalazimika kuandika barua ya kuomba ruhusa ya kutumia mfumo.

(iv) Ni kweli kumekuwa na changamoto ya kutofanyika kwa upimaji wa vihatarishi katika mfumo, hii ni kutokana na kukosa uwezo wa kufanya zoezi hilo kwa taasisi zetu za serikali na si vyema zoezi hili kulipatia taasisi binafsi kwani itakuwa tumeshaonesha udhaifu ulipo wa mfumo kwao, na mfumo huu ni wa serikali na una taarifa nyingi ambazo ni siri. Hata hivyo uongozi umeona ni vyema kuwaandikia barua Wakala wa Serikali Mtandao kwa ushauri zaidi.

(v) Ni kweli katika kipindi cha ukaguzi administrator user alikuwa active, hii ni kutokana na kuwa katika kipindi hicho kulikuwa na maboresho ya mfumo wa Window server 2012 na kuelekea window server 2016 hivyo user hiyo ikawa inatumika. Hata hivyo tayari user hiyo ilishafungwa na kuendelea kutumia users binafsi. Kwa upande wa user 'manager' pamoja na kuwa ni users yenye kuendesha huduma za mfumo lakini pia imekuwa ni vigumu kuifunga kwani hakuna haki itakayotolewa kwa user yoyote

ikaweza kufanyakazi pale VOTI mpya inapotengenezwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kwa ujumla kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Wizara katika kutatua dosari zilizoainishwa hatika hoja hii, Kamati ya PAC imeridhika na hatua hizo zilizoelezwa katika Majiu ya Wizara.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri katika dosari namba IV (inayohusu kutokufanyika kwa upimaji wa vihatarishi katika mfumo) Kamati imeshauri kuwa kazi ya upimaji wa vihatarishi katika Mfumo asipewe kampuni wala binafsi kwa ajili ya usalama wa Mfumo wenyewe na shughuli za Kiserikali kwa ujumla.

Hoja Namb 1.6.8: Kukosekana Kwa Muunganiko wa Moja kwa Moja wa Mawasiliano Baina ya Mfumo wa *IFMS* na Mifumo Mingine ya Fedha ya Taasisi za Serikali

Serikali imetengeneza Mfumo wa Usimamizi wa Fedha-*IFMS* ambao madhumuni yake ni kuhifadhi na kudhibiti taarifa za mapato na matumizi ya fedha za Serikali, kuanzia hatua ya utayarishaji wa bajeti, utekelezaji wa bajeti na utoaji wa ripoti za bajeti katika mawizara, idara na wakala katika Sekta za Umma.

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa *IFMS* haujaunganishwa moja kwa moja na mifumo mingine ya fedha ya Serikali, kama vile mifumo ya kukusanyia mapato na kodi (*ZRB* na *TRA*), Mifumo ya Kibenki (*PBZ*) pamoja na mifumo ya taasisi nyengine za Wakala wa Serikali, ambapo mifumo hiyo kwa pamoja ingeweza kuwasiliana na kupelekea taarifa za mapato kuingia moja kwa moja na kwa wakati ndani ya mfumo wa *IFMS* (*automatically*), ili kudhibiti makosa katika usahihi wa kuingiza taarifa hizo kwa mkono na kusababisha upotevu wa mapato na matumizi ya fedha.

Kukosekana kwa muingiliano wa moja kwa moja baina ya mifumo ya fedha ya Serikali (*IFMS, ZRB, TRA, PBZ* n.k) kunaweza kupelekea kufanyika kwa makosa katika uingizaji wa taarifa za mapato na matumizi ya fedha za Serikali na hatimae kutokea kwa upotevu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Idara ya Mhasibu Mkuu kufanya mchakato wa kuunganisha mifumo hiyo mikuu ya fedha moja kwa moja, ili kuweza kupata usahihi wa taarifa za fedha na kudhibiti upotevu wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Ni kweli Zoezi hili halikufanyika kwanza ni kutokana na hapo nyuma Taasisi nyingi za Serikali zilikuwa na changamoto ya mifumo yao kutokuwa sawasawa, Mfano ZRB ikapelekea kuboresha mfumo wake na kuuacha mfumo wa zamani, PBZ pia walikuwa katika mchakato wa kuhamia mfumo mpya. Hata hivyo baada ya ukaguzi, Ofisi ilianza taratibu za maandalizi ya muunganiko huo wa Mifumo kwa kushirikishana na wadau wote wa suala hili (SOFTECH, PBZ na ORFM).

Kutokana na uwepo wa mpango wa kubadilisha mfumo wa matumizi Serikalini, Ofisi iliwaandikia barua Wakala wa Serikali Mtandao (EGAZ) ya kuomba muongozo wa muendelezo wa hatua za muunganiko wa Mifumo. Ofisi ilipokea maelekezo ya kuzuia mpango wa maboresho ya Mfumo na kusubiri mfumo Mpya wa BAMAS utakaoanza kutumika mwaka mpya wa fedha 2022/2023 kupitia barua yenye kumbukumbu nambari OR/EGAZ/SYS/VOL.1/23. Hivyo, changamoto hiyo itaondoka mara baada ya kumalizika Mfumo wa Zan Malipo kuunganishwa na Mfumo Mpya wa BAMAS.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuthibitisha hatua zilizochukuliwa na Wizara suala miunganiko ya mifumo, Kamati ya PAC iliikagua barua kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Serikali Mtandao kwenda Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ya tarehe 8 November 2021 kumbukumbu namba EA.184/372/01/01/27 inayohusu Muongozo juu ya usimamizi na uboreshaji wa mfumo wa kihasibu wa Serikali IFIMIS –EPICOR

Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa Idara ya Mhasibu Mkuu inachukuwa juhudi yenyewe za kurekebisha baadhi ya matatizo kwenye mfumo, huku ikisubiri muongozo kutoka e-goverment kama walivyoeleza. Kamati imeridhika na majibu pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Wizara kuhusu Hoja hii.

Hoja Namba 1.6.9 Kukosekana Kwa Mpango wa Muendelezo wa Biashara na Mpango wa Kupona Maafa "Lack of *BCP*&*DRP*".

Lengo la kuwa na Mpango wa Muendelezo wa Biashara na Mpango wa Kupona Maafa katika taasisi ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na udhibiti mzuri wa upatikanaji wa taarifa na kuendelea kutoa huduma bora za biashara wakati janga lolote litakapotokea katika idara au miundombinu ya idara.

Moja ya njia nzuri ya kuzilinda taarifa na kuendeleza Mpango wa Uendelezaji wa Biashara, wakati janga litakapotokea kwenye idara ni kuwa na mpango maalum na miundombinu madhubuti ya kuhifadhi taarifa katika sehemu iliyotengwa (*offsite backup*) nje ya idara kuu.

Mpango mzuri wa Muendelezo wa Biashara ni ule ambao mara zote unakuwa imara katika usafirishaji wa taarifa kutoka sehemu kuu ya taarifa (*Datacenter*) kwenda sehemu nyengine ya kuhifadhia taarifa ambayo ina umbali wa masafa (*offsite backup*). Taarifa hizo zinasafirishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine kupitia mtandao ulio salama.

Taarifa hizo zinapohifadhiwa katika sehemu ya pili (*Offsite – Backup Location*) zinatakiwa zichunguzwe na kujaribiwa kwa kushirikishwa uongozi wa idara, ili kuweza kuona na kuhakikisha kwamba taarifa hizo ziko sahihi na zinaweza kupatikana wakati zitakapohitajika.

a) Kasoro Zilizobainika Katika Sehemu ya Pili ya Kuhifadhia Taarifa (*Disaster RecoverySite*)

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu inayo sehemu ya pili (*Disaster RecoverySite*) iliyopo nje ya mji kwa ajili ya kuhifadhia taarifa wakati janga likitokea katika sehemu kuu ya kuhifadhia taarifa iliyopo Vuga Mjini.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwamba taarifa zilizohifadhiwa sehemu ya pili hazifanywi majaribio yoyote ya kuzichunguza, ili kuhakikisha kwamba ziko vizuri na zinaweza kufanya kazi kwa usahihi wakati zitakapohitajika.

Kutokufanya majaribio ya kuchunguza taarifa zinazohifadhiwa katika sehemu ya pili, kunaweza kusababisha hatari ya kutopatikana kwa taarifa wakati janga litakapotokea katika sehemu kuu ya kuhifadhia taarifa na hatimae kupelekea kukosekana kwa muendelezo wa huduma za fedha katika mfumo wa *IFMS*.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Idara ya Mhasibu Mkuu kuzifanyia majaribio taarifa zinazohifadhiwa katika sehemu ya pili, ili kupata uhakika wa taarifa hizo kama zinaweza kufanya kazi kwa usahihi wakati zitakapohitajika.

b) Kukosekana Kwa Nyaraka za Mpango wa Muendelezo wa Biashara na Nyaraka za Mpango wa Udhibiti wa Kupona Maafa *Lack of BCP & DRP Documentation*)

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu haina nyaraka rasmi ambazo zinaonesha mpango/muongozo kamili wa Muendelezo wa Biashara na kupona maafa, endapo maafa (majanga) yakitokea katika idara hiyo.

Kutokuwa na nyaraka ambazo zitakazoonesha Mpango wa Muendelezo wa Huduma za Biashara na Mpango wa Kupona Maafa katika Idara kunaweza kusababisha hasara ya kuharibika kwa vitendea kazi vya kompyuta, miundombinu ya mawasiliano na hatimae kupotea taarifa muhimu katika mfumo wa *IFMS*.

Ukaguzi unashauri idara kuandaa nyaraka za mpango utakaoonesha muongozo kamili wa Muendelezo wa Biashara na nyaraka zenye kuonesha mpango kamili wa kupona maafa, ikiwa maafa (majanga) yatatokea katika idara

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

(i) Taarifa zinazohifadhiwa (Disaster Recovery Site) zinafanyiwa majaribio na zinafanyakazi, kwani taarifa hizo huhifadhiwa katika sehemu mbili tofauti ambazo ni DRS na katika Mtambo ya majaribio na hutumika kama kawaida

inapoingizwa. Ingawaje kumbukumbu za majaribio hayo hazikuwa zikiwekwa. Hata hivyo, utaratibu wa kuweka kumbukumbu za majaribio hayo umeanza kufanyika.

(ii) Ofisi ilitayarisha muongozo wa TEHAMA (ICT Security Guideline) ambao umeonesha mpango wa biashara na udhibiti ambao ndio unaotumika kwa sasa. Hata hivyo, kwa utaratibu uliopo Jukumu la Uandaaji wa Sera ya TEHAMA (ICT Policy) linasimamiwa na Wakala wa Serikali Mtandao ambayo bado inaendelea kutumia sera yake ya zamani. Ndani ya sera hiyo itajumuisha nyaraka za Mpango wa muendelezo wa Biashara (BCP) na nyaraka za mpango wa udhibiti wa kupona maafa (DRP) na Taasisi zilizo chini yake zitatakiwa kutayarisha miongozo kupitia Sera hiyo kuu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kutokuwekwa kwa kipindi kirefu kumbukumbu za taaarifa za kufanyiwa majaribio na kutokuwepo kwa ripoti ya kufanyika ya majaribio ya sehemu ya pili ya kuhifadhia taarifa (*Disaster Recovery Site*). Idara ya Mhasibu Mkuu imekiri kuhusu jambo hilo lakini tayari utaratibu wa kuweka kumbukumbu za majaribio hayo umeanza kufanyika ikiwemo kuandaa ripoti kwa ajili ya kufanywa majaribio hayo

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri

Wizara ifanye juhudi ya haraka ya kurekebisha changamoto zote zilizopo katika eneo la Kuhifadhia Taarifa (*Disaster Recovery Site*) ili taarifa zote za kimfumo ziweze kuaoatikana pindi liatapotokea jambo lolote lisilotatarijiwa.

Hoja Namba 1.6.10 Kukosekana Kwa Mkataba wa Viwango vya Utoaji wa Huduma ya Mfumo wa IFMS Baina ya Idara ya Muhasibu Mkuu na Mshauri Elekezi (*Service Level Agreement-SLA)*.

Utaratibu uliobora unaeleza kwamba taasisi inatakiwa kufunga mkataba rasmi uliosainiwabaina ya pande mbili (mtoaji huduma na Taasisi itakayopewa huduma) ambapo mkataba huo utaonesha aina gani ya huduma itakayotolewa nakiwango gani cha huduma kitatolewa na "*Services Provider*", ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Muhasibu Mkuu inatumia Mfumo wa Usimamizi wa Fedha- *IFMS* ambao umetengenezwa na Kampuni ya *Soft Tech Consultant Limited (STCL)*. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kukosekana kwa mkataba rasmi uliosainiwa ambao unaonesha kiwango gani cha huduma za mfumo kinachotakiwa kutolewa na Kampuni ya *STCL* kwa ajili ya idara ya Muhasibu Mkuu, ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kukosekana kwa Mkataba wa Viwango vya Utoaji wa Huduma (*SLA*) za Mfumo wa *IFMS* kunaweza kupelekea Idara ya Mhasibu Mkuu kutofahamu kiwango halisi cha utendaji kazi wa mfumo huo na kupelekea kutoa huduma chini ya kiwango, kutopata msaada wa kiufundi kwa wakati, kukosa matengenezo na maboresho ya mfumo na hatimae kuingia gharama za uendeshaji zisizo za lazima.

Ukaguzi unashauri uongozi wa idara kuhakikisha kwamba mkataba wa viwango vya utoaji wa huduma unatengenezwa rasmi na kusainiwa, ili kupata msaada mzuri wa upatikanaji wa huduma kutoka kwa kampuni ya *STCL*.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Mkataba wa Viwango vya utoaji wa huduma ya mfumo wa IFMIS baina ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Mshauri Elekezi (SLA) ulichelewa kuwasilishwa kwa watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa sababu za kufuata taratibu za kupelekwa Wakala wa Serikali Mtandao na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, kwa sasa Mkataba huo umekamilisha taratibu zote na unapatikana kwa ukaguzi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa kazi ya kufunga na kutumia Mfumo wa Usimamizi wa Fedha (IFMIS) imefanyika mwanzo na mkataba ukafuata baadae ambapo Mfumo wa IFMIS (awamu ya pili) ulianza kutumika rasmi mwaka.2015 lakini Mkataba wake umetiwa saini mwaka 2021. Hata hivyo, Idara ya Mhasibu Mkuu wamekiri kutokea kwa dosari hii kama walivyoelezwa kwenye majibu ya Wizara

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaishauri Serikali kujipanaga vizuri zaidi katika kuandaa mikataba kwa wakati uliopangwa kulingana na kazi inayokusudiwa kutekelezwa ili kuepusha dosari mbalimbali zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelazaji wa mikataba hiyo.

Hoja Namba 1.6.11 Dosari Zilizobainika Katika Kudhibiti Matumizi ya Programu za Kompyuta na Media.

Utaratibu uliobora unaeleza kwamba Taasisi ambazo zinatumia mifumo muhimu ya *TEHAMA*, zinatakiwa kuweka udhibiti na usalama mkubwa wa taifa ambazo zitahifadhiwa ndani ya mifumo hiyo.

Moja kati ya njia imara za kudhibiti na kuweka usalama wa taarifa za kwenye mifumo ni kuweka sera zilizobora katika matumizi ya kompyuta za ofisi pamoja na sera za matumizi ya programu (*software*) zinazotumika katika kompyuta hizo.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya kompyuta za Idara ya Mhasibu Mkuu- *IFMS* zinadosari mbali mbali za kiusalama, ambazo zinaweza kusababisha upotevu wa taarifa zilizohifadhiwa ndani yake na kupelekea kutokea kwa hatari ya kushambuliwa mfumo mzima wa usimamizi wa fedha IFMS. Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

(a) Utoaji wa "*Antivirus*" zilikuwa huru na hazina leseni za matumizi. Kiambatisho nambari 2(e) kinahusika.
(b) Utumiaji wa Programu za Mfumo wa Uendeshaji wa Kopyuta na Seva (*OperatingSystems*) ambazo hazina leseni za matumizi na nyengne zimeshapitwa na wakati (*Windows7).* Viambatisho nambari 2(c) na 2(f) vinahusika.
(c) Kutodhibitiwa kwa sehemu za mawasiliano katika kompyuta, kama vile sehemu za kuingiza *flash*, sehemu za kuingiza *wire* za simu, pamoja na milango ya *CD/DVD*.
Sehemu hizi zinaweza kusababisha uingizaji wa virus kwenye kompyuta na seva za ofisi, zikiwa hazitakuwa na udhibiti mzuri.
(d) Utumiaji wa programu za "*Microsoft Office*" ambazo ni feki na hazina leseni za matumizi.

Kutoweka udhibiti mzuri katika matumizi ya kompyuta na media, kunaweza kusababisha hatari ya upotevu wa taarifa muhimu za idara na kupelekea kuharibika kwa mfumo wa usimamizi wa fedha.

Ukaguzi unashauri idara kuweka udhibiti imara katika matumizi ya kompyuta pamoja na milango ya media, ili kuweza kulinda taarifa ziliomo ndani ya kompyuta na Mfumo wa Usimamizi wa Fedha. Baadhi ya njia imara za kudhibiti upotevu wa taarifa katika kompyuta ni kama zifuatazo:-

- Kuweka sera imara za matumizi ya kompyuta katika ofisi.

- Kuweka sera imara za kudhibiti matumizi ya media kwenye kompyuta kama vile matumizi ya flash disk, *CD/DVD* na kuunganisha simu katika kompyuta.
- Kutumia mfumo wa network za ndani (*file and folders sharing-LAN*) kwa ajili ya kuhamisha taarifa kutoka kompyuta moja kwenda nyengine ndani ya ofisi.
  Vile vile kutumia baruapepe (*emails*) rasmi za ofisi kwa ajili ya mawasiliano na kusafirisha taarifa nje na ndani ya ofisi, ili kuweza kudhibiti upotevu na uharibikaji wa taarifa na mfumo wa fedha wa idara.
- Kununua programu halisi (*Original and Genuine Software*) zenye ubora na za kisasa, ili kuweza kupata usalama "*updates*" na leseni za matumizi halali ya programu hizo kwa ajili ya ofisi. Programu halisi za kununua ili kupata usalama wa kutosha na leseni za matumizi halali zikiwemo "*Windows Operating Systems, Computer Antiviruses*" pamoja na "*Office Packages*".

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

*(i)* Kompyuta zote zinazotumika kwa mfumo wa IFMIS zimewekewa antivirus na hazitakiwi kutumika kwa matumizi mengine nje ya Mfumo. Aidha, Ofisi imetenga kompyuta kwa matumizi mengine ya kiofisi ambazo watumiaji hujifunza mambo mbali mbali kupitia intaneti n.k. Ni kweli miongoni mwa kompyuta hizo zipo ambazo zimekutwa na antivirus huru ambazo zimeingizwa kimakosa. Hata hivyo kupitia ushauri huu tayari kompyuta hizo zimeshawekwa antivirus zenye leseni ya matumizi.

*(ii)* Wakati wa Ukaguzi, Ofisi ilikuwa katika hatua za maboresho (Upgrading) ya Mfumo (MS server 2012) kwenda Mfumo (MS server 2016) hali iliyopelekea kukosekana kwa leseni za matumizi. Kwa sasa hatua hiyo imekamilika na leseni ya matumizi zimeshawekwa.

*(iii)* Ni kweli katika kompyuta za mfumo sehemu za mawasiliano zilikuwazi, hii ni kutokana na kuwa Ofisi ilikuwa ikitumia antivirus kwenye kompyuta na seva zote zilizounganishwa na Mfumo na ilionekana hakukuwa na haja ya kudhibiti matumizi ya Sehemu za mawasiliano katika kompyuta kutokana na uhitaji wake. Hata hivyo, kupitia ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi imeshazuia matumizi ya sehemu za mawasiliano katika kompyuta.

*(iv)* Utaratibu wa awali leseni zote za MicroSoft zilikuwa zikipatikana kutoka Idara ya Serikali Mtandao (EGAZ) na kutakiwa kuziomba kwa maandishi. Hivyo, kutokana na kumalizika kwa mkataba baina ya (EGAZ) na MicroSoft kulipelekea kukosekana kwa leseni hizo kwa wakati kwa komputa ambazo leseni zake zimeisha muda. Ingawa Ofisi iko katika hatua za kupata leseni hizo

Uchunguzi wa Kamati PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa wakati ukaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti kulikuwepo komputa na seva ambazo hazina leseni za matumizi na nyengine zimeshapitwa na wakati (window 7) Aidha, Kamati ilielezwa kuwa wakati wa ukaguzi huo baadhi ya komputa na poti za flashi zilikuwa wazi kitu ambacho hakina usalama kwa komputa. Kwa upande wa utumiaji wa programu za "Microsoft Office " ambazo ni feki na hazina leseni za matumizi ya Idara ya Mhasibu Mkuu imekiri kutokea dosari hii na ofisi wamechukua hatua za kupata leseni na watendaji wao wa Wizara wanaohusika na ununuzi wapo kwenye hatua .

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri kuwa ofisi ya kitengo cha TEHAMA komputa zote za mifumo watumie jalada la pamoja litalotengenezwa ndani ya komputa (sharing folder) au watumie inteneti ili kuepusha komputa isiingie virus.

HOJA NAMBA1.6.12 Dosari za Kiusalama Katika Kituo Kikuu cha Taarifa (Datacenter) Kilichopo Vuga

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali za kiusalama katika Kituo Kikuu cha Kuhifadhia na Kusambaza Taarifa (*Dacenter*) kilichopo katika Idara ya Mhasibu Mkuu – *IFMS* Vuga Mjini.

Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Idara ina Kamera za *CCTV* kwa ajili kusimamia shughuli zinazofanyika katika chumba cha seva. Hata hivyo, ujazo wa vifaa vya kurikodia matukio (*NVR- Hardisk*) ni mdogo ambao ni 8TB ukilinganisha na idadi ya kamera 36 zilizopo katika jengo hilo, hii inamaanisha kwamba vifaa vya kuhifadhia matumio havitakuwa na uwezo mzuri wa kuhifadhi taarifa kwa muda mrefu.
- Mfumo wa uzimaji wa moto ndani ya kituo hicho cha taarifa haufanyi kazi. Hali hii inaweza kusababisha hatari na hasara kubwa endapo ikitokea hitilafu zozote za moto.
- Kukosekana kwa kitabu cha kumbukumbu ambacho kinatumika kwa mahudhurio ya watu wanaoingia katika chumba cha seva.
- Kukosekana kwa mkusanyiko wa seva za mfumo ambazo ziloungwa na kufanya kazi kwa pamoja (*clustering& load balancing*), ili kuweza kupunguza mzigo wa kufanya kazi kwa seva moja na kuondoa tatizo za upole upole (*slowness*) na kuongeza uhakika wa kupata huduma.
- Seva ya uzalishaji inatumia teknolojia ya "*Virtualization – Type 1 Hypervisor*", ambapo toleo lake la mfumo wa uendeshaji (*Operating System*), ni la zamani "*ESXi vCenter Server 5.5*", ambapo toleo hili kwa sasa halipati huduma kamili za kiusalama (*security updates*) kutoka kwa muuzaji wa mfumo huu (*Vendor*).
- Kukosekana kwa ripoti za kufanya "backup" ambapo zitaonesha muda gani backup imeanza na muda gani imemaliza na muhusika alofanya huo mchakato na nani alothibitisha kama backup hiyo ipo kamili na inafanya kazi.
- Kukosekana kwa ripoti zitakazoonesha uwezo wa utendaji kazi wa wafanyakazi wa Kitengo cha *TEHAMA* (*performance repors*) ambazo zitaweza kusaidia kuelewa uwezo wa utendaji wao wa kazi na usimamizi wa mfumo wa *IFMS*.

Dosari za kiusalama zilizotajwa hapo juu kusababisha upotevu wa taarifa za fedha katika mfumo wa *IFMS*.

Ukaguzi unashauri idara kuongeza usalama kwa jumla katika Kituo Kikuu cha Taarifa kwani sehemu hiyo ni muhimu sana na kwa vile taarifa zote za mfumo wa usimamizi wa fedha zimehifadhiwa hapo.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

*(i)* Ofisi imeweka (NVR-Hard Disk) zenye uwezo wa 8TB zinazokidhi mahitaji yaliyokusudiwa kwa kamera 36 zenye kuhifadhi taarifa kwa muda wa mwezi mmoja kutoka siku iliyorikodiwa. Kwa kupitia ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Ofisi imeona ni vyema kuongeza uwezo huo na

sasa iko katika hatua za manunuzi ya kuongeza uwezo wa (NVR- Hard Disk) 24TB yenye uwezo wa kuhifadhi taarifa kwa muda mrefu zaidi.

*(ii)* Ni kweli kumetokea changamoto ya mfumo wa kuzimia moto 'Horse reel system' ambao unakhitilafu inayotakana na uwepo wa bahari karibu inaathiri vifaa vya maadini chuma (Mashine za kusukumia maji). Kutokana nachangamoto hiyo Ofisi imepanga kuuhamisha Mfumo huo kutoka eneo uliopo na kuuweka eneo jengine litakalokuwa salama zaidi. Hata hivyo, Ofisi inatumia mifumo miwili ya ziada ya uzimaji moto ambayo ni 'Automation system', pamoja na 'Cylinder gas and powder system' ambayo inaendelea kufanya kazi

(iii) Ofisi imeweka vitabu maalum vya kumbukumbu kwa watendaji na wageni wote wanaoingia katika Ofisi za IFMIS. Kwa lengo la udhibiti wa uingiaji watu katika vyumba hivyo. Hivyo, haikuona haja ya kuwepo kitabu cha kumbukumbu kwa upande wa Server room pekee. Hata hivyo, ushauri huo wa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali umechukuliwa na tayari umeshafanyiwa kazi.

(iv) Ofisi inatumia Muundo wa Seva moja katika Mfumo wa IFMIS yenye uwezo wa kuhudumia mifumo minne ikiwa ni 'virtualization' ambayo imejikusanya pamoja na kufanya kazi bila ya kuleta upoleupole (Slowness) wa aina yoyote. Hata hivyo Ofisi inafanya jitihada mbali mbali ili kuepusha changamoto hiyo

(v) Nikweli kwamba IFMIS inatumia teknolojia ya 'Hypervisor' vmware (EXSi 5.5) ambayo ina leseni yake kamili ingawa ni ya zamani. Hata hivyo, hatua za kuboresha (upgrading) zilikuwa tayari zilishaanza kufanyika, kutokana na ujio wa mfumo mpya wa BAMAS ifikapo Julai 2022 Wakala wa Serikali Mtandandao (EGAZ) umeishauri Ofisi kutoendelea kufanya maboresho yoyote ya mfumo uliopo. Ingawa suala la kupata msaada iwapo kutatokea changamoto litapatikana kwa muuzaji wa pili kama ilivyo kwenye makubaliano (SLA). Hata hivyo mfumo wetu haujaunganishwa na huduma ya intaneti ya moja kwa moja hivyo haitaweza kupokea 'security updates' hizo, suala hilo hutegemea vifaa vyengine vya usalama.

(vi) Ni kweli hapo awali hakukuwa na utamaduni wa kuhifadhi ripoti zinazohusiana na ufanyikaji wa backup ingawa backup hizo zinafanyika kila siku kwa awamu mbili na zinakuwa na 'log file' ambayo zinaonesha ripoti kamili ya ufanyikaji wake na huwa inafutika na kuweka 'file' mpya kila backup hiyo inapofanyika.Ofisi haikuona haja ya kuweka nyaraka (hard copies) ya backup hizo kutokana na wingi wa kurasa na gharama za kuchapisha kwa siku. Aidha, kuwafuatia ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Ofisi imeona ni vyema kuhifadhi kumbukumbu hizo kila siku kwa njia ya nakala laini (soft copy).

(vii) Ripoti zinazoonesha uwezo wa utendaji kazi wa Wafanyakazi zipo kwa Watendaji wote wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango wakiwemo watendaji wa kitengo cha TEHAMA na zinasimamiwa na Idara ya utumishi na Uendeshaji.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kutokana na majibu pamoja na ufafanuzi ulitolewa na Wizara, Kamati ya PAC imebaini kuwa muda wa mwezi mmoja uliowekewa kwa ajili ya kuhifadhi picha za matukio katika CCTV Camera ni mdogo ukilinganisha na umuhimu wa Ofisi hiyo na majukumu yake.Hivyo basi kamati inashauri kuwa kuongeza muda wa mwezi mmoja kutoka na kwenda angalau miezi miwili.

Aidha, Kamati ya PAC inashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipngo iwafanyie mafunzo ya mara kwa mara wafanyakazi wake wa kitengo cha TEHAMA ili kuwajengea uwezo zaidi ili waweze kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia yaliyopo Duniani .

HOJA NAMBA 1.6.13 Kutokuwepo na Mipangilio Imara ya Kiusalama Katika Vifaa Vya Kuchuja Mawasiliano (*Firewalls*) ya Mtandao.

Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imefunga vifaa maalum (*Sophos Firewall*) kwa ajili ya kuchuja taarifa zinazoingia na kutoka kwenye mtandao wa idara kwa lengo la kudhibiti matumizi ya mtandao na kuepuka uhalifu wa mitandao kutokea katika idara.
Ukaguzi umebaini idara haijaweka sera na mipangilio imara katika vifaa hivyo vya kuchuja mawasiliano ili kuweza kudhibiti matumizi yasiyo salama ya mtandao wa "*internet*".

Matumizi yasiyo salama ya *internet* ni kama vile kuweza kufungua tovuti ambazo haziko salama na zina vihatarishi vikubwa katika kusambaza virusi na kupenya kwa wahalifu wa mitandao. Baadhi ya tovuti hizo zikiwemo tovuti za kupakua, tovuti za kubeti, tovuti za mambo yanayoenda kinyume na maadili, baadhi ya mitandao ya jamii na kadhalika. Kiambatanisho nambari 2(d) kinahusika.

Kutokuweka sera imara za usalama kwenye vifaa vya kuchuja taarifa za mawasiliano, kunaweza kupelekea hatari ya kuingia virusi katika kompyuta na seva zenye mfumo wa *IFMS* kupitia mtandao wa *internet*, na vile vile kuweza kufanyika kwa mashambulizi ya mfumo huo kwa wahalifu wa mitandao.
Ukaguzi unashauri idara iweke sera madhubuti za usalama katika vifaa vyake vya kuchujia mawasiliano, ili kuweza kudhibiti matumizi ya mtandao yasiyosalama na kujilinda dhidi ya uhalifu wa mitandao pamoja na virusi.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Kompyuta zote zinazotumika kwa mfumo IFMIS zimedhibitiwa kutokana na matumizi yasiyo salama ya mtandao. Aidha, watendaji wamepatiwa ruhusa ya kutumia intaneti kwa lengo la kujifunza kwa kompyuta zilizo nje ya mfumo wa IFMIS.
Hata hivyo, kwa upande wa Sera na Mipangilio imara katika vifaa vya kuchuja mawasiliano Iinsimamiwa na Wakala wa Miundombinu na Mawasiliano ya Tehama (ZICTIA) pamoja na Wakala wa Serikali Mtandao (EGAZ). 'Setup and configuration' kwa Taasisi zote zimefanywa na Taasisi hizo ambazo zina mfanano na kutengeneza sera ndani ya kifaa kinachochuja mawasiliano hayo na kuruhusu muunganiko wa mfumo wa IFMIS tu, ingawa bado hawakutoa machapisho na mpangilio huo. Na pale inapotokea kuunda muunganiko wa Taasisi na Taasisi nyengine wataalamu hukaa na kutengeneza mpango wao wa kiusalama kwa pande zote mbili ili kunusuru muingiliano usio rasmi. Kwa sasa, Ofisi inafuata muongozo wake wa Kitehama (ICT guideline) ambao umeeleza kiwango

Fulani uwepo wa uchujaji wa mawasiliano.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kutokana na dosari hii Kamati imebaini kuwa wakala wa Miundominu na Mawasiliano ya Tehama (ZICTIA) pamoja na wakala wa Serikali Mtandao (EGAZ) hawajatoa muuongozo rasmi kwenye Taasisi. Idara ya Mhasibu Mkuu inatengeneza muongozo wenyewe kwa hatua za awali, pia Kamati imebaini kuwa kwa upande wa vifaa vya kuchuja mawasiliano ya mtandao Kamati imeona kuwa control zipo lakini zipo dhaifu zinahitaji kuimarishwa.

Vile vile, wakati Kamati ilipokuwa ikifanya ukaguzi katika komputa zilizounganishwa na Mfumo wa IFMIS ilielezwa kuwa baadhi ya wakati komputa hizo hutumia internet kwa ajili ya kazi maalum kama vile kuingiza antivirus katika komputa hizo. Kamati ya PAC imeridhika na ufafanuzi uliotolewa na Wizara.

Hoja Namba 1.6.14 Kasoro Zilizobainika Katika Sera za Usalama wa Matumizi ya Vifaa vya *TEHAMA* na Mfumo wa *IFMS (ICT Security Policy).*

Sera za Usalama katika matumizi ya vifaa vya *TEHAMA*na mifumo, ni nyaraka ambazo ndani yake zimekusanya miongozo inayoonesha matumizi sahihi ya vifaa vya *TEHAMA* na mifumo, pamoja na sheria za matumizi hayo na adhabu zinazoweza kutolewa kutokana na ukiukwaji wa sheria hizo. Sera hizo zinapoandaliwa zinatakiwa zizingatie vihatarishi vyote ambavyo vinavyoweza kutokea wakati wa utumiaji wa vifaa hivyo, pamoja na mifumo ya *TEHAMA* kwa wafanyakazi.

Aidha, nyaraka hizo zitatakiwa kusainiwa na uongozi kwa ajili ya kupata idhini ya matumizi na zinatakiwa zitolewe nakala, na kupewa wafanyakazi wa idara wanaotumia vifaa hivyo na mifumo ambapo wafanyakazi hao baadae watahitajika kupata mafunzo yenye kuleta ufanisi na weledi, juu ya matumizi sahihi na salama ya vifaa hivyo, pamoja na mifumo na hatimae kuvitunza na kuviweka katika hali ya usalama.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba nyaraka za Sera za Usalama za Idara ya Mhasibu Mkuu, zilizoandaliwa kwa matumizi ya *TEHAMA* zina mapungufu,ikiwani pamoja na kutokufanyiwa mafunzo kwa wafanyakazi, ili kupata uelewa wa matumizi salama ya vifaa vya *TEHAMA* pamoja na mifumo yake.

Kutofanyika kwa mafunzo ya Sera za Usalama wa Matumizi ya Vifaa vya *TEHAMA* kwa wafanyakazi, kunaweza kupelekea kufanyika kwa matumizi mabaya ya vifaa, pamoja na mifumo na baadae kusababisha upotevu na kuleta vihatarishi katika taarifa za ofisi na rasilimali zake.

Ukaguzi unashauri Idara ya Mhasibu Mkuu kuimarisha taarifa zilizomo ndani ya nyaraka za Sera ya Usalama wa Matumizi ya vifaa vya *TEHAMA*, pamoja na mifumo yake na kutoa mafunzo kwa wahusika, ili kuweza kutumika vifaa hivyo kwa uweledi na ufanisi na kupelekea kupunguza hatari za upotevu wa taarifa na uharibifu wa vifaa.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Ofisi haikuwa na Sera ya Tehama (ICT Policy) bali imeitumia Sera ya Idara ya Serikali Mtandao kwa wakati huo na kuitumia kwa kutengenezea Muongozo wa TEHAMA kwa Ofisi hii (ICT Guideline), Na ni kweli mafunzo kwa watendaji wote bado hayakukamilika, lakini tayari yalishafanyika kwa wakuu wote wa divisheni na vitengo kwa awamu hii baada ya muongozo huo kusainiwa rasmi. Hatua za kufanya mafunzo zinaendelea na Ofisi imepanga kuwapatia mafunzo watendaji wote kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kwa kuwa mafunzo ya mfumo wa TEHAMA yametolewa kwa wakuu wa divisheni na vitengo tu, Kamati ya PAC inashauri kuwa mafunzo hayo yatolewe mara kwa mara kwa wafanyakazi wote wanaotumia mfumo huo, ili wapate kuelewa matumizi ya mfumo na kuleta ufanisi katika majukumu yao ya kazi.

Hoja Namba 1.6.15 Kutofanyika kwa Upimaji wa Mazingira Hatarishi na Jaribio la Upenyaji Katika Mtandao *(Vulnerability Assesment and Penetration Testing – VAPT)*.

Utaratibu uliobora unaeleza kwamba Taasisi inatakiwa kufanya zoezi la upimaji wa mazingira hatarishi na jaribio la kupenya kwenye mtandao, ili kupata taarifa. Lengo la kufanya zoezi hilo ni kuweza kuangalia viashiria hatarishi vyote ambavyo vipo au vinavyoweza kutokea katika Mtandao wa Idara, na kuziba maeneo yote yaliyo hatari, ili kuweza kuongeza usalama katika mtandao kwa kudhibiti vyanzo vyote hatarishi.

Aidha, zoezi hilo la upimaji wa mazingira hatarishi pamoja jaribio la kupenya kwenye mtandao wa idara. Kwa kawaida linafanyika angalau mara mbili kwa kila mwaka, ili kuweza kujiridhisha kwamba hali ya mtandao wa Idara ni salama dhidi ya virusi na wahalifu wa mitandao.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu – *IFMS* haijawahi kufanya zoezi hilo la upimaji wa mazingira hatarishi na jaribio la kupenya kwenye mtandao wake, ili kuweza kuona maeneo gani yaliyo na vihatarishi vya kupatikana kwa taarifa.

Hivyo basi, idara haiwezi kujua ni sehemu gani katika mtandao wake na miundombinu yake ya mawasiliano inaweza kuwa dhaifu, na kusababisha vihatarishi na kuweza kudhibiti sehemu hizo.

Kutokufanya zoezi hilo kunaweza kusababisha taarifa za kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Fedha – *IFMS*, kuingiliwa na wahalifu wa mitandao na kuweza kubadilishwa kwa taarifa za fedha za taasisi mbali mbali, na hatimae kupelekea upotevu wa fedha za Serikali pamoja na uharibifu wa taarifa za fedha za Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa idara kufanya zoezi la upimaji wa mazingira hatarishi, na jaribio la kupenya kwenye mtandao wa idara kupitia miundombinu ya idara, ili kuweza kudhibiti maeneo yote hatarishi katika mtandao huo.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

Kutokana na usalama wa Mfumo wenyewe, Ofisi haikujiridhisha kwa wakati huo kufanyiwa upimaji wa viashiria hatarishi kupitia mtu au taasisi binafsi. Hii ni kutokana na changamoto ya kukosa uwezo wa kufanya zoezi hilo kwa taasisi zetu za serikali na si vyema zoezi hili kulipatia taasisi binafsi kwani itakuwa

tumeshaonesha udhaifu ulipo wa mfumo kwao, na mfumo huu ni wa serikali na una taarifa nyingi ambazo ni siri. Hata hivyo uongozi umeona ni vyema kuwaandikia barua Wakala wa serikali Mtandao kwa ushauri zaidi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kujiridhisha na majibu ya Wizara Kamati ya PAC imeikagua barua kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Serikali Mtandao ya tarehe 19 Januari, 20121 kumbukumbu namba DS.180/199/01/04/60 inayohusu Zoezi la "Penetration Test"kwa Mfumo wa Usimamaizi wa Fedha na Bajeti (IFMS). Kwa ujumla Kamati imeridhika na ufafanuzi wa Hoja hii.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kamati ya PAC inashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kufuatilia kwa karibu zaidi suala la Upimaji wa Mazingira Hatarishi na Jaribio la Upenyaji Katika Mtandao *(Vulnerability Assesment and Penetration Testing – VAPTkwa* Wakala wa Serikali Mtandao ili kuweza kuongeza usalama katika mtandao kwa kudhibiti vyanzo vyote hatarishi.
ii. Kwa kuwa taarifa za Mfumo ni siri za Serikali ambazo hazitakiwi kwa mtu wa nje kujua, Kamati ya PAC inashauri Wakala Serikali Mtandao iwajengee uwezo mkubwa zaidi watendaji wa ndani (wa mfumo wa TEHAMA) ili waweze kufanya upimaji wa viahatarishi wenyewe.

Hoja Namba 1.6.16 Kukosekana Kwa Nyaraka za Haki za Watumiaji wa Mfumo wa *IFMS*.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu imeunganisha watumiaji mbali mbali wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha-IFMS, lakini Idara haina nyaraka ambazo zinaonesha mipaka ya haki za watumiaji hao wa Mfum wa IFMS. Aidha, ukaguzi umebaini kwamba hakuna mapitio yoyote ya mara kwa mara ya kuchunguza mipaka ya haki za watumiaji wa mfumo huo.

Ukaguzi ulipata taarifa kutoka kwa Msimamizi wa Mfumo wa IFMS kwamba uhakiki wa mwisho uliofanyika kuangalia watumiaji wa mifumo, ulifanyika mwezi wa Disemba 2020, lakini hakuna nyaraka rasmi zozote zilizotengenezwa kuhusiana na uhakiki huo.

Kukosekana kwa nyaraka za uhakiki wa haki za watumiaji wa Mfumo wa *IFMS* na kutofanya uhakiki wa mara kwa mara wa haki za watumiaji wa Mfumo wa *IFMS*, kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya mfumo na hatimae kupelekea upotevu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unashauri kwamba idara iandae nyaraka za haki za watumiaji wa mifumo na kuzipitia nyaraka hizo mara kwa mara, ili kudhibiti utumiaji mbaya wa mfumo wa IFMS.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

(i) Nyaraka zinazoonesha haki za watumiaji wa mfumo wa IFMIS ziliombwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa **barua nambari AUD/WN/AR/FM/2/VOL.1/19 ya tarehe 19 Julai, 2021** ikiwa kama maombi ya taarifa za ziada na ziliwasilishwa kwa njia ya email ya tarehe 5 Agosti 2021.

(ii) Aidha, ushauri wa ukaguzi umepokelewa na tayari uhakiki umeanza kufanyiwa kazi. Hata hivyo, kazi hii ni endelevu na uhakiki unaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, kwa upande wa mapitio ya kuchunguza mipaka ya watumiaji wa mfumo na upatikanaji wa nyaraka changamoto hii ilikuwepo. Hatua zimechukuliwa kwa kuanzisha utaratibu wa kuwafanyia uhakiki watumiaji waliokuwa hawaingii katika mfumo kuanzia siku 20 kwa kuzuiwa "inactive" na nyaraka za watumiaji hao huhifadhiwa. Endapo watahitaji kuingia katika mfumo wanalazimika kuandika barua kuomba ruhusa ya kutumia mfumo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa vielelezo havikupatikana kwa ukaguzi wa mwanzo uliofanyika mwezi wa Febuari, 2021 vielelezo vilitolewa katika ukaguzi wa mara ya pili uliofanyika mwezi wa Agosti, 2021.ingawa watendaji wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango walieleza kuwa vielelezo hivyo havikutakiwa na Mkaguzi.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Watumiaji wa Mfumo wa IFMS kutoka Wizara, Idara na Taasisi nyengine za Serikali wakati wanapokwenda likizo, Wizara na Taasisi zao zijuilishwe kuwasilisha barua Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ili watumiaji hao wa Mfumo kutoka Wizara na Taasisi nyengine waweze kuwekwa katika "Inactive Status"

HOJA NAMBA 1.6.17 Kukosekana Kwa Mpango Mkakati wa TEHAMA

Ukaguzi umebaini kwamba, Idara ya Mhasibu Mkuu –*IFMS* haijaandaa mpango mkakati wa*TEHAMA*, ambao ungeweza kusaidia idara kufanikisha malengo yake kwa ufanisi zaidi kupitia *TEHAMA*.

Kutokuwepo kwa Mpango Mkakati wa *TEHAMA* katika idara kunaweza kusababisha malengo ya *TEHAMA* kutokwenda sambamba na malengo ya idara na kufanyika maamuzi ya *TEHAMA* yasiyokuwa na tija ambayo yanaweza kupelekea kupungua kwa kasi ya maendeleo ya utoaji wa huduma ya Mfumo wa *IFMS* kwa idara na hatimae kusababisha upotevu wa taarifa za fedha.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Idara ya Mhasibu Mkuu kuandaa Mpango Mkakati, ili kufanya malengo yake yaende sambamba na malengo ya idara na kupelekea kupatikana kwa huduma bora ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Ofisi inakubaliana na Ushauri huo. Hata hivyo, Ofisi iko katika hatua za kukamilisha mapitio ya Mpango Mkakati wake kwa mwaka 2022 – 2025 Mpango mkakati ambao umehusisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa Tehama ndani ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Baada ya ya mahojiani na Uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha, na Mipango Kamati imeelezwa kuwa ingawa Wizara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha rasimu ya Mpango Mkakati wa Wizara wa miaka mitano, hata hivyo, kwa upande wa Mpango Mkakati wa TEHAMA, Wizara ipo katika hatua ya kutafuta mtaalam wa kuandaa Mapngo Mkakati huo wa TEHAMA

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaisisitiza Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuharakisha hatua za kumpata mtaalam wa Mpango Mkakati wa TEHAMA ambao utasaidia katika masuala mablimbali yakiwemo ya kufanya maamuzi ya *TEHAMA* yenye tija ambayo yanaweza kupelekea kuongeza kasi ya maendeleo ya utoaji wa huduma ya Mfumo wa *TEHAMA* kwa Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na hatimae kuepusha upotevu wa taarifa za fedha.

Hoja Namba 1.6.18 Kukosekana Kwa Kamati Tendaji ya Mifumo ya *TEHAMA*

Utaratibu uliobora (*Best Practise*) unaeleza kwamba Mkuu wa Idara atapaswa kuunda Kamati Tendaji, ambayo itakuwa na lengo la kushughulikia masuala yote ya maendeleo ya utendaji wa *TEHAMA*, maendeleo ya utoaji wa huduma za *TEHAMA* na maamuzi yake katika idara, pamoja na kuhakikisha sera na mikakati yote ya *TEHAMA* katika idara inasimamiwa na kutekelezwa kwa ufanisi na kwa wakati. Aidha, wajumbe wa kamati hiyo wanatakiwa kupewa Hadidu Rejea na kutengeneza Hati za uendeshaji wa vikao vya *TEHAMA*.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu- *IFMS*, haina Kamati Tendaji ya *TEHAMA*, ili kuweza kusaidia utekelezaji wa malengo na mikakati ya *TEHAMA* katika idara.

Kukosekana kwa Kamati Tendaji ya *TEHAMA* katika Idara ya Mhasibu Mkuu, kunaweza kusababisha mipango ya *TEHAMA* kutotekelezwa ipasavyo na kupelekea kutofanikisha malengo kwa ufanisi katika idara.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Idara kuunda Kamati Tendaji ya *TEHAMA*, ili kuandaa mipango mizuri ambayo italeta maendeleo katika utoaji wa huduma za *TEHAMA* na kupelekea kufanyika kwa maamuzi yenye tija katika idara.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango
Muundo wa Utumishi unatuelekeza tuwe na Kamati mbili nazo ni Kamati tendaji na Kamati ya uongozi. Hivyo, masuala ya Tehama huzungumzwa kupitia kamati hizo na kutolewa maamuzi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa masuala yote ya Wizara yakiwemo ya TEHAMA huchukuliwa kama masuala ya Wizara na hupitia katika taratibu za kawaida za Wizara zikiwemo za vikao na nyenginezo. Katika Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali huwa inafanya kikao kila wiki ambapo mtendaji kutoka kitengo cha ICT anakuwemo na anawasilisha masuala yake ya ICT na kujadiliwa kabla ya kuwasilishwa katika vikao vya juu vya Wizara.

Aidha, Kamati imebaini kuwa kwa mujibi wa miongozo ya Jumuiya ya Ukaguzi ya Kimataifa (INTOSAI) na Jumuiya ya Ukaguzi ya Afrika (AFROSAI), inatakiwa iwe na Kamati Tendaji ya TEHAMA. Hata hivyo, Wakala wa Serikali Mtandao (EGAZ) bado hawajatoa muongozo kuhusiana na kuundwa kwa Kamati Tendaji ya TEHAMA katika Wizara na Taasisis za Serikali.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kukaa pamoja na Wizara yenye dhamana na Utumishi wa Umma, Wakala wa Serikali Mtandao (EGAZ) pamoja Wakala wa Miundominu na Mawasiliano ya Tehama (ZICTIA) ili kujadiliana juu ya utaratibu unaoweza kutumika katika kuanzisha Kamati Tendaji ya Tehama

Hoja Namba 1.6.19 Kukosekana Kwa Mafunzo ya Usalama wa Mfumo wa *IFMS* Kwa Wafanyakazi Wanaosimamia Mfumo wa *IFMS* Katika Idara ya Mhasibu Mkuu.

Ukaguzi umebaini kwamba wafanyakazi wa Idara ya Mhasibu Mkuu wanaosimamia Mfumo wa Usimamizi wa Fedha (*Technical Support & Application*) kwa muda mrefu hawajapatiwa mafunzo maalum ya Usalama wa Mfumo Usimamizi wa Fedha (*IFMSSecurity Awareness Training Program*). Aidha, ukaguzi umebaini mara ya mwisho kupata mafunzo ya usalama kwa wafanyakazi hao ni mwaka 2018, ambapo hadi sasa kuna mabadiliko mengi yamefanyika katika mfumo, lakini hakuna mafunzo kamili yaliyofanyika kuhusiana na mabadiliko hayo.

Kukosekana kwa mafunzo ya mara kwa mara ya usalama, Usimamizi na Uendeshaji wa Mfumo wa *IFMS*, kunaweza kusababisha kukosekana kwa usimamizi mzuri wa utumiaji wa mfumo na hatimae idara kuingia gharama za uendeshaji wa mfumo zisizo na ulazima.

Ukaguzi unashauri idara kuwafanyia mafunzo ya mara kwa mara ya usalama wa mfumo kwa wafanyakazi wa Kitengo cha *IFMS*, ili kuweza kusimamia vizuri na kupata taaluma ya kisasa kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya sayansi na teknolojia. Aidha, mafunzo hayo yataweza kuondosha gharama za kumwita Mshauri Elekezi mara kwa mara kuja kutatua changamoto zitakazojitokeza katika mfumo.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Ushauri umepokelewa. Ofisi imejipanga kufanya mafunzo ya mifumo mipya kupitia bajeti ijayo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Uchunguzi wa PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa kweli wafanyakazi wanaosimamaia mfumo wa usimamizi wa fedha kwa muda mrefu hawajapatiwa mafunzo, ingawa Ofisi imejipanga kufanya mafunzo ya mifumo mipya kupitia bajeti ijayo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kwa kuwa Ofisi ya Rais Fedha imejipanga kuanzisha mifumo mipya ukiwemo wa Bajeti na Matumzo (BAMAS), Kamati ya PAC inashauri kuwa Idara ya Mhasibu Mkuu ijipange vizuri ili iweze kuwafanyia wafanyakazi wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha mafunzo ya usalama, Usimamizi na Uendeshaji wa Mfumo na kupata usimamizi na utumiaji ulio bora wa mifumo hiyo.

ii. Wakala wa Serikali Mtandao (EGAZ) ifanye jitihada za kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara watendaji wengine Wizara na Taasisi za Serikali wanaohusika na masuala ya fedha badala ya kuwapatia mafunzo hayo watendaji wa Mfumo wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango peke yao.

Hoja Namba 1.6.20 Kukosekana Kwa Hati ya Muongozo wa Mtumiaji wa Mfumo wa IFMS (Lack of Updated User Manual Document-IFMS)

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu imeingia mkataba na Kampuni ya Mshauri Elekezi ya *Soft Tech(Soft Tech Consultancy Ltd)*, kwa ajili ya utengenezwaji wa Mfumo wa *IFMS*, ambao unatumika kwa ajili ya kusimamia taarifa za matumizi ya fedha kwa Serikali.

Mfumo huo wa IFMS ulianza rasmi kufanyakazi mwezi Julai 2015, ambapo hati ya muongozo wa matumizi *(User Manual Version 1*) wa 09/04/2015 uliotolewa, na baadae mfumo huo kufanyiwa marekebisho mwezi wa Machi 2018.

Hata hivyo, ukaguzi haukuweza kupata kwa hati ya sasa ya Muongozo wa Mtumiaji wa Mfumo wa IFMS, iliyotolewa rasmi kwa ajili ya toleo jipya lililofanyiwa marekebisho la Mfumo wa Usimamizi wa Fedha-IFMS.

Kukosekana kwa muongozo wa sasa wa Mtumiaji wa Mfumo wa IFMS, kunaweza kusababisha watumiaji wa mifumo kutotumia vizuri mifumo hiyo na kupelekea kupotea taarifa.

Ukaguzi unashauri kwamba idara iongeze jitihada za uwekaji wa muongozo mpya wa Mtumiaji wa Mfumo wa IFMS (IFMS Current User Manuals Document), kutoka kwa Mshauri Elekezi, ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi na kwa usalama kwenye mfumo huo.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

Hakuna Muongozo wa Toleo jipya la marekebisho ya Mfumo wa March 2018, kwa sababu marekebisho hayo hayakubadilisha taratibu zozote za utumiaji (functionalities). Hivyo, hakukuhitajika "user manual" nyengine bali maboresho yaliyofanyika kwa mwaka 2018 ni kuondoa "slowness" na kuongeza utendaji kazi wa mfumo (Perfomance). Kwa sasa, muongozo unaotumika ni ule wa mwaka 2015

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kwa ujumala kamati ya PAC imekubaliana na majibu ya Wizara na hakukua na maelezo zaidi juu ya Hoja hii.

Hoja Namba 1.6.21 Kukosekana kwa msaada wa kiufundi kwa watumiaji wa mfumo wa IFIMIS walipo

kwenye Wizara, Idara na mawakala( MDAs)

Moja ya majukumu ya wafanyakazi wa Kitengo cha IFMS, ni kutoa msaada wa kiufundi kwa watumiaji wa mfumo ambao wapo ndani ya Idara ya Mhasibu Mkuu na watumiaji wa mfumo ambao wanaotumia wakiwa katika wizara, Idafa na Wakala.

Ukaguzi umebaini kwamba wafanyakazi wa Kitengo cha Utoaji wa Msaada wa Kiufundi (*Technical Support Unit)* hawatoi ushirikiano mzuri wa msaada wa kiufundi kwa watumiaji wa mfumo ambao wapo katika Mawizara, Idara nyengine na Mashirika.

Kutotoa ushirikiano mzuri wa msaada wa kiufundi kwa watumiaji wa mfumo walioko katika Mawizara, Taasisi na Mashirika mengine kunaweza kusababisha watumiaji wote walioko kwenye Mawizara na Taasisi kufuata huduma hiyo katika Idara ya Mhasibu Mkuu, na hatimae kupelekea ucheleweshwaji wa malipo ya fedha katika Serikali.

Ukaguzi unashauri kwamba Uongozi wa Idara ya Mhasibu Mkuu kuandaa mpango mzuri wa kuwapa msaada wa kiufundi watumiaji ambao wapo nje ya idara.

MAJIBU YA WIZARA

Kitengo cha utoaji wa msaada wa kiufundi(Technical support unit) kinatoa msaada wa kiufundi kwa watumiaji wote kila unapohitajika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuna changamoto nyingi katika watumiaji wa mfumo wa IFIMIS waliopo kwenye Wizara na Taasisi za Serikali ni kama zifuatazo :-

- Kwa upande wa Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Kamati imebaini wapo wafanyakazi wachache wa sehemu Ufundi wa Mfumo wapatao watano tu ambao hutoa huduma za kiufundi za mfumo wa IFMS kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali.
- Aidha, imebainika kuwa Wahasibu wa Mawizara na Taasisi za Serikali huwa hawatoi taarifa kwa Kitengo cha Ufundi wa Mfumo pindipo wanapopata matatizo ya mfumo.kwenye maeneo yao ya kazi.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaishauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ishirikiane na Wizara yenye dhamana na Utumishi wa Umma katika kulishughulikia suala la kuongeza wafanyakazi wa kutosha wenye fani ya ufundi wa mifumo ili kutoa huduma iliyo bora katika Wizara na Taasisi za Serikali.

Hoja Namba 1.6.22 kukosekana kwa hati ya Muongozo wa Mpangilio wa Usalama wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA iliyopo katika kitengo cha IFIMIS

Ukaguzi umeangalia kwa kina mipangilio ya kiusalama ya mfumo wa IFMS, programu pamoja na kompyuta

ambazo zimeunganishwa na mfumo huo kwa kiasi gani, taarifa zinalindwa na kubaini kasoro za kiusalama katika maeneo yafuatayo:-

a) Kukosekana Kwa Hati za Mipangilio ya Usalama

Ukaguzi umebaini Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali haikuandaa nyaraka/ hati ambazo zinaonesha mipangilio ya usalama wa mfum pamoja na vifaa vyote vinavyotumika katika mazingira ya mfumo.

Mpangilio wa usalama wa mifumo ni sera au nyaraka ambazo zimetengenezwa na zimehakikiwa na uongozi, na zinaeleza kwa uwazi jinsi ya kuweka mipangilio iliyobora katika kuimarisha usalama wa taarifa katika mifumo na vifaa vyote vinavyotumika katika idara hiyo.

Kutokuwepo mipangilio ya usalama wa taarifa katika mifumo kunaweza kusababisha ongezekola hatari, kwa taarifa zilizomo ndani ya mfumo.

Ukaguzi unashauri idara iandae nyaraka/ sera ambayo itaonesha mpangilio mzima wa usalama wa Mfumo wa IFMS na vifaa/kompyuta zote ambazo zimeunganishwa na mfumo huo.

b) Kukosekana Kwa Utaratibu wa Kupitia Mipangilio ya Usalama wa Taifa

Utaratibu uliobora *(Best Practise)* unaeleza kwamba, Taasisi inahitaji kufanya mpitio ya mara kwa mara katika mipangilio yake yote ya kiusalama katika seva na kanzidata zake, ili kuweza kupata uhakika wa usalama wa taarifa hizo dhidi ya wahalifu wa mitandao au wasaliti kutoka ndani ya Taasisi.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali haijaweka utaratibu wa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mipangilio ya usalama katika seva, pamoja na kanzidata (*database*), pamoja na miundombinu ya mawasiliano katika kitengo chake cha IFMS, hali inayopelekea kushindwa kutambua iwapo kama seva, kanzidata na miundombinu yake ipo salama.

Kutokuweka utaratibu wa mapitio ya mpangilio wa kiusalama wa taarifa pamoja na vifaa, unaweza kusababisha hatari ya uvujaji na upotevu wa taarifa.

Ukaguzi unashauri Idara ya Mhasibu Mkuu kuanzisha na kufanya mapitio (kukagua) ya mara kwa mara mipangilio yake ya usalama wa mifumo na vifaa vya mtandao vilivyounganishwa na mfumo huo, ili kuweza kuongeza usalama wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha na taarifa zake.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

*(i)* Ofisi imeandaa mpango wa kiusalama kupitia muongozo wake wa ICT Guideline ambao umeeleza jinsi ya kujikita masuala mazima ya kiusalama kwa upande wa Miundmbinu ingawa mpango huo umeonekana kuwa na mapungufu na kuhitaji kufanyiwa maboresho zaidi kulingana na mabadiliko ya kiteknolojia.

*(ii)* Mapitio hayo huwa yanafanyika kwa vifaa vilivyounganishwa ndani ya Ofisi tu kama moja ya

majukumu ya watendaji na hutoa taarifa za maandishi kwa uongozi pale itakapobainika kwa kifaa kuharibika au kutofanyakazi ipasavyo. Hatua za kutoa ripoti za kila siku ya mapitio ya vifaa ingeweza kusababisha matumizi makubwa na uchapishaji.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa "security settings"zikiwemo "Passwords" zinatakiwa zihifadhiwe sehemu maalum na kuwe na mtendaji wa kuzisimiamia. Aidha, Kamati imebaini kuwa makabidhiano ya "Password" kwa maandishi yamefanywa mwaka 2007 na 2014 na baada ya hapo hakujafanyika makabidhiano mengine .Na viongozi wa Wizara waliopo hivi sasa (Mhasibu Mkuu wa Serikali na Naibu Mhasibu Mkuu wa Serikali) walieleza kuwa hawakumbuki bahasha yenye "Passwords" ilipo. Idara ya Muhasibu Mkuu wamekiri kuwepo kwa jambo hilo na imeahidi kulifanyia kazi

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri uongozi wa Idara ya Mhasibu Mkuu ushughulikie kwa haraka Utaratibu wa Kupitia Mipangilio ya Usalama na Vifaa yakiwemo masuala yanayohusiana na Passwords ili kuepusha hatari ya uvujaji na upotevu wa taarifa

Hoja Namba 1.6.23 Kukosekana kwa Usimamizi wa Matukio ya Usalama

Kukosekana Kwa Usimamizi wa Matukio ya Usalama

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu-IFMS haina utaratibu na mpango mzuri wa kuonesha jinsi ya kuripoti, kuchunguza na kutatua matukio ya usalama. Hali hii imesababishwa na kukosekana kwa nyaraka/muongozo rasmi ambao utaonesha utaratibu mzima utakaotumika kusimamia matukio ya usalama.

Kutokuwa na usimamizi mzuri wa matukio ya kiusalama kunaweza kupelekea uvujaji au ubadilishwaji wa taarifa za fedha katika Mfumo wa IFMS na hupelekea upotevu na matumizi mabaya ya fedha.

Ukaguzi unashauri Idara ya Mhasibu Mkuu kuanzisha utaratibu maalum wa usimamizi wa usalama na kuthibitishwa na uongozi wa Idara, ili kuongeza usalama wa taarifa zilizomo ndani ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha *(IFMS)*

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Ofisi imeandaa mpango wa kiusalama kupitia muongozo wake wa ICT Guideline ambao umeeleza jinsi ya kujikita masuala mazima ya kiusalama kwa upande wa Miundmbinu ingawa mpango huo umeonekana kuwa na mapungufu na kuhitaji kufanyiwa maboresho zaidi kulingana na mabadiliko ya kiteknolojia.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa miongoni mwa kasoro za mpango wa kiusalama wa mfumo wa Wizara ni

kuwa hauoneshi utaratibu wa namna ya kufanya endapo itakapotokea hatari katika Mfumo kwa mfano iwapo mtu akifanya uhalifu katika Mfumo.

MAapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuufanyia mapitio mpango wa kiusalama kupitia muongozo wake wa ICT Security Guideline ili iweze kubaini kasoro nyengine zaidi  za kiusalama kwa lengo la kuepusha uvujaji au ubadilishwaji wa taarifa za fedha katika Mfumo ambao unaweza kupelekea upotevu na matumizi mabaya ya fedha.

Hoja Namba 1.6.24 Kukosekana kwa daftari la kumbukumbu za utendajikazi kwa muuzaji wa mfumo wa IFIMS

Usimamizi wa Utendaji Kazi wa muuzaji wa mifumo unajumuisha ufuatiilaji na uaminifu wake katika kufanyakazi, pamoja na kutoa huduma bora kwa mteja wake, ambapo muuzaji anatakiwa kutoa huduma hizo kwa usahihi na kwa wakati.

Aidha, Taasisi za Umma zinapaswa kutunza kumbukumbu za utendaji wa kazi za muuzaji, ili kuweza kusaidia kufanya maamuzi sahihi ya kuendelea naye wakati mkataba wake unapoisha wa utendaji kazi.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu yaani IFMS haijatayarisha daftari la kuweka kumbukumbu za utendaji kazi wa muuzaji wa Mfumo wa IFMS, ili kuweza kuwa na kumbukumbu za utendaji kazi.

Kutokuweka kumbukumbu za utendaji wa kazi wa muuzaji wa huduma, (Mfumo wa IFMS), kunaweza kufanya maamuzi yasiyo sahihi kwa kumuongezea mkataba muuzaji ambaye utendaji wake ni dhaifu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Idara kuanzisha daftari maalum la kuweka kumbukumbu za utendaji kazi wa muuzaji wa Mfumo wa IFMS, ili kuweza kupima utendaji kazi wake na kufanya maamuzi sahihi endapo mkataba wake utakapomaliza.

Majibu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

Kipindi cha ukaguzi hakukuwa na daftari la kumbukumbu la utendaji kazi kwa muuzaji wa mfumo. Kasoro hii imerekebishwa kwa kuweka kumbukumbu za utendaji kazi wa Muuzaji wa Mfumo wa IFMIS

Uchunguzi wa Kamati PAC

Kamati imelikagua daftari hilo la kumbukumbu la utendaji kazi kwa muuzaji wa mfumo na kuridhika nalo.

SEHEMU YA TANO

UCHUNGUZI WA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC)

JUU YA RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

KWA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO (CDF)

KUANZIIA MWAKA 2016 HADI 2018

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KWA MKOA WA MJINI MAGHARIBI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017

### Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Mjini

| Nam | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha Zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Amani | 20,000,000 | Utengenezaji njia hatua ya kifusi | Amani | 20,000,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Utengenezaji njia hatua ya kifusi | Kilima hewa bondeni | | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Amani

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Amani imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zilitumika katika utekelezaji wa miradi miwili kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imeelezwa kuwa kutokana na jitihada za aliyeuwa Mwenyekiti wa Kmati ya Mfuko wa Jimbo hilo miradi hiyo iligharimu jumla ya shilingi 63,000,000m ingawa kwa mujibu wa stakabdhi zilizokaguliwa na Kamati zilionesh matumizi ya shilingi 23,000,000.

Aidha, ilibainika kuwa poshi ya Vikao kwa Wajumbe wa Kamati ya Mfuko ilikuwa inalipwa na Mwenyekiti wa Kmati hiyo.

Kamati pia imebaini kuwa Katibu wa Kamati ya Mfuko huo wa Maendeleo ya Jimbo hatokani na Baraza la Manispaa Mjini kama inavoelekeza Sheria ya Mfuko wa Jimbo Namba 4 ya mwaka 2012. Vile vile Kamati ioibainini kuwa utiaji wa kifusi ulihusisha maeneo mbalimbali yakiwemo ya Amani Fresh, Makawa, Matopeni hadi Ziwatuwe.

Kamati ya PAC ilkagua nyaraka mbalimbali za utekelezaji pamoja na matumiz ya miradi hiyo pamoja na maeneo ya barabara zilizotiwa kifusi ambapo kwa ujumla Kamati imeridhika na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Chumbuni | 20,000,000 | Usambazaji wa Maji | Chumbuni | 20,000,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | | Karakana | | |
| | | | | Banko | | |
| | | | | Masumbani | | |
| | | | | Muembe makumbi | | |
| | | | | Maruhubi | | |
| | | | | Kilimahewa juu | | |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chumbuni

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chumbuni imekiri kupikea jumla ya shilingi 20,000,000 kutoka Serikalini ambzo zimetumika katika kutekelza mradi wa usambazaji maji katika maeneo mbali mbali ya jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kmati ya PAC imebaini kuwa mradi waKilimahewa juu haukuhusika na Jimbo l;a Chumbuni. Aidha, Shehia ya Shukurana kwa hivi sasa imo katika Shehia ya Karakana.

Aidha, Kamati pia imebaini kuwa Katibu wa Kamati ya Mfuko huo wa Maendeleo ya Jimbo hatokani na Baraza la Manispaa Mjini kama inavoelekeza Sheria ya Mfuko wa Jimbo Namba 4 ya mwaka 2012.

Kamati ilikagua nyaraka mbalimbali za mradi zikiwemo fomu za mradi pamoja na nyaraka za matumiz ya mrdai huo. Aidha, Kamati ilipata nafasi ya kukagua Shehia ya MwembeMakumbi ikiwa ni moja ya Shehia iliyosambaziwa maji hayo. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa mradi pamoja na matumizi ya fedha za mradi huo, licha ya dosari ya Katibu wa Kamati ya Mfuko kutototokana na Baraza la Manispaa Mjini.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | Jang'ombe | 20,000,000 | Uwekaji wa Umeme katika Mnara wa Kisima | Jang`ombe | 206,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Usambazaji wa mipira na Ununuzi wa mashine ya maji | Jang`ombe | 1,600,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Uchimbaji wa kisima na ujenzi wa mnara | Jang`ombe | 7,954,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Uungaji wa umeme katika mnara wa maji Bomani | Kwalinatu | 1,055,526 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Mnara wa Maji | Urusi | 2,000,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Uchimbaji wa | | 7,954,000 | Mradi |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>kisima na ujenzi wa mnara</td><td></td><td></td><td>Umekamilika</td></tr>
<tr><td colspan="7">Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Jang'ombe<br><br>Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Jang'ombe ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 kutoka Serikialini ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mbali mbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti<br><br>Uchunguzi wa Kamati ya PAC<br><br>Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-<br>i. Uwekaji usoridhisha wa kumbukumbu za miradi ambapo ilibainika kukosekana kwa vielelezo halisi (Original documents). Kamati ya Mfuko wa Jimbo ilieleza kuwa waliwasilisha vielelezo halisi kwa Ofisi ya Uratib wa miradi iliyopo kwa Ofisi ya Makmo wa Pili wa Rais. Hata hivyo, Watendaji wa Ofisi ya Uratib wa Miradi hiyo katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais nao walieleza kuwa hawakuwa nazo.<br><br>ii. Kutokutiwa saini kwa kumbukumba za vikao vya Kamati ya Mfuko wa Jimbo.<br><br>iii. Kitengo cha ufuatiliaji wa miradi ya Jimbo katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kushindwa kufuatilia ya Majimbo kila baada ya miezi mitatu kama inavyotakiwa kutokana na uhaba wa fedha.<br><br>iv. Katika ziara ya kutembelea miradi ya usambazaji wa maji katika Shehia za Jang'ombe na Urusi Kamati ya PAC imeridhika na hali ya upatikanaji wa maji katika Jimbo hilo kutokana na miradi hiyo pamoja na utataratibu uliowekwa na wananchi wa kuchangia shilingi 5,000,000 kwa mwezi. Aidha, ilielezwa kuwa miradi hiyo imefanikiwa kwa ushirikiano mkubwa pia na Mbunge wa Jimbo hilo kwa wakati huo.<br><br>Mapendekezo ya Kamati ya PAC<br><br>Serikali iangalie kwa uzito unaostahili suala la kukiimarisha na kukiwezesha kitengo kinachofuatilia miradi katika Ofasi ya Makamo wa Pili wa Rais ili kiweze kufanya kazi zake kama inavyotakiwa hasa ikizingatiwa kuwa miradi inayohitaji kuzimamaiwa na kufuatiliwa ni mingi na imegharimu fedha nyingi za Serikali.</td></tr>
<tr><td>4.</td><td>Kikwajuni</td><td>20,000,000</td><td>Mchango wa Bima ya Afya kwa wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kushirikiana na Mbunge</td><td>Jimbo zima</td><td>3,000,000</td><td>Mradi Umekamilik a</td></tr>
</table>

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ujenzi wa Choo Rahaleo (P.Toilet) | Rahaleo | 7,500,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Ngazi njia ya kikwajuni | Kikwajuni | 800,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Mchango wa ununuzi wa gari ya kikundi cha usafi cha Jimbo | Jimbo zima | 1,500,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Vifaa vya maji pump 2 pamoja na mipira 4 | Rahaleo<br>Mwembe Madema | 800,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Utiaji wa kifusi barabara ya Hospitali ya Rahaleo pamoja na Jumba No. 4 | Rahaleo | 1,400,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Mchango wa mfuko wa elimu wa Jimbo | Jimbo zima | 2,000,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Mchango wa ukarabati wa Skuli ya Chekeche Jang'ombe Polisi. | Mwembe Madema | 500,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Mchango wa Maendeleo ya Michezo kwa vijana Jimboni kwa ushirikiano na Mbunge pamoja ujenzi wa Club ya Miembeni. | Jimbo zima | 2,500,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kikwajuni

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kikwajuni ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 kutoka Serikialini ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mbali mbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa aliyekuwa Katibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hilo amefariki. Hata hivyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hilo alifanya jitihada za kupatikana kwa vielelezo mbalimbali vinavyohusika na utekelezaji wa miradi katika Jimbo hilo ambavyo vilikaguliwa na kuridhiwa.

Katika ukaguzi wa baahi ya miradi iliyotekelezwa Kamati ilipata nafasi ya kukagua ngazi iliyojengwa katika njia ya Kikwajuni na Choo (Public Toilet) kilichojengwa Rahaleo.

Katika ukagazi wa miradi hiyo, Kamati ya PAC haikuridhika na mradi wa ujenzi wa choo uliogharimu shilingi 7,500,000 kwa kuwa uetekelezaji wa mradi huo haukuzingatia thamani halisi ya fedha (Value for Money)

Mapendekezo ya Kamati

Viongozi wa Kamati za Mfuko wa Jimbo weaw karibu zaidi na watendaji wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wanaohusika na Miradi ili wapate ufahamu wa kina wa tataribu za miradi pamoja na kupata maelekezo mbalimbali yanayohusu utekelezaji ulio bora wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5. | Kwahani | 20,000,000 | Uchimbaji wa Kisima, Ujenzi wa Mnara (hadi kozi nane), Ununuzi wa mashine na ununuzi wa paipu kwa Kwaalimsha Bondeni. | Kwaalimsha | 18,000,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Uchimbaji wa Kisima, Ujenzi wa Mnara (hadi kozi nane), Ununuzi wa mashie na ununuzi wa paipu kwa Kwaalimsha Juu. | Kwaalimsha | | |
| | | | Ununuzi wa mashine na mipira ya maji | Sebleni | | |
| | | | Usafishaji wa Mtaro wa Maji | Kwahani | 900,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kwahani

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kwahani ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 Uchunguzi wa Kamati ya PAC ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:

1. Uwekaji mbaya wa nyaraka mbalimbali zinazohusu utekelezaji na matumizi ya miradi ya Mfuko wa Jimbo. Hali hiyo imepelekea kukosekana kwa baadhi ya nyaraka wakati wa Kikao cha Kamati ya PAC zikiwemo stakabadhi halisi (original) za miradi ukiwemo mradi wwa usafishaji wa mtaro, stakabadhi za Poling Pipe pamoja na Fomu ya Miradi ya Jadweli la Kwanza. Hadi Ripoti hii inaandaliwa nyaraka hizo zilikuwa bado hazijawasilishwa katika Kamati ya PAC.

2. Kuchelewa kufuatilia stakabadhi (risit) madukani ambapo baadhi ya stakabadhi zilizoonekena na Kamati ya PAC zilikuwa ni za mwaka 2018 wakati miradi hiyo ilitekelezwa mwaka 2016/2017.

3. Kukoeskana kwa umakini katika uandaaji wa ripoti mbalimbali kumepelekea kumbukumbu za vikao kutoainishwa tarehe zilizofanyika vikao hivyo vya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

4. Kukosekana kwa ushirikiano baina ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo hilo na Baraza la Manispaa Mjini.

5. Mradi wa Usafishaji Mtaro umeainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti kutumia shilingi 900,000 wakati katika Fomu za utekelezaji wa miradi zilizowasilishwa kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais zinaonesha kuwa Mradi huo ulitumia shilingi 1,000,000.

Kamati hikurdhishwa na uwekaji mbaya wa kumbukumbu za miradi iliyotekelezwa katikaJimbo hilo kwa mwaka 2016/2017.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kamati za Mfuko wa Jimbo zitekeleza miradi ya Jimbo kama Sheria ya Mfuko wa jimbo inavyoelekeza ikiwa ni pamoja na kutekeleza miradi inayokubalika kisheria na kushirikiana na Mabaraza ya Mji na Halmashauri ambako ndiko anapopatikana Katibu wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo kisheria.

ii. Kamati za Mfuko wa Jimbo zihakikishe kuwa kumbuiumbu za utekelezaji na za matumizi ya miradi ya Mfuko wa Jimbo zinapatikana kikamilifu wakati wote ambao Vyobo vya ukaguzi vinapofanya kazi zake

iii. Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo zitoe ushirikiano wa kutosha kwa Wakaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti kwa kutoa maelezo na vielelezo kikamilifu wakati wa ukaguzi.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 6. | Magomeni | 20,000,000 | Uchmbaji wa Kisima | Magomeni | 8,444,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Uwezeshaji wa wananchi kiuchumu - Vikundi 23 | Shehia zote | 5,998,000 | Mradi Umekamilik a |
| | | | Mafunzo ya Ufundi kwa Vijana 25 | Shehia zote | 5,000,000 | Mradi Umekamilik a |

Majibu ya Kmati ya Mfuko wa Jimbo la Magomeni

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Magomeni ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ambazo zimetumikam katika kutekeleza miradi mbalimbali kama ilivoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

1. Kutokuwepo kwa mashirikiano mazuri kutoka Manispaa ya Mjini kwa kuwa ilielezwa kuwa

Kamati ya Mfuko wa Jimbo iliwajuilisha wahusika wa Manispaa Mjini lakini hawakuwa wakishiriki katika utekeleaji wa miradi ya Jimbo.

2. Kuwepo kwa ufahamu tofauti baina ya Miradi ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na miradi ya kijamii ambayo ndio inayopaswa kutekelezwa kwa Mujibu wa SheriaNamba 4 ya mwaka 2012 (Sheria Mfuko wa Jimbo/ CDF)

3. Baadhi ya Miradi ikiweo ya Kisima inaonekana kulegalega uendelezaji wake kwa vile imekosa huduma kutoka kwa Kamati ya Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo kama walivyokuwa wakipatiwa awali. Mfano Kamati imegundua kuna kisima cha maji kilichopo mtaa wa Magomeni kinahitaji kusafishwa lakini huduma hiyo hakijafanyiwa, ingawa huduma ya maji yanapatikana kwa wananchi.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Pamoja na kwamba kuna baadhi ya Wenyeviti wa Mifuko hii ya Maendeleo ya Jimbo hawakupata nafasi ya kuchaguliwa kwa kipindi chengine lakini miradi ambayo wameianzisha inatakiwa iwe endelevu kwa kupata mashirikiano ya kutosha kutoka katika Kamati mpya za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

ii. Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kupitia kitengo chake cha miradi itoe muongozo ambao pamoja na mambo mengine utafafanua kwa uwazi zaidi miradi hasa inayopaswa kutekelezwa kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo (wa Mwakilishi).

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 7. | Malindi | 20,000,000 | Kufanikisha upatikanaji wa maji kisima cha Mchangani. | Mchangani | 1,500,000 | |
| | | | Kutengeneza bomba la maji la | Mitiulaya | 350,000 | Mradi Umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Mitiulaya | | | |
| | | | Kufanikisha upatikanaji wa maji kisima cha Baraste. | Mlandege | 1,800,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Kufanikisha upatikanaji wa maji Shehia ya Gulioni na Mlandege kwa kulaza mabomba mapya. | Gulioni na Mlandege | 2,300,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Kufanikisha upatikanaji wa maji Skuli ya Makadara kwa ujenzi wa mnara. | Mitiulaya | 1,200,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ununuzi wa komputa tatu kwa Skuli ya tumekuja, Kidutani na kajificheni. | Shangani na Mkunazini | 4,500,000 | |
| | | | Ununuzi wa meza nane na viti 60 kwa skuli ya maandalizi Mkunazini. | Mkunazini | 8,500,000 | Meza 10 na viti 25. (Mradi haujakamilika) |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuzisaidia Kambi | Mitiulaya | 3,000,000 | Mradi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | za skuli za Lumumba, Hurumzi na Tumekuja – Mitihani ya kidato cha nne. | Kiponda na Shangani | | Umekamilika |
| | | | Kambi ya Skuli ya Mkunazini | Mkunazini | 500,000 | Mradi Umekamilik a |
| | | | Skuli ya Makadara utengenezaji wa Umeme na photokopi | Mitiulaya | 150,000 | |
| | | | Kuwapa zawadi wanafunzi bora wa Sekondari ya Hurumzi. | Kiponda | 1,380,000 | |
| | | | Kuwazawadia wanafunzi walioshinda mashindano ya kuhifadhi Qur-an kwa Skuli ya Tumekuja, Hamamni, Haile-Salasie na Kionda. | Kiponda Shangani na Mkunazini | 1,700,000 | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kufanikisha safari ya walimu | Kiponda | 600,000 | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | na wanafunzi wa Skuli ya Hamamni kwenda Uengereza. | | | |
| | | | Mfuko wa kufanikisha watoto wa wazee wasio na uwezo na mayatima kuendelea na masomo yao. | Jimbo zima | 3,000,000 | |
| | | | Kuweka kifusi maeneo yaliyoathitrik na mvua kubwa maeneo ya Gulioni, Makadara na Miti-Ulaya. | Gulioni na Mitiulaya | 2,600,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Kusomesha vijana 20 Chuo cha Ujasiriamali Mwanakwerekwe kila mwanafunzi 130,000/- kwa mwaka. | Jimbo zima | 2,600,000 | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuwapa mafunzo ya Ujasiriamali | Jimbo zima | 250,000 | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | vijana 50. | | | |
| | | | Kuwapa mafunzo ya Ujasiriamali vijana 25. | Jimbo zima | 875,000 | |
| | | | Kuwapa mafunzo ya Ujasirimali wanawake 9. | Jimbo zima | 315,000 | |
| | | | Kuwawezesha kimtaji makundi ya wanawake na vijana. | Jimbo zima | 2,500,000 | |
| | | | Kusaidia wazee wasiojiweza. | Jimbo zima | 3,000,000 | |
| | | | Kusaidia viongozi wa Chama kuanzia ngazi ya Shina hadi Jimbo na wazee vipindi vya Ramadhani na Sikukuu. | Jimbo zima | 15,000,000 | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kusaidia Ujenzi wa Vyoo na nyumba zilizoathirika kipindi cha masika Shehia za Mitiulaya, Mwembetanga, Mchangani na | Mitiulaya, Muembe tanga, Mchangani na Mkunazini | 1,300,000 | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Mkunazini. | | | |
| | | | Kusaidia matibabu ya wananchi wasiojiweza Zanzibar na rufaa Muhimbili na Ocean Road. | Jimbo zima | 2,500,000 | |
| | | | Kusaidia umeme Madrasa ya Gulioni. | Gulioni | 432,000 | Mradi Hujakamilika |
| | | | Kuwasaidia vijana wa kifulioni Lumumba wanaojishughulisha na ukoshaji magari, mipira ya maji na usafishaji wa msingi wa maji machafu. | Mitiulaya | 600,000 | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Michezo – Kusaidia Timu za Jimbo:<br><br>Malindi 700,000<br>Rangers 200,000<br>Vikokotoni 500,000<br>Gulioni 500,000<br>Shangani 200,000<br>Mwembeladu 300,000 | Jimbo zima | 2,400,000 | |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Malindi.

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Malindi imekiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000) kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbali mbali katika Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya P.A.C

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya P.A.C imebaini kuwa kwa mujibu wa Fomu ua utekelezaji wa Miradi ya Jimbo hilo, kwa mwaka 2016/2017 miradi iliyotekelezwa kutokana na shilingi milioni ishirirni (20,000,000/=) zilizoingizwa ni kama ifuatavyo:-

1. Ukarabati wa Skuli ya Hurumzi – Shilingi milioni mbili laki nane na ishirini elfu (2,820,000/=_
2. Ununuzi wa vyerahani kumi (10) Skuli ya Forodhani Shilingi milioni mbili na elfu hamsini (2,050,000/=)
3. Ununuzi wa Desktop, CPU na Printer, Skuli ya Mkunazini – Shilingi 1,700,000/=
4. Ununuzi wa photocopy moja – Skuli ya Hamamni – Shilingi 2,950,000/=
5. Ujenzi wa barabara kwa kifusi – Malindi, Gulioni, Miti Ulaya na Mlandege – Shilingi 10,000,000/=
6. Gharama za ufuatiliaji – Shilingi 480,000/=

Kamati baada ya kupitia nyaraka za utekelezaji wa miradi na vielelezo vya matumizi ya miradi hiyo

pamoja na kukagua baadhi ya miradi iliyotekelezwa, imeridhika na utekelezwaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 8. | Mpendae | 20,000,000 | Uchimbaji wa Kisima na usambazaji maji safi na salama katika shehia ya Kilimani, Migombani na Kwa Binti-Amrani | Kilimani<br>Migombani<br>Kwa Binti-Amrani | 20,000,900 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mpendae

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mpendae imekiri kupokea kiwango shilingi 20,000,000 amabazo zimetumika kutekeleza kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti inagawa uongozi wa Jimbo hilo imetoa fedha za ziada kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilkagua nyaraka mbalimbali zinazohusiana na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo, Aidha, Kamati ya PAC ilipata nafasi ya kukagua kisima cha kwa Binti Amrani. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi katika jJimbo hilo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 9. | Shaurimoyo | Ununuzi wa gari ya Jimbo | Ununuzi wa gari ya Jimbo | Kwamtipura<br>Mboriborini<br>Mkele<br>Mapinduzi<br>Shaurimoyo<br>Saateni | 28,000,000 | |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Shaurimoyo

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Shaurimoyo imekiri kupokea kiwango hicho cha fedha na kutekeleza mradi wa ununuzi wa gari ya Jimbo kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imechumguza nyaraka mbali mbali zinazohusu zinazohusu utekelezaji wa Miradi zikiwemo fomu za maombi ya miradi na fomu za utekelezaji wa miradi. Aidha. Kamati imechunguza wa nyaraka za ununuzi na usajili wa gari husika pamoja na kuikagua gari yenyewe aina ya Mitsubishi – Canter tani mbili yenye nambari ya Chesis . FE51 CBD - 561029 na nambari za usajili Z 570 HV.Gari hiyo imenunuliwa kwa ajili ya shughuli za kijamii na usafi wa mazingira ndani ya Jimbo hilo. Kwa ujumla, Kamati ta PAC imeridhika na matumizi ya fedha za mradi na utekelezaji wa mradi huo,

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Magharibi A (2016/ 2017

| Nam | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bububu | 20,000,000 | Ujenzi wa kibanda cha kuekea pampu ya maji kizimbani. | Dole | 2,253,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Hozi la maji safi na salama katika Skuli ya Kijichi. | Kijichi | 1,036,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununuzi wa Pampu na mipira ya maji. | Kizimbani | 4,346,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ukarabati wa Vyoo Skuli ya Mbuzini | Mbuzini | 795,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uchimbaji wa kisima, Ujenzi wa Mnara na ununuzi wa pampu. | Mbuzini | 5,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Daraja | Kijichi | 5,029,500 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ukarabati wa vyoo na | Kizimbani | 1,200,000 | Miradi imekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Usambazaji wa maji Skuli ya Kizimbani. | | | |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo waJimbo la Bububu

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Bububu imekiri kupokea kiwango hicho cha fedha na kutekeleza mradi wa ununuzi wa gari ya Jimbo kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti inagawa uongozi wa Jimbo hilo imetoa fedha za ziada kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

i. Kutopatikana kwa ajili ya ukaguzi vielelezo halisi (original) vya utekelezaji na matumizi ya miradi husika kwa sababu iliyoelezwa kuwa aliyekuwa Katibu wa Kmati ya Mfuko amehama (yuko nje ya Zanzibar).
ii. Kukoseakana kwa tarehe katika kumbukumbu za kikao kilichojadili na kuidhinisha miradi iliyotekelezwa mwaka 2016/2017.

Hata hivyo, Kamati ya PAC ilikagua nakala za nyaraka mbalimbali zinazohusu utekelezaji na matumizi ya fedha za miradi hiyo zikiwemo Fomu za Miradi na stakabadhi za malipo. Aidha, Kamati ya PAC ilipata nafasi ya kukagua baadhi ya miradi iliyotekelezwa loikiwemo daraja la Chemchem katika Shehia ya Kijichi na kibanda cha kuwekea pampu ya maji Kizimbani. Licha ya dosari za hapa na pale katika baadhi ya nyaraka za miradi, kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi ya Jimbo hilo kwa mwaka 2016/2017

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | Mfenesini | 20,000,000 | Ukarabati wa barabara kwa kiwango cha kifusi. | Mwakaje | 7,000,000 | Mradi haujakamilika |
| | | | Ununuzi wa matenki Mawili | Chuini na Kihinani | 2,100,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uchimbaji wa Visima viwili na ujenzi wa minara. | Chuini na Kihinani | 10,821,500 | Mradi wa Chuini haujakamilka, Mradi wa Kihinani umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mfenesini

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mfenesini imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Jimbo hilo kwa mwaka 2016/2017 kama ilivyaoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali zinazohusu utekelezaji na matumizi ya fedha za miradi hiyo zikiwemo stakabadhi za malipo na kumbukumbu za kikao cha tarehe 28/2/2018 cha Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hilo ambacho ndich0 kilichoidhinisha miradi iliyotekelezwa kwa mwaka 2016/2017

Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na matumizi ya fedha zilizotumika kwenye utekelezaji wa miradi hiyo

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | Mtoni | 20,000,000 | Uchangiaji wa mifuko mia moja ya saruji kwa hospitali ya KMKM | Kibweni | 1,360,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Darasa la Skuli ya Msingi Kibweni | Kibweni | 5,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Matangi manne na mashine ya Maji | Kibweni | 4,300,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Utiaji wa Kifusi Barabara za ndani | Mwanyan ya | 2,800,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Matangi manne na mashine ya maji | Mwanyan ya | 4,300,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Matangi mawili na mashine ya maji | Mtoni | 2,300,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mtoni

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mtoni imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi miradimbali ya Jimbo hilo kwa mwaka 2016/2017 kama ilivyaoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

i. Kamati ya Mfuko wa Jimbo kuwasilisha marejesho kabla ya kukamilisha miradi. Hali hii imepelekea kuonekana kwa utaofauti wa viwango vya fedha za miradi hiyoo vilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na vile vilivyoainishwa katika Fomu za Utekelezaji wa miradi Mfano,katika mradi wa Ujenzi wa Darasa la Skuli ya Msingi Kibweni ambao uliainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti kutumia shilingi 5,000,000 lakini katika Fomu ya utekelezaji wa miradi imeelezwa kuwa ununuzi wa vifaa vya ujenzi skuli hiyo kugharimu shilingi 3,933,000. Ingawa ililiezwa kuwa wakati wakaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti wanafanya ukaguzi Kamati hiyo ya Mfuko wa Jimbo ilikuwa imenunua vifaa tu vya ujenzi, lakini ilipaswa kujaza Fomu za utekelezaji wa miradi pamoja na kuwasilisha marejesho Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais baada ya kukamilisha miradi hiyo.

ii. Muundo wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hilo kutofuata masharti ya Kisheria kwa kutokuwemo kwenye Kamati hiyo Mjumbe mwenye mahitaji maalum na Mjumbe kutoka Asasi za Kiraia (CSO) kutoka katika Jimbo hilo, Hali hiyo ilielezwa kuwa imetokana na kuchelewa kuundwa kwa Kmati hiyo.

iii. Kumbukumbu za kikao kutoainishwa tarehe iliyofanyika kikao hicho wala miradi iliyoidhinishwa kutekelezwa.

iv. Kukosekana kwa mashirikiano baina ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo na Manispaa ya Magharibi “A” kwa vile watendaji wa Manispaa hiyo walikuwa hawashiriki vikao ingawa ilielezwa kuwa walikuwa wakipewa taarifa.

v. Kukosekana kwa stakabadhi (risiti) halisi wakati wa kikao cha awali cha Kamati ya PAC. Hata hivyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko huo aliziwasilisha stakabadhi hizo halisi katika kikao kilichofanyika baadae tarehe 22/1/2021 baina yake na Kamati ya PAC

Hata hivyo, Kamati ilikagua darasa lililojengwa katika Skuli ya Msingi ya Kibweni pamoja na matangi mawili ya maji yaliyopo katika Shehia ya Mtoni.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kamati za Mfuko wa Jimbo zinapaswa ziwasilishe kopi za marejesho katika Ofisi ys Makamo wa Pili wa Rais baada ya kumaliza utekelezaji wa miradi ili hesabu kamili ya miradi hiyo iweze kupatikana.

ii. Wenyeviti wa Kamati za Kamati za Mfuko wa Jimbo wahakikishe kuwa Wajumbe waliomo katika Kamati hizo ni wale tu wanaokidhi vigezo na masharti ya kisheria.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | MTOPEPO | 20,000,000 | Uchimbaji wa Kisima | Munduli | 8,004,782 | Mradi umekamilika |
| | | | Uchimbaji wa Kisima – Basra | Mtoni Kidatu | 3,095,218 | Mradi umekamilika |
| | | | Mradi wa Barabara za Ndani | Shehia zote | 8,700,000 | Mradi Umekamilik a |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo lla Mtopepo

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mtopepo imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi miradimbali ya Jimbo hilo kwa mwaka 2016/2017 kama ilivyaoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilielezwa kazi mbalimbaii zilizotekelezwa katika kila mradi kama ifuatavyo:-

i. Katika Mradi wa kisima cha Monduli ambacho awali kilichimbwa kwa msaada wa Shirika la KIOCA la Korea tangu 2015 na kuachwa shimo tu, kazi zMfuko wa Jimbo zilihussha upigaji plasta eneo la mbele la mnara wa maji,, ununuzi wa milango na kujengewa, ununuzi wa matenki mawili ya ya maji (lita 5000 kila moja), ununuzi wa pampu ya maji na kuweka kisimani, kuvuta line ya umeme, kufanya fiting na kuunganishwa umeme na ununuzi wa mipira na kuwaunganishia wananchi.

ii. Katika mradi wa maji safi na salama – Kismia cha Basra, Kamati ya PAC ilibaini kuwa kisima hicho awali kilichimbwa na Mamalaka ya Maji (ZAWA) kupitia mradi wa Ras el Hema lakini kiloiachwa bila ya kuendelezwa. Kazi zilizofanywa kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo (shilingi 3,095,218) ni uwekaji wa kifusi katika eneo la kisima, Kujenga msingi (Foundationa) na kujenga kibanda cha maji kwa matofali hadi kozi ya tano.

iii. Mradi wa matengenezo ya barabara ulihusisha barbara ya Madaraka Basra, Garagara Basra, Mina na Msikiti Madole hadi Welezo ambapo kazi zilizofanyika ni kufukia mashimo kwa mawe na kuweka kifusi kwa baadhi ya maeneo.

iv. Katika ukaguzi wa nyaraka mbalimbali za miradi hiyo,Kamati ya PAC imebaini kuwepo kwa mapungufu kadhaa katika ujazaji wa Fomu za Jadweli la Pili ambapo jina na aina ya mradi haikuainishwa.

Kamati ilipata nafasi ya kutembelea miradi yote hiyo (Kisima cha Basra, Kisma cha Monduli na Barabara za ndani) ambapo kwa ujumla imeridhika na utekelezaji na matumizi ya fedha za miradi hiyo.

Mapendekezo ya Kamati ya Kamati ya PAC

Viongozi wa Kamati za Mfuko wa Jimbo wahakaikishe kuwa Fomu za miradi zinajazwa

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| kikamilifu katika maeneo husika yaliyoainishwa katika Fomu hizo. | | | | | | |
| 5. | MWERA | 20,000,000 | Ununuzi vifaa vya maabara skuli ya kianga na Usambazaji wa mipira | Kianga | 4,860,000 | Miradi imekamilika |
| | | | Ununuzi wa tenki na vifaa vyake na Ukarabati wa kituo cha afya KMKM na mchango wa Vifaa | Masingini | 4,987,000 | Miradi imekamilika |
| | | | Ununuzi vifaa vya maabara skuli ya regeza mwendo. Ununuzi wa transfoma Msikiti mzuri. Usambazaji wa maji Regeza mwendo na Gudini. | Mwera | 10,037,000 | Miradi imekamilika |

**Majibu ya Kmati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mwera**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mwera ilikiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyojipangia kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC baada ya kupitia nyaraka zote zinazohusiana na miradi hiyo zikiwemo fomu za maombi ya miradi na fomu za utekelezaji wa miradi pamoja na vielelezo vya matumizi na kukagua baadhi ya miradi hiyo iliridhika na utekelezaji wake.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| 6. | WELEZO | 20,000,000 | Usambazaji maji shehia zote | Mtofaani<br><br>Mchikichini<br>Hawaii<br><br>Welezo<br><br>Uholanzi | 20,000,000 | Miradi imekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maenedeleo ya Jimbo la Welezo**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Welezo ilikiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/-) kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyojipangia kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kukosekana kwa mashirikiano kati ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo na iliyokuwa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hilo. Hata hivyo, Kamati ya PAC baada ya kukagua nyaraka mbalimbali za utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kukagua baadhi ya miradi iliyotekelezwa mwaka 2016/2017 ikiwemo kisima cha Welezo (Kwa Bi Mgeni), kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mependekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilimshauri Mwenyakiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Welezo aunde Kamati mpya ya Mfuko wa Jimbo la kwa mujibu wa Sheria na kushirikiana nayo kikamilifu katika uibuaji na utekelezaji wa miradi ya kijamii katika Jimbo hilo katika kipindi cha mwaka 2020 - 2025.

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Magharibi B ( 2016/2017)

| Nam. | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha Zilizotumika | Hatua Ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | CHUKWANI | 20,000,000 | Ukarabati wa barabara kwa kiwango cha Kifusi kuanzia Kisauni, Shakani hadi Chukwani | Kisauni. Shakani. Chukwani. | 19,800,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chukwani

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chukwani ilikiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/-) kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ukarabati wa barabara kama zilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali za utekelezaji na matumizi ya mradi huo zikiwemo Fomu za Miradi na stakabadhi ya malipo (yenye namba 002 ya tarehe 10/1/2017 kutoka Construction and Supplier Limited yenye jumla ya shingi 20,000,000 kwa ajili ya malipo ya utengenezaji wa barabara). Kamati ya PAC ilipata nafasi ya kuzikagua barabara zilizofanyiwa ukarabati kwa mwaka 2016/2017 ambapo kwa ujumla imeridhika na utekelezaji wa mradi na matumizi ya fedha za mradi huo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | DIMANI | 20,000,000 | Skuli ya Maungani | Maungani | 860,000 | |
| | | | Uungaji maji Kombeni-Muembe Mafunza | Kombeni | 6,775,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Huduma mbali Mbali | Jimbo zima | 4,255,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Nyamanzi skuli | Nyamanzi | 467,160 | Mradi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | ya maandalizi (umeme) | | | Umekamilika |
| | | | Skuli ya msingi Dimani (huduma za maji) | Dimani | 263,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Dimani Misufini (mashine ya maji) | Dimani | 450,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Skuli ya | Kombeni | 3,835,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kombeni (matengenezo ) | | | |
| | | | Huduma mbali Mbali | Jimbo zima | 4,170,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Dimani

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Dimani ilikiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/-) kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ununuzi ya gari ya Jimbo hilo kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

1. Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hakuwa na risiti na fomu halisi (original) Ameeleza kwamba risiti hizo ameziwasilisha Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kama alivyoelekezwa na barua kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi. Hata hivyo, Watendaji wa Offisis ya Makamo wa Pili wa Rais walisema hawakupokea barua hiyo wala Mwenyekiti hakuwa na nakala ya barua hiyo..
2. Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo haikuwa na muhiri wake.

Hata hivyo Kamati ya PAC ilikagua nyaraka zilizokuwepo zikiwemo stakabadhi (risiti) pamoja na mchanganuo wa matumizi ya miradi hiyo ambazo Kmati ya PAC iliridhika nazo. Aidha Kamati ilikagua

kisima cha maji Kombeni Mwemba Mafunza pamoja na Skuli ya Maandalizi Nyamanzi. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika nautekelezaji wa miradi hiyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wenyeviti wa Kamati za Mfuko wa Jimbo wawe karibu na Watendaji wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wanaohusika na miradi kabla na wakati wa kutekeleza miradi hiyo ili kupata maelekezo yanayofaa kuhsu taratibu za miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | FUONI | 20,000,000 | Uchimbaji wa kisima katika kijiji cha Fuoni Kiembeni | Fuoni Migombani | 3,500,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa daraja katika Kijiji cha Kidarajani | Fuoni Mambo Sasa | 2,500,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Usambazaji wa umeme katika kijiji cha Fuoni Jumba la Mawe | Chunga | 4,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Usambazaji wa Maji safi na salama - maeneo ya yote ya Jimbo- Fuoni Michenzani, Fuoni Kipungani, Fuoni Birikani, Kimara na Mnarani | Jimbo zima | 9,395,000 | Miradi imekamilika |
| | | | **N.B** Daraja la Fuoni Mambo Sasa limevunjwa wakati wa ujenzi wa barabara ya lami | | | |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Fuoni

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Fuoni ilikiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/-) kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ununuzi ya gari ya Jimbo hilo kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

i. Kukosekana kwa kwa nyaraka halisi za utekelezaji wa miradi (original) ambapo Kamati ya Mfuko wa Jimbo ilieleza kuwa iliwasilisha nyarka halisi katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wakati ambapo Maofisa wa Miradi kutoka Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais walieleza kuwa Ofisi yao ilipokea kopi tu za nyaraka hizo mnamo tarehe 18/1/2018. Hata

<table>
<tr><td colspan="7">hivyo Kamati ya PAC ilielndelea na ukaguzi kwa kutumia kopi hizo zilizokuwepo.<br><br>ii. Katika Fomu za Utekelezaji wa Miradi. Imebainika kutoainishwa majina halisi ya miradi na kazi zilizotekelezwa bali imeainishwa majina ya miradi kwa ujumla tu.. Kwa mfano katika Mradi wa Umeme ilipaswa kuainishwa idadi ya nguzo na waya zilizotomika katika mradi huo.<br>Aidha, Kamati ilikagua stakabadhi za malipo (risiti) ya miradi hiyo pamoja na kukagua mradi wa kismia cha Fuoni Kiembeni ambao Kamati imeridhika nao.<br><br>Mapendekezo ya Kamati ya PAC<br><br>Katibu wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Fuoni pamoja na Makatibu wengine wa Kamati za Mfuko wa Jimbo wawe karibu zaidi na Watendaji wanaohusika na Miradi katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili kupata maelekezo ya kina juu ya taratibu mbalimbali zinazohusu miradi hiyo.</td></tr>
<tr><td rowspan="5">4.</td><td rowspan="5">K/SAMAKI</td><td rowspan="5">20,000,000</td><td rowspan="5">Ununuzi wa Gari ya Jimbo</td><td>K/samaki</td><td rowspan="5">19,500,000</td><td rowspan="5">Mradi umekamilika</td></tr>
<tr><td>Mbweni</td></tr>
<tr><td>Mombasa</td></tr>
<tr><td>Michumng wani</td></tr>
<tr><td>Kwamchina</td></tr>
<tr><td colspan="7">Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kiembe Samaki<br><br>Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kiembe Samaki ilikiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/-) kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ununuzi ya gari ya Jimbo hilo kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.<br><br>Uchunguzi wa Kamati ya PAC<br><br>Kamati ilielezwa kuwa awali gari iliyonunuliwa ilipelekwa Jimboni kichama lakini ilikataliwa kupokelewa kwa kuwa haikuwa gari ya Chama (CCM) bali ni mali ya Jimbo la KiembeSamaki. Aidha, Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali za utekelezaji wa Mradi zikiwemo Fomu za Miradi, na nyaraka za ununuzi wa gari hiyo. Kamati pia ilipata nafasi ya kuikagua gari hiyo ( HIACE/Minibus yenye nambari za usajili Z 325 HZ) na kuridhika nayo</td></tr>
<tr><td>5.</td><td>KIJITOUPE LE</td><td>20,000,000</td><td>Ujenzi wa Kituo cha Afya –</td><td>Taveta</td><td>18,920,000</td><td>Mradi umekamilika</td></tr>
</table>

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Magirisi | | | |
| | | | Ujenzi wa Njia za ndani | Meli Nne | 1,050,000 | Mradi umekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kijitoupele**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Kijitoupele ilikiri kupokea Shilingi Milioni Ishirini (20,000,000) ambazo zilitumika katika utekelezaji wa miradi miwili ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kazi mbalimbali zilifanyika katika kila Mrdai kama ifuatavyo:-

i. Katika mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Magirisi, kaiz zilizofanyika ni kutia dari(cyling) kupiga plasta, na kutia madirisha na milango.

ii. Katika mradi wa ujenzi wa niia za ndani, njia zilizohusika ni Taveta –Uzi, Magereza Mshelisheni, Njia ya Uzi na Njia ya Nyumba Moja.Kazi iliyofanyika ilikuwa ni kuziba mashimo katika njia hizo.

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali za utekelezaji wa miradi na za matumizi ya fedha za miradi hiyo zikiwemo Fomu za Miradi, stakabadhi za malipo (risiti) pamoja na kumbukumbu za kikao cha Kamati ya Mfuko wa Jimbo cha tarehe 26/3/2017 ambacho kilijadili na kuidhinisha miradi hiyo.
Kamati ya PAC pia ilikagua Kituo cha Afya Magirisi na njia za ndani zizofanyiwa matengenezo. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na matumzi ya fedha za miradi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 6. | M/KWERE K WE | 20,000,000 | Uendelezaj i wa Skuli ya Amali | Jitimai | 10,000,000 | Mradi umekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mwanakwerekwe**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Mwanakwerelwe ilikiri kupokea Shilingi Milioni Ishirini (20,000,000) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Jimbo hilo..

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

1. Baadhi ya kumbukumbu za vielelezo vya matumizi havikuwepo zikiwemo risiti za ujenzi wa jengo la kituo cha Mafunzo ya Amali hii imetokana na Katibu wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo kutokuwepo wakati wa kikao cha Kamati ya PAC kichofanyika tarehe 21/1/2021, ingawa Mwenyekiti wa Kmati ya Mfuko alikuwepo

2. Milango Tisa na mafeni mawili ya jengo hilo la Kituo cha Mafunzo ya Amali yameibwa bila ya kuvunjwa sehemu yoyote ya jengo ambapo kesi hiyo wameshairipoti kituo cha Polisi kwa hatua stahiki.

3. Kutokana na kutokuwepo Katibu wa Mfuko wa Jimbo katika kikao cha tarehe 21/1/2021 Kamati ya PAC ilielekeza kufanyike kikao chengine siku iliyofuata ya taerhe 22/1/2021 katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi kutamjumuisha Katibu wa Mfuko na Mwenyakiti wa Mfuko ili kupata vielelezo na maelezo ya kina juu ya miradi hiyo.

4. Kuwepo kwa mkanganyiko taarifa za miradi ambapo Miradi iliyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti kwa mwaka 2016/2017 ni tofauti na ile iliyoainishwa katika Fomu ya Utekelezaji na Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mwanakwerekwe. Hata hivyo, ilibainka kuwa miradi iliyoainshwa katika Ripoti ya Mdhibiti kuwa imetekelezwa 2016/2017 ilitekelezwa mwaka 2017/2018 na ile iliyoainishwa kutekelezwa 2017/2018 ilitekelezwa mwaka 2016/2017. Katika wa Mfuko wa Jimbo alikiri kufanya makosa hayo

5. Kutokana na uwekaji mbaya wa kumbukumbu za uterkelezaji wa miradi na za matumizi ya fedha za miradi (zikiwemo stakabadhi za matumizi), Kamati yya PAC haikuweza kuthibitisha matumizi kamili ya shilingi 20,000,000 zilizotumiwa katika Jimbo hilo kwa mwaka 2016/2017. Aidha, kutokana na kasoro hiyo Kamati pia haikuweza kuthibitisha uhalali wa uibuaji wa miradi hiyo kwa wananchi kwa kuwa kumbukumbu za vikao zikiwemo za kikao cha Kamati ya Mfuko wa Jimbo kilichojadili na kuidhinisha miradi hazikupatikana kwa ukaguzi.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mwanakwerekwe ihakikishe kuwa kumbukumbu za utakelezaji na za matumizi ya miradi zinatunzwa vizuri kwa ajili ya kazi mbaoimbali zikiwemo za Ukaguzi.

ii. Kamati ya Mfuko wa Jimbo iandae utaratibu mzuri utaowezesha miradi iliyotekelezwa inatunzwa vizuri bila ya kufanyiwa wizi au uharibifu wowote.

iii. Kamati ya Mfuko wa Jimbo ifuatilie kwa kina katika vyombo vya Sheria vifaa vilivyoibiwa ktika Skuli ya Amali Mwanakwerekwe.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 7. | PANGAWE | 20,000,000 | Ujenzi wa ukuta wa skuli ya Kijitoupele | Pangawe | 400,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ujenzi wa Mtaro; Pangawe-Pangawe bonde la mpunga | Pangawe | 18,600,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Pangawe

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Mwanakwerelwe ilikiri kupokea Shilingi Milioni Ishirini (20,000,000) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamat ya PAC ilielezwa kuwa Ukuta wa Skuli ya Kijitoupele haujajaengwa badala yake wananchi wamejenga aprone katika Skuli hiyo. Aidha katika mradi wa mtaro, ilibainika kuwa awali walianza kujenga mtaro huo kienyeji lakini mtaalam wa mitaro alipokua akaja na vipimo vyake upya.

Kamati ilikagua vielelezo mbalimbali vya utekelezaji na vya matumizi ya miradi zikiwemo kumbukumbu
za vikao mbalimbali, Fomu za Miradi na Stakabadhi za malipo.

Vilevile, Kamati iliukagua mtaro uliopo katika Shehia ya Pangawe. Kwa ujumla Kamati ya PAC imerdhika na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KWA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Kaskazini A

| Nam | Jimbo | Fedha zilizoingiz wa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | CHAANI | 20,000,000 | Ununuzi wa Power Tiller mbili | Shehia zote | 20,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununuzi wa Mashine mbili za kumwagilia Maji | | | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Uchangiaji wa Gharama za Kutolea Gari za Jimbo | | | Mradi umekamilika |
| Kamati ya PAC haikuweza kufanya ukaguzi wa miradi iliyotekeleaawa katika Jimbo la Chaani kwa mwaka 2016/2017 kutokana na kutotimizwa kwa masharti na utaratibu wa Kamati ya PAC wa kupatiwa kopi za vielelezo kwa kila Mjumbe wa Kamati ili kila Mjumbe aweze kupata nafasi ya kuvipitia kwa kina na kwa muda muafaka. Katika kikao cha Kamati ya PAC kilichokusudiwa kujadili miradi hiyo, iliwasilishwa kopi moja tu ya vielelezo na hivyo ukaguzi huo kutoweza kufanyika. | | | | | | |
| 2. | KIJINI | 20,000,000 | Uchimbaji wa Kisima. | Kijini Matemwe | 2,500,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Matengenezo ya Kisima. | Kivunge | 1,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Ukuta wa Skuli ya Chekechea Kivunge. | Kivunge | 2,030,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Usambazaji wa Nguzo za Umeme na Ununuzi wa waya. | Juga Kuu | 10,002,509 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununuzi wa Pampu. | Potoa | 1,270,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Usambazaji wa Maji Skuli ya Potoa. | Potoa | 4,022,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kijini.

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Kijini ilikiri kupokea kiwango cha fedha Shilingi Milioni ishirini (20,000,000) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya P,A,C imegundua kuwa miradi iliyotekelezwa katika Jimbo la Kijini kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni kama ifuatavyo:-

1. 1, Kupeleka umeme Kachongwa (Matemwe) Shehia ya Juga Kuu – Tsh10,000,000/=
2. Kuchimbisha kisima Kijini kwa Sheha wa Shehia Tsh 2,500,000/=
3. 3, Kuweka mlango wa geti na kupandisha ukuta skuli ya maandalizi Kivunge – Tsh,2,663,500
4. Kukifukua kisima Kivunge karibu na Madrasa ya Mwalimu Haji Tsh.1,000,000/=
5. Ununuzi wa pump za maji kwa ajili ya visima viwili Potoa – Tsh.1,270,000/=
6. Upelekaji wa maji Skuli ya Maandalizi ya Potoa – Tsh.600,000/=
7. Posho la wajumbe 9 kwa vikao vine Tsh.1,800,000/=
8. Nauli na gharama za ufuatiliaji Tsh.285.935

Kamati ya P,A,C imepitia nyaraka mbalimbali za utekelezaji wa miradi hiyo zikiwemo fomu za Miradi pamoja na nyaraka za matumizi ya fedha za miradi zinazojumuisha stakabadhi za malipo na mikataba ya kazi zilizotekelezwa (ikiwemo mkataba wa kazi ya ujenzi wa ukuta wa skuli ya Maandalizi ya Kivunge uliotiwa saini tarehe 25/4/2017 wenye jumla ya shilingi 350,000/=.

Aidha, Kamati ilipata nafasi ya kukagua mradi wa kuweka mlango wa geti na ukuta uliojengwa katika skuli ya maandalizi ya Kijini.

Kwa ujumla, Kamati ya P.A.C imeridhika na utekelezaji wa miradi pamoja na matumizi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | MKWAJUNI | 20,000,000 | Ujenzi wa skuli ya Msingi ya Kibeni | Kibeni | 4,890,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa | Kidombo | 706,000 | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | ukuta wa choo katika skuli ya Kibuyuni | | | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa skuli ya Sekondari ya Gamba | Gamba | 4,650,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa skuli ya Msingi ya Moga | Moga | 4,810,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uchangiaji wa fedha kwa ajili ya Madawati katika skuli ya msingi Mkwajuni | Mkwajuni | 1,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa ukuta wa uzio katika skuli ya msingi Mkwajuni | Mkwajuni | 1,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uwezeshaji wananchi walofikwa na maafa | | 800,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mkwajuni

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Nungwi ilikiri kupokea Shilingi Milioni ishirini (20,000,000) kutoka Serikalini ambazo zilitumika katika utekelezaji wa miradi miwili kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

i. Ucheleweshwaji katika katukeleza miradi wa miradi ambapo fedha za mwaka 2016/2017 zimeanza kutumika mwaka 2018.

ii. Fedha nyingi kutumika katika kulipana posho za vikao ambapo jumla ya shilingi 1,500,000 zilitumika katika matumizi hayo. Kufanya hivyo, ni kwenda kinyume na utaratibu wa matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

iii. Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kutopata ushirikiano kutoka Halmashauri ya Wilaya Kaskazini "A"

Aidha, Kamati ya PAC ilipata nafasi ya kukagua miradi mbali iliyotekelezwa kama ifuatavyo:-

1. Skuli ya Sekondari Gamba: Ujenzi ulihusisha madarasa mawili kuanzia chini hadi gebo.

Baadae Mbunge wa Jimbo hilo pamoja na Serikali walimalizia ujnzi huo.

2. Skuli ya Msingi Moga; Ujenzi ulihusisha madarasa matatu, Ofisi moja na Ukumbi (Hall) ambapo ujenzi ulianzia hatua ya kujenga msingi hadi matofali kozi ya tano.

3. Banda la Skuli ya Kibeni: Ujenzi ulihusisha banda la lenye madarasa manne kuanzia hatua ya kujenga msingi (Foundation) hadi karibu na linta ya juu. Jengo nado halijakamilika.

4. Muathirika wa Maafa Ndg Khamis Jaku Khamis alikutana na Kamati ya PAC na kuithibitishia kuwa alipata mchango wa maafa kutoka Mfuko wa Jimbo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kutokana na kuwepo kwa miradi ya Mfuko wa Jimbo isiyoendelezwa likiwemo jengo la la madarasa matatu ya Skuli ya Msingi ya Moga, Kamati ya PAC inashauri Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mkwajuni pamoja na Kamati nyengine za Mfuko wa Jimbo kuhakikisha kuwa inapanga na kutekeleza miradi michache inayoweza kukamilika kwa kipindi kifupi badala ya kutekeleza miradi mingi ambayo inabaki bila kuendelezwa wala kutoa tija inayokusudiwa kwa wananchi.

2. Iwapo kutakuwepo na miradi iliyokuwa haijawahi kukamilishwa na Kamati za Mfuko wa Jimbo zilizopita ni vyema kwa Kamati za Mfuko wa Jimbo zilizopo ziandae utaratibu wa kuikamilisha miradi hiyo kwanza kabla ya kutekeleza miradi mipya ili miradi hiyo iweze kutoa manufaa na tija iliykususdiwa kwa wananchi

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | NUNGWI | 20,000,000 | Ujenzi wa Skuli ya Msingi Nungwi Madarasa manne. | Nungwi | 10,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Skuli ya Sekondari Kidoti Madarasa manne . | Kidoti | 10,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Nungwi

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Nungwi ilikiri kupokea Shilingi Milioni ishirini (20,000,000) kutoka Serikalini ambazo zilitumika katika utekelezaji wa miradi miwili kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilikagua nyaraka mabalimbali za utekelezaji na matumizi ya miradi iliyotekelezwa zikiwemo Fomu za Miradi na Stakabadhi za malipo (risiti) ambapo katika Fomu za Miradi yalibainika mapungufu ya hapa na pale ikiwa ninpamoja na Fomu hizo kutojazwa tarehe husika. Aidha Kamati ya PAC ilipata nafasi ya kukagua miradi iliyotekelezwa kama ifuatavyo:-

i. Skuli ya Msingi Nungwi: Ujenzi uulihusisha madarasa manne kuanzia hatua ya msingi hadi gebo, Ujenzi ulianza mwaka 2017/2017 na kumalizika mwaka 2017/2018. Kwa hivi sasa ujenzi wa madarasa hayo umemalizika na yameanza kutumika.

ii. Skuli Sekondari Kidoti: Ujenzi ulihusisha madarasa manne kuanzia hatua ya msingi hadi kumalizia. Kwa bhivi sasa madarasa hayo yamekamilika na yanatumika.

Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Nungwi iwe makini katika ujazaji wa nyaraka mbalimbali zikiwemo Fomu za Miradi kwa kuhakikisha kuwa inajaza nyaraka hizo kikamilifu

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5. | TUMBATU | 20,000,000 | Ujenzi wa vyoo | Kipange<br>Mkokotoni<br>Mto wa Pwani | 5,263,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ujenzi wa madarasa mawili | Mkokotoni | 13,981,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Tumbatu

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Tumbatu ilikiri kupokea Shilingi Milioni ishirini (20,000,000) kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebani kuwa miradi iliyotekelezwa katika Jimbo la Tumbatu kutokana na shilingi 20,000,000 zilizoingizwa ni kama ifuatavyo:-

i. Ukamilishaji wa nyumba ya walimu Mkokotoni; Ukarabati huo ulitumia jumla ya shilingi 13,981,00. Fedha hizo zilitumika kwa ajili ya matumizi mablimbai yakiwemo ununuzi wa vifaa vya ujenzi kama saruji kwa ajili ya plasta, ununuzi wa rangi na kupaka rangi.

ii. Ujenzi wa vyoo vya jamii; Ujenzi huu uligharimu jumla shilingi 6,019,000 na ulihusisha vyoo vitatu vilivyojengwa katika maeneo ya Kipange,Mto wa Pwani na Mkokotoni. Fedha hizo zilitumika katika ununuzi wa mchanga, kokoto,mbao, bati na vifaa vyengine vya

ujenzi.

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbali mbali za uteekelezaji wa miradi na za matumizi ya miradi ya miradi hiyo pamoja na kukagua miradi iliyotekelezwa. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo.

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Kaskazini B (2016/2017)

| Nam | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | BUMBWINI | 20,000,000 | Usambazaji maji mibiboni,kidanzini<br><br>Uezekaji ofisi ya walimu skuli ya bumbwini<br><br>Kambi ya wanafunzi misufini na makoba | Misufini | 19,000,000 | Miradi imekamilika |
| | | | Uchimbaji wa kisima pangatupu (kiongwe)<br><br>Utiaji umeme kisima cha maji<br><br>Usambazaji maji vidimni juu<br><br>Ununuzi wa pampu vidimni(zawa)<br><br>Ujenzi wa daraja | Kidanzini | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Utiaji geti la skuli ya sekondari makoba<br><br>Kambi ya | Makoba | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | wanafunzi | | | |
| | | | Ujenzi wa msingi wa skuli ya chekechea | Mafufuni | | |
| | | | Uchimbaji visima viwili, Kiongwe kidogo na pangatupu | Kiongwe kidogo | | |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Bumbwini

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Donge ilikri kupkea jumla ys hilingi 20,000,000

Ambazo zilitumika katika kutekeleza miradi mablimbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilibaini kuwa vielelezo halisi (original) havikupatikana kwa ukaguzi wakati wa

Kikao cha Kamati ya PAC kwa sababu iliyoelezwa kuwa vielezo hivyo alikuwa navyo Afisa Mipango wa Halmshauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B" ambae alihamishwa katika Halmashauri hiyo, na watendaji waliokuwepo hawakuweza kuviona. Hata hivyo, kopi za vielelezo hivyo zilikuwepo katika kikao cha PAC na Kamati iliendelea na ukaguzi wa vielelezo hivyo.

Kamati ya PAC imebaini kuwa kuna baadhi ya Miradi inaonekana kuleta utata kuingia katika tafsiri ya kuwa ni miradi ya Jamii ambayo Kamati ya Mfuko wa Jimbo imeitekeleza kama vile kuchangia kambi za wanafunzi

Aidha, Kamati ya PAC ilikagua vielelezo vinavyohusika na utekelezaji pamoja na matuimizi ya miradi hiyo zikiwemo fomu za Miradi, Stakabadhi za matumizi pamoja nakumbukumbu za kikao cha Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Bumbwini cha tarehe 6/12/2016 ambacho ndicho kilichoidhinisha miradi iliyotekelezwa, Kamati ilipata nafasi ya kukagua pampu ya maji Vidimni ambapo kwa ajumla imeridhika na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo.

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kupitia kitengo cha miradi ihakikishe inawapatia uelewa Wajumbe na Viongozi wa Kamati za Mfuko wa Maendeleo ili waweze ili waweze kufahamu taratibu mbalimnbali zinzoongoza mifuko ya Jimbo ikiwa ni pamoja na kuweza kutofautisha miradi ya kijamii na miradi mingine. | | | | | |
| 2. | DONGE | 20,000,000 | Usambazaji wa Umeme | Donge Mtambile | 21,465,999 | Miradi imekamilika |
| | | | Usambazaji wa Maji | Njia ya Mtoni | | |
| | | | Usambazaji wa Umeme | Donge Karange | | |
| | | | Usambazaji wa Maji | | | |
| | | | | | | |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Donge

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Donge ilikri kupkea jumla ys hilingi 20,000,000

Ambazo zilitumika katika kutekeleza miradi mablimbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imekagua vielelezo mbalimbali vinavyohusiana nautekelezaji pamoja na matumzi ya miradi hiyo zikiwemo Fomu za Miradi, kumbukumbu za vikao na stakabadhi za malipo. Aidha, Kamati ilipata nafasi ya kukagua huduma ya maji na umeme katika Shehia ya Donge Karange na huduma nyengine ya umeme katika Shehia ya Donge Mtambile ambapo jumla ya nguzo 15 zilitumika katika utekelezaji wa mradi huo wa umeme (Donge Mtambile). Kwa ujumla Kmati ya PAC imeridhika na matumizi ya fedha pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | KIWENGWA | 20,000,000 | Ununuzi wa vifaa vya maabara skuli ya Upenja | Upenja | 20,255,997 | Miradi imekamilika |
| | | | Ununuzi wa vifaa vya maji | Kitope kwa Gube | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Usambazaji wa umeme Muembe Majogoo | Mbaleni | | |
| | | | Uchimbaji wa Kisima cha kalbi katika kituo cha afya cha Kitope | Mbaleni | | |
| | | | Ujenzi wa skuli ya Kilombero | Kilombero | | |
| | | | Ujenzi wa njia za ndani Boma, Kwa Goa, Mbaleni na Kichwele | Mbaleni | | |

Majibu ya Kamati ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Kiwengwa

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kiwengwa ilikri kupkea jumla ys hilingi 20,000,000

Ambazo zilitumika katika kutekeleza miradi mablimbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibti

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mabalimbali za utekelezaji na za matumzi ya miradi ilitokelezwa zikiwemo

stakabadhi (risiti), Fomu za Miradi, pamoja na kumbukumbu za kikao cha tarehe 7/4/2017 ambacho ndicho kilichoidhinisha miradi hiyo iliyotekelezwa. Aidha Kamati ilipata nafasi ya kukagua Skuli ya Kilombero pamoja na umeme katika Shehia ya Mbaleni. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | MAHON D A | 20,000,000 | Ujenzi wa mnara wa kisima cha maji | Mangap w ani | 17,752,000 | Miradi imekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ukarabati wa skuli ya maandalizi na Utengenezaji wa vyoo vya Skuli | Fujoni | | |
| | | | Ujenzi wa vyoo vya skuli ya mkadini | Mkadini | | |
| | | | Ukarabati wa vyoo vya skuli pamoja na utiaji fitting | Zingwezingwe | | |
| | | | Uendelezaji wa jingo la soko kuanzia kozi | Kinduni | | |
| | | | Umalizaji wa skuli ya maandalizi mto mchanga | Mahonda | | |
| | | | Usambazaji mipira ya maji | matetema | | |
| | | | Ujenzi wa madarasa mawili | Mkokotoni | | |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mahonda

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mahonda imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali katika Jimbo hilo kama ilivyoanishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali zinazohusiana na matumzi pamoja na utekelezaji wa miradi. Aidha Kamati ya PAC ilipata nafasi ya kulikagua soko la Kinduni ambapo kwa ujumla imeridhika na miradi iliyotkelezwa

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KWA MKOA WA KUSINI UNGUJA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Kati

| Nam | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | CHWAKA | 20,000,000 | Ununuzi wa mipira ya maji | Pete | 20,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chwaka.

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chwaka imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zimetumika katika kutekeleza mradi moja katika Jimbo hilo kama ilivyoanishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kukosekana kwa Fomu ya Utekelezaji wa Miradi ambapo hata katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwenye Kitengo cha Miradi Fomu hiyo pia imekosekana, ingawa mradi uliokusudiwa umetekelezwa.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kamati ilikagua nyaraka mbalimbali za utekelezajji na za matumizi ya fedha za miradi hiyo zikiwemo stakabadhi (risiti za malipo) pmoja na kumbukumbu za Kikao cha Kamati ya Mfuko wa Jimbo hilo cha tarehe 21/6/2017 ambacho kilijadili na kuidhinisha mradi huo. Aidha, Kamati imeakagua huduma ya upatikanaji wa maji Pete inayotokana na utekelezaji wa mradi huo na kuridhika nayo.<br><br>Mapendekezo ya Kamati ya PAC<br><br>Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ziwe karibu zaidi na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (Kitengo cha Miradi) kabla na wakati wa utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. | | | | | | |
| 2. | TUNGUU | 20,000,000 | Ujenzi wa msingi skuli ya Kibele | Tunguu | 3,920,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa skuli ya Dunga Kiembeni | Dunga Kiembeni | 3,825,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Usambazaji wa maji Pongwe | Ubago | 2,000,000 | Mradi Umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Umaliziaji wa ujenzi wa skuli ya Bungi | Bungi | 6,933,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Utiaji wa Umeme skuli maandlizi ya U/Ukuu Kae Pwani | Unguja Ukuu Kae Pwani | 2,912,840 | Mradi umekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Tunguu**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Tunguu imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali katika Jimbo hilo kama ilivyoanishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mabalimbali za utekelezaji na za matumizi ya miradi iliyotekelezwa zikiwemo stakabadhi (risiti), Fomu za Miradi, pamoja na kumbukumbu za vikao vya Kamati ya Mfuko wa Jimbo hilo. Aidha Kamati ilipata nafasi ya kukagua miradi iliyotekelezwa kama ifuatavyo:-

i. Skuli ya Dunga Kiembeni – Ujenzi ulihusiasha madarasa matatu na hodhi la maji. Awamu ya kwanza ilijumuisha ujenzi wa msingi hadi kozi ya nne na ukanda.. Awamu ya pili ilijumuisha uendelezaji na ujenzi wa gebo na linta (zaidi ya shilingi milioni 10 zilitumika katika mradi huo kwa mwaka 2016/2017 na mwaka 2017/2018)
ii. Skuli ya Kibele – ujenzi ulihusisha madarasa matano kuanzia msngi, linta hadi gebo. Kazi za uezekeaji na nakazi nyenginezo za umaliziaji zilifanywa na Serikali.
iii. Umaliziaji wa ujenzi wa Skuli ya Bungi – ulihusisha ujenzi wa gebo, uezekaji madarasa mawili,kutia sakafu

Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji pamoja na matumizi ya fedha za miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | UZINI | 20,000,000 | Ununuzi wa vifaa vya afya kwa jimbo zima Vikiwemo kompyuta 8 na vigari vya walemavu 8 katika vituo vifuatavyo: Mwera,Machui, Uzini,Miwani,Umbuji,Bambi,Ki | | 22,911,616 | Mradi Umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | boje Mw/shauri na Mchangani | | | |

Kamati ya PAC haikuweza kufanya ukaguzi wa miradi ya Jimbo la Uzini kwa sababu ya kutokuwepo katika Kikao cha Kamati ya PAC Katibu wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo hilo ambae ndie aliyekuwa na maelezo na vielelezo vinavyohitajika kwa ukaguzi, ingawa baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo hilo walikuwa wameshafika katika kikao hicho

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Kusini Unguja (2016/2017)

| Nam | Jimbo | Fedha zilizoingiz Wa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MAKUNDUCHI | 20,000,000 | Uchimbaji wa Kisima cha Maji safi na Salama. | Muyuni A | 1,750,000 | Mradi unaendelea |
| | | | Uchimbaji wa kisima cha Maji safi na salama. | Kiongoni Makunduchi | 2,150,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Nyumba ya walimu | Kizimkazi Mkunguni | 2,600,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa michirizi ya mvua. | Mzuri/Tasani | 3,985,800 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ujenzi wa uzio/Skuli ya chekechea Muyuni C. | Muyuni C | 4,000,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ukarabati wa nyumba ya walimu. | Kibuteni | 1,997,500 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ununuzi wa Komputa kwa jumuiya ya Saccos. | Kizimkazi Dimbani | 1,000,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Makunduchi

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Makunduchi imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali katika Jimbo hilo kama ilivyoanishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilielezwa kuwa mradi wa Uchimbaji wa Kisima cha Maji safi na Salama – Muyuni "A" ulikumbwa na matatizo ambapo maji yalikuwa mbali na mchimbaji kadri alivyokuwa akichimba alikuwa akikosa hewa (Oxygen), kisima hicho kilichukua mwaka mmoja kukichimba Hatimae kisima kilifukiwa na wakati huo zilikuwa zimeshatumika shilingi 1,750,000, Fedha zilizobakia zilitumika katika Mradi wa Umeme katika mwaka uliofuata wa 2017/2018. Kamati ilikagua nyaraka mbalimbali zinazohusu utekelezaji na matumizi ya fedha za miradi hiyo na kuridhika nazo. Aidha, Kamati ya PAC ilikagua baadhi ya miradi iliyotekelezwa ukiwemo uzio wa Skuliya Maandalizi ya Muyuni "C na nyumba ya Walimu iliyopo Skuli ya Kizimkazi Mkunguni. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | PAJE | 20,000,000 | Ununuzi 7wa pampu mbili za maji. | Kibigija | 12,200,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Usambazaji wa | Michamvi | 2,500,000 | Mradi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Maji | | | Umekamilika |
| | | | Ununuzi wa Dawa. | Jambiani Kikadini.<br>Kitogani.<br>Paje.<br>Bwejuu. | 4,008,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununuzi wa pampu katika kijiji cha Mfumbwi. | Jambiani Kikadini | 1,700,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Paje

Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Paje ilikiri kupokea jumla ya Shiingi 20,000,000/= ambazozimetumika katika kutekeleza miradi minne kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kutohudhuria kwa Wajumbe wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo Paje katika kikao cha Kamati ya PAC (alihudhuria Mwenyekiti peke yake). Aidha, Kmati ilibaini kuwa kumbukumbu za vikao kwa mwaka 2016/2017 na mwaka 2017/2017 hazikupatikana kwa ukaguzi.

Kamati pia ilikaguapampu ya maji katika kisima cha Jambiani Kibigija, Pampu ya maji, pamoja na kufika kituo cha Afya Jambiani kujirdhish akupokelewa kwa dawa. Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi

miradi hiyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Ni vyema Wenyeviti wakawa wasimamizi wazuri wa taratibu zinazohusiana na utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Jimbo

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KWA MKOA WA KASKAZINI PEMBA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017 Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Wete

| Nam | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | GANDO | 20,000,000 | Utengenezaji wa barabara ya kizimbani | Kizimbani | 6,010,500 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Upron skuli ya Gando | Junguni | 4,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ukarabati wa skuli ya ukunjwi | Ukunjwi | 4,009,500 | Mradi umekamilika |
| | | | Ukarabati wa madarasa 3 skuli ya kizimbani | Kizimbani | 4,980,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Gando.

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Gando ilikiri kupokea jumla ya Shiingi 20,000,000/= ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi minne kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa mradi waukarabati wa Skuli ya Ukunjwi ulipangiwa kutumia shilingi 11,202,200/= ambapo matumizi halisi ya mradi huo ni Shilingi 4,009,500/= (matumizi ya kiasi kidogo cha fedha ikilinganishwa na makadirio). Aidha, mradi wa ukarabati wa madarasa matatu ya Skuli ya Kizimbani ulipangiwa kutumia Shilingi 2,843,000/= ambapo matumizi halisi yalikuwa ni Shilingi 4,980,000/=. Pia ilibainika kuwa Shilingi 1,000,000/= zilitumika katika uendeshaji wa

shughuli za miradi hiyo.

Kamati ilikagua nyaraka mbali mbali ziizohusiana na utekelezaji wa miradi pamoja na matumizi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo. Miongoni mwa nyaraka (vielelezo) vilivyokaguliwa ni Fomu za Miradi, mikataba ya kazi mbali mbali (ikiwemo ujenzi wa Airport, skuli ya Gando Msingi, upigaji plasta na utiji sakafu madarasa manne ya Skuli ya Ukunjwi, utiaji rangi nje na ndani na utiaji umeme madarasa hayo), stakabadhi za malipo na kumbukumbu za kikao cha tarehe 21/6/2017 cha Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Gando ambapo ndicho kilichoidhinisha miradi hiyo iliyotekelezwa. Pia Kamati ya P.A.C ilipata nfasi ya kukagua badhi y miradi iliyotekelezwa katika Jimbo hilo kwa mwaka huo wa fedha ingawa kwa ujumla Kamati iliridhika na utekelezaji wa miradi hiyo ilishauriifuatavyo:-

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati za Mfuko Mfuko wa Maendeleo ya Majimbo zishirikiane na viongozi wa Shehia zinazowsilisha maombi ya miradi katika kufanya utafiti wa bajeti hizo ziendane na uhalisia wa gharama halisi zinazzohitajika katika utekelezaji wa miradi hiyO.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | MGOGONI | 20,000,000 | Kuunga Maji kutoka kinyasini hadi makundeni na Fiting banda la skuli ya kinyasini | Kinyasini | 2,750,400 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa bwawa la chumvi na ufugaji wa samaki | Kiungoni | 1,000,000 | Mradi Umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ujenzi wa banio bonde la tovuni | Kiungoni | 3,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Nguzo tatu za umeme pamoja na waya wake kijiji cha Gumba | Finya | 4,164,727 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Utiaji sakafu na Apron skuli ya kiungoni mabanda mawili | Kiungoni | 4,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Msaada wa saruji na mpira wa maji kituo cha afya JKU | Pandani | 1,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamai ya Mfuko wa Maeneleo ya Jimbo la Mgogoni.

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mgogoni imekiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutok Serikalini ambazo zimetumika katika utengezaji wa miradi mbali mbali katika jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya P.A.C imebaini kuwa pamoja na miradi iliyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti, kulikuwa pia na mradi mwengine was aba ambao ulitekelezwa katika Jimbo hilo kwa mwaka huo 2016/2017. Mradi huo ni uwekaji wa fusi njia ya Kwale Mpona ambao umegharimu Shilingi 3,000,000/=. Aidha, imebainika kuwa jumla ya shilingi 1,000,000/= zilitumika kwa ajili ya kazi za uendeshaji.

Kamati ilikagua nyraka mbali mbali zinazohusiana na utekelezaji pamoja na matumizi ya miradi hiyo zikiwemo stakabadhi za malipo, mikataba ya kazi pamoja matumizi ya miradi hiyo zikiwemo stakabadhi za malipo, mikataba ya kazi pamoja kumbukumbu za kikao cha tarehe 14/1/2016 ambcho kiliidhinisha mirdi mbali mbali iliyotekelezwa. Kamati pia ilipaa nafasi ya kukagua baadhi ya miradi hiyo na kwa ujumla, imeridhika na utekelezaji wa mtumizi ya miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | MTAMB WE | 20,000,000 | Usambazaji maji kutoka Mkanjuni mpaka Mahujuu (kivumoni) | Mtambwe kusini | 17,350,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mtambwe.

Kamati y Mfuko wa Maeneleo y Jimbo la Mtambwe imekiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= ambapo ilitekeleza mradi mmoja kama ulivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya P.A.C imebaini kuwa kulikuwa na feha shilingi 2,600,000/= ambazo Menyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo hilo ilizitoa na kukaa nazo bila ya kumuarifu mtu. Aidha, Kamati ilibaini kuwa Mamlaka ya kuzuia Rushwa n Uhujumu Uchumi (ZAECA) ilifuatilia tatizo hilo hapo baadae ambapo ilimtaka Mkurugenzi w Baraza Baraza la Mji Wete kuwsilisha taarifa na nyaraka zinazohusu utekelezaji na matumizi ya miradi ya Mfuko wa Jimbo la iliyotekelezwa na kusimamiwa na Baraza la Mji Wete kwa mwaka 2017/2018 /Baru kutoka ZAECA yenye nambri ya kumbukumbu 10/CRC/ZAECA/KS.P/48/03/VOL.11/32 inahuska.

Aidha, kupitia Slip ya Benk ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ya tarehe 9/7/2018 na "Bank Statement ya tarehe 1 Julai 2018 hadi tarehe 9 Julai, 2018 kamati ya P.A.C imebaini kuw fedha hizo zilirejeshwa kwenye akaunti ya Maendeleo ya Jimbo hilo la Mtabwe (041108001070). Mwenyekiti huyo wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mtambwe tarehe 1 Julai, 2018.

Vile vile Kamati ya P.A.C imebaini kuwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambayo ndiyo inayoratibu miradi ya Mfuko wa Majimbo haikupewa taarifa juu ya kutokea kwa tatizo hilo na muwepo kwa fedha za mwaka 2016/2017 mbazo zimetumika kwa mwaka uliofuata wa 2017/2018.

Kutokana na mazingira hayo Jimbo la Mtambwe kwa mwaka 2016/2017 liliweza kutekeleza mradi mmoja tu wa usambazaji maji kutoka Mkanjuni mpaka Makujuu (Kivumoni) ambao ulitumia jumla ya shilingi 17,350,000/= na mrdi huo umekamilika.

Fedha zilizochukuliwa na baadae kurejeshwa mwaka 2017/2018 (Shilingi 2,600,000/=) zilitumika katika mradi wa ujenzi wa msingi (foundation) ya vyoo matundu manne katika Skuli ya Uondwe Msingi amba ulitumia Shilingi 2,500,000/= kwa mwaka 2017/2018 na mradi huo umekamilika.

Katika uchambizi wa matumizi ya fedha za mradi wa usambazaji maji Mkanjuni (Mtambwe) Kamati ya P.A.C imebaini yafuatayo;-

i. Ununuzi wa bomba na vifaa vya well head Shilingi 5,917,700/=
ii. Ununuzi wa pampu na mota ya 7 kw shilingi 7,788,000/=
iii. Uwekaji w umeme Shilingi 4,578,280.42/=

Jumla Shilingi 18,283,980.42/=

Fedha za ziada Shilingi 933,980,.42/= zilitolewa na Mamlaka ya Maji (ZAWA) ili kukamilisha kazi hiyo.

Kamati ilikagua nyaraka mbali mbali za mradi na matumizi ya mradi huo zikiwemo kumbukumbu za kikao cha tarehe 4/8/2017 ambacho ndicho kilichoidhinisha mradi huo, Kamati pia ilikagua Fomu za miradi, barua ya maombi yam rai (ya tarehe 25/7/2017) stakabadhi ya ZAWA yenye nambari B 55875 ya tarehe 5/9/2017 yenye jumla ya shilingi 17,350,000/= kwa ajili ya mradi huo wa maji.

Kamati imeridhika na nyaraka hizo. Vile vile Kamati ilipata nafasi ya kukagua ene lililotelekezwa mradi huo na kuelezwa kuwa awali kisima kilichimbwa na mradi wa visima vilivyochimbwa kupitia Ras el Hema na baadae Mfuko wa Jimbo ambapo Kamati ilipofika katika maeneo ya Mradi (Mkanjuni Kivumoni) ilishuhudia huduma ya maji ikipatikana kwa wananchi . Kwa ujumla Kamati imeridhika na utekelezaji wa mradi huu.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Viongozi wa Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wahakikishe kuwa matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo yanafanyika kikamilifu kwa leng lililokusudiwa na kwa wakati unaohusika ili kundoa usumbufu kwa wananchi .
2. Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo zinapaswa kutoa taarifa kwa ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais pindi zinapotokea changamoto za utekelezaji au matumizi ya miradiya Mfuko wa Jimbo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | KOJANI | 20,000,000 | Kumaliza skuli ya Chwale msingi,kupiga plasta na apron na floo vyumba vitatu | Chwale | 6,212,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Uwekaji wa madirisha skuli ya kojani na utiaji wa Milango | Mpambani | 4,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uwekaji umeme kijiji cha Kage Kiuyu | Minungwini | 5,054,435 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa tuta (njia) kutoka kojani hadi Mpambani | Kojani | 1,500,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa banda la kusuburia abiria Likoni Kojani | Chwale | 2,500,000 | Mradi umekamilika |

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Kojani

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kojani ilikiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= ambazo zilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo ya Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilkagua nyaraka za matumizi ya miradi pamoja na nyaraka nyenginezo zinazohusiana na utekelezaji wa miradi hiyo zikiwemo stakabadhi za matumizi na kubaini kutokuwemo kwa Fomu ya Utekeleaji wa Miradi ambapo ilielezwa kuwa zamani Kamati ya Mfuko wa Jimbo ilikuwa haijapata Fomu za Utekelezaji wa Miradi lakini miaka iliyofuata Fomu hizo ziliweza kupataikana. Hata hivyo, kwa ujumla Kamati ya PAC iliridhika na nyaraka hizo.

Aidha Kamati ilipata nafasi ya kutembelea madarasa matatu ya Skuli ya Msingi Chwale pamoja na banda la kusubiria abiria la Likoni.Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5. | WETE | 20,000,000 | Uwezekaji wa mabanda mawili skuli ya sekondari Chasasa | Utaani | 3,780,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununuzi wa mashine ya umwagiliaji majieneo la Weni | Limbani | 550,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununuzi wa kokoto na kifusi | Mtemani | 380,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Mchango wa usafishaji karo | Limbani | 500,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ununuzi wa mpira wa maji Msera | Limbani | 300,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa msingi wa skuli ya maandaliz i Tungamaa. | Limbani | 7,862,000 | Mradi haujakamilika |
| | | | Uwezekaji wa mabanda mawili skuli ya sekondari ya Chasasa | Utaani | 3,780,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Mradi wa ununuzi wa fanicha(viti na meza) | Utaani | 5,000,000 | Mradi haujakamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Wete

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Wete ilikiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= ambazo zilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo ya Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC umebaini kuwa Mradi wa uezekaji wa madarasa mawili Skuli ya Sekondari ya Chasasa imeainishwa mara mbili katika Ripoti ya Mdhibiti (Mradi nambari 1 na Mradi nambari 7). Hivyo Mradi nambar saba (7) ufutwe. Aidha Mradi wa ujenzi wa msingi wa Skuli ya Maandalizi Tungamaa ulioainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti kuwa haujakamilika sasa umekamilika ingawa ulihamishiwa katika eneo jengine.

Kamati ya P.A.C ilikagua nyaraka mbali mbali zinazohusiana na utekelezaji pamoja na matumizi ya miradi hiyo. Zikiwemo fomu za miradi, mkataba wa upelekaji mawe gari 15 na mchanga gari 6 kwa ajili ya ujenzi wa msingi (foundation) wa Skuli ya maandalizi Tungamaa (gari 15 za mawe Shilingi 2,100,000/= ). Pia Kamati ilikagua stakabadhi mbali mbali za malipo pamoja na kumbukumbu za kikao cha tarehe 24/12/2017 ambacho kiliidhinisha miradi mbali mbali iliyotekelezwa mwaka 2016/2017. Katika uchunguzi wa matumizi ya fedha za miradi ilibainika kuwa jumla ya Shilingi 528,000/= zilitumika kukidhi gharama za ufuatiliaji wa miradi hiyo. Kamati pia ilipata nafasi ya kutembelea Skuli ya Sekondari ya Chasasa ili kuona mabanda mawili yaliyoezekwa ambapo kwa ujumla Kamati imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Micheweni (2016/2017)

<table>
<tr><th>Nam</th><th>Jimbo</th><th>Fedha zilizoingizwa</th><th>Mradi</th><th>Shehia</th><th>Fedha Zilizotumika</th><th>Hatua ya Utekelezaji</th></tr>
<tr><td rowspan="2">1.</td><td rowspan="2">Tumbe</td><td rowspan="2">20,000,000</td><td>Uezekaji wa vyumba viwili vya madarasa skuli ya Tumbe Sekondari</td><td>Tumbe</td><td>5,600,000</td><td>Mradi umekamilika</td></tr>
<tr><td>Uendelezaji wa mradi wa skuli ya Chimba (Kuezeka)</td><td>Chimba</td><td>13,400,000</td><td>Mradi umekamilika</td></tr>
<tr><td colspan="7">Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Tumbe,<br><br>Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Tumbe ilikiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutoka serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi miwili kama ilivyoidhinishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.<br><br>Uchunguzi wa Kamati ya PAC<br><br>Kamati ya PAC Imekagua nyaraka mbaimbali za matumzi na za utekelezaji wa miradi hiyo zikiwemo stakabdhi, na nyaraka nyenginezo na kubaini kuwa Kamati ya Mfuko wa Jimbo haikuwa na Fomu ya Utekelezaji wa Miradi.<br><br>Aidha, Kamati ya PAC ilipata nafasi kukagua madarasa mawili yaliyoezekwa katika Skuli ya Tumbe Sekondari na pia kukagua madarasa manne manne na mbili yaliyoezekwa katika Skuli ya Msngi Chimba. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na matumizi na utekelezaji wa miradi pamoja na uwekaji mzuri wa kumbukumbu za miradi hiyo.</td></tr>
<tr><td>2.</td><td>Konde</td><td>20,000,000</td><td>Ujenzi wa choo Skuli ya Kiuyu Kipangani</td><td>Kifundi</td><td>2,661,400</td><td>Mradi Umekamilika</td></tr>
</table>

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Uendelezaji wa ujenzi skuli ya Maandalizi Konde | Konde | 4,916,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Kusaidia maji kijiji cha Ujinga Basi | Konde | 1,972,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Umeme kijiji cha Kifundi kiumbe mzito | Kifundi | 3,000,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Kusaidia Theatre Hospitali ya Micheweni | Majenzi | 5,000,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Konde,

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Tumbe ilikiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutoka serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi miwili kama ilivyoidhinishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

1. Wajumbe wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo kutumia shilingi 150,000,000 kwa ajili ya posho ya vikao vya Kamati hiyo kwa sababu iliyoelezwa kuwa hawakujua awali kiwango cha kulipana ba hawakujua muongozo wake.
2. Kamati imegundua kwamba kuna kutofautiana kati ya Mwenyekiti wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni na kuonnekana kila mmoja kati yao kuhisi fedha hizo ana mamlaka nazo (ni zake). Aidha, kuna dhana ya kuonekana fedha za Mfuko wa Jimbo kama zimedhibitiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri.
3. Kamati ya Mfuko wa Jimbo haikuwa na fomu za utekelezaji wa miradi
4. Baadhi ya stakabadhi (risiti) kutokuwa na Tin Number. Hili limebainika Katika mradi wa kuisaidia shilingi 5,000,000 Jumuiya ya Maendeleo ya Jimbo la Konde kwa ajili ya kujenga vyoo na 'apron,

Aidha, Kmati ya PAC ilipata nafasi ya kukagua vyoo katika Skuli ya Kiuyu Kipangani pamoja na

mabanda mawili ya Skuli ya Maandalizi ya Konde.. Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Wenyeviti na Katibu wa Kamati za Mfuko wa Jimbo wawe na ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Jimbo.

ii. Kamati za Mfuko wa Jimbo zifanye ununuzi wa bidhaa katika maduka yenye risiti zenye tin Number amabzo ni uthibtisho wa maduka hayo kulipa kodi za Seriikali.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | Micheweni | 20,000,000 | Uendelezaji wa ujenzi wa ukumbi wa mitihani Skuli ya Kiuyu | Kiuyu | 8,755,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Uendelezaji wa Ujenzi wa Maktaba Skuli ya Micheweni | Majenzi | 4,160,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Uchangiaji katika mradi wa | Mapofu | 4,040,000 | Mradi Umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | uchimbaji wa kisima cha maji-Kironjo | | | |
| Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Micheweni,<br><br>Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Micheweni ilikiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutoka serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbali mbali kama ilivyoidhinishwa katika ripoti ya Mdhibiti.<br><br>Uchunguzi wa Kamati ya PAC<br><br>Kamati ya P.A.C imebaini kuwa katika mradi wa uendelezaji wa ujenzi wa ukumbi wa mitihani Skuli ya Kiuyu ambao awali ulitumia shilingi 8,755, 000, lakini kutokana na kutokidhi kwa fedha hizo ililazimu kuongeza shilingi 874,000/= kwa ajili ya kuongeza mbao futi 647.5 ili kufanikisha kazi ya uezekaji na kufanya jumla ya fedha zote zilizotumika katika mradi huu kufikia shilingi 9,629,000/=.<br><br>Kazi zilizofanyika katika mradi huu ni ufungaji wa linta, kuongeza matofali kozi mbili juu ya linta, kuweka bim na nguzo na uezekaji.<br><br>Aidha, Kamati ya P.A.C imebaini kuwa jumla ya shilingi 2,171,000/= zimetumika kwa ajili ya uendeshaji wa miradi yote kwa ujumla. Katika mwadi wa uendelezaji wa maktaba ya Skuli ya msingi ya Micheweni, kazi zilizofanyika ni kufanya makabati, kupiga plasta, kuweka milangi mitatu na madirisha manne pamoja na kutia sakafu, rangi na chipping.<br><br>Kamati ya P.A.C ilikagua nyaraka mbali mbali za matumizi ya miradi yote iliyotekelezwa pamoja na myaraka nyengine zilizotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo zikiwemo fomu za miradi na kumbukumbu za kikao cha tarehe 15/4/2017 cha Kamati ya Maendeleo ya Jimbo la Micheweni ambacho ndicho kilichoidhinisha miradi.<br><br>Kamati ya P.A.C imepata nafasi ya kutembelea baadhi ya miradi iliyotekelezwa na kwa ujumla imeridhika na utekelezaji ya miradi hiyo. | | | | | | |
| 4. | Wingwi | 20,000,000 | Usambazaji wa maji kijiji cha Sebudawa | Mjini wingwi | 2,500,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Usambazaji wa maji kijiji cha Mapofu | Mapofu | 2,000,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Uchimbaji wa kisima kijiji cha Kilindini | Mapofu | 1,700,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa skuli ya maandalizi ya Sizini | Sizini | 4,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Kupeleka umeme kwa hatua ya nguzo Mbili | Mjini Wingwi | 2,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa vyoo vitano skuli ya Wingwi Maandalizi | Njuguni | 4,000,000 | Mradi umekamilika |

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KWA MKOA WA KUSINI PEMBA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017 Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Chake Chake

| Nam. | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 11. | OLE | 20,000,000 | Ukarabati chumba cha maktaba skuli ya Ole Msingi | Ole | 4,222,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ukarabati chumba cha kompyuta Skuli ya Ole Msingi | Ole | 3,666,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Kupeleka umeme vitongoji Vumba | Vitongoji | 1,370,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ujenzi wa vyumba viwili skuli ya Uwandani | Uwandani | 4,500,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Upelekaji wa umeme Vikunguni Mtumbwi | Ng'ambw A | 3,380,469 | Mradi umekamilika |
| | | | Utiaji plasta na sakafu Skuli ya Sekondari ya Vitongoji | Vitongoji | 1,857,931 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya PAC

Kamati ya Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo la Chonga imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali za matumizi na zile zinazohusiana na utekelezaji wa miradi zikiwemo Fomu za Miradi na stakabadhi za malipo nakubaini kuwa mikataba kutoambatanishwa na risiti husika (uwekaji usioridhisha wa kumbkumbu za miradi)

Pia, Kamati ilipata nafasi yakutembelea Skuli ya Msingi Ole na kubaini kuwa kutokana na upungufu wa madarasa chumba cha Maktaba kinatumika kama darasa na chumba cha 'compyuter' kimekuwa ghala ambapo kompyuta zilizohifadhiwa hazitumiki. Sambamba na hilo dari ya chumba cha Maktaba amabacho kwa sasa ni darasa imeharibiwa na wanafunzi.

Mependekezo ya Kamati ya PAC

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Ni busara kuwepo na nidhamu hususan katika miradi iliyoibuliwa na wananchi ili isiweze kubadilishwa matumizi yake.<br>2. Kompyuta zilizohifadhiwa zianze kutumiwa na wanafunzi ili kuwaongezea wigo wa kutambua masuala ya kiteknolojia.<br>3. Kilichokuwa chumba cha Maktaba ambapo kwasasa kinatumika kama darasa kiwekewe milango ili kuzuia wanafunzi kuingia ovyo ndani na kufanya uharibifu wa dari. | | | | | | |
| 12. | CHONGA | 20,000,000 | Upelekaji wa Maji safi na Salama katika kijiji cha Tundauwa | Kilindi | 10,000,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Uwekaji wa kifusi katika barabara ya Chanjanja wiri Kisahanini | Matale | 2,600,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uwekaji wa kifusi katika barabara ya Kilindi Tunguni | Kilindi | 2,600,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Utengenezaji na utiaji wa madirisha kumi Skuli ya Msingi Pujini | Pujini | 888,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Upelekaji wa umeme Kijiji cha Pujini Bora Hatima | Pujini | 3,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Maendeleo ya Jimbo la Chonga

Kamati ya Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo la Chonga imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa gharama kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:

1. Kamati ya PAC kuagua koip za stakabadhi kwa kuwa Stakabadhi halisi (Risiti 'original') hazikupatikana kwa ukaguzi kwa maelezo kwamba zimepotea kutokana na kuhama kwa Ofisi ya Baraza la Mji Chake Chake na Kuhamia Ofisi mpya .Miongoni mwa stakabadhi hizo ni stakabadhi ya ZAWA ya usambazaji maji, stakabadhi za uwekaji umeme kutoka ZECO hawakuwa nazo badala yake walikuwa na BOQ.
2. Kamati ya Mfuko wa Jimbo zaidi ya watu 10 wamelipana posho ya vikao Posho zaidi

ya milioni moja.

Aidha, Kamati ya PAC, ilipata nafasi ya kukagua mradi wa umeme Pujini amabao ulijuisha uwekaji wa nguzo na waya na kuridhika na mradi huo. Vile vile, Kamati iliukagua Mradi wa Maji Tundauwa.na kubaini kuwa mipira ya maji katika baadhi ya maeneo imeanza kupasuka.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Chonga ihifadhi vizuri vielelezo vyake hususan kumbukumbu halisi za utekelezaji wa miradi.
2. Kamati iweke utaratibu wa kudai risiti kwa Taasisi za Serikali inazofanya kazi nao.
3. Kamati itumie vizuri fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwani malengo ya fedha hizo badala ya wajumbe kulipana posho zaidi ya kile kiwango cha shilingi milioni moja kilichowekwa kwa mujibu wa taratibu za Mfuko wa Jimbo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | WAWI | 20,000,000 | Ujenzi wa Skuli ya Msingi Furaha | Mvumoni | 3,073,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uendelezaji wa skuli ya Ditia | Mgogoni | 6,327,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Utengenezaji wa viti sitini na meza thelathini Skuli ya Maandalizi Machomane | Wara | 9,600,000 | Mradi haujakamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Wawi

Kamati ya Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo la Wawi imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa gharama kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imekagua nyaraka mbalimbali za matumizi na za utekelezaji wa miradi zikiwemo Fomu za Miradi, baadhi ya Stakabadhi za malipo na mikataba mmbalimbali ambapo Kmati ya PAC imebaini kuwa Utengenezaji wa viti na meza umekamilika ana walikabidhiwa mwezi wa Disemba =, 2018 mbapo wakai alipopiata Mkaguzi wa Mdhibiti vilikuwa bado hajakamilika ingawa risiti za kazi hiyo haikupatikana kwa ukaguzi. Aidha Kamati ya PAC ilikgua miradi iliyotekelezwa na kuridhika nayo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati za Mfuko wa Jimbo zidai risiti kwa malipo ya kazi wanazofanyiwa badala ya kutegemea gharama zilizoainishwa katika mikataba peke yake.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | ZIWANI | 20,000,000 | Upelekaji wa maji safi na Salama | Ndagoni | 10,000,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ndagoni | | | |
| | | | Upigaji plasta ,pamoja na sakafu skuli ya Kwale | Kwale | 9,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Ziwani

Kamati ya Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo la Ziwani imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi miwili kwa gharama kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya P.A.C imebaini yafuatayo:-

1. Kuwepo kwa matumizi ya vifaa vya mradi wa maji – Ndagono (shilingi 10,000,000/=) yalivyofanyika kinyume na utaratibu. Ankara (invoice) iliyowasilishwa katika Kamati ya P.A.C inaonesha gharama za vifaa hivyo ni shilingi 9,430,000/= na hakukuwa na uthibitisho wa matumizi ya fedha zilizobakia kati ya shilingi 10,000,000 zilizotumika (Ankara namba 1833 ya tarehe 8/5/2017.
2. Kuwepo kwa matumizi ya Shilingi 344,717 zilizotumika kwa ajili ya posho ya Katibu wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Ziwani (Ndugu Iddi Said Salim) kwa ajili ya safafi ya Dar es Salaam kufuatilia ununuzi wa mshine ya maji. Matumizi hayo ni kinyume na sharia ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Nambari 4 ya mwaka 2012 inayoelekeza kuwa fedha za miradi ya Maendeleo ya Jimbo zitumike katika miradi hiyo ya wananchi.
3. Hakuna uthibitisho wa hati ya malipo au subvoucher ya matumizi kwa ajili ya malipo ya safari ya Dar es Salaam.
4. Katika uchunguzi wa Mkataba wa ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Kwale baina ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Ziwani na Bwana Amour Hamad Mussa (Mwajiriwa/mjenzi) uliotiwa saini tarehe 1//2017 kw gharama ya kazi Shilingi ;9,000,000/= imebainika kuwa mjenzi kulipwa fedha nyingi Zaidi katika awamu ya kwanza tu ya malipo ambapo kwa mujibu wa mkataba huo mjenzi alitakiwa kulipwa jumla ya Shilingi 8,000,000/= kama malipo ya awamu ya kwanza. Jambo hili ni la hatri na linaweza kuibua changamoto kubwa katika utekelezaji wa mikataba.

Kamati pia ilikagua madarasa matatu na ofisi mbili za Skuli ya Kwale pamoja na mradi wa

maji Ndagoni na kuridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo zifanye matumizi ya fedha za miradi ya Mfuko wa Jimbo kwa kufuata Sheria na taratibu zilizopo.
2. Katika uingiaji wa mikataba mbali mbali Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ziandae vizuri kipengele cha utaratibu wa malipo kwa kuhakikisha kuwa kunawekwa masharti ya kulipa fedha kidogo kidogo katika miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5. | CHAKE CHAKE | 20,000,000 | Ujenzi wa vyoo na uungaji wa maji skuli ya Madungu | Madungu | 9,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ukarabati wa vyoo na ujenzi wa hozi la kuhifadhia maji katika skuli ya Michakaini | Msingini | 10,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Chake Chake

Kamati ya Mfuko wa Jimbo Chake Chake ilikiri kupokea Shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi miwili kama ilivyoaonishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.na Mkaguzi Mkuu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali za matumizi ya fedha za miradi na utekelezaji wa miradi hiyo zikiwemo Fomu za Miradi na stakabdhi za malipo ambapo Kamati iliridhika nazo. Aidha, Kamati ya PAC imekagua vyoo skuli ya Michakaeni. Kwa ujumla Kmati ya PAC

| |
|---|
| imerdhika na matumizi ya fedha za miradi pamoja na utkelezaji wa miradi hiyo |

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Mkoani Mwaka 2016/2017

| Nam. | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | CHAMBANI | 20,000,000 | Ujenzi wa barabara ya Wambaa kwa Azani | Wambaa | 18,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Mchango wa madawati | Wilaya ya Mkoani | 1,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Chambani

Kamati ya Mfuko wa Jimbo Chambani ilikiri kupokea Shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi miwili kama ilivyoaonishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya P.A.C ilielezwa kazi mbali mbali zilizofanyika katika utekelezaji wa kila mradi kama ifuatavyo:-

1. Mradi wa ukarabati wa barabara ya Wambaa kwa Azani uliogharimu Shilingi 18,000,000/= uliohusisha kazi za kuichonga barabara na kuweka kifusi pamoja na kutengeneza njia za kupita maji ya mvua.
2. Mchango wa madawati kwa skuli ya Wilaya ya Mkoani ulihusu kuchangia ununuzi wa madeski ili kushirikiana pamoja na wadau wengine kuwafanya wanafunzi wa Wilaya ya Mkoani kusoma kwenye mazingira ya kuridhisha.

Kamati ilikagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji wa miradi hiyo zikiwemo kumbukumbu za kikao cha tarehe 25/6/2017 kilichojadili na kuidhinisha miradi hiyo. Aidha, Kamati ilikagua nyaraka za matumizi ya miradi hiyo.

Kwa ujumla, Kamati ya P.A.C imeridhika na utekelezaji pamoja na matumizi ya fedha za miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | MKOANI | 20,000,000 | Ukamilishaji wa nyumba ya Daktari | Makombe ni | 7,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa banda la vyumba vitatu Skuli ya Mtuhaliwa | Changaaweni | 4,555,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa vyoo 12 Skuli ya Sekondari Chokocho | Chokocho | 6,604,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Mchango wa madawati | Wilaya ya Mkoani | 1,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Mkoani ,

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mkoani ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa Miradi ya Jimbo la Mkoani kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya P,A,C ilielezwa kazi mbali mbali zilizofanyika katika utekelezaji wa kila Mradi kama ifuatavyo:-

1. Katika Mradi wa ujenzi Skuli ya Msingini Mtuhaliwa uliotumia Shilingi 4,555,000/= kazi zilizofanywa ni ujenzi wa matofali, na nguzo za zege hatua ya GEBO kwa vyumba vitatu vya madarasa.
2. Katika Mradi wa vyoo 12 vya Skuli ya Sekondari Chokocho uliotumia Shilingi 6,600,000/= kazi zilizofanywa ni kuendeleza ujenzi kwa kunyanyua matofali kutoka chini hadi kuezeka, kuweka mfumo wa maji safi na maji machafu na kujenga mashimo na makaro ya maji machafu.

3. Kwenye mradi wa umalizaji wa nyumba ya Daktari ya Makombeni iliyogharimu Shilingi 7,000,000/= , kazi zilizofanywa ni kupiga plasta sakafu, kujenga Aproni na shimo la maji machafu, kujenga dari (silingi), milango na nyaya za mbu, kutia umeme na rangi na kuweka mfumo wa maji safi.

4. Mchango wa madawati kwa skuli za msingi za Wilaya ya Mkoani – Shilingi 1,000,000/= zilitumika kugharamia ununuzi wa madawati kwa skuli za Wilaya ya Mkoani.

Kamati ilikagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji wa Miradi zikiwemo Fomu za Miradi husika na kumbukumbu za kikao cha tarehe 5/5/2017 kilichoidhinisha miradi iliyotekelezwa.

Aidha, Kamati imekagua nyaraka mbali mbali za matumizi ya miradi hiyo pamoja na kukagua baadhi ya miradi iliyotekelezwa ukiwemo mradi wa nyumba ya daktari ya Makombeni iliyojengwa kutokana na fedha hizo ambayo imekamilika ingawa ilikuwa haijahamiwa , Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi pamoja na matumizi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | MTAMBILE | 20,000,000 | Ujenzi wa banda la Skuli ya Minazini | Minazini | 7,240,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Skuli ya maandaliz i Kukuu | Kukuu | 7,584,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Skuli ya msingi Mjimbini | Mjimbini | 3,176,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Mchango wa madawati | Mkoani | 1,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mtambile

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mtambile ilikiri kupokea shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini na kutekeleza miradi mbali mbali katika Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali .

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilikagua nyaraka mbali mbali zinazohusiana na utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo kumbukumbu za kikao cha tarehe 15/6/2017 kilichoidhinisha miradi iliyotekelezwa. Aidha, Kamati ilikagua nyaraka za matumizi ya miradi hiyo pamoja na kukagua Skuli ya msingi Minazini ambayo ilianza kujazwa kifusi na kujengwa kwa matofali .

Aidha, Mbunge pia alisaidia ujenzi wa Skuli hiyo na sasa ujenzi umekamilika na wanafunzi wanasoma vizuri.

Kamati ya P.A.C imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na matumizi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji wa miradi husika.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | KIWANI | 20,000,000 | Mradi wa kukamilish a ujenzi wa skuli ya sekondari Kiwani, Kijiji cha Kendwa | Kendwa | 14,700,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Mradi wa kusambaz a mipira ya maji safi, Kijiji cha Tomondo | Mwambe | 500,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Mradi wa ujenzi wa skuli ya maandalizi Chanjaani | Jombwe | 3,500,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kiwani.

Kamati ya Kfuko wa Maendeleo umekiri kupokea jumla ya Shiliongi 20,000,000/= ambazo zilitumika katika utekelezaji wa miradi mitatu ifuatayo:-

1. Umalizaji wa ujenzi wa banda la madarasa ya kusomea na ghala Skuli ya Kiwani uliotumia Shilingi 14,700,000/=
2. Kusaidia mipira ya kusambazia maji Tomondwe uliogharimu Shilingi 500,000/=
3. Kuchangia madawati kwa Skuli ya Wilaya ya Mkoani uliogharimu Shilingi 1,000,000/=

Uchunguzi wa Kamati ya P.A.C

Kamati ya P.A.C ilielezwa juu ya kazi za utekelezaji wa kil mradi kama ifuatavyo:-

1. Kwenye mradi wa umalizaji wa banda la Skuli ya Kiwani, kazi zilizotekelezwa ni kujenga ukanda (linta), kuta plasta, kupaka rangi, kuezeka, kuweka madirisha na milango, kutia umeme na dari , Mradi umekamilika.
2. Katika mradi wa usambazaji maji Tomondwe kazi zilizofanyika ni ununuzi wa mipira maji

roll nne (4) kwa kiwango cha ¾ , wananchi kujitolea kuchimba na kugharamia uunganishaji wa maji katika nyumba zao. Mradi umekamilika.

3. Kwenye kuchangia madawati, ulikusudia kuunga mkono juhudi za Wilaya katika Kampeni ya kutatua changamoto ya uhaba wa madawati.

Kwa ujumla Kamati ya P.A.C imeridhika na utekelezaji wa miradi ya Jimbo hilo kwa mwaka 2016/2017.

| Nam | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha Zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Amani | 20,000,000 | Uchimbaji wa kisima,mita ya umeme na uwekaji tenki | Amani | 10,475,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Uchimbaji wa kisima, mita ya umeme na uwekaji tenki | Kilima hewa juu | 10,475,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Amani

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Amani imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambaz Zimetumika katika kutekeleza miradi miwili kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa kazi ya uchimbaji wa kila kisima iligharimu jumla y shilingi 9,000,000 ambapo stakabadhi za matumizi yote kwa ujumla zinaonesha matumizi ya shilingi 22,000,000,000.

Aidha, Kamati ilikagua nyaraka za miradi zikiwemo fomu za miradi pamoja na nyaraka za matuumzi ya f za miradi hiyo na kuridhika nazo.
Vilevile, Kamati ya PAC ilipoata nafasi kukagua Visima pamoja na matenki katika meneo ya Kilimahewa Amani na kubani yafutayo:-

Katika Kisima cha Kilimahewa Juu ambacho kimefungwa vyema na mifereji, Kamati ya PAC imeridhika upatikananji wa maji katika kisima hicho.

Kwa upande wa Kisima cha Amani wananchi wa eneo hilo waliiambia Kamati ya PAC kuwa kisima hicho hakipandishi maji na hakifanyi kazi kwa kuwa kimeingiam changa na kinahitaji marekebisho, ingawa aliy Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Mfuko alieleza kuwa hakuwa na taarifa juu ya tatizo hilo.

Mapendekezo ya Kamti ya PAC

Kamati za Mfuko wa Jimbo zilizopo zianadae mpango mzuri utakaohakikisha uendelezwaji mzuri wa miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo mara baada ya Wenyekiti wa Kamati za Mfuko wa Jimbo wanapokosa nafasi ya uwakilishi ili miradi hiyo iwe na tija endelevu.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Chumbuni | 20,000,000 | Ukarabati madarasa 2 na ofisi ya walimu skuli ya Chumbuni | Chumbuni | 5,838,640 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ununuzi wa pampu,mipira na tenki la lita 5000 naUjenzi wa daraja | Karakana | 14,164,484 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chumbuni

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chumbuni imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazozimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa miradi iliyotekelezwa katika Jimbo hilo kwa mwaka 2017/2018 ni hii ifuatayo:

i. Ukarabati wa madrasa mawili na Ofisi ya walimu katika Skuli ya Chumbuni ambo ulihusisha

uezuaji na uezeakji pamoja na upigaji plasta

ii. Usamabazaji wa maji na ununuzi wa pump"ya maji

iii. Ujenzi wa daraja – Karakana

Kamati ilikagua nyaraka za miradi zikiwemo Fomu za miradi pamoja na nyaraka za matumizi ya miradi hiyo ambapo kwa ujumla iliridhika nazo.

Aidha, Kamati ya PAC ilitembelea madarasa ya Skuli ya Skuli ya Chumbuni yaliyofanyiwa ukarabati na kuridhika nayo.
Aidha Kamati ya PAC ilitembelea eneo lililojengwa daraja la Krakana kubaini kuwa daraja hilo limebomoka ambapo ilielezwa kuwa daraja hilo lilibomoka kutokana mvua kubwa zilizonyesha mwaka 2018 na halikuwahi kutumika. Vilevile Kamatai ilielezwa kuwa ingawa Mfuko wa Jimbo ulitumia shilingi 7,000,000 katika mradi huo lakini kwa ujumla mradi huo ulighjarimu jumla ya shilingi 31,000,000.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | Jang'ombe | 20,000,000 | Ujenzi wa Mnara wa Kisima cha maji Matarumbeta | Jang`ombe | 3,434,500 | Mradi Umekamilik a |
| | | | Ujenzi wa Mnara wa Kisima cha maji | Kwalinatu | 4,215,500 | Mradi Umekamilika |
| | | | Manunuzi ya vifaa vya usafi wa Mazingira | Kwalinatu | 369,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Fedha zilizobakia hadi ukaguzi unakamilika | | 10,981,000 | Fedha haijatumika hadi ukaguzi Unakamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Jang'ombe

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Jimbo la Jang'ombe ilkiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti

Uchunguzi wa Kamati ya PAC
Kamati ya PAC imebaini kuwa shilingi 10,000,000 zilijumuishwa pamoja na fedha nyengine ambapo Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo hilo alinunua basi la Jimbo lililogharimu zaidi ya shilingi 30,000,000. Hata hivyo, wakati Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti anafanya Ukaguzi wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko alikuwa hajaziwasilisha nyaraka za ununuzi wa basi hilo kwa Katibu wa Mfuko.

Katika ukaguzi wa nyaraka za matumizi ya miradi hiyo, ilionekana kuwa nyaraka za ununuzi wa basi whilo ni za mwaka 2016

Aidha, katika ukaguzi wa miradi hiyo. Kamati ilibaini kuwa basi hilo lenye namba za usajili Z575 GV limeahiribika bteri,haina ryhysa ya njia (Road licence) na Bima.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati za Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo zilizopo ziandae utaratibu wa kuiendeleza miradi iliyoanzishwa na Kamati za Mfuko wa Jimbo zilizopita ili kuepusha upotevu wa gedha za Serikali na kuifanya mirdai hiyo iwe endelevu.
2. Wenyeviti wa Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wahahakikishe kuwa nyaraka zote zinazohusiana na utekelezaji pamoja na matumizi ya miradi ya Mfuko huo zinawasilishwa kwa Katibu wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo badala ya kukaa nazo wao.
3. Kamati za Mfuko wa Jimbo zinashauriwa kuwa pindi fedha zinpopatikana kwa wakati, ni vyema kwa matumizi ya miradi ya Mfuko wa Jimbo yakafanywa katika mwaka wa fedha husika pamoja na kuhakikisha kuwa nyaraka za matumizi zinaendana na mwaka halisi wa utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | Kikwajuni | 20,000,000 | Ununuzi wa gari Mazda Titan | Jimbo zima | 11,500,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ununuzi wa gari Nissan Atlas | Jimbo zima | 11,500,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kikwajuni
Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kukwajuni alikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo amabazo zilitumika katika ununuzi wa gari mbili kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti

Uchunguzi wa Kamati ya PAC
Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mabalimbali zinazohusiana na utekelezaji na matumizi ya miradi hiyo pamoja na kuzikagua gari husika (Nissan Truck Z 584 JG na Titan Z 593 JG) Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5. | Kwahani | 20,000,000 | Ujenzi wa Mabanda mawili ya Madrasa. | Sebleni | 7,814,330 | Mradi Umekamilika |
| | | | Umalizwaji wa mnara wa maji | Sebleni | | |
| | | | Umalizwaji wa mnara wa maji, Kwaalimsha Bondeni. | Kwaalimsha | 11,079,840 | |
| | | | Ununuzi wa matank mawili (2) yenye uwezo wa lita 5000. | | | Mradi Unaendelea |
| | | | Ujenzi wa mnara wa maji Kwaalimsha Juu. | | | |

Majibu ya Kmati ya Mfuko wa Jimbo la Magomeni

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Magomeni imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zilitumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti

Uvhunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mabalimbali za matumizi na za utekeleaji wa miradi miradi zikiwemo Fomu za Miradi, Stakabadhi za malipo pamoja na kumbukumbu mbalimbali za vikao ambapo Kamati ya PAC imeridhika na nyaraka hizo. Htahivyo Kamati ya PC imebaini kuwa hakuna mashirikiano mazuri na Manispaa ya Mjini na Kmati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo

Kamati ya PAC ilikagua miradi iliyotekelezwa vikiwemo visima vya Magomeni (Mzalendo) na kisima vha Magomeni Barabara (karibu na msikiti wa Mchekeni. Kutokana na Ukaguzi huo Kamati imegundua kuna kisima cha maji kiliopo Magomeni barabarani kinahitaji kusafishwa lakini huduma hiyo hakijafanyiwa ingawa maji yanapatikana.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati za Mfuko wa Jimbo zilizopo hivi sasa zitataue changamoto zinzoikabili miradi muhimu iliyoanzishwa na Kamati za Mfuko wa Jimbo zilizopita ikiwemo miradi ya maji ili miradi hiyo iweze kutoa tija endelevu kwa wananchi

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| 6. | Magomeni | 20,000,000 | Ukarabati wa Kisima | Nyerere | 4,680,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ukarabati wa Kisima | Kwa Mtumwajeni | | Mradi Umekamilika |
| | | | Ununuzi wa Gari ya Jimbo: Z 141 JN, Mitsubidh Canter, White | Jimbo zima | 15,320,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Magomeni

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Magomeni.iloikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Jimbo hilo

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 7. | Malindi | 20,000,000 | Ununuzi wa Mashineya Fotokopi Skuli ya Hamamni. | Kiponda | 2,950,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Vyarahani kwa ajili ya mafunzo ya Ujasiriamali Skuli ya Forodhani. | Kiponda | 2,005,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ununuzi wa Komputa SKuli ya Mkunazini. | Mkunazini | 1,950,000 | Mradi Umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Matengenezo Skuli ya Hurumzi. | Kiponda | 3,000,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Matengenezo ya Barabara kifusi. | Jimbo zima | 16,000,000 | Mradi haujakamilika |
| | | | Matengenezo sehemu iizoharibika mipira ya maji Gulioni na Mitiulaya. | Gulioni na Mitiulaya | 500,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Malindi

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Malindi.iloikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Jimbo hilo

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa kwa mujibu wa Fomu ya utekelezaji wa Miradi ya Jimbo la Malindi kwa mwaka 2017/2018 Jimbo hilo lilitekeleza miradi mbali mbali kama ifuatavyo:-

1. Ujenzi wa barabara kwa hatua ya kifusi Gulioni, Mwembetanga, Miti Ulaya na Malindi Shilingi 15,000,000/=.
2. Usafi wa Wadi na utunzaji wa Mazingira Wadi ya Mlandege – Shilingi 1,455,000/=.
3. Kuwapunguzia joto walimu na wanafunzi darasani Skuli ya Kajificheni – Shilingi 1,600,000/=.
4. Ununuzi wa vifaa vya maabara Skuli ya Forodhani – Shilingi 1,100,000/=
5. Ununuzi wa pump ya maji katika Skuli ya Mkunazini Shilingi 300,000/=
6. Matengenezo ya pump ya maji katika eneo la Miti Ulaya Shilingi 400,000/=

Gharama za ufuatiliajiwa Miradi – Shilingi 143,130/=

Kamati baada ya kukagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji wa Miradi zikiwemo Fomu za Miradi, BOQ ya barabara za ndani na nyaraka za matumizi zikiwemo stakabadhi za malipo mbali mbali pamoja na kutembelea baadhi ya miradi iliyotekelezwa, iliridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 8. | Mpendae | 20,000,000 | Uchimbaji wa Kisima na usambazaji maji safi na salama katika shehia ya Kilimani, Migombani na Kwa Binti-Amrani | Kilimani Migomban i Kwa Binti-Amrani | 5,015,000 | Mradi Umekamilik a |
| | | | Ukarabati wa njia za ndani - Kutoka kwa Mchina Mwisho hadi kutokea Migombani | Mpendae | | Mradi unaendelea |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mpendae

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mpendae imekiri kupokea shilingi 20,000,000 kutoka Serikalini na kuteleleza miradi mbali mbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali .

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa ukarabati wa njia za ndani uliokuwa haujakamilika wakati wa ukaguzi wa Mdhibiti, hivi sasa ukarabati huo umekamilika

Kamati ilikagua nyaraka mbalimbali za matumizi ya mirdai hiyo pamoja na kukagua njia za ndani na kisima cha Kwa bint Amrani. Kwa ajumla Kmati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 9. | Shaurimoy | 20,000,000 | Ukarabati wa njia | Kwamtipura | 16,048,000 | Mradi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | o | | | Mboriborini<br>Mkele<br>Mapinduzi<br>Shaurimoyo<br>Saateni | | umekamilika |
| | | | Uchimbaji kisima,mnara pampu na mita ya umeme | Mapinduzi | 9,750,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| | | | Ukarabati wa kisima | Shaurimoyo | | |
| | | | Uchimbaji kisima,mnara, pampu, mita ya umeme na tenki mbili za lita 5000 | Saateni | | |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa jimbo la Shaurimoyo

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Shaurimoyo imekiri kupokea kiwango hicho cha fedha kutoka Serikalini na kuteleleza miradi mbali mbali kama iliyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali .

Uchunguzi wa Kamati ya PA,C

Kamati ilkagua nyarka mbalimbali zinazohusiana na matumzi pamoja na utekelzaji wa miradi hiyo. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Magharibi A (2017/2018)

| Nam. | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5. | Bububu | 20,000,000 | Ukarabati wa Soko la Dole | Dole | 6,163,700 | Mradi umekamilika |
| | | | Utiaji wa kifusi eneo la Kizimbani, Daraja la Kijichi, Chemchem, Dole kwa | Kijichi | 9,486,300 | Mradi Umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Shabuta | | | |
| | | | Usambazaji Umeme Kijiji cha Mpopooni na Midodoni. | Mbuzini | 2,408,445 | Mradi Unaendelea |
| | | | Ujenzi wa Mnara na Ununuzi wa Tenki | Bububu | 2,824,000 | Mradi Umekamilika |
| **Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Bububu**<br><br>Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Shaurimoyo imekiri kupokea kiwango hicho cha fedha kutoka Serikalini na kuteleleza miradi mbali mbali kama iliyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.<br><br>**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**<br><br>Kamati ya PAC imekagua nyaraka mabalimbali za utekelezaji wa Miradi pamoja na za matumizi ya miradi hiyo zikiwemo Fomu za Miradi na Stakabadhi (risisti) za malipo. Aidha, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea eneo la soko Dole na kuelezwa kuwa soko hilo kwa sasa limebadilishwa na kufanywa maduka baada ya kuona kuwa soko hilo lilikuwa halifanyi kazi. Hivyo, fedha za Mfuko wa Jimbo zilitumika katika kutengeneza milango ya maduka na uwekaji wa umeme. Wakati Kamati ya PAC ilipoyatembelea maduka hayo yalikuwa yamekodishwa shilingi 50,000,000 kwa mwezi na fedha za kodi hiyo zinaingia katika Mfuko wa Shehia ya Dole. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo. | | | | | | |
| 6. | Mfenesini | 20,000,000 | Ununuzi wa Vifaa | Chuini Kihinani | 1,310,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununuzi wa matenki | Chuini. Mfenesini. | 2,200,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Mawili | | | |
| | | | Usambazaji wa Umeme Bumbwisudi | Bumbwisudi | 1,828,874 | Mradi Umekamilika |
| | | | Usambazaji wa Umeme kisima cha Chuini | Chuini | 1,825,952 | Mradi Umekamilika |
| | | | Usambazaji wa umeme kisima cha Bububu Kihinani | Kihinani | 554,952 | Mradi Umekamilika |
| | | | Usambazaji wa umeme Bumbwisudi | Bumbwisudi | 1,881,974 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ununuzi wa kompyuta, stabalaiza, printa na Fotokopi | Mfenesini | 2,900,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Usambazaji wa umeme Chuini Ziwani | Chuini | 594,482 | Mradi Haujakamilika |
| | | | Ununuzi wa mchanga gari Moja | Mwakaje | 450,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ununuzi wa Kokoto | Mwakaje | 150,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mfenesini

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mfenesini imekiri kuwepo kwa matumizi ya fedha kutoka Serikalini ambazo zilizotumika kwa ajili ya kuteleleza miradi mbali mbali ya Jimbo hilo kama

iliyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kaamti ya PAC

Kamati ya PAC ilibaini kuwa kwa ujumla na kwa mujibu Fomu ya utekelezaji wa Miradi, miradi iliyotekelezwa katika jimbo la Mfenesini kwa mwaka 2017/2018 ni kama ifuatavyo:

i. Uchimbaji Kisima Chuini kwa Asali Chungu shilingi 3,000,000
ii. Ununuzi wa matenki mawili ya ,maji – Kwa Asali Chungu shilingi 2,200,000
iii. Mipira ya Maji na vifaa vya kuungia shilingi 2,500,000
iv. Usambazaji umeme – Bumbwi sudi, Gudini Ziwani,Mkoroshoni,na Skuli ya Kihinani shilingi 6,686,208
v. Ujenzi wa Banda la Skuli ya Mwenge (Kitundu) shilingi 2,345,000
vi. Ununuzi wa vifaa vya Skuli ya Msingi Mfenesini (kopmpyuta, moja, photokopi moja, printa moja na stabliaza moja) shilingi 2,900,000

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka za matumzi ya miradi pamoja na za utekelezaji wa miradi hiyo zikiwemo Fomu za miradi, Stakabadhi za malipo pamoja na kumbukumbu za kikao cha tarehe 15/10/2018. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na miradi ya Jimbo hilo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | Mtoni | 20,000,000 | Ujenzi wa darasa la skuli - skuli ya Kibweni | Kibweni | 9,040,500 | Mradi umekamilika |
| | | | Utiaji wa Kifusi – Mshelishelini | Kibweni | 2,150,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Utiaji wa Kifusi – Mdoriani | Mwanyanya | 750,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Utiaji wa Kifusi - Mtoni hadi Mwanyanya | Mtoni | 1,200,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Utiaji wa Umeme katika Kisima cha Kiboko Yao | Sharifumsa | 573,832 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mtoni

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mtoni imekiri kuwepo kwa matumizi ya fedha kutoka Serikalini ambazo zilizotumika kwa ajili ya kuteleleza miradi mbali mbali ya Jimbo hilo kama iliyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

i. Kamati ya Mfuko wa Jimbo kutoshirikishwa katika masuala ya kifedha mbapo ilikuwa haijui kama kuna Akaunti ya Mfuko wa Jimbo na haijawahi kushirikishwa katika kutia saini Hundi yoyote.
ii. Kuwepo kwa changamoto kubwa ya kutopatikana marejesho katika Kamati ya Mfuko kwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo hilo alikuwa akitoa fedha yeye mwenyewe kupitia hundi anayojaza yeye mwenyewe.
iii. Kamati ya PAC haikuridhdika na kuwepo kwa kasoro hizo, hivyo iliamua kufanya kikao na Mhe Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo hilo (tarehe20/1/2021) na kujadiliana juu ya dosari hizo ambapo pamoja na mambo mengine. Ilibainika kuwa Mwenyekiti huyo alikuwa akimtumia Katibu wa zamani wa Mfuko wa Jimbo hilo katika masuala ya kifedha.

Aidha, Kamati ilikagua darasa ilojengwa katika Skuli ya Kibweni pamoja na njia iliyotiwa kifusi Kibweni. Katika utekelezaji wa miradi hiyo Kamati ya PAC imeridhika ingawa ilikuwa na mapendekezo juu ya tatartibu za uendeshaji wa Mfuko wa Jimbo hilo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Uuundwaji wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mtoni ufanyike kwa kufuata Sheria na tataribu za Mfuko wa Jimbo.
2. Utoaji wa fedha za Mfuko wa Jimbo ufanyike kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilipo kwa kuishikisha Kamati ya Mfuko wa Jimbo hilo.
3. Mwenyekiti na Kmati ya Mfuko wa Jimbo la Mtoni wawe karibu zaidi watendaji wanaohusika na miradi katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili kupata miongozo itakayowe
4. zesha utekelezaji bora wa miradi ya Mfuko wa Jimbo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | MTOPEPO | 20,000,000 | Ukarabati wa Kisima –Basra | Mtopepo | 3,346,500 | Mradi umekamilika |
| | | | Kuwezesha kimtaji wanakikundi cha Tujiamini | Mtopepo | 1,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ukarabati wa njia za ndani – Mina | Mtoni Kidatu | 4,872,500 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa jengo la Maabara | Kidatu Chemche m | 900,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Utiaji wa greda jimbo Zima | Jimbo zima | 2,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununnuzi wa vifaa vya usambazaji wa maji | Kidato Chemche m<br><br>Mtopepo. | 3,534,500 | Mradi unaendelea |
| | | | Ukarabati wa Kisima –Basra | Mtopepo | 3,346,500 | Mradi umekamilik a |
| | | | Kuwezesha kimtaji wanakikundi cha Tujiamini | Mtopepo | 1,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Mtopepo

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mtopepo imekiri kupokea kiwango hicho cha fedha kutoka Serikalini na kuteleleza miradi mbali mbali kama iliyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika ukaguzi wa nyaraka za matumizi na za utekelezaji wa miradi Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:

1. Fomu ya utekelezaji haikuwepo.
2. Risiti halisi (original) hazikuwepo wakati wa kikao.

3. Muhtasari wa vikao vya Kamati ya Mfuko wa Jimbo pia haukupatikana kwa ukaguzi

Kamati ya PAC ilikagua njia za ndani za Mona hadi Msikitim Magufuli pamoja na Kisima cha Basra na kuridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo zisimmamie vyema utunzaji wa vielelezo vya matumizi ya fedha za miradi

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5. | MWERA | 20,000,000 | Uchimbaji wa kisima | Kianga | 4,500,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununuzi wa vifaa vya maji Gudini pamoja na ukarabati | Mwera | 3,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa | Muembe | 7,000,000 | Mradi |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>Daraja Kinuni</td><td>Mchomeke</td><td></td><td>Umekamilika</td></tr>
<tr><td colspan="7">Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mwera<br><br>Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mwera alikiri kupkea jumla ya shilingi 20.000.000 kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali katika Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.<br><br>Uchunguzi wa Kamati ya PAC<br><br>Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali za matumizi ya fedha za miradi pamoja na nyaraka zinazohusiana na utekelezaji wa miradi hiyo zikiwemo Fomu za Miradi, na stakabadhi za malipo, Aidha, Kmati ya PAC oilipata nafasi ya kukagua baadhi ya miradi iliyotekelezwa ambapo kwa ujumla iliridhika na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo.</td></tr>
<tr><td>6.</td><td>WELEZO</td><td>20,000,000</td><td>Kamati haijafanya matumizi</td><td>Mtofaani.<br>Mchikichini.<br>Hawaii.<br>Welezo.<br>Uholanzi.</td><td>Fedha hazijatumika</td><td>Miradi haijatekelezwa</td></tr>
<tr><td colspan="7">Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Welezo<br><br>Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Welezo alikiri kupkea jumla ya shilingi 20.000.000 kutoka Serikalini kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali katika Jimbo hilo.<br><br>Uchunguzi wa Kamati ya PAC<br><br>Kamati ya PAC ilielezwa kuwa kwa mwaka wa 2017/2018 Jimbo la Welezo lilitumia jumla ya shilingi 10.000.000 kwa jili ya mradi uchimbaji wa kisima katika Shehia ya Hawaii. Mradi huo ulihusisha kazi zifuatazo:<br><br>1. Uchimbaji wa kisima – shilingi 4,500,000<br>2. Ujenzi wa mnara, vifaa na malipo ya ufundi – shilingi 2,500,000<br>3. Ununuzi wa vifaa vya maji na usambazaji wa maji kwa wananchi – shilingi2,950,000<br><br>Kwa upande wa shilingi 10,000,0 zilizobakia Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo aliwapa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi Ä”kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Hawaii lakini Halmashauri hawakuitengeneza ingawa ilielezwa kuwa suala hilo lilikuwa linashughulikiwa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA)</td></tr>
</table>

Kutokana na majibu hayo Kamati ya PAC iliandaa kikao cha pamoja tarehe 15/4/2021kati yake na Mwenyekiti wa Mfuko wa Jimbola Welezo, ZAECA na watendaji waliohusika na suala hilo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi "A" akiwemo aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Ndg Said Juma Ahmada. Hata hivyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Welezo hakuweza kuhudhuria kikao hicho. Kutokana na kikao hicho ilifahamika kuwa suala hilo lilishughulikiwa Mahakamani ambapo baadhi ya Watendaji wa Halmashauri hiyo akiwemo Ndg Said waliamriwa na Mahakama kulipa faini ya shilingi 30,000,000 ambazo tayari zimeshalipwa (Mahakama Kuu ya Zanzibar, Criminal No.1/2020 File Vote G02 C) Hivyo, shilingi 10,000,000 zimo katika shilingi 30,000,000 zilizolipwa kupitia Mahakama.

Hivyo, kwa kuwa Shilingi 10,000,000 zilirudi Serikalini kupitia Mahakama, na kwa kuwa barabara ya Hawaii imeshatengezwa na Serikali, Hivyo Kamati ya PAC haikuwa na maelezo zaidi juu fedha hizo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wenyeviti wa Kamati za Mfuko wa Jimbo wawe makini katika ufuatailiaji na usimamizi wa fedha za Mfuko wa Iimbo ili malengo yalitowekwa na Serikali ya kuanzisha Mfuko huo yaweze kufikiwa kwa ufanisi

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Magharibi B (2017/2018)

| Nam. | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha Zilizotumika | Hatua Ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | CHUKWANI | 20,000,000 | Ukarabati wa barabara kwa kiwango cha Kifusi kuanzia Kisauni, Shakani hadi Chukwani. | Kisauni<br>Shakani<br>Chukwani | 10,000,000 | Mradi umekamilika |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>Bado fedha haijatumika</td><td>Jimbo zima</td><td>Fedha haijaumika</td><td>Fedha iliyobakia 10,000,000</td></tr>
<tr><td colspan="7">Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chukwani<br><br>Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Chukwani amekiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) ambazo zimetmika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.<br><br>Uchunguzi wa Kamati ya PAC<br><br>Kamati ya PAC ilielezwa kuhusu shilingi 10,000,000 ziloizoelezwa katika Ripotui ya Mdhibiti kuwa hazikutumika, fedha hizo zilitumika katika miradi ya maji safi na salama katika maeneo ya Tomondo, Kisauni, Chukwani na Buyu ambayo iligharimu shilingi 9,000,000.<br><br>Kamati ya PAC ilikagua vielezo mbalimbali vinavyohusiana na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi zikiwemo Fomu za Miradi pamoja na stakabadhi za malipo ambapo Kamati ya PAC imeridhika na nyaraka mbalimbali zilizowalishwa kwa ukaguzi.. Aidha, Kamati ya PAC ilikagua miradi iliyotekelezwa yakiwemo matangi ya Maji ya maji (Kisauni/ Shehia ya Mtaponi tangi la lita 3000 na Sarayevo tangi la lita 2000)<br><br>Pamoja na barabara zilizokarabatiwa. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo</td></tr>
<tr><td>2.</td><td>DIMANI</td><td>20,000,000</td><td>Plasata skuli ya fuoni msingi</td><td>Kibondeni</td><td>20,000,000</td><td>Mradi umekamilika</td></tr>
</table>

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kutia Kifusi njia ya Kibonde Mzungu/Wizo | Kibondeni | | Mradi umekamilika |
| | | | Utiaji fusi | Kibondeni | | Mradi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | njia ya Dampo Jumbi mpaka Skuli ya Kibondeni pamoja na Mbunge. | | | Umekamilika |
| | | | Utiaji fitting ya umeme Skuli ya Maandalizi Nyamanzi | Nyamanzi | | Mradi umekamilika |
| | | | Kuezekwa upya banda ya Skuli ya Kombeni | Kombeni | | Mradi umekamilika |
| | | | Plasta Skuli ya Kibondeni. | Kombeni | | Mradi umekamilika |
| | | | Kuinua kuta jengo la SACCOS Jumbi. | Kibondeni | | Mradi umekamilika |
| | | | Kunyanyua kuta mabanda ya Wajasiriamali Kibondeni/Uwandani. | Kibondeni | | Mradi umekamilika |
| | | | Kutia Kifusi njia ya | Kibondeni | | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | kichaka Punda mpaka kwa Mzee Muharami. | | | |
| | | | Utiaji madirisha na milango madrasa ya Mkadini. | Kibondeni | | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Dimani

Kamati ya Mfuko wa Jimbola Dimani imekiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) ambazo zimetmika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

3. Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hakuwa na risiti na fomu halisi (original) Ameeleza kwamba risiti hizo ameziwasilisha Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kama alivyoelekezwa na barua kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi. Hata hivyo, Watendaji wa Offisis ya Makamo wa Pili wa Rais walisema hawakupokea barua hiyo wala Mwenyekiti hakuwa na nakala ya barua hiyo..
4. Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo haikuwa na muhiri wake.

Hata hivyo Kamati ya PAC ilikagua nyaraka zilizokuwepo zikiwemo stakabadhi (risiti) pamoja na mchanganuo wa matumizi ya miradi hiyo ambazo Kmati ya PAC iliridhika nazo. Aidha Kamat ilikagua madarasa manne ya Skuli ya msingi Kombeni na kurdhika nayo

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wenyeviti wa Kamati za  Mfuko wa Jimbo wawe karibu na Watendaji wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wanaohusika na miradi kabla na wakati wa kutekeleza miradi hiyo ili kupata maelekezo yanayofaa kuhsu taratibu za miradi hiyo.
2. Kamati za Mfuko wa Jimbo ziandae mihuri kwa ajili ya nyaraka mbalimbali za Kamati hizo..

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | FUONI | 20,000,000 | Ununuzi wa Pump ya Kisima - Fuoni Msikiti Mwekundu | Fuoni Migombani | 920,400 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa daraja katika Kijiji cha Kwa Mzee Masanja | Fuoni Mambo Sasa | 2,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Usambazaji wa umeme Fuoni Birikani na Fuoni Michenzani | Chunga | 9,117,446 | Mradi unaendelea |
| | | | Mradi wa ujenzi wa njia za ndani kwa kutia kifusi | | 6,600,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Fuoni.

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Fuoni  imekiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) ambazo zimetmika katika  utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa mradi wa usambazaji Umeme katika Shehia ya Chunga umekamilika kwa mujibu wa mpango (maombi) na walivyokusudia kutekeleza. Aidja Kamati ya PAC imekagua nyaraka za matumzi ya fedha za miradi zikiwemo stakabadhi (risiti) pampoja na nyaraka nyenginezo zinzohusiana

na utekelezaji wa miradi zikiwemo Fomu za Miradi na kumbukumbu za vikao mbalimbali vya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hilo ikiwa ni pamoja na kumbukumbu za kikao cha tarehe 21/6/2018 ambacho ndicho kilichoidhinisha miradi iliyotekelezwa. Aidha Kmati ilipata nafasi ya kukagua baadhi ya miradi iliyotekelezwa. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na matumizi ya fedha za miradi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | K/SAMAKI | 20,000,000 | Uchimbaji wa kisima na vifaa vyake kijijini.<br>Ununuzi wa tenki lita 2000 na vifaa vyake kituo cha afya K/samaki | K/samaki | 20,000,000 | Miradi imekamilika |
| | | | Ujenzi wa minara mitatu na vifaa | Mbweni | | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Vyake | | | |
| | | | Uchimbaji wa kisima/mnara na vifaa vyake. Ujenzi wa mnara kwa Msuri. | Kwamchina | | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kiembe Samaki

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Kiembe Samaki imekiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) ambazo zimetmika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imepata nafasi ya kutembelea miradi iliyotekelzwa ikiwemo kisima cha cha Kwa Mlekwa, na Kisima cha Kwa Juma Vipesa Kiembe Samaki na kubaini yafuatayo:-

1. Kisima cha kwa Mlekwa na kisima cha kwa Juma Vipesa vimeibiwa pampu mbili mbili kila moja ambapo kamati imeoneshwa pampu nyengine ya tatu lakini bado haijaingizwa kisimani.
2. Watendaji wa Serikali za Mitaa hawashiriki ipasavyo katika utekelezaji wa kazi za Kamati ya Maendeleo kama inavyoelekeza Sheria kwamba Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa awe katibu wa Kamati hiyo.
3. Kamati za Mfuko wa Jimbo zinatekeleza miradi kabla ya kujaza fomu za miradi.
4. Wananchi wanalalamika iwapo fedha za mradi zikipelekwa sehemu moja.

Kwa ujumla, Kamati ya PAC imeridhika na matumizi na utekelezaji wa miradi ya Jimbo hilo ka mwaka 2017/2018

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kamati za Mfuko wa Jimbo zihakikishe kuwa zinatekeleza miradi ya Mfuko wa Jimbo kwa kuzingatia misngi ya Sheria na taratibu zinazoongoza miradi ya Mfuko wa Jimbo.

ii. Kamati ya PAC imeshauri maeneo ya visima yawekewe udhibiti imara ikiwa ni pamoja na

kujengwa vizuri kwa nondo na saruji ili kudhibiti wizi.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5. | KIJITOUPELE | 20,000,000 | Ujenzi wa njia za ndani na Vivuko | Meli Nne | 10,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununuzi wa Vifaa vya kusambazia Maji | Meli Nne | 5,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununuzi wa Vifaa vya kusambazia Maji | Kijitoupele | | |
| | | | Ununuzi wa Kiwanja cha Skuli | Kijitoupele | 5,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kijitoupele

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Kijitoupele imekiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) ambazo zimetmika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa katika ununuzi wa Kiwainja cha Skuli ya Msingi Kwarara, shilingi 5,000,000 zilizoainishwa, ziliztumika kwa ajili ya kulipa fidia kwa wenye vipando vilivyokuwepo katika kiwanja hicho.

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali zinazohusiana na matumizi na utekelezaji wa miradi hiyo zikiwemo Fomu za Miradi, stakabadhi za malipo pamoja na kumbukumbu za kikao cha Kamati ya Mfuko wa Jimbo hilo cha tarehe 29/4/2018 kilichoidhinisha miradi hiyo.

Aidha Kamati ilikagua miradi iliyotekelezwa ikiwemo Kivuko kwa kIdema (Magirisi), Kivuko cha Kwa Bi Mariam (Tomondo Uzi) ambavyo vimebainika kuwa vina uchafu. Pia Kiwanja katika Skuli ya Msingi Kwarara kimekaguliwa na kuonekana kuwa Skuli tayari imeshajengwa kiwanja hicho. Kwa ujumla Kmati ya PAC imeridhika na matumizi ya fedha pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 6. | M/KWEREKWE | 20,000,000 | Usambazaji wa maji | Magogoni | 2,920,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ujenzi wa njia | Sokoni | 3,250,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa daraja.<br>Ujenzi wa skuli ya Maandalizi.<br>Ujenzi wa njia<br>Mita ya umeme. | Mikarafuuni | 8,127,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uendelezaji wa chuo cha Amali | Mw/kwere k we | 8,367,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mwanakwerekwe.

Kamati ya Mfuko wa Jimbola Mwanakwerekwe imekiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) ambazo zimetmika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

i. Uwekaji usioridhisha wa kumbukumbu za matumizi pamoja na kumbukmbu nyenginezo zinazohusiana na utekelezaji wa miradi.
ii. Fomu ya utekelezaji wa miradi haikujazwa jina wala Saini ya Mwenyekiti bali imejazwa na Saini ya Katibu tu iliyojazwa tarehe 6/5/2019.

Kamati ya PAC haikuridhishwa na uwekaji usioridhisha wa kumbukumbu za matumizi ya miradi ya Jimbo hilo

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati ay Mfuko wa Jimbo la Mwanakwerekwe isimamia vizuri uwekaji wa kumbukumbu za matumizi na nza utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Jimbo.

2. Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo iwe karibu zaidi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili iweze kupta maelekezo yafaayo katika utekelezaji wa miradi husika

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 7. | PANGAWE | 20,000,000 | Mchango wa Skuli ya Tutu | Pangawe | 1,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Madaraja mawili madogo - Pangawe bonde la Mpunga | Pangawe | 7,784,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ununuzi wa Mabati 50 kwa ajili ya kuezeka kituo cha Polisi Kijitoupele | Pangawe | 975,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa mageti mawili ya skuli ya Kinuni | Kinuni | 3,216,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Utengenezaji wa miundo mbinu ya Maji | Mwemb e Majogoo | 5,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Pangawe.

Kamati imekiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) ambazo zimetmika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali za matumizi na za utekelezaji wa miradi zikiwemo Fomu za miradi, stakabadhi za malipo, na kumbukumbu za kikao cha tarehe 8/4/2018 ambacho kioiidhinisha miradi.

Aidha, Kamati ya PAC ilipata nafasi ya kukagua mageti mawili katika Skuli ya Kinuni. Kwa ujumla Kamati imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KWA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2017/2018 Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Kaskazini A

| Nam | Jimbo | Fedha zilizoingiz Wa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | CHAANI | 20,000,000 | Mradi wa utiaji wa vibomba kwenye njia kwa ajili kupitisha maji | Kinyasini. Chaani Masingini. Kandwi. Banda Maji. Mcheza Shauri. Chaani Kubwa. Kikobweni. Pwani Mchangani. | 20,000,000 | Miradi inaendelea |
| | | | Mradi wa Ujenzi wa Njia za Ndani kwa kutia Kifusi | Jimbo zima | | Mradi unaendelea |
| Kamati ya PAC haikuweza kufanya uchunguzi wa matumizi ya fedha za miradi iliyotekelezwa katika Jimbo la Chaani kwa mwaka 2017/2018 kwa sababu ya kukosekana kwa vilelezo vyote vya matumizi ya fedha za miradi pamoja na vielelezo vyengine vinavyohusiana na utekelezaji wa miradi hiyo. | | | | | | |
| 2. | KIJINI | 20,000,000 | Ujenzi wa Mtaro wa Maji taka. | Kigomani | 10,860,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Kuwezeka Banda la Skuli | Potoa | 7,710,000 | Mradi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | na kupiga Flow. | | | umekamilika |
| | | | Ununuzi wa Misumari. | Potoa | 1,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kijini.

Kamati imekiri kupokea kiwango hicho cha fedha cha shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini utekelezaji wa miradi na viwango vya fedha vilivyotumika katika katika miradi hiyo kama ifuatavyo:-

1. Utekelezaji wa Mtaro – Kigomani –Shilingi milioni kumi na mbili laki tatu na sitini elfu (12,360,000/=)
2. Uezekaji wa skuli ya sekondari ya Potoa – Shilingi milioni nane laki mbili na sabini elfu (8,270,000/=)

Kamati ya P.A.C ilikagua nyaraka za utekelezaji wa miradi na nyaraka za matumizi ya fedha za miradi hiyo pamoja na kutembelea miradi iliyotekelezwa, Kwa ujumla Kamati imeridhika na utekelezaji na matumizi ya fedha za miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | MKWAJUNI | 20,000,000 | Mradi wa maji safi na salama na Mradi wa Usambazaji wa Umeme | Matemwe Kaskazini | 20,000,000 | Miradi imekamilika |
| | | | | Matemwe Kusini | | |
| | | | Ujenzi wa darasa la skuli ya msingi Chutama | Chutama | | |
| | | | Uchimbaji wa Kisima cha maji Safi | Gamba | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ujenzi wa darasa la skuli ya msingi Mkwajuni | Mkwajuni | | |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mkwajuni

Kamati imekiri kupokea kiwango hicho cha fedha cha shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

1. Kukosekana kwa fomu zote za miradi ambapo imebainika kuwa Kamati ya Mfuko wa Jimbo hllo haijawasilisha Fomu zozote kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.
2. Kukosekana kwa ushirikiano baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A" na Kamati ya Mfukowa Maendeleo ya Jimbo la Mkwajuni, Pia, imebainika kuwa hakuna ushitikiano baina ya Halmshauri hiyo na Kamati za Mfuko wa Majimbo ya Nungwi, na Kijini.
3. Kutofautiana kwa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Kamati ya Mfuko wa maendeleo ya Mfuko wa Jimbo na ile iliyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti. Aidha, Kamati imebaini kuwa wakati wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti wanafanya Ukaguzi, Kamati ya Mfuko wa Jimbo ilkuwa imo katika utekelezaji wa miradi. Kwa mujibu wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mkwajuni Miradi ilitekelezwa katika Jimbo hilo kwa mwaka 2017/2018 ni hii ifuatayo:
    i. Uchimbaji wa Kisima – Gamba, uliogharimu shllingi 4150,000.
    ii. Ujenzi wa madarasa mawili – Skuli ya Chutama uliogharimu shilingi 3,500,000.
    iii. Usambazaji maji – Gamba, Chutama, Moga, Kifuruni uliogharimu shilingi 11,500,000

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali zikiwemo risiti za malipo mbalimbali ambazo Kamati ya

PAC iliridhika nazo. Aidha, Kamati ilikagua miradi ya Kisima cha Gamba na Mradi wa usambazaji maji katika vijiji mbalimbali

Katika mradi wa kisima cha Gamba, kazi zilizofanyika ni kuchimba kisima, kuweka makalbi, na kuweka mnara. Kwa hivi sasa kisima hicho hakitumiki sana na kinatumika inapotokea mahitaji ya dharura kwa kuwa maji yanapatikana kupitia kisima chengine cha Ras el AL Hema walichokiendeleza.

Katika mradi wa usamabazaji maji katika viji mbalimbali Kamati ya PAC Iimebaini kukosekana kwa usambazaji wa mabomba ya maji katika kisima cha Moga Kibeberu kilichochimbwa na mradi wa Rasul - kheimar ambapo ZAWA iliahidi kuweka tenki kubwa lakini bado haijatekeleza.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Serikali ifanye jitihada zitakozowezsesha kupatikana kwa ushirikiano wa kutosha baina ya Halmashauri. Mabaraza ya Mji na Kamati za Mfuko wa Jimbo ikiwemo kutoa elimu ya kutosha kwa pande zote mbili
2. Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mkwajuni iwe karibu zaidi na watednaji wanaohusika na miradi katika Ofisis ya Makamo wa Pili wa Rais ili kupata maelekezo juu ya tataratibu mbali mbali zinazohusu miradi ya Jimbo zikiwemo za ujazaji wa Fomu za Miradi pamoja na taratibu nyenginezo.
3. Kamati ya Mfuko wa Maendelo ya Jimbo la Mkwajuni kupitia Mwenyekiti wake wafuatilie Mamlaka ya maji ZAWA juu ya kusambaza mabomba ya maji katika maeneo yaliyobakia kama ilivyoahidi amabapo katika kisima cha Moga Kwa Kibeberu kilichochimbwa kupitia mradi wa Ras el – kheima, ZAWA iliahidi kuweka tenki kubwa la maji la lita milioni mbili lakini bado ilikuwa haijatekeleza.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | NUNGWI | 20,000,000 | Kuendeleza Ujenzi wa Skuli ya Msingi Nungwi. | Nungwi | 3,045,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Kuendeleza Ujenzi wa Skuli ya Sekondari Kidoti. | Kidoti | 3,490,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Skuli ya Sekondari Kidagoni. | Kidoti | 2,325,000 | Mradi Umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ujenzi wa Skuli ya Bwereu Madarasa Matano . | Bwereu | 5,140,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Matengenezo ya Uwanja wa Mpira. | Kigunda | 6,000,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Nungwi

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Tumbatu ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zilitumika katika utekelezaji wa miradi mbali mbali katika Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilibaini yafuatayo:-

1. Kutokamilika kwa matengenezo ya uwanja wa mpira Kigunda: Katika mradi wa matengenezo ya uwanja wa mpira Kigunda, kazi ya hatua ya mwanzo ni kuuweka sawa (kwa grader) kwa kuwa uwanja ulikuwa una mawe, Hatua ya pili ya kuweka udongo haikufikiwa kwa mwaka uliofuata kwa kuwa fedha walizibadilisha matumzi na kuzielekeza katika sSkuli ya Nungwi. Kazi ya kupiga "grader tu iligharimu shilingi 6,000,000.
2. Kukosekana kwa mashirikiano mazuri baina ya Kamati Mpya ya Mfuko wa Jimbo  na ile ya zamani
3. Kukosekana kwa ushirikiano mbaina ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo na Halmashauri ya Wilaya Kaskazini  "A" ambapo Kmati ilielelezwa kuwa hapo awali mashirikiano baina yao yalikuwa mazuri lakini baadae yalihararibika kwa sababu iliyoelezwa kuwa ni matumizi yasiyoridhisha yaliyokuwa yakifanywa na baadhi ya watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A

Kamati ilikagua nyaraka mbalimbali za matumizi na za utekelezaji wa miradi . Aidha, Kmati ilipata nafasi ya kutembelea baadhi ya miradi iliyotekelezwa kama ifuatavyo:-

i. Skuli ya Msingi Bwereu: Madarasa  sita na Oifsi moja walikuta yamefikia kozi ya nne. Walienedelleza ujenzi hadi hatua ya gebo. Madarasa mawili walimalizwa kujengwa na Serikali yamebakia manne kuezekwa na kumalizia
ii. Uwanja wa Mpira – Kigunda: umepigwa "grader"

Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na matumizi ya fedha za miradi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo ingawa ilikuwa na mapendekezo kadhaa.

Mapendeezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati za Mfuko wa Jimbo zifanye utafiri wa kutosha kwa miradi inayokusudia kuitekekeza Fedha za mfuko zitumike vizuri kama inavyoelekezwa na Sheria ya Mfuko wa Jimbo hususan uwashirikishaji wa Mkurugenzi wa Serikali ya Mitaa husika.

2. Kamati mpya ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Nungwi ihakikishe inaandaa mazingira mazuri ya kufanya kazi na wajumbe wa kamati iliyomaliza muda wake.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 5. | TUMBATU | 20,000,000 | Ununuzi wa Myundu. | Mtakuja.<br>Gomani.<br>Uvivini. | 10,000,000 | Mradi Umekamilik a |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jongowe. | | |
| | | | Shughuli za Usasi wa Kima | Mtakuja.<br>Gomani.<br>Uvivini.<br>Jongowe. | 2,205,000 | Mradi Umekamilik a |
| | | | Ununuzi wa Komputa na Mashine ya Fotokopi. | Muwanda.<br>Mkokotoni<br>.<br>Mto wa Pwani. | 11,220,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Usambazaji wa maji Skuli ya White Star. | Mtakuja | 326,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Tumbatu

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Tumbatu imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zilitumika katika utekelezaji wa miradi mbali mbali katika Jimbo hilo.

Uchuuguzi wa Kamati ya PAC

Kwa mujibu wa Ripoti ya Utekelezaji wa Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Tumbatu iliyowasilishwa mbele ya Kamati ya PAC ni kwamba Jimbo la Tumbatu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilitekeleza Miradi miwili ifuatayo:'

i. Ununuzi wa miundu. Ununuzi wa vifaa hivi uligharimu jumla ya shilingi 10,000,000 ambpo miundu hii ilinunuliwa kwa ajili ya Shehia tatu ambazo ni Uvivini, Mtakuja na Shehia ya Gomani,
ii. Ununuzi wa Stationeries. Mradi huu uligharimu jumla ya shilingi 11,220,000. Stationeries hizi zilihusisha skuli tatu ambazo ni Skuli ya Pale,, Skuli ya Muwanda na Mkokotoni.

Kamati ya PAC ilikagua vielelezo mbalimbali vinavyohusiana na utekelezaji pamoja na matumizi ya miradi zikiwemo stakabadhi za matumizi pamoja na kutembelea baadhi ya miardi iliyotekelezwa. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo.

| Nam | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | BUBMWINI | 20,000,000 | Uchimbaji visima viwili na vifaa vyake Mperani na Bwaga.<br><br>Utengenezaji ukuta wa hospitali ya Misufini | Misufini | 18,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Utengenezaji wa skuli ya chekechea | Mafufuni | 2,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Bumbwini

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Bumbwini ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyobainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imekagua nyaraka mbalimbali zinazohusiana na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi zikiwemo Fomu za Miradi, stakabdhi za malipo pamoja kumbukumbu zakikao cha tarehe 14/5/2017 ambacho ndicho kilichoidhinisha miradi iliyotekelezwa.

Aidha, Kamati ya PAC ilikagua miradi iliyotekelezwa kama vile Kisima cha Mperani, Ukuta wa Hospitali wa Misufini na Skuli ya Maandalizi ya Mafufuni.Kamati ya PAC imebaini kuwa kisima cha Mperani Maendeleo hakifanyi kazi kutokana na kudidimia kulikosababishwa na mvua kubwa iliyonyesha katika maeneo hayo. Kwa ujumla Kamati ya PAC imerudhika na matumizi ya fedha za miradi na utekelezaji wa miradi hiyo,

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inaishari Kamati ya Mfuko wa Maendeleo Jimbo la Bumbwini kukishughulikia kisima cha Mperani ili kiweze kuendelea kufanya kufanya kazi

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | DONGE | 20,000,000 | Ujenzi wa mnara wa maji na tenki | Mkatal e ni | 5,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Donge

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Donge ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo ya Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Ingawa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeainisha mradi mmoja tu lakini kwa mujibu wa Fomu za Utekelezaji wa Miradi, Kamati ya PAC imebaini kuwa miradi mbali imetekelezwa katika Jimbo la Donge kwa mwaka 2017/2018 kama ifuatavyo:-

i. Uchumbaji Kisima – Mkataleni uliogharimu shilingi 7,000,000
ii. Ujernzi Minara ya Matangi – Mkataleni, - uliogharimu shilingi 2,852,,000
iii. Usambazaji maji safi na salama – Karange, Kitaruni,, Fuasini na Mkataleni – uliogharimu shilingi 10,240,00

Kamati pia ilikagua vielelezo vya matumizi na vya utekelezaji wa miradi zikiwemo Fomu za Miradi na stakabadhi za malipo ambapo kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na vielelezo hivyo. Aidha, Kamati ya PAC ilikagua Kisima cha Mkataleni pamoja na usambazaji maji safi na salama Karange,Kitaruni na viji vyenginevyo ambapo Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | KIWENGWA | 20,000,000 | Ujenzi wa mnara katika | Kiwengwa | 5,100,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | kituo cha afya Kiwengwa | | | |
| | | | Ujenzi wa vyoo vya skuli ya Pangeni | Pangeni | 6,693,296 | Mradi unaendelea |
| | | | Usambazaji wa umeme kibanda cha maji cha kisima Kitope | Mbaleni | 4,788,704 | Mradi umekamilika |
| | | | Umaliziaji wa ujenzi wa skuli ya Kilombero | Kilombero | 3,418,000 | Mradi unaendelea |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kiwengwa

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Kiwengwa ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa ingawa jumla ya matumizi imefikia shilingi 20,000,000 lakini gharama za matumzi ya mradi mmoja mmoja zinaofautiana baina ya gharama zilizoainishwa katika Fomu za Utekelezaji wa Miradi na zile zilizomo katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. za Serikali.

Aidha, Kamati ya PAC imebaini kuwa baadhi ya vielelezo vya miradi kutowekwa pamoja kulingana na mradi husika. Hali hiyo ilitokana na kwamba kwa mwaka 2017/2018 Kamati ya Mfuko wa Jimbo ilichanganya matumizi kwa kukununua vifaa vyote vya miradi ya ujenzi kwa pamoja..

Vile vile Kamati ya PAC ilibaini Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hilo haikuwa na muhuri

wake, jambo lililopelekea subvoucher na nyaraka nyengine za Kamati ya Mfuko wa Jimbo kutumia muhuri wa Halmshauri ya Wilaya ya Kaskazini "B"

Kamati ilipata nafasi ya kukagua Usambazaji wa umeme kibanda cha maji cha kisima Kitope pamoja na vyoo katika Skuli ya msingi – Pangeni.

Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi ingawa ilikuwa na mapendekezo kadhaa.

Mapendekezo ya Kamatta ya PAC

1. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu iwe na ushirikiano wa karibu zaidi na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wakati wa ukaguzi wa miradi ya Mfuko wa Jimbo ili taarifa zinatolewa ziwe na usahihi unaofanana.
2. Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kiwengwa iandae muhuri wake ili iweze kuutumia katika uidhinishaji wa malipo ya miradi.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | MAHONDA | 20,000,000 | Ukarabati wa ,mnara wa maji skuli ya Mangapwani | Mangapwani | 1,900,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununuzi wa mashine ya boti | Fujoni | 3,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uendelezaji wa jingo la skuli ya kitipe (hall) | Kitope | 4,797,700 | Mradi umekamilika |
| | | | Uezekaji wa skuli ya vuga | Mkadini | 4,357,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa daraja | Matetema | 5,000,000 | Mradi umekamil ika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mahonda

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Mahonda ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya

maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka za matumizi na za utekelezaji wa miradi zikiwemo stakabadhi za malipo na Fomu za Miradi ambapo kwa ujumla Kamati imeridhika nazo. Aidha, Kamati ya PAC ilikagua baadhi ya miradi iliyoytekelezwa ambayo kwa ujumla imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KWA MKOA WA KUSINI UNGUJA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2017/2018 Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Kati

| Nam | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | CHWAKA | 20,000,000 | Uchimbaji wa misingi ya usambazaji ya maji safi | Pete | 5,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi nyumba ya walimu | Marumbi | 15,000,000 | Mradi unaendelea |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chwaka

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Chwaka ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka za matumizi na za utekelezaji wa miradi zikiwemo stakabadhi za malipo na Fomu za Miradi ambapo kwa ujumla Kamati imeridhika nazo.

Aidha Kamati, ilikagua mradi wa maji Pete na nyumba ya Walimu – Maumbii ambayo ilkuwa imeshaezekwa bado madirisha, milango na kumalizia hatua nyenginezo (finishing). Kwa ujumla Kamati ya PAC IMEridhika na utekelezaji wa miradi hiyo

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | TUNGUU | 20,000,000 | Ujenzi wa mnara wa maji safi na salama kijiji cha Dunga Gongoni | Binguni | 3,856,180 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Uendelezaji wa ujenzi wa msingi skuli ya Kibele | Tunguu | 5,920,000 | Mradi unaendelea |
| | | | Ujenzi wa mnara wa maji safi na salama kijiji cha Mtakuja | Dunga Bweni | 3,234,430 | Mradi umekamilika |
| | | | Uendelezaji wa ujenzi wa skuli ya Dunga Kiembeni | Dunga Kiembeni | 5,615,000 | Mradi unaendelea |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Tunguu

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Tunguu ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katikam utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa baadhi ya miradi iliyoelezwa katika Ripoti ya Mdhibti kuwa inaendelea wakati wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti walipopita, Miradi hiyo hivi sasa imekamilika Aidha, Kamati ya PAC ilikagua virlelezoa mbalimbali vya matumzi na vya miradi zikiwemo stakabdhi za malipo,Fomu za Miradi Miradi na kumbkumbu za vikao na kuridhika navyo.

Vilevile Kamati ya PAC ilikagua Skuli ya Dunga Kiembeni na Skuli ya Kibele ambapo kwa ujumla imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | UZINI | 20,000,000 | Kupewa mkono wa pole waathirika ya maafa ya mvua | Kiboje mkwajuni | 2,000,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ujenzi wa skuli yamaandalizi Bambi | Bambi | 3,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa karo | Mpapa | 1,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Pongezi kwa wanafunzi | Jimbo zima | 10,500,000 | Mradi umekamilika |
| Kamati ya PAC haikuweza kufanya uchunguzi wa matumzi ya fedha zilizotumika katika miradi ya Jimbo la Uzini kwa sababu vielelezo vya matumizi hayo havikupatikana kwa ukaguzi. Hali hiiyo ilisababishwa na kutokuwepo wakati wa kikao cha Kamati yaPAC Katibu wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Uzini ambae ndie aliyekuwa navyo vielelezo hivyo. | | | | | | |

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Kusini Unguja (2017/2018)

| Nam | Jimbo | Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MAKUNDUCHI | 20,000,000 | Kupelekwa huduma ya Umeme katika kisima cha maji safi na salama. | Muyuni A | 1,378,044 | Mradi Haujatekelezwa |
| | | | Kupelekwa nguzo sita za umeme na waya katika Mtaa wa Kipanga. | Muyuni B | 2,034,400 | Mradi Haujatekelezwa |
| | | | Uchimbaji wa kisima cha maji safi na salama. | Muyuni C | 2,000,000 | Mradi Haujatekelezwa |
| | | | Ununuzi wa matofali mia nane pamoja na usafiri Skuli ya Kizimkazi Mkunguni ya Maandalizi. | Kizimkazi Mkunguni | 1,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa uzio Skuli ya Kiongoni. | Kiongoni Makunduchi | 963,000 | Mradi Umekamilika |
| | | | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa nyumba ya Daktari Kizimkazi | Kizimkazi Dimbani | 2,880,000 | Mradi Umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Dimbani. | | | |
| | | | Kupeleka Umeme katika | Kijini Makunduchi | 1,000,000 | Mradi Unaendelea |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | kisima cha maji safi na salama Shehia ya Kijini Makunduchi. | | | |
| | | | Ujenzi wa msingi jingo la kituo cha kulelea watoto wadogo. | Tasani Makunduchi | 2,500,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa msingi jingo la Skuli ya Maandalizi | Mzuri Makunduchi | 2,060,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ukarabati wa Jengo la nyumba ya walimu skuli ya Kibuteni | Kibuteni | 2,122,500 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa msingi uzio Skuli ya Kajengwa | Kajengwa | 2,000,000 | Mradi Umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Makunduchi

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Makunduchi ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katikam utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa miradi iliyoainishwa katika Ripoti Mdhibiti kuwa haijatekelezwa, hivi sasa imekamilika. Aidha Kamati ilikagua nyaraka mbali zinzohusiana na matumzi pamoja na za utekelezajiwa miradi hiyo zikiwemo Fomu za mIradi na stakabadhi za malipo na kuridhika nazo.

Vilevile Kamati ya PAC ilkagua umeme Muyuni B na Skuli ya Kizimkazi Mkunguni. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | PAJE | 20,000,000 | Mradi wa Maji Ununuzi wa mashine (mota) za visima | Jambian i Kibigija | 5,500,000 | Mradi umekamilik a |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Paje

Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Paje alikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= kutoka serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo ya Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kutotumika fedha za miradi kwa wakati ambapo wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti wanafanya ukaguzi katikaJimbo la Paje walikuta utekelezaji wa mradi mmoja tu ambao umeainishwa katika Ripoti ya Ukaguzi. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kwa mwaka wa 2017/2018 Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Paje ilitekeleza miradi mbali mbali kama ifuatavyo:

i. Ununuzi wa mipira na usambazaji – Bwejuu na Jambiani Mfumbwi uliogharimu shilingi 5,000,000
ii. Ununuzi wa pampu ya maji – Jambiani Kibigija uliogharimu shilingi 5,500,000
iii. Ununuzi wa pampu ya maji – Skuli ya Kitogani uliogharimu shilingi 9,000,000
iv. Ununuzi wa pampu ya maji – Paje uliogharimu shilingi 5,000,000
v. Utengenezaji wa pumpu – Bwejuu uliogharimu shilingi2,500,000
vi. Utiaji kifusi nia ya Bwejuu uliogharimu shilingi 1,000,000
vii. Ununuzi wa mipira miine ya gari ya kuchukulia wagonjwa (Ambulance ya Jinbo) uliogharimu

shilingi 1,000,000.

Mapendekeo ya Kamati ya PAC

Kamati yaMfuko wa Jimbo la Paje ihakikishe kuwa fedha za Miradi zinatumika kwa wakati kama inavyoelekeza sheria na taratibu husika.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KWA MKOA WA KASKAZINI PEMBA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2017/2018

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Wete

| Nam. | Jimbo | Fedha Zilizoingizwa | Mradi uliotekelezwa | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | GANDO | 20,000,000 | Ukarabati wa vyoo – skuli ya kizimbani | Kizimbani | 6,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ununuzi wa gari kwa ajili ya jimbo la Gando | Jimbo zima | Fedha hazijatumika | Fedha zilizobakia 14,000,000 |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Gando

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Gando ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000/= kutoka serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo ya Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ya P.A.C imebaini kua miongoni mw miradi iliyokuwa itekelezwe katika Jimbo hilo kwa mwaka huo wa fedha ni ununuzi wa gari kwa ajili ya Jimbo hilo. Hata hivyo, ununuzi wa gari hiyo haukufanyika na feha kwa ajili ya ununuzi wa gari hiyo zilitumika katika miradi mengine ya ununuzi wa mashine ya maji Junguni n ujenzi wa Skuli ya Msingi Ukunjwi. Kwa ujumla kwa mwaka wa fedha 2017/2018 miradi iliyotekelezwa katika Jimbo la Gando ni hii ifuatayo:-

1. Ukarabati wa vyoo ktika Skuli ya Kizimbani uliogharimu Shilingi 6,000,000/= - Mradi huo umekamilika
2. Ununuzi wa Mashine ya Maji – Junguni uliogharimu Shilingi 8,173,500/=
3. Ujenzi wa Skuli ya Msingi Ukunjwi uliogharimu shilingi 4,614,000/=

Shilingi 10,000,000/= zimetumika kwa ajili ya kazi za uendeshaji zinazohusiana na miradi hiyo.

Kamati ya P.A.C ilikagua nyaraka mbali mbali zinazohusiana na utekelezaji wa miradi hiyo zikiwemo Fomu za Miradi, stakabadhi za malipo, miktaba ya kazi (ikiwemo wa ujenzi a vyoo Skuli ya Sekondari Kizimbani na ujenzi wa adarasa matatu na ofii ya mwalimu Mkuu Skuli ya Ukunjwi ) pamoja na pamoja na kumbukumbu za kikao cha tarehe 26/11/2018. Kamati pia ilikagua baadhi ya miradi na kwa iliridhik na miradi iliyotekelezwa.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | MGOGONI | 20,000,000 | Ujenzi wa mabanda matatu ya skuli ya maandalizi Pandani | Pandani | 8,875,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa mabanda matatu skuli ya maandalizi ya Mjananza | Mjananza | 9,193,500 | Mradi unaendelea |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mgogoni.

Kamati ya Mfuko wa Maeneleo ya Jimbo la Mgogoni imekiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika kutekeleza miradi miwili kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hasabu.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ya P.A.C imebaini kuwa mradi wa ujenzi wa mabanda matatu ya Skuli ya Maandalizi ya Mjananza umekamilika . Vile vile imebainika kuwa Shilingi 20,000,000/=zilitumika katika mired hiyo. Aidha, Kamati ya P.A.C ilikagu nyraka mbali mbali zilizotumika katika utekelezaji wa miradi, stakabadhi za malipo, mikataba ya kazi, na kumbukumbu za kikao cha tarehe 21/7/2018 cha Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ambacho ndicho kilichoidhinisha miradi hiyo na kwa ujumla imeridhika na utekelezaji pamoja na matumizi ya fedha za miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | MTAMBWE | 20,000,000 | Ununuzi wa mota kwa ajili ya usambazaji maji Uondwe | Mtambwe kaskazini | 9,000,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kunyanyua kuta na kuezeka kituo cha afya Maziwani | Maziwani | Fedha hazijatumika | Fedha iliyobakia 10,000,000 |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Mtambwe.

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Mtambwe ilikiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= ambazo zimetumika katika uekelezaji wa miradi mbali mbali katika jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya P.A.C. imebaini kuw mwaka 2017/2018 Jimbo la Mtambwe ilitekeleza miradi ifuatayo ;-

1. Ununuzi wa mota kwa ajili ya usambazaji maji Uondwe ambao ulitumia shilingi 7,200,000/= na mradi huo umekamilika.
2. Kunyanyua kuta na kuezeka kituo cha Afya Maziwani ambao umetumia shilingi 10,755,000/= na mradi huo umekamilika.
3. Ujenzi wa msingi (foundation) ya vyoo, matundu manne katika Skili ya Uondwe Msingi 2,500,000/= 9Fedha hizi zinatokana na fdha za mwaka 2016/2017 mbazo zilichukuliwa na baadae mwaka 2017/2018 kurejesha katika Akaunti ya Kamati ya Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo).

Katika ukaguzi wa nyaraka za miradi hiyo Kamati ya P.A.C imebaini kuksekana kwa Fomu ya utekelezaji wa miradi ambapo ilielezwa kuwa Fomu hizo zilichelewa kupelekwa Pemba. Hata hivyo Kamati ya P.A.C haikuridhika na kutokamilika kwa nyaraka hizo pamoja na majibu hayo ambapo Fomu za utekelezaji zilikuwa zinapatikna katika majimbo mengine ya Pemba na zilikuwa zikiwasilishwa katika vikao vya Kamati y P.A.C . Pia Kamati ilikagua miradi iliyotelekezwa kama ifuatavyo:-

a. Kituo cha Afya – Maziwani – Awali kituo hich kilijengwa kwa nguvu za wananchi ambapo kilisita kwa muda mmrefu baadae. Kazi zilizofanyika ni kunyanyua kuta hadi linta na kuezeka. Kituo hicho bado hakijatiwa umeme, dari, (syling) na samani (faniture). Hata hivyo Kamati imeridhika ma mradi huo.
b. Mota – Mtambwe Kaskazini (Uondwe) Huduma ya maji imepatikana ingawa ni kwa mgao (kila baada ya siku mbili) kutokana na kuwepo kwa vijiji vingi vinavyohitaji maji vikiwemo Nyali, Kiapaka, Kidundo, Mtambwe Mkuu, Chanjaani,, Kwale, Mchngani, Jambaji, Chekea, Mpaka Njia na Uondwe. Kamati imeridhika na thamani halisi ya matumizi ya fedha za mradi huo (Value for money) licha ya dosari za hapa na pale zilizobainika katika nyaraka za miradi.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Kamati ya P.A.C inawashauri uongozi wa Jimbo la Mtambwe kuwa kuna haja ya kupunguza hali ya mgao wa huduma ya maji inayohitajika katika vijiji vingi vya Mtambwe Kaskazini kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma hiyo.<br>2. Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mtambwe kwa kushirikiana na Baraza la Mji Wete ifanye jitihada za kukimaliza kituo cha Afya Maziwani ili kituo hicho kuweza kutoa tija iliyokusudiwa kwa wananchi.<br>3. Makatibu wa Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wazidishe umakini katika uandaaji wa ripoti za miradi hiyo pamoja na kuambatanisha kikamilifu vielelezo vyte vinavyohusika na miradi hiyo, | | | | | | |
| 14. | KOJANI | 20,000,000 | Kupiga plasta,kutia sakafu na apron skuli ya maandalizi Kangagani | Kangagani | 10,864,830 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kutengeneza barabara(kutia fusi) Kiuyu barabarani hadi Kigongoni | Kiuyu-Kigongoni | 3,033,520 | Mradi umekamilika |
| 15. | | | Ujenzi wa mnara wa kuekea tangi la maji na kutoa maji kisimani na kuyapeleka kwenye tangi kijiji cha Gasi | Kinyikani | 4,192,650 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Kojani

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kojani ilikiri kupokea shilingi 20,000,000/= kutoka serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mitatu kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti

Uchungyuzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua vielelezo vyote vinavyohusiana na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi zikiwemo Fomu za Miradi na stakabadhi za malipo na kubainia kuwa fedha za malipo ya posho za Wajumbe wa Kamati ya Mfuko wa jimbozimetumika 1,600,000 kinyume na utaratibu ikiwa ni ongezeko la shilingi 600,000. Kamati ya Mfuko wa Jimbo ilieleza kuwa ilikuwa haijapata muongozo wa malipo ya uendeshaji na posho za vikao.

Aidha Kamati ya PAC ilikagua Skuli ya Kangagani kuona kazi zilizofanywa za Kupiga plasta,kutia sakafu na apron skuli ya maandalizi Kangagani. Pia Kamati ya PAC ilikagua mradi wa maji Kinyikani.(ununuzi wa pump, unuzi wa tangi, ujezni wa manara na uungaji wa umeme. Hata hivyo, Kamati imegundua kisima hicho hakifanyi kazi kwa miaka miwili kwani kulitiwa waya katika vipindi viwili tofauti lakini zote ziliungua ambapo kwa hivi sasa wananchi wanapata maji ya ZAWA ingawa huwa hayatabirikia.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati mpya ya Mfuko wa Jimbo ishirikiane na Baraza la Mji Wete kuhakikisha anapatikana mtaalamu mtaalamu atakaeweza kugundua sababu inayofanya waya za pampu ya kisima Kimyikani na kufanya marekebisho
2. Mwenyekiti wa Kamati mpya ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kojani afanye utaratibu wa kupatikana waya mpya ili kisima kiweze kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi wa maeneo hayo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Kojani iwe makini inapotumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kamati yetu imegundua 'Apron' za skuli ya Kangagani zimeshaanza kufanya ufa.<br>4. Baraza la Mji Wete liwe linafuatilia miradi iliyotekelezwa ili liweze kutambua changamoto inazokabiliana nazo. | | | | | | |
| 16. | WETE | 20,000,000 | Mradi wa ujenzi wa skuli ya msingi Tungamaa | Limbani | Fedha hazijatumika | Fedha iliyobakia 20,000,000 |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Wete

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Tumbe ilikiri kupokea shilingi 20,000,000/= kutoka serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa kwa mwaka 2017/2018 Jimbo la Wete lilitekeleza miradi ifuatayo:

i. Ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ua Skuli ya Maandalizi Jadida (madarasa mawili) uliogharimu shilingi 1,555,000
ii. Ujenzi wa Msingi (Foundation0 Skuli ya Msingi Tungamaa uliogharimu shilingi 10.128.000
iii. Utengenezaji wa Matofali kwa ajili ya kwa ajili Skuli Maandalizi Tungamaa shilingi 6,730,000

Kamati ilikagua nyaraka mbalimbali za matumizi na na za utkelelezajiwa wa miradi zikiwemo stakabadhi za malipo, Fpmu za Miradi pamoja kumnbukumnhu za kikao cha tarehe 5/11/2018 ambacho ndicho kilichoidhinisha miradi iliyotekelezwa. Aidha, Kamati ilikagua miradi iliyotekelezwa. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Micheweni (2017/2018)

| Nam. | Jimbo | Fedha Zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 9. | Tumbe | 20,000,000 | Uezekaji wa jengo la mama na mtoto kituo cha Afya | Tumbe | 7,914,450 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Tumbe | | | |
| | | | Uendelezaji wa ujenzi skuli ya Chimba | Chimba | 6,904,125 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Tumbe

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Tumbe ilikiri kupokea shilingi 20,000,000/= kutoka serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imakagua nyaraka zote zinazohusiana na matumzi na utekelezaji wa miradi ya Jimbo hilo na kubaini kuwa skuli ya Chimba imeingiziwa fedha katika awamu mbili (2016/2017 na mwaka 2017/2018 badala ya kuingiziwa fedha kwa awamu moja na kukamilisha kabisa ujenzi.

Aidha, Kmati ya PAC imebaini kuwa barua zinazohusu Mfuko wa Jjimbo anandikiwa Mkurigenzi wa Halmashauri ya Micheweni ingawa nae ndio Katibu wa Kamati ya Mfuko. Hata hivyo, Kamati imeridhika na uwekaji mzuri wa kumbkumbu

Kamati pia ilipata nafasi ya kukagua uezekaji uliofanywa katika jengo la afya ya mama na mtoto katika kituo cha Afya Tumbe na Skuli ya Msingi Chimba. Kwa ujumla imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Ni vyema Miradi ipangwe vizuri ili iweze kuwekewa fedha za kutosha zitakazoweza kukamilisha utekelezaji wake kwa kipindi kifupi.

ii. Ili kutofautisha shughuli na nyaraka za Mfuko wa Jimbo na zile za Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, Kamati inashauri kuwa Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Tumbe iwe na Sub voucher zake,aidha, barua zinazohusu masuala ya Mfuko wa Jimbo ziwe na anuani ya Katibu wa Mfuko wa Jimbo badala ya kuandikwa kwa anuani ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| 10. | Konde | 20,000,000 | Ujenzi wa choo skuli ya Kiuyu Kipangani | Kifundi | 2,375,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uendelezaji wa ujenzi skuli ya | Konde | 9,025,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Maandalizi Konde | | | |
| | | | Kusaidia maji kijiji cha Ujingabasi | Konde | 2,375,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uwekaji wa fusi njia ya Konde Upembani | Konde | 3,920,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Konde

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Konde ilikiri kupokea shilingi 20,000,000/= kutoka serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mitatu kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mabalimbali zinazohusiana na matumzi pamoja na utekelezaji wa miradi zikiwemo Fomu za Miradi na stakabdhi za malipo. Kwa ujumla iliridhika na nyaraka hizo.

Aidha Kamati ya PAC ilipata nafasi ya kukagua mabanda mawili skuli ya Maandalizi Konde na Vyoo katika Skuli ay Kiuyu Kipangani. Kamati imegundua kwamba vyoo vya skuli ya Kipangani haina mlango madhubuti badala yake limewekwa bati. Hivyo Kamati imeelekeza mlango huo uwekwe wa mbao ili kuzuia wananchi wa kijiji cha Kambu wasiingie na kutumia vyoo hivyo.

Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi iliyotekelezwa katika Jimbo hilo kwa mwaka 2017/2018

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 11. | Micheweni | 20,000,000 | Umalizaji wa ukumbi wa mkutano skuli ya Kiuyu | Kiuyu | 10,940,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ukaratabi wa ukumbi wa shughuli za kijamii | Micheweni | 4,254,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ukaratabi wa visima Vitatu | Maziwa Ngombe | 3,473,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Micheweni

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Micheweni ilikiri kupokea shilingi 20,000,000/= kutoka serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mitatu kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya P.A.C ilielezwa kazi zilizotekelezwa katika kila mradi kama ifuatavyo:-

1. Katika Mradi wa ukarabati wa visima vitatu vya maji huko Maziwang'ombe uliogharimu shilingi 3,473,000/=, kazi zilizofanyika ni kupiga plasta, kujenga upya kuta za visima kwa zile sehemu zilizoharibika na kuweka sakafu chini sehemu zote zilizozunguka visima hivyo.

2. Katika ukarabati wa ukumbi wa shughuli za kijamii – Micheweni uliogharimu shilingi 4,334,000/= ambazo zimetumika kwa kazi ya kupiga plasta nje na ndani ya jingo, kuweka sakafu mpya, kuezeka upya, kupaka rangi na kutia chipping.

3. Kwenye mradi wa ukamilishaji wa ujenzi wa ukumbi wa Skuli ya Kiuyu msingi uliogharimu Shilingi 10,940.000/=, kazi zilizofanyika ni kuweka sakafu za aproni, kupaka rangi, kutia chipping nje ya jingo,kuweka miundombinu ya umeme na kujenga gebo.

Kamati ya P.A.C ilikagua nyaraka mbali mbali zilizohusiana na utekelezaji wa miradi hiyo zikiwemo Fomu za Miradi, stakabadhi za malipo, mikataba, barua za maombiya miradi, mchanganuo wa fedha za matumizi ya miradi na kumbukumbu za vikao, Kamati pia ilipata

nafasi ya kukagua ukumbi wa shughuli za kijamii – Micheweni na kuridhika na kazi zilizofanywa, Kwa ujumla Kamati ya P.A.C imeridhika na utekelezaji na matumizi ya fedha za miradi iliyotekelezwa katika Jimbo hilo kwa mwaka 2017/2018.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 12. | Wingwi | 20,000,000 | Ujenzi wa skuli ya Mjini Wingwi | Mjini Wingwi | 5,600,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Kusaidia ununuzi wa vifaa vya kituo elimu mbadala kijiji cha Mtemani | Mtemani | 3,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Wingwi

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Ole imekiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC
Kamati ya PAC imebaini kuwa kwa mwaka 2017/2018 Kamati ya Mfuko wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Wingwi ilitekeleza miradi ifuatayo:

1. Kusaidia vifaa Skuli ya Mbadala – Sizini uliogharimu shilingi 3,000,000
2. Usambazji maji Kijiji cha Njuguni uligharimu shilingi 6,000,000
3. Ujenzi skuli ya Mjini Wingwi ulioghariumu shilingi 9,500,000

Shilingi 1,500,000 zilitumika kwa ajili ya posho la vikao vya Wajumbe wa Kamati ya Fuko wa Jimbo ambapo walieleza kuwa walikuwa hawajajua idadi ya wajumbe wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo kisheria.

Aidha , Kamati ilibaini kuwa ingawa Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti alipofika Jimboni kwa ukaguzi jumla ya shilingi 11.400,0000 zilikuwa hazijatumika ambapo alikuta miradi miwili tu imetekelezwa kwa gharama ya shilingi 8,6000,000 na miradi mengine iliyobakia ilitekelezwa baada ya Ukaguzi.

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka za matumizi na za uteklezaji wa miiradi hiyo zikiwemo stakabadhji za matumizi. Aidha, Kamati ilikagua madarasa mawili ya Skuli ya Sizini pamoja na banda lenye madarasa manne katika Skuli ya Mjini Wingwi. Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi ya Jimbo hilo ingawa ilikuwa na mapendekezo kadhaa.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati za Mfuko wa Jimbo ziwe makini zinapotumia fedha za mradi kwa kuzingatia muda wa matumizi wa fedha hizo.
2. Kamati za Mfuko wa Jimbo zisimamie vyema uhifadhi wa kumbukumbu za vielelezo vya matumizi ya fedha za mradi.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KWA MKOA WA KUSINI PEMBA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2017/2018

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Chake Chake

| Nam. | Jimbo | Fedha Zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 11. | OLE | 20,000,000 | Usambazaji mipira ya maji,kijiji cha Makaani | Mjini Ole | 12,270,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Kujenga madarasa matatu ya skuli ya Uwandani | Uwandani | 4,819,500 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Ole.

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Ole imekiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi miwili kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali za matumizi zikiwemo stakabadhi za matumizi pamoja na nyaraka nyenginezo zinzohusiana na utkelezaji wa matumizi.na kubaini kuwa Kamati ya Mfuko wa Jimbo imetumia fedha nyingi zipatazo Shilingi 2,330,500 kwa ufuatiliaji.

Aidha Kamati ya PAC imepata nafasi ya kukagua Skuli ya Uwandani ili kuona madarasa matatu yaliyojengwa katika madarasa hayo. Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi ya Jimbo hilo kwa mwaka 2017/2018.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Ole iwe karibu zaidi na Watendaji wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wanaohusika na miradi ya Mfuko wa jimbo ili wapate maelekezo ya kutosha juu ya taratibu za Miradi ya Mfuko wa Jimbo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 12. | CHONGA | 20,000,000 | Muendelezo wa maji safi na salama kijiji cha Tundauwa | Kilindi | 7,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa kituo cha afya wa Tundauwa | Kilindi | 3,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa kalavati kijiji cha Pujini | Pujini | 9,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chonga.

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Chonga imekiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mitatu kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika uchunguzi wa vielelezo vya matumizi ya miradi, Kmati imebaini kuwa stakabadhi hailsi za malipom (original) zimepotea kutokana na kuhama kwa Ofisi ya Baraza la Mji Chake Chake na kuhamia katika Ofisi mpya ngawa kopi za vielelezo hivyo vilikuwepo..

Kamati pia ilikagua miradi mbalimbali iliyotekelezwa kama ifuatavyo:-

i. Kalavat – Pujini: Kamati imebaini kuwa Kalavat hilo limeanza kuwa nyufa
ii. Kituo cha Afya Tundauwa: Kituo kilianza kujengwa kwa nguvu za wananchi, Fedha za Mfuko wa Jimbo (Shilingi 3,000,000) zimetumika kujenga nguzo tatau na kuendelea na

ujenzi kuanzia kozi ya saba hadi juu, Hata hivyo Kamati ya PAC imebini kuwa kituo hicho kimejenegwa bila kushirikishwa kwa wataalam wa Afya. Jengo la kituo hicho cha Afya limekaa kwa muda mrefu bila ya kuezekwa wala kuendelezwa na kimenaza kukatika katika sehemu za bim. Kwa hivi sasa wananchi wa Tundauwa wanatumia kituo cha Afya cha KMKM Tundauwa.

Kwa ujumla Kamati ya PAC haikurudhika na utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwa miradi hiyo imebainika kuwa haina viwango.

.

4. Kamati za Mfuko wa Jimbo ziwe makini katika utunzaji wa kumbukumbu za matumizi ya miradi hasa ikizingatiwa kuwa fedha hizo ni za Serikali na zinapaswa kukidhi taratibu za Srrikali ikiwemo kukaguliwa kwa matumizi ya fedha hizo.
5. Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Chonga pamoja na Kamati nyengine za Mfuko wa Jimbo ziandae mipango mizuri ya utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Jimbo pamoja kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa inakidhi viwango vinavyokubalika na inalingana na thamani halisi ya fedha. zilizotumika.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 13. | CHAKE CHAKE | 20,000,000 | Ujenzi wa mabanda ya skuli ya Chanjaani | Chanjaani | 12,443,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Banda la wafanyabiashara eneo la soko la Tibirinzi | Kichungwani | 3,557,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uungaji wa maji safi na salama kutoka Weles Michakaeni | Msingini | 2,800,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | hadi Msingini Kilimani | | | |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chake Chake.

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Chake Chake imekiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilikagua nyaraka za matumizi ya miradi pamoja na nyaraka nyenginezo zinazohusiana na utekelezaji wa miradi zikiwemo stakabadhi (risiti) za malipo na Fomu za miradi ambapo Kamati iliridhika na nyaraka hizo. Vile vile Kamati ya PAC ilipata nafasi ya kukagua miradi iliyotekelezwa katika Jimbo hilo na kwa ujumla imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 14. | WAWI | 20,000,000 | Ujenzi wa njia Ndugukitu | Mkorosho n i | 7,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Uendelezaji wa ujenzi wa jengo la mabanda matatu skuli ya maandalizi Ditia | Mgogoni | 12,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Wawi.

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Wawi imekiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi miwili kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilkagua nyaraka mbalimbali za matumizi ya fedha za miradi pamoja na nyaraka zinazohusiana na utekelezaji wa miradi hiyo zikiwemo Fomu za Miradi na stakabadhi za malipo na kuridhika nazo.

Aidhaa Kamati ya PAC ilkagua mirdai iliyotekelezwa kama ifuatavyo:

i. Mabanda matatu Skuli ya Maandalizi Ditia: ujenzi ulihusisha kujenga nguzo za zege, kujenga mkanda baada ya kozi tano na kuendelea hadi juu.. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeezeka mabanda hayo.

ii. Njia ya Ndugu Kitu: ujenzi wa njia hiyo yenye urefu wa mita 5000 ulihusisha upigaji wa "grader" na utiaji na utandazaji wa kifusi. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilibaini kuwa utiaji a utandazaji wa kifusi hicho ilifanywa kienyeji kwa kutumia mikono (majembe na mapauro) na njia hiyo ilikuwa tayari imeharibika. Kamati ya PAC haikuridhika na utekelezaji wa mradi huu.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chake Chake kwa kushirikiana na Baraza la Mji Chake Chake liikagua na kusimmamia vizuri miradi ya Mfuko wa Jimbo wakati wa utekelezaji wake ili iweze kutekelezwa kwa ufanisi uliokusudiwa.
2. Kamati ya Mfuko wa Maendelo ya Jimbo la Wawi itekeleze miradi ya Jimbo hilo kitaalamu ili miradi hiyo iweze kudumu kwa muda mrefu na kuweza kutoa tija endelevu kwa wananchi.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 15. | ZIWANI | 20,000,000 | Ujenzi wa kituo cha Afya Birikau | Michungwani | 10,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa banda la kutwangia mpunga Michungwani | Michungwani | 6,000,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ununuzi wa mashine ya boti kwa kikundi cha ushirika Michungwani | Michungwa ni | 3,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Ziwani.

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Ziwani imekiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mitatu kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa ununuzi wa mashine ya boti ilielezwa kugharimu shilingi 3,000,000/= , hata hivyo, stakabadhi ya malipo hayo inaonesha kuwa ni shilingi 2,854,000/= ambapo shilingi 150,000/= zilielezwa kuwa zilitumika kama kodi ya zuio (irithholding tax) ingawa hakukuwa na uthibitisho wa Fomu ya TRA kuthibitisha kodi hiyo ya zuio.

Hata hivyo, Kamati imekagua nyaraka nyenginezo zikiwemo Fomu za miradi, kumbukumbu za kikao cha Kamati ya Mfuko kilichofanyika tarehe 5/4/2018 kilichoihinisha miradi hiyo, pamoja na nyaraka nyenginezo za matumizi ya miradi hiyo. Kamati kwa ujumla imeridhika na nyarakaa hizo. Kwa upande wa ukaguzi wa miradi, Kamati ya PAC ilifanya ukaguzi wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

i. Mashine ya Boti (Horse power 15 aina ya Sail) imekaguliwa na kubainika kuwa imehribika kwa karibu miezi mitatu ingawa imefanyakazi kwa miaka minne. Mashine hiyo ilikuwa ikitumiwa na kikundi cha uhirika kiitwacho “Mmoja” kwa ajili ya uvuvi wa chaza. Imeelezwa kuwa gharama za matengenezo yam shine hiyo zinafikia shilingi 700,000/=. Hadi kikundi hicho kilipokutana na Kamati ya PAC walikuwa wanakwenda kuvua chaza kwa kutumia Boti na tanga (bila yam ashine).

ii. Banda la kusagi Mpung- Kamati ya PAC imebaini kuwa ingawa banda la kusagia Mpunga limjengwa lakini banda hilo pamoja na mashine nyengine yenyewe ya kusagia mpunga haviko katika mazingira masafi. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa mashine hiyo haijatumika kwa karibu miezi sita kutokana na kutoridhisha kwa msimu wa mpunga uliopelekea uzalishaji mdogo wa mpunga . Mashine iliyomo katika banda hilo la kusagia mpunga

kutumika na wnakijiji wa Michungwani na Kukuchuni.

Kamati ya PAC haikuridhika na hali ya mashine ya boti pamoja na banda la kusagia mpunga.

Mapendekezo ya Kamai ya PAC

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Ziwani kwa kushirikiana na Baraza la Mji Chake Chake liandae utaratibu wa kufuatilia na kuikagua miradi yote ya Mfuko wa Jimbo baada ya utekelezaji wake ili kuona namna inavyendelea na tija inavyopatikana.

Utekelezaji wa Miradi Wilaya ya Mkoani (2017/2018)

| Nam. | Jimbo | Fedha Zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha iliyotumika | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 9. | CHAMBANI | 20,000,000 | Ukarabati wa Skuli ya Ukutini | Ukutini | 7,000,000 | Mradi unaendelea |
| | | | Ukarabati wa kituo cha chekechea Chwale | Chambani | 4,184,000 | Mradi unaendelea |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ukarabati wa Skuli ya Dodo msingi | Dodo | 5,761,000 | Mradi unaendelea |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chambani.

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Chambani imekiri kuingiziwa jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini na kutekeleza miradi mbali mbali katika Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti,

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imekagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji wa miradi zikiwemo kumbukumbu za kikao cha tarehe 3/4/2018 kilichoidhinisha miradi iliyotekelezwa . Vile vile Kamati ilielezwa kazi mbalimbali zilizotekelezwa katika kila mradi kama ifuatavyo:-

1. Mradi wa ukarabati wa Skuli ya Ukutini ulihusisha kazi za ujenzi wa uzio, kuta, madirisha na kutia milango ya mageti kwenye maeneo yaliyo wazi.
2. Kwenye mradi wa ukarabati wa Skuli ya Dodo Msingi, kazi zilizofanyika ni kugonga na kutoa mavumbi kwenye vyumba vine vya madarsa, kusafisha kwenye kuta za madarasa na kutia plasta, kuingiza kifusi katika vyumba vine na kutia sakafu na kujenga Apron sehemu ya ndani ya skuli.
3. Katika mradi wa ukarabati wa kituo hicho cha chekechea cha Chwale, kazi zilizofanyika ni kutia sakafu na plasta pamoja na kutia madirisha na milango kwenye banda la kituo hicho lenye vyumba viwili.

Kamati ilikagua nyaraka za matumizi ya miradi hiyo pamoja na kukagua kazi zilizofanyika katika skuli ya Ukutini ambapo iliwakuta mafundi wakifanya marekebisho katika mlango.

Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 10. | MKOANI | 20,000,000 | Ujenzi wa Skuli ya Kisiwa Panza | Kisiwa Panza | 5,000,000 | Mradi unaendelea |
| | | | Upelekaji umeme Chanjaani Chokocho | Chokocho | 6,000,000 | Mradi unaendelea |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ujenzi wa Skuli ya TUTU Jondeni | Ng'ombeni | 2,000,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Ujenzi wa Jengo la Redio Jamii Mkanyageni | Mkanyageni | 5,000,000 | Mradi unaendelea |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mkoani,

Kamati ilikiri kupokea Shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbali mbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti ambapo kwa hivi sasa miradi yote imrkamilika,

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya P.A.C ilielezwa kazi zilizotekelezwa katika kila mradi kama ifuatavyo;-

1. Katika mradi wa umeme kijiji cha Chanjaani, Chokochouliotumia Shilingi 6,000,000/= kazi iliyofanyika ni upelekaji wa umeme nguzo katika kijiji cha Chanjaani Chokocho.
2. Kwenye Mradi wa ujenzi wa jingo la Radio Jamii Mkanyageni – kazi iliyofanyika ni kusafisha kiwanja, kutengeneza michoro na ununuzi wa kifaa cha kurushia matangazo.
3. Katika mradi wa ujenzi wa Skuli ya msingi Kisiwa Panza uliogharimu Shilingi 5,000,000/= - kazi zilizofanywa zilihusisha ujenzi wa "foundation" yenye vyumba vitano (5).
4. Ujenzi wa Skuli ya TUTU Jondeni iliyoghrimu shilingi 2,000,000/= ulihusisha kazi ya ujenzi wa matofali kutoka hatua ya linta ya kati mpaka kumalizia Gebo.

Kamati ya P.A.C ilikagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji wa Miradi zikiwemo Fomu za Miradi na kumbukumbu za kikao ca tarehe 3/5/2018 kilichoidhinisha miradi iliyotekelezwa. Aidha, Kamati ilikagua nyaraka mbali mbali za matumizi ya miradi hiyo pamoja na kukagua baadhi ya miradi iliyotekelezwa. Transmitter ya Radio Jamii imepelekwa TBC(Tanzania Bara) kwa marekebisho.Kwa ujumla Kamati ya P.A.C imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na matumizi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji wa miradi husika

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 11. | KIWANI | 20,000,000 | Mradi wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa skuli ya Chwaka | Mtangani | 5,000,000 | Mradi unaendelea |
| | | | Mradi wa uezekaji wa darasala kusomea skuli ya Mwambe Sekondari | Mwambe | 3,176,000 | Mradi umekamilika |
| | | | Mradi wa ununuzi wa saruji, mawe na mchanga kwa ajili ya uendelezaji wa skuli ya | Mwambe | 2,000,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Mwambe sekondari na skuli ya maandalizi Chanjaani | | | |
| | | | Mradi wa kusaidia Polisi jamii ya Mwambe na Kiwani | Mwambe | 2,000,000 | Mradi umekamilika |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kiwani.

Kamati ya Mfuko wa Jimbo imekiri kupokea jumla ya Shilingi 20,000,000/= kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo katika Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya P,A,C

Kamati ya P.A.C imebaini miradi na kazi mbali mbali zilizotekelezwa katika miradi hiyo pamoja na gharama zake kama ifuatavyo:-

1. Ujenzi wa Madarasa ya kusomea Skuli ya Chwaka uligharimu jumla ya Shilingi 5,000,000/= ambazo zilitumika kwa ajili ya kununua vifaa vya ujenzi ikiwemo saruji, mchanga na nondo, Mradi huo umekamilika.
2. Uendelezaji wa vyumba vya darasa la kusomea Skuli ya Mwambe uligharimu Shilingi 8,326,000/= ambazo zilitumika kuezeka, kupiga plasta na kutia sakafu. Mradi huo umekamilika,
3. Mradi wa umalizaji wa Skuli ya Maandalizi Chanjaani ulitumia Shilingi 3,175,000/= ambazo zilitumika katika kupiga plasta na kutia sakafu.
4. Kusaidia Polisi Jamii Shehia ya Mwambie na Kiwani ambapo Shilingi 2,000,000/= zilitumika. Mradi ulilenga kudhibiti utoro uliokithiri, utumiaji wa madawa ya kulevya na wizi wa mazao na mifugo.

Aidha, Kamati ya P.A.C ilikagua nyaraka mbali mbali zinazohusiana na matumizi na utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo kumbukumbu za kikao cha tarehe 9/7/2018 kilichoidhinisha miradi hiyo. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi ya Jimbo hilo.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 12. | MTAMBILE | 20,000,000 | Hakuna miradi iliyoainishwa | Jimbo zima | Fedha hazijatumika | Fedha iliyobakia<br>20,000,000 |

Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Mtambile

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mtambile ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Jimbo hilo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya P.A.C imebaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 , Jimbo la Mtambile limetekeleza mradi mmoja tu wa ujenzi wa barabara ya Jambangome kwa hatua ya kifusi ambapo jumla ya Shilingi 18,000,000/= zimetumika na mradi huo umekamilika.

Aidha, Kamati ilikagua nyaraka mbali mbali zinazohusiana na miradi hiyo ikiwemo kumbukumbu za kikao cha tarehe 24/4/2018 kilichoidhinisha miradi hiyo,  Pia Kamati ilikagua nyaraka za matumizi ya mradi huo pamoja na kuikagua barabara hiyo ya Jambangome.

Kwa ujumla Kamati ya P.A.C imeridhika na utekelezaji wa mradi huo pamoja na matumizi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji mradi huo.

Mapendekezo ya Jumla

i. Kwa kuwa miradi ya Mfuko wa Jimbo imeonekana kuwasaidia sana wananchi katika kuwaondolea kero mbali mbali zilizokuwa zinawakabili, na kwa kuwa changamoto za huduma za  kijamii bado zipo na zinaendelea knaongezeka siku hadi siku, hivyo ni vyema kwa Serikali kuzingatia kwa uzito unaostahili suala la kuongeza kiwango cha fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo kwa ufanisi zaidi na kuzidi kuwaondolea wananchi kero zinazoendelea kuwakabili.

ii. Kwa kuwa baadhi ya majimbo bado hayana ushirikiano wa kutosha na Wakurugenzi wa Mmalaka za Serikali za mitaa ambao ndio wanaopaswa kuwa Makatibu wa Kamati za Mfuko wa Jimbo kisheria, na kwa kuwa yale majimbo yanaayotimiza sharti hilo (la Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa kuwa Katibu wa Mfuko wa Jimbo) yameonekana kukumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ya Wenyeviti wa Kamati za Mfuko wa Jimbo kuhisi kufanyika kwa matumizi mabaya ya fedha na ucheleweshwaji wa matumizi ya fedha za miradi hiyo kunakofanywa na baadhi ya

Watendaji wa Serikali za Mitaa , hivyo ni vyema Serikali ikalifikiria upya suala hilo kwa kuwashirikisha wahusika wote wa miradi hiyo ili kupata maoni yenye muafaka wenye kuleta tija endelevu katika suala hili.

iii. Kwa kuwa utekelezaji wa miradi ya Jimbo kwa ufanisi unhiataji mambo mengi yakiwemo utoaji wa elimu ya kutosha kwa Kamati zote za Mfuko wa Jimbo (Unguja na Pemba) usimamizi wa karibu na ufuatailiaji wa mara kwa mara wa miradi hivyo hivyo ,kuna haja kubwa kwa Serikali kukiimarisha kitengo kinachosimamia miradi ya Mfuko wa Jimbo kilichopo katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kukipatia watendaji wa kutosha, nyenzo za kufanyia kazi ukwemo usafiri wa uhakika pomaja na mambo mengine yanyohusiana na ufanikishaji wa shughuli za uratibu wa miradi hiyo

SEHEMU YA SITA

RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM UNAOHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI MHE.DK.HUSSEIN ALI MWINYI WAKATIWA WA KUWAAPISHA VIONGOZI WAKUU

UCHUNGUZI WA KAMATI YA PAC KUHUSU RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM WA MFUKO WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI PEMBA

Hoja Namba 7.3.1 Mikopo Ambayo Haikurudishwa Shilingi 125,654,000

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia nyaraka na kumbukumbu mbali mbali zinazohusiana na utoaji wa mikopo midogo midogo kwa wajasiriamali kupitia katika vikundi vyao vya ushirika. Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya wajasiriamali 152 ambao wamepatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi 125,654,000, zilizokopeshwa na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Taarifa za urejeshwaji wa fedha hizo hazikuweza kupatikana kwa ukaguzi.

Kutokurejeshwa kwa mikopo kutoka kwa wajasiriamali imepelekea kuwepo kwa uhaba wa fedha kwa ajili ya kuendelea kuwakopesha wajasiriamali wengine ambao wangeweza kupata fursa ya kujiendeleza kiuchumi kupitia mfuko huo.

Hadi tunakamilisha ukaguzi huu hakuna hatua zozote zilizoweza kuchukuliwa kwa wadaiwa wa mikopo hiyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 5.5 cha Muongozo wa Uendeshaji wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wa mwaka 2014.

Jadweli lifuatalo hapo chini linaonesha malimbikizo ya madeni wanayodaiwa wajasiriamali kwa kila Wilaya.

| WILAYA | IDADI YA WADAIWA | THAMANI YA MKOPO | KIASI KILICHOLIPWA | DENI |
|---|---|---|---|---|
| WETE | 26 | 73,660,000 | 34,346,000 | 41,714,000 |
| MICHEWENI | 20 | 22,885,000 | 14,882,000 | 8,003,000 |
| CHAKE CHAKE | 71 | 112,092,500 | 61,839,500 | 50,253,000 |
| MKOANI | 35 | 63,825,000 | 26,806,000 | 38,019,000 |
| JUMLA | 152 | | | 125,654,000 |

Kutokana na mchanganuo wa madeni hayo yanayoonekana katika jadweli hapo juu ambayo yameonesha ujumla ya malimbikizo ya madeni yanayodaiwa kwa kila Wilaya. Aidha, idadi ya wajasiriamali kutoka kila Wilaya, majina yao pamoja na taarifa zinazowahusu wajasiriamali hao zinaonekana katika kiambatisho namba 7(A) kama kilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti

Majibu ya Ofisi ya Raisi kazi Uchumi na Uwekezaji

Mfuko kwa kutumia vyombo mbalimbali umekuwa ukijitahidi sana kufuatilia mikopo yote inayotolewa kuona kuwa inatumiwa ipasavyo na inalipwa kwa mujibu wa ratiba ya ulipaji wa mikopo.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na:-

a) Mfuko kuandaa ziara za ufuatiliaji wateja wa Wilaya zote kila mwezi kupitia kikosi kazi kilichoandaliwa kinachowashirikisha watendaji wa Idara nyingine zilizo chini ya Ofisi..Utaratibu huu umekuwa chachu ya kuongezeka marejesho ya mikopo kutoka kwa wakopaji.

b) Ripoti za watu ambao hawalipi vizuri (wadaiwa sugu) zimekuwa zikipelekwa katika vikao vya viongozi wa Wizara na katika Vikao vya Bodi ya Mfuko, na Bodi ya Mfuko imefanya ziara mara mbili Kisiwani Pemba - Disemba mwaka 2019, na Juni mwaka 2021, na katika ziara zote hizo wamekutana na wajasiriamali wanaofanya vizuri, na wale ambao hawafanyi vizuri na kuwahimiza juu ya wajibu wao wa kulipa madeni yao ya muda mrefu.

   Pia, viongozi wa Wizara kwa nyakati mbalimbali wamekuwa wakikutana na wadaiwa sugu na kuwahimiza walipe mikopo yao ili waepuke hatua za kisheria

c) Maafisa wadhamini wote waliopita na aliyepo sasa, wanawafuatilia kila mara wateja ambao hawalipi mikopo yao na kuwashauri kufanya malipo ili waepukane na hatua za kisheria

d) Pia, mikutano na masheha wa Wilaya zote 11 inafanyika kwa lengo la kuwajulisha juu ya Mfuko na taratibu zake, na masheha wamekuwa msaada mkubwa katika kusaidia upatikanaji wa mikopo isiyolipwa vizuri.

e) Mfuko pia unafanya kazi kwa karibu na Mamlaka za Mikoa na Wilaya zote jambo linalorahisisha kuwafikia wananchi katika kuwapatia huduma za kifedha, lakini pia kusaidia katika kufuatilia marejesho yake.

f) Mfuko kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali za Mitaa unakuwa unatoa barua za wito kwa wadaiwa sugu na kufanya nao vikao vya kuwataka kurudisha mikopo yao

g) Mfuko umekuwa ukishirikiana na mwanasheria wa Wizara kuchukua hatua za kisheria kwa wale wateja walioendelea kukaidi kulipa mikopo yao ingawa hatua hii baadae ilisimamishwa ili busara zaidi itumike.

   Kutokana na juhudi zote hizo, kuna baadhi ya wateja wameanza kulipa kidogo kidogo mikopo yao na wengine wamemaliza.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa Wizara imefanya jitihada mbalimbali ili mikopo irudishwe ambapo hapo awali ilikuwa inawapeleka wakopeshwaji mahakamani na ilionekana kuwa kuwapeleka wajasiri amali mahakamani ni kuwarudisha nyuma na Serikali ilishauri kutumia busra zaidi katika kufuatilia mikopo.

Kamati ya PAC imefanya vikao na wajasiriamali mbalimbali kutoka wailaya za Chake Chake,Wilaya ya Mkoani, Wilaya Wete na Wilaya ya Micheweni kwa ajili ya kuzungumza nao juu ya masuala mbalimbali yakiwemo sababu zilizopelekea kutokulipa madeni hayo kwa muda mrefu. Miongoni mwa wajasiriamali waliokutana na Kamati ya PAC ni kama wafuatao:-

Wilaya ya Chake Chake

- Ndg, Moh'd Ali Moh'd
- Ndg Sudi Ali Said
- Ndg. Mo'hd Juma Dau

Wilaya ya Mkoani

- Ndg. Asha Juma Shaali
- Ndg, Ali Makame Rajab
- Ndg. Sulieman Ussi Rajab (Kikundi cha Nguvu Kazi)

Wilaya ya Wete

- Hatuna Chuki Society
- Ndg. Rashid Juma Salum
- Kigongoni Co operatives

Wilaya ya Micheweni

- Ndg, Mosi Salum Khamis
- Ndg.Hassan Khamis Rashid
- Ndg. Mbarouk ALI Mbwana

Kutokana na vikao vilivyofanyika baina ya Kamati ya PAC na Wajasiriamali hao Kamati imebaini sababu za msingi zilizopelekea wajasiriamali kushindwa kurejesha mkopo kwa wakati zikiwemo zifuatazo:-

- Uelewa mdogo wa wajasiriamali juu ya dhamani ya deni amapo imebainika baadhi ya wajasiriamali baada ya kuona fedha za Serikali waliona hakuna umuhimu wa kulipa deni hilo.
- Kukosekana kwa elimu inayohusu maeneo mbalimbali ya ujasiriamali kwa mfano wakulima kukosa elimu ya aina ya kilimo wanachotaka kuanzuisha.
- Kukosekana kwa soko la uhakika la bidhaa zinazozalishwa kwa Wajasiriamali la kuuzia bidhaa zao
- Kukosekana kwa utafiti kwa kazi za ujasiriamali ambapo wajasiriamali hao hujihusisha na ujasiriamali bila ya kufanya utafiti kwa kazi wanazozifanya na soko la bidhaa zao, hali hii imepelekea wajasiriamali wengi kutokufikia malengo.
- Kukosekana kwa wataalamu wa fani mbalimbali zinazohusiana na kazi za wajasiriamali kama kilimo cha mboga mboga, mifungo na biashara kwa wajasiri amali
- Kuwepo kwa mabadiliko ya hali ya hewa kumepelekea wajasiriamali ambao wanajishughulisha na

kilimo kushindwa kuendelea na kazi zao kutokana jua kali liloathri mimea yao.

Pamoja na sababu hizo ambazo kimsingi zimepelekea kushindwa kwa wajasiriamali kurejesha mikopo kwa wakati pia Kamati imebaini kuwa kuna changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili wajasiriamali kwa ujumala zikiwemo zifuatazo:-

- Baadhi ya Wajasiriamali wamekumbwa na matatizo ya kifamilia kwa hiyo wameshindwa kuendelea na mradi yao.
- Kuwepo kwa udanganyifu kwa baadhi ya wajasiriamali ambapo imebainika wajasiriamali wenyewe kwa wenyewe .

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. kamati ya PAC inashauri Wizara iwe karibu na waliopewa mikopo kwa kuwapatia mafunzo ya ujasiri amali,ushauri ili wawaze kuendesha kazi zao kwa ufanisi na kuweza kurejesha fedha walizokopa.

2. Wizara Nchi Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji ishirikiane na Wizara ya kilimo ili kuwapatia wajasiriamali wa kilimo wataaluma watakaoweza kuwasaidia wajasiriamali hao waweze kufanya kazi zao kwa tija.

3. Wizara iwe na usimamizi mzuri katika kufuatilia urejeshaji wa mikopo kwa ichukue juhudi za makusidi za kuhamasisha wakopaji kurejesha mikopo iliyobakia na wakopaji wapya walipe kwa wakati.

4. Kamati ya PAC inashauri Wizara ifikirie kuengeza kifungu katika masharti ya mkopo kitakacho wapana kidogo wakopaji ikiwemo kuweka sharti la kuchukua kitu cha mkopaji iwapo mkopaji atashindwa kurejesha mkopo.

5. Kwa kuwa wajasiriamali wanashughulikiwa na Wizara mbalimbali zikiwemo Wizara zenye dhamana ya Vijana, Biashara,Kilimo na Uwezeashaji Kamati ya PAC inasisitiza Wizara Nchi Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji kuandaa kanzi data (data base) imara itakayoweka takwimu sahihi za wajasiriamali.

Hoja Namba 7.3.2 Mikopo Iliyotolewa Kinyume na Utaratibu Shilingi 4,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 4,000,000 zilitumika kuwakopesha wajasiriamali kinyume na utaratibu, kwa mujibu wa Muongozo wa Uendeshaji wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kwani wajasiriamali hao walitakiwa kurejesha deni la awali kabla ya kukopa deni jipya. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Muongozo wa Uendeshaji wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wa mwaka 2014, kifungu nambari 4.9.2(iii).

Wajasiriamali hao ni kama inavyoonekana katika Jadweli lifuatalo:-

| JINA LA MKOPAJI | TAREHE YA MKATABA | THAMANI YA MKOPO | TAREHE YA KUMALIZA | TAREHE ALIYOPATIWA | THAMANI YA MKOPO |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | WA AWALI | WA AWALI | MKOPO WA AWALI | MKOPO MPYA | MPYA (Tshs) |
| Juma Khamis Abdalla | 07/03/2018 | 2,000,000 | 9/9/2019 | 9/04/2018 | 2,500,000 |
| Khamis Kombo Ali | 05/03/2019 | 5,000,000 | 3/5/2023 | 22/10/2019 | 1,500,000 |

Ufafanuzi wa maelezo ya jadweli lililokuwepo hapo juu, wajasiriamali hao walipaswa kulipa madeni yao kwa mujibu wa mkataba wa awali kabla ya kufunga mkataba mpya wa ukopeshwa wa fedha, ukaguzi umebaini uwepo wa dasari kubwa katika usimamizi wa mikataba, jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa udhaifu wa udhibiti wa ndani.

Majibu ya Ofisi ya Raisi kazi Uchumi na Uwekezaji

Wajasiriamali waliotajwa hapo ni Bwana Juma Khamis Abdalla aliyepatiwa mkopo wa Shilingi 2,000,000/= ; baadae mkopo wa shilingi 2,500,000/=.

Mjasiriamali mwengine ni Bwana Khamis Kombo Ali aliyepatiwa mkopo wa Shilingi 5,000,000/=; baadae mkopo wa shilingi 1,500,000/=.

Bwana Juma Khamis alipewa mkopo wa Shilingi 2,000,000/= na Mfuko wa Uwezeshaji.

Baadae Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ilimpatia mashine ya kukamulia miwa yenye thamani ya shilingi 2,500,000/=.

Baada ya Mfuko kupatiwa taarifa hizi na Idara ya Uwezeshaji, ukaliongeza deni la Bwana Juma kwa Shilingi 2,500,000/= na kuanza kufuatilia madeni yote mawili.

Utaratibu huu ni wa kawaida kwani kabla kulikuwa na mradi wa vihori ambapo wakulima wa mwani walipewa vihori na Idara ya Uwezeshaji na wakatakiwa wavilipie kupitia Mfuko wa Uwezeshaji.

Na Bwana Khamis Kombo Ali yeye alipewa mkopo mwengine kabla ya kumaliza wa awali kwa kutumia kifungu namba 5.6 cha REFINANCING ambapo kinatoa fursa ya kupandikiza mkopo mwingine katika mazingira mahsusi ambayo yataleta tija kwa mkopaji au kwa jamii ya wajasiriamali.

Bwana Khamis alipewa mkopo wa ziada ili kumuwezesha kushiriki katika maonesho ya Afrika Mashariki ambayo kwa Tanzania yalifanyika kitaifa Zanzibar eneo la Fumba, mwaka 2019 mwishoni. Fedha zile zimemuwezesha kushiriki maonesho hayo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imepitia kifungu 5.6 cha Muongozo wa Uwendeshaji wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kinachohusu urekebishaji wa mkopo na utoaji wa fedha nyengine za mkopo “loan restructuring and

refinancing.”ambacho pamoja na mambo mengine kimeeleza kuwa hakuna mkopo utakaorekebishwa au kupewa fedha nyengine ila kwa mazigira maalum na baada ya ombi kuwasilishwa na afisa Mikopo. Baadaya ya kupitia kifungu hicho Kamati imeridhika na ufafanuzi na haikuwa na maelezo zaidi.

Hoja na Namba 7.3.3 Gharama za Maombi ya Mikopo Zilizolipwa Kinyume na Utaratibu Shilingi 2,874,000

Kwa mujibu wa muongozo wa uendeshaji wa Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi unaelekeza kumtoza mkopaji jumla ya shilingi 8,000, ambazo zitajumuisha gharama ya fomu ya maombi, utayarishaji mkataba, kitabu cha mwanachama “Loan Pass Book” na mafunzo kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi. Aidha, muongozo huo unamtaka mkopaji kulipa asilimia moja ya thamani ya mkopo anaopatiwa.

Ukaguzi umebaini utozaji wa gharama kubwa za maombi ya mkopo kuliko inavyostahiki, jambo ambalo ni kinyume na kifungu 4.4 cha muongozo wa mfuko huo.

Majina pamoja na taarifa zinazowahusu wajasiriamali waliotozwa gharama kubwa za maombi ya mkopo kuliko inavyostahiki, zinaonekana katika kiambatisho nambari 7(B).

Majibu ya Ofisi ya Raisi kazi Uchumi na Uwekezaji

Mfuko unafanya shughuli zake kwa kufuata Muongozo wa Uendeshaji ambao umetengenezwa kutokana na hali halisi ya wanachi wetu na pia kuhakikisha uendelevu (Sustainability) wa Mfuko wenyewe.

Kifungu Namba 4.4 cha Muongozo ambacho kinaelezea gharama za mikopo kwa wajasiriamali kilikuwa na matatizo katika tafsiri, na utekelezji wake ulileta tabu kwa maafisa wote wa mikopo Unguja na Pemba.

Tatizo hili lilifikishwa katika kamati ya mikopo (Kwa kuwa Bodi ilikuwa haijaanza kufanya kazi zake) ambapo katika kikao chake cha mwaka 2017, kiliamua kuondoa utata kwa kusema kuwa zipunguzwe idadi ya tozo, na ziongezwe thamani tozo chache zitakazobakia.

Tozo zilizobaki na viwango vyake vikawa Fomu ya maombi (5,000/=), Leja (5,000/=) na Kitabu cha mteja (5,000/=).

Kwa gharhama za ufuatiliaji, mteja alipie asilimia mbili ya gharama za mkopo aliopewa.

Mwaka 2020 Oktoba, kulitokea mabadiliko mengine ya Muongozo wa Mfuko kwa kuondoa sharti la mkopaji lazima kutoka katika kikundi, na pia kuongeza viwango vya mikopo kutoka shilingi 5,000,000/= kuwa shilingi 10,000,000/= .

Nyaraka za mabadiliko hayo zipo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kujiridhisha na majibu ya Wizara Kamati ya PAC imekagua kumbukumbu cha kikao cha pili cha kamati ya kutadhamini mikopo ya tarehe 19 febuari 2017,na kubaini maamuzi yaliyofikiwa katika kuhusu gharama zinazohusiana na maombi ya mikopo ambapo kikao hicho kimeamua gharama za mafunzo na mikataba

ziondolewe kwa kuwa hazina tija na badala yake zipaki gharama tatu tu, ambazo mteja atatakiwa ndio alipie.Gharama hizo ni ununuzi wa Fomu ya maombi (5,000/=), Leja (5,000/=) na Kitabu cha mteja (5,000/=) na kuhusu ufuatiliaji wa mikopo kila mteja alipiwe asilimia mbili iliyopitishwa.

Kamati ya PAC ilihoji juu ya sababu za kutokupatiwa mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibi taarifa ya ufafanuzi na vielelezo vinavyohusiana na hoja hii na kuelezwa kuwa wakati mkaguzi alipokwenda kufanya ukaguzi mkuu wa kitengo alikuwa kwenye mafunzo.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

i. Kamati ya PAC inashauri Wizara Nchi Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji Pemba kutoa mashirikianao mazuri pale anapokwenda mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti, kuweka utaratibu utakao muezesha mkaguzi kupata maelezo na vielelezo vinavyohitajika endapo mtumishi anaehusika atadharurika wakati wa ukaguzi.
ii. Kamati ya PAC inahauri wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji Pemba kuwa na mawasiliana mazuri mingoni mwa watendaji kwa kupeana taarifa juu ya maamuzi muhimu yanayofikiwa na badala maamuzi hayo kujulikana na viongozi tu.

Hoja Namba 7.3.4 Kukosekana kwa Vielelezo vya Malipo ya Fedha za Mikopo Shilingi 6,500,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokufuatwa kwa baadhi ya masharti ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kukosekana kwa vielelzo muhimu vyenye thamani ya shilingi 6,500,000, ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo ya fedha za mkopo kwa wajasiriamali.
Kukosekana kwa vielelezo muhimu vya mfuko ni kwenda kinyume na muongozo wa Uendeshaji wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wa mwaka 2014, pamoja na sheria ya usimamizi wa fedha za Umma ya Zanzibar, nambari 12 ya mwaka 2016 kifungu nambari 34(1)

Jadweli lifuatalo hapo chini linaonesha wajasiriamali kwa kila Wilaya ambao vielelezo vyao havikupatikana kwa ukaguzi.

Majibu ya Ofisi ya Raisi kazi Uchumi na Uwekezaji

Mahitaji ya hoja hii yamewekwa sawa baada ya vielelezo husika kupatikana.

Mfuko ulikuwa na kipindi kigumu cha kuhamahama kuanzia 2014 mpaka 2020 ambapo ulikaa katika sehemu nne tofauti kuanzia Madungu jengo la ZSTC, kwenda jengo la NMB Miembeni, kwenda Tibirinzi, na kuishia Ofisi za Serikali Gombani.

Kuhamahama huku kulipelekea baadhi ya nyaraka kuchanganyika na nyaraka zisizohusika.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba kuhama kwa Ofisi haikuwa sababu ya msingi ya kukosekana kwa vielelezo muhimu wakati wa ukaguzi.Hata hivyo kamati ilikagua vilelezo hivyo vilivowasilishwa kwenye kikao chake ikiwemo vifuatavyo:-

i. Hati ya usajili ya Chama cha Ushirika cha Siri Moyoni cooperative yenye namba P.2762/2016 iliyotiwa sainina Mrajis wa vyama vya Ushirika Zanzibar tarehe 06 Disemba

ii. Hati ya usajili ya Chama cha Ushirika Tumaini Jipya yenye namba P.2511/2017 iliyotiwa saini na Mrajis wa Vyama vya Ushirika Zanzibar tarehe 10 Ogosti 2017

iii. Hati ya usajili ya Chama cha Ushirika Atowaye ni Karima Cooperative yenye namba P.1795/2011 iliyotiwa saini na Mrajis wa Vyama vya Ushirika Zanzibar tarehe 1 April 2021

iv. Mkataba wa mkopo wa shilingi 2,000,000 baina ya Khamis Salim Khamis na Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi tarehe 20 Octoba 2016

Mapendeko ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imewashauri watendaji Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi Pemba kutunza kumbukumbu za mikopo vizuri ili kuepusha upotevu wa nyaraka muhimu.

Hoja Namba 7.3.5 Kukosekana kwa Majalada ya Wakopaji:

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa wajasiriamali waliokopeshwa fedha lakini majalada yao "files" yenye kuonesha taarifa za mikopo waliokopeshwa hayakupatika kwa ukaguzi.

Kukosekana kwa Majalada kwa woakopeshaji imepelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa mikopo iliyotolewa kwa wajasiriamali hao . Aidha kufanya hivo ni kwenda kinyume na Muongozo wa Uendeshajiwa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wa mwaka 2014.kiambatanisho 7c Kama inavoonekana kwenye ripoti ya mdhibiti..

Majibu ya Ofisi ya Raisi kazi Uchumi na Uwekezaji

Kuna wateja wanne, wawili kutoka Wilaya ya Chake Chake na wawili kutoka Wilaya ya Mkoani majalada yao hayakupatikana wakati wa ukaguzi

Tatizo lilikuwa ni huko kuhamahama kwa ofisi,Majalada yamepatikana na yapo kwa kuangaliwa.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imekaguavielelezo vifuatavyo:-

i. Mkataba wa mkopo wa shilingi 1,200,000 baina ya Subura Njema Coperative na Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi wa tarehe 8 Machi 2016.

ii. Mkataba wa mkopo wa shilingi 1,500,000 baina ya Salim Ali Shaali na Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi wa tarehe 3 Disemba 2014.

iii. Mkataba wa mkopo wa shilingi 1,500,000 baina ya Asakheri na Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi wa tarehe 5 Machi 2016.

iv. Mkataba wa mkopo wa shilingi 1,500,000 baina ya Zubeda Said Hamad na Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi wa tarehe 5 Julai 2014.

Kamati ya PAC baada ya kupitia vielezo hivyo imeridhika navyo.

## SEHEMU YA SABA

## HITIMISHO

Kwa ujumla Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC) imechunguza hoja mbali mbali zilizojitokeza katika Ripoti za Mdhibiti na Mkauguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilzoainishwa,

Katika kutekeleza hayo, Kamati hii ilieleza mambo ambayo imeyabaini na kutoa Maoni au Mapendekezo yake kwa Wahusika kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Taasisi za umma. Hivyo basi, Kamati inaliomba Baraza la Wawakilishi, kuipitia, kuijadili na hatimaye kuiridhia Ripoti hii kwa lengo la kufanyiwa kazi na Serikali.

Kwa kumalizia, Kamati inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Wizara, Mashirika na Taasisi zote za Serikali kwa pamoja Kamati za Mfuko wa Jimbo kwa mashikiano makubwa waliyoipatia Kamati wakati inatekeleza majukumu yake ya kikatiba. Shukurani pia ziwafikie Watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mashirikiano yao kwa Kamati hii.

Vile vile, tunatoa shukurani za pekee kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kuiandalia mafunzo mbali mbali Kamati hii ili iweze kutekeleza vyema majukumu yake.

Kwa namna ya pekee tunatoa shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza wakiongozwa na Katibu wa Baraza hilo kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoyaonesha kwa Kamati kwa kipindi chote cha kazi za Kamati.